सन्दर्भ पुस्तकालय
प्रतिग्रहण क्रमांक .. 656
दयानन्द महिला महा

# SATYARTHPRAKASH

Mwangaza wa Ukweli

**Author:**
Maharshi Dayanand Saraswati

गुरु विरजानन्द दण्डी
सन्दर्भ पुस्तकालय
प्रतिग्रहण क्रमांक .. 656
दयानन्द महिला महा

**Published by:**
Aryasamaj & Arya Stree Samaj
Nairobi, Kenya.

SATYARTHPRAKASH CENTENARY YEAR - 1981

All rights reserved

First Edition 1981, 5000

**Translated into Kiswahili by:**
Dr. J.A. Tejani, Chairman Languages &
Linguistics Dept.
Kenyatta University College, Nairobi
&
Mrs. Naseem Tejani

**Available at:**
International Vedic Institute - Kenya, P.O. Box 40243
Nairobi.



SWAMI DAYANAND SARSWATI.
FOUNDER OF THE ARYA SAMAJ.

## UTANGULIZI

Ninapenda kuandikia dibaji kitabu hiki ambacho chenye mafunzo ya Veda. Katika kurasa mia tatu na hamsini kitabu hiki kimegusia maudhui mbali mbali madogo madogo kwa tafsiri, k.m. kuhusu uzazi, malezi ya watoto, mafunzo mema, wajibu wa wazazi, ibada, ndoa na kanuni zake, uhusiano baina mume na mke, wajibu wa mfalme, mawaziri, falsafa ya Veda, n.k. Kwa ufupi madhumuni ya kitabu hiki ni kuwaeleza wasomaji kinaga-ubaga mafundisho ya Veda kwa lugha fasihi ili msomaji ye yote akiisoma orodha ya yaliyomo mara tu ataathirika na maudhuni mazuri na ya kusisimua.

Jinsi binadamu amezongwa na mazingira ya kisasa hata humsahau Mungu, na muhali kuipata fursa ya kutenda vitendo vya uadilifu na haki. Kwa hivyo kitabu hiki kitamzindua msomaji na kitamraghabisha kumcha Mungu, na kujishughulisha na nyendo zinazompasa binadamu kuzifuata. Binadamu ni kiumbe dhaifu, pengine hushikwa na ugonjwa na maumivu, pengine hupambana na njaa na shida za ukata, na haya yote ni majaribio ya kumangalia jinsi atavyovumilia shida hizo. Huenda pengine afanikiwe na ukwasi, na hayo pia hua majaribio kwake; maana huangaliwa vipi atatumia huo ukwasi wake kwa njia za haki zinazofaa, au ataendesha vitimbi na vituko kwa ajili ya huo ukwasi aliotunikiwa na Mungu. Kwa hivyo vitabu vingi vya dini huwaongoza watu kuzifuata nyendo na njia za haki na za uadilifu. Kitabu hiki yaani "Mwangaza wa Ukweli" kimetungwa kwa shabaha hiyo hiyo yaani kumwongoza binadamu na kumpa mawaidha juu ya tabia na nyendo nzuri, na ili ajieupushe na tabia na nyendo mbaya.

Ninatumai wasomaji watastafidi na nasiha zilizomo katika kitabu hiki.

J.A. TEJANI
Head, Department of Languages & Linguistics
Kenyatta University College

December, 1980

## SWAMI DAYANAND SARASWATI (Habari za Maisha)

Swami Dayanand Saraswati, alikuwa mmoja katika watu waliojitokeza kwa kuanzisha uhuishaji wa mila, dini na ujamii katika India mnamo karne ya 19, alizaliwa Phalgun Badi Dashami, 1881 (12th February, 1825 A.D.) katika Tankara, kijiji cha State - Tankara ambacho kiko kwenye reli nyembamba ya upande wa Western Railway katika Rajkot, Gujrat, Baba yake Karshanji Lalji Tiwari, aliyejulikana kama Amba Shankar, alikuwa Audichya Brahmin na mtu mwenye mali nyingi na sifa njema. Alikuwa Zamindar tajiri na Banker na State Official. Alikuwa mfuasi thabiti wa Shiva na alitaka mtoto wake wa kiume awe mwana wa kustahili na kufuata nyayo zake.

Dayanand alikuwa na majina mawili katika utoto wake. Dayalji (au Daya Shankar) na Mool Shankar, la kwanza likitumika zaidi, kwa sababu lina jina lake la kupanga. Alikuwa na ndugu wawili wa kiume na wawili wa kike. Dayalji alikuwa na akili timamu na ufahamu wa ajabu mno. Fahamu yake yakutambua mambo na kuchambua kwa makini ilikuwa dhahiri. Alipokuwa na umri wa miaka mitano aliweza kusoma kwa ufahamu wa akili wa madondoo mengi ya maandishi fasihi ya Sanskrit. Alipokuwa na umri wa miaka minane alipambwa kwa uzi mtakatifu pia kama Gayatri Mantra na lisomesha Sandhya. Katika muda mfupi wa miaka kumi na tatu alikuwa ameshafahamu kwa akili sarufi ya Sanskrit na Shabdarupavali, Rudradhyaya na Shukla Yajurveda Samhita pia baadhi ya vipande vyengine vya Vedas nyinginezo.

Karshanji alikuwa shaiva thabiti na, kwa hivyo aila yake alifuata dini ya Shaiva. Dayalji au Moolji, kama alivyoitwa, pia alifundishwa kumwabudu Mola Shiva kwa hisani za kufunga na kufanya kazi nyingi nyinginezo za dini. Baba mtu, mwenyewe alikuwa mtaalamu na mwenye kuijua maarifa ya Veda, alitaka mwanawe pia awe mtu maarufu na awe mfuasi wa Mola Shiva. Basi alikuwa anamchukua kwenye hafla zote za dini. Alitaka kumfanya mwenyeji na mwongozi wa nyumba aliyeongoka. Lakini Mungu aliamuru vyengine. Dayalji. alipopambana mara ya kwanza tu na kupenda kanuni za dini basi ushurikina ulitikisa mizizi ya dini yake na ulimfanya awe mtu mwenye shaka shaka na awe mwenye kufanya uchuguzi daima.

Katika 1894 V.S. (1837 A.D.) wakati wa mkesho wa Shivaratri, alihakikishiwa kuona panya wakicheza kwenye sanamu ya Mola Shiva na kula sadaka zake. Aliamka na kumwamsha baba yake ili amfahamishe lakini hakuweza kupata jawabu la kumtosha. Imani yake katika uwezo wa Mola Shiva (sanamu) ilitikisika. Alianza kujua kama roho ya Mungu mwenye uwezo wote kama Mola Shiva haiwezi kuwemo katika sanamu. Ikiwa sanamu ya Mola Shiva lilikuwa na sifa za kupewa za juu juu tu, vipi panya wangeweza kula sadaka zake? Mkasa huo mfupi tu ulitia dosari sawasawa uaminifu wa dini ya Dayalji. Alirudi nyumbani, alifungua kinywa na alipata usingizi. Kifo cha ndugu yake wa kike na ami yake, ambaye alikuwa mwalimu wake, vilimtia huzuni nyingi na kwa hivyo alianza kufikiria kupunguza huzuni za binadamu na vipi kutafuta Shiva ya

kweli. Katika muda huo wazazi wake walitayarisha harusi ambayo yeye alitaka kuiepuka. Wakati wazazi wake walikuwa hawako tayari kuyasikiliza malalamiko yake ati wangoje kwa muda kidogo, basi alikimbia nyumbani jioni mmoja. Ilitokea katika siku za joto za mwaka wa 1846 A.D. (1903 VS). Alikuwa na miaka ishirini na mbili wakati huo. Majaribio ya baba yake ya kumleta nyumbani hayakufaulu.

Baada ya kuacha nyumba ya baba yake alitembelea nyafi nyingi kuwatafuta ma Yogi ambawo wataweza kumwongoza kwenye njia ya uwokovu. Alipofika Sayla (Shaila) kwenye kituo cha reli cha Joravarnagar Sayla kilicho chembamba kwenye Western Railway, alikaa na Lala Bhakta na alianza kujaribu Yoga. Hapo alionana na Brahmachari (aliekuwa hajaoa) na kwa nasiha yake aliapa kuwa yeye pia hataoa na alipewa jina la Shuddha Chaitanya. Baada ya muda aliondoka kwenda Koth Gangada, 84 kilometers kusini magharibi ya Ahmedabad, na kutoka hapo kwenda Siddhapur ambapo watu wengi walikushanyika. Kutoka Siddhapur alifika Chanod na alikaa hapo kwa muda wa zaidi ya mwaka. Hapo alisoma Vedant kutoka Paramanand Paramahansa. Alipoona kupika (kutengeneza) chakula chake mwenyewe kikipoteza wakati wake wa masomo, basi alikusudia kuwa Sannyasi. Alimwomba Swami Chidanand kumfanya kasisi kama Sannyasi lakini baadaye alikataa, kwa sababu, alivyoona yeye Shuddha Chaitanya bado alikuwa hajabobea katika dini na bado alikuwa mwanafunzi, Baada ya hapo alikwenda kwa Poornanand Saraswati, Swami wa Decca, ambaye baada ya kusita sana, alimkubalia kijana anayejinyima na akamfanya kasisi wa Sannyasi na akampa jina la Dayanand Saraswati.

Kutoka Chanod Dayanand aliendelea kwenda Vyas Ashram ambapo alisoma masomo ya kwanza katika yoga kutoka Jwalanand Puri na Shivanand Giri. Baada ya hapo alikwenda Abu na alisoma zaidi habari za yoga kutokana na Yogis walioishi hapa, lakini kiu chake cha kujua ujuzi zaidi wa yoga haikuweza kutoshelezwa. Yeye, hapo aliazimia kuitembelea Uttarakhand kutafuta mabingwa wa yoga na alifika Hardwar katika 1854 wakati wa Kumbha Fair. Hapo aliona mkusanyiko mkubwa wa Sadhus na Sannyasis na alioweza kuonana na Mahatmas wengi na mawalii. Ulichanganyika vizuri na Sannyasis, pia alijishughulisha mara kwa mara kwenda kwenye milima ya Chandi kufanya yoga. Kutoka Hardwar alikwenda Tehri kupitia Rishikesh ambapo alisomea machafu ya fasihi hii ilimfanya achukie mswada mdogo juu ya Tantra pia. Maneno fasihi yote ya Tantra. Tena hapo alitembelea Kedarghat, Rudra Prayag Guptakashi, Trijuginarayan na vilele vya Tunganath na Okhimath, ambapo msimamo mdogo ulifanywa kwa mapumziko. Kedarnath ilipandwa tena pia Joshimath na Badrinath. Alipokuwa Joshimath aliweza kujua kuwa kulikuwa na Mahatmas walioishi katika sehemu hizo. Ili apate kuwashuhudia wao au aweze kuonana nawo ili aweze kutumia wakati kidogo na wao aliweza kuvumilia njia za hatari za Himalayas, ambazo zimejaa wanyama mwitu, na alipanda milima na kushuka bila kujali kula wala kupumzika. Kwa sadfa alisafiria njia ile ile aliyopitia Pandavas katika siku za zamani alipambana na baridi kali ya Dronasagar.

Safari, hizi za Swami Dayanad katika Himalays zilifanyika hasa kwa matumainio makali ya kuwatafuta mayogi wa kweli na mawalii wanaoishi katika mahali pasipofikika katika mapangoni na mabondeni mwa milima, karibu na vijito vitakatifu na kwenye vilele vya milima, ambapo wamebobea katika ibada zao. Bila ya kujali taabu zake na hatari za kusafiri milimani kwenye wanyama wakali wa mwitu, na bila kujali njaa yake au machofu, yeye alivumilia yote haya peke yake. Yeye hakujali taabu zote hizi kuwatafuta yogi na mawalii ambawo wataweza kumtosheleza kwa ukweli na hekima na hakujali kujitolea kwa chochote ili apate mradi wake. Yeye alikaa Himalayas kwa muda wa karibu miaka miwili.

Katika 1856 A.D. (1913 V.S.) Dayanad alishuka kwenye milima na baada ya kutumia muda kidogo kwenye ufuoni mwa Ganga karibu na Garhmukteshwar, aliondoka kwenda Farrukhabad na kutoka hapo alifika Kanpur. Baada ya kutumia kiasi cha miezi mitano katika safari za kwendea hapa na hapa vijiji vilivyopo katika Kanpur na Allahabad, alipitisha mwezi mmoja Vindhyachala na tena hapo alikwenda Kashi (Varanasi) ambako yeye alibaki kwa muda wa wiki mbili hivi na aliweza kuzungumza na mapandit wataalamu.

Tena hapo alikusudia kuitembelea sehemu za misituni za mikoa ya kati na mwanzo wa Narmada na baada ya kuona mwisho yeye alikwenda kusini katika mwanzo wa mwaka wa 1857 A.D. (1914V.S.) Katika safari hii pia aliyakuta yale yale aliyoyapata katika safari ya Himalayas. Alipambana na wanyama wengi wakali wa mwituni hasa kwenye milima. Alitumia miaka mitatu katika sehemu hizo. Vipi alitumia wakati wake msituni bado haijulikani. Labda alitumia wakati wake kufanya yoga, kuwa karibu na maumbile ya mwituni na kuonana na Sannyasis. Shri Jayachandra Vidyalankar amefikiria kuwa kajtika wakati huu Swami Dayanand Saraswati alionana na kuungana na wanamapinduzi wa India ya kati na huenda alihusikana na uasi wa 1857. Lakini ujumbe huo haujakubaliwa na waandishi wengine wa maisha ya Swami Dayanand. Swami Dayanand mwenyewe alikaa kimya kuhusu wazazi wake, kwao na maisha yake ya baadaye, japokuwa alitoa habari kidogo kuhusu kazi yake na kufahamisha ujuzi wake wa Himalayas.

Baada ya kupitisha miaka mitatu katika sehemu za Narmada Swami Dayanand aliendelea kwenda kaskazini na akafika Mathura katika 1860 A.D. (1917. V.S.) ambako alitaka kuvisoma vitabu vitakatifu kutoka Swami Virajanand, mtaalamu mashuhuri wa Veda. Ha Virajanand alikuwa na umri wa miaka thamanini. Ijapokuwa alikuwa kipofu, alikuwa pande kizi la bingwa na mtu yoyote alikuwa hawezi kumshida katika kupenda masomo ya Veda. Hata katika umri huu wa utu uzima yeye alikuwa na hamu kufanya kitu cha kufufua dharma ya Veda kote India. Yeye alikuwa na ujuzi kamili wa sarufi ya Veda na elimu ya lugha. Katika pathashala, ambayo aliianzisha huko Mathura, yeye alisomesha vitabu vile tu ambavyo viliandikwa na Rishi wa kale tu. Alipata kujua guru wa kweli na uwongozi, Dayanand alimwomba kumkubali yeye awe mwanafunzi wake na amfundishe maandishi fasihi ya Veda. Virajanand, baada ya kusita kidogo yeye alimkubalia awe mwanafunzi wake na alimwambia avitupe

vitabu vyake vyote katika Yamuna na asahau yote yale aliyoyasoma mpaka sasa. Pia yeye alimwongoza zaidi (Dayanand) ili ajitafutie pakulala na pakula. Kwa bahati nzuri kwa ajili ya Dayanand, Amar Lal Joshi, Brahmin wa Audichya kutoka Gujrat, alikuwa anaishi Mathura. Yeye alikubali kunyanyua mzigo wa Dayanand wa kumlisha na kumpa pakukaa kwa miaka mitatu kamili na kumlisha katika nyumba yake mwenyewe. Mtu mwingine aliyeitwa Hardev alimuahidi kumpa rupia mbili kila mwezi kununua maziwa. Kwa kukaa Dayanand alihitaji chumba kidogo jirani ya hekalu.

Baada ya kufanya mipango ya kutosha ya kukaa na kula, Dayanad alivitupa vitabu vyake vyote katika mto Yamuna, kama alivyoamrishwa na guru wake mpya, na akaanza kusoma. Kwanza alisomeshwa Ashtadhyayi ya Panini na Mahabhashya kwa kuwa na ujuzi wa vitabu hivi viwili. Dayanand aliweza kupata ruhusa ya kuikaribia nyumba ya hazina ya Veda na Vedangas na kufahamu siri za maandishi fasihi za Veda. Pia yeye alivisoma vitabu vingi vingine pamoja na Nighantu, Nirukta, Vedant Sutras na Manusmriti. Katika mwisho wa masomo yake, yeye, kutaka kumwaga Swami Virajanand, alisimama mbele yake na nuru ya jimbo la askofu ya karafu kuwa kama guru-dakshina (ujira unaolipwa na mwanafunzi kwa mwalimu wake anapomaliza muda wa masomo yake). Lakini Swami Virajanand hakukubali kupokea karafuu zake. Yeye alimwomba kujitolea maisha yake kwa kuanzisha fahari ya masomo ya zamani na kwa kuweka dini ya Veda katika Aryavarta. Yeye aondoe madhehebu na atoe wazi ujumbe wa Veda katika dunia nzima. Yeye awe tayari kufa katika utume wa kuiweka dharma ya Veda katika hali ya utukufu kama ilivyokuwa hapo zamani za kale. Dayanand alitoa idhini kwa ombi la guru wake bila ya kusita hata kidogo na akatamka maneno haya: "Upendavyo tafadhi". Tena hapo yeye alionyesha heshima kwa guru wake kwa kumwangukia miguuni pake na akaondoka kwenda Mathura katika Aprili, 1863 (1920 V.S.)

Baada ya kutoa idhini ya kujitolea kufanya kazi ngumu kabisa ambayo ilitaka ustahmilivu na bidii, na kuupiga moyo konde na busara, Dayanand alifika Agra ambako yeye aliwasomesha mawalii maadili ya Sandhya na aliwanasihi waimbe Gayatri mantra. Na kuwa na kusudio hili moyoni, yeye aligawanya vitabu vidogo vidogo kwa maelfu vya Sandhyopasana. Yeye pia aliwafundisha watu umuhimu mkubwa wa kujizuia wenyewe na kujinyima na wasiwe na tamaa. Kutoka Agra yeye alikwenda kuitembelea Dholpur, Lashkar, Gwalior, Karauly, Jaipur na Pushkar. Katika Jaipur yeye alikuwa na mahojiano na Pandits wa madhehebu ya Vaishnavi ambamo yeye aliweza kuwashinda wote. Katika Pushkar yeye aliyahujumu vikali madhehebu ya Viashnavi na Shaiva na kulaumu watu wanaoabudu sanamu. Yeye alisema Mungu hana umbo lolote, na kwa hivyo kuabudu masanamu ni kama kipofu anaye papasa gizani. Juu ya hayo, kuabudu sanamu, kwa mujibu wake, imewapotosha jumuia ya Hindu. Pahali pengine alipopatembelea palikuwa ni Ajmer, ambako yeye alijadiliana na kushindana na Maulvis wa kiislamu na mapadri wa Kikristo kuhusu Mungu, asili ya maisha na roho ya mtu kuingia katika mwili mwingine mtu afapo. Ilikuwa katika Ajmer

ambapo alianza suali hili la kuwahifadhi ngombe na akamtia moyoni Col. Brook haja ya kupiga marufuku kuchinjwa kwa ng'ombe kwa sheria.

Baada ya miaka mitatu hivi Swami Dayanand alirudi Mathura na akaonana na guru wake na akamtunukia yeye guinea mbili na kipande cha kitambaa. Pia yeye aliweza kuyalipa baadhi ya madeni yake. Katika 1866 A.D. (1923 V.S.) Kumbha Fair ilifanywa katika Hardwar. Swami Dayanand pamoja na Brahmacharis na Sannyasis wengi walifika Hardwar na akapiga hema lake, na akatia alama ambayo aliandika 'Pakhand Khandani Pataka, Yeye alikuwa navyo vifaa vizuri vya vitabu pamoja naye, na kwa wakati huo alikuwa ameshapata kitabu cha Veda kutoka Ujerumani. Yeye alikuwa mtu wakuvutia na elimu yake ya Veda na maandishi mengineyo ilikuwa madhubuti hata mamia ya watu walianza kujikusanya kwenye hema lake, ambalo lilipigwa kwenye umbali wa maili tatu kutoka mjini kusikiliza hotuba zake. Yeye alianza hotuba zake kwanza kwa kusoma mantras (beti) kutokana na Veda na alishikilia umoja wa Mungu na kutokuwa na faida ya kuabudu sanamu. Yeye pia aliwahoji Puranas na tabia nyingi za kienyeji za Hindu. Yeye pia aliwasisitiza wasikilizaji wake umuhimu wa vitendo vizuri, kwa sababu bila hivyo mtu yoyote hawezi kupata faraja na wokovu. Yeye aliwaambia wazi wasikilizaji wake kama haimkiniki kamwe kufuta dhambi kuwa safi kwa kujitumbukiza katika mito mitakatifu kwa pamoja huku kutojali kufuata njia za haki na ukweli. Wasikilizaji wake walizisikiliza hoja yake na majadiliano kwa furaha na makini. Matokeo yalikuwa kama haya na watu walianza kufika kwa wingi zaidi kwenye hotuba zake na umashuhuri wake ukaanza kuenea mbali na kwa upana pia.

Alipokuwa Hardwar Dayanand alisikitishwa kuona tamasha na fahari za masadhu na maonyesho ya mali na utajiri wa mamahant na maaskofu. Yeye alichukizwa sana hata akaamua kuepukana na vitu kidogo tu alivyokuwa navyo, kama nguo kidogo, vitabu na pesa kidogo. Aligawa vitu vyake vyote papohapo, alimpelekea Mahabhashya, kitambaa kirefu na rupia 35 guru wake na akabaki na kitambaa cha kiunoni tu kwa ajili yake mwenyewe. Hivyo ndivyo alivyoviwacha vyote na akaanza safari zake za kuhutubia na kueneza risala za Veda. Kutoka Hardwar yeye alikwenda Farrukhabad na kutoka hapo alikwenda Anupshahr ambako wafuasi wengi wa madhehebu ya chakrankit - tawi la madhehebu ya Vallabha walionana naye na waliwacha kushika itikadi zao. Katika Ramghat Brahmin mmoja aliathirika sana na majadiliano ya Swami Dayanand juu ya kuabudu sanamu hata aliwaachilia mbali kufanya hivyo kabisa. Katika Karnavasa yeye alimshinda Pt. Amba Datta na Pt. Hiravallabha, mmoja badaa ya mmoja, katika majadiliano. Pt. Amba Datta alitangaza wazi wazi kama kuabudu sanamu ni kinyume cha mafundisho ya Veda Pt. Hiravallabha alikubali kushindwa na akazitupa sanamu zake zote katika mto Ganga. Pt. Tika Ram alikata uhusiano wake na heikalu, ambako yeye alikuwa askofu, na akapata kazi nyingine. Pt. Angad Shastri alizitupa sanamu zake katika mto Ganga na aliahidi kutoa hotuba za dini juu ya Shrimad Bhagavat.

Katika Karnvasa Swami Dayanand alipambana na Rao Karna Singh, rais

wa Rajput ya Baroli, mfuasi wa madhehebu ya Chakrankit na mfuasi wa Rangacharya, ambaye alikuja kukoga katika Ganga. Mwenendo wa Rajput ulikuwa wa kumdharau Swami Dayanand na akampiga kwa upanga ambao ulikatika vipande viwili. Baadaye Rao Singh aliwapeleka wafuasi wake wawili au watatu wenye silaha za upanga, ili wakamwue Swami Dayanand usiku kwenye hema lake, lakini wao pia hawakuweza kufaulu katika kazi hiyo. Pigo hili la kutaka kumwua Swami Dayanand lilileta rais nyingine ya Rao Krishna Singh kumhifadhi na kumwunga mkono Swami. Yeye alishindana na Rajput mwovu na akasema, "Ikiwa utamhujumu Swami tena basi mimi nitakufanya ujute kwa ujinga wako; utachukua kichwa kilicho pasuka tu kutoka hapa." Mke wa Rao Karna Singh alimnasihi aondoke pahali hapo, kwa sababu Kshatriyas wa pahali hapo walikusudia kulipa kisasi. Rao aliogopa na akaondoka pahali hapo. Swami Dayanand, hata hivyo, hakuogopa. Yeye alimwambia Rao Krishna Singh, "Mtu yo yote hawezi kunidhuru mimi. Mimi silindwi na mtu bali Mola Mkarimu ndiye ananihifadhi kila pahali. Usiwe na wasi wasi wangu."

Kutoka Karnavasa Swami Dayanand alikwenda Farrukhabad na kupitia Ambagrah, Shahbazpur na Kaimganj alifika huko katika 1868 (1925 V.S.). *Alibaki hapo kwa muda wa siku kidogo na akaanzisha Pathashala ya kisanskrit* ya kusomeshea maneno halisi ya Veda. Yeye aliwatunukia watu wengi uzi mtakatifu na aliwanasihi awe na imani yakujiunga na Sandhya na Agnihotra. Yeye pia aliwanasihi vijana wengine wasiwe Wakristo, wale waliokuwa na nia ya kugeuza dini. Hapo, pia, Swami Dayanand alikuwa na majadiliano juu ya kuabudu sanamu na mapandit wataalamu ambao walikubaliana naye ya kuwa kuabudu sanamu ni kinyume cha ujuzi wa Veda. Kwa mujibu wa waandishi wengine, ilikuwa hapa Farrukhabad ambapo Swami Dayanand alipokea nakili nne za Veda kutoka Ujerumani.

Kutoka Farrukhabad Swami Dayanand alikwenda Kanpur ambako tena alikuwa anafanya majadiliano na mapandit walioitwa Halder Ojha, Guru Parshad Shukla na Prag Narain Tiwari. Msaidizi wa Komishna, Bw. W. Thaine, aliyasikiliza majadiliano hayo. Yeye alimwunga mkono Swami Dayanand kabisa. Na jambo hili lilimfanya Swami Dayanand kuwa mashuhuri sana katika Kanpur na watu wengi, walianza kumfuata Swami, na wakatupa sanamu zao katika mto. Katika 1869 (1926 V.S.) Yeye aliitembelea Benares (Varanasi) ambako alikuwa na majadiliano na mapandit wa Kashi aliyeongozwa na Pandit Bal Shastri. Majadiliano yalichukua muda wa saa nne na karibu watu elfu hamisini walikusanyika kuja kusikiliza. Kwa bahati mbaya mkutano ulisikizwa na Maharaja Ishwari Prasad Narain Singh, mtawala wa Kashi, ambaye yeye mwenyewe akiabudu sanamu, alikuwa mshupavu na afuataye kwa bidii kabisa. Yeye pia aliamua kuwaunga mkono mapandit. Swami Dayanand alijionea huzuni kwa tabia ya kinyama na mbaya ya mapandit na uamuzi mbaya wa mtawala wa Kashi. Hata hivyo, magazeti yalimuunga mkono na yakatangaza kuwa yeye ndiye aliyefaulu. Pioneer, katika tangazo lake lilimwita Swami Dayanand kama Luther wa India. Ukweli ulijulikana na wote. Maharaja Ishwari

Prasad Narain Singh alimwalika Swami kwenye Qasri na akamwomba msamaha kwa tabia yake mbaya wakati wa majadiliano. Pandit Bal Shastri pia alikidhi kwamba ilikuwa si haki yeye kushindana na Swami Dayanand katika majadiliano. Baada ya kukaa Khasi kwa mwezi mmoja na kuwasihi watu wamwabudu Mungu mmoja, Swami Dayanand aliondoka kwenda Prayag ambako maelfu ya watu walikusanyika kwa mkutano na Kumbha Fair. Kwa wakati huu yeye alikuwa ameshakuwa mtu mashuhuri kabisa na watu walikuwa na hamu ya kumwona na kusikiliza hotuba zake. Yeye aliwafahamisha umuhimu wakumwabudu Mungu ambaye hana umbo na wala hafanai na kitu, ambaye yuko pote na mwenye enzi zote. Yeye pia aliwanasihi wafanye yoga ambayo huleta afya nzuri na humfanya mtu awe na imani. Yeye aliwanasihi Mahindu kutoingia katika Ukiristo, Maharshi Devendra Nath Thakur, ambaye pia alikuwa amekuja Prayag kwa mkutano wa Kumbha Fair, alionana na Swami Dayanand na akamwalika kuitembelea Calcutta. Swami Dayanand alikubali kwa furaha mwaliko huo. Kutoka Prayag yeye alikwenda Mirzapur na akaanzisha huko Pathshala ya Veda ya Kisanskrit. Tena Yeye alitembelea Kashi na baada ya kutoa hotuba nyingi za dini na kuanzisha Pathshala basi hapo alifika Anup Shahr tena katika 1870 (1927 V.S.) katika wakati wa Sherehe za Vijayadashami (Dasehra). Yeye alitoa hotuba nyingi kuonyesha kinyume cha Ramlila na akatetea kuwa watu wa kawaida wanaume na wanawake wasiwaigize Rama na Sita ambawo ni wakuu. Yeye alilaani vitendo vya Shraddha-Karma. Yeye alisema kupinga kwa kuabudu sanamu na akawashawishi watu wamwabudu Mungu asiye na umbo na wala hafanani na kitu. Brahman mmoja alikasirika sana na hotuba za Swami Dayanand hata akampa sumu katika tambuu. Swami Dayanand alipokuja kujua kama amepewa sumu, yeye alitapika kwa kufanya riyadha za yoga. Brahman huyo, alikamatwa na tehsildar wa kiislamu na akaletwa mbele ya Swami ambaye alimwachisha na akamwambia tehsildar kama yeye hakuja hapo kuwakamatisha watu bali amekuja kuwafungulisha. Tehsildar alistaajabishwa na moyo mkuu wa Swami Dayanand.

Katika baadhi ya hotuba zake alizozitoa katika Anup Shahr, Swami Dayanand alizungumza siasa pia na alisema suali la kuchinja ng'ombe. Yeye alitaka kuchinja ng'ombe kusiruhusiwe kwa sheria. Yeye pia alilaani uendeshaji wa kazi wa kiingereza katika India na akaomba kuwa kuanzishwe kwa sharia Yeye pia alilaani gram-panchayats na nyaya-panchayats, i.e. mahakama ya vijijini. Katika 1872 (1929 V.S.) Swami Dayanand alifika Calcutta kupitia. Munghhyr na Bhagalpur na alikaa huko kwa muda wa miezi mitatu na nusu. Wakati wake huu aliokaa Calcutta alionana na wataalamu wengi wa Kibengali na akatoa hotuba nyingi ambazo zilitangazwa katika magazeti ya kienyeji na zikajadiliwa hadharani na majumbani. Yeye aliweza kuonana na watu maalum kama na wakuu wa Brahmo Samaj, kama Maharshi Davendra Nath Thakur, Babu Keshav Chandra Sen, Hemchandra Chakravarti, Naryan Basu. Yeye aliweza kuzungumza bila kujicha kitu juu ya elimu ya kuchunguza asili ya kila kitu na elimu ya kiroho na ujuzi wa Veda. Hotuba za Swami Dayanand zilihudhuriwa vizuri na watu huko Calcutta na safari ya Calcutta ilikuwa ya

mafanikio mengi. Mpaka sasa hotuba zake zote zilikuwa katika Sanskrit. Alipokuja kujua kwamba wakalimani wake wa hotuba zake walikuwa hawazifasiri hotuba zake sawa sawa ili watu wapate faida, yeye, baada ya kuelezwa na Keshav Chandra Sen, alikubali kusema katika Hindi siku za mbele atoapo hotuba zake. Yeye pia alikubalia ombi la Keshav Chandra Sen ili awache kuvaa Kaupeen na aanze kuvaa nguo hadharani na faraghani. Yeye alivaa dhoti yenye pindo, alijiviringa na kitambaa na kuvaa viatu.

Siku ya Aprili, 1873 (1930 V.S.) Swami Dayanand aliondoka Calcutta na kwenda Kanpur kupitia Hooghly, Bhagalpur, Chhapara, Patna, Dumraon na Prayag. Alipokuwa Hooghly yeye alimshinda Pandit Taracharan katika majadiliano ya kuabudu sanamu. Pia yeye alizungumza varnashrama katika hotuba na akasema kama katika siku za zamani varna walikuwa hawategemei uzazi tu bali na shughuli na uchumi pia. Katika Patna yeye alitoa hotuba mbili na katika hizo zote mbili yeye alilaani vikali kuabudu sanamu sherehe za Shraddha na za pinda-dan. Katika Chhapara yeye alipokelewa kwa shangwe na aliwekwa katika Dakbungalow karibu na Shiva Gulam, mwenye ardhi wa kienyeji. Pandit Jagannath, aliyejulikana kwa utaalamu wake na kwa ucha Mungu alishindwa katika majadiliano. Kutoka Kanpur Swami Dayanand alikwenda Lucknow na kutoka hapo alikwenda Aligarh ambako Sir Syed Ahmed Khan alikuja kumwona na kumwuliza vipi kafara inaweza kusafisha hewa. Yeye alimtosheleza Sir Syed kwa kumpa mfano wa nafaka zilizopikwa na kutoa harufu nzuri zilipoiva. Hapo Aligarh Raja Jai Krishan Dass alikuwa mfuasi wa Swami Dayanand na akamwomba kuzichapisha hotuba zake katika vitabu.

Mwanzoni wa Januari, 1874 Swami Dayanand alifika Mathura na alishindana na Rangacharya, mkubwa wa madhehebu ya Chakrankit, kuhakikisha kwamba kuabudu kwa sanamu ulikubaliwa na kufanyika na MaAryan wa Veda, lakini wapili hakukubali kushidana. Swami alipokuwa Mathura, mipango ilifanywa ya kumuua lakini haikufaulu. Yeye aliondoka Mathura na akafika Benares (Varansi) ambako alipitisha siku zake za joto na akaanza kuandika Satyarth Prakash, tahriri ya kwanza ambayo ilichapishwa kwenye Light Press na kupigwa chapa katika 1875 kwa hisani ya Raja Jai Kishan Dass. Julai 1, yeye alifika Prayag na baada ya kukaa kwa muda wa siku kidogo aliondoka kwenda Bombay ambako alikuwa anapokea mwaliko mara kwa mara. Hotuba yake ya kwanza Bombay ilikuwa 25 Novemba 1874, lakini ilikwishia kwa mzozo kwa sababu wafuasi wa madhehebu ya Vallabh walikataa hoja zake na maoni yake ya kutoabudu sanamu Gosain Jiwaji, mkubwa na madhehebu ya Vallabh, hata walijaribu kumnywisha sumu na mfanyi kazi wake Baldev lakini matayarisho ya kihaini hayakufaulu. Katika hotuba yake ya pili katika Bombay, Swami Dayanand alizungumuza historia ya zamani ya Maarya na akawalaumu watawala wa Aryan kwa kuanguka kwa Aryavarta. Katika mwisho wa hotuba yake yeye aliwafanyia mzaha na aliwaeleza watawala wa dini pia. Hotuba hii ilikuwa ya kustaajabisha kwa kupigia vijembe na mzaha na ikaleta mzozo

mkubwa kwa watu waliohudhuria. Wasikilizaji waliathirika sana na kuvutika.

Katika Bombay Swami Dayanand aliandika na kuchapisha baadhi ya vitabu na vijitabu ambamo aliihujumu madhehebu ya Vallabh na madhehebu ya Narayan Swami. Yeye pia alianza kuandika Samskar Vidhi na Rig Vedadi-Bhashya Bhumika, Dr. R.G. Bhandarkar, mtaalamu akijulikana wa Kisanskrit, pia alionana naye kuzungumza juu ya kumwamini Mungu mmoja, katika Veda. Lakini kazi muhimu zaidi ya Swami Dayanand katika Bombay ilikuwa ni kuanzisha Arya Samaj ambayo ilianza kazi zake katika Aprili, 10, 1875 (5th ya Chaitra Shukla, 1932 V.S.) Madhmuni na mradi wa Arya Samaj ulizungumza kwa urefu na mwishoni sharti ishirini na nane zilipasishwa ili ziwe uwongozi kwa wafuasi wake wafuate. Baadaye Swami Dayanand alizipunguza sharti hizi ziwe kumi tu. Maskani ya Arya Samaj katika Bombay ilifuatwa na maskani nyingi zaidi ya mia katika mahali pengi huko kaskazini mwa India.

Baada ya kufanya maskani ya Arya Samaj huko Bombay Swami Dayanand aliitembelea Poona ambako alialikwa na Mahadev Govind Ranade na Mahadev Moreshwar Kunte. Hapo Poona yeye alitoa hotuba kumi na tano. Thelathini na tano alizitio mahali pengine. Baadaye hotuba zote hamsini zilikusanywa na kupigishwa chapa na kufanywa kitabu katika lugha ya Marathi. Baada ya kupitisha robo ya 1875 katika Poona, Satara, na Bombay yeye aliondoka kwenda Baroda ambako mipango ya kukaa kwa raha ilitayarishwa na serikali. Yeye alihutubu kila siku kwenye jengo la dharamshala hapo. Kutoka Baroda yeye alirudi Bombay katika mwezi wa Machi, 1876 (1933 V.S.) na akatoa hotuba nyingine hapo. Sasa yeye alikuwa anasema lugha rahisi ya Hindi ijapokuwa ilikuwa ina changanyika mara nyingi na maneno au mafumbo ya Kisanskrit. Katika Aprili, yeye aliondoka Bombay na baada ya kutumia siku kidogo huko Indore aliendelea kwenda Farrukhabad kuanzisha mambo ya Arya Samaj katika Uttar Pradesh. Katika Muradabad yeye alikuwa na mashindano na Askofu wa Kiingereza ambayo yalichukua muda wa wiki mbili. Miezi michache ijayo ilitumika katika kuitembelea Banares, Jaunpur, Ayodhya, Lucknow, Shahjahanpur, Bareilly na Karnavase. Katika Januari, 1877, Lord Lytton wa Darbar ya Delhi kuonyesha uzuri na utukufu wa Utawala wa Kiingereza. Swami Dayanand alifikiria kuwa wakati umefika wa kueneza ujumbe wa Veda, na akafika hapo. Aliitisha mkutano wa waanzishaji katika matengenezo katika jamii, pamoja na Sir Syed Ahmed Khan na Keshav Chandra Sen, na wakashauriana kufanya kazi kwa kuungana kwa maendeleo ya nchi, lakini mashauri yake hayakubaliwa na wengine, na kwa hivyo, mkutano haukufaulu mwishoni.

Kutoka Delhi Swami Dayanand alirudi Uttar Pradesh na kupitia Meerut na Saharanpur akafika Shahjanapur katika Marchi, 1877, kushiriki katika majadiliano ya dini ambayo ilimalizika katika siku mbili bila ya kufaulu. Sasa aliamua kwenda Punjab ambako alikuwa amealikwa mara nyingi. Alifika Lahore na akatoa hotuba yake ya kwanza huko Aprili 25, 1877 (1934 V.S.) ya kuwafafanulia zaidi juu ya Maveda na elimu ya Veda. Yeye alianzisha tawi la

amaj huko Lahore mwezi wa June tarehe 24, 1877 (Jyeshtha Shukla 13, .S.) Tena hapo alikwenda matembezi ya kutoa hotuba na akaitembelea vijiji vya Punjab, kama Amritsar, Jullundur, Gurdaspur, Gujranawala, Rawalpindi, Multan, etc. Kila pahali alipokwenda mamia ya watu unguka kuja kusikiliza hotuba zake na jambo muhimu hasa la kusema kila ikuwa juu ya kuabudu sanamu, maveda, tabia za jamii, za Veda etc. ishwa kuwa Mahindu hawasomi vitabu vyao vya dini sawa sawa na mu vyema dini yao wenyewe. Hesabu ya hotuba ambazo Swami ınd alizitoa katika muda wa mwaka mmoja huo katika Punjab zilikuwa kuliko alizotoa pahali pengine po pote.

ada ya kuondoka Punjab Swami Dayanand alitumia miezi michache masharīki ya Rajasthan na tena kisha akarudi Uttar Pradesh na pia ɔelea baadhi ya miji ya Bihar. Kutoka Februari 20 mpaka Aprili 14, 1879 S.) alipiga hema Hardwar, ambako tena kulikuwa na Kumbha Fair tena. ya kurudi kutoka Hardwar alitumia nusu ya mwisho wa mwaka belea miji ya mashariki na ya magharibi ya Uttar Pradesh na akianzisha ya Arya Samaj. Miji mikuu ya hapo ilikuwa Saharanpur, Meerut, h, Moradabad, Badayun, Bareilly, Shahjahanpur, Lucknow, habad, Agra, Mirzapur na Benares katika Uttar Pradesh na Danapur Bihar.

ıda ya safari zake nyingi za wilaya na majimbo ya Kiingereza kwa muda ka kumi na sita na kueneza risala za Veda, Swami Dayanand alikata shauri da Rajasthan ambapo alikuwa amepata barua nyingi za mwaliko kutoka tu mbali mbali binafsi na pia kutoka kwa vyama vya huduma za jamii na ɔka kwa watawala wa nchi kama kawaida, alifika Bharatpur mwezi wa 10, 1881 na baada ya kukaa kwa muda wa siku kumi na kutoa hotuba zake ı dharma kwa watu, aliondoka kwenda Ajmer kupitia Jaipur. alipokuwa ılitoa hotuba nyingi na tena alikwenda Masuda ambako Alijadiliana na :o na Majain juu ya mambo ya dini. Hapo pia alizitunukia nyumba nyingi uzi takatifu. Kutoka hapo yeye alikwenda Chittore. Maharana Sajjan limpokea kwa heshima kubwa na akafanya matayarisho yake ya kukaa ukingo wa mto Gambhiri, karibu na Chittore. Watu wa eneo hilo keza kwa wingi kuja kuzisikiliza hotuba zake na waliathirika sana. ına Sajjan Singh na Maharaj Nahar Singh wa Shahpura walionana na Dayanand mara nyingi na kujadiliana naye juu ya dini na siasa.

ıtoka Chittore Swami Dayanand ilimbidi kwenda Bombay kushiriki shughuli za kila mwaka za Arya Samaj, lakini kabla hajaondoka aliahidi Udaipur. Alipokuwa Bombay alipitisha wakati wake wote kwa kuandika yake na maelezo juu ya Rigveda ambayo yeye aliianza baada ya kumaliza na maelezo juu ya Yajurveda. Katika mikutano mingi hapo Bombay umza juu ya kuwalinda ng'ombe na mwishoni kumpeleka Malkia wa za kumbukumbu za majina ya watu kwa malakhi. Lakini mpango huu

haukufaulu kwa sababu ya kifo chake kisichotazamiwa. Baada ya kukaa kwake Bombay kwa muda wa miezi michache Swami Dayanand alirejea Udaipur kupitia Khandwa, Indore, Ratlam na Jaora. Maharana wa Udaipur kwa sasa alikuwa amemzoea sana na alimweka kwa hadhi kubwa. Kwa kuomba kwake mwenyewe Swami Dayanand alimsomesha Sanskrit kwa njia iliyo rahisi kabisa hata aliweza kuifahamu manusmriti na kuisoma kwa mahadhi Mahabharat. Swami aliweza kuzigeuza tabia zake. Ulijizuia kwa tabia za uchu na akatoa ruhusa ya kuwa agnihotra yajan ifanywe katika kasri yake.

Baada ya kukaa Udaipur kwa muda wa zaidi ya miezi sita Swami Dayanand aliondoka kwenda Shahpura na alikaa huko kutoka Machi 9 mpaka Mei 23, 1883 (1940 V.S.) Maharaja Nahar Singh, mtawala wa Shahpura, alikuwa anampenda sana Swami na, kadi siku alikuwa huko Shahpura Swami alionana naye kwa muda wa saa tatu kila siku kusoma maandishi matakatifu na kuzungumza juu ya mambo mbali mbali. Yeye angependa Swami Dayanand abaki katika utawala wake kwa muda wa miezi michache zaidi, lakini Swami Dayanand hakuweza kufanya hivyo, kwa sababu alipokea mwaliko kutoka His Highness Maharaja Jaswant Singh wa Jodhpur ya kuutembelea mji wake. Maharaja Nahar Singh hakupenda Swami Dayanand aende Jodhpur. Yeye alikuwa nazo sababu zake mwenyewe. Maharaja Jaswant Singh alikuwa ameushirki ulevi na wanawake na pia alikuwa anampenda sana mcheza ngoma wa kike aliyeitwa Nanhi Jan. Baada ya hayo, Waislamu wa Jodhpur hawatapenda Swami aseme na kuwalaumu vikali kupinga Uiislamu. Lakini hakuweza kumzuia Swami Dayanand asiende Jodhpur, kwa sababu hata kitiso cha kifo wala upinzani mkali usingeweza kumfanya ageuze njia aliyoichagua.

Swami Dayanand alifika Jodhpur Mei 31, na akabaki huko mpaka Oktoba 16, 1883 (1940 V.S.) Aliwahutubia umati kila siku kutoka saa kumi mpka kumi na mbili za jioni na kuwambia mambo mengi ya hotuba. Alitilia mkazo sana kwenye tabia nzuri hasa kwa Rajputs. Yeye aliwalaumu watawala wa Rajput kwa kuwa maasherati na walevi. Lakini kwa kusema kweli na kuwalaumu watu wa heshima yeye alijifanyia madhara ya kupata adui wengi katika Jodhpur. Waislamu, wafuasi wa madhehebu ya Chakrankit na Hindu wenye kuabudu sanamu walikuwa wameshaanza kumchukia. Nanhi Jan, kipenzi na mcheza ngoma, wa Maharaja, pia alianza kuwa adui wake, kwa sababu yeye, baada ya kumpiga vijembe, akawa mwenye hofu katika qasri ya kuweza kubaki huko. Tena zaidi ya hayo, yeye aliandika barua kali kwa Rao Raja Pratap Singh, kaka wa mtwala, kumwonya yeye na mtawala kwa kuharibu sifa zao na kupoteza nguvu zao kwa kushirika mambo ya uchu. Maharaja, kwa upande wake, alipuuza onyo hilo la Swami Dayanand na katika kukaa kwake hiyo miezi minne katika Jodhpur yeye alimtembelea mara tatu tu. Yeye hakuweza kuuwacha ulevi, wala hakuweza kuwachana na Nanhi Jan. Swami Dayanand alifikiri ujumbe wake wa Jodhpur haukufaulu. Yeye, kwa hivyo, alifanya mipango ya kuondoka Jodhpur tarehe 1 October 1883 kwenda Masuda katika Ajmer na mipango yote ya safari yake ilikuwa iko tayari. Lakini, kwa bahati mbaya, alishikwa na maradhi makali tarehe 29 Septemba. Inasemekana kama alipewa sumu na maadui zake

kupitia mahishi wake. Kwa shaka ya kuwa amepewa sumu, alijaribu kuitapika sumu hiyo kwa kunywa maji mengi na kufanya yoga lakini hakuweza kufaulu. Dr. Surajmal aliitwa, lakini matibabu yake hayakumfaa kitu. Baada ya siku kidogo hali ya Swami Dayanand ilizidi kuwa mbaya na akawa mgonjwa zaidi tena hapo daktari wa Kiingereza wa utawala wa hapo aliwanasihi kuwa apelekwe Mount Abu. Wakati huo wa kuondoka Swami Dayanand kutoka Jodhpur siku ya Oktoba 6, Maharaja na kaka yake Sir Pratap Singh walikuja kumwona na walisikitishwa sana kuona hali yake. Maharaja alimwomba Dr. Surajmal amfuate Swami Dayanand mpaka Mount Abu.

Swami Dayanand alifika Abu asubuhi ya Oktoba 21, 1883 (1940 V.S.) lakini ilivyokuwa hali yake haikuendelea kuwa nzuri, yeye pamoja na wafuasi wake, alipelekwa Ajmer tarehe 27 Oktoba. Hali yake ilizidi kuwa mbaya na akavuta pumzi zake za mwisho saa kumi na mbili za jioni Oktoba 30, 1883 A.D. (Amavasya ya Kartik 1940 V.S.) Wakati huo watu wa kaskazini mwa India walikuwa wanajitayarisha kuwasha taa za Dipawali, lakini mwangaza mkubwa ambawo ungeangaza dunia kwa muda mrefu zaidi ulizimwa kwa mkono adui wa ajali.

Picha fupi ya maisha ya Swami Dayanand inaonyesha kazi kubwa ajabu iliyofanywa kwa kuhuisha dini ya Veda na ustaarabu. Yeye alijaribu kurudisha tena ufahari wa India iliyopita na kuwatia moyo vijana waliosoma wa nchi hiyo na kuwa sihi waushike urisi tajiri walioritbishwa na hivyo ndivyo aliweza kuwaokoa kutokuwa mateka wa upotovu wa utamaduni wa magharibi. Maisha yake yote yalikuwa marefu na ya shughuli nyingi ya kuondoa ujinga, tabia za kuchukiza za jamii na vitendo vya dini vya kuchukiza. Yeye alijaribu kutengeneza na kujenga tena maisha ya kijamii na ya kidini ya dini ya Hindu ambayo imekuwa yenye maana moja ya kuwaida na kanuni za dini, isiyo ya akili na fundisho za kanuni za elimu ya dini au madhehebu. Yeye aliweza kujulia sawa sawa taabu na huzuni ambazo mtu mwema alikuwa anavumilia na kwa uthabiti alitoa njia iliyo sawa na yenye faida ya kufuatwa kwa jambo hilo. Kwa ajili ya kutochoka kwake yeye aliweza kuziregeza pingu zilizo tia nanga ambazo zikirudisha nyuma maendeleo ya jamii. Yeye aliwaamsha Hindus kutokana na uelegevu na akawajaza wao na matumainio ya moyo na fahari na uthabiti wa utukufu uliopita. Yeye ilimpasa kupambana upinzani na mashutumu ya uchongezi lakini yeye alibaki shwari na hakuudhika kamwe. Yeye alikuwa amejaliwa na utakatifu na utulivu, ujuzi na elimu, huruma na uzuilifu wa tamaa wa Marishi wa kikale. Aurobindo Ghosh alimwita kwa ukweli "askari wa mwangaza, shujaa katika dunia ya Mungu, mchoraji wa watu na kawaida zao, shujaa na mshindi mkali wa shida ambayo huweza kuifika roho" na mtu mwenye kuwa na Mungu katika roho yake, mwenye kuona busara katika macho yake na nguvu katika mikono yake ya kuichonga busara nayoiona katika macho yake. Robindra Nath Tagore pia, kwa kumsifu Swami Dayanand, alisema kwamba Swami Dayanand alikuwa shujaa mkubwa wa uongozi katika India ya Kisasa - ambaye kwa kuishangaza misitu ya imani na mazoezi - na uzito wa kutoendelea wa kuwa siku mbaya zaidi za nchi yetu - aliiongoza njia iliyonyooka ambayo iliwaongoza Hindus kwenye njia rahisi ya maisha yenye busara ya kumtumikia Mungu na binadamu.

Kazi kubwa za Swami Dayanand ni:-

Tafsiri za Rigveda na Yajurveda

Ashtadhyayibhashya

Utangulizi wa tafsiri ya Rigveda

Satyarth Prakash

Aryabhivinaya

Satyadharmavichar

Sanskarvidhi

Panchmahayagyavidhi

Kashishastrarth

Aryoddeshyaratnamala

Vyavaharabhanu

Veda - viruddh - mata - khandan

Bhramochchhedan

Gokarunanidhi

Bhranti - nivararnam

Shastrarth Ferozabad

Anubhramochchhedan

Vedantadhwanta - nivaran

Swami Narayana - mata - khandan

Vedangaprakash, sehemu kumi na nne (kamili)

Sanskrit - vakya - prabodh

## YALIYOMO


| | Ukurasa |
|---|---|
| **UTANGULIZI** | 24 |
| **SURA I** | 29 |
| Maelezo ya Aum | 29 |
| Maneno yanayotoa maana | 30 |
| Majina 100 ya Mungu | 32 |
| Maana ya Kwanza | 31 |
| Nirguna na Saguna | 42 |
| Muhtasari | 45 |
| **SURA II** | 47 |
| Kawaida za kula wakati wa mimba | 47 |
| Wakati wa mtungo wa mimba | 47 |
| Uzazi | 47 |
| Uongozi wa utoto | 48 |
| Kuwafunza watoto na wamama | 48 |
| Elimu ya watoto | 49 |
| Uchawi | 49 |
| Unajimu | 50 |
| Ndui na uchawi | 51 |
| Elimu ya alkimia | 52 |
| Kutunza nguvu | 52 |
| Onyo la wazazi | 52 |
| Malezi | 53 |
| Mafunzo mema | 53 |
| Tabia nzuri | 54 |
| Ukweli na Uadilifu | 54 |
| Hadhari ya kuhifadhi afya | 54 |
| Wajibu wa wazazi | 54 |
| Muhtasari | 55 |

Ukurasa


| | |
|---|---|
| **SURA III** | 56 |
| Pato na shirikisho | 56 |
| Hekima na Ufadhili | 56 |
| Kuingia skuli | 56 |
| Mahali pa skuli | 56 |
| Uchunguzi juu ya tabia | 57 |
| Elimu ya Lazima | 57 |
| Maana ya Gayatri, shairi la imani | 57 |
| Sala | 57 |
| Jinsi ya kuabudu | 58 |
| Kuvuta pumzi nyingi | 58 |
| Injia zake | 59 |
| Daraja zake nne | 59 |
| Faida zake | 59 |
| Taamuli | 59 |
| *Kafara ya Moto* | 60 |
| Zana zake | 60 |
| Faida za Muhanga wa moto | 61 |
| Brahmacharya | 62 |
| Daraja zake tatu | 63 |
| Sehemu nne za mwili | 64 |
| Kanuni za mafunzo | 64 |
| Mafunzo mema | 67 |
| Hakika | 69 |
| Namna nane za Ushuhuda | 69 |
| Tabaka sita | 71 |
| Vitu tisa | 71 |
| Sifa za Akili | 71 |
| Maelezo yao | 71 |
| Mipango ya masomo | 76 |

| | Ukurasa |
|---|---|
| Soma Veda na tafsiri | 80 |
| Vitabu vilivyopendekezwa | 81 |
| Vitabu vilivyokataliwa | 81 |
| Nasiha | 83 |
| Wanawake, Shudra wasome Veda | 84 |
| Muhtasari | 87 |
| Puranas na Upapuranas | 88 |
| **SURA IV** | 89 |
| Harusi, Ndoa | 89 |
| Nani kumwoa | 90 |
| Umri wa kufunga Ndoa | 91 |
| Nani afanye matayarisho ya ndoa | 93 |
| Dhanvantari | 93 |
| Nyumba ya furaha | 93 |
| Maoni ya Veda kuhusu ndoa | 93 |
| Hadhari | 94 |
| Ndoa ya mtu mzima | 94 |
| Ukabila na sifa njema | 94 |
| Wajibu wa mtu wa dini | 98 |
| Wajibu wa Mashujaa | 99 |
| Wajibu wa Wafanyi Biashara | 99 |
| Wajibu wa Wafanya kazi | 100 |
| Aina nane za ndoa | 100 |
| Ndoa ya kustahili sifa | 101 |
| Wakati wa sherehe za kufunga ndoa | 101 |
| Tabia wakati wa mimba | 102 |
| Chakula wakati wa mimba | 102 |
| Kanuni za uzazi | 102 |
| Mapenzi ya watu wawili | 103 |
| Jinsi ya kutendewa wanawake | 103 |

| | Ukurasa |
|---|---|
| Sharti ya kiroho ya kusema kweli | 104 |
| Kazi tano Muhimu | 105 |
| Wajibu wa wazazi | 105 |
| Utumishi wa Wanajimu | 106 |
| Utumishi wa Wakubwa | 106 |
| Utumishi wa Mahakimu | 106 |
| Wajibu wa Viumbe | 107 |
| Wajibu wa Wageni | 108 |
| Uzandiki | 108 |
| Kuamka mapema | 109 |
| Insafu ya kulipiza kisasi | 109 |
| Kusema kweli | 109 |
| Amani na watu kumi na tatu | 110 |
| Watu watatu waovu | 110 |
| Ishara za Uzandiki | 111 |
| Uwezo wa lazima | 111 |
| Furaha na Maumivu | 112 |
| Mume na Mke | 112 |
| Wajibu wa Brahmin wa kawaida | 112 |
| Sifa za Mabwana | 112 |
| Alama za watu wadhaifu | 113 |
| Sifa za wanafunzi | 114 |
| Muwafaka wa kupata elimu | 114 |
| Wajiou wa Kshatriyas, Vaishyas na Shudras | 114 |
| Makosa ya Mume na Mke | 115 |
| Kufunga ndoa tena | 115 |
| Niyoga (harusi Imara) | 116 |
| Veda na Niyoga | 119 |
| Devara au Mume wa Niyoga | 119 |
| Manu juu ya Niyoga | 120 |
| Urithi | 122 |

| | Ukurasa |
|---|---|
| ɜlezo ya ndoa | 122 |
| ɔenda nchi na uaminifu | 123 |
| hanga wa farasi na ng'ombe | 123 |
| 'andiko wa uwongo wa vitabu | 124 |
| uhimu wa kuiendesha nyumba | 124 |
| htasari | 125 |
| dhya au Sala | 127 |
| **ƐA V** | 130 |
| ɩafu | 130 |
| :ati wa ustaafu | 130 |
| :atao | 131 |
| ibu wa Uaskofu au Sannyasins | 133 |
| ɹhimu kumi wa dini | 134 |
| ɪmin pekee anaweza kukataa | 135 |
| :asisi wa kisasa | 136 |
| ɩuti baina ya Mungu na Roho | 137 |
| ɪtasari | 140 |
| **ƐA VI** | 141 |
| ibu wa Mfalme | 141 |
| mashauri tatu | 141 |
| awinazo Raisi | 142 |
| ɪlme wa Kweli | 142 |
| ɔfisa wa Kuu | 143 |
| mashauri | 143 |
| ɪachama wa halmashauri | 144 |
| ɔvu ya ghadhabu | 145 |
| waziri | 146 |
| ɹdhui ya mijadala | 146 |
| ɪuzi wa watu wengi | 146 |
| waziri wenye ujuzi | 146 |
| waziri wa nchi za nje na wa mambo ya nyumba | 147 |

| | Ukurasa |
|---|---|
| Watu muhimu na wajibu wao | 147 |
| Ushuru au mapato | 148 |
| Kanuni za ushujaa | 149 |
| Wajibu wa Watawala | 150 |
| Siasa | 151 |
| Uangamizi wa Milki | 151 |
| Maofisa wa Amani | 152 |
| Kutoza kodi | 152 |
| Kazi ya kila siku ya Mfalme | 153 |
| Namna sita za busara | 153 |
| Mara sita za tabia zake | 154 |
| Vita | 154 |
| Uvamizi | 155 |
| Hila | 157 |
| Namna ya kuwaweka mahabusu | 157 |
| Rafiki | 157 |
| Nguvu zisizoelemea huku wala huko | 158 |
| Wajibu wa Kifalme wa kila siku | 158 |
| Orodha ya Ushuru | 158 |
| Mipango ya mahakama | 159 |
| Vichwa 18 vya sheria | 159 |
| Umuhimu wa Haki | 159 |
| Dhambi za kudhulumu | 160 |
| Mashahidi | 161 |
| Ushahidi | 161 |
| Adabu | 162 |
| Namna ya adabu | 162 |
| Sifa mbaya mno za mtu | 163 |
| Adabu ya kuzini | 163 |
| Ushuru na Bima | 164 |
| Siasa katika Sanskrit | 165 |

| | Ukurasa |
|---|---|
| Muhtasari | 165 |
| **SURA VII** | 169 |
| Mungu | 169 |
| Miungu 33 | 169 |
| Umoja wa Mungu | 170 |
| Dalili ya kuwapo kwa Mungu | 170 |
| Mungu yupo kila pahali | 170 |
| Huruma ya Mungu na haki | 171 |
| Mungu ni Roho | 172 |
| Mungu ni Mwenye Enzi | 173 |
| Mungu ni wa daima na milele | 173 |
| Shauri ya Mungu | 173 |
| Sifu, sala na ibada | 173 |
| Sala | 174 |
| Usafi wa Akili | 174 |
| Faida za sala | 175 |
| Ibada | 176 |
| Yamas na Niyamas | 176 |
| Faida ya Ibada | 177 |
| Wingi wa Mungu | 179 |
| Kufanyika mtu | 179 |
| Kusamehewa kwa dhambi | 181 |
| Uombozi wa Roho | 181 |
| Yenye sifa pekee ya Mungu na roho | 182 |
| Kuona mbele kwa Mungu na uhuru wa mtu | 182 |
| Nafasi ya Roho katika kiwiliwili | 182 |
| Uhusiano wa Mungu na Mtu | 183 |
| Mafunzo ya Veda | 184 |
| Kutokuwa na ujinga wa kutomjua Mungu | 187 |
| Nadharia za Kiveda | 188 |

| | Ukurasa |
|---|---|
| Hitilafu ya Mungu na Roho | 189 |
| Kutokuwapo kutopatana | 190 |
| Bila mapenzi ya Mungu | 190 |
| Veda | 191 |
| Namna ya wahii | 191 |
| Kwa nini Vedas ziko katika Sanskrit | 192 |
| Uthabiti wa wahii wa Kiveda | 193 |
| Umuhimu wa wahii | 193 |
| Asili ya vitabu vya ki Brahmana | 194 |
| Tofauti kati ya Vedas na Brahamanas | 194 |
| Tafsiri za Vedas | 194 |
| Vedas ya Milele | 195 |
| Muhtasari | 196 |
| **SURA VIII** | 198 |
| Kuumba, kutunza, kuangamiza | 198 |
| Tabia au Prakriti | 198 |
| Vitu vitatu vya milele | 198 |
| Sababu za dunia | 200 |
| Kusadiki ulimwengu wote ni Mungu | 200 |
| Tofauti baina ya Mungu na Kitu | 201 |
| Kitu kilichoumbwa | 202 |
| Kuwepo kote kwa Mungu | 203 |
| Hakuna kitu bila ya sababu | 204 |
| Sababu au monad haina sababu | 204 |
| Kutosadiki kwa Mungu | 205 |
| Yuko makatazo yamejibiwa Wakiristo na Waislamu | 205 |
| Asadikiye | 205 |
| Maveda | 205 |
| Mabudha na Majaini | 206 |
| Wanaoamini | 207 |
| Kutokuwapo Mungu bali Roho tu | 208 |

Ukurasa


| | |
|---|---|
| Usawa wa Muumbo | 208 |
| Uthabiti wa elimu sita | 209 |
| Ndovu wa Kipofu Hadithi | 210 |
| Nini Muumbo | 210 |
| Muumbo wa kwanza | 212 |
| Mwanzo wa dunia | 212 |
| Hitilafu za maisha | 213 |
| Pahali alipoumbwa binadamu | 213 |
| Majilio ya MaArya | 214 |
| Dasyus au watu katili | 215 |
| Nguzo ya Dunia | 216 |
| Dunia hulizunguka jua | 217 |
| Dunia zingine zinazokaliwa | 218 |
| Ufalme wa Mungu | 219 |
| Muhtasari | 219 |
| **SURA IX** | 221 |
| Elimu, ujinga, utumwa, uhuru | 221 |
| Laana ya milele na wokovu | 221 |
| Mungu na Roho imepambanuliwa | 222 |
| Roho | 222 |
| Dunia ni wazo | 224 |
| Wokovu na kuwa Mtu | 225 |
| Njia za wokovu | 226 |
| Asili ya roho | 226 |
| Sifa za roho | 227 |
| Roho haijamezwa kabisa | 227 |
| Upanishads juu ya uwokovu | 227 |
| Kurudia uwokovu | 228 |
| Muda wa uwokovu | 229 |
| Roho haijaumbwa | 229 |
| Njia za Wokovu | 230 |
| Njia ndogo | 233 |

| | Ukurasa |
|---|---|
| Njia nyingine | 233 |
| Namna za Wokovu | 234 |
| Kuwa mtu | 235 |
| Ubaguzi wa Hali | 236 |
| Kadhaa na kudra | 237 |
| Usawa kwa wote | 237 |
| Roho za binadamu na za wanyama | 238 |
| Alama za tabia za binadamu | 240 |
| Guna au Sifa tatu | 241 |
| Matokeo ya Tabia nzuri | 242 |
| Muhtasari | 243 |
| **SURA X** | 245 |
| Tabia na chakula | 245 |
| Kazi za Uadilifu | 246 |
| Nywele na ndevu | 246 |
| Vyanzo vya Heshima | 247 |
| Tabia | 248 |
| Safari za kigeni | 248 |
| Safari ya bahari | 249 |
| Namna mbili za chakula | 250 |
| Shudra au wapishi wa kabila duni | 251 |
| Faida za ng'ombe | 252 |
| Chakula cha dini | 253 |
| Kula pamoja | 254 |
| Chakula kilichopikwa na mtu ye yote | 254 |
| Muhtasari | 257 |

Salamu za Unyenyekevu kwa Bwana Mungu, ambaye ni Mkweli, Hodari, au Dhamiri, na Furaha.

## UTANGULIZI

Nilipotoa jumla za nakala za kitabu hiki mara ya kwanza, zilizoitwa Satyarth Prakash, mimi sikuwa mjuzi wa lugha ya Hindi; kwa sababu lugha ya kwetu ilikuwa Gujrati, na lugha niliyoisema wakati wa masomo yangu ilikuwa Sanskrit. Kwa sababu hiyo makosa mengi yalitokea katika nakala hiyo. Lakini kwa kuitumia lugha hii ya Hindi kila mara katika hotuba zangu za dini kumerahisisha na kunipatia mazoezi ya kuisema na kuiandika, ninafikiri ni muwafaka kupigisha chapa tahariri ya pili ya kitabu hiki, baada ya kusahihisha mbinu na maelezo yake kwa mujibu wa kanuni za nahau na saruji ya Bhasha. Tahariri hii ambayo iliyorejewa na kufanywa kubwa zaidi imeleta matatizo kidogo katika mpangilio wa maneno, mbinu, muundo wa sentensi na maudhui kwa jumla; kwa sababu bila ya mabadiliko haya ya lazima ingekuwa vigumu mno kueleza mbinu za ki-Hindi. Lakini hata kwa hivyo hapakutokea tofauti kubwa ya madhehebu ya kidini humo. Vile vile makosa ya kupiga chapa katika tahariri ya kwanza yamesahihishwa katika tahariri ya pili.

Kitabu hiki kimegawika katika sura kumi na nne na kimegawika katika sehemu mbili. Sura kumi za mwanzo kutoka sehemu ya kwanza na sura nne, katika sehemu ya pili.

Tahariri ya kwanza haikuwa na sura mbili za mwisho na moja katika imani zangu kwa sababu kadha wa kadha ambayo sitapenda zitajwe hapa.

Sura ya kwanza inahusu maana na maelezo ya majina ya Mwenyezi Mungu, kama Om na mengine kama hayo; ya pili, ya masomo ya watoto; ya tatu, ya maisha ya mwanafunzi (brahmacharya), ya za kanuni ya mafundisho orodha ya vitabu vilivyokuwa sahihi na ya visiokuwa sahihi na mipango ya masomo; ya nne; kawaida ya ndoa na maisha ya jamii (grihastha); ya tano, maisha ya kustaafu (vanaprastha) na maisha ya ki-mishneri (sannyasta); ya sita, wajibu wa kazi za Wafalme; ya saba, Ma Veda na Mungu; ya nane, ya muumba, kuihifadhi na kuiangamiza dunia; ya tisa ya elimu, ujinga, laana ya milele na wokovu; ya kumi, tabia adilifu na tabia mbaya vyakula vilivyo ruhusiwa na vilivyo katazwa; ya kumi na moja, ya maelezo na makanusho ya imani za watu wa India; ya kumi na mbili, ya kutomsadiki Mungu ya kuamini Budha (kufuata akili za binadamu), kutomsadiki kuwa Mungu yuko na kumsadiki Jaini au sanamu; ya kumi na tatu, ya ki-Kristo, na ya kumi na nne ya kusadiki Islamu. Kitabu kina malizika kwa muhtasari wa dini ki Arya ya kizamani kama ilivyosomeshwa katika Veda ambayo mimi ninayo Imani yangu yote katika humo.

Nia hasa ya kukiandika kitabu hiki ni kuleta ufafanusi hasa ya maana ya maandishi ya Veda ya kawaida. Inathibitisha ya kweli na kuyafunua ya uwongo.

गुरु विरजानन्द दण्डी
सन्दर्भ पुस्तकालय
प्रविष्टि क्रमांक 656

Si kweli ambapo uwongo unatiwa mahali pa ukweli na ukweli kwa uwongo; lakini, kwa kinyume, ukweli umo katika kusema, kuandika na katika kuamini mambo kama yalivyo. Mtu ambaye anapendelea upande mmoja, yuko tayari kudhibitisha uwongo wake kuwa kweli, na ukweli wa dini nyingine zinazoipinga dini yake, kuwa ni uwongo. Yeye, kwa hivyo hawezi kupata dini ya kweli. Kwa hivyo, ni wajibu wa watu waadilifu na wataalamu kuwajulisha watu wote kuwa ni lipi la kweli na lipi la uwongo, kwa njia ya kuandika au kwa kuhutubia hadharani. Hapo ndipo wao wenyewe wataamua lipi zuri na lipi ni ovu, na labda watachagua la kweli na kuwacha la uwongo bila ya taabu yo yote na kwa furaha. Ijapokuwa uwezo wa kufahamu wa ukweli na uwongo ni wa kuzaliwa nawo katika roho ya mtu, hata hivyo maongozi ya nia, ushupavu wa dini, chuki bila sababu, ujinga na hisia nyingine kama hizo humtenganisha na ukweli na kuulemea upande wa uwongo. Lakini kitabu hiki hakina makosa yote haya. Pia, hakuna hata wazo la mbali kabisa la kumuudhi mtu ye yote kwa dhahir na kwa kichini chini; lakini kwa kinyume chake, kitabu hiki kinatoa shauri ya kuwa watu lazima waweze kubagua ukweli kutokana na uwongo. Kwa njia hii tu ndiyo watu wataweza kuendelea kwenye njia ya furaha; ilivyokuwa hakuna kingine isipokuwa kuhutubia ukweli ni sababu ya kuendelea kwa jamii za binadamu.

Makosa yo yote ambayo yamefanyika katika kitabu hiki ambayo si ya uangalifu au katika kusahihisha nakala ya kitabu cha kuchapisha, yataangliwa kwa haraka ikiwa yataonyeshwa kwa nia safi. Lakini sauti ya kutoamini na kuegemea upande mmoja na kuleta ubishano hafifu wa kuharibu ukweli basi yatapuuzwa, na kutojaliwa kabisa. Ijapokuwa, ikiwa mtu anatujulisha jambo ambalo litaleta faida kwa watu wote, na ikiwa mashauri yake yameonekana ni sawa basi yatakubaliwa mara moja tu. Ilivyokuwa kuna wataalamu wengi katika vyama vya dini, watu wa kawaida wanaweza kupata na kufurahia raha na furaha, hasa ikiwa wawache kuegemea upande mmoja na kuukubali ukweli na hekima za dunia, ambazo ni za kweli saa zote na zina faida kwa watu wote, na wao hukataa ambayo ni ya kuhasiri kwa uzuri wao wenyewe na huishi katika amani na wenzi wao; kwa sababu, ugomvi baina ya wataalamu huchochea moto wa chuki na utovu wa adabu na huzidisha shida mbali mbali na hupunguza raha na utuluvu. Hasaara hii ambayo hupendwa na watu wasiojali mambo ya wenzi wao huwatupa watu katika bahari ya huzuni. Mtu ye yote anapotaka kutekeleza jambo zuri kwa ajili ya watu wote huhangaishwa na shida nyingi zinazoletwa na waovu kutaka kumpinga yeye. Kama walivyosema wahenga - ukweli hujuzu daima, lakini si uwongo; ukweli huwâfunguliya njia wataalamu na kutokana na itikadi thabiti ya fumbo hili, wataalamu na waadilifu hawa siti siti kamwe kudhihirisha ukweli wa mambo, na wala hawawi wakavu wa macho kuhusu ukarimu. Huu ni ukweli thabiti kama ulivyosemwa katika Gita. Yaani jitihada zote za kupata maarifa na uadilifu ni kama sumu kwanza lakini hugeuka kinywaji kitamu baadaye. Fikra kama hizo ndizo zilinipeleka mimi kuandika kitabu hiki. Msomaji atayashika anayo ya wafiki baada ya kukisoma kwa makini na kuzifahamu maana zake. Sifa nzuri zote za kitabu hiki zinakubaliana na ukweli ulioko katika dini zote na hazibishani na zingine, na kukataa uwongo na kujipendelea binafsi wa

madhehebu nyingine. Sifa nyingine ya kitabu hiki ni kuwa imefungua wazi siri na uwovu wa madhehebu zote kwa kuwajulisha wote wataalamu na watu wasio wataalamu, ili wao wenyewe wapate kuyafikiria, kumaliza tofauti zao, kuwa marafiki, na fuata dini moja tu iliyo ya kweli. Kama mimi, niliyezaliwa katika Aryavarta na kuishi hapo, mimi sipendelei upande mmoja wa rai za uwongo za dini nyingine, lakini hutetea ukweli tu, kwa hivyo mimi sipendelei wala sipendelei wala sipendelezi, lakini tendea watu wa nchi nyingine na dini zao haki na uadilifu kamili. Mimi ni rafiki wa hawo wanaoujaribu kuikuuza hali ya nchi hii, na wa hawo wanafanya kazi kwa ajili ya nchi nyingine pia, na pia iwe hivyo hivyo, ninavyoona mimi; watu wote waadilifu wanafanya. Ingekuwa mimi nimeegemea dini yo yote, ningekuwa kama hawo waheshimiwa wa kisasa, ambawo wako tayari kutukuza, kuunga mkono wa eneza madhehebu yao wenyewe kuaziri, pinga na kuchokoza madhehebu ya watu wengine. Lakini vitu hivi si vya heshima kwa binadamu. Kwa sababu hiyo ni sifa mbaya ya wanyama duni kuwa wenye nguvu huwa dhuru na kuwawinda dhaifu. Na ikiwa mtu atautumia mwili wake mzima kufanya hayo hayo anayofanya mnyama duni, basi yeye hawezi kujaliwa kuwa mcha Mungu na kuwa na utu, na hakuna sababu yo yote kuwa yeye asiitwe mnyama duni. Yeye ni mtu wa kweli ambaye humhifadhi dhaifu katika nguvu zake. *Lakini yeye anayeumiza hisia za wengine wa kujipendelea nafsi yake, yuko* karibu na wanyama, kama inavyosemekana.

Sura kumi na moja za kwanza za kitabu hiki zimetoa mengi juu ya adabu za dini na tabia za watu wa Aryavarta. Dini waliyoileta ni ya chanzo cha msingi na inafurahiwa na Ma Veda. Watukufu na kwa mujibu huu nimejiweka chini ya dini hii, mafundisho ya buthe ya Puranans ya Kisasa (Hadithi za miungu na vitabu vya elimu ya ulimwengu) na Tantras (Vitabu vya kanuni na elimu ya pepo) ambavyo vimebainishwa na kugiongwa daima kwa nguvu na dharau.

Dini ya Charvaka (kusadiki kuwa hakuna roho) iliyotolewa katika sura ya kumi na mbili, kwa sasa imeshapotea; inafanana sana na Budhism na Jainism katika mafunzo na kusadiki kuwa yuko Mungu na mengineyo, lakini Charvakism tu ndiyo bora zaidi kuliko vyote viwili hata vikichanganywa pamoja. Maenezi yake lazima yajadiliwe na kuchunguliwa; kwa sababu, ikiwa dhana za uwongo zitawachiliwa kuendelea bila ya kuzuiwa basi dunia itapatwa na ghamu. Charvakism ni kama moja ya Jainism na Buddhism na kwa hivyo imedhihirishwa kwa maneno machache katika sura ya kumi na mbili. Jainism ina kubaliana na Charvakism na Buddhism kwa mengi, lakini zinatafautiana katika mambo machache tu; kwa hiyo, inajulikana kama madhehebu mengine kabisa. Habari za mgawanyiko wa kwanza umeelezwa kwa uangalifu katika sura ya kumi na mbili, ambayo pia imeeleza kanuni za madhehebu ya Buddhism na Jainism. Hoja za Buddhism zimetolewa katika "Dipavansha" na katika vitabu vingine, ambavyo vimeufupisha Buddhism. Watungaji wafuatawo wa Jainism walishauriwa katika matayarisho ya kitabu hiki:-

4 Mool Sutras:- (1 Avashyaka Sutra (2) Vishesha Avashyaka Sutra (3) Dashavaikalika Sutra, na (4) Pakshika Sutra.

11 Angas:- (1) Acharanga Sutra, (2) Sugadanga Sutra, (3) Thananga Sutra, (4) Samavayanga Sutra, (5) Bhagawati Sutra, (6) Jnatadharma - katha Sutra, (7) Upasaka Dasha Sutra, (8) Antagadadasha Sutra, (9) Anuttarovaai Sutra, (10) Vipaka Sutra, na (11) Prashnavyakarana Sutra.

(12) Upangas:- (1) Upavai Sutra, (2) Rayapseni Sutra, (3) Jivabhigama Sutra, (4) Pannachana Sutra, (5) Jambudwipapannati Sutra, (6) Chandapannati Sutra, (7) Surapannati Sutra, (8) Niriyavali Sutra, (9) Kepyiya Sutra, (10) Kapabarhisaya Sutra, (11) Puppyyia Sutra na (12) Papyachuliya Sutra.

5 Kalpan Sutras:- (1) Uttaradhyayana Sutra, (2) Nishitha Sutra, (3) Kalpa Sutra (4) Vyavahara Sutra, na (5) Jitakalpa Sutra.

Chhedas:- (1) Mahanishithavrihadvachana Sutra (2) Mahanishithalaghuvachana Sutra, (3) Madhyamavachana Sutra, (4) Pindanirukti Sutra, (5) Ougha nirukti Sutra, na (6) Paryushana Sutra.

10 Payanna Sutras:- (1) Chatussarna Sutra, (2) Panchakhans Sutra, (3) Tadulavaiyalik Sutra, (4) Bhaktiparijnana Sutra, (5) Mahapratyakhnyan Sutra, (6) Chandavijaya Sutra, (7) Ganivijaya Sutra, (8) Maranansamadhi Sutra, (9) Devendrastamana Sutra, (10) Sansar Sutra; na Nandi Sutra, Yogoddhara Sutra pia huhesabiwa katika hivo thabiti.

5 Panchangas:- (1) Tafsiri za vitabu vyote vilivyotajwa hapa juu, (2) Nirukti, (3) Charani, (4) Bhashya. Hizi huitwa sehemu, na hizi pamoja na maneno yenyewe huitwa Panchangas. Katika hivi, MaDhundhiya hawakubaliani na Sehemu. Pamoja na hivi, kuna vitabu vingi vya dini ya Jain. Sura ya kumi na mbili ya kitabu hiki kutoa habari zote za elimu na mafundisho ya dini hii. Vitabu vya Ki Jain vina makosa ya kurudi hayo, kwa hayo mara mia na elfu. Ni tabia yao ya kufikiria kuwa ni kitabu cha uwongo ikiwa anacho mtu wa dini nyingine, au ikiwa kimepigwa chapa tu. Kuamini kwao huku kunachekesha kutosha, kwa sababu kitabu hakiwezi kuwa cha kweli ila kiwe na kiguzo cha Jainism, ikiwa wenye madhehebu yao wanataka wakiamini. Hakika kitabu hicho hakiwezi kuitwa chao na wao hawakiamini na yeyote katika wao. Lakini hakuna hata kitabu kimoja kama hicho ambacho kimetajwa hapo juu kilichokuwa hakijaaminiwa na mmoja au wengi wenye madhehebu ya Jain. Hata hivyo mwenye kuamini kitabu peke yake amehusika kajtika kukanusha au thibitisha madhehebu haya. Lakini kuna baadhi yao, ambawo wakiwa wanajadiliana katika mikutano, wao huanza kubadilisha imani zao za hicho kitabu wanachokiamini wao. Kwa hivyo, inawapasa kuviweka vitabu vyao kwa siri. Wao hawavitoi, wala hawavisomi wala kuvisomesha hawo wanaopingana nawo katika dini. Kwa sababu vitabu hivyo vina mambo mengi ya upuuzi ambayo Ma-Jain hawawezi kuyashika. Kuuacha uwongo huo ni jawabu dhahiri.

Sura ya kumi na tatu inaelezea dini ya Kikristo. Watu hawa huamini katika Biblia kuwa ni kitabu chao cha dini. Yote kuhusu madhehebu yao muhimu yamejadiliwa katika sura iliyosemwa.

Sura ya kumi na nne inaeleza dini ya Mohamed yaani ya Kiislamu. Watu hawa wanaamini Quran ambayo ni kitabu chao cha dini, na mambo muhimu kuhusu madhehebu yao yameelezwa vyema na kuzungumzwa kwa uthabiti na ufupi.

Kitabu kimemalizia kwa muhtasari za muhimu za madhehebu ya dini ya Veda. Msomo wa uangalifu wa kitabu ambacho hakimwingii rohoni mwandikaji au makusudio yake, hakitadhihirisha kabisa madhumuni hasa; kwa sababu kuna sharti nne za kufahamu maudhui sawa sawa, viz, (1) akanksha: ya akili, (2) yogyata:usawa, (3) asatti: matumizi, na (4) tatparya: nia. Yeye anafahamu maana halisi ya maudhui ambaye anayekisoma kwa kufuata sharti nne hizi muhimu. 1. Ya akili (nguvu ya kujulisha fikra au nia) ni maelekeano kati ya msemaji na maneno ya lugha yeye anayoitumia pamoja na maana yake. 2. Usawa (utaratibu) ni maneno yanayofaa kutumika, kama maji yanavyofaa kunyunyuzia. 3. Matumizi (lugha) ni kanuni iliyo sawa sawa ambayo hutengeneza mahali pao. 4. Nia ni sababu ya mwandishi kukiandika kitabu au msemaji ametoa hotuba. Na sababu hii lazima ije kwanza akilini kwa kuifikiria nia. Kuna watu wenye chuki ambawo wana dhana kinyume cha nia ya mwandishi au msemaji. Waungwana hawa kwa kawaida huwa waliojitolea katika dini. Akili zao huwa zimeharibiwa kwa kiza cha ujinga kilicholetwa na waliojitolea katika dini. Lakini tokea mwanzo mimi sitazamii kwa jicho la dhana mbaya ya Puranas, vitabu vya Jain, Biblia, na Koran, kwa hivyo mimi nayakubali yaliyokuwa mazuri na kuyakataa yaliyo na dosari. Mimi najaribu kuwaendeleza Mahindu na mataifa mengine pia. Mimi ninafikiri hata watu wengine pia wafanye hivyo. Hitilafu kidogo za dini hizi zimedhihirishwa hapa. Watu wenye akili timamu wataweza kuamua ipi ni ya kweli na ipi ina dosari kwa kuzilinganisha wenyewe, na kwa mujibu wa akili zao wakubaliane na ya kweli na wayakatae yenye dosari. Ni jambo geni kabisa kwa mtu mtaalamu halisi kuwachocheza watu na kuleta chuki baina yao, na kuwagombanisha na kuwaangamiza. Ijapokuwa watu waliowajinga watafikiria vyengine kwa kukisoma kwa makini kitabu hiki, lakini wataalamu na watu wenye busara tu ndiyo wataweza kukifahamu kitabu hiki na makusudio yake hasa. Kwa thibitisho imara na matumainio mema ya kazi zangu kufaulu, naiweka kazi yangu mbele ya uamuzi wa watu wazuri. Wanaweza kuipendelea bila ya kuegemea upande mmoja ili kuzifanya kazi zangu zifaulu na ziwe za maana kwao. Hivyo hivyo, ni wajibu muhimu wangu na watu waadilifu kudhihirisha ukweli na ukweli mtupu tu. Mwenyezi Mungu, ambaye ni Mkweli, Mjuzi wa yote, Mwingi wa Furaha na wa roho ya ndani kabisa kwa rehema zake, aifanye kazi yangu hii ifaulu! Veruam sat sapientia - neno moja tu linamtosha mtu mwenye akili.

DAYANAND SARASWATI.

UDAIPUR
BHADRAPAD, Bright Fortnight,
1939 A.V.

# AUM

# SATYARTH PRAKASH

## Mwangaza wa Kweli

## SURA I

## MAELEZO YA AUM

Neno Aumkara ni jina zuri sana la Mungu; kwa sababu herufi a,u,m, ambazo zinafanya neno aum, lionyeshe sifa zake nyingi. Kwa mfano a ina maana ya Virat: Mtawala wa ulimwengu, Agni: Mjuzi wa yote, Vishwa: Wa kuwepo kote na kama jina au sifa za Mungu; u ina maana ya Hiranya Garbha: Mwenye kuimarisha nyota na sayari, Vayu, Mwenye Enzi zote, Tejah: Mwenye utukufu wote, na hizo ndiyo sifa za Mungu, na m inayonyesha Ishwara: Mwenyezi Mungu; wa Daima na Milele, Prajna, Mtaalamu wa Dunia yote, na majina kama haya ya Mungu. Kwa hivyo Majina Matukufu yameelezwa wazi wazi katika Veda na katika vitabu vyengine vya falsafa, na katika karina za aya za vitabu vyote majina haya hutokea, hurejea kwa Mwenyezi Mungu pekee.

Swali - Kwa nini si Virat na maneno mengine yafahamike kama vitu vyengine kuliko Mungu. Jee hayo si yana maana kama dunia, na ulimwengu, na vitu vyengine kama hivi; Indra na waliofanana na Miungu, na tangawizi na kama vidonge katika dawa?

Jawabu - Ndiyo. Lakini pia yana maana ya Mungu Muweza.

Swali - Jee wewe huchukulia kama kwamba ni Mungu tu?

Jawabu - La. Nini satwa yako ya kusema kuwa hayo yana maana ya pekee tu?

Swali - Miungu wanajulikana sana na pia wanahesabika kuwa ni bora kuliko wote: na mimi nina chukulia maneno haya na kuyaamini.

Jawabu - Kwani Mungu hajulikani? Jee kuna mtu bora kuliko Yeye? Basi kwa nini wewe huamini kuwa wao ni Miungu pia? Vipi kitu cho chote kitakuwa bora kuliko Mungu, ambaye yeye anajulikana kabisa, na hakuna aliye sawa na yeye? Kwa hivyo pingamizo lako haliwezi kukubaliwa, kwa sababu, halipatikani vyema: Kwa mfano, maana, ikiwa mtu anacho chakula tayari, na hata hivyo bado anaendelea kuomba zaidi basi hawezi kuwa mtu mwadilifu; kwa sababu yeye anajaribu kupata vitu zaidi vilivyo mbali ilhali wewe unavyo vyako karibu nawe. Katika njia hii hii, uthabiti wako ni muhali kama hekima ya mtu yule asiestahiki. Sababu iko dhahiri kuwa wewe huyafuati hukumu ya maneno Virat & C. (ambayo yana maana kama ya Mwenye Enzi pekee, ulimwengu, na vitu vyote vyengine vya maumbile), kuwa na maana ya Miungu na vinavyoweza kuwazika tu bali havionekani. Aya ifuatayo inatoa maana yake.

Wewe utaweza kusema, kuwa wakati wenyewe utatoa maana ya maneno.

Kwa mfano, mwungwana anamwambia mfanya kazi wake.

Ewe mtumishi, niletee Saindhava yenye maana mbili, 1. Farasi, 2. Chumvi. Ikiwa ni wakati wa bwana wake umefika wa kutoka nje, basi atamletea farasi; na ikiwa yeye anakula chakula, basi mtumishi atamletea chumvi; lakini ikiwa amefanya kinyume cha mambo, yeye ameleta chumvi wakati bwana wake anataka kwenda nje na akamletea farasi wakati wa kula chakula badala ya chumvi , bwana wake atahamaki na atasema, "Wewe ni mjinga. Ina maana gani kuniletea mimi chumvi wakati wakutoka nje na kuniletea farasi wakati wa chakula? Wewe hufikiri wakati, au wewe ungeleta kile kilichotakiwa kwa wakati wake. Wewe hukufikiria wakati ule kitu gani kilitakiwa; kwa hivyo wewe ni juha. Basi toka leo wewe uende zako kutoka kwangu.

Haya basi, mchezo huu una bainisha nini? Unabainisha kuwa kionyo juu ya wakati unaohitajika, na basi kwa hivyo sisi sote pia tufanye hivyo na tutanabahi kila wakati kwa uangalifu zaidi.

**Mifano**

Kwa hivyo, yataka ufahamu akilini mwako kama Om na maneno mengine wenye maana kama hii huwa ni Mungu Muweza katika Veda na katika vipande kama vilivyotajwa hapa chini. Nia hasa ya maneno haya ni kuonyesha (1) kama Aum na maneno yaliyofanana nayo katika humu huonyesha Mungu; (2) Kama hakuna jina hata moja la Mungu lisilo na maana yake, kama katika lugha isio ya adabu maskini huitwa dhampati; bwana wa mali, na mengineyo. Zaidi ya hayo, wao wanabainisha kuwa maneno haya huonyesha tabia, vitendo, mavumilio, au asili ya vitu katika mahali mbali mbali.

Sasa basi, Aum na majina mengine ya Mungu yaliyomo katika mashairi yanayofuata yana maana, kama,

Mungu anaitwa Aum kwa kutulinda sisi, Kham kwa kuenea katika vitu vyote vya mbinguni, na Brahma kwa kuwa Mkubwa kuliko vitu vyote.

Yeye peke yake anaitwa Aum, na yeye ni wa milele, na wakusujudiwa, bila mwingine ye yote - Chh. Up.

Aum ni dhahiri, mwenye maana ya asili na ni jina muhimu kabisa la Mungu katika Veda na nakala zingine, na majina yake mengine yana umuhimu wa pili. Mandukya Upanishat.

Yeye huitwa Aum ambaye anaimbwa katika Veda zote, anaombwa katika vitendo vyote vya ibada na katika hali ya kuwa na bila raha na pia anaombwa katika viapo vyao kutoa. Kath 11,12.

Yeye atazamiwe kuwa ni Mwenye Enzi, na ni mwalimu wa wote, mwenye nguvu zaidi kuliko nukta, ni mtukufu, na anajulikana kwa akili, yeye ni mtulivu katika hali ya usingizi au alitolewa katika hathari za kitu cho chote. Manu, XII, 112.

Mungu anaitwa Agni, kwa sababu yeye ni mtukufu; Manu, kwa sababu yeye ana ujuzi wote wa binadamu; Indra, kwa sababu yeye ni mlinzi wa wote; na Brahman, kwa sababu yeye ni msimamizi aliyeenea kote ulimwenguni - ib. 128.

Yeye anaitwa Brahma, kwa sababu yeye ndiye anatengeneza dunia yote, Vishnu kwa sababu yuko ameenea kote; Rudra, kwa sababu yeye huwapa taabu na huzuni wale waovu. Shiva, kwa sababu yeye ana furaha ya daima na ni mtoaji yaliyo mazuri kwa wote; Aksharo, kwa sababu yeye yuko kila pahali na haonekani; Swarat, kwa sababu yeye ni mtukufu; na Kalagni, kwa sababu yeye huwaangamiza wote wakati wa mafuriko na ni, kama alivyokuwa, mwangamizi wa kifo, ambaye huusafisha moto wa roho:-

Indra na maneno mengine kama haya ni majina ya Mungu ambaye si wa watu wawili tu, anayejiweka mwenyewe, na anayejizungusha kote - Rig - 1.164 46.

(1) Yeye anaitwa Indra, kwa sababu ameenea katika utawala wa maumbile na vyote vilivyomo humo; (2) Suparna, kwa sababu ulinzi wake na vitendo vyake ni vikamilifu; (3) Gaurtman, kuwa utukufu wake ni wa ulimwengu mzima; na (4) Matarishwa, kuwa yeye ni mwenye nguvu zaidi kuliko upepo. Kwa hivyo Divya, Suparna, Garutman na Matarishwa ni majina ya Mungu. Majina yaliyobakia yataelezwa baadaye.

Yaju. XIII. 18 Mungu anitwa Bhumih, kwa sababu ya viumbe vyote wako naye. Majina mengine ya Mungu katika shairi hili yatafahamishwa baadaye.

Indra ni jina la Mungu katika shairi hili: hata hivyo, hapa lina maana ya mamlaka ya nguvu:- Sam Veda, pr 7 Mantra. 8

Mungu anauzuifu wa dunia yote kama puumzi zinavyoendesha mwili - Atharva Veda, Kand II, Anuvak 2, Sukta 4, Mantra 1.

Maana ya mwanzo ya Agni, & C

Tafsiri sahihi ya mamlaka haya ya hapa juu yanadhihirisha, kuwa majina haya ya hapo juu ni ya Mungu tu, kuwa Aum, Agni na majina yanayofanana na haya, kusema kweli, huonyesha Mungu, kama ilivyooneshwa na Vyaarkana au sarufi, Nirukta au katika elimu ya lugha, Brahmanas au maelezo ya Vedic, Sutras au mithali ya maneno na maelezo ya maandishi matakatifu ya hadhithi za kale na watu wa falsafa. Hata hivyo maana haya yanatakiwa yakubaliwe na wote; Aum tu ndiyo jina la pekee la Mungu, lakini Agni na mengine maana yake ni Mungu, ambapo maudhui na sifa huonyesha sala, sifa na kuabudu. Ambapo, inaonyesha kuwa kila mara majina haya hupunguzwa nguvu na kufuatwa na maneno kama wa kujua yote, wa kuenea kote, mtukufu, wa milele, muumba wa dunia, na maneno kama haya mengine, huwa na maana ya Mungu.

**Maana ya Pili za Agni, & C.**

Katika vipande vyengine kama - Tait, Brahmanand V. III, 1st An. Maneno virvat, purusha, deva, akasha, vayu, agni, jala, bhumi, & C huvionya vitu kama

mfano wa dunia; kuwa, po pote penye muumbo, hifadhi, uangamizi, maarifa yasiyo kamili, isiyo ya akili, inayoonekana na sifa kama hizi zilizotajwa, yote haya haya mwonyeshi Mungu. Sababu ni kuwa Mungu yuko juu ya vyote vilivyo umbwa na vyenginevyo kama hivyo ambavyo uwezo wake uliotajwa hapa juu ni wa vitendo vya kawaida tu. Kwa hiyo, kama si kuwa majina ya Mungu, Virat, & C huonyesha vitu vya tabia. Lakini vinapotumika kwa sifa kama mjuzi wa kila kitu, & C. huonyesha Mungu Mwenyezi, na zinapotumikana na maneno kama haya hivi kuonyesha matakwa, uadui, machofu, furaha, maumivu, maarifa kidogo, na kama hayo, yote haya yana maana ni roho ya binadamu. Hii huwa na nguvu kila pahala, kwa sababu kuzaliwa na kufa kwa Mungu hakutokei kabisa. Kwa hiyo kuzaliwa, & C. inafanya Virat na maneno mengine huwa na maana ya vitu na vitendo vya akili, lakini si Mungu.

Sasa vipi virat na maneno mengine huwa na maana ya Mungu maana yeye hana asili na kitu cho chote.

**Majina 100 ya Mungu**

Om, Divya, Suparna, Garutman na Matarishwa ni majina matano ambayo yalielezwa, tazama ukarasa 31, na 95 majina yako hapa yametajwa moja baada ya moja.

1. **Virat**
   Neno Virat (Mwenye kuangaza) limetokana na neno raj. 1., Kuwasha au angaza, na kinachotanguliwa na vi na kumalizia a kvip. Yeye ambaye anaiangaza na kuidhihirisha dunia katika njia mbali mbali, inaitwa Virat kwa hivyo ni Mungu.

2. **Agni**
   Neno Agni (Mwenye kuabudiwa) limetokana na neno anchu: kuondoa au kuabudu au mizizi agi na ina ambayo hudhihirisha havakati. Agni ni jina la Mungu kwa sababu yeye ana elimu ya kiwili wili cha binadamu, mjuzi wa kila kitu, anaye stahiki kujulikana na kustahiwa.

3. **Vishwa**
   Neno Vishwa limetokana na neno vish: kuingia, na va kama ni neno la kati, lenye maana ya mwenye kutenda au pahali. Mungu anaitwa Vishwa kwa sababu yeye ni mtunza wa pepo na viumbe vyake vyote, au yeye ameenea kote na yumo katika kila kitu. Majina haya ya hapa juu yameonyeshwa kwa herufi ya A katika neno Aum.

4. **Hiranya Garbha**
   Mungu anaitwa Hiranya Garbha (kitovu cha mwangaza) kwa sababu jua na vitu vyengine vitukufu vimetangenezwa na kuwekwa na Yeye. Shairi lifuatalo la Yajur Veda, XIII. 4. hii:- Pia kuna mashairi mengi mengineyo ambayo hufanya Hiranya Garbha ni jina la Mungu.

5. **Vayu**

Neno Vayu (Mwondoaji) linatokana na neno va kuondoa, kuua. Mungu anaitwa Vayu, kwa sababu yeye huondoa, harakisha, husaidia, na huangamiza kila kitu kinachokwenda na kisichokwenda na mwenye nguvu kabisa kuliko wote.

6. **Tejah**

Neno Tejah (Mwangazaji) limetokana na neno tij:Kuangaza au kuwasha,na tejas limetokana na neno hilo hilo lakini jina limetiwa mwishoni Mungu anaitwa Tejah, kwa sababu yeye ni mtukufu na aliangaza jua na vinginevyo vinavyo ngara pia. Majina haya yaliyopo hapa juu yametajwa katika herufi ya U katika neno Aum.

7. **Ishwara**

Neno Ishwara (mtawala) linatokana na neno ish: kutawala au kuwa tajiri, kuwa na var kama ni mwisho wa neno, maana yake ni mtendaji. Mungu anaitwa Ishwara, kwa sababu yeye ni maumbile, elimu yake na utajiri wake hauna mwisho.

8. **Aditya**

Neno Aditya (Asiyedhurika au Asiye na mwisho) linatokana na neno do: kuikata, kuwa a ni mwanzo wa neno yaani kukanusha na ti kuwa mwisho wa neno, kuleta maana ya mtendaji, na o hubadilika kuwa e, ambayo huifanya kuwa aditi, na a kuwa mwisho wa neno la jina huwa aditya. Aditya ni jina la Mungu kwa sababu yeye hafi.

9. **Prajna**

Neno Prajna (Mjuaji) linatokana na neno jna: kujua, na pra, kuanzia neno, huwa prajna kwa kumalizia jina. Prajna ni jina la Mungu, kwa sababu yeye anajua vitendo vya viumbe vyote wanauweza kwenda na wasioweza pia wa dunia na ambaye maarifa yake yako wazi na bila shaka yo yote. Majina haya yamedhihirishwa katika herufi M. katika neno Aum. Hapa sifa tatu tu zimetajwa ambayo zimeonyeshwa katika kila herufu ya neno Aum. Katika njia hii, majina **mengine yanafahamika pia.**

Majina katika ubeti wa hapa juu, kama mitra na mengine yote ni ya Mungu, kama ilivyokwisha semwa, dua, sala na ibada ni za Shreshta tu(Bora sana) au Mungu, huwashinda wote katika sifa, tabia, mwendo ulio sahihi. Yeye ambaye mtukufu kupita watukufu wote, ambaye anaitwa Mwenyezi Mungu. Hapana aliyekuwa, au, anakuwa au atakuwa sawa na yeye. Ikiwa hapana hata mmoja aliye sawa na yeye, basi vipi ataweza kuwa mkubwa kuliko Yeye. Ukweli, haki, huruma, mwenye enzi zote, mwenye kuenea pote, na sifa zisizo na mwisho haziwezi kubashiriwa vizuri zaidi kuliko kitu cho chote kama Mungu mtawala wa dunia. Mungu, ambaye ni mkweli au hasa, pia ana dhana za kweli, tabia na sifa za asili. Hata hivyo binadamu lazima aombe, asihi na asimwabudu mwingine ila Mungu; kwa sababu, wataalamu wa zamani

ambawo majina yao yalikuwa Brahma, Vishnu, Mahadeva, hasha, hata Ma-Titan, mapandekizi ya watu na watu wadogo pia, walimwamini Mungu tu, na walimsifu, kumtukuza na kumwomba rehema yeye peke yake. Sisi wote pia tufanye hivyo tu. Maudhui haya yata zungumzwa kwa urefu katika sura ya uwokovu na moyo wa ibada.

Q. - Ikiwa itasisitizwa kuwa maneno mitra na mengineyo yafahamike kwa maana yao hasa ya marafiki wa dunia, Indra na watukufu wengine, kama vitendo vyao ni vya kujulikana sana. A - Inajibiwa kuwa maana hizo hazifai hapa, kwa sababu, mtu aliye rafiki wa huyu ni adui wa yule, na pia huwa vingine na mtu watatu. Hata hivyo, marafiki na maana nyingine maarufu haziwezi kujulikana. Lakini Mungu ni rafiki bila shaka wa wote, lakini binadamu hawezi kuwa hivyo, majina hayo yana maana ya Mungu tu katika vipande kama hivi. Kweli, katika maana ya pili ya mitra na maneno mengine yana maana kuwa marafiki wa dunia na mengineyo.

10. **Mitra**
Neno Mitra (Rafiki) linatokana na neno nimid: kupenda na ktra kuwa mwisho wa neno. Mungu anaitwa Mitra, kwa sababu yeye anawapenda wote na anastahiki kupendwa na wote pia.

11. **Varuna**
Neno Varuna linatokana na neno vri kuchagua, kuwa na unan kumalizia neno. Mungu anaitwa Varuna, kwa sababu yeye anakubali au anakubaliwa na tabia ya Mungu, ana nguvu ya kuona yasiyoonekana na wengine, wataalamu aliyejitolea katika uwokovu, aliyeokolewa, na mwaadilifu.

12. **Aryama**
Neno Aryama linatokana na neno arya na ma kuhishimu, na, ni ya kutiliwa mkazo, na arya limetokana na ri kwenda, kupata, na ya ni ya kutiliwa mkazo. Mungu anaitwa aryama, kwa sababu anawahishimu wale ili wafanye ya haki na insafu, na anaamua vitendo vya haki na vya uovu vya waadilifu na ukosefu.

13. **Indra**
Neno Indra linatokana na neno idi; kuwa na nguvu za Mwenye Ezi Mungu na kutilia mkazo ra. Mungu anaitwa Indra, kwa sababu yeye ana nguvu za Mwenyezi Mungu.

14. **Brihaspati**
Neno Brihaspati linatokana na neno pa: kuhifadhi, na briha, kuwa mwazo wa t ya brihat hutolewa na herufi s kutiwa badala yake. Tena inatanguliwa na herufi ti inayoongezwa hapo mwanzo. Mungu anaitwa Brihaspatit, kwa sababu yeye ni mkubwa wa wakubwa na ni Bwana wa pepo na dunia na ulimwengu wote.

15. **Vishnu**
Neno Vishnu linatokana na neno vish: kuenea kote na linatilia mkazo mtendaji. Mungu anaitwa Vishnu, kwa sababu yeye ameenea kote katika vitu vinavyokwenda na visivyokwenda vya dunia.

16. **Urukramah**
Kwa ajili ya nguvu za milele, Mungu anaitwa Urukramah. Ubeti una maana kuwa: Ewe (Bhavatu) Roho ya milele (Parmatma) Mwenyezi ni yeye (Urukramah), ambaye ni rafiki wa wote (Mitra) ambaye ni mtoaji wa furaha (Sham), aimbaye ni bora kuliko wote, (Varun), ambaye ni chemchemu ya furaha (Sham) ambaye ni hakimu wa haki kwa wote (Aryama) ambaye ni mwenye nguvu (Indra), ambaye ni mtowaji wa utajiri wote (Sham) ambaye ni msaidizi wa wote (Brihaspati) ambaye ni mwalimu wa maarifa (Sham) ambaye ameenea kote (Vishnu), bariki (Sham) sisi (nah)?

17. **Brahma**
Neno Brahma linatokana na neno brih au brihi linazidi kwa kuishia na ma mwisho wa neno. Maana ya ubeti - Sisi tunamtolea salamu Mungu Mkuu Brahma ambaye yuko juu ya wote, anaye wazunguka wote na mwenye nguvu za milele. Mungu Muweza, wewe ni peke yako tu mtafutaji wa moyo na bila ya shaka yo yote mtawala wa wote. Mimi nakuenzi wewe kuwa Mola wangu, na kuwa dhahiri kila pahali, tabaan watu wote wanaweza kufika kwako. Mimi nitatenda na kuhutubia wengine kwa mujibu wa amri zako za Veda. Nitafuata ukweli katika fikra, usemi, na vitendo. Ni hifadhi mimi, Ewe, Mola nihifadhi, mwadilifu, na mkweli nilivyo ili akili yangu izikamate sawa sawa; amri yako ni dini na kinyume chake ni kuchukia dini.

Kukariri ibara ya mwisho huonyesha upendo wa ibada na mwanzo wa kusoma. Kwa mfano, mtu anapomwambia mwenzake, "Nenda, nenda kijijini," kukariri neno "nenda" inaonyesha haraka, i.e. Nenda kijijini upesi. Vivyo hivyo, katika sentensi iliyotangulia, inaonyesha mkazo, i.e. Nihifadhi mimi, Ewe Mungu, nihifadhi fanya hivyo ewe Mola ili mimi niwe imara na bila shaka yo yote katika dini na nichukie kutoshika dini. Ewe Mungu, nisaidie, maisha nitaienzi neema yako.

Madhumuni ya kukariri neno Shanti (amani) mara tatu ni kuonyesha kuwa kuna namna tatu ya maumivu, ya akili, ya mwili na ya tabia, 1. Adhyatmic, i.e. ujinga, mapenzi, chuki na hatia yote haya ni hisia za akili; na homa na mabaya kama haya ya mwili. 2. Adhibhoutic i.e. mabaya ya ulimwengu kutokana na adui, kama chui, chatu, na kama hawo wengine 3. Adhidaivic, i.e., mabaya ya pasipo budi hutendeka kama mvua nyingi kupita kiasi, baridi, joto na kuleta hali ya wasi wasi ya akili na hisia. Kwa hivyo: 'Tuweke sisi sote, Ewe Mola, mbali na maumivu haya matatu, na tushughulishe sisi daima katika ukarimu wako, kwa sababu Wewe ndiye chanzo cha furaha, mfadhili wa dunia nzima; mwongozi wa hali ya heri kamili na ya unyofu na kwa waliojitolea. Kwa hivyo, Ewe Mola, kuwa dhahiri katika mioyo ya watu wote kwa rehema zako, ili wao wafuate dini na

wasiwe wasiona dini, wapate furaha ya milele, na waepukane na namna zote za maumivu.

18. **Surya**

Mwenye enzi Mungu anaitwa Surya katika ubeti huu wa Yajur Veda, kwa sababu yeye ni mtukufu, huangaza yote, na ni roho ya ndani ya kila kinachoweza kujisongeza; wanyama wenye akili na viumbe vinginevyo, na vyote ambavyo haviwezi kusongea au kwenda, kama mimea, vitu, kama dunia na kama hivyo.

19. **Paramatma**

Neno atma limetokana na neno at: kuenea kote. Mungu anaitwa Paramatma Mwenyezi Mungu, kwa sababu yeye yumo katika wanyama wote na viumbe vyengine, na kwa sababu yeye ni kiumbe bora kuliko vyote na ni mdogo kuliko chembe ndogo ya kitu, roho na mbingu, na ni maisha au ni roho za viumbe vyote.

20. **Parameshwara**

Mungu anaitwa Ishwara Mola. Yeye ni Mtawala wa watawala na hapana aliye sawa naye, naitwa Parameshwara Mwenyezi Mungu.

21. **Savita**

Neno Savita linatokana na neno su: kuzalisha, ta huja mwisho wa neno, kabla ya hapo su huwa savi. Kuwa mzalishaji wa dunia nzima, Mungu anaitwa Savita.

22. **Deva**

Neno Deva linatokana na neno div, maana yake cheza, kutaka, kushinda, kazi, utukufu, sifu, furaha, ota, uzuri, mwendo. Mungu anaitwa Deva, kwa sababu yeye anamiliki furaha ya wale wasio na hatia wa shangilio ya waadilifu, kuwa mtoaji wa utajiri na akili wa juhudi na vitendo vyote, wa kuwa na utukufu wake mwenyewe na kuwaangaza wote,mwenye kustahiki sifa zote, wa kuwa na furaha mwenyewe na pia kuwapa wengine, kwa kuwa kinga wa wale wenye kiburi, kwa kuwa mfanya usiku na mghariko wa yaliobakia yote, kwa kuwa wazo wa matakwa ya wote, na kwa kuwa chemchemi ya elimu. Kwa maneno mengine, Mungu anaitwa Deva, kwa sababu yeye anafurahisha kwa furaha yake na anaifanya dunia kwa uwezo wa tabia yake na bila ya usaidizi wa kiumbe cho chote, na ni chanzo cha furaha yote, kwa sababu yeye huyashinda yote na yeye mwenyewe hadhuriki na hashindiki, kwa sababu yeye anajua na anasomesha ukweli na si ukweli, kwa sababu yeye anatoa mwangaza kwa wote, kwa sababu yeye anastahiki sifa zote na hamgombezi ye yote, kwa sababu yeye ni furaha katika yeye mwenyewe na pia huwapa wengine, na hana hata dalili za maumivu hata kidogo, kwa sababu yeye ni furaha ya milele, hawezi kuwa na maumivu mwenye furaha na huwaweka wengine mbali na majonzi ya maumivu, kwa sababu yeye huwapumzisha viumbe vyote katika wakati wa dhiki au mafuriko, kwa sababu yeye ni nguzo ya ukweli, na yeye tu ndiye anaye ombwa na waadilifu, na kwa sababu yeye ameenea kote na ni miuaji.

23. **Kuvera**

Neno Kuvera, (mzungukaji) linatokana na neno kuvi: kufunika, kuzunguka. Mungu anaitwa Kuvera, kwa sababu yeye ameuzunguka uadilifu wake kila pahali.

24. **Prithwi**

Neno Prithwi linatokana na neno prithu: kutawanya. Kama Mungu anavyotawanyika au anavyoifanya dunia, yeye anaitwa Prithwi.

25. **Jala**

Neno Jala linatokana na neno jala: kuua. Mungu anaitwa Jala, kwa sababu yeye humtia adabu mwovu na hutengeneza na kuharibu chembe zote au vitu visivyoweza kuonekana.

26. **Akasha**

Neno Akasha (Mwangazaji) linatokana na neno kash: kuangaza. Mungu anaitwa Akasha, kwa sababu yeye ni mwangaza wa dunia kwa kila njia.

27. **Anna, 28. Annada**

29. **Atta**

Neno Anna linatokana na neno ad: kula. Mwisho ni msemo mfupi wa Sharirak au Vedant na St. Vyasa. Kama yeye anavyo, anashika na anaendesha, Mungu anaitwa Anna, Annada na Atta. Mrudio wa mara tatu wa Anna katika Upanishat ni kwa njia nzuri mno. Dunia nzima imo katika Mungu kama mdudu katika tunda la 'Gular' (tini) ambamo wanazaliwa na pia kuharibika mumo humo.

30. **Vasu**

Neno Vasu linatokana na neno vas. Kuishi, lenye neno la mwisho kuwa u. Kama Jana zote na viumbe vyengine huishi katika yeye, na Yeye huishi katika wao wote, Mungu anaitwa Vasu.

31. **Rudra**

Neno Rudra linatokana na heno rudir: Kutiririsha machozi na neno la kati lake ni nich, huwa a. Mungu anaitwa Rudra, kwa sababu yeye humletea mwovu huzuni na huwafanya wao walie.

Hiki ni kifungu cha maneno kutokana na Brahmana wa Yajur Veda. Ina maana: Mtu hubainisha katika usemi wake yale aliyonayo akilini mwake. Yeye anatekeleza kauli yake. Yeye huvuna kila anachokitenda. Hii hudhihirisha kama mtu apandacho ndiyo avunacho. Waovu wanapopata adabu kwa dhambi zao za insafu za haki ya Mwenyezi Mungu, wao hulilia na kuhuzunikia. Na hivi ndivyo Mungu anavyo wafanya walie. Hata hivyo, ukuu wa Rudra ni kuwa jina lake.

32. **Narayana**

Nara ni jina la jala, maji na jiwa: roho. Ilivyokuwa Mungu ameenea katika maji na ulimwenguni na pia katika roho zote, ambazo ni misikiti yake kama tunavyosema, yeye ni Narayana wa kweli. Ayana maana yake ni makao.

33. **Chandra**

Neno Chandra linatokana na neno chadi: kuwa furahani. Kama Mungu ni chanzo cha furaha na pia yeye huwapatia wote pia, yeye anaitwa Chandra.

34. **Mangala**

Neno Mangala limefanyika kutokana na neno la kizamani au la kale neno

mang, lakuonyesha kitendo pamoja na al kuwa mwisho wa neno. Hasa ilivyokuwa Mungu ni mtukufu wa daimana ni mwenye furaha na pia ni chanzo cha furaha kwa wote wengine, yeye anaitwa Mangala.

35. **Budha**

Neno Budha linatokana na neno budh; kujua. Mungu ndiye huyu mjuaji, kwa sababu yeye ni mjuzi na mwenye busara na pia ni mpaji wa busara wa hawo wenye busara.

Maana ya neno Brihaspati limeshaelezwa.

36. **Shukra.**

Neno Shukra linatokana na neno shu: kutoharisha pamoja na kra kuwa mwisho wa neno. Mungu anaitwa Shukra, kwa sababu yeye ni mtukufu zaidi na kwa rehema zake au ujuzi wake, roho huweza kutakasika.

37. **Shanaishchar**

Neno Shanaishchar linatokana na neno char, kusogea na kula pamoja na shanaisha kuwa ni sifa inayokuja mwanzo. Hasa ilivyokuwa Mungu kwa uwezo wa rehema zake ameenea kote na ni mstahmilivu na mwenye huruma, yeye anaitwa Shanaishchara.

38. **Rahu**

Neno Rahu linatokana na neno rah: kujitenga. Ilivyokuwa Mungu ni mmoja na ni peke yake tu, hapana kitu cho chote kilicho changanyika naye au bila kuwepo wa pili, ambaye anawakataa wenye dhambi na kuwaongoa wengine yeye anaitwa Rahu.

39. **Ketu**

Neno Ketu linatokana na neno kit: kuishi na kuondoa maradhi. Ilivyokuwa Mungu yuko mbali na maradhi yote, huwaponyesha wote na magonjwa yote, katika uokofu wakujitolea na ni mahali pa kupumzika kwa wote, yeye anaitwa Ketu.

40. **Hota**

Neno Hota linatokana na neno hu: kutoa na kuchukua pia kupokea tu kwa mujibu wa wengine, kuwa na herufi ya kutiliwa mkazo ni ta. Mungu anaitwa Hota, kama yeye ndiye anatoa kile unachostahiki kupewa na anakichukua mwenyewe kila kinachostahiki kuchukuliwa kutoka kwa watu wote.

41. **Yajna**

Neno Yajna linatokana na neno yaj: kuabudu, mwaandamano, na kutoa Sadaka. Imetokana na Brahmana. Mungu anaitwa Yajna, kwa sababu yeye ni mwenyezi anayejitengeneza vitu vyote duniani, na ana abudiwa na St. wote, na sasa wanaabudiwa na watu wote.

42. **Bandhu**

Neno Bandhu linatokana na neno bandh: kufunga, kuwa na mkazo kwenye herufi U. Mungu anaitwa Bandhu, kwa sababu yeye ana funganisha dunia na sayari kwa uwezo, zimeratibishika vyema kwa amri zake, kwa hivyo hazipitani katika njia zao na kuvunja sheria zisizoweza kubadilika, na ni

msaada kwa viumbe vyote kama ndugu mama mmoja na baba mmoja, mwenye kutoa nafuu na msaada kwa dunia zote na vyote vilivyomo humo.

43. **Pita**
Neno Pita linatokana na neno pa: kuhifadhi, kuwa na mkazo herufi ta. Mungu anaitwa Pita, kwa sababu yeye anawahifadhi wote, na kuzitakia roho zote mafanikio na kuongoka kwa rehema zake na huruma zake za wema na baba mwema kwa wanawe wa kiume na kike.

44. **Pitamaha**
Mungu anaitwa Pitamaha, kwa sababu yeye ni baba wa mababa.

45. **Prapitamaha**
Mungu anaitwa Prapitamaha, kwa sababu yeye ni baba wa mababu wa mababa.

46. **Mata**
Mungu anaitwa Mata, kwa sababu yeye anayo katika moyo wake heri ya wote, kama mama mwema anapowatakia heri na raha na wema watoto wake. Linatokana na neno ma: kuhishimu na ta ni herufi yakutiliwa mkazo.

47. **Acharya**
Neno Acharya linatokana na neno char: kula na kwenda, kuwa a mwanzoni na ya kuwa la kutiliwa mkazo. Kwa hivyo Yeye hufurahia tabia nzuri, na kwa kuwa yeye ni chemuchemu ya elimu, ambayo anawapa binadamu, Mungu anaitwa Acharya.

48. **Guru**
Neno Guru linatokana na neno gri: kufanya sauti. Mungu anaitwa Guru, kwa sababu Yeye anasomesha Vedas, inayoonyesha dini ya kweli na yenye elimu yote; kwa sababu Yeye ni mwalimu hata wa Agni, Vayu, Aditya, Angira; Brahma na kama walimu wa kale wakati wa mwanzo wa muumbo na kwa sababu kifo Chake hakitokei kamwe.

49. **Aja**
Neno Aja linatokana na neno aja: kusongea au kurusha, ja: kudhihirisha au bainisha. Mungu Mwenyezi anaitwa Aja, kwa sababu yeye anaunganisha vipande vidogo kabisa vya hewa nyepesi sana na vingenevyo kama hivyo, na huunganisha mwili na roho kuvifanya kuwepo na yeye Mwenyewe katu hazaliwi.

50. **Brahma**
Neno Brahma linatokana na neno brih, kuzidisha kuwa mkuu, Mungu anaitwa Brahma, kwa sababu Yeye hukuza, huitengeneza dunia au huifanya iwe imekamilika baada ya kuiumba.

Ni mateuzi kutokana na Taitteriya Upanishat. Brahman au Mwenyezi anaitwa Satya, Jnan na Anant.

51. **Satya**
Mungu anaitwa Satya, kwa sababu yeye ni mwenye kujua kila kitu, ambavyo vinaitwa sat katika Sanksrit.

52. **Jnana**
Mungu anaitwa Jnana, kwa sababu Yeye anajua yote (yaliyotokana na jna kujua)

53. **Anant.**
Mungu anaitwa Anant kwa sababu Yeye hana mwisho, au kiwango, kipimo kinachoeleza, urefu, na upana na urefu wa kwenda chini au ukubwa (a: si ant: mwisho).

54. **Anadi**
Neno Anadi linatokana na neno do: kutoa, kuwa a na na mwanzoni. Mungu anaitwa Anadi (isiona mwanzo) kwa sababu hakuna kilicho kabla yake na yeye yuko mbele ya yote, kwa hivyo, Yeye hajamfuata mtu lakini anafuatwa na wote.

55. **Anand**
Neno Anand linatokana na neno nad: kuzidisha au kusitawi, kuwa a ni mwanzo wake. Mungu anaitwa Anand kwa sababu Yeye ni furaha yenyewe, na wote walio chaguliwa hufurahia hali ya heri Yake, na Yeye huwa rehemu wote wale waadilifu kwa furaha.

56. **Sat**
Neno Sat linatokana na neno as: kuwa. Mungu anaitwa Sat-(kuwa), kwa sababu Yeye yuko wa milele na hatatanishiki kwa nyakati tatu zilizo gawanyika za saa, viz iliyopita; iliyopo sasa, na itakayo kuja.

57. **Chit**
Neno Chit linatokana na neno chit: kujua vizuri. Mungu anaitwa Chit, kwa sababu Yeye ni mjuzi wa Yote, na huwapa ujuzi roho zote, na huwawezesha kubagua ukweli kutokana na uwongo.

58. **Satchidanand**
Mungu anaitwa Satchidanand kwa sababu maneno haya matatu sat, chit, anand - kuwa, ujuzi, furahisha, yanabainisha mambo matatu matukufu.

59. **Nitya**
Mungu anaitwa 'Nitya' kwa sababu yeye ni wa milele, asiebadilika na asiyekufa.

60. **Shuddha.**
Neno Shuddha linatokana na neno shudh, kutahirisha. Mungu anaitwa Shuddha, kwa sababu Yeye mwenyewe ni mtukufu na hana ila yoyote, na yeye pia ni mtahirishaji wa wote.

61. **Buddha**
Neno Buddha linatokana na neno budh: kujua ta ni kutiliwa mkazo. Mungu anaitwa Buddha kwa sababu Yeye ni mjuzi kuwa yote.

62. **Mukta**
Neno Mukta linatokana na neno much: kuacha kuwa ta ni lakutiliwa mkazo mwisho. Mungu anaitwa Mukta, kwa sababu Yeye hana dosari yo yote na huwachia huru wale wanaotaka kuokolewa kutokana na dhamana ya

maumivu. Hata hivyo, Mungu anaitwa Nitya, Shuddha, Buddha, Mukta - wa milele; mtukufu; mwenye busara; na ni kamili.

63. **Nirakar**

Neno Nirakar linatokana na neno kri: kufanya, kuwa nir na a mwanzo wa neno. Mungu anaitwa nirakar kwa sababu Yeye hana umbo wala Yeye hana mwili pia.

64. **Niranjan**

Neno Niranjan linatokana na neno anj: kuwa dhahiri, kuonyesha, kutaka, kusogea na mwanzo wa neno kuwa nir na an ni la kutiliwa mkazo. Mungu anaitwa Niranjan, kama Yeye alivyo mbali na vitu vyote vinavyo fahamika, na mbali na wenye miili, vitendo viovu na matakwa.

65. **Ganesh,** 66. **Ganapati.**

Maneno Ganesh na Ganapati yanatokana na neno gan: kuhesabu, ambayo esh na pati yakitiliwa mkazo hufanya Ganesh na Ganpati, Mola au bwana wa wadhamini. Mungu anaitwa Ganesh au Ganpati, kwa sababu Yeye ni Bwana na mlinzi wa vitu vyote, vinavyoishi na visivyoishi au wale wanawo kwenda kujenga mazingira.

67. **Vihsweshwar**

Mungu anaitwa Vishweshar, kwa sababu Yeye ni Mtawala Mtakatifu wa dunia. (Vishwa: Dunia, ish kutawala, var ni ya kutiliwa mkazo.)

68. **Kutastha**

Mungu anaitwa Kutastha, kwa sababu Yeye hageuzi fikra yake, ijapokuwa maeenea katika fikra zote na mabadiliko, na pia kuwa sababu ya vitendo hivyo vyote (Kuta: ni mwanzo wa kitu, na stha: kusema:- kuishi kwa kitu)

69. **Devi**

Neno Devi lina maana nyingi kama neno Deva lililokwisha tajwa hapo juu. Majina ya Mungu ya jinsi tatu. Neno Deva linatumiwa linapoonyesha Ishwara; Mtawala (kuwa kiume) na Devi linapoonyesha Chiti Ufahamu (kuwa kike). Hata hivyo Devi ni jina la Mungu.

70. **Shakti**

Neno Shakti linatokana na neno 'shak'; kuweza. Mungu anaitwa 'Shakti' kwa sababu Yeye anaweza kuifanya dunia yote.

71. **Shri**

Neno 'Shri' linatokana na neno 'shri': kutumikia. Mungu anaitwa 'Shri'. Yeye ni uzuri usioelewezeka, kwa sababu Yeye anatumikiwa na dunia nzima, wataalamu na wale wanao jinyima raha zote za dunia pia.

72. **Lakshmi**

Neno 'Lakshmi' linatokana na neno 'lakshmi': kuona na kutia alama. Mungu anaitwa 'Lakshmi' (mali za wote), kwa sababu Yeye anaona yote yanayo sogea na yasiyo sogea ya dunia, na viipa umbo na sura, pia huvitukuza kwa

alama, kama macho, pua katika kiwili wili cha binadamu; majani, maua, matunda, na mizizi ya miti; rangi nyeusi, nyekundu na nyeupe: udongo, mawe katika ardhi ya maji,jua,mwezi na vitu vyenginevyo vya dunia; na Yeye ni saa zote macho ulimwenguni. Yeye ni mzuri kushinda wazuri, mshangao wa Vedas na maandishi matukufu kama hayo, wenye dini na wataalamu.

73. **Saraswati**

Neno Saraswati linatokana na neno sri: kwenda, ambayo huwa 'saras', 'wat' and 'i' inayokuja mwisho. Mungu anaitwa 'Saraswati' (mama wa usemi), kwa sababu yeye anawo ujuzi mwingi na ana fikra sahihi za maneno na maana yake, uhusiano na ardhilhali.

74. **Sarvashaktiman**

Mungu anaitwa 'Sarvashaktiman' (Mwenyezi Mungu) kwa sababu katika kazi zake Yeye hahitaji mwingine na kwa sababu Yeye humaliza kazi zake zote zisizopimika kwa nguvu Zake mwenyewe.

75. **Nyayakari**

Neno 'Nyayakari' linatokana na neno 'ni': kupata, na 'cri' kufanya, kuwa 'in' kutiliwa mkazo mwishoni. Hayo hapo juu ni kifungu cha maneno kutoka Vatsyayana kuelezea msemo mfupi wenye maana. Haki imebainishwa kuwa kweli kwa ushahidi wa fikra, au ni uwezo wa tabia isiopendelea upande wo wote. Mungu anaitwa 'Nyayakari' kwa sababu ni tabia yake kufanya haki.

76. **Dayalu**

Neno 'Dayalu' linatokana na neno 'daya': kutoa, kusogeza, kuhifadhi, kuua, kupokea, na 'lu' ni neno la mwisho lakutiliwa mkazo. Mungu anaitwa 'Dayalu' kwa sababu yeye ni mpaji wa kutokuwa na khofu, mjuzi wa haki na si sawa na aina zote za sayansi, mhifadhi wa watu wema wote, na mtia adabu wa haki wa waovu.

77. **Adwaita**

Mungu anaitwa Adwaita (asie na mwingine kama yeye), kwa sababu Yeye ni wa pekee na mmoja tu ambaye ni Mkuu Mungu asiye na mwenzake, au msaidizi katika utukufu wake, bila kuwa na mshabihi naye, kama mtu ana mtu mwingine aliyefanana naye, wala hana kinyume chake, kama mtu anayo miti, mawe na vitu vinginevyo vilivyo kinyume na fikra za mazingira, na bila kuwa na mgawanyo wa wepesi wakuonekana, katika Nafsi Yake, au katika tafauti ya kimwili au sura katika tabia Yake ya kiroho, kama vile jicho, sikio, na viungo vyengine katika mwili wa binadamu.

Kwa hivyo, Mwenyezi Mungu ametukuzika kwa umoja mtakatifu, bila kuwa na mwingine kama yeye, au kuwa na mpinzani mwingine au mchanganyiko wa mambo mazuri katika utakatifu wake.

78. **Nirguna,**

Mungu anaitwa Nirguna, kwa sababu yeye yuko mbali na vitu, kama satwa (vinavyoonekana), raja (kitendo), tama (ulegevu), mwangaza, na ladha, nusa, na kama hivyo kutokana na akili ya kiumbe, kama ujinga, ujuzi usiotosha

mapenzi, chuki kama mapenzi na adhabu kama hizo.

Ushuhuda wa Upanishats unatilia nguvu fikira hii, kwa mfano:- ni kusema, Mungu yuko mbali na kuwa na vitu kama, sauti, uwezo wa kugusa, umbo, & C. (Nir: si, guna: sifa za vitu).

79. **Saguna**
Mungu anaitwa Saguna, kwa sababu fadhila Zake ni kuu, yote tukufu na sifa kama hizi za tabia zisizo na mwisho. Kumpa sifa au kutompa sifa Mungu.

Kama inavyosemekana kuwa dunia ni zote mbili saguna, i.e. yenye sifa za kitu, kama harufu, & C. na nirguna, i.e. kutokuwa na sifa za akili, kama matakwa, & C. kwa hivyo Mungu anaitwa majina yote mawili Nirguna, kama ilivyo kuwa Yeye hafikiwi na sifa za akili na za vitu na Saguna, kwa sababu Yeye anazo sifa za milele na kama nguvu zisizokadirika. Kwa maneno mengine hakuna kitu cho chote kisichokuwa na kumiliki au kutomiliki sifa. Kama kitu ni nirguna, i.e. bila sifa, kutokuwa na sifa za akili, na ni saguna, i.e. na sifa, kuwa na sifa za kuzimiliki mwenyewe; basi roho ni nirguna, kutokana na kuwa dhahiri sifa za matakwa na uwezo wa akili. Basi na hivyo hivyo kwa Mungu.

80. **Antaryami**
Mungu anaitwa Antaryami (Mdhibiti wa ndani) kwa sababu Yeye anazo dunia nzima chini yake, zote mbili yenye uhai na isiyokuwa na uhai, kutokana na kuwepo Kwake katika zote.

81. **Dharmaraja**
Mungu anaitwa Dharmaraja (mfalme wa haki) kwa sababu Yeye ametukuka katika haki na ni kamili katika haki bila ya kuwa na hata chembe ya kupendelea au isioyahaki.

82. **Yama**
Neno Yama linatokana na neno yam; kuzuia. Mungu anitwa Yama, kwa sababu Yeye ni wakili wa haki mwenye kutoa zawadi za vitendo vya viumbe vyote na haathiriki na yasio ya haki.

83. **Bhagwan**
Neno Bhagwan linatokana na neno bhag. ambalo tena limetokana na neno bhaj: kutumikia, na mwishoni wan. Mungu anaitwa Bhagwan, kwa sababu Yeye ni Bwana wa mali za dunia na ni kitu cha kuabudiwa.

84. **Manu**
Neno Manu linatokana na neno man: Kufikiri. Mungu anaitwa Manu, kwa sababu Ujuzi Wake ni Utukufu wake, na Yeye peke yake ndiye anaabudiwa.

85. **Purusha**
Neno Parusha linatokana na neno pri: kulinda na kujaza, au pur mwili au dunia na shi ni kukaa, maana yake ni wakaazi wa dunia. Mungu anaitwa Purush, kwa sababu Yeye anaijaza dunia yote.

86. **Vishwambhar**

Neno Vishwambhar linatokana na neno bhri: Kukamata na kulisha, kuwa na neno vishwa; dunia, linatiwa mbele yake. Mungu anaitwa Vishwambhar kwa sababu Yeye huikamata na kuisaidia dunia.

87. **Kala**

Neno Kala linatokana na neno kal: kuhisabu, na a kuwa neno la mwisho. Mungu anaitwa Kala kwa sababu Yeye huhisabu roho na vitu vyote vya dunia.

88. **Shehsa**

Mungu anaitwa Shesha (Mwisho), kwa sababu Yeye hubaki mwisho baada ya kuumba na kuangamiza dunia zote. Shis: kuainisha, kubaki.

89. **Apta**

Neno Apta linatokana na neno ap: kuenea, na ta ndiyo ya kutiliwa mkazo. Mungu anaitwa Apta, kwa sababu Yeye ni hatibu wa kweli, ana miliki elimu yote, anapatikana na kuweza kuendewa na watu wa dini wote, na yuko mbali na unafiki wote, udanganyifu na uovu mwingine.

90. **Shankar**

Neno Shankar *linatokana na neno kri: kufanya na sham: nzuri kuwa mwanzo wa neno na a kuwa herufu ya kati.* Mungu anaitwa Shankar, kwa sababu Yeye hufanya yote mazuri na huwapa wote furaha na kumsahilishia kila mtu.

91. **Mahadeva**

Neno Mahadeva linafanyika kutokana na neno deva kuwa mahata kuja mwanzoni. Jina la Mungu ni Mahadeva, kwa sababu Yeye ni Mungu Mkuu wa miungu yote, i.e. mtaalamu wa wataalamu wote, huipa jua mwangaza na vitu vyenginevyo vinavyo ngaa.

92. **Priya**

Neno 'Priya' linatokana na neno 'pri': kufurahisha, kufanywa iwe nzuri. Jina la Mungu ni 'Priya' kwa sababu Yeye anawafurahisha mawalii wote, waliojitolea katika wokovu na wazuri, na Yeye ni kitu cha kutakwa na wote.

93. **Swayambhu**

Neno Swayambhu linatokana na neno 'bhu' linafuatwa na Swayam: mwenyewe. Jina la Mungu ni Swayambhu, ilivyokuwa Yeye yuko peke yake, yeye hajazaliwa na mwingine.

94. **Kavi**

Neno Kavi linatokana na neno 'ku' kuvuma au kusomesha. Kavi ni jina la Mungu, kwa sababu Yeye ni mwalimu wa matawi yote ya elimu kwa njia ya Vedas na anawajua wote.

95. **Shiva**

Neno Shiva linatokana na 'shiv': kuwa na furaha. Pia, shi: kupumzika, na va kuwa mwishoni, i.e. mmoja ambaye dunia inajielemea juu yake. Jina la Mungu ni Shiva, ambaye ni umbo la furaha na huwa furaha watu wote.

Hivi basi ndivyo yalivyoelezwa majina mia ya Mungu. Lakini pia bado yapo majina mengi yasiyoweza kuhisabika ya Mungu pamoja na haya. Ilivyokuwa sifa za Mungu, vitendo na tabia ya milele isio na mwisho, basi hata majina yake hayana hisabu. Na kila moja lina sifa yake ya kitendo au sura ya tabia yake. Kwa hivyo majina ya Mungu yaliyotajwa hapa juu ni kama tone kulinganisha na bahari; kwa sababu Vedas na maandishi mengine matukufu yatoa sifa zisizoweza kuhisabika, vitendo na tabia zake. Kuyajua au kuyasomesha huiamsha akili. Wao tu ndiyo wanaweza kupata elimu sahihi ya vitu vyengine, wanaosoma Vedas na maandishi matukufu mengineyo.

**Dibaji ya kuhubiria**

Swali:- Kama waandishi wengine, kwa nini wewe hujaandika mangalacharan dibaji ya kuhubiria heri, mwanzoni au katikati au mwishoni mwa kitabu?

Jawabu:- Si sawa kwa ajili yetu, kwani yeye anayeandika dibaji ya heri mwanzoni, katikati au mwishoni, atayafanya maandishi yake kuwa si ya heri mwanzoni, katikati na mwishoni. Kwa hivyo, huu ni usemi mfupi wa Sankhya falsafiya.

Mangalacharan (washa: tabia njema) ni mazoezi ya haki bila ya kupendelea upande wowote, ukweli, na utiifu kwa Mungu na kufuata mafunzo yake kila pahali na kila mara. Kuandika cha kweli kutoka kwanza mpaka mwisho wa kitabu, unaitwa mangalacharan. Lakini si vizuri kuandika kile kilicho sawa katika sehemu nyingine na ubaya katika sehemu nyingine.

Taitteriya Upanishat, Prapathak 7, Anuvak II - Maana yake: Ewe watoto wapenzi! Nyinyi lazima mfanye yasiyo ya hatia na yasiolaumika au kazi ya uadilifu lakini si yale yaliyokuwa si ya uadilifu. Hata hivyo maelezo kama haya yanavyoonekana katika vitabu vya kisasa yanahisabika na watu wenye busara kuwa si ya kweli kwa sababu maandishi haya yanapingwa katika Vedas na maandishi ya hekima. Lakini vitabu vya Rishis (wakuona Vedic) yanayo maneno Om na Atha.

Haya ni maneno ya kuanzia maandishi. Katika njia hii hii, maneno ya hekima, na kazi za waandishi huanza na Om na Atha. Mwanzo wa Veda zote nne zina maneno haya, Agni, Indra & C. Lakini hakuna po pote maelezo kama 'Shri Ganeshaya Namah' etc.

Wale watu wanaosoma Veda kwa kutamka au kuandika Hari Om basi wamejifundisha kwa itikadi za uwongo na hadithi za uwongo au wafuasi wa Puranas na itikadi za maandishi. Neno Hari katu haliandikwi kwenye maandishi tu. Hata hivyo neno Om au Atha lazima yaandikwe mwanzoni mwa kitabu. Kwa ufupi kumhusu Mungu. Tuna sema juu ya elimu ya msingi katika sura ifuatayo.

**Muhtasari**

1. Neno Om ni jina tukufu la Mungu. 2. Maneno Agni Indra, & C yana

maana ya Mungu katika sala na mambo mengine ya dini; lakini yanaonyesha vitu vya kawaida katika elimu ya tabia na mambo ya kila siku ya maisha. Yale yaliyomo ndiyo hueleza mambo ya kweli. Kwa mfano (Saindhava) maana yake farasi na chumvi. Wakati wa safari basi huwa na maana ya farasi, na wakati wa kula huwa ni chumvi tu. 3. Kwa hivyo mifano mia imetolewa na maana zake sahihi ya maneno, ambayo yanamwonyesha Mungu katika dini. Kwa mujibu ya wakati mwingine na maana sahihi. 4. Vitabu lazima vianze na Om na Atha kama hapo zamani, na si na dua ya kunyenyekea, kama kumwamkia Mungu.

## SURA II

## ELIMU YA WATOTO

Mateuzi hava kutoka Shatapath Brahmana. Ni hakika mtu huwa mwadilifu na mtaalamu, anapobarikiwa na waalimu hawa watatu, kama (1) mama, (2) baba, (3) mwalimu. Jamii inabarikiwa, kwa sababu mtoto mwenye bahati ni yule mwenye, mama na baba waadilifu na wataalamu. Watoto hawawezi kupata faida zaidi kutoka kwa mtu ye yote isipokuwa kwa mama yake. Hapa mwingine ila mama tu ndiye apendaye kuwafanyia mema watoto wake. Hata hivyo maandisha yanatangaza: Yeye amebarikiwa ambaye ana mama anayestahiki kusifiwa na mcha Mungu. Amebarikiwa mama yule anayemfunza mwanawe jambo gani linadhihirisha tabia nzuri kutoka anapozaliwa mpaka anapomaliza masomo.

Taratibu za vyakula wakati wa Mimba. Kabla ya kuchukua mimba, wakati wa mimba, na baada ya kuzaa, mama na baba lazima wajikinge kutokana madawa ya kulewesha, mvinyo, vilivyooza na vitu vilivyo vichungu ambavyo si vizuri kwa akili; na kutumia vyakula vyenye kutia siha kama, siagi safi, maziwa, sukari, nafaka, maji na kama chakula safi na vinywaji; ambavyo ni vizuri kwa siha, nguvu, utulivu, akili timamu, ushujaa, tabia nzuri, na mwendo mzuri. Taratibu kama hizi za vyakula vitatakasa mayai ya uzazi ya mwanamke na shahawa dosari zote na kuifanya iwe mbegu nzuri.

**Wakati wa kushika mimba.**

Wakati wa kuingiliana huwa kutoka siku ya tano mpaka siku ya kumi na sita ya kupata hedhi. Siku nne za kwanza ziipukwe. Katika siku mbili zilizobaki, usiku wa kumi na moja na kumi na tatu ya mwezi pia uziipuke. Siku 10 zilizobaki ni nzuri zaidi za kuingiliana ili kupata mimba. Baada ya siku kumi na sita ya hedhi kusiwepo kuingiliana. Tena hapo kusiwepo kuingiliana mpaka hedhi nyingine itapoanza, au baada ya mwaka ikiwa mimba ilichukuliwa. Mume na mke ikiwa wana siha nzuri na akili iliyochangamka, na ikiwa hawana huzuni rohoni mwao, basi lazima waingiliane kupata watoto. Wao lazima waishi kwa mujibu wa chakula, vinywaji na mavazi kama walivyoandikiwa na daktari wa Charak na Sushrut, na waonane kila wakati ulionasihiwa na Code ya Manu, ambayo imeweka shuruti za siha na raha. Mwanamke lazima awe mwangalifu wa vyakula vinywaji na mavazi baada ya kushika mimba. Yeye asimwendee mume wake mpaka atimize mwaka baada ya kuzaa, na pia atumie vyakula mpaka wakati wa kujifungua vitavyokuza ufahamu, nguvu, uzuri, afya, ushujaa, utulivu, na sifa nyinginezo za kupendeza.

**Kuzaa.**

Baada ya kuzaa, mtoto lazima akogeshwe katika maji ya marashi na mji wake ukatwa kwa uangalifu. Mafusho yachanganyishwe na siagi safi na kufukizwa kwenye madhabahu. Mipango mwafaka lazima itengenezwe ya kukoga kwa mama na chakula chake, ili wote wawili mama na mtoto waweze

kuendelea vizuri kujipatia siha zao. Mama au wazazi lazima wale vyakula vitavyofanya maziwa kuwa mazuri zaidi.

**Utunzaji wa Utoto.**

Mama lazima anyonyeshe mwanawe 'siku sita', baada ya hapo anaweza kulelewa na mlezi. Lakini wazazi wa mtoto wampe mlezi vyakula na vinywaji vyenye siha. Wale wazazi maskini ambawo hawawezi kumwajiri mlezi, basi wavowanishe madawa ambayo yatamsaidia kupata akili, ushujaa na afaya katika maji safi, kuchemsha, na kuyachuja, na kumchanganyishia na maji kama maziwa, na kumnywisha mtoto. Baada ya kuzaa mama na mwanawe wapelekwe mahali penye hali ya hewa nzuri na yenye siha. Nyumba yao iwe na harufu nzuri na vitu vizuri. Wao wachukuliwe nje ya nyumba kujinyosha nyusha miguu na kupata hewa safi. Lakini watu wanaweza kufanya wapendavyo kuhusu mambo haya ambako mlezi au maziwa ya ngombe hayawezi kupatikana. Ilivyokuwa mwili wa mama ndiyo unawomtengeneza mtoto, mwanamke hudhofika baada ya kuzaa, na kwa hivyo yeye asimnyonyeshe mtoto wake. Kuyafunga maziwa ya mama yasitiririke dawa lazima ipakwe na matiti yasitowe maziwa. Dawa hii humfanya mzazi kujipatia siha yake kamili katika muda wa mwezi tu. Wakati huu, mwana mume asipoteze uume wake bali ajiweke safi. Wanaume na wanawake wale ambawo watafuata sheria hizi, watatunukiwa na watoto wazuri kabisa, - wataoishi maisha marefu, wenye nguvu, shujaa na wachangamfu. Na wao pia (hawo watoto) watapata watoto waadilifu na wenye tabia nzuri, na hivyo jamii zitaweza kuendelea milele. Wanawake lazima wajaribu kujponesha miili yao ya uzazi na mwanamume azitunze nguvu zake na asizipoteze bure. Njia hii itawapatia watoto wengi wenye nguvu na afya njema.

**Mafunzo ya watoto na Wamana.**

Mama lazima awape watoto wake mafunzo mema ili wao wapate kukua watoto wazuri na wenye nguvu na wasiviharibu viungo vyao vyo vyote vya miili yao. Mtoto anapoanza kusema, mama yake ajaribu kumsaidia kutamka maneno sawa sawa na kwa sauti dhahiri. Kila herufi lazima itamkwe kama itakiwavyo na kuikazia sauti. Kwa mfano, sehemu ya mdomo ya kutamkia neno pa ni midomo na mkazo wa sauti ya neno hilo iko wazi. Lazima itamkwe kwa kuchanganyisha midomo miwili na kuifungua iwe wazi. Fupi, refu, na pia herufi yenye ncha kali, na sauti nyinginezo lazima zitamkwe sawa sawa, ili sauti laini, ngumu, herufi ya kufuatanisha, mahadhi, maneno na vituo yaweze kusikika sawa sawa.

Watoto wanapoweza kusema na kufahamu kidogo, wao lazima wafundishwe maneno matamu, namna ya kuongea na wakubwa wao, watukufu, walio si watukufu, baba, mama, mfalme, wataalamu na wengineo, na vipi kuwawekea heshima wanapokuwa nawo, ili tabia zao zisiwe mbaya mahali popote, na waweze kuhishimiwa kila pahali. Mtu katu asishindwe kuwafanya watoto wapate akili, wapende kusoma, na kupenda kuwa pamoja na wale wenye adabu njema. Wao wasiwachiwe kucheza bila ya kiasi, kulia ovyo, kufanya masihara, kugombana, kucheka, kunungunika, au kuchezea kitu. Wao katu

wasiachiliwe kuwa na wivu, uadui na tabia nyingine mbaya. Wao wasijiguse guse kwa sababu watapoteza shahawa na kupata maradhi ya uhanithi, na kuufanya mkono unuke. Watoto lazima wafunzwe wawe wenye tabia ya ukweli, ushujaa, uvumilivu, ukunjufu na usafi.

**Masomo ya watoto.**

Watoto wa kiume na kike wafikapo miaka mitano, wao wafundishwe tabia za Devangari na pia za lugha ya kigeni. Tena hapo wao wafundishwe kuhifadhi kwa moyo na kujua na maana zake za Veda Mantras, mashairi au shlokas, mithali, mafungu ya nathari na mashairi yaliyo ya kuonya mema, nasiha, na adabu, na kuwafundisha namna ya kumhishimu Mungu, mama, baba, mwalimu, mtaalamu, mgeni, mfalme, raia, jamaa, dada, mfanya kazi, na wengineo, ili wasiweze kupotezwa au kudanganywa na wadanganyi.

**Uchawi.**

Wao pia lazima waambiwe habari za vitendo viovu ambavyo ni tofauti na hekima, au dini, na humfanya mtu kulaghaika; ili wao wasiamini mashetani, na mambo mengine ya upuuzi.

Manu. V. 65. - Maana ni:- Mwalimu apokuwa amekufa, maiti inaitwa 'preta': shetani. Wanafunzi wanaichoma hiyo maiti na kusaidia kuichukua maiti hiyo mahali pachomwapo maiti, inadhifishwa katika siku kumi pamoja na hawo walioichukua jeneza hiyo. Maiti inapochomwa, inaitwa 'bhuta', maana yake kilichokwenda, i.e. yeye alikuwa fulani bin fulani. Wale wanazaliwa lakini hawapo tena, wanaitwa waliokwisha pita: 'bhuta' maana yake hasa ni 'iliyopita'. Haya ni maoni ya wataalamu kutoka Brahma mpaka mabingwa wa kisasa pia. Lakini yule aliyena wasi wasi, ndiyo huwa na marafiki wabaya, na tabia ovu, na lazima awe na khofu na shaka ambayo hugeuka kuwa mashetani, zimwi, jini, pepo na madanganyo ya kuadhibisha, atayopata kwa khiyali yake mwenyewe. Mtu anapokufa, roho yake inaingia katika mwili mwingine kuchuma matunda ya furaha na maumivu kutokana na vitendo vizuri na vibaya katika serekali ya Mungu Mwenyewe. Jee kuna mtu anaye weza kuvunja amri ya Mungu Mwenyewe? Watu wajinga ambawo wao hawajasoma au kufikiria vitabu vya utabibu au ujuzi wa mwili, husema weweseko, homa na maradhi mengineyo ya mwili, na wazimu na magonjwa ya akili kama hayo kuwa ni mambo ya uchawi, mashetani na mengineyo. Bila ya kuwafanyia dawa za madaktari na kuwa ponyesha, wao huweka itakadi zao kwa wadanganyifu, walaghai, wapumbavu, wafanya maovu, watu wanaozipenda nafsi zao, matopasi, washona viatu, watu wa kabila hafifu, washenzi na takataka wengine wa mji. Wao hufanya ushirikina wa namna nyingi, hila, ulaghai., kula takataka za chakula, kuvaa nyuzi za zinguo, hirizi, kauri na maneno ya kunuizia uchawi, na kuwa shawishi watu wengine pia kutumia vitu vya uwongo. Wao hupoteza pesa zao, huwaharibu watoto wao, huengeza magonjwa, na kujizidishia shida.

Hapo hawa majuha, ambawo ni vipofu wa akili na waliovimba kwa dhahabu, wanakwenda kwa hawa waovu, watu wenye dhambi na wanaojipenda wenyewe

tu na kuwa hutubia wao: Ewe mfalme mkubwa, haijulikani mtoto huyu wa kiume, kike, bibi, au bwana ana nini. Wao hujibu: Shetani mkubwa, pepo, jini, shetani wa tete kuanga, au zimwi kama hilo ndilo limemvaa. Yeye hata weza kutokana nawo hawa mpaka nyinyi mfanyie dawa halisi au yeye anaweza kufa. Ikiwa nyinyi mtaweza kutuletea mikate ya sukari au zawadi, sisi tutamtoa pepo kwa nguvu za uchawi wetu, wanatamka maneno ya kichawi na vitendo vinginevyo vya ujanja. Tena hapo watu na jamaa zao na wafuasi wao ambawo vipofu wa akili hulia: Ewe mfalme mkubwa, sisi tuko tayari kuitoa mali yetu yote, ikiwa wewe utaweza kumponya huyu tu. Tena hapo hawo majambazi hujiona wamo katika dunia yao wenyewe. Tena hapo husema: Haya basi, lete chakula kiasi maalum, na kiasi maalum cha zawadi ili tuwape miungu ya kike, na toweni sadaka ili mujikinge na bahati mbaya za nyota. Tena hapo wao huimba na kucheza kwenye toazi, na kijigoma kidogo, ngoma, nakumpigia huyo mgonjwa au huyo aliyepatika na pepo. Mmoja katika majambazi hawa huanza kucheza na kufanya mzaha wa kiwazimu na kusema: Nitamuua yeye. Tena hapo hawo majuha humwangukia miguuni huyo mshona viatu au mwenye kabila ya chini na kumlilia: Chukua utakacho, lakini mponyeshe mgonjwa. Jambazi hujibu: "Mimi ni Hanuman (Jemedari wa kima wa maha). Nipeni mimi siagi, mafuta ya kupikia, rangi nyekundu, mkate mmoja kwa kipimo na robo (100ths), na suruali nyekundu." au, mimi ni miungu wa kike au Bacchus wa India. Nipeni mimi chupa tano za divai, kuku ishirini, mbuzi wa tano, haluwa na nguo." Tena hapo hawo hujibu: Wewe unaweza kuchukua cho chote unachotaka. Hapo mchawi huanza kucheza cheza na kuruka ruka sana. Lakini ikiwa mtu mwenye busara akimpiga mara tano na viatu, na kumrushia gongo, ampige kofi au amsukume huyo aliyejifanya Hanuman, mungu wa kike, au Bacchus, atatosheka mara moja na kumwachilia mbali yeye kabisa; kwa sababu, ulikuwa uwongo dhahiri wa kunyanganya pesa na vitu vyengine vya maana kutoka kwa watu wa kawaida.

**Unajimu.**

Wao wanapokwenda kwa wanaojitia kuwa ni wanajimu, ambaye ametandwa na nyota ya uovu, na mwenye umbo la nyota ovu, na kumwuliza: Ewe mfalme mkubwa, huyu ana nini? Yeye hujibu: Yeye amedhurika na jua na sayari nyingine katili. Ikiwa nyinyi mtashika maandishi ya Veda mantras, inayoanza kwa neno shanti: amani, mpango wa ibada, na kutowa sadaka: yeye atapona, ama si hivyo si ajabu kama atakaiona kifo baada ya kuugua sana.

Mtu wa kawaida - Ati si kwa sababu ya sayari ndiyo wafalme na raia zao hufurahia na kuwa na raha au taabu katika dunia?

M. - La, na matokeo ya vitendo vizuri na vibaya.

M.K. - Basi ujuzi wa sayari ni uwongo?

M. - La, kila kinachosemwa kuhusu ujuzi, nambari na mistari, yote ni kweli; lakini yote yale yanayosemwa kuhusu athari za nyota basi yote ni uwongo.

M.K. - Jee falaki haina maana?

गुरु विरजानन्द दण्डी
सन्दर्भ पुस्तकालय
परिग्रहण क्रमांक 622

M. - Ndiyo; haina maana. Haitaki iitwe falaki, lakini "falaki za huzuni"; kwa sababu mtoto anapozaliwa watu wa nyumbani wote wanafurahi. Lakini furaha zao huishia hapo falaki yake inapokwisha tengenezwa. Askofu anapoomba ruhusa ya kutengeneza falaki, wazazi wa mtoto humwomba: Ewe mfalme mkubwa, tengeneza falaki nzuri. Ikiwa baba wa mtoto ni tajiri, basi askofu atachora mistari miekundu mingi, manjano na mingineyo ya rangi nyingine; lakini ikiwa baba ni maskini, yeye hutengeneza falaki ya desturi tu na kuichukua nyumbani kwa mtoto na kuwasomea wazazi wake, ambawo hukaa mbele yake na kumwuliza:- Jee falaki ya mwana wetu ni nzuri? Mnajimu hujibu: Mimi nitawasomea kama ilivyo. Nyota za kuzaliwa na zile zilizo za kirafiki zote zinaonyesha heri. Nguvu zao zitamfanya awe mheshimiwa. Mkutano wo wote atakaohudhuria yeye, wote wale watakao kuwapo hapa watamheshimu. Yeye atakuwa na afya na atatukuzwa sana mjini. Baada ya kusikia yote haya ya kuwalaghai wazazi na majamaa wa mtoto watashangiriana kusema, Ewe mnajibu mtaalamu, wewe ni mtu mzuri kabisa. Lakini yeye anajua vilivyo kuwa hayo maneno mazuri tu hayamletei faida yo yote. Kwa hivyo yeye husema kweli hayo yote yanaonyesha mambo mazuri sana, lakini kuna nyota mbaya pia, ni kusema kwamba, kupambana kwa nyota hii na hii italeta kifo chake katika mwaka wake wa nane. Hapo tena wazazi hupoteza furaha waliyoiona hapo alipozaliwa mtoto wao, basi huzama katika bahari ya huzuni, na humwuliza mnajimu: Ewe mfalme mkubwa, sasa sisi tufanye nini? Tena yeye hujibu: Tengenezeni zawadi. Baba mtoto anauliza: Tuchukue hatua gani sisi? Mnajimu tena hapo anafahamisha kwa urefu viz, sadaka kadha wa kadha itolewe. Amekaa na kuonyesha onyesha huko kwenye nyota mbaya. Walisheni Ma Brahman kila siku. Mpango huu inaweza kugeuza ubaya ya nyumba tisa. Neno inaweza linatumika ili pawepo njia ya kuokoka, ili ikiwa mtoto atakufa, yeye ataweza kusema kuwa hakuna msaada wa jambo kama hilo. Hapana aliye na uwezo juu yake Muweza Mwenyewe. Mimi nimejaribu niwezavyo, na nyie pia; lakini ni bahati ya mtoto, au ndiyo vilikuwa vitendo vya maisha yaliyopita. Ikiwa mtoto ataishi, yeye hujivuna na kusema: Tazama nguvu za uchawi mungu wa kike na Brahmanas! Wao wamemhifadhi mtoto wako. Kwa hivyo inatakikana kuwa ikiwa huo uchawi wao unapokosa kuleta mafanikio yo yote watu kama hawo lazima walazimishwe kulipa mara mbili au tatu kuliko matumizi yaliyotumika kutokana na amri zao. Lazima watoleshwe wao hata ikiwa mtoto amehifadhika; kwa sababu, kama wanajimu wanavyosema, "Hapa mwenye uwezo wa kuangamiza vitendo vya mtoto vya maisha yaliyopita, au kupinga amri zake Mola," kwa hivyo watu husema, "Mtoto huyu amehifadhika na kifo kwa sifa za kazi zake za maisha yake ya ndani na kwa sheria zake Mungu, lakini si kwa nguvu zao wao. Pia waalimu hawo na hawo wengineo wanaowababaisha watu kutoa sadaka na misaada ambayo wao wenyewe huitia mifukoni mwao wenyewe, lazima wahisabiwe kuwa ni wanajimu.

**Ndui na Uchawi.**

Kuhusu Mungu wa kike wa ndui, uchawi, ushirikina, na mambo mengine ya kichawi, kifua kikuu hayo yote ni ushirikina tu. Waganga wengine wanasema kuwa ikiwa wao wakimpa mtu kitu kilichotiwa uchawi au uzi wa uchawi baada ya

kuusomea maneno ya kichawi, Mungu wao wa kike na bwana wa shetani ataondosha maovu yote kutokana naye kwa nguvu za vitu vyao vya uchawi. Wachawi hawa na wa shirikina yapasa waulizwe: "Mnaweza kumvusha mtu asife, uwezo wa sheria ya Mungu, na matokeo ya vitendo? Watoto wengi wanakufa kwa kutoweza kustahamili matokeo ya vitendo hivyo vyenu. Wewe mwenyewe unampoteza mpendwa katika jamii. Utaweza kukiepuka kifo?" Maswali kama haya huwanyamazisha watu kama hawa, na wana kuwa na hakika kama ujanja wao hautafaulu mbele yako. Basi vituko hivi vyote lazima viwachilieni mbali. Waadilifu, wakarimu na wasiojipendelea nafsi zao tu wahutubu na watu wenye busara lazima wasaidiwe na kuandikiwa ilivyokuwa wao wanaifanya dunia mambo mazuri. Upendeleo wa kusoma katu usidharauliwe.

**Elimu ya alkimia.**

Hawo wanaojifanya kama wao wanatengeneza dawa yenye nguvu za ajabu ya kuongeza urefu wa maisha, kuiletea kifo kwa uchawi, kuleta wazimu, kuwafanya watu kuwa watumwa na kufanya miujiza, lazima wawekwe chini kama wajinga wa mwisho. Watoto lazima waanze kuambiwa na kufahamishwa vilivyo uchawi na vituko viovu, ili wao wasije wakadhuriwa kwa kuangukia mitegoni pao hawa wahalifu.

**Kuzitunza Nguvu.**

Wao pia waambiwe kuwa kuzitunza nguvu zao itawaletea furaha na kwa kuzipoteza hizo nguvu huleta uharibifu wa mwili na mashaka. Kwa mfano, mtazame mtu, furaha aliyonayo na uchangamfu anaouhisi kwa kuwa na afya nzuri, akili za mtaalamu, kujihisi mwenye nguvu na bashasha, navyo vyote ni matokeo ya kuzitunza shahawa katika mwili. Njia bora zaidi ya kujitunza ni wanafunzi wajiepushe na kusoma au kusikiliza hadithi za mapenzi au hekaya za uchu, marafiki asherati, na kufikiria vitu vya kuleta raha, kuwatazama wanawake, na kushirikiana nawo, kuzungumza nawo, kuwakumbatia na mambo mengineyo ya mapenzi. Wao wajishughulishe na kujilinda na kujipatia, ukweli wa heshima na ujuzi wa kweli katika masomo yao. Yeye anayepoteza uume wake, huwa hanithi na asherati sana na fisadi. Yeye anayepata ugonjwa wa kaswende, hudhoofika, huwa hana damu, hana rangi, hana uwezo, upara, hawezi kudumu, hana ushujaa, ujasiri, na sifa nyingi, na mwishowe huangamia.

**Onyo la wazazi.**

"Ewe nyinyi watoto! ikiwa nyinyi mtapoteza jursa hii ya kupata mazoezi ya uadilifu na elimu sahihi, na kuujenga mwili kwa kufuata kiapo cha utakatifu, basi hamtapata tena wakati kama huu wa thamani katika maisha yenu. Ilivyokuwa sisi, wazazi wenu, tunaziweza kuzifanya kazi zetu za nyumbani na tuko hai kwa rehema zake Mungu, nyinyi mjishughulishe kupata elimu na kuendeleza mbele hali zenu na kuijenga miili yenu." Mawaidha kama haya ndiyo inapaswa wapewe watoto na wazazi wao. Pia ni maneno haya matriman; heshima ya mama na pitriman; heshima ya baba - yanatumika katika vitabu vilivyotanjwa hapo juu.

Kwa maneno mengine, mama lazima amsomeshe mtoto tokea anapozaliwa mpaka anapotimia umri wa miaka mitano na baba kutoka mwaka wa 6 mpaka mwaka wa 8, na anapoingia mwaka wa 9, anaanza kufanya (Brahmans, Kshatriyas, na Vaishyas), baada ya kuwapatia watoto wao uzi mtakatifu, wao wawapeleke; watoto wa kiume na kike Acharya Kula (gurukul), ambako wataalamu mashuhuri wa kiume na kike wanasomesha na wafungua skuli za kuwafunza vijana. Shudras (Wale wa Kabila la chini) na makabila mengine hafifu, bila ya kufanya sherehe za uzi mtakatifu, lazima wawapeleke watoto wao Guru Kula kwa ajili ya elimu.

**Adabu.**

Watoto wale wasiodekezwa, lakini kwa upande mwingine wao wanawakazania sana hapa wanapokuwa wanapata mafunzo, huwa wataalamu, wenye heshima, na wastaarabu. Imesemwa kwa usahihi katika ufasaha wa Sanskrit, unaoitwa Mahabhashya, VIII, i, 8, kuhusu jambo hili:

Mababa, na wamama, na waalimu ambawo wanatilia nguvu masomo ya watoto wao na wanafunzi wao, basi kama ilivyo, wanawapa kinywaji cha Mungu mikono yao wenyewe, lakini wale wanaowapenda kwa mapenzi mengi, wanawapa sumu kula, kwa mfano tu, kuwaharibu na kuwaangamiza. Kwa sababu, kuwapenda sana huleta uharibifu wa tabia nzuri. Watoto na wanafunzi huwa na furaha zaidi ikiwa wanalazimishwa na kuwa hawana furaha kuliko kutendekezwa saa zote. Hata hivyo, mama, baba na mwalimu asiwatie adabu watoto wao au wanafunzi wao kwa kuwaonea wivu au chuki. Kwa nje wawaonyeshe macho makali lakini moyoni wawe na mapenzi na huruma.

**Mafunzo Ya Uadilifu.**

Kama masomo ya vitabuni, basi wao lazima pia wafundishwe wajiepushe na wizi, uasherati, uwivu, dharau, ulevi, uwongi, kuchinja, udhalimu, wivu, tamaa ya mali na maovu kama haya mengi mengineyo, na wajifunze tabia njema, kwa sababu mtu hata akiiba mara moja tu au akizini, na kusema uwongo, au akifanya uovu wo wote mbele ya mwingine, basi hupoteza heshima yake ya milele mbele za watu. Hapana mwenye aibu zaidi kama yule anayevunja ahadi au anaye sema uwongo. Kwa hivyo ikiwa utatoa ahadi basi lazima uitimize. Kwa mfano, mtu amemwambia mwenzake: mimi nitakuona wewe saa kadha na pahali kadha, au nitakupa kitu kadha wakati mahsusi, basi lazima atimize ahadi yake sawa sawa, au hapana atakaye kumwamini tena. Kwa hivyo wote lazima waseme kweli na watimize ahadi zao. Mtu asiwe mwenye kiburi. Udanganyifu, hila, na ukosefu wa hisani huchoma moyoni mwa mtu huyo anayeyatenda haya, bali na maumivu ya watu wengine wanaofanyiwa ubaya kama huu. Udanganyifu na hila ni vitendo viovu ambayo mtu hujitia navyo ambazo mtu utamwona vengine usoni lakini moyoni yeye huwa mwengine hujaribu kumghilibu mtu awe anamsikiliza yeye tu, na hajali hata chembe upotovu wa wengine, lakini huyazungusha yake tu kwa njia yo yote ile. Kukosa hisani nikutajali yote unayofanyiwa ya wema na wenzako.

**Tabia njema na utiifu wa Wazazi.**

Uchungu, lugha isiyo na huruma, na tabia nyingi nyinginezo mbaya kama hizi lazima ziachiliwe mbali. Maneno ya upuuzi lazima yaepukwe. Wao wasiseme haba wala zaidi kuliko wanavyotakiwa. Wao lazima wawaheshimu wakubwa zao. Wakubwa zao wakija basi wao lazima wanyanyuke na kuwakaribisha kwenye kiti cha juu. Baada ya kuwaamkia au kuwatolea namaste (salamu zako), wao lazima wakae kwenye kiti cha chini. Katika mkutano wao wakae pahali ambapo mtu hawezi kuwaondoa kuwatoa nje. Wao wasigombane na mtu. Wao wawe na bashasha, wakubali ya hadhi na kukataa ya uwongo. Wawe na marafiki wema na kuwaepuka waovu. Wao wawatumikie mama, baba, mwalimu kwa maisha yao, moyo, uwezo, vitu jamili na mapenzi.

**Ukweli na wema.**

Uko ubeti katika taithriya Upanishat, vii II. Madhumuni yake ni kuwa mama, baba na mwalimu lazima awafundishe watoto na wanafunzi ukweli. Pia wao lazima wawaambie kuwa na kufuata vitendo vyao ambavyo ni vya mwema na kuvikataa vitendo vile ambavyo si vyema. Ukweli wo wote ule wao wanaujua basi lazima wahutubie na kuuandika. Wao wasiwaamini wajanja na watu walaghai. Wao wafanye yote kwa moyo wa dhati kazi za wema ambazo baba, mama na mwalimu wanazowaamrisha kufanya. Mwalimu lazima afahamishe tena maana ya vile vipande vya Nighantu, Nirukta na Ashtadhyayi, ambayo wazazi wao waliwahifadhisha, au mashairi mengine au Mantra za Veda. Wao lazima wamtukuze Mungu katika roho zao kama alivyoelezwa Mungu katika sura ya kwanza ya kitabu.

**Hadhari ya Afya.**

Wao lazima wale, wanywe, na wavae na wafanye kazi yo yote ile yenye kuwaletea faida katika siha, elimu na nguvu zao. Kwa maneno mengine ni kusema, wao wale kidogo kasoro ya njaa walionayo, na wasile nyama, mvinyo na vyenginevyo vinavyo levya. Wao wasijitumbukize katika maji ambayo hawajui urefu wake, au wao watapatikana na shida kutokana na wanyama wa majivi au vitu vyengine, au kama wao hawajui kuogelea basi wanaweza kuzama. Manu anasema - usiingie kuoga katika maji usiyoyajua.

Manu, VI,46 - Wakati wa kwenda mtu lazima aweke macho yake kwenye njia, na kuendelea baada ya kuona urefu na upana wa njia. Maji lazima yachunjwe kwa kitambaa kabla ya kunywa. Yale yalo sahihi lazima yasemwe. Kazi lazima ifanywe baada ya kufikiriwa sawa sawa.

**Wajibu wa Wazazi.**

Haya yamesemwa na mwandishi wa mashairi katika Chanakya Niti. Wale mababa na wamama ambawo hawajawasomesha watoto wao elimu yo yote basi wao ni maadui wao wakubwa. Watoto hawo wanapokuwa wakubwa wanadharauliwa katika miongoni mwa wataalamu na kuonekana kama kunguru kwenye ndege kama bata. Ni wajibu mkuu wa wazazi na wema mkuu wao

wakujulikana wanapowafanya watoto wao wawe wataalamu, wastaarabu na wenye elimu ya kutosha kwa kujinyima wenyewe raha, fikira na mali. Mashauri haya mafupi kuhusu elimu ya watoto wa kike na kiume yanatosha kumfanya mwenye busara kuyakuza.

**Muhtasari.**

Mtu huwa mzuri ikiwa mama yake, baba, na mwalimu ni waadilifu na wataalamu. Wakati mwanamke ana mimba lazima ale mboga na maji safi, lakini asile nyama na vinywaji vya kulevya. Mume wake asipoteze shahawa zake. Wao wasionane kimwili mpaka mwaka mmoja baada ya kushika mimba. Siku za kuonana ili kupata mimba ni siku kumi baada ya siku ya nne ya hedhi usiku wa kumi na moja na kumi na tatu uepukwe. Baada ya kuzaa mama na mtoto waishi pahali pazuri na safi. Mama au mlezi anaweza kumnyonyesha mtoto. Lakini wao lazima wale vyakula vyenye siha. Mama na baba lazima wamfundishe mtoto kutamka maneno sawa sawa na kumsomesha elimu ya mwanzo kama mashairi ya Veda maneno mengine ya uadilifu na maana zao. Mtoto lazima aonywe kuhusu uchawi, ulozi, unajimu na ualakamia.

Utakatifu na mila za kimwili lazima zifunzwe. Masomo ya uadilifu na ya elimu ya chooni yafuatane pamoja mkono kwa mkono. Tabia nzuri na heshima isijeikapotea. Kwa ufupi, ni wajibu wa wazazi kuwasomesha watoto wao vyema kwa vyo vyote.

## SURA YA III

## ELIMU YA CHUONI
## (KUPATA NA KUTOA ELIMU)

Sasa katika sura ya tatu tutaelezea nidhamu ya elimu - kupata na kutoa elimu. Kazi muhimu ya baba, mwalimu, na jamaa ni kumwelimisha mtoto kwa elimu iliyo bora zaidi, wajibu wa kazi na kupata sifa nzuri, uadilifu na tabia nzuri. Roho ya mtu haiwezi kupambwa kwa vyombo vya dhahabu, fedha, yakuti, lulu, marijani na vito vyengine vya thamani. Kwa sababu, mapambo ya mtu kwa vyombo hufanya sifa ya bure tu ya mwili na kupendeza kwenye raha zipatikanazo mwilini tu, na pia zinaleta wasiwasi wa waizi na wenginewo, hata huweza kufikwa na ajali ya kifo. Inaonekana dhahiri hapa duniani watu waovu wanavyo waua watoto na watu kwa ajili ya tamaa ya mapambo.

**Elimu na Ukarimu.**

Wamebarikiwa wanaume na wanawake wale ambawo akili zao zimeshughulika kutafuta elimu, tabia latifu na adabu nzuri, wao ambawo wanafuata kanuni za ukweli na uadilifu mwingine, wao ambawo wako mbali na kiburi na uchafu, wao ambawo wanaangamiza maovu ya wenzao, wale ambawo wamepambwa na mapambo ya kushiriki ukweli, wao ambawo wanapunguza maumivu ya utu katika dunia kwa kuwapa maarifa watu na wao ambawo wanawafanyia wengine vizuri kwa njia na nidhamu ambazo zimeamrishwa na Vedas.

**Kutiwa Skuli.**

Wakati watoto wa kiume na kike wanapofika miaka minane, wao inatakiwa wapelekwe kwenye (wanaume kwenye za kiume na wanawake kwenye kike) skuli zao. Walimu wa kiume na kike wenye adabu mbaya wasiachiliwe kusomesha watoto. Wale wanaofaa kusomesha ni wale tu wenye ujuzi na waadilifu. Kuwapamba watoto wa kiume kwa uzi mtakatifu na kuwapatia ushirika mtakatifu na muwafaka kwa watoto wa kike nyumbani, wale watu wa kabila duni na waliozaliwa mara mbili lazima wawapeleke watoto wao kwenye skuli zao ambazo zinaendeshwa na waalimu wenye sifa kama zilizokwisha semwa.

**Mahali pa skuli.**

Pahali pa nchi ambapo hapatembelewi ndipo lazima pachaguliwa kuwa pahali pa elimu. Skuli za watoto wa kiume na kike lazima zijengwe kwenye masafa ya umbali wa maili mbili kutoka umbali mwengine. Waalimu, watumishi na wafuasi lazima wote wawe wanaume katika skuli za kiume na wanawake katika skuli za kike. Mtoto wa kiume hata wa miaka 5 asiachiliwe kuingia skuli ya kike na mtoto wa kike asiachiliwe kuingia skuli ya kiume. Kwa maneno rahisi zaidi watoto, wanapokuwa wajane na wasichana bado wao lazima wajifunze kuwa watakatifu katika masomo yao ya shuleni, wao wasijizoeze kuwa kuonyeza wanaume au wanawake, kuwakumbatia, kuishi kwa siri, kuzungumza, kusikiliza

hadithi za mapenzi, kufanya riyadha pamoja na kufikiria furaha za uchu na raha zao, ambazo ni namna nane za uasherati.

**Kuangalia mwenendo na kuwachukia kwa usawa.**

Waalimu lazima wawaepushe wanafunzi wao kutokana na tabia za uharibifu ili wao waweze kujipatia elimu iliyo bora zaidi, uadilifu, adabu, tabia na kujipatia maendeleo ya akili na mwili, na waweze kukuuza furaha yao ya milele katika maisha yao. Skuli lazima ziwe umbali wa maili 4 kutoka mjini. Wanafunzi wote ikiwa tajiri au maskini wawekwe sawa sawa kwa kupewa chakula, kinywaji na pa kukaa na kulala. Wao wote iwe wanapenda kupata elimu. Wanafunzi wala wazazi wasiachiliwe kuonana au kuandikiana, ili wanapokatizwa na shughuli zote za dunia, wao wataweza kupata fikra za kupata elimu tu katika akili zao. Wanapotoka kwenda kutembea nje, lazima wafuatwe na waalimu wao, ili wao wasifanye kitendo cha uovu cha aina yo yote na kijifundisha tabia ya kupuuza.

**Elimu ya lazima.**

Kwa hakika lazima iwepo amri ya serikali na desturi za kitaifa kuwa watu wasiwaweke watoto wao wa kiume na kike nyumbani wanapotimia umri wa miaka 8. Wao lazima wawapeleke skuli au watatiwa adabu. Kwanza kuvishwa watoto wa kiume uzi mtakatifu ufanywe nyumbani na kisha kwenye nyumba ya wasimamizi wa shule.

**Maana ya Gayatri au Mashairi ya Itikadi ya dini.**

Wazazi na waalimu lazima wawafunze watoto na wanafunzi itikadi ya Gayatri shairi ya Veda na maana yake. Hayo ni kama ifuatavyo.

**"Aum, Bhur, Bhuvah, Swah, tat Savitur varenyam bhargo devasya dhimahi, dhiyo yo nah prachodayat."** Maana ya AUM katika mwanzo wa shairi la hapo juu imetolewa katika sura ya kwanza, ambayo itaweza kusomwa. Sasa sisi tutatoa maana kwa ufupi ya silabi zilizofichika zinazoitwa **Vyahrities.**

Bhuh ni jina la Mungu, ni kuonyesha maisha ambayo ni nguvu au kuwepo kwa dunia zote, ambayo imejiweka wenyewe na ya thamani zaidi kuliko maisha ya binafsi.

Bhuvah ni jina la Mungu, kwa sababu neno hili lina maana kuwa yeye ambaye yuko mbali na adhabu na ushirikiano wake huwatowa watu katika utumwa wao.

Swah ni jina la Mungu, kwa sababu neno hili lina maana kuwa ni yeye aliyeenea katika dunia nzima, na yeye ndiye anayewasaidia viumbe vyote vilivyomo humo.

Silabi hizi tatu zimetolewa katika **Taitteriya Aranyak.**

**Sala**

Na tukumbuke daima utukufu ukunjufu na wa juu kabisa, Mwenyezi

Mungu mwenye hekima na busara, ambaye ni mtukufu na anyeitakasa tabia, ambaye ni mzazi wa dunia nzima na mtoaji wa rehema zote, yeye ambaye ni mpaji wa raha zote, na maarifa yake yanatakiwa na watu wote, ili yeye ambaye ni baba na wa kiroho na mwongozi wa wataalamu wetu, atuhifadhi kutokana na vitendo viovu na kutuongoza sisi kwenye kazi nzuri.

Enyi watu, hebu na tuutukuze utukufu wa Mwenyezi Mungu, ambaye ni Bwana wa mabwana, Yeye ni Mwenye nguvu kuliko wenye nguvu wote, mwenye tabia ya ukweli, uaminifu na furaha, ambaye ni Mtukufu wa daima, maisha Yuko Macho, na maisha yuko Huru katika tabia zake, yeye ambaye ni Bahari ya Huruma hakimu asiyependelea upande wowote, aliye mbali na adhabu ya kuzaliwa na kufa, yeye ambaye hana umbo au si kama kitu chochote miuzi wa fikira za mioyo yote, msaidizi wa wote, Baba Mmoja, Mzalishaji, na mpaji wa chakula na vitu vyenginevyo duniani! Yeye ni mwenye kumiliki mali zote, Mtengeneza wa dunia, mtakatifu, na mpendewa na wakufikiriwa kwa haja zote, Yeye, Mwenyezi Mungu anaeishi katika moyo wetu na kuwangarisha wataalamu wetu, anayeweza kutuepusha na tabia mbaya na isio adilifu na kutuongoza kwenye tabia za kiadilifu na njia ya kweli. Sisi katu tusimwache na kupendelea kitu chengine; kwa sababu hapana aliye sawa naye, si mrefu kuliko Yeye! Yeye Peke Yake tu ndiye Baba Yetu, Mtawala, Hakimu na mpaji wa Rehema zote.

**Namna ya kuabudu.**

Kwa kuwapa mafunzo ya dini, Gayatri ubeti wa Veda, wazazi na waalimu wa wanafunzi lazima wafunze modus operandi ya kusali na kuabudu, ambayo inashikilia kukoga, kunywa maji kidogo ili kusafisha koo, na kuifanya damu izunguke na mambo madogo ya mpango kama huu.

Kusudi ya kukoga ni kuhusu usafi na kuviweka viungu vya nje vya mwili. Kwa kuthibitisha kauli hii, tunataja beti ya 109 uthabiti wa sura ya Muhtasari wa Manu.

Maji yanasafisha viungo vya nje vya mwili, tabia nzuri husafisha nia, elimu na kutokuwa na raha za dunia, haya ni kuwa, kuaadilisha uadilifu katikati ya shida zote; safisha akili, hekima, au kubagua elimu kwa wote kutoka katika dunia mpaka ufikapo kwa Mungu, inang'arisha ufahamu na kuifanya imara katika dini. Kwa hivyo kukoga ni lazima kabla ya chakula cha usiku.

**Kuvuta puumzi kwa nguvu.**

Kuabudu kwa roho inahitaji kanuni za kuvuta puumzi, ambayo inatiliwa mkazo na satwa ifuatayo:- Yoga, 11 28

Hizi ni mithali ya maneno kutoka falsafa ya Yoga. Mtu anapoanza kufanya mazoezi ya kuzuia kuvuta puumzi, uchafu wote au tamaa mbaya inaangamizika pole pole katika wakati huo, kwa hivyo ujuzi wa roho yake hung'ara zaidi na zaidi ili ujuzi wake unaendelea kuzidi mpaka uwokovu wake pia unaathirika.

Kuweza kuzizuia puumzi kunatakasa. Upande wa juu ya koo na ubongo na huzifanya kuwa na nguvu, kama usafi wa dhahabu na shaba nyinginezo inaathirika kwa moto, ambawo huondoa uchafu.

**Namna zake.**

Ni mithali fupi ya Yoga. Kama matapishi ya nguvu hufanya chakula na maji ya tumboni kutoka mdomoni, kwa hivyo pumzi hutolewa kwa nguvu wakati wa kupumzika na zisiwachiliwe kurudi tena kwa kadiri ya nguvu za mtu. Kupumua puumzi sehemu ya chini kabisa (mkundu) inatakiwa kuvutwa juu. Puumzi zinatolewa nje mpaka mvutano unapomalizika. Katika njia hii puumzi zinazimiwa mpaka unapoanza kusikia vibaya, hapo basi utaanza kuzishusha puumzi kwa kadiri ya uwezo wako. Hivi mtu aendelee kufanya mara zote zile anazoweza. Neno Om lazima lisemwe kila mara akilini. Kazi hii inasaidia kusafishi na kutuliza roho na moyo.

**Sehemu zake Nne.**

Kwa maneno mengine, namna hizi nne 1. Kutoa puumzi nje kwa muda mrefu 2. Kuvuta puumzi ndani kwa muda mrefu 3. Kuwacha kuvuta puumzi mara moja kwa muda mrefu. 4. Kuzizuia puumzi za ndani pale zinapotoka nje, kwa kuzivuta ndani tena, kwenda kinyume nazo, na kuziziwia puumzi za nje, hapo zinapotaka kutoka nje, kwa kuzitoa nje na kuzizungusha na kuzizuia. Kwa kuvuta puumzi kinyume na ilivyo kitendo cha kuvuta na kushusha puumzi husahihishika, na kupumua pia huzuilika, moyo na akili huletewa pamoja na kuwa chini ya akili au roho.

**Faida zake.**

Ushujaa huzidi, ufahamu huwa mwingi na mkali ili kurahisisha jambo ngumu na kuwa rahisi kwa upesi. Husaidia kupatisha nguvu mwili, pia huongeza uthabiti ngumu, ushujaa, kumiliki hisia, ili mtu aweze kuzishika namna zote za falsafia katika muda mfupi tu. Wanawake pia lazima wafanye Yoga au kuitenga akili katika njia hii hii.

**Mafunzo ya adabu nzuri.**

Wanafunzi lazima wafundishwe namna nzuri ya kula, kuvaa, kwenda, kukaa, kuondoka, kuongea, na namna ya kuwaheshimu watu duni na watukufu.

**Brahma Yajna au kuabudu.**

1. Watoto lazima wafundishwe Sandhyopasana: Ushirika Mtukufu - sala za asubuhi, ambazo zinaitwa kuabudiwa kwa Mwenyezi. (Vide wajibu kubwa tano za Ma-Arya).Unapokaa kuomba inakupasa unywe maji kidogo tu yale yanayoitwa Achaman, ambayo yanaweza kuchukulia katika kiganja chako tu na ambayo ya kufika kwenye koo tu, si zaidi wala kasoro kuliko hayo. Yananyonywa kwa kuweka midomo katikati ya kiganja. Hii huondosha kooni balgham na nyongoni pia.

Tena ahadi ya busara, inayoitwa Marjan, lazima ifanywe. Maji yanyunyizwe

juu ya macho na viungo vyingine na sehemu za kati na kwenye vidole ili kuuondoa usingizi. Ikiwa usingizi haupo, na hapana maji hapo karibu, basi unaweza usifanye yote haya.

Wao lazima wafundishwe Pranayam: kuzizuia puumzi kwa ubeti wa Vedic, tukufu kwa akili au mandhari kamili ya maumbile, inaitwa Manasa Pakriama, kujidhihirisha kwa Mungu katika akili, inaitwa Upasthan, kuimba sifa zake Mungu, sala na fikira zake. Yeye, zinaitwa Upasana. Pia wache wajifundishe Aghamarshan, i.e. kutaka kufanya maovu katu yasifikiriwe. Sala hii ya asubuhi na jioni isaliwe pahali pa kupumzikia kwa furaha na uangalifu.

Hivyo ndivyo anasema Manu, II, 104. Watu lazima wende mwituni au Pahali pa Ukiwa, wajiweke kwa makini, wasimame ukingoni mwa maji, na ufanye ibada ya kawaida na usome tena gayatri au nyimbo za dini na maana zake (katika akili). Lazima wazitengeneze tabia zao kwa mujibu huo. Lakini mazoezi yafanywe kwa upesi kama iwezekanavyo.

**Deva Yajna au kuabudu Moto.**

Huduma ya pili ni kafara ya Moto, ambayo ni kuunguza madawa katika moto, jamii ya wataalamu na huduma zao. Sala na Kafara ya moto lazima lifanywe mara mbili asubuhi na jioni tu; kwa sababu kuna viungo viwili tu vya usiku na mchana na hakuna chengine tena. Taamuli lazima ifanywe saa moja kabla na baada ya kufanya Yoga ya kujinyima vitu na mambo ya kufurahishua, yeye ambaye ana uazimia utukufu wa Mungu anapokuwa katika hali ya kuzirai.

**Zana za Kuabudia Moto.**

Wakati wa Kafara ya Moto ni jua linapokwisha chomoza tu na kabla ya jua kutua. Kwa kazi hii (1) Namna ya meza au bafu kama la kukogea ya shaba au udongo, ambayo lazima iwe vidole 12 au 16 pande zote tatu, lakini sehemu yake ya chini iwe vidole 3 au 4 mraba, ni kusema, mdomo wake uwe mara nne kuliko tako lake katika eneo. (2) Vipande vya sandali, "palash (butea frondosa) au kuni za mwembe, ambazo ni mzuri kushinda kuni zote, zinaweza kufanywa vipande vikubwa au vidogo kwa mujibu wa hiyo meza na kutiwa humo. Katikati ya moto utiwe na kuni zilizotajwa hapo juu zipangwe pembezoni. (3) upawa (4) Sufuria (5) Sufuria ya siagi safi, na (6) kijiko kiwe cha dhahabu, fedha, au bao. Maji yatiwe katika sufuria na upawa, au kikombe kilichotengenezwa kwa ajili hii. Lazima kiyeyushwe kwenye moto. Vyombo hivi, upawa na sufuria ni vitu ambavyo ni rahisi kuchotea maji na kukoshea mikono. Siagi iliyosafishwa inataka itizamwe sawa sawa ifanyiwe kafara katika moto kwa mashairi haya:-

Kila kafara inapotolewa lazima ubeti usomwe. Lakini ikiwa sadaka nyingi zinataka kutolewa basi ubeti ufuatawo wa Veda na shairi la dini lisomwe tena kwa kila sadaka inayotolewa.

Om, Bhu, Pran, na mengineyo ni majina ya Mwenyezi Mungu. Maana zao zimeshaelezwa. Neno Swaha (Amin! au Selah!) maana yake ni yale uliyonayo

moyoni, lazima yasemwe, na la kama si hivyo basi. Kama Mungu Muweza ameumba, vitu vya dunia hii kwa ajili ya urahisi na raha za wanyama wote, basi kwa hivyo binadamu pia wawafanyie wenzawo yote yale yaliyo ya wema kadi wawezavyo.

**Faida za Havan au Sadaka za Moto.**

Swali - Nini faida za Havan au Sadaka za Moto?

Jawabu - Watu wote wanajua kuwa harufu mbaya ya hewa na maji machafu huleta magonjwa, ambayo humletea binadamu maumivu. Lakini, kwa upande mwingine, hewa na maji safi hukuletea siha, na kutokuwa na maradhi hukuletea raha.

Swali - Haileti faida kujisugua na kujipaka sandali kwenye maungo ya mtu, kumpa mtu ale siagi safi, badala ya kuvitia vitu hivi kwenye moto kupotea bure? Jee inaonyesha kitu chenye maana yo yote kwa mtu anayefanya hivyo?

Jawabu - Ingekuwa wewe unajua elimu ya tabia za vitu vyote, hutasema hivyo, hakiharibiki kitu au kupotea bure. Watazame watu wanawo simama mbali na nafsi ya havan au kuabudu moto, nusa harufu inayopeperusha na hewa.

Katika njia hiyo hiyo, wao pia husikia harufu mbaya pia. Kwa hivyo inakuonyesha wazi kuwa kitu kikitupwa motoni husafishika na kwenda na upepo mbali ambako inaondoa harufu mbaya.

1. Kumwabudu Om, Mungu msifiwa, wa maisha.
2. Kumwabudu Om, Mungu Mwenyezi, mtukufu.
3. Kumwabudu Om, Mungu wa milele, mwenye furaha.
4. Kumwabudu Om, wa maisha, mtukufu, mwenye furaha, Mwenyezi, na wa milele.

2. Ewe Mungu, Baba, huondoa uovu wote na hutupa yale yaliyo mema kwa ajili yetu.

Swali - Ikiwa hivyo ndivyo, basi kwa nini wewe huweke katika nyumba yako zaafarani meski, maua ya kunukia, mafuta mazuri, na vitu kama hivi vya kuleta harufu nzuri ili kuinukiza vizuri hewa iliyomo katika chumba na kuwa furaha wote?

Jawabu - Harufu haina nguvu ya kusafisha hewa isiyo safi ya nyumba na kuleta hewa safi kutoka nje; kwa sababu haina nguvu ya kuiozesha hewa iliyokwisha oza au hewa yenye dhara na kuitoa nje ili kuifanya hewa safi ya nje ije ndani.

Swali - Nini faida ya kusoma mashairi au mantras kwenye shughuli za kuabudu moto?

Jawabu - Mashairi au mantras huelezea faida za kuutolea sadaka moto na ukizisoma kwako hukufanya uzikumbuke, na kwa hivyo hukukumbusha yale

uliyosahau ya Masomo ya Veda.

Swali - Jee ni dhambi ikiwa huuabudu Moto?

Jawabu - Ndiyo, watu hufanya dhambi nyingi kwa sababu wao huleta maumivu na mashaka kwa viumbe kwa kuongeza maradhi, ambayo hutokea kwa kuiharibu hewa na maji kwa kuyatia harufu mbaya na uchafu ambazo hutokana katika miili yao. Kwa hivyo, kufuta dhambi zilizokwisha fanywa, harufu, sawa na hivyo au zaidi ya hivyo ili ilete furaha, lazima ziongezwa katika hewa na maji. Utoaji wa chakula na vinywaji huleta furaha na nafuu kwa mtoaji tu. Siagi iletayo harufu nzuri na kusafisha ambayo mtu hula, huwaletea faida mamia na maelfu ya watu kwa kutolea kama sadaka ya moto.

Ikiwa watu hawapati siagi safi au vyakula maakuli vya kujenga akili, basi nguvu za miili yao na akili hazitakuwa bora. Kwa hivyo vyakula maakuli vya kujenga mwili lazima wapewe watu kula na kunywa. Lakini havana lazima ifanywe na watu. Iwe ni lazima katika sherehe za kuabudu.

Swali - Sadaka ngapi zifanywe lazima, na iwe kiasi gani kila kafara?

Jawabu - Kila mmoja afanye mara 16, na siagi safi na manukato mengine au vitu vyakuua wadudu kila mara iwe na uzito wa masas 6 au nusu ya rupia moja. Ikiwa inaweza kutolewa zaidi ya hiyo basi ni vizuri zaidi. Kwa hivyo, vito vya thamani na majivuno ya Ma-Arya, watu wakubwa, watu wanaojua elimu ya tabia na mazingira, profesars na wale wenye hekima tukufu, wafalme na wafalme katika siku za zamani walifanya havan kwa wingi, na waliwaomba wengine pia wafanye hivyo. Mpaka hapo mazoezi na tabia za havan zikifanywa zaidi, India hapo Aryavarta, ilikuwa haina magonjwa na ilikuwa imejaa raha. Hata mpaka sasa ikiwa tabia hii italetwa tena, basi raha hiyo hiyo na itarudi tena.

Hizi ni kazi mbili mwanafunzi anahitajiwa kufanya, viz. (I) Brahma Yajna, ambayo ni kusoma, na kutoa elimu, kuzisoma sifa za Mungu sala, na kuabudu, (2) Deva Yajna, ambayo ina kutolea sadaka moto, ashwamedha na mambo mengine ya dini, kuwatumikia wataalamu na wafuasi wao. Basi sala na sadaka za moto peke yake zifanywe na mwanafunzi katika maisha yake ya skuli aliyoyatolea kupata elimu.

Maneno haya yametoka katika sura ya pili ya Sushrut. Maana yake ni kuwa Brahman anaweza kuwa na vyeo vitatu, viz, Brahman, Kshatriya na Vaishya, kwa uzi mtukufu na kuvisomesha; Kshatriya, amri mbili, viz, Kshatriya na Vaishya; na Vaishya, moja tu, viz, Vaishya. Ikiwa pana Shudra (mtu mwenye kabila la mtumishi) aliyetoka katika jamii nzuri na mwenye adabu nzuri, yeye lazima asomeshwe maandishi yote matakatifu na vitabu vya Ma Veda. Shudra anaweza kusoma; lakini asitunukiwe uzi mtakatifu. Hii ni fikra ya Ma - Acharyas wengi au profesas wa dini.

**Brahmacharya: Maisha ya skuli kabla ya kuoa au kuolewa.**

Watoto wa kiume na wa kike, baada ya mwaka wa tano, wanapelekwa

kwenye skuli zao, wao lazima waanze kila wakati mafunzo yafuatayo.

Kiapo cha kuoa kifanywe na wanafunzi kutokana miaka 8 mpaka 36, i.e. miaka 12 lazima itumike kusomea kila moja ya Vedas tatu na tafsiri pamoja na majafanuzi zao, ambayo kwa jumla hufanya iwe miaka 36 pamoja na miaka 8 ya kabla ya skuli ikicahnganywa huwa ni miaka 44. au kiapo kinaweza kuwekwa kwa miaka 18, ambayo pamoja na miaka 8 kama ya hapo kwanza huifanya iwe miaka 26. Au, inaweza kuwekwa kwa muda wa miaka 9, au mpaka unapomaliza kupata masomo:- Manu, III, I.

**Daraja zake tatu.**

Masemo sita ifuatayo imetokana na Chhandogya Upanishat. Kuna daraja tatu za kiapo cha kutofunga ndoa za mwanafunzi.

1. Daraja ya chini kabisa ni mtu ambapo, mwili wake uliofanyika kwa chakula, na vitu vyengine vya kujenga mwili, imejawa na roho, na mwenye wajibu wa kuishi na wenzake wazuri na kutenda vitendo vyema, lazima asome Vedas na maandishi mengine matukufu na ajifunze tabia nzuri katika miaka 24 ya kiapo cha mwanafunzo cha kutofunga ndoa na kuziweka akili zake ziwe timamu. Yeye asijishughulishe na mambo ya uchu hata baada ya kuoa. Ndipo hapo mwili wake utakuwa wenye nguvu katika maisha na sifa nzuri zitamwandama yeye.

Sehemu ya kwanza ya maisha itumike katika kutafuta elimu. Mwalimu lazima awahimize na kuwanasihi ili wasome. Mwanafunzi kila mara anataka aamini kuwa ikiwa ataweka na kukifuata kiapo cha utakatifu sawa sawa katika sehemu yake ya mwanzo ya maisha, mwili wake na roho yake zitakuwa na siha, na nguvu, na maisha yake yatakuwa na sifa njema. Ewe kiumbe, zidisha furaha na raha katika njia hii. Jiambie mwenyewe, ikiwa sitageuza nakukivunja kiapo cha kutooa, na ikiwa nitaoa baada ya miaka 24 ya umri wangu, inaonyesha wazi nitakuwa mwenye siha na maisha yangu yatafikia miaka 70 au 80.

2. Sehemu ya kati ya utakatifu ni wakati ule mtu anapokiweka kiapo cha kutofunga ndoa cha mwanafunzi kwa muda wa miaka 44 na akajiweka kujipatia elimu saa zote, puumzi zake, akili, ushujaa, na roho yake pia huwa na siha na yenye nguvu. Yeye huupinga upungufu na kuuhifadhi uwezo.

Yeye lazima amwambie mwalimu wake, ikiwa mimi nitaitumia sehemu yangu ya kwanza ya maisha katika Brahmacharya: kiapo cha utakatifu na unguvu, maisha yangu yatakuwa ya furaha na nitaweza kuyashinda sehemu ya kati ya utukufu. "Ewe mwanafunzi", mwalimu lazima awambie wanafunzi wake, "kama mimi nilivyofanya na nimekuwa mwenye kiwili wili cha binadamu kilicho jitolea kwa kukishika kiapo cha utakatifu. Mimi nimetoka katika jamii za waalimu wale wa kale, na nimejiepusha na magonjwa na mimi nina siha nzuri daima. Fanya yale mwanafunzi mzuri hufanya katika maisha yake.

3. Sehemu ya tatu ya utakatifu ni bora kuliko zote. Unaendelea mpaka miaka 48 ya kuishi. Yeye huwa mwalimu wa nafsi yake na kuwa na ujuzi wa sehemu zote,

yeye ambaye hujiweka mjane wakati wa kupata elimu.

Mwalimu, baba na mama lazima wawazoeze watoto kujinyima raha zote kwa kupata elimu na tabia njema na kila mara wawaeleze faida ya mambo haya katika sehemu ya kwanza ya maisha yao. Watoto na wao pia lazima wakiweke kiapo cha ujane imara na kwa njia hii wao wataweza kuitimiza sehemu ya tatu ya utakatifu wanakuwa wataalamu na kuishi kikamilifu kwa miaka 40. Wao lazima wafuate mawaidha ya waalimu wao. Kwa, wanafunzi wale wanaokifuata kiapo hicho cha ujana na katu hawakivunji, wao wako huru daima kutokana na maradhi na wametunukiwa uwezo, mali na wokovu.

**Sehemu nne za Mwili.**

**(Sushrut.)** Mwili huu una sehemu 4. sehemu ya kwanza ni kukua, ambayo kukwishia kutoka miaka 16 mpaka 25 ya maisha, na katika miaka hii sehemu zote za mwili zinakua. Sehemu ya pili ni ile ya ujane, ambayo inaanzia kutoka miaka 25. Sehemu ya 3 ni ile ya ujana na ya ukamilifu, ambayo huendelea mpaka mwaka wa arubaini, ambapo sehemu zote za mwili hufikia utu uzima. Sehemu ya nne ni ile ya ukamilifu, ambapo viungo vyote vya mwili hukamilika katika kukua. Baada ya wakati huu wingi wa shahawa hutoka usingizini, huzidi jasho na ni wakati wa kuusafisha mwili, hasa ilivyokuwa hauwezi kujiweka tena. Mwaka huu wa 40 ni bora hasa wa kufunga ndoa. Lakini mwaka bora zaidi wa kufunga ndoa ni 48.

Swali - Jee hii sheria ya kiapo cha utakatifu ni sawa kwa mwanamume na mwanamke?

Jawabu - La. Ikiwa mwanamume anakiweka kwa muda wa miaka 25, basi mwanamke aweke kwa muda wa miaka 16. Ikiwa mwanamume anabaki mjane kwa muda wa miaka 30, mwanamke abaki hivyo mpaka miaka 17. Ikiwa mwanamume hajaoa mpaka miaka 36, mwanamke abaki hivyo mpaka mwaka wa 18. Ikiwa mwanamume amebaki mpaka miaka 40, mwanamke abaki mpaka miaka 20. Ikiwa mwanamume amebaki kwa miaka 44, mwanamke abaki mpaka miaka 22. Ikiwa mwanamume amejiweka mpaka miaka 48, mwanamke afanye hivyo mpaka miaka 24. Hivyo ni kusema, mwanamume asiendelee na kiapo cha zaidi ya miaka 48, wanawake zaidi ya miaka 24. Lakini sharia hii ni wale wanaotaka kuoa. Lakini wale wasiotaka kuoa kabisa, wanaweza kubaki hivyo mpaka kufa kwao, wao wana hiari. Hata hivyo, hii inaweza kufanywa na wale wanaume na wanawake waliosema sawa sawa, wao ambawo ni makwana wa akili zao na ni hawo wasioweza kushindwa na hata na kosa moja, hawa ni wale waliojinyima raha za dunia au ni Ma-Yogi. Ni kazi ngumu kabisa kujizuia na nguvu za uchu na kuiweka akili chini ya moyo mgumu.

**Sharia za mafunzo.**

**(Tait.)** Imeweka sharia kwa ajili ya waalimu na wanaowafundisha. Sharia zenyewe ni. 1. Kusoma na kusomesha huhitaji uwe na tabia njema na iliyosawa. 2. Watu lazima wajifunze na wasomeshe yale ya kweli katika elimu. 3. Wao lazima wawe wenye kujinyima na kufanya mazoezi ya uwema katika kusoma

na kusomesha Vedas na maandishi matakatifu. 4. Wao wajizuie na upungufu wakati wa kusoma na kusomesha. 5. Wao saa zote wapime akili zao ili kujepusha na namna zote za ukosefu wakati wa masomo na kusomesha. 6. Elimu ya sheria ya kutoa sadaka ya moto na moto wa umeme lazima yafikiriwe katika kusomesha na kusoma. 7. Kafara ya kuabudu moto lazima ifanywe katika kusoma na kusomesha. 8. Wao lazima wawakaribishe na kuwatumikia wageni au wazifuate hekima wakati wa kusomesha na kusoma. 9. Utulivu wa mwalimu na anayesomeshwa hukaribishwa kwenye elimu iliyo thabiti kwa mwanadamu. 10. Wao wasome na wasomeshe sheria za kuwahifadhi watoto na serikali. 11. Wao wajihifadhi na wazidishe nguvu zao wanapokuwa masomoni. 12. Wao lazima wajue namna ya kuwahifadhi watoto wa kiume na wanafunzi wanaosomeshwa.

**(Manu, IV, 204)** Mtu mwadilifu lazima afikirie Yamas (kazi za uadilifu) na si Niyamas (sherehe za dini) tu. Bila ya kufanya Yamas, mtu huanguka kutoka kwenye wema, ijapokuwa yeye anafuata Niyamas. Yamas ziko za namna tano. Hizo zimetolewa katika mithali za falsafia ya Yoga.

**(Yoga, II. 30)**

1 Kuhusu ukweli wa fikra, usemi na vitendo.
2 Kuwacha kuiba kwa akili, neno, na vitendo.
3 Kuwa na nia njema.
4 Kutokuwa na kutokuwa na fahari.
5 Kuwacha kujipendelea mwenyewe na kuwa kigeugeu kupita kiasi. Hizi Yamas tano au vitendo vya maadili. unadhitu wa tabia, lazima uangaliwe, na si Niyamas tu.

**(Yoga, II, 32)** Mithali hii inahesabu Niyamas 5. Kujisafisha kwa kukoga na kama hivyo (2) Kutosheka (si kuwa mvivu) bali kwa kutumia nguvu zako zote bila ya kushangiria faida na kuhuzunishwa na hasara. (3) Kuendelea na vitendo vya uadilifu hata ukiwa na shida ya mwili. (4) Kusoma na kusomesha (5) Kujitolea kwa maisha katika ibada ya Mwenyezi Mungu. Hizi ni Niyamas 5. Hizi lazima zifuatwe na si kwa kutolewa kwa wajibu wa uadilifu. Lakini yote mawili yafuatwe. Yeyote hawezi kuendelea ambaye anafanya Niyamas bila ya Yamas, lakini huendelea kushuka chini na chini, i.e. hata huwa wa dunia.

Kuwa na hamu ya kupita kiasi na kutoathirika hata kidogo si mambo mema kwa mtu ye yote; kwa sababu ikiwa hakuna nia ya kujipatia elimu ya Vedas na kutenda kazi zake zinazotaka kufanywa na wao na kazi nyinginezo za uadilifu haziwezi kutekelezeka, - Manu, 11, 28.

Mwili umetengenezwa Brahman (mwili) unaofaa kumwabudu Mungu na masomo ya Veda, kwa masomo na mafundisho ya kila namna ya elimu, kwa kutii viapo vya utakatifu na ukweli, na kwa kutoa sadaka za moto, kuwa na ukweli na kukataa ya sio ya kweli, kwa vipawa vya maarifa mbali mbali, kwa kuabudu na mambo mengineyo yanayohusika na Vedas, kwa kufanya yote haya katika wiki

mbili na sadaka nyinginezo, pia kwa kuzaa watoto, kwa kufanya wajibu mkuu (1) Tendo la kusujudu, (2) kuabudu moto (3) kuwatumikia wazee (4) kuwalisha wasiojiweza na wanyama pia (5) ukarimu wa wataalamu, wageni, kwa kutoa sadaka na kujifunza kazi za mikono na kutengeneza vitu, na sayansi na sanaa nyingine. Bila ya kutokuwa na haya yote, mtu huwa si Brahmanized.

Kama dereva stadi huwaweka farasi wa gari lake kwenye njia ilivyo sawa, basi mtu pia ajaribu kwa njia zote kuziziwia hisia zake zisitamani raha za uchu, ambazo hufanya nia na akili kufanya vitendo vya dhambi:- Manu, 11, 88.

Roho inafanywa kuwa mtumwa wa hisia basi hupatwa na uovu na udhaifu; lakini unapoziweka hisia zako sawa sawa, basi utaongoka; kwa ajili. Yeye ambaye ana tabia mbaya na hawezi kuziziwia hisia zake, hawezi kufanikiwa katika Veda, kumshukuru Mungu, Yoga, kujitolea na kutoa sadaka, Niyamas, utakatifu, ajinyimaye raha za dunia hata za halali, au kazi nyingine zo zote - Manu, 11, 97.

Hakuna njia ya mkato au mapumziko katika elimu na mafunzo ya Veda, kutimiza kazi au wajibu tano kubwa na kujitolea muhanga wa moto:- Manu, 11, 105.

Kwa sababu, hapana kikomo katika kazi za dini za kila siku, ambazo lazima zifanywe, kila siku kazi za kutanafusi zinaendelea na katu haisimami. Haitaki isimamishwe hata kwa vyo vyote, kwa sababu, muhanga wa moto hata katika mapumziko vitendo vya dini vinastahiki kutimizwa. Kama inavyojulikana kuwa ni dhambi kusema uwongo, na ni sifa njema kusema ukweli, kwa hivyo kila mara inakatazwa kuwa wa wafisadi na inaidhiniwa kufanya vitendo vya uadilifu- Manu, 11, 106.

Sifa zake nne, viz, umri, elimu, umashuhuri, na nguvu au uwezo, unazidi daima, yeye ambaye ni mpole na mwenye adabu nzuri, yeye ambaye ni mtaalamu na anawatumikia wakubwa zake na vizee: lakini wale ambawo hawafanyi hivyo, wao wamenyimwa maendeleo ya sifa hizi nne. - Manu, 11, 121.

Wataalamu na wanafunzi lazima wawache kuoneana wivu na lazima wahutubu mambo mazuri kwa binadamu wote. Wahubiri lazima wazungumze maneno mazuri na matamu. Wale wanaotaka kufaulu katika dini, lazima wafuate ukweli na wahubiri ukweli: - Manu, 11, 159.

Mtu yule hustahili masomo ya Vedant au krimu ya ukweli wa Vedic, lugha yake na mawazo yake ni safi na mwenye kuweza kuzizuwia hisia zake sawa sawa- Manu 11, 160.

Brahman yule anayemjua Mungu na Veda nzima na ambaye anazikimbia sifa kama mtu anayoikimbia sumu, na staha haihimidi kama maji matamu katika maua. Manu, 11, 162.

Katika njia hii, wanafunzi wakisasa, wote wanaume na wanawake wajishughulishe katika masomo ya Vedas, watiwe roho tena kwa kutunukiwa kwa uzi mtakatifu, lazima waendeleze elimu yao ya Vedas. Manu 11, 164.

Yeye ambaye hajifunzi Veda na anajaribu sana katika masomo mengine basi hugeuka kuwa Shudra kwa haraka au hua mwenye kabila duni na watoto wake wa kiume na wajukuu wa kiume:- Manu, 11, 168.

Wanafunzi wanaume na wanawake waliojishughulisha na masomo ya Vedas lazima wajiepushe na utumiaji wa mvinyo, nyama, mafuta mazuri, mapambo ya maua, vinywaji, kumtazama au kumkumbatia mwanamume au mwanamke, achari, uchinjaji wa wanyama. - Manu, 11, 177.

Wacha wao wasijipake mafuta ya mwili, kugusa tupu zao, wasitie wanja katika macho yao, wasitumie viatu, na miavuli, matamanio ya uchu, uchungu, tamaa ya mali, unyonge, woga, huzuni, wivu, uadui, dansi, kuimba, kutumia ala za muziki - Manu, 11, 178.

Wao wawache kucheza kamari, kusengenyana, uchongezi, uwongo, kuwatazama wanawake kwa uasherati, maumivu kwa wengine, na ufisadi mwingine kama huu - Manu 11, 179.

Wao lazima walale pekee yao daima - wasipoteze nguvu zao katu, ikiwa mtu anapoteza shahawa yake kwa uasherati tu, basi yeye huangamiza kiapo chake cha utakatifu, ndivyo inavyosema.

**Mafunzo ya uadilifu.**

1. Mwalimu lazima awafundishe masomo ya uadilifu kwa wanafunzi wake wa kike na kiume:- 2. Daima sema kweli. 3. Tenda uadilifu. 4. Wacha kuwa bila ya uangalifu katika kusoma au kusomesha. Ukiweke kiapo cha utakatifu bila ya kukivunja kwa kujipatia elimu za aina zote. 5. Mpe mwalimu vitu vya thamani. Oa na zaa watoto. 6. Usiuache ukweli kwa kuwa mzembe. 7. Usiache dini kwa kuipuuza tu. 8. Usiiharibu siha, ustadi, na ufanisi kwa dharau tu. 9. Usiwache kusoma na kusomesha kwa kuwa mzembe. 10. Usiwe mdhaifu wa kumtumikia Mungu, wataalamu, baba, mama na wakubwa zako. 11. Daima watumikie baba, mama, mwalimu na wageni kama unavyowatumikia wataalamu. 12. Tenda vitendo vizuri na kazi zenye uadilifu, kama kusema kweli mengineyo kama haya. Usifanye katu yale yaliyo kinyume ya haya, kama vile kusema uwongo na mengineyo. 13. Viige vitendo vyetu vizuri, ambavyo vimefungamana na dini, lakini katu usiviige vitendo vyetu viovu. 14. Daima ujiweke na Ma-Brahmin walioosoma na wenye dini, ambawo ni waaminifu, na wewe pia uwaamini wao. 15. Toa sadaka, kwa kuamini, toa bila ya kujali, toa kwa kujulikana, toa kwa stara, toa kwa kuogopa, toa kwa kulipa ahadi. 16. Wakati wo wote unapopatwa na watu ambawo hawapendelei upande wo wote, Ma Yogi au wale wanaoweza kuana ambayo wote hawayaoni, watu wenye mioyo yenye huruma, wenye nia ya na matatizo ya namna yo yote, basi ujiweke imara kama wanavyojiweka wale watu ambawo hawapendelei upande wo wote, Ma Yogi au wale wanaoweza kuona ambayo wote hawayaoni, watu wenye mioyo yenye huruma, wenye nia ya kufanya vitendo vizuri na wanaomcha Mungu. 17. Hii ni sharia, hili ni somo, hii ni Upanishat. (arki) ya Ma-Veda, Hii ni nasiha. Fanya haya tu, na zitengeneze tabia zako zilingane na hizi tu.

Watu lazima wafahamu kuwa hata kupepesa jicho haiwezekani ila mtu anapokuwa na nia, hata hivyo inaaminiwa kuwa mtu afanyapo chochote basi huwa hafanyi bila ya kuwa na nia ya namna yo yote mbele yake.

Mtu lazima awe mwadilifu daima; kwa sababu ni mwisho wa msemo wa kusikia kuhutubia na kusomesha watu lazima watimize kazi zilizounganishwa na Ma-Veda na sheria zinazofuatana nawo.

Kwa hivyo, mtu yule hawezi kupata matunda ya uadilifu uliounganika kwa mazoezi na Ma-Veda, mwenye tabia zisizo njema, lakini yeye peke yake anapata furaha ya ukamilifu ambaye anaishi maisha ya uadilifu baada ya kumaliza masomo yake. - Manu, I, 109.

Mtu anayewapinga Ma-Veda, na kazi zilizoandikwa na hekima na uangalifu na Ma-Veda, lazima afukuzwe yule mtu asiyesadiki kuwa yuko Mungu na anayewatukana Ma-Veda mbali na waadilifu kabila, jamii na mji.

Ishara nne za uadilifu ambazo zinajitenga na ubaya, ni: 1. Veda 2. Mafuatanisho ya sheria, ambazo ziliandikwa na ulinganifu unaokubalika na Ma Veda, kama vile sheria za Manu. 3. Tbia za uadilifu au kazi za maisha. Mungu kufuatia Veda. 4. Kutosheka kinafsi, au kile kichopendwa na roho kama vile kusema kweli. Dini ni tabia, ambayo ina mazoezi ya sheria na haipendelei upande wo wote, kuukubali ukweli na kuukataa uwongo kabisa. Tabia kinyume na hii, iliyojaa mapendeleo, kutofuata sheria, kuukataa ukweli, kuukubali uwongo inaonyesha ukosefu wa dini.

Wao wanapata masomo ya dini ni wale wasio kuwa na tamaa ya dhahabu na johari, na washiriki wanawake na raha nyinginezo. Wao wale wenye kutaka elimu ya dini, basi lazima waihakikishe kwa Ma-Veda; kwa sababu dini na kutokuwa na dini haviwezi kubagulika sawa sawa bila ya kuwategemea Ma-Veda - Manu, II, 13.

Mwalimu lazima awaonye wanafunzi wake. Pia mfalme na wanachama wengine wa daraja ya kishujaa, na wadaraja ya wafanya biashara na watu wenye hekima lakini wa daraja ya watumwa basi hawa wote lazima wafunzwe kwa uangalifu; kwa sababu ikiwa Brahmans tu ndiyo watakawo someshwa, na si wengine, basi hapatakuwa na maendelea katika masomo, serikali, utajiri na kwenye vyuo vyenginevyo. Brahmans wanategemea majeshi na amri nyinginezo kwa ajili ya kujihifadhi na ndiyo waongozi wao. Hawana mwongozi aliye juu yao. Pia hakuna wakuwa adhibisha kwa makosa yao. Lakini, amri zote zinafuatwa kwa unafik. Lakini shujaa na watu wa tabaka nyingine wanapo elimishwa, Brahmans husoma zaidi na kuifuata njia ya dini. Wao hawawezi kuufuata unafik na uwongo mbele ya watu wa daraja nyinginezo. Lakini majeshi wanapo amrisha wafanya biashara, wafanya kazi, na ikiwa wao hawana elimu, Brahman hufanya wapendavyo na huwafundisha wengine pia kufanya yayo hayo. Kwa hivyo, ikiwa Brahmans wenyewe wanajipendelea, basi wao wawaombe mashujaa na watu wengine wafuate Vedas na maadishi matakatifu kwa sababu wao tu ndiwo wanaweza kuendeleza ujuzi wa elimu, dini, serekali na utajiri. Wao hawa ombi maisha, kwa hivyo wao hawawezi kupendelea upande mmoja zaidi katika anasa za dunia na elimu. Watu wa daraja zote wapopata elimu ya kutosha na kuwa na tabia njema basi hawawezi kudanganywa na kughalibiwa. Basi kwa sababu hii

inayojulikana ni Brahmans na watawa huwaongoza mashujaa na wenginewo kwenye njia ya dini na wao wenyewe wana wekwa kuwa wa kweli na watawa. Kwa hivyo elimu lazima itiliwe mkazo na wanaume na wanawake wa daraja zote.

**Sababu ya majaribio**

Cho chote kile kilichosomwa na kusomeshwa, lazima kijaribiwe kwa vilivyo. Sababu za majaribio ni za aina tano (1) Yale yaliyo dhaniwa, vitendo na namna ya Mungu, na pamoja na maelekeo ya Vedas, ni kweli; na ni kinyume chake; si kweli. (2) Chochote kile kilicho sawa na amri ya maisha, ni kweli; na chochote kile ni kinyume chake, si kweli; kwa mfano, kauli ya kuwa mtoto anazaliwa bila ya kuwa na baba wala mama si kweli, kuwa kinyume cha amri za maisha. (3) Chochote kile kilicho thabiti na mafunzo ya waokozi, wataalamu, wenye kusema kweli na yakunyooka, hukubaliwa, lakini yale yaliyo kinyume na haya, basi hukataliwa. Ukweli wa mtu katika usawa huwa wazi kwenye elimu, i.e. kama sisi tunavyopenda raha na kuchukia maumivu, basi lazima tufahamu daima kuwa, ikiwa sisi tunampa raha au taabu mtu yo yote, basi yeye ataadhirika kwa mujibu huo huo. (5) Namna nane za madhihirisho, viz (i) Hisia (ii) Kujua jambo kwa kuijua sababu yake (iii) usawa wa tabia (iv) mafunzo ya mtaalamu au maandishi matukufu, (v) Historia, (vi) Mazungumzo (vii), Uwezekano, (viii) Kutokuwapo.

**Namna nane za ushuhuda**

Mithali zilizotolewa hapa chini ni kama ufupisho wa namna ya ushuhuda na zimo katika Sura ya II ya mantiki.

I. Elimu inayopatakikana pale penye nia na akili, ya akili na nia, - shikio, ngozi, jicho,ulimi, pua, na akili na vitu vyake, sauti, mguso, umbo, ladha, harufu. huitwa Pratyaksha: Hisia (a) Lakini kile kinachotokana na vyapadesha, i.e. uhusiano wa neno na jambo, si hisia kwa ukweli wake. Kwa mfano, mtu humwambia mwenzake, "Niletee maji". Yeye huyaleta na kuyaweka mbele yake na anasema, 'Haya ni maji'. Lakini neno maji, haliwezekani kuonekana na watu hawo wote wawili. Kitu ambacho kinaitwa maji, kinaweza kuhisiwa tu. Elimu inayo patikana kutokana na sauti, huangukia kwenye kichwa cha mtu binafsi au kwenye ushahidi wa maandishi (b) Kwa mfano mtu anapoona nguzo usiku na akasadiki na kufikiria kuwa ni mtu, lakini anapoona mchana kitu kile kile kuwa ni nguzo tu na si kuwa ni mtu kama alivyofikiria hapo usiku kwenye giza. Basi ujuzi kama huu wa kuitakidi kitu unaitwa Vyabhichari. (c) Kwa mfano mtu anapoona mchanga kwenye ukingo wa mto na akafikiria kuwa ni nguo zimeanikwa kutoka mbali au labda pana kitu chengine. "Yupo Deva Datta amesimama au Yajna Datta". Ikiwa hakuna uhakikisho wo wote basi haiwezi kuitwa hisia. Kwa hivyo hisia ni elimu ile ambayo si ya kudanganya, inayoweza kugeuka, si isiyo na hakikisho.

II. Ikiwa sehemu ya kitu au kitu kizima kimeweza kukisiwa kwenye pahali kadha au saa kadha, ujuzi wa kitu hicho, japo hakijaonekana, lakini kupatikana kwa kuhisi tu japo sehemu moja tu ya kitu hicho kwenye sehemu moja tu ya pahali kadha, huitwa, kujua jambo kwa sababu yake. Kwa mfano, sisi huanza kumjua baba kwa kumwona mtoto wake, kujua kuna moto kwa kuona moshi kwenye mlima, kuona maisha kwa kupata furaha na maumivu katika dunia. Kujua kitu

kabla ya kuliona jambo hasa ni ya namna tatu:- Purvavat: kama tunavyoiona mvua inakuja tunapoanza kuyaona mawingu, kuona watoto wanakuja tunapoona harusi inaposherehekewa, na kupata elimu tunapowaona wanafunzi wanaposumbuka kuitafuta hiyo elimu. Kwa ufupi, ni ujuzi wa kujua matokeo ya kitendo kinachofanyika (2) Sheshavat: ambayo ni elimu ya kitendo inayotokana na jambo: kwa mfano sisi hutambua kuwa mvua nyingi inayoanguka mashambani husababishwa na mto, kuwepo kwa baba kwa kumwona mwanawe wa kiume, kwa kutojua mwanzo wa sababu ya kuwepo kwa Mungu muumba na alivyoviumba, na furaha zake na maumivu kutokana na kuchungua uzuri na uhalifu katika tabia za mtu. (3) Samanyatodrishta: ni ujuzi ule ambawo hauna uhusiano kuwa sababu ya matokeo, lakini huwa na mambo yenye tabia namna moja. Kwa mfano, hapana mmoja anayeweza kwenda kutoka pahali hapa kwenda pengine bila ya kujiondoa, basi hata mtu fulani naye pia hawezi. Neno anuman huleta ujuzi huo ambalo hupatikana husia inapofanyika. Kwa hivyo hapana awezaye kufikiria moto usionekana bila ya kuhisi au kuona moshi.

III. Ushahidi wa kifani ni uhakikisho ambawo unatokana na mapatano muhimu ya kujulikana kwa akili.

Kwa mfano, mtu anamwambia mfanya kazi wake amletee Vishnu Mitra ambaye amefanana na Deva Datt. Mfanya kazi husema kama yeye hajapata kumwona. Bwana wake hujibu, Vishnu Datta ni kama Deva Datta hapa. Au, chukua mfano mwingine; Nil gao (paa) katika msitu ni kama ng'ombe huyu. Mtumishi anapokwenda pahali hapa, anaona Vishnu Mitra anafanana na Deva Datta, na kwa hivyo yeye anahakikisha kwamba yeye ndiye mtu anayetakiwa hapo. Kwa hivyo anamchukua mtu huyo mpaka kwa bwana wake. Au, kwa mfano mwingine, anapokwenda msituni na anapomwona mnyama kama ng'ombe, yeye anahakikisha kuwa ndiye nil gao, na humleta nyumbani. Huitwa usawa wa tabia.

IV. Amri ni ule ushahidi ambawo ni mawazo ya mtu aliye mtaalamu, mwadilifu, mkarimu, mkweli, mwenye nguvu, mtulivu, anayependelea uzuri wa watu wote, na anayejilazimisha kuwaambia wenzake kwa busara namna ya kujipatia furaha kwa yale yaliyo mazuri akilini mwake, haya ni mambo ya mtu aliye na elimu duniani na ya Mwenyezi Mungu pia. Maoni ya mwanachuoni kama huyu na ujuzi wa kuwepo kwa Mungu, ambapo ma-Veda wanapoweza kuhesabikana kama ni wenye amri na ushahidi wa Hati takatifu. Inaweza kuitwa Ya kibinafsi au ushahidi wa maandishi matakatifu.

V. Ushahidi wa Kihistoria unaonyesha matokeo hasa ya vitendo vya watu, hasa ni, maisha au maandiko ya habari za maisha ya mtu.

VI. Ushahidi wa usemi: kwa mfano, inapohakikishika kuwa kuwepo kwa mawingu huleta mvua, au kila kitu kina sababu yake, imehakikishwa bila ya shaka yo yote kuwa haiwezekani kabisa kuja mvua bila ya kuwepo mawingu, na hakuna kitu bila ya sababu.

VII. Uwezekano. Kwa mfano, maneno thabiti ya watu kama - fulani bin

fulani alizaliwa bila ya wazee, mtu fulani alimwamsha maiti, aliinyanyua milima, aliieleza mawe kwenye maji ya bahari, augawanya mwezi vipande viwili, Mungu alikula nyama; mtu fulani ana pembe, mtu wa kiume na wa kike wa mwanamke tasa walioana, na mengi kama haya, yote ni vitendo ambavyo haviwezi kutokea, kwa sababu ni kinyume cha sheria za maisha. Yale yaliyoelekea na maisha ndiyo yanawezekana kutokea.

VIII. Yasiyokuwapo kabisa. Kwa mfano, mtu anapomtaka mfanya kazi wake amletee tembo kutoka pahali kadha. Lakini anapokwenda hapo pahali alipoambiwa, yeye hamwoni huyo tembo. Hata hivyo, yeye humleta kutoka pahali ambako ataweza kupatikana.

Hizi ni namna 8 za uhakikisho au ushahidi. Ikiwa historia inaweza kutiwa katika amri, na mazungumzo, uwezekano na hisia zisizokuwapo, uhakikisho wa namna nne tu ndizo zilizobaki. Mtu anaweza kuhakikisha ukweli au menginе kwa majaribio haya matano: viz, sharia za kiroho, sharia za tabia, busara ya watu wenye hekima, sauti ya dhamiri, namna nane za ushahidi; lakini si katika njia nyingine zo zote.

**Uokozi kwa Maarifa - Tabaka sita za kuishi**

Mtu huweza kuokoka au kuwa katika hali ya heri, ambapo, yeye anapojinadhifisha kwa uadilifu kamili, na anapofuata filsafia za ujuzi za tabaka sita za kuwapo, Sadharmya, kujulikana i.e. kuwa mmoja wa vitu vya dunia kama udongo na maji, Vaidharmya: tofauti, kama ugumu wa udongo na ulainifu wa maji, kama, I. dravya: kitu, 2. guna, sifa, 3. karma: kitendo au ujuzi, 4. samanya: mkataba, 5. vishesha; tofauti; na 6. samavaya mapatano ya lazima au uhusiano wa juu juu.

**Vitu tisa.**

Udongo, maji, moto, hewa, anga, wakati, mahali, roho, na nia au akili ni vitu tisa vinavyoitwa dravyas katika Sanskrit.

Kitu ni kile chenye nguvu, mali, au hata ikiwa kina mali tupu. Katika hivo vitu, udongo, maji, moto, hewa, nia na roho ni vitu sita ambavyo vina vyote viwili, sifa na kitendo. Moja kati ya wakati na mahali ni vitu vitatu ambavyo vina mali, lakini havina vitendo au nguvu.

Kitu au asili ya kitu (dravya) ni kitendo kilichopo kabla ya mahitaji yake halisi, yanayotokana kwa kukikutanisha au kukigawa katika hâli yake halisi. Kwa sifa ile kitu hicho kinajulikana, kinaitwa busara: kama mwangaza au umbo hutambuliwa kwa kutumia macho.

**Maelezo Yao.**

1. 'Prithvi'

Ardhi ina sifa za umbo au za mwili, ladha, harufu na ya kuwa ya kugusika. Ina sifa hizi kwa mfungamano wake wa moto, maji na hewa.

Harufu ni kitu muhimu cha ardhi; pia ladha ile ya maji; umbo au mwangaza ni ule wa moto; mguso ni ule wa hewa; na sauti ni ile ya anga.

**2. 'Apa'**

Maji yana sifa za umbo, mguso, umaji maji na ulainifu. Lakini katika hizi, ladha ni sifa muhimu. Umbo na mguso yanatokana na muungano wa moto na hewa.

Ubaridi pia ni sifa muhimu ya maji.

**3. 'Teja'**

Mwangaza au rangi na mguso ni sifa muhimu za moto. Lakini umbo (rangi) si sifa yake ya kwaida na mguso unatakika kwa mwungano na hewa.

**4. 'Vayu'**

Hewa ni sifa ya mguso. Lakini hunywa joto na baridi kwa mwungano wake na moto na maji.

**5. 'Akasha'**

Anga haina umbo, ladha, harufu, na mguso; lakini sauti peke yake tu ndiyo sifa iliyonayo.

Sifa ya anga ni kuruhusu kuingia na kutoka.

Sauti peke yake ni sifa ya anga, kwa sababu haipatikani katika udongo na vitu vyengine au mazao yao.

**6. 'Kala'**

Wakati ni ule ambawo ardhi hali ya kujulisha fikra hivi sasa, kupitia, kwa umoja, upesi, pole pole na sifa kama hizi ni sawa na ulinganifu.

Wakati hauonekani katika jambo, lakini huonekana tu katika shani. Fikra ya wakati huja kwa kuyachukulia yaliyotokea.

**7. 'Disha'**

Pahali ni pale penye mashariki, kusini, magharibi na kaskazini, juu na chini ili kuonyesha pahali kadha, inawezwa kusemwa.

Mashariki ni upande ule jua linachomoza au litachomoza, na upande ule litakapotua unaitwa magharibi. Kusini ni upande wa kulia wa mtu anayeelekea mashariki, na kaskazini ni upande wake wa kushoto.

Upande baina ya Mashariki na kusini unaitwa agneyi: E.S. Upande baina ya kusini na Magh. nairiti: kus. Magh. na ile kati ya Magh. na Kask. Vayavi: Magh. Kask. na ile kati ya Kask. na Mash, aishani: Kask. Mash.

**Sifa za Roho**

**8. 'Atma'**

Ni zile zinazodhihirisha sifa za kutaka kuchukia, nguvu, raha, mε wazo inaitwa roho. Falsafa ya Vaisheshik inayo haya yafuatayo kuengez yaliyokwisha tajwa hapo juu.

Kuvuta puumzi, kutoa puumzi, kufunga macho, na kuyafumbua, k uhai, kufikiri au fikra, kwenda bila ya kulazimishwa kuzitumia hisia kat na kuviona vitu hivyo, njaa, kiu, homa, magonjwa na mabadiliko kam yaliyopo juu, kwa majina ni, raha, maumivu, kutaka, kuchukia, na ngu haya ni nguvu na sifa za roho.

**9. 'Manas'**

Ni ile ambayo haiwezi kufanya mambo mawili wakati mmoja, huitw nia, kuwa dhahir au kutaka. Zaidi kwa tabia na sifa za vitu. Na sasa ku zao.

**Sifa. (24)**

**II 'Guna'**

Mwangaza (umbo), ladha, harufu, mguso, sauti, idadi, mgawanyiko, kuambatana, mkawanyiko, umbali, ukaribu, ufahamu, maumivu, kutaka, kuchukia, machofu, uzito, umaji maji, mnyato, mfungamano, na tofauti ni sifa 24 za vitu.

Sifa ni ile inayotegemea kuwepo kwake juu ya kitu na haichuk nyingine. Na katu haiwi sababu ya muungano au mtengamano.

**Maelezo Yao. Mahabhashya.**

Shabda:- Sauti ni ile inayoweza kusikika shikioni, kufuatwa na ufal kudhihirisha kwa kutamka, na nyumba yake ni kitu ambacho ni ang Rangi au umbo ni kile kinachoonekana na jicho. Rasa: Ladha ni ile ina ulimi, kama utamu, etc. Gandha: Harufu ni ile inayoweza kusikika Sparsha: Mguso unaoweza kupatikana kwa ngozi. Sankhya: Idadi ni zile moja, mbili na nyinginezo kama hizo. Parimana: Kipimo ni kile kinachc uzito kuwa mwepesi au mzito. Prithaktwa: Mtengano ni kuwa mba Sanyoga: Muungamano ni kuwa pamoja. Vibhaga: Mgawanyiko ni kuv kilichoungana katika sehemu nyingi. Paratwa: Umbali ni masafa kutok Aparatwa: Ukaribu ni kupakana kutokana na pahali. Buddhi: Akili ni kujua la kweli na la uwongo. Sukha: Furaha ni raha. Dukha: Maumivu Ichha: Kutaka ni kuungana. Dwesha: Kuchukia ni kutopenda. F Kujichokesha ni kutumia nguvu na uwezo kwa njia nyingi. Gurutwa: uzani. Dravatwa: Maji maji ni sifa ya kuweza kuyeyushwa. Sneha: Ulain wa mafuta na mapenzi. Sanskara: Mvuto hupatikana linapotokea jambc

mdhahirisho wa kitu chengine. Dharma: Kushikamana ni tabia au mfungamano na sifa kama hizo. Adharma: Msemo usio na maana ni tabia isio ya halali, ulainifu na sifa nyinginezo, kinyume cha mfungamano na nyinginezo. Hizi ndizo sifa 24.

**III "Karma"**

Mpao, mshuko, kunywea, kupanuka, mwendo na mengine kama haya ya kugeuka kuitwa vitendo. Sasa ni maelezo ya namna ya vitendo.

Kitendo ni kile kinachotegemea kitu, hakina sifa zake na sababu huru katika mwungano na mgawanyiko.

**IV. "Samanyam"**

Kitu cha kawaida ni kile ambacho ni sababu ya mazao, sifa katika uadilifu, vitendo. Mazao ya vitu ni ya kawaida au kama sawa na mazao katika audilifu na kuwa ndiyo sababu.

**V. "Vishesha"**

Shabaha katika vitendo, harakati katika vitendo, tabia katika tabia za asili, ni mawafikiano na tofauti au mamoja na udhahiri. Kwa, harakati katika vitendo ni dhahiri kutokana na sifa au tabia na vitendo. Yayo hayo yanaweza kusemwa ya yote katika kila pahali.

Mapatano na tafauti zina hakikishwa kwa kumhoji mtaalamu; kama, kwa mfano, utu katika kila binadamu ni jambo la mapatano lakini ni jambo tafauti ukilinganisha na wanyama na viumbe vyengine. Sifa ya Brahmin au ucha Mungu, sifa ya Kshatriya au ushujaa, sifa ya Vaishya au uwafikiano wa biashara, sifa ya Shudra au utumwa pia ni sifa za ubaguzi miongoni mwa binadamu, ziada ya uke na udume katika jinsia yao. Ucha Mungu au sifa ya Brahman ni tabia ambayo inakubaliwa na Brahman wote; lakini inatafautisha Kshatriyas au wapiganaji vitu katika wao. Sharia hiii hufaa kila pahali, kama, sifa za lazima za aina moja ambayo haipatikani katika nyingine.

**VI. "Samavaya."**

Uhusiano wa kila mara baina ya sehemu na kitu kilicho kizima; ni kitendo; kitendo na mtendaji; sifa na kitu, tabaka na watu, sababu na athari, inaitwa ni asili. Uhusiano kati ya vitu viwili unaitwa muungano, i.e. tukio au uhusiano wa muda.

Ya jinsi moja na mgeuzo wa jamii moja kutokana na sababu inaitwa jinsi moja - Sadharmya. Kwa hivyo, dunia ina vitu ambavyo vinagawanyika pia na mazao yao, kama magudulia na vyombo vyenginevyo vya udongo. Katika njia hii hii, kitu kinafanana ambacho kinapatikana katika maji na mazao yake, kama barafu na vitu kama hiyo: kuwa ardhi na maji yanafanana, katika kumiliki vitu namna moja.

Inaonyesha kwamba tabia ya kinyume ya sifa na ya kitu huitwa ya namna mbali mbali - Vaidharmya. Kwa hivyo sifa za ugumu, ukavu, na za harufu za udongo ni kinyume cha miliki ya umaji maji, ulainifu, na umaji maji wa maji.

Athari hutokea panapo kuwa na sababu.

Kutokuwapo kwa athari haihakikishi kuwa hapajakuwapo na sababu.

Ukubwa ni wa namna mbili. Ndogo, kubwa, kama kipande kidogo (cha chembe tatu ndogo) ni kidogo zaidi kuliko chembe au punje moja, na ni kubwa kuliko chembe mbili, na milima ni midogo zaidi kuliko ardhi na ni kubwa zaidi kuliko miti.

Neno sat: linatumika kwenye vitu, sifa, na vitendo; i.e. neno sat linaonyesha wakati wa sasa hivi (neno la kuunga mafungu) na kuunganishwa na yote.

Kuwepo hupatikana katika vitu vyote, inaitwa mwafikiano mkubwa unaokuwapo Mahasamanya. Hii na sheria ya kuwapo kwa vitu.

**Namna 5 za Kutokuwapo.**

1. Kutokuwapo kuna namna zake tano. Kuwapo kwa kitu, sifa au kitendo kabla ya sababu inaitwa Prag-abhava; kama sufuria, kipande cha kitambaa, au kitu cho chote chengine hakiwezi kuwapo kabla ya kuzaliwa au kutengenezwa.

2. Kutokuwapo kwa kitu kuwepo kwa kitu huitwa Pradhwans-abhava kama sufuria inapotengenezwa na kuangamizwa.

3. Kuwepo ni kitu kimoja na kutokuwapo ni kitu kingine na inaitwa Anyonya abhava ya kutoana; kama, farasi si ng'ombe, na ng'ombe si farasi, kwa hivyo, hakuna uhusiano wa farasi katika ng'ombe na ng'ombe katika farasi Kuwepo kwa ng'ombe kinaopatikana katika ng'ombe tu, na hivyo hivyo kuwa farasi, katika farasi tu.

4. Ni ile iliyotofauti kutokana na namna tatu zilizopo hapo juu, inaitwa Atyantabhava kutokuwapo kabisa; kama pembe za mtu, mau ya mbinguni, mtoto wa kiume wa mwanamke aliyetasa na mengineyo.

5. Sufuria haliko katika nyumba, i.e kuwa lipo pahali pengine. Sufuria halina uhusiano wo wote na nyumba. Hizi ni namna 5 za kutokuwepo.

Ila za hisia, na tabia (sanskar) huzaa ujinga.

Maarifa ya uwongo au habari za uwongo ni ujinga au ni uwongo.

Bila ila au habari za kweli inaitwa elimu au maarifa au ukweli.

Kuwepo kwa ajabu kwa dunia na vitu vyenginevyo ni si ya kweli na mali zao viz. rangi, ladha, harufu, mguso piya si ya kweli kutokana na vitendo vya ajabu vya kutokuwapo.

Lakini sifa za harufu na mengineyo, vilivyopo katika dunia na vitu vyengine ni vya kweli.

Na yale yaliyokuwapo na hayana sababu ni ya daima au ni ya kweli. Sifa za sababu zinazoonekana katika dhahiri si ya kweli.

Namna nne za maarifa hupatikana inaposemwa kuwa hii ni athari ya ile, i.e. kutokana na uhusiano wa kitu na sifa zake, viz. Samavayi elimu au maarifa ya asili au uhusiano wa karibu sana, kama anga ni ya kupimika; Sanyogi maarifa

muhimu ya kufuatana na mwili, na ngozi; Uhusiano kama huu na mwingine ni wa daima. Ekarthasamavayi: maarifa ya vitu viwili kama mguso unahusiana na kitu cha kugusa na msisimko wa mguso; Virodhi maarifa ya kinyume, kama mvua ambayo imeshakunya, ni kinyume cha mvua ambayo itakunya.

Tabia ya kitu hugeuka kufuatana na mhakikisho na namna ya kuhakikisha, au hata moja katika hizo, viz mambo yaliyothibitishwa kwa sababu maalum yanaitwa vyapti. Kwa hivyo, kuna mwandamano usiobadilika baina ya moshi na moto.

Moshi ni kitu, ulioenea kwenye moto, na kutengenezwa na nguvu zake wenyewe, huenda mbali ambako hubaki bila ya mwungano na moto. Jambo hili linaitwa vyapti. Kwa maneno mengine, moshi hutokana na ujoto wa moto onaotokana na maji na vitu vyengine.

Uhusiano baina ya mweneo wa nguvu wa kitu katika ulimwengu, inaitwa Mahattatwa, na nguvu za kuweza kuenea za wataalamu na wengineo, inaitwa vyapti au mwandamano usiobadilika kama uhusiano baina ya nguvu na mwenye kuwa nazo au kuwemo katika kilicho kuweka.

Kwa njia hii masomo na mafunzo lazima yafunzwe na kusahihishwa na kuhahikisha kwa mujibu wa falsafi. Kama si hivyo wanafunzi hawataweza kupata elimu thabiti: vitabu vyo vyote vinavyosomeshwa, lazima visahihishwe kwa mujibu wa kanuni zilizotolewa hapo juu na vitabu vile vitavyofuzu tu ndiyo visomeshwe. Lakini vile vile ambavyo havikufuzu basi visisomwe wala kusomeshwa. Kwa, maelezo ya vitu (kama Gandhavati Prithvi, cho chote chenye udongo kina harufu) na mhakikisho (kama ufahamu na mengineyo) huonyesha ukweli na uwongo na huonyesha mdhihirisho wa vitu.

Bila ya ukweli huu hapana kitu kinachoweza kuhakikishwa.

**Namna ya Kusoma na Kusomesha - Taratibu za Masomo.**

Sasa tunaeleza njia za masomo na kusomesha na kutoa taratibu za masomo.

1. **Shiksha.** Orthoeny Irabu zilizoandikwa na Panini, ambacho kina misemo ya kitaalamu. Lazima kisomeshwe hivyo. Wanafunzi lazima wasomeshwe viungo, nguvu na namna ya kutamka herufi; kama kiungo cha kutamka neno pa ni midomo, nguvu au namna ya kuitaja ni kuufungua mdomo, puumzi na kuuendesha ulimi huwezesha kulitamka. Katika namna hii, baba, mama, na mwalimu lazima wawafundishe matamshi ya herufi zote kwa mujibu wa irabu.

2. **Vyakaran:** Sarufu na nahaw: Ashtadhyayi au hotuba nane za Panini lazima zisomwe kama: (i) misemo ya wataalamu, kama Vriddhiradaich; (ii) mgawanyiko wa maneno yake kama, vriddhi - at, aich, katika mifano iliyopo hapo juu (iii) mahali pao ni kama, ach cha aich cha - adaich, na maana yake, kama ai na ow zinaitwa vriddhi; herufi zilizochanganyika: Herufi kabla ya ta na herufi baada ya ta zinaitwa tapara, i.e. a kabla ya ta na aich baada ya ta zote ni tapara. Kitu chenye sheria ya hii tapara ni herufi zile za urefu na haziitwi vriddhi.

Mifano - I. Bhaaga linatokana na neno bhaj, ambalo ghanj linatiwa mwishoni ambayo gh na ny yanafupishwa. Baada ya mfupisho inakuwa kama bhaj a. Hapa a ya bha kabla ya j inarefushwa na kuwa a (refu). Tena hapo huwa bhaaj. Hapa hugeuka kuwa g, ambayo baadaye a huwa ga, na kuilifanya neno bhaaga. Hivi ndivyo inavyofanyika. 2. Adhyaaya linatokana na neno eng pamoja na adhy a mwanzoni. E fupi inaondolewa na kuwekwa ai, vriddhi yake, kabla ya mwisho wa ghany. Ai inageuzwa kuwa aay, ambayo pamoja na a ya ghanj huwa adhyaaya. 3. Naayaka linatokana na neno neenj. Kwa urefu wake wa e inawekwa mahali pa ai, vriddhi yake ni, kabla ya kuongeza nvul (mfupisho) na ai kubadilishwa kuwa aay, na kuunganisha na a inayofuatwa huwa naayaka 4. Staavaka hutokana na neno stu pamoja na kuengezwa nvul. Ufupisho wake u inafanywa kuwa refu na kuwa ow, ambayo hugeuka na kuwa aav, na baadaye a huwa staavaka 5. Kaaraka inafanyika kutokana na neno krinj pamoja na nvul kuja mwishoni, ambamo herufwi na 1 zinafupishwa. Baada ya mfupisho vu inawekwa badala aka, na aar inaondoshwa na ri kuwekwa, kuwa ni vriddhi au sauti ya urefu. Hapo tena huwa kaaraka.

Mwalimu lazima afahamishe sheria au mithali zinazotumika katika mifano hii. Namna ya kufanyiza ionyeshwe kwenye ubao. Namna isiyotengenezwa lazima iandikwe na kisha mgeuzo wake uonyeshwe kwa pole pole; kama bhaj, ghanj - su. Baada ya kuondoa gh na nj moja baada ya mwenzake, lazima iandikwe bhaj-a-su kama ilivyobaki baada ya mfupisho. Hapo tena a hufanywa kuwa refu na j hugeuzwa kuwa g, na huwa kama bhaag-a-su. Inapoungana na a, huwa bhaaga-su. Hapa u inafupishwa na s hugeuka kuwa ru, ambayo u tena inafupishwa. Baada ya mfupisho neno huwa bhaagar. Sasa: visarga (h) inapoondeshwa na kutiwa r, huwa bhaagah. Hivyo bhaagah hutengenezwa kutokana na bhaj. Sheria au mithali ambazo zinatumika na mgeuzo athari, lazima isomwe vizuri na kusomeshwa na kuandikwa ili kumwezesha mwanafunzi afahamu njia ya kutengeneza. Kusoma na kusomesha katika njia hii huleta mafanikio makubwa katika elimu. Baada ya kusomesha Ashtadhyayi katika njia hii, mwalimu asomeshe yafuatayo.

**3. Dhatupath:**

Vitendo pamoja na maana zao na namna vinavyobadilika vitendo hivyo vya Lakaras kumi au jinsi na namna ya vitendo hivyo vilivyotendeka kwa wakati mbali mbali. Tena utsarga sutra: sheria za kawaida lazima zisomeshwe kwa mpango pamoja na maelezo yao. Kama, Karmanyan: hapo neno karma linapotumika kama upapad kabla ya neno lenyewe, au lazima liunganishwe nalo; kama, kumbhaakaarah. Tena apvad Sutra: sheria maalum au mithali inayohusiana katika njia za pekee lazima zisomeshwe; kama. Ato nupasarge kah - 'aka' iengezwe mwishoni pa neno linalomalizia katika 'a' inapofuatwa na 'karm' kwa kuleta maana halisi bila ya kuwepo mwuhusiano; kama 'vayu' 'vyapak'. Ikiwa 'karma': Ikiwa kitu kinaonyeshwa; maneno yote huchukua 'an'. Sheria nyingine ndogo ndogo zimetiwa katika sheria zinazohusika na asili ya maneno yanayokwishia kwa 'a' na kwishia kwa 'ka'. Sheria muhimu au mithali maalum ambazo zinazofuata mambo yanayo husika na sheria za kawaida. Kwa mfano

watawa wa wafalme na machifu wa miji mikubwa inaweza kutiwa katika utawala wa mfalme wa dunia nzima, lakini ya mwisho haiwezi kutiwa katika ya mwanzo. Kwa hivyo Panini ameiweka elimu yote ya maneno na uhusiano wake wa nahaw katika ubeti 1,000. Baada ya kufundisha sarufi, mwalimu lazima asomeshe vilivyo mgeuko wote kwa kuyapitia vilivyo sehemu ya sarufi au ya nahaw unadi kwa kutoa sheria ya maneno yanayofuatwa kwa un. Tena Ashtadhyayi lazima isomeshwe mara ya pili, na kufahamisha mapingano yote ya sheria, vartik zao, maelezo, karika zao: marefusho, paribhasha; echnology, na mifano yake.

4. **Mahabhashya,** tena hapo lazima isomeshwe. Ikiwa ni hodari, wenye bidii wapenda kweli wa elimu ya kila siku au kusomesha sarufi, wao watamaliza Ashtadhyayi na Mahabhashya kila moja katika miaka 1½, i.e wamalize masomo ya sarufi katika muda wa miaka mitatu, na kuwa wataalamu thabiti wa nahaw. Wao wataweza kufahamu Vedic na Sanskrit mashuhuri na nahaw yake kwa msaada wa ujuzi wao katika nahaw, tena hapo wasome na kusomesha vitabu vyengine vya Sanskrit kwa upesi na urahisi. Masomo ya vitabu vyengine havihitaji kazi nyingi kama nahaw inavyohitaji. Faida nyingi ya elimu hupatikana kwa kuvisoma vitabu hivi. Ashtadhyayi na Mahabhashya, katika miaka mitatu, ambayo huwezi kupasa kwa kusoma vitabu visivyokuwa vya maana hata katika miaka 50, kama Saraswat, Chandrika, Manorama na vyenginevyo.Vipi vitabu vya u vongo vya watu wasio na akili timamu wenye elimu haba visaweza kuwa na elimu an ujuzi ambawo wataalamu hasa, wanajimu na wanavyuoni wameweza kuvionyesha dhahiri katika kazi zao? Mipango ya wataalamu wanayoweza kuitumia kukieleza kitu kwa uhodari, na katika muda mfupi kama iwezekanavyo. Madhumuni ya watu wasiokuwa na elimu ya kutosha na fikra haba ni kuandika lugha ngumu kama iwezekanavyo ili kumfanya msomaji apate taabu zaidi na faida kidogo. Ni kama kuuchimba mlima kupata kaure. Lakini kusoma maandishi ya mtaalamu ni kama kuvua chopi za lulu anapozamia mara moja tu baada ya kusoma nahaw yake.

5. **Yaska's Nighantu na Nivukta** lazima isomeshwe katika miezi sita au minane pamoja na maana zake. Watu wasipoteze miaka yao mingi kwa kusoma Amar Kosh na vitabu kama hivyo vilivyoandikwa na watu wasio amini Mungu.

6. **Pingala,** kitabu kidogo cha mashairi cha Prof. Pingala, hapo tena kipitiwe kwa sababu kinatoa elimu ya Vedic na Sanskrit maarufu pia namna mpya za ulinganifu wa sauti za maneno na mashairi katika mpango mzuri kabisa. Kitabu hiki na mifano ya mashairi ya kisasa pamoja na ulinganifu wa maneno kinaweza kusomwa katika miezi 4. Miaka mingi isipotezwe bure kwa kusoma Vritta Ratnakar na vitabu vyenginevyo vya ulinganifu wa maneno ambavyo vimeandikwa na watu wenye elimu haba.

7. **Muhtasari wa Manu, ya Ramayana wa Valmika, Niti ya Vidur.** Akhlak katika Udyoga Parva wa Mahabharata na vipande vyengine vya Maandishi Matakatifu, inayotakasa akili ya matumainio ya mambo mabaya na kuleta uzuri na ustaarabu, hapo tena yafanywe. Haya yasomwe baada masomo ya mashairi,

mtengamano wa maneno, kutoa maana ya maneno lugha ya nathari, uhusiano wa sifa na elimu ya sarufi na sababu zao kwa ufupi zielezwe na mwalimu na yasomwe kwa makini na wanafunzi. Somo hili linaweza kusomwa muda usiotimia mwaka mmoja.

8. **Purva Mimansa, Vaisheshik, Nyaya, Yoga, Sankhya, na Vedanta** tena hapo yasomwe. Skuli hizi sita za falsafa lazima zisomwe kama iwezekanavyo kwa msaada wa maelezo ya wataalamu na watu wenye hekima na wana wa falsafa au na maelezo mapesi ya wataalamu mashuhuri. Lakini kabla ya kusoma misemo ya akili ya Vedanta, Upanishats kumi kama:-

9. **Isha, Kena, Katha, Prashna, Mundaka, Mandukya, Aitareya, Taittiriya, Chhandogya, na Brihadaranyaka,** yapitiwe, na tena hapo masomo sita ya Kifalsafa yamalizwe katika miaka miwili.

10. **Rig, Yajur, Sama, na Atharva,** Ma Veda wane tena hapo yasomwe pamoja na maelezo yao, maana ya maneno, uhusiano wa sarufi, na ya kupungia mkono, pia Ma Brahmana 4.

11. **Aitareya, Shatapatha, Sama, na Gopatha** katika muda wa miaka sita.

**Kusoma Veda pamoja na Maana zake.**

Ubeti huu kutoka Nirukta ni mamlaka ya hii:-

**(Nirukta 1.18)**

Yeye ambaye husoma Vedas kwa mahadhi tu na hajui maana zake, yeye ni kama mtu ambayo umebeba matawi, yasiyo na majani, na matunda, au ni kama mnyama ambaye hunyanyua nafaka na vitu vyenginevyo. Lakini yule asomaye Vedas na kujua maana zake sawa sawa, hupata raha kamilifu katika maisha, na kwa kuyawacha madhambi kwa kupata elimu na kuwa na tabia za uadilifu na kufanikiwa na hali ya heri baada ya kufa.

**(Rig. 10.17.4)**

Wale walio wajinga, wanayo mashikio, lakini wao hawasikii. Wao wanayo macho, lakini wao hawaoni. Wao wana ndimi katika midomo, lakini wao hawasemi. Kwa maneno mafupi, mjinga hawezi kujua siri ya maneno haya ya elimu. Elimu huonyesha utukufu wake, lakini si kwa mjinga huyu, lakini kwa mtaalamu ambaye anajua maana yake na umuhimu wa maana wa msemo, kama mwanamke mzuri aliyepambwa kwa mapambo na nguo nzuri kumwonyesha kuwa hana mapenzi na mume wake.

**(Rig. 1.164.39)**

Utapata raha gani yeye kutokana na kusoma Rig na Vedas nyingine, yeye ambaye hamjui Mola Muweza, ambaye ameenea kote asiyeweza kufa na ni mzuri kabisa Mungu Juu, elimu yake ni mwisho wote wa Vedas, na katika yeye wataalamu wote wa dunia, jua na Sayari nyingine huenda na kuwa na viumbe

vyao? Hapana kitu ila, wao tu hupata uwokovu na milele, wao wenye itikadi katika Mungu, husoma Vedas, na kuwa, waadilifu wa mayogi, na kuweza kufahamu Uwezo wa Pekee wa Mungu. Hata hivyo yote yanayosomwa au someshwa lazima yafuatwe kwa maana na sababu zake.

Masomo ya Vedas yanapomalizika, Ayurveda, sayansi ya (maisha) utabibu, lazima ianzwe kusomwa, ambayo imetolewa katika:-

**12. "Charak, Shushrut"**, Maandiko mengi ya kitabu yenye hekima na ya wataalamu wa utabibu. Lazima imalizike katika muda wa miaka minne.

Tena hapo:-

**13. "Dhanurveda"** lazima isomwe, ambayo ni ya kuhusika na mambo ya serikali. Imegawanyika katika sehemu mbili; kwa majina, sehemu moja kuwahusu watawala na nyingine kuhusu watu. Maofisha wote katika jeshi la serikali lazima wafunzwe namna ya kutumia silaha za jamii zote, silaha na vitu vyakutupia mabomu, na kufanya mazoezi katika kila namna ya vikosi na kuunda majeshi, yanayoitwa gwaride, na kutumika katika viwanja vinavyotumika wakati wa kupigana na maadui. Hayo yote yanataka kujulikana kwa vilivyo. Sehemu ya sayansi ya serikali ambayo inakusudia ulinzi waraia na kupendelea mahitaji yao, lazima yasomwe ili uwezo wa kuwatawala raia kwa haki na usawa ili wao wawe na furaha na kutosheka. Wanafunzi pia lazima wajifunze sheria za wahalifu ili waweze kukomesha uhalifu na kuwalinda wale watu wanaoishi kwa usalama. Mafunzo haya ya sehemu mbili za sayansi ya serikali lazima imalizwe katika miaka miwili kila mmoja.

**14. "Gandharvaveda"** ambayo inaitwa Sayansi ya muziki, hapo tena isomwe. Sauti moja moja, kanuni, mgeuzo, saa, kipimo, mizani, wimbo, hewa, ala, ngoma, kuimba, na mambo kama haya lazima yasomwe sawa sawa. Lakini kuimba kwa Sam Veda na kucheza nyimbo kwenye ala za muziki hasa lazima zifundishe. Muziki ulioandikwa na St. Narada na mashairi yatakatifu lazima yafunzwe. Lakini katu wasididimie katika kelele za wenda wazimu, malaya, na wahuni, wa kidini, kupiga kelele kama punda ili kuwa na uchu.

**15. 'Arthaveda'** inaitwa ufundi wa viwanda lazima ifunzwe kwa vilivyo katika miaka miwili pamoja na vifaa vyake, elimu ya kujua sifa za vitu, unda kwa mikono, ufundi, kufanya namna mbali mbali za vitu na namna ya viwanda vinavyotumika juu ya ardhi na kwenye sehemu za hewani. Ni ufundi wakujipatia mali. Hapo tena huja elimu ya nyota kama ilivyotolewa katika:-

**16. "Suryasidhanta"** na vitabu vyengine kueleza nguvu ya peponi, ambazo zimo kama, algebra, hesabu, giografia, na elimu ya habari za mawe lazimwa zifunzwe kwa intidhamu.

**17.** Kazi za mikono, ufundi wa magari, ufundi wa mashine na ufundi mwingineo wa mashine lazima ufunzwe. Lakini vitabu vyote vya elimu ya nyota, vinavyoeleza uwezekano wa nyota, sayari, kupiga ramli, majumba, ishara za

nyota, falaki, wakati wa bahati njema na mengineyo kama haya, yasisomwe, maana yanaaminiwa kuwa ni ya uwongo mtupu na hayana ukweli.

Mwalimu na anayefunzwa lazima ajaribu kumaliza masomo yanavyotakikana na mafunzo halisi katika miaka 20 au 21. Baada ya kufanya ambayo yaliwapasa kufanya, watu wataishi kwa raha duniani. Mpango huu wa elimu utawa elimu ya kutosha katika miaka 20 au 21 ambao hauwezi kupatikana kwa mpango mwingine wo wote hata katika miaka mia.

Sababu ya kuwa kwanini visomwe vitabu vilivyo andikwa na wataalamu tu ni kuwa wao ndiyo walikuwa wanavyuoni wakubwa wenye ujuzi thabiti wa vitabu na walikuwa waadilifu wakati huo huo. Lakini vitabu vilivyoandikwa na watu wenye elimu ya juu juu tu na si ya kutosha na akili zao zilijaa ubaguzi na vyenye vivuli vya waandishi wao.

**Vitabu vya Wataalamu vilivyopendekezwa kusomwa.**

1. Jaimini's Purva Mimansa pamoja na Maelezo ya Vyasa.
2. Kanada's Vaisheshika pamoja na Maelezo ya Gotama.
3. Nyaya ya Gotama pamoja na Maelezo ya Vatasyayana.
4. Yoga ya Patanjali pamoja na Maelezo ya Vyasa.
5. Sankhya ya Kapila pamoja na Maelezo ya Bhaguri.
6. Vedanta ya Vyasa pamoja na Vatsyayna na maelezo yake au Boudhyana pamoja na mafafanusi yake.

Vitabu hivi vyenye misemo ya uadilifu vimehesabiwa miongoni mwa "kalpa" na mashuhuri katika masomo ya Vedas. Kama Rig.Yajur, Sama, na Atharva Ma Veda 4 waliofanywa na Mungu au Madhihirisho; pia ni Aitareya Shatapath, Sam na Gopath, Brahman 4; Shiksha, Kalpa, Vyakarana, Nighantu, Nirukta, Chhanda na Jyotish, Angas 6. vilivyo fuatana na masomo ya Vedas; Mimansa na Upanga 6 nyingine: Mkamilisho wa masomo ya Vedas: na Ayur, Dhanur, Gandharva, na Artha Vedas, "Upavedas": Namna ya pili ya Veda zote zimeandikwa na wataalamu na Mafalsafa. Katika hizi tena, ni vile vinavyo onekana kama vinavikana Vedas basi visikubaliwe kwa sababu Vedas, imefanywa na Mungu, ni vyenye uhakikisho na pasipo hitilafu ye yote na yenye kujitosheleza kwa maelezo yote, haya ni kusema, Vedas ni wenye hukumu zao wenyewe. Bhahmans na vitabu vyote vinginevyo vya namna hii vina hukumu ya kujitegemea ni kuwa ukweli wao unategemea juu ya ukweli wa Vedas.

Maelezo zaidi kuhusu Veda yanaweza kupatikana kutoka Maelezo yetu ya Rig na Vedas nyingine "Rigvedaadi Bhashya Bhumika". Sisi pia tutaendelea nacho mbele juu ya kitabu hiki.

**Vitabu vinavyokatazwa katika masomo.**

Vitabu ambayo lazima vikatazwe kusoma vimetajwa hapa kwa ufupi, vitabu

vifuatavyo hapo visisabiwe katika vile visivyo kuwa halisi:-

Katika nahaw au sarufi: Katantra, Saraswat, Chandrika, Mugdhabodh, Koumudi, Shekhar, Manorama, na vyenginevyo. Makamusi: Amar, Kosh, & C. Katika kanuni: Vrittaratnakara na vyenginevyo. Katika ukamilifu:· Atha Shiksha, & C. Jatika Elimu ya Nyota: Shighrabodha. Muhurta Chintamani na vyenginevyo. Katika Mashairi: Nayikabheda (uonyesho wa tabia za kike). Kuvalayanand, Raghuvansha, Magha, Kiratarjuniya na vyenginevyo. Katika Mimansa: Dharma Sindhu, Vriatarka & C. Katika Vaisheshik: Tark Sangrah na vyenginevyo. Katika Nyaya: Jagdishi na vyenginevyo. Katika Yoga: Hath Pradipika na vyenginevyo katika Sankhya: Sankhyatatwa Koumudi & C. Katika Vedant: Yogavasishtha, Panchdashi na vyenginevyo. Katika utabibu: Sarangdhar na vyenginevyo. Katika sheria. Codes zote isipokuwa maandishi maalum ya Manu. Tantras zote (vitabu) kuhusu elimu ya pepo. Puranas zote (elimu ya ulimwengu) Uppuranas, Tulsi Das' Ramayan, Rukmini Mangal na vyenginevyo, na Bhasha zote au Vitabu vya lugha lazima vikataliwe, kwa sababu ni vya kufikiria tu na vya uwongo.

Q. Ati kweli havina ukweli hata kidogo?

A. Vina ukweli kidogo, lakini vina uwongo zaidi. Kwa hivyo vikataliwe kama chakula kitamu kinavyokataliwa kabisa, kwa sababu kimechacha na kina sumu.

Q. Wewe hukubaliani na Puranas na vitabu vya historia?

A. Ah - kweli, sisi tunavikubali. Lakini sisi tunaamini ukweli tu na si uwongo.

Q. Vipi vitabu vya kweli na vya uwongo?

A. **Grihya Sutra.** Aitareya, Shatapath na Brahmanas wengine, ambawo sisi tumekwisha wataja kabla ya hapo, pia vinaitwa kwa majina 5 ya historia, purana (elimu ya ulimwengu) Kalpa (umashuhuri) gatha (kimila) na narashansi (maandiko ya habari za maisha ya mtu). Shrimad Bhagwat na vitabu vyenginevyo si Puranas.

Q. Kwa nini wewe hukubali ukweli uliyoko katika vitabu vya uwongo?

A. Cho chote kile cha ukweli kilichomo humo kinatokana na Vedas na vitabu vyenginevyo vya ukweli; lakini yote yale ya uwongo yalitokana na wao wenyewe. Kukubali Vedas na vitabu vyengine vya ukweli pia ni kuukubali ukweli wote. Ikiwa mtu yo yote anataka kuukubali ukweli wa vitabu hivi basi atanaswa na uwongo wao. Hata hivyo, ukweli wa kitabu kilicho changanyana na uwongo kitupwe kama kinavyotupwa chakula kilicho changanywa na sumu.

Q. Wewe unaamini nini?

A. Sisi tunaamini katika Vedas, cho chote kinachoamrishwa na kukatazwa kimetiwa kasisi na Vedas. Ilivyokuwa sisi tunaamini Veda basi dini yetu inaitwa Vedic. Kuamini huku lazima kukubaliwe na watu wote hasa Aryas ili wawe na dini moja miongoni mwao hapo wanapoishi duniani.

Q. Maandishi ya kweli pia yanatafautiana katika maoni yao kuhusu ukweli na uwongo baina ya moja na ya pili kama vitabu vya kuiga na uwongo, kwa mfano tabaka sita za falsafa zina maoni mbali mbali au tafauti kuhusu khulka Tukichukua mifano madhbuti. Asili ya khulka ni alama ya Mimansa kwa vitendo, katika Vaisheshik ni kuchagua vyema sana, katika Nyaya chembe ndogo ndogo, katika Yoga kwa nguvu, katika Sankhya kwa maumbile, na katika Vedant kwa Brahma au Mungu Mwenyezi. Je huu si mbainisho?

A. Kwanza, asili ya muumba haijaelezwa wazi katika tabaka nne za falsafa Sankhya na Vedant peke yao tu ndio vinatoa. Ya pili, ni kuwa hakuna mkanusho katika hivi; kwa sababu wewe huwezi kujua tafauti baina ya upatano na uhitilafiano. Mimi nina kuuliza uniambie upinzani uko wapi? Inaonekana katika somo moja la per se au katika masomo mbali mbali.

Q. Uhitilafiano wa watu wengi juu ya somo huitwa mkanusho. Katika tabaka hizi 6 za falsafa, kitu chenyewe ni kimoja,. tu asili ya muumba.

A. Elimu ni moja au mbili? (Jee, kuna umoja katika elimu?)

Q. Ni moja tu.

A. Ikiwa ni moja, basi vipi masomo ya sarufi au nahaw; utabibu, unajimu na vitatu vyenginevyo vina tafautiana? Kama katika sayansi, matawi mbali mbali ya sayansi nyingi yameelezewa kwa utafauti. Hata hivyo, hakuna mkanusho wo wote katika tabaka sita za falsafa. Kwa mfano, vitu vinavyotakikana kufinyangia vyungu ni kitendo, wakati, udongo, nakshi au akili ya kuchanganya na kugawanya ya vipande na habari nyinginezo, nguvu, vitu, na mfinyazi. Vivyo hivyo, jambo muhimu la·kusababisha chimbuko la dunia kwa vitendo au harakati linaelezwa katika Mimansa, na kwa wakati linaelezwa katika Vaisheshik, kwa kitu kinaelezwa katika Nyaya, kwa nguvu inaelezwa katika Yoga, kwa chembe ndogo kabisa inaelezwa katika Sankhya, ambaye inatowa sababu mwafaka, katika falsafa ya Vedant. Hivyo, havina mpinzano. japokuwa, kwa mfano, utambulizi, matibabu, dawa taratibu hasa ya chakula na kufunga au kutokula ni mambo tafauti yaliyotolewa katika vitabu vya utibabu, hata hivyo sababu zao kubwa ni kuuponyehsa ugonjwa. Basi ni kama hivyo, kuna sababu 6 za kukhulukiwa ulimwengu. Kila khulka imeelezwa na kila mwandishi wa tabaka sita au mgawanyiko wa falsafa. Kwa hivyo hakuna kile kilicho kinyume cha falsafa hizi. Sisi tutatoa maelezo zaidi katika kitabu hiki kwenye sura ya "juu ya maumbile".

**Nasiha**

Mwalimu na anayefunzwa lazima aepukane na mapingamizi katika kutafuta na kufundisha elimu. Hivi ni kama - kuwa na marafiki wabaya, kwa kutumia tembo na vinavyolewesha, umalaya na namna zote za kuzini, kuoa mapema, kama mwanamume kabla ya miaka 25, na mwanamke kabla ya kufika

miaka 16; kutokamilika katika kiapo cha utakatifu; kutaka mapenzi kwa ajili ya kueneza elimu ya Vedas na vitabu vyengine vya kweli katika kifua cha mfalme, mama, baba na mtaalamu, uroho; kukesha; au kufanya kazi bila ya kiasi; kudanganya; ujinga wa umuhimu mkuu wa elimu; kutoamini katika kuzidisha nguvu, akili, ushujaa, siha, jumia ya madola kwa kutekeleza kiapo cha utakatifu; kupoteza wakati bure kwa kuyatembelea majengo ya ibada na kuabudu masanamu yaliyochongwa ya mawe na vitu vyengine katika mahali pa ibada ya Mungu; bila ya kumtumikia au kumsaidia mama, baba, mgeni, mwalimu na wataalamu, ambawo: kama ilivyokuwa, taswira zenye uhai za Mungu; kukichora kipaji kwa msalaba wa maji ya sandali na alama nyinginezo kama nishani badala ya kumtumikia na kufanya maamrisho manne ya watu; kuvaa kamba zenye shanga, tasbihi; kufunga siku ya kumi na moja na kumi na tatu ya sehemu mbili za kila mwezi na fungo nyinginezo; kuhiji kwenye Kashi kwengineko; kuamini kuwa utaweza kusamehewa dhambi kwa kumtaja Rama, Krishna, Narayana, Shiva, Bhagwati, Ganesh na miungu mengine; bila ya kuwa na hamu ya kupata elimu kutokana na mafunzo ya wanafiki; kuamini kuhusu kujitolea kama kupatikana si kutokana na elimu, sifa au uadilifu, mngao, na kumwabudu Mungu. Lakini kwa kusikiliza hadithi na au hadithi ndogo ndogo za Bhagwat na vitabu vyenginevyo, vinavyoitwa kwa uwongo kama Puranas au elimu ya viumbe vya kale sana; bila ya kuwa na mapenzi ya elimu kwa kushughulikia kukusanya mali kutokana na tamaa, kutembea ovyo bila ya kujali kitu; na vitendo vyenginevyo vya uwongo na vibaya kujishughulisha bila kiasi hata kukawafanya watu kusahau kuwa watakatifu na elimu na kuwawezesha wao kupata maafa ya magonjwa na ujinga. Madhehebu ya kisasa na maaskofu wanaojipendelea wenyewe, Brahmanas na wengineo kama hawa, wanaowaondolea wenzao kutokana na kutaka kujipatia elimu na kuwa na marafiki wazuri, na kuwafanya wawafuate wao, huharibu siha zao, mali na raha. Wao wanafikiri ya kuwa, ikiwa mashujaa na watu wengine wakiwaelimisha kwa kupewa elimu, wao wataanza kutoka kwenye mitego ya wadanganyifu, na kuanza kujua ulaghai wao, wataanza kuwavunjia heshima na kuwadharau Mfalme na raia lazima wawaondoe na wajaribu kama wawezavyo kuwasomesha watoto wao wanaume na wanawake bila ya kujali taabu na pesa.

**Wanawake kusoma Vedas**

Q. Jee wanawake au watumwa (Shudras) wasome Vedas? Ikiwa wao wanasoma sisi tufanye nini? Hakuna amri inayo waidhinisha masomo yao. Hapa haparuhusiwi. Ni onyo la Veda kuwa mwanamke na mtumwa wasiachiwe kusoma.

A - Laani macho yako! Binaadamu wote, ikiwa wanaume au wanawake wanayo ruhusu ya kusoma. Ubeti huu umetengenezwa na wewe tu. Haya hayawezikani kuonekana katika maandishi ya kweli po pote. Kwa upande mwingine, ubeti wa pili wa sura ya ishirini na sita ya Yajur Veda ni ushahidi kamili unaounga mkono ya kuwa watu wote wasome na kusikiliza na kuelezea Veda na maandishi mengineyo matukufu, -

(Yaj. 26.2)

Mungu anasema: Mimi natangaza hotuba za Vedas 4, Rig na nyinginezo, kwa watu wote ili wao waweze kupata yaliyo mema kote katika dunia hii na ya baadaye. Hapa inaweza kujadiliwa kuwa neno 'jana' linaeleza kuzaliwa tena tu; kwa sababu, kanuni za sheria huwapa maaskofu, mashujaa na wafanya biashara ruhusa ya kuisoma Vedas, lakini kwa wanawake, watumwa na watu wa namna hivi.

A. Tazama, Mungu mwenyewe anasema: Sisi tumewashushia Vedas, kwa Brahmans, Kshatriyas, Vaishyas, Shudras na watumishi wetu, wanawake, na watu wa tabaka la chini, ni kusema, kwa watu wote, ambawo lazima wasome na wasomeshe Vedas, kuisikiliza na kuwasomea wengine, ili waweze kuizidisha elimu yao, ili waweze kuwa na akhlak nzuri, kuepukana na maovu, kuepukana na dhiki na kupata raha. Sasa, niambie ikiwa mimi nikufuate wewe au Bwana Mungu aliye juu yetu. Maamrisho ya Mungu lazima uyatii. Kwa hivyo, ikiwa mtu hakubaliyani na maarisho ya Vedas, anaitwa mtu asiyeamini Mungu. Kwani Mungu hapendi kuwafanyia wema wale watu walio watumishi? Kwani kweli Mungu hana haki hata akawazuwia wao wasipate elimu zao wasiwasikilize hawo watumwa wao na kuwa wachia wale waliozaliwa mara ya pili tu wapate? Ikiwa hiyo ndiyo ilikuwa nia ya Mungu kama watumwa na wengine wale walio kama hawo tu ndiyo lazima wasome na wasomeshe, basi kwa nini Yeye aliitia miili yao iwe na sauti, na pia kuwa na uwezo wa kusikia? Kama Mungu ameitengeneza dunia, maji, moto, hewa, jua, mwezi, vinavyoweza kulika na vitu vyenginevyo kwa ajili ya wote; basi Yeye pia ameishusha Vedas kwa ajili yao wote.

Popote panapokatazwa masomo yake, inaonyesha kuwa, yeye ambaye hasomi kitu, kwa kusoma na mwalimu anaitwa baradhuli mjinga kwa sababu ya kuwa hajui kitu na ni mjinga. Msomo wake au kusomeshwa kwake huwa haina maana. Ni mhakikisho wa ujinga, kujipendelea mwenyewe na ujinga ambao hukufanya kuwazuia wanawake wasisome. Tazama maamrisho ya Veda yanayotilia nguvu masomo ya watoto wa kike. Atharva Veda, K.II Pt. 24 Ad. 3, Verse 18 - Kama watoto wa kiume wanapata elimu ya kutosha, na tabia nzuri kwa kutii kiapo cha utakatifu na, wanapobalegh, huoa wanawali vijana, waliosoma, wazuri, wenye kustahiki, sawa na wao wenyewe; pia wacha watoto wanawake pia wajipatie elimu ya kutosha na tabia nzuri kwa kuisoma Vedas na maandishi mengineyo ya dini wakati wao wa kiapo cha utakatifu na kubaleghe na wengi wao huolewa na vijana wazuri, waliosoma na walio sawa nawo. Hata hivyo wanawake pia lazima watii amri ya kiapo cha utakatifu na kupata elimu.

Maana yake hi ni kuwa mke lazima asome ubeti huu wa Vedas wakati wakutoa muhanga. Ikiwa yeye hajaisoma Veda na masomo mengine matakatifu, vipi ataweza kusoma beti za Veda kwa mahadhi sawa sawa na matamshi yaliyo bora na kusoma Sanskrit wakati wa kuomba Mungu? Gargi na wanawake wengine, johari za wanawake wa kale wa India, wakawa wenye elimu kwa kusoma Vedas na masomo matakatifu. Haya yameandikwa wazi wazi katika Shatpath. Basi ikiwa bwana wa nyumba amesoma na ikiwa mke hajasoma au iwe mke amesoma na mume hajasoma, basi kila siku kutakuwa na ugomvi baina ya

miungu na mashetani katika nyumba. Vipi nyumba hiyo itakuwa na raha? Ikiwa wanawake hawasomi vipi wao wataweza kuwa waalimu katika shule za kike? Bila ya elimu, mwanamke hawezi kuendesha kazi za nyumba sawa sawa, kama kutengeneza nyumba, haki kwa wote, kazi zote zinazohusu maisha ya ndoa, kufahamiana kwa mke na mume, mapambo ya nyumba chini ya uongozi wa mwanamke wa nyumba, na kazi nyinginezo kama hizi.

Tazama, wake wa wafalme na Aryavarta watukufu wa (India ya zamani) walijua mambo ya kivita na mambo ya kishujaa kwa vizuri sana. Ikiwa walikuwa hawajua yote haya, vipi Malkia Kekayee na wengine walifuatana na Mfalme Dashrath na wenzao kwenye vita na kusaidia kupigana? Basi Brahman na wanawake walio shujaa lazima wajifunze namna zote za elimu, wale wenye asili ya wafanyi biashara lazima wajifunze ujuzi wa biashara na wale wenye asili ya kitumwa lazima wajifunze na kujua upishi na kazi za kutumikia. Wanaume lazima wajifunze japo nahaw kidogo, dini na kumwamini Mungu, wanawake pia lazima wajifunze nahaw, dini, utabibu, hesabu, kazi za mikono ili kuweza kujisaidia. Kwa sababu bila ya ujuzi huu wote wao hataweza kufafanua ya kweli na ya uwongo, na kujiweka katika hali nzuri pamoja na waume zao na majamaa wengine, kuzaa watoto vizuri, chakula kizuri, na kuwalea vizuri na kuwafunza, fanya au ona kama kazi za nyumba zinafanyika kama zinavyotakikana, pika au simamia upishi wa chakula, na tengeneza kinywaji cha dawa kwa njia inayotakikana na matabibu wenyewe ili ugonjwa usije ukawadhuru watu wako, na wote wanaoishi hapo waishi kwa furaha. Bila ya ujuzi wa kazi za mikono, wao hawataweza kuusimamia ujenzi wa nyumba, kutengeneza au kusimamia ushonaji wa nguo, mapambo, na mambo mengineyo; bila ya ujuzi wa hesabu, wao wataweza kuweka au kutoa hesabu za matumizi yote; na bila ya kuwa na ujuzi wa Veda na maandishi mengine matakatifu, ambayo yanawafanya kujua kwa ukweli wa Mungu na dini, wao hawataweza kujikinga na kutokuwa na dini au urafiki. Hata hivyo, wamebarikiwa ni wale ambawo wamewafunza watoto wao kwa sheria za utakatifu kupata tabia njema na elimu, na kukuuza uwezo wao wa kimwili na akili kuwa timamu, ili watoto hawo wanapobaleghe wao wanajiweka vizuri na kuwa na heshima sawa sawa tukufu na wanawaenzi mama, baba, mume, mkwe wa kike na kiume, wenziwao, majirani, wanaowapenda, marafiki, watoto, majamaa, na watu wengine wote. Elimu ni mali isiyoweza kwisha. Kadiri ikitumiwa zaidi basi nayo inazidi kuwa nyingi. Mali nyinginezo zote hupungua kila zikitumika. Warithi huchukua sehemu zao. Lakini hakuna mrithi au mwizi wa mwenye mali ya elimu. Mfalme na raia pia ni walinzi maalum na ni waendelezaji mbele wa mali hii isiyo julikana.

**(Manu VII, 152.)** Mfalme lazima aamrishe umuhimu wa kiapo cha utakatifu miongoni mwa watoto wa kike na kiume wa utawala kwa muda maalum, na kuwafanya wapate ujuzi ili wastaaribike. Ikiwa haitafuatwa na kijana yo yote, basi mama yake na baba yake lazima watiwe adabu. Kwa maneno yaliyo rahisi ni kuwa, iwe sheria ya mtawala kuwa hapana mtu atakaye ruhusiwa kumweka mtoto wake nyumbani baada ya kufikisha miaka minane. Wao lazima waishi katika skuli inayoitwa Acharyakul. Harusi zao zisifanyike mpaka wao

wanaporudi kwenye chuo kikuu baada ya kumaliza masomo yao.

**(Manu IV, 233.).** Kuliko zawadi zote duniani, kama vile chakula, kinywaji, ng'ombe, ardhi, nguo, ufuta, dhahabu, na siagi safi, lakini elimu ya Vedic ni bora kabisa. Kwa hivyo watu wajaribu kadi wanavyoweza kwa nguvu zao zote, na fikra zao zote kuiendeleza elimu mbele. Nchi ili imebarikiwa na kuendelea ambamo utakatifu wa wanafunzi, maendeleo ya elimu, na mwangaza wa dini ya Vedic imeendelezwa. Kwa ufupi kwa masomo na maendeleo ya wanafunzi. Katika sura ya 4 kurudi kwa wanafunzi kutoka skuli na maisha ya nyumbani yataelezwa.

**Muhtasari**

Masomo ya skuli yana sehemu nne: 1. Ya kidini, 2. Tabia, 3. Elimu, 4. Ya kujenga mwili.

Watoto wa kiume na kike baada ya kumaliza mwaka wa nane wapelekwe kwenye skuli zao, zilizojengwa maili nne na zinazosomeshwa na waalimu wenye adabu na muruwa nzuri. 1. Wao lazima wafundishwe sala zenye maana na kufanya muhanga wa moto. Kuoga kila siku na kuvuta puumzi refu kufuatia maombi. Wao lazima wajiweke kwenye kiapo cha utakatifu, ambacho kina sehemu tatu: ya mwanzo inakwishia kwenye miaka 24, ya pili mpaka miaka 44 na ya tatu mpaka miaka 48. Watoto wa kike wajiweke kwenye kiapo mpaka miaka 16 au 24.

2. Umuhimu mkuu wa ukweli, uaminifu, kuishi maisha ya wastani, kujinyima, na kujitosheleza lazima kuwepo katika akili. Wao lazima wafahamu kuwa mtu huwa hana thamani anaponyenyekea Mungu na ilhali yeye hana akhlak nzuri (Manu, 4. 204). Adabu na tabia nzuri katu zisisahauliwe. Wale wasiojifunza Veda wanajishusha na kuwa watu wa chini.

Wao wajiepushe na chakula cha nyama, vinywaji vikali, kutumia mataji ya maua, mafuta mazuri, vinywaji vinavyolewesha, achari, bizari, mafuta ya dawa, kutia wanja machoni, kuchukua mwavuli, ukatili kwa wanyama, matamainio ya kimwili, kutongoza, kuimba, kucheza ngoma, kucheza kamari, kusengenya, na kujisuhubisha na wanawake.

Wao lazima walale peke yao, manii yao uwanawali wao utunzwe, uasherati ambawo utawavunja kiapo cha utakatifu.

Wao katu wasidharau kusema kweli na wawe waokovu, wasome Veda, wamheshimu mwalimu, baba, mama, na wageni. Wao lazima wawe watakatifu kwa njia yo yote, na wawe waadilifu na wasifuate vitendo viovu vya wakubwa zao. Wakiwa hawana hakika katika jambo lo lote, wafuate mifano ya wataalamu na waadilifu, nia ni njia iliyo sawa kuliko zote.

3. Katika masomo ya elimu, masomo yao lazima yatosheleze mambo haya matano; sheria za kiroho, sheria za asili, busara ya hekima, tabaka nane za elimu ya kuwaza kwa akili halisi, na sauti ya dhamiri. Tabaka nane za elimu ya kuwaza. Kwa akili halisi ina ufahamivu, kujua jambo kwa kujua sababu yake, usawa wa

tabia, Maandishi Matakatifu, historia, ya kinyume, uwezekano, na kutokuwapo. Kwa maneno mengine masomo yao lazima yawe na elimu ya hali na tabia za vitu vyote na elimu ya kuchunguza asili ya kila kitu, inayoeleza tabaka sita za kuwepo, kwa majina ni, kitu, sifa, kitendo, mkataba, tafauti, na sababu. Kukuuza elimu kufikia ukubwa wa Aryavara, Mipango ya masomo lazima iwe na Ramayan, Mahabharat, tabaka sita za falsafa; - Mimansa, Yoga, Nyaya - Vaisheshik, Sankhya na Vedant - kumi Upanishats - Isha, Kena, Katha, Prashna, Mundak, Mandukya, Aitareya, Taittireya, Chhandogya, na Brihdarayanyak - Vedas nne - Rig, Yajpur, Sama na Atharva - Brahmana wanne - Aitareya, Sama, Gopath na Shatpath - Dawa - Charak na Sushrut - Unajimu - Suryasiddhanta - Muziki - Navad Samhita, Arthaveda au Siyasa na Sanaa 4 za kijeshi. Kuwa salimisha wanafunzi kuvisoma vitabu vya uwongo, Puranas zote (vya uwongo) na Tantras (uwongo) pia vitabu ya kidini, kama Tulsi, Ramayan yatolewe kabisa kutoka katika taratibu za masomo. Baada ya kumaliza haya katika muda wa miaka ishirini, mwanafunzi lazima arudi nyumbani, kuoa na kuingilia dunia.

**Puranas.**

1. Brahma 2. Padma 55,000 3. Vishnu 23,000 4. Shiva 24,000 5. Vayu 24,000 6. Bhagwat 18,000 7. Narada 25,000 8. Markanday 9,000 9. Agni 15,400 10. Bharishya 14,500 11. Brahmavaivarta 18,000 12. Linga 11,000 13. Varah 24,000 14. Skanda 81,100 15. Vamana 10,000 16. Kurma 17,000 17. Matsya 14,000 18. Garuda 19,000 19. Brahmananda 12,000

**Up-Puranas**

1. Adi 2. Nrisinha 3. Vayu 4. Shiva Dharm 5. Durvasa, 6. Kapila 7. Narad 8. Nandikeshwar 9. Shukra 10. Varuna 11. Samba 12. Kalki, 13. Maheshwar 14. Padma 15. Devas 16. Parashar 17. Marich 18. Bhaskar.

## SURA YA IV
## WANAFUNZI KURIDI NYUMBANI KUTOKA KUSOMA
## NDOA NA MAISHA YA JAMII

Kijana yule au mwanamwali yule tu lazima aingie duniani, ambaye yeye hajavunja sheria za utakatifu, ambaye amemaliza uwanafunzi wake kwa ukamilifu kwa mujibu wa matakwa ya mwalimu, na ambaye amesoma zote Veda nne, tatu, mbili, au hata moja pia, Angas; vya zaidi na Upangas: Maongezo ya Veda. **Manu - 3.2.**

Kwisha tunukiwa kwa sifa nzuri za kuweza kutimiza wajibu wa kuwa mwanafunzi kwa mwalimu wake; kwa kujipatia zawadi ya elimu ya Vedas kutokana na mlezi, baba, au mwalimu wake; na kupatiwa heshima na kuwekwa kwenye kiti, yeye lazima awe arusi na kupewa zawadi ya ng'ombe na baba yake na pia mkewe ampe ng'ombe wakati wa kufunga ndoa. **Manu - 3.3.**

Baada ya kupata ruhusa kutoka kwa mwokozi wake wa dini, na kumaliza kujitahirisha kwa mujibu wa sheria, yeye lazima aoe mwanamwali wa tabaka yake mwenyewe, aliye mkarimu. **Manu - 3.4.**

Mwanamwali huyo iwe hayumo katika tabaka sita za ukoo wa mama yake, na ambaye hahusiani na watu wa kale wa jamii ya baba yake, basi ni halali kwa ndoa. **Manu - 3.5.**

Kukataa umbali huu wa kufunga ndoa ni-

**(Shatapath. 14.4.11)** Kuwa imehakikishwa kuwa pasipo na umbo la kiwili wili huwa bora zaidi kuliko penye asili moja ya vitu. Akili ya mtu huvutika zaidi kwenye utamu ambawo yeye ametengeneza lakini ambawo yeye bado hajauonja. Kama mtu anavyotamani kuona kitu kisichoonekana baada ya kusikia sifa zake nzuri, basi hata msichana achaguliwe kwa njia hii hii ya sifa kwa kufunga ndoa, ambaye hana uhusiano wo wote wa karibu wa baba au mama. Hizi ni faida za ndoa za watu wasiohusiana kwa karibu:-

**Ndoa Kwenye Pahali Mbali**

1. Ndoa yao haipendelei mapenzi baina yao, ambayo kutoka utotoni mwao wanaishi, kucheza, kugombana, kupendana, kujua hamaki baina yao, uadilifu na uadui wa maisha ya kitoto, na tabia mbaya, na wameonana katika hali ya kuwa uchi.

2. Huwa hakuna mastawisho yo yote ya umbo au afya ikiwa watu wanaonana ni majamaa kwa sababu mchanganyika wa maji haya mawili hauwezi kuzaa kitu cha namna tafauti na chenye maana.

3. Ndoa baina ya wanaume na wanawake wa wazazi mbali mbali na wa asili mbali mbali ni nzuri kabisa na ndivyo inavyotakikana, kama mchanganyiko wa maziwa, sukari, tangawizi na dawa kama hizi mchanganyiko wa kupatana.

4. Ndoa ya watu wanaoishi nchi mbali mbali huhudhuriwa kwa shangwe na furaha, kwa sababu hali ya siha huwa nzuri kwa kubadilisha hali ya hewa na chakula kutoka kwenye nchi ambako mtu huwa ni mgonjwa na kwenda nchi nyingine na kusikia vizuri.

5. Huenda mtu akapatwa na furaha au msiba au kutiwa katika ugomvi wa majamaa kwa sababu ya kuoa papo na hapo. Haya hayawezi kutokea ikiwa majamaa wa ndoa wote wako mbali katika nchi nyingine. Kwa upande mwingine, kwamba ya *mapenzi hurefushwa kwa ndoa ya jamii mbili zinazoishi nchi mbali* mbali lakini haya hayawezekani kabisa na hawa wanaoishi pamoja.

6. Ndoa za watu wanaoishi nchi mbali mbali huwezesha kupata vitu vya nchi za mbali na msaada wa watu wao, hayo hayawezekani kwa wale wanaofunga ndoa karibu na makwao.

(Nirukta III,4.) Mtoto mwanamke anaitwa Duhita, kwa sababu harusi yake katika nchi mbali na kwao huwa yenye kuleta faida, lakini haya hayawi ikiwa anaolewa karibu na kwao.

7. Wazazi wa mtoto mwanamke wanaweza kuwa na fikira, kwa sababu itawabidi kuumpa kitu kila mara mtoto wa kike anapokuja kuwaona.

8. Watu walioana hutafakhar kwa kupata msaada kutoka kwa wazazi wao. Kwa kosa dogo tu baina yao, mwanamke mara atarudi kwao kwa baba yake. Ndoa za watu wanaohusiana na wa hapo na hapo huenda ikapata jina mbaya na kuchukiana; kwa sababu, hamaki za mwanamke huja juu upesi na si za nguvu. Hizi ndiyo sababu za kufunga ndoa na majamaa au asili moja na kuwa na umbali wa tabaka sita kwa upande wa mama.

**(Manu, III - 6.)** Jamii hizi kumi zisikubaliwe katika kufunga ndoa, hata iwe wamebarikiwa vipi kwa mali, wingi wa ngombe, mbuzi, tembo, farasi, ardhi, pesa na mali nginginezo.

**(Manu - 3.7)** Bwana au Bibi harusi asichaguliwe kwa ajili ya ndoa kutoka katika jamii zile, ambazo hazifanyi vitendo vya uadilifu, ambazo hazina watu waadilifu, ambazo zimedharau masomo ya Vedas, wenye watu waliona nywele ngumu au refu kwenye miili yao, wale wanaoweza kupata bawasiri, kifua kikuu, pumu, makohozi, kifafa, ukoma, matende, na ugonjwa wa kutoweza kuweka chakula tumboni, kwa sababu ndoa huhawilisha maradhi haya na kuwaambukiza jamii ya wanaofunga ndoa. Hata hivyo, vijana wa kiume na kike wa jamii nzuri kabisa lazima waunganishwe kwa ndoa.

**Nani wa Kumwoa**

**(Manu - 3.8)** Kijana asioe msichana wa rangi ya manjano, mwenye umbo kubwa, i.e. mrefu, mpana na mwenye nguvu kuliko yeye mwenyewe, anayehangaishwa na ugonjwa, mwenye nywele kidogo sana au mwenye nywele

nyingi sana, mwenye maneno mengi, au mwenye macho ya kahawia au mach yenye maradhi.

**(Manu 3.9)** Si mwenye jina la nyota za falaki kama Ashwani (Castor na Pollux), Bharni, Rohoni, Devi, Revati Bye, Chitri, na kama vitu vya peponi; miti, kama Tulsia, Genda, Gulabi, Champa, Chameli na mimea kama hii; ya mito kama, Ganga, Yamuna na kama mito mengineyo; Chandali na kama majina ya watu wa tabaka za chini; ya milima kama, Vindhya, Himalaya, Parvati, na milima mengineyo, ya ndege kama, Kokila, Mena, na ndege wenginewo; ya nyoka, kama Nagi, Bhujanga na chatu wenginewo; ya watumwa kama, Madho Dasi, Mira Dasi, na watumwa wenginewo; ya kitu cha kustaajabisha kama Bhim Kunvari, Chandika, Kali na vitesho vyenginevyo; kwa sababu majina haya ni ya kutokubaliana na ya vitu zisivyo sawa.

**(Manu 3.10).** Yeye aoe mwanamke mwenye umbo zuri na mwenye jina lakufuata na mwili wake, i.e. zuri kama Yashoda, na mengine kama haya, yenye maringo kama ukunjufu wa bata mzinga au tembo wa kike, mwenye nywele laini na meno mazuri, mwenye mwili laini:-

**Umri wa Kufunga Ndoa**

Q. Wakati gani na namna gani za ndoa ni nzuri kabisa.?

A. Wakati mzuri wakufunga ndoa ya mwanamke ni kutoka miaka 16 mpaka 24, kwa kijana wa kiume ni miaka 25 mpaka 48. Ndoa ya mwanamke wa miaka 16 na mwanamume wa miaka 25 ni amri ya chini kabisa; ya mwanamke wa miaka 18 au 20 na mwanamume wa miaka 30, 35, au 40 ni amri ya kati; ya mwanamke wa miaka 24 na kijana wa miaka 48 ni nzuri kuliko zote. Nchi huendelea vizuri ambapo sheria hii ya ndoa inafuatwa, ina utakatifu, na yenye watu wakupenda kupata elimu; Lakini nchi hudindimia katika mashaka ikiwa haina utakatifu, haina taa ya elimu, na yenye tabia za kuozana watoto wadogo, au yenye vijana waliooana lakini hawasikilizani. Kwa uzuri wa jamii unategemea juu ya utakatifu wa murua na kupata kwa elimu na kuangamia kwake pia unategemea kutakana haya na kutokuwa na elimu.

Q. Beti hizi zimetolewa katika Parashari na Shighrabodh:-

1. Mtoto mwanamke anaitwa Gowrie katika mwaka wake 8, Rohoni anapofika miaka 9, na Kannya (mwanamwari) afikapo miaka 10, na anaitwa Rajaswala (baleghe) baada ya umri huo.

2. Ikiwa yeye hajafungiwa ndoa katika mwaka wake wa kumi, mama yake, baba, kaka watakwenda jahanam wakiona siku zake za miezi (au damu).

A. Huu ni ushahidi wa Papo hapo wa Brahma Purana (Kitabu cha Mungu.)

Bwana Saith; kshana ni ule wakati ambako chembe ndogo kuliko zote inapoanza kugeuka Haya basi msichana anapozaliwa, anaitwa Gowrie, katika

kshana ya kwanza (udogo mno), Rohini katika ya pili, Kannya katika ya tatu, na Rajaswala katika ya nne. Kuonekana kwa msichana huyu huwapeleka, mama, kaka na dada, wote kwenda Jahanam (motoni).

Q. Beti hii hazina ukweli au ushahidi.

A. Kwanini hazina ushahidi? Ikiwa beti za Brahma (aliye umba utatu mtakatifu wa Hindu) hazi thibitishi, basi zako pia hazina uzani wo wote.

Q. Hollo! Wewe huukubali uthibitisho wa Parashara na Kashinath?

A. Heko! Wewe huukubali uthibitisho wa Brahma? Kwani Brahma si mkubwa kuliko Parashar na Kashinath? Ikiwa wewe huukubali uthibitisho wa beti za Brahma, sisi hatuzikubali za Parashar na za Kashinath.

Q. Ukweli wa beti zako unabadilisha uthibitisho wao kabisa; kwa sababu, sehemu nyingi za udogo zaidi ya elfu hupita tokea mtoto anapozaliwa; basi vipi ndoa yake inaweza kufungwa? Pia hakuna faida itakayopatikana ya ndoa hiyo ya umri wa miaka kumi tu.

A. Ikiwa beti zetu haziwezi kukubalika, basi zako pia ziko hivyo tu; kwa sababu ndoa ya msichana wa umri wa miaka 8 au 10 huwa haina faida. Watoto huwa wazuri wao toka katika ndoa ya wanawake wa miaka 16 mpaka 24, ambapo matumbo yao ya uzazi yameshakuwa tayari kuchukua mimba na miili yao inayo nguvu, na ya wanaume wa miaka 25 mpaka 48, shahawa zao vimepevuka na miili yao imekuwa yenye nguvu. Ilivyokuwa mtoto wa kike hawezi kuzaa anapokua na umri wa miaka 8, basi haielekei kumwita Gowrie, Rohini, na mengineyo. Ikiwa msichana huyo si mweupe ni maana ya neno Gowrie, lakini ni mweusi, basi ni kinyume kumwita Gowrie au mweupe. Pia gowrie ni mke wa Mungu Mahadeva. Rohoni ni mke wa Baladeva. Hawa ni kama wamama kwenu watu, wenye maarifa ya hadithi za muingu au wanaoamini Puranas. Hapo, mnapomwita mtoto wa kike kama Gowria na kama miungu ya kike vipi itawezekana na kuwa haki na yenye sheria ya kumwoza? Kwa hivyo beti zake na zetu zote ni za upuuzi na za uwongo. Kama tulivyotunga beti za jina la Brahma kwa kutia "Bwana Saith", kwa hivyo beti zilizotajwa na wewe zimeandikwa na kukusudiwa Parashara na wengine wa kutunga sheria. Kwa hivyo, ni bora kuwa kataa hawo wanaojiita wathabiti na kuyafuata yale yanayofuatana na Vedas ambawo ni wathabiti wa kweli katika mambo yote. Inasema Manu:-

**(Manu IX. 90)** Mwache mwanamwali ajitafutie mume ambaye amesoma kama yeye mwenyewe, miaka mitatu baada ya kukua (kubaleghe). Damu ya mwanamke huja kila mwezi, na kuna hedhi 36 katika miaka 3, baada ya hapo ndoa inakubaliwa, lakini si kabla ya hapo.

**(Manu - 89)** Afadhali vijana wa kiume na kike wasioane mpaka kuja kwao kuliko kuoana ikiwa hawana elimu sawa sawa, kuwa, biharusi na bwana harusi wasiwe wenye sifa za kuchukizana, tabia, na desturi. Kwa hivyo, inaonyesha ndoa huwa si mwafaka kabla ya wakati ulionyeshwa hapa juu au baina ya watu wa tabia zisizo fanana.

**Namna ya Kupanga Ndoa**

Q. Niambie kama kupanga kwa ndoa iwe katika mikono ya wazazi au wawachiliwe wenyewe vijana na wanawali.?

A. Itakuwa afadhali ikiwa itakuwa katika mikono ya wanaotaka kufunga ndoa wenyewe. Ikiwa wazazi watapenda kuyatia mambo haya vichwani mwao na kutaka kuwaoza watoto wao wa kiume na kike; basi wasiyamalize bila ya ruhusa za watoto wao wenyewe; kwa sababu ndoa zinazofungwa kwa kutakana wenyewe basi si aghlabu kuleta ugomvi na mabishano, na huleta watoto wazuri. Ndoa bila ya idhini ya bi Arusi na Bwana Arusi maisha huwa na shida. Jambo muhimu la ndoa ni Bi Arusi na Bw. Arusi na si wazazi wao; ikiwa wao wanapata, wao huwa na furaha; lakini ikiwa hawapatani, wao ndiyo wenye taabu.

**Nyumba Yenye Furaha**

**(M. 3, 60.)** Furaha, bahati nzuri, na sifa nzuri huwepo katika nyumba ambayo mke ametosheka na mumewe daima, na kinyume chake; na mashaka, umaskini, na kusutana hutokea katika ile jamii isiosikilizana na kugombana. Kwa hivyo, kanuni ya mwanamke kuachagua mume (Swayamvara) ambayo inapendelewa katika Aryavarta kutoka hapo zamani, inahesabiwa kuwa ni yenye faida katika ndoa. Mwanamume na mwanamke wanapotaka kufunga ndoa lazima waangalie ulinganifu wa elimu walionayo watu hawa wawili, adabu, tabia, uzuri, umri, uhodari, jamii, kimo, na ustahiki mwingineo. Ndoa huwa haina furaha ikiwa haina mapatano katika tabia za hawo waliooana. Pia, furaha haiwezi kupatikana ikiwa ndoa inafungwa kabla ya miaka yake kufika. Inasema Veda:-

**Vedas Kuhusu Umri wa Ndoa**

**(Rig. 3. 8.4)** Kweli, kijana huwa mwenye ufahari na mwenye faida kwa wote, ambaye ametakaswa kwa kila njia na kutumikiwa na uzi mtakatifu, ambaye amekiweka kiapo cha utakatifu na amepata sifa katika elimu na kujilikana kama mtaalamu, wanavyuoni wenye ujuzi, shauku ya kukuuza maarifa ya taalima, na jilihada, na kumfanya mtu mwenye kustahiki heshima. Lakini wale wanaume na wanawake ambawo bila ya kuki weka kiapo cha utakatifu na bila kupata elimu na welekevu katika akhlak nzuri, kuoa katika umri mdogo, huharibika na kuangamia, na wao hawafaulu kuwa katika hali za heshima baina ya wataalamu.

**(Rig. 3.55.16)** Kama ngombe ambawo hawajakamwa, basi hata hawo wanawake vijana wachukue jukumu la uzazi, ambawo wameshaupita utoto, wao ambawo wanauwezo wa kufanya kazi zote za binadamu kwa njia iliyobora kama iwezekanavyo, wao ambawo wameshaupita utoto au kutokamilika, wao ambawo wamekuwa vijana kamili na wenye akhlak nzuri, wao ambawo wanapenda masomo ya maandishi matakatifu na maandishi ya busara yaliyondikwa na maandishi mashuhuri ambawo wanajulikana kwa kikiweka kiapo cha elimu na wenye kufuata sheria zao, na ambawo wameolewa na wanaume vijana.

**Hadhari.**

Wanawake wajihadharishe na wasiende kwa wanaume; kwa sababu, tabia zao uzuri, na uwanawali wao katika zama za ustawi wa ujana wao wa maisha, ni kitu cha furaha hapa na baadaye. Lakini ndoa kabla ya ujana huharibu miili ya wanawake zaidi kuliko ya wanaume.

**Ndoa ya Ngumbaru**

Wanaume na wanawake ikiwa wataishi kama wale ambawo wako tayari na wenye nguvu za ujana wao na wanaweza kupata watoto na kuoa vijana wanawake walio wazuri, na kuendelea kuishi miaka 100 au hata zaidi kwa furaha na wamebarikiwa na watoto na wajukuu. Basi kila mmoja wao aseme:.

**(Rig 1.179.1).** "Mimi nitaoa baada ya kukua kikamilifu na nguvu ya akili na mwili, na kupata elimu kamili na mafunzo ya akhlak kwa mujibu wa sheria za wanafunzi, ili niweze kupata maisha mazuri ya uzee wangu ambapo usiku na mchana hupunguza uzuri na kudhaifisha nguvu za mwili kwa kupunguza maisha kama wao wanapoinyimia masika na mapambazuko uzuri wao." Kinyume cha haya na kinachopinga mafunzo ya Vedas, haifanyi ndoa kuwa yenye furaha.

Nchi hii ya Aryavarta ilipata ustawi wa daima na maendeleo madhali wenye hekima, wana wa falsafa, wanawa kiume wa kifalme, watawala, na watu ambawo waliweza kupata elimu wakati wa kiapo cha elimu katika ujana wao na wakafuata sheria za ndoa kwa mwanamwali kujichagulia mume wake (Swayamvara: yakujitafutia mwenyewe). Lakini hapo kujipatia elimu wakati unapokuwa kijana husita na kufunga ndoa kuwa mikononi mwa wazazi, wananchi kupungua thamani na mwili kupungua nguvu, na hiri hutokea kwa utaratibu katika nchi yote. Kwa hivyo, tabia mbaya ya kufunga ndoa kabla ya miaka yake iwachiliwe mbali na watu wenye akili, wao ambawo lazima wafuate yaliyosomwa katika desturi za ndoa, ambapo msichana humchagua mume wake mwenyewe (Swayamvara.) Lazima ifanye katika tabaka zao wenyewe. Tabaka hizo lazima ziwe za ulinganifu wa elimu, tabia, na hamaki.

**Ukabila Na Sifa.**

Q. Kama vile Brahmin ni yule ambaye wazazi wake ni Brahmins jee inawezekana kuwa watoto wa watu wa tabaka nyingine kuwa Brahmins?.

A. Ndiyo, wapo wengi, sasa pia wako wengi, na watakuwa wengi zaidi mbeleni. Kwa mfano, Chhandogya Upanishat ana mwonyesha St. Jabal ambaye ni wa wazazi wasiojulikana, Mahabharta St. Vishwamitra wa tabaka ya Kshatriya, na St. Matanga wa Chandal au tabaka ya chini, kwa kuwa Brahmins. Kwa sasa yeye anastahiki kuwa Brahmin ambaye amepata elimu ya juu kabisa na tabia, na mtu njinga anastahiki kuitwa kama Shudra au kwenye tabaka ya watumwa. Tabaka hii ya kawaida taendelea hata hapo mbele.

Q. Haya basi, vipi mwili, uliozaliwa kutokana na tumbo na shahawa za tabaka hili, nakugeuka kuwa tabaka jengine?

A. Mwili wa Brahmin hautokani kutoka mchanganyika wa tumbo za uzazi na shahawa. Bali, kinyume, mtu huwa Brahmin kwa kuwa mwadilifu.

**(Manu, 11.28)** Maana ya maneno haya imefahamishwa kabla ya hapo. Lakini inaelezwa tena hapo. Mwili huu unafanywa kuwa Brahmin kwa kusoma na kusomesha, kwa kufikiri na kuwa fanya wengine pia wafikirie, kwa kutoa muhanga wa moto, kwa kusoma Vedas zote na maelezo yao, sababu, kuzitumia yaliyomo, matamishi, kuziimba, kwa kutoa muhanga wakati wa mwezi mpevu na wakati mwingineo kwa mujibu kama iliyoelezwa hapa juu, kwa kuzaa watoto waadilifu, kwa kufuata sheria tano muhimu zilizotajwa hapa juu, sala, kujitakasa kwa moto, kuwatumikia wazazi, kuwasaidia wasiojiweza na watu wa tabaka la chini na wanyama pia, na ukarimu, kwa muhanga maalum wa moto na kutoa muhanga kwa kujiweka pamoja na wataalamu na kuwaheshimu, kwa kujipatia elimu katika sanaa zote na vitendo vya uadilifu, kwa kusema kweli na kuwafanyia wenzako wema, kwa kuacha kuwa mushirikina, na kujaribu kufanya yote yaliyo mazuri.

Q. Jee wewe huaamini maneno haya?

A. Ndiyo tunaamini.

Q. Kwa nini basi munaamini kuwa tabaka za watu zinatokana na watu walio wazaa?

A. Si mimi tu na amini hivyo, bali watu wengi wanaamini hivyo tokea kale.

Q. Wewe bado unaamini mambo ya kale?

A. La; lakini sisi hatukubali akili yako iliyo kuwa si sawa, na kwa hivyo tunakupinga.

Q. Uhakikisho gani unao kuonyesha kama sisi ni waongo na wewe ni ukweli?

A. Uhakikisho ni maneno yako mwenyewe, kuwa nyinyi mnaamini desturi iliyopotokea mababu watano au sita waliopita na mkaona hayo ndiyo yenye kufuatwa, lakini si tunawaamini Vedas na sheria zilizowekwa tokea mwanzo wa viumbe mpaka leo kuwa ni uhakikisho wa zamani za kale. Ona, mara nyingi hutokea kuwa baba kuwa mwadilifu na mtoto wake wa kiume kuwa mbaya: Mwana mwadilifu kuwa na baba mwovu, wakati mwingine utaona baba na mtoto wake wakiume wote wawili huwa waadilifu au waovu,. Basi, wewe si mkweli na unayo maono ya uwongo. Tazama Manu anasema nini.

**(Manu 4.178.)** Watu wafanye vile baba zao na baba zao walivyofanya; lakini wafuate njia za baba na babu wazuri lakini wasiwafuate baba na babu waovu. Kwa sababu hakuna dhambi au maumivi ikiwa utawafuata wale waliokwenda njia ya haki na uadilifu. Wewe una amini au huamini?

Q. Ndiyo sisi tunaamini.

A. Tazama yaliyowekwa wazi na Mungu katika Vedas ni ya milele; lakini yale yanayopingwa haya wezi kuruhusiwa. Si lazima watu waamini hivyo?

Q. Kweli kabisa.

A. Waulize wao, nani asiye amini kuwa ikiwa mtu ambaye ni tajiri na baba yake ni maskini, lazima aitupe mali yake yote kwa heshima ya umaskini wa baba yake. Lazima kwani mtu baba yake akiwa kipofu basi na yeye pia ayapofue macho yake?

Jee mtu baba yake akiwa mwovu, ifanye ubaya peke yake?

Q. La, sivyo, sivyo. Lakini ni kinyume chake watu lazima wawache kufanya uovu na kujaribu kufanya yaliyo mema wanayoyaona watu wakifanya.

A. Mwulize yule ambaye anaona mgawanyiko wa madhehebu ambayo yanafanyika kwa mwungano wa nguvu za mwanamume na mwanamke, na si mgawanyiko wa tabia za mtu, vitendo, na kwanini. yeye hayaita haya yote kuwa Brahmin. Brahmin ambaye anawacha madhehebu yake na kufanya kuwa mtu wa chini au mchafu, au kugeuka kuwa Mkristo au Mwislamu. Hakika atasema yeye haitwe Brahmin, kama yeye alivyowacha kufanya kazi za U-Brahmin. Pia imehakikishwa kwamba wale Brahmin na madhehebu mengine ambaye yanafanya kazi nzuri, lazima wahesabiwe kama; wale watu wa madhehebu ya chini ambawo wana tabia njema, desturi, na asili, wahesabiwe kuwa ni wa madhehebu ya juu; na ikiwa watu wa madhehebu ya juu na wanafanya dhambi na vitendo vya madhehebu ya chini, basi wao pia wawekwe na watu wa chini kwa sababu ya desturi zao.

Q. Hizi ni beti II za sura ya 31 ya Yajurveda:-

Brahmin anazaliwa kutoka kwenye mdomo wa Mungu, Kshatriya kutoka kwenye mikono yake, Vaishya kutoka kwenye mapaja yake, na Shudra kutoka kwenye miguu yake. Kama vile mdomo hauwezi kuwa mikono na viungo vingine vile vile, basi Brahmin hawezi kugeuka kuwa Kshatriya na tabaka nyinginezo, wala Brahmin hawezi kuwa Kshatriya au Kashtriya kua Brahmin.

A. Maana ya ubeti uliofanya wewe, si kweli, kwa sababu, ibara "bila ya umbo na aliyeenea kote mweza wa yote" inataka ionyeshwe kwenye karina ya kizamani katika kuifasiri. Ambapo Mungu hana umbo, yeye hawezi kuwa na mdogo na viungo vyengine vya kiwili wili. Ikiwa yeye anawo mdomo na sehemu nyinginezo yeye hawezi kueenea kote. Ikiwa yeye hayuko kote, hawezi kuwa na uwezo wote, mwuumba, mthibitishaji, na mwangamizi wa dunia, hakimu wa vitendo vya roho vilivyo vizuri na viovu, roho mjuzi, wa daima, au mwenye sifa nyinginezo kama hizi. Hata hivyo, maana ya maneno haya ni kama huyo anayeupenda mdomo katika mwili ni bora na kuonekana wenye kuliko viungo vyenginevyo katika alivyoviumba Mungu mweza, na Brahmin; yeye ambaye ana nguvu zaidi kuliko

wengine, ni Kshatriya kwa sababu, Shatpath anasema kuwa neno bahu maana yake ni bidii na nguvu; yeye ambaye anasafiri ikiwa kwa uwezo na nguvu za mapaja yake, ambayo ni sehemu ya chini ya mwili wake na juu ya magoti, katika nchi yake mwenyewe au anakwenda kwenye nchi za kigeni na kufanya biashara huko katika vitu vyote, ni Vaishya; na yeye ambaye ni mjinga na mwenye sifa za kijinga kama miguu ya sehemu ya chini kabisa ya mwili, ni SHudra. Katika sehemu nyingine Shatpath anafasiri maneno haya katika kuleta maana hii hii, kwa mfano kama huu.

Kutaja habari za Brahmin, inasema kuwa kama wao ni wanachama wakubwa wa jamii, basi inasemwa kuwa wamezaliwa kutokana na mdogo wa Mungu. Hii ni tafsiri maakul ya maneno ya Vedic. Kwa maneno yaliyo wazi, kama mdomo ni sehemu bora kuliko sehemu zote za mwili basi pia Brahmin huhesabika kuwa ni bora katika binadamu kwa uwezo wa maarifa yao kamili na tabia nzuri, desturi, na asili. Ilivyokuwa utukufu usiokuwa na umbo na usiofanana kitu hauwezi kuwa na mshabihiano wo wote mdomo na viungo vyenginevyo vya kiwili wili cha binadamu, kuzaliwa kwa Brahmin kutoka kwenye mdomo wa Mungu ni muhali au haiwezekani. Ni kama harusi ya mtoto wa kiume wa mwanamke tasa. Pia, ikiwa Brahmins na watu wengine wamezaliwa na mdomo na viungo vyengine, basi muambo yao yatakuwa kama viungo vile, kwa sababu sifa za kitu hutokana na kitu chenyewe. Miili yao ingekuwa duara na yenye shimo kama mdomo, ile ya Kshatriyas kama mikono, na miili ya Vaishyas kama mapaja, na ile ya kina Shudras kuwa kama miguu. Lakini haiko hivyo. Wewe utasema nini ikiwa mtu atakwambia kuwa hawo ndio Brahmins na madhehebu mengineyo, waliozaliwa kwenye midomo na viungo vyengine; lakini huwezi kuitwa kwa majina hayo, kwa sababu wewe umezaliwa kutoka kwenye tumbo la mwanamke kama watu wengine. Kutokuzaliwa kutoka kwenye mdomo wa Mungu na kujisifu kwako kwa kuitwa Brahmin na mengineyo si kitu na ni aibu. Hata hivyo, tafsiri unaifasiri wewe ya maneno haya ni ya upuuzi, lakini yetu ni sahihı kabisa. Pia imetiliwa nguvu na Manu inasema 10,65.

Ikiwa mtu anazaliwa na Shudra au katika jamii ya madhehebu ya chini na anawo uwezo, tabia na desturi za Brahmin, Kshatriyas, na Vaishyas, yeye atambuliwe kwa sifa alizonazo na si kwa ukabila. Na vivyo hiyo, ikiwa mtu amezaliwa Brahmin, Kshatriya au jamii yaa Vaishya, na anazo sifa, tabia, na desturi za zile zinazofanana na Shudra, basi lazima azame chini na kufika waliko Shudras. Pia, mtu anatoka kwenye jamii ya Kshatriyas na Vaishyas na anazo sifa za Brahmins na Shudras, anafananishwa nawo kwa mijibu wa uwezo wake. Kwa ufupi, wanaume na wanawake wa tabaka nne wafanishwe na tabia zao.

Hivi ni vipande vya Apasthamba. Maana yake ni: 1. Tabia nzuri humwondoa mtu wa tabaka ya chini na kumpandisha cheo cha juu na yeye lazima ahesabiwe katika cheo ambacho yeye anastahiki. Katika njia hii 2. Tabia mbaya humshusha mtu cheo, na yeye ahesabiwe kuwa kama hawo. Kama mwanamme hushuka cheo kwa tabia mbaya ya kutokuwa mwadilifu, pia wanawake

huwekwa kwa mujibu wa sifa zao nzuri au mbaya. Mhakikisho huu wa kidini hutuletea kubainisha kuwa hii tu ndiyo njia inayomfanya mtu awe na tabia, akhlak, na desturi, na kuhifadhi usaji wa kabila lao; hivyo ni kusema, itakuwa hakuna mtu kama Kshatriya, Vaishya, au Shurdra baina ya Brahmins; pia amri za Kshatriya, Vaishyas na Shudras watajiwekea heshima nzuri za kabila. Hapatakuwa na wana wa haramu katika kabila lolote. Hivi hauta kuwapo uchumvi au udhaifu katika kabila lolote.

Q. Nani atamsaidia mwana mume yule na mke wake katika uzee wao, ilhali mtoto wao wa kiume au wa kike mmoja tu ajitia katika kabila jengine? Kuna khofu ya jami yao kuangamia kabisa. Kifanywe nini katika hali kama hii?

A. Hapana mtu ambaye ataweza kuposa msaada kwa watoto wake mwenyewe au jamii yake kuangamia kabisa; kwa sababu, yeye atapewa watoto wengine ambawo ni wenye kufuata amri zake na Baraza za Taalimu na utawala. Hata hivyo hapatakuwa na mchafuko. Mgawanyiko huu wa utawala kwa mujibu wa uzuri wake na tabia ya kufaa inaweza kuonekana katika umri wa miaka 16 kwa wanawake na miaka 25 kwa wanaume kwa mtihani thahiri. Pia, ndoa zao zifungwe katika kabila zao i.e Brahmin aoe mwanamke wa Ki-Brahmin kwa sheria, Kshatriya, wa Ki-Kshatriya, Vaishya aoe mwanamke wa Ki-Vaishya na Shudra aoe wa Ki-Shudra. Kwa njia hii watu wataweza kufanya kazi zao kwa heshima na kuishi kwa mapenzi na amani kama mume na mke baina yao na miongoni mwa jamii.

**Wajibu wa Kabila 4.**

Yafuatayo ni desturi na wajibu wa kabila nne:-

**Wajibu wa Maaskofu.**

**(Manu, 1,88).** Wajibu sita za Brahman ni 1. Kusoma 2. Kusomesha, 3. Kutoa muhanga, 4. Kutumika katika kutoa muhanga. 5. Kutoa na 6. Kupokea sadaka. Lakini kupokea zawadi ni kazi ya chini kwa mujibu wa Manu.

**(Gita.)** Tabia kumi na tano ambazo lazima mtu awe nazo na wajibu ambawo lazima ufanywe na watu wenye madhehebu ya Brahmin ni 7. shama: kutosheka, na hata isikupitie akilini mwako fikra ya kutenda uovu, usiyawachie matakwa yako kuwa si ya vitendo vya uadilifu, 8. dama: kuzizuia hisia za kusikia, kuona na nguvu nyinginezo kutokana na vitendo visivyo vya haki na kuvitumia katika uadilifu. 9. tapa: adhabu ya kudumisha, iwe ya nguvu na ya kuzuia tamaa, kuziweka tamaa chini, kujifanya uwe mwadilifu saa zote; 10. shoucha: ufaji, Manu inasema 5.1000.

Mwili unasafishwa kwa maji ile sehemu yake ya nje tu, moyo unasafishwa kwa mazoezi ya kweli, roho zenye uhai husafishwa kwa elimu na kwa kujitolea, na ufahamu kwa husafishwa kwa busara na falsafa: i.e. ili kujiweka bila ya maasi ya ndani kwa ndani ya kupenda na kuchukia na mengineyo na kutokana na uchafu wa ndani ya roho na kutokana na uchafu wa nje ya kiwli wili:- Kwa maneno

mengine, mtu huwa amehadhifika hakika kwa kupata sifa ama upungufu na ukweli wa baadaye na kukataa uwongo II, Kshanti: kustahili kuwa na itikadi kamili katika dini baada ya fika kwenye kiwango cha kusifiwa na kutosifiwa; raha na maumivu, joto na baridi, njaa na kiu, faida na hasara heshima na aibu, furaha na huzuni, na mengineyo pamoja na kinyume na hayo: 12. arjava: uaminifu, kuutukuza wema, unenyekevu, urahisi, tabia nzuri, na kuwacha ubaya na ushari; 13. jnana: kupata elimu kwa kusoma Vedas na maandishi mengineyo ya dini na maelezo yao, na kuwa na nguvu ya kuweza kuyasomesha haya yote, bila ya kupendelea, kuwa na ukweli, kujua ukweli wa mambo kama valivyo, kama vile, kujua na kuamini chenye uhai na kisicho na uhai, 14. vijinana: elimu maalum ya vitu vyote vya duniani na kwendea juu mpaka kwa Mungu, na namna ya kuitumia sawa sawa elimu hii: 15. Astikta: Amini, kati hutaigeukia Veda na kuipunga na kumpinga Mungu, uokovu, usafirishaji, dini, elimu, marafiki wazuri, kumtumikia mama, baba na wageni.

**Wajibu wa Wapiganaji Vita.**

Wajibu wa desturi za Kshatriyas ni, 1. rakshana: kuwahifadhi watu kwa uadilifu. i.e. bila ya kupendelea upande wo wote, na kuuheshimu ukweli, kuwatisha waovu, na kuwasaidia wote kwa njia zote; 2. dana: kutumia pesa na mali nyingine katika kuendeleza elimu na dini na katika utumishi wa wanaohitajia; 3. ijya: kujitolea muhanga wa moto na matakatifu mengineyo: 4. adhyayana: kusoma Vedas na maandishi mengine matakatifu, na kuiweka akili na mwili katika hali ya usafi saa zote kwa kuweza kujizuia kwa mambo yote na kutobabaishwa na uasherati; 5. shourya: kutokuwa na hofu kupigana kwa mkono mmoja na mamia au maelfu; 6. teja: kuwa daima mwenye heshima au mbali na ubaya, shujaa na mjasiri. 7. dhriti: kuwa mstahimilivu na mwenye kujiwekea heshima; 8. dakshya: kuwa hodari katika kazi zote za mfalme na raia na katika sheria na falsafa; 9. kutokasirika au kukiwacha cheo wakati wa vita, alkini kuwa mgumu na bila hofu katika vita, kuwa, kupigana kwa ushujaa na mhakikisho wa kushinda na pia kuyalinda maisha yake, na ikitakikana, kuacha kazi kabla ya auni au kutumia njia nyinginezo kujipatia ushindi kutoka kwake; 10. dana: kuwa mkarimu; 11. Ishwara bhava: Kujiwekea heshima mbele ya wote na bila ya kupendelea upande mmoja, kufanya zawadi baada ya kupendelea, kutekeleza ahadi, na katu kutoivunja. Hizi ndizo wajibu II muhimu za Kshatriyas. M. 1,89, na Gita.

**Wajibu wa Wafanyi Biashara.**

**(Manu, 1,90.)** Wajibu na shahada za Vaishya ni, 1. pashuraksha: kuchunga na kuzalisha ngombe; 2. dana: kutumia pesa na kujishughulisha kuendeleza elimu na dini na kuwasaidia wengine katika kazi kama hizi; 3. ijya: kufanya muhanga wa moto na kutukuza kazi nyinginezo za dini; 4. adhyayana: kuisoma Veda na maandishi matakatifu mengine pia; 5. vanik patha: kufanya namna zote za biashara; 6. kuseed: kushirikisha fedha ilikupata faida @ 4, 6, 8, 12, 16, au 20, annas kwa centum, lakini si lazima, na asichukue faida kupita thamani ya kitu, yaani ikiwa rupia moja imeshirikishwa basi ushuru usizidi kuliko rupee mbili hata ikiwa ni imechukua miaka mia basi yeye asitoe zaidi kuliko hivyo; na 7 krishi:

kulima.

**Wajibu wa Mfanya kazi**

**(Manu 1, 91.)** Kazi ambayo amewekewa Shudra tu na tabia iliyokuwa dhahir ni yeye lazima amtumikie kwa vilivyo Brahmanas, Kshatryisas na Vaishyas, kujiepusha na kusengenya, husda, kiburi na tabia nyinginezo zilizokuwa mbaya. Hivyo tabia na wajibu wa jamii umeelezwa wazi. Watu wote hufurahia mafanikio kwa kufuata amri, yaani wao wapewe haki na fursa za mambo yote kwa mujibu wa sifa na shahada zao. Kwani, watu wa tabaka ya juu wataogopa watoto wao kuwa wajinga na kupatikana na maovu wa lazima watiwe katika tabaka ya Shudras, na wafuasi wao wenyewe watakuwa wakijihadharisha ili wasijizamishe na kuwa katika tabaka ya Shudras ikiwa wao hawatapata elimu na shahada zao. Pia, watu watabaka wa chini watashajiishwa watamani kuwa kwenye daraja za tabaka za juu.

Brahmanas lazima awe na uwezo wa kueneza na kushika elimu na dini; kwa kuwa mjuzi wa elimu na dini; wao wawe tayari daima kutekeleza wajibu. Ujumbe wenye sativa wa serekali kwa Kshatriyas hauleti udhuru wo wote kwa nchi na au kuleta adha yo yote ya amani. Vaishyas ni watu hasa wa kuchunga wanyama wa nchi: kwa sababu wao ni watu ambawo wanaweza kuifanya kazi hii kwa vilivyo. Shudra anapewa kazi za kuhudumia, kwa sababu, ilivyokuwa wao hawana elimu ye yote ni wajinga wao hawawezi kazi nyingine ye yote ambayo inahitaji akili au shahada. Lakini yeye anaweza kufanya kazi zote nyingine za kuhitaji nguvu. Hivyo ni wajibu wa mfalme na watu wengine wastaarabu kiigawanya enzi za kazi kwa mujibu wa uwezo wa tabaka zote sifa zao.

**Namna za Ndoa.**

**(M. 3,21.)** Kuna namna nane za ndoa, viz, 1. Brahma, 2. Daiva, 3. Arsha. 4. Prajapatya, 5. Asur, 6. Gandharv. 7. Rakshasa na 8. Paishacha. Maelezo yao ni: Kijana na mwanamwari, baada ya kuzitimiza sifa za kuwa mwanafunzi na kupata elimu ya kisasa, ni waadilifu na wenye heshima, na wamefikiria kuungana katika ndoa kwa kutakana wenyewe kwa wenyewe, basi ndoa yao huitwa Brahma. Namna ya ndoa ya Daiva ni ile ambayo Bi Harusi anapambwa na kupewa Bw. Harusi kwa sherehe na askofu kwenye muhanga mkubwa. Namna ya ndoa ambapo mahari yanapokewa kutoka kwa Bw. Harusi, anaitwa Arsha. Ndoa inayofungwa ili kuendeleza dini inaitwa Prajapatya. Bi Harusi na Bw. Harusi wanapoana kwa kufikiria zawadi kutokana na wao, ndoa hiyo huitwa Asura. Mwungano wa wao kwa wao baina ya kijana na mwanamwari kwa sababu maalum kwa kutokana wenyewe na bila ya ujamaa na bila ya wakati mwafaka inaitwa Gandharva. Kumkamata msichana kwa nguvu katika vita kwa ghafla au kwa kumdanganya, inaitwa Rakshasa. Kumkumbatia msichana kwa nguvu na kulala naye kwa sababu ya ulevi au cho chote kinacholevya, inaitwa ndoa ya Paishach. Ndoa zote hizi zilizotajwa, Brahma ndiyo ndoa bora kabisa, Daiva ni ya kati na kati, na Arsha, Asura na Gandharva ni mbaya, Rakshasha ni ya chini kabisa, na ndoa ya Paishacha ni ya dhambi kubwa.

**Ndoa Yenye Sifa Nzuri.**

Hata hivyo, kuyapunguza maovu, lazima iwepo sheria maalum, kuwa Bi. Harusi na Bw. Harusi wasiwachiliwe kuonana kwa siri kabla ya ndoa; kwa sababu kuonana kwa wanawake na wanaume katika ujana wao huleta hatari na ni jambo la aibu. Lakini wakati wa kufunga ndoa ya msichana na kijana unapokaribia, ni kusema, kama inapobakia mwaka au miezi sita tu wao kumaliza masomo yao, picha na vyenginevyo lazima vipelekwa kwa waalimu wakubwa wa skuli za kike na za kiume. Wafunga ndoa watachaguliwa, habari za maisha yao kutoka wamezaliwa mpaka hapo walipofika lazima zipatikane na zilinganishwe sifa, tabia na hamaki zao. Tabia zao zinapofanana picha na mengineyo tena hapo watu wawili hawo wapelekwe kwa wanaotaka kufunga ndoa na maombi yao, na mabwana na mabibi zao waambiwe makusudio yao. Tena hapo vyama viwili vimesikilizana katika ndoa hiyo basi wao wapelekwe nyumbani. Ikiwa wanataka kuoana mbele ya waalimu wao, basi ndoa yao ishangiriwe hapo tu. Ikiwa si hivyo, basi ni bora kufunga ndoa katika nyumba ya mtoto wa kike. Kijana na msichana wanapoletwa pamoja kuwa uso kwa uso, waalimu na wazazi wa mtoto wa kike watengeneze mkutano ambawo utawafanya watu wa wili hawa kuzungumza juu ya kitu maalum mbele ya watu wengi wazuri. Ikiwa wao wanataka kuuliza mambo ya siri, basi wao wayaandike maswali hayo kwenye karatasi na kupeyana mikononi.

**Wakati wa Kusherehekea Ndoa.**

Wao wanapotaka sana kufunga ndoa, basi wazazi wao wajishughulishe sana na vyakula vyao, ili miili yao ambayo imedhoofishwa na shida na lamu za masomo na shuruti au sheria za kuwa wanafunzi, lazima katika siku chache tu itaanza kupata nguvu na uchangamfu kama tarakimu za mwezi katika wiki mbili. Baada ya hapo msichana apatapo siku zake za miezi na anapokoga kumaliza hedhi, pazia litiwe kwenye meza ya kutolewa dhabihu na sadaka za moto zifanywe kwa udi wa kila namna zenye harufu nzuri na madawa dawa na siagi safi na vitu vyenginevyo pia vifanywe. Wataalamu wa kiume na kike na majamaa zao waalikwe na kuheshimiwa. Siku yao ya kutiwa nyumbani inapofika, sherehe za harusi au za kufunga mikono lazima zifanywe usiku sana au kama saa 4 za usiku kwa mujibu wa Sanskar Vidhi na baada ya kumaliza sherehe za kutiwa nyumbani basi vijana hawa wawili waingie kulala katika chumba chao cha faragha. Kuingiliana kimwili, wao lazima wafuate mafunzo ya makungwi mwanamume alitie mimba tumbo la uzazi kwa shahawa zake na mwanamke ajaribu kuziweka na kuzipokea hizo shahawa. Wao wasipoteze nguvu zao ambazo walizitunza walipokuwa hawajoa; kwa sababu mtoto anayezaliwa katika mwingiliano huo, huwa mwenye nguvu na mzuri. Wakati wakuzitia hizo shahawa (manii) katika mfuko wa uzazi, mwanamke na mwanamume wote wawe wametulia, miili yao inyoke, pua kwa pua, na macho kwa macho, na akili zao ziwe zimejaa furaha. Wao wasisogee: mwanamume aupumzishe mwili wake, na mwanamke avute puumzi wakati wa kutiwa manii, aibane kuma yake ili manii yote iingie katika tumbo la uzazi. Baadaye wote wawili waoge kwa maji safi. Mwanamke mtaalamu

hujua kama ana mimba mwishoni mwa kuingiliana; lakini ikiwa hedhi hajaonekana mwisho wa mwezi ukifika basi hiyo huonyesha wazi.

**Tabia zinahitajika wakati wa Mimba.**

Baada ya kukoga wao lazima wanywe maziwa ambayo yamechemshwa na kutiwa tangawizi, zaafarni; mane mane au asagndha iliki na salam misri zote zichanganyishwe na kupikwa kisha zipozwe kwa ajili ya sherehe hii, kisha walale kwenye vitanda mbali mbali. Hedhi inaposita kuja mwishoni mwa mwezi huonyesha ishara ya mimba, basi mume na mke wasionane ki mwili kwa muda wa mwaka mmoja; kwa sababu mtoto huwa mzuri, na mtoto wa pili pia huwa mzuri kama wa kwanza. Kwa kupuuza nasiha hii hupoteza nguvu na kujipunguzia umri, nakujiletea maradhi mengi kwa wao wote wawili. Lakini wao waishi kwa mapenzi katika mazungumzo yao na mambo yao yote na lazima wavute puumzi za masikilizano na urafiki. Mwanamume lazima aitunze manii yake isimwagike bure, na mwanamke ailinde mimba yake kutokana na madhara yo yote. Chakula chao na nguo zao zisiwe za kuvutia ili mwanamume asijeakapoteza manii yake na wakati wa mimba wa mwanamke uwe wa raha na pia kwa mwili wa mtoto ambaye bado hajazaliwa, kwa kupata msingi mzuri, uzuri, siha, nguvu na ushujaa, na kupata uzazi usiokuwa na taabu kwenye mwisho wa mwezi wa kumi tokea siku ya kuchukua mimba. Mimba itunzwe kutoka mwezi wa nne, na pia ituzwe zaidi kutoka mwezi wa nane.

**Chakula Wakati wa Mimba.**

Mwanamke mwenye mimba asitumie vitu vile katika chakula chake ambavyo vinaharisha bila ya mafuta, vyenye kulevya vyenye kuleta madhara ya akili na mwili. Kwa kinyume chake, yeye lazima ale chakula na kunywa vinywaji vilivyotengenezwa kwa siagi safi, maziwa, mchele mzuri, ngano, matunda, nafaka, kunde, choroko, na mbaazi, na vitu vyenginevyo vyakuleta nguvu. Pia lazima ajihadhari na mchanganyiko wa chakula usiokubaliaana na hali ya hewa pia.

**Haki za Kuzaliwa**

Sherehe mbili zifanywe za kufuatia kanuni za dini nazo ni: (1) utakatifu wa uhakikisho wa mimba unaitwa Punsavana, katika mwezi wa nne, na (2) ya mimba inapokuwa imekua miezi minane. Baada ya uchungu na uzazi na wakati wa kujipumzisha baada ya kujifungua lazima siha itazamwe kwa vilivyo ya mama na mtoto mchanga. Kabla ya kuzaa tangawizi huchemshwa au mchanganyiko wa tangawizi - shunthipak au soubhagya shunthipak - laziwe iwe tayari. Baada ya kuzaa na mji kutoka, mama na mtoto waogeshwe kwa maji ya mfereji yenye marashi yaliyopashwa moto. Hapo tena kitovu kinakatwa lakini kwanza lazima kigungwe kwa uzi laini vrefu wa vidole vinne kutoka kwenye tumbo. Kifungwe kwa uangalifu na hata tone moja la damu lisimwagike. Hapo tena chumba cha mzazi kisafishwe na kifukizwe kwa mafusho na madawa, siagi safi vyakula zitolewe sadaka ya moto humo ndani. Baada ya maombi baba wa mtoto lazima amnuongoneze mtoto shikioni pake: Vedosi: jina lako ni Veda, na

kuandika maandishi Aum (Jina la Mungu) kwa kalamu ya dhahabu na mchanganyiko wa siagi safi na asali juu ya ulimi wake, na iache ainyonye pamoja na dawa hizi. Hapo mtoto aachiliwe mama yake amlee. Ikiwa yeye atapenda, yeye anaweza kumunyonyesha mtoto. Ikiwa mama haana maziwa ya kutosha basi, mlezi mwenye maziwa aajiriwe lakini kwanza lazima matiti yake kukaguliwa. Mama na mwanawe wahamishwe kwenye chumba hicho na kupelekwe kwenye chumba chenye hewa safi, ambapo muhanga na mafusho ya siagi kwenye moto lazima ifanywe asubuhi na jioni. Kwa muda wa siku sita mtoto atanyonya kutoka kwenye matiti ya mama yake, na mama lazima ale chakula kizuri cha namna nyingi na kitachoweza kusaidia siha yake kuwa nzuri; na kuma kupona pia tumbo la uzazi kujikunja na kurudia hali yake ya kwanza. Siku ya sita baada ya kuzaa mwanamke anaweza kuamka na kuwajiri mlezi wa kunyonyesha mtoto. Yeye apewe chakula na vinywaji vizuri na huyo mlezi anyonyeshe na kumlea mtoto. Lakini mama pia iwe anamwangalia kila mara. Namna yo yote ya dharau au kuto kumwangalia mtoto sawa sawa usiruhusiwe katika kumlea mtoto. Kufunga maziwa yasitoke kwenye matiti dawa ipakwe kwenye machuchu ambayo itayakausha bila ya kujaletea dhara yo yote. Yeye itampasa ale chakula cha kusaidia kufanya hivyo. Hapo pia ifanywe sherehe ya kupewa jina kwa mjibu na kanuni za sheria za dini, inayoitwa Sanskar Vidhi katika wakati ulio sawa. Mwanamke anapoanza kupata hedhi tena, sheria hizi hizi za utakatifu zitafuatwa na hadhari za madawa lazima zichukuliwe kuhusu kuchukua mimba na kuzaa.

Mwenye nyumba ni kama kijana ambaye anamwingilia mwanamke wakati wa kuweza kumwingilia, na anatosheka na yeye tu, na kuto kumwingilia zile siku zilizokukatazwa.

**Kupendana.**

Baraka zote na bahati huwemo daima katika jamii ambapo mwanamume ametosheka na mkewe, na mwanamke awe ametosheka na mumewe. Ubaya na hasira hutia nanga kwenye vita kati ya mwanamume na mkewe **(Manu 3,60.)**

Mwanamke asipompenda mume wake, wala hamchangamshi, yeye (mume) hatamani kumwingilia ili ajichangamshe **(Manu 3,61.)**

Ilivyokuwa furaha ya nyumba inategemea juu ya mwanamke wa nyumba, kutotosheka kwake ni sababu ya huzuni na shida kwa wote wanaohusika naye **(Manu, 3,62.)**

**Wanawake wawekwe vipi.**

Wanawake waheshimiwe na kupambwa kwa johari na mababa, makaka na kaka wa waume zao pia, ikiwa wao wanatafuta ustawi mwingi. **(Manu, 3,55.)**

Baada ya kutumukiwa elimu, wanaume wa nyumba ambayo wanawake wanahishimiwa, wanaitwa miungu na wanaishi kwa furaha nyumbani. Lakini vitendo vyao vya dini vya jamii ambazo haziwaheshimu wanawake, huwa hazina maana **(Manu 3.56.)**

Jamii ile huangamia upesi ambapo wanawake wao hawana furaha na wenye huzuni. Jamii huwa yenye furaha ya daima ambapo wanawake zao wamejaa furaha, harakati na bashasha. **(Manu, 3,57.)**

**(Manu, 3,50.)** Kwa hivyo, wanaume wenye kutaka mali lazima wawaheshimu wanawake daima na kuwatunukia johari, mavazi, vyakula na vyenginevyo kwenye sherehe na mashangirio. Lazima ifahamike akilini kuwa neno pujya maana yake ni heshima. Kila mara wao wanapokuwa na shughuli za kuonana na kuagana ikiwa ni mchana au usiku wao lazima waseme "namaste" kila mmoja amwambie mwenzake kwa mapenzi na uchangamfu.

**(Manu, 5,150.)** Mwanamke lazima awe na bashasha, mwelekevu wa kazi katika nyumba, aviangalie vilivyo vitu vyote vya nyumba, asiwe mharibifu katika matumizi, na lazima aiweke nyumba iwe safi na kwa intidhamu; i.e. achungue utunzaji wa pesa, na apike vitu vile ambavyo viwe vizuri na vyenye kuleta faida katika mwili na akili na kutoweza kupata maradhi. Yeye lazima aweke hesabu za matumizi sawa sawa. Yeye lazima utumike kwa ukamilifu nyumbani na amtume mtumishi kwa ukamilifu, na asidharau kazi za nyumba na kuziwacha ziharibike

Wanawake wazuri, namna zote za vito, elimu, ukweli, usafi, maneno mazuri; na namna zote za sanaa na viwanda, lazima vichaguliwe kutoka nchi zote na kabila zote **(Manu, 2.240.)**

**Kanuni ya Milele ya Kusema Kweli.**

Ni sheria ya zamani za kwanza ni kusema kweli daima wenye kufurahisha na wenye faida kwa wengine, lakini katu si ukweli ambawo hautafurahisha, kama kumvita mtu anayeona kwa jicho moja kama chongo. Katu usiseme uwongo kuwafurahisha wengine. Ukavu au ukhasama usiokuwa na maana na ugomvi au ubishano na mtu yo yote usiwepo. Yale yenye maana kwa wengine, japo kuwa hayakubaliana nawo, lazima yasemwe **(Manu, 4, 138, 139.)**

(Vidur Niti, Udyoga Parva, Mahabharat.) O Dhritrashtra, kuna walaghai wengi duniani ambawo daima husema yale yanayo wapendeza wengine; lakini si wengi ambawo husema au husikia yale ambayo si mazuri ya kusikilizwa lakini yana faida. Kwa sababu, ni wazi kwa watu wazuri kusema kweli mbele ya nyuso zoa, kusikiliza kwa haraka makosa yao, na daima kusifu wema wao wanapokuwa hawapo wenyewe. Ni tabia wa waovu kusema sifa zake mbele yake na maovu yake anapowapa mgongo wake. Mtu hawezi kuyawacha maovu yake na kupata uadilifu ikiwa yeye hawezi kuwaambia wenzake ila zake. Mtu yo yote asimtie aibu mwenzake au kusema mabaya ya wenzake. Sifa nzuri na mbaya yanaelezwa:-

Kutokusifu ni kutoa mfano ya sifa za wengine kama uovu, na kadhalika. Kusifu ni kuonyesha imani kuwa imani na ukosefu kuwa ukosefu. Kwa maneno mwuwafaka ni kusema uwongo kunaitwa kama mpunguo wa sifa, na kusema kweli kunaitwa sifa au maneno ya kusifu.

Watu lazima wasome na wafasiri Veda daima na falsafa, ambayo huzidisha akili, mali na hali ya jamii. Wote wanawake na wanaume lazima wafikirie Veda daima na kusomesha yale waliyoyasoma wakati wao walipokuwa wakisoma kupata elimu. 2. kwa sababu elimu ya mtu huwa nzuri zaidi na huzidi kuipenda hiyo elimu yeye anapoisoma kwa vilivyo na utaratibu wa ufasaha wa namna ile:- **(Manu 4.19, 20.)**

**Wajibu wa kazi za namna tano au Ushirika Mtakatifu.**

Namna mbili za ushirika Mtakatifu imeelezwa katika maelezo ya amri ya kwanza au uanafunzi kutaja kwa majina ni - 1. Rishi Yajna kuisoma na kuisomesha Veda na maandishi mengineyo matakatifu, kutia nia na sala, na mazoezi ya kujiwazia au Yoga: 2. Deva Yajna kuwa miongoni mwa wenye hekima, utumishi wao, utakatifu, kujipatia sifa za utakatifu, ukarimu, kuifuata elimu. Kazi mbili hizi lazima zifanywe asubuhi na jioni.

Dawa zinazotiwa kwenye moto jioni kuisafisha hewa, zinaonyesha ni za kuleta faida mpaka siku ya pili asubuhi. Na zile zinazotiwa asubuhi kwenye moto zinaonyesha ni za kuleta faida mpaka jioni tena. Atharva, K, 19, An, 7, M, 3, 4.

**(Shadvinsh, Brah, K19, Pr, 4, Kh. 5)** Kwa hivyo, tafkira za Mungu na kuabudu moto lazima ifanywe kwenya muwungano wa mchana na usiku, ni kuwa, wakati wa jua linapochomoza na jua linapotua.

Yule ambaye hafanyi wajibu wa namna hizi mbili asubuhi au jioni, lazima atengwe na watu wazuri na wale wanaoamini kuzaliwa mara mbili; haya ni kuwa, yeye ahesabike kuwa ni mtu wa tabaka ya chini au Shudra:- **(Manu, 11.103)**

Q. Kwani kuabudu huku hakufanyiwi mara tatu siku moja?

A. Hakuna mwungano wa kudumu katika mara tatu. Mwungano wa mwangaza na kiza hufanyika mara mbili tu-asubuhi na magharibi. Kwa nini yule asiyetaka kuyafikiria haya huamini katika muwonganisho wa tatu wakati wa adhuhuri, asifanye maombi yake katikati ya usiku? Kwa nini yeye ambaye huomba kati ya usiku, asiombe kila prahar, ghari, pala, na Kshana ambapo kuna mwunganisho wa wakati kama wa kati kati ya mchana. Ikiwa mtu atapenda hivyo haiwezi kufanyika. Pia, hakuna amri kutokana na maandishi matakatifu yo yote ya kuomba wakati wa adhuhuri. Kwa hivyo ni sawa kuomba na muhanga wa moto kutiwa mara mbili tu, viz, asubuhi na jioni, lakini si mara ya tatu. Mgawanyiko wa namna tatu kama huu wa wakati unafanywa tu kuonyesha sasa hivi, iliyopita na itakayokuja, lakini si katika kuabudu.

**Wajibu kwa Wazazi.**

3. Kafara ya tatu ni Pitri Yajna ambayo inayo utumishi kwa wataalamu, wenye hekima, wanafunzi, waalimu, baba, mama, na wataalamu wengine walio watu wazima, na watakatifu wanaojulikana au wale wenye nguvu ya kuona yaliyokwisha pita. Wajibu huu wa kuwatumikia wakubwa ni wa namna mbili kwa

majina ni. 1. Shraddha na, 2. Tarpana, sadaka za chakula na sadaka ya maji.

Neno Shraddha linatokana na shrat; ni jina jengine la ukweli.

Nafasi ya kutokuukubali ukweli inaitwa Shraddhaa, kitendo kinachofanyika na kutokubali kinaitwa Shraddha.

Tarpana linatokana na Sanskrit kama.

Ni kuwa cho chote kinachofanywa kuwatosheleza wazazi wanaoishi na wakubwa wenginewo au kufanya kile kinacho wafurahisha wao inaitwa Tarpana. Lakini haya yote hufanyiwa kwa wale walio hai, na si kwa waliokwisha kufa.

**Huduma za Mtazamiaji.**

Shatapatha inasema, wale walio wataalamu wanaitwa miungu wa Vedas. Wale wanaozijua Vedas nne pamoja na tafsiri na maelezo yake wanaitwa Brahma. Wao pia wanaitwa muingu ambawo ni hafifu kidogo kuliko wao. Kuwa, deva maana yake ni mtaalamu. Wake zao ambawo ni wataalamu kama wao wanaitwa Brahmani na devis au miungu wa kike. Watoto wao wanaostahiki wa kiume na jamaa zao pamoja na watumishi wao na wafuasi wao waadilifu pia wanawekwa kwenye tabaka hiyo pamoja na wao. Utumishi wa watu wote hawa unaitwa Shraaddha na Tarpana.

**Utumishi wa Wenye Hekima**

Rishi Tarpana au utumishi wa wenye hekima umo katika kuheshimu na kutosheka na waalimu ambawo ni wataalamu kama Marichi, kitukuu wa ikume wa Brahma, kwa wake zao wenye elimu kama wao wenyewe wawaelimishe watoto wa kike, watoto wao wa kiume, na wanafunzi ambawo ni sawa nawo kwa utakatifu wa tabia na watumishi wao ambawo ni waadilifu kama wao.

**Utumishi wa Wahenga**

1. Watu wajuzi wa elimu takatifu na sayansi ya mazingira wanaitwa Somasad.

2. Wale waojua sayansi ya joto, nguvu za umeme na vitu vyenginevyo, wanaitwa Agnishwat.

3.. Wale waliojaliwa na elimu nzuri na wanajishughulisha katika biashara: wanaitwa Barlishad.

4. Wale ambawo ni walinzi wa mali na hawana maradhi kwa kunywa maji wa dawa, na wanalinda mali za wenzao na kuwaponyesha wengine maradhi zao kwa kuwapa madawa waitwa Somapa.

5. Wale ambawo chakula chao hakina kinacholewesha na vitu vilivyochinjwa na kutoka na uangamizi wa maisha, wanaitwa Havirbhuj.

6. Wale ambawo ni walinza wa vitu vinavyotaka kulindwa na kujulikana, na wanaotumia siagi safi, maziwa na vingenevyo vinavyotengenezwa kwa

maziwa, wanaitwa Ajyapa.

7. Wale ambawo saa zake za kupumzika zinafurahishwa kwa kufanya uadilifu, wanaitwa Sukalin.

8. Wale waliokuwa ni wahakimu; wanaowatia adabu wahalifu na kuwalinda watu wazuri wanaitwa Yamas.

9. Yeye ambaye anapata watoto na anawapatia chakula, mavazi, na kuwalinda kwa heshima anaitwa Pita: Baba.

10. - 11. Yeye ambaye ni baba wa baba, anaitwa Pitamaha: babu; na baba wa babu anaitwa Prapitamaha: baba wa babu.

12. Yeye (mwanamke) anayewapa watoto chakula, na vinywaji na kuwalea kwa heshima, anaitwa Mata: mama.

13. - 14. Yeye (mwanamke) ambaye ni mama wa baba, anaitwa Pitamahi na mama wa babu anaitwa Prapitamahi.

15. 16. 17. Kwa vizuri, Shraaddha pia Tarpani ni utumishi wakupendana wa majamaa wa mkewe mtu na dada yake, wa jamaa wa jamii moja na wengine wote watu walio wazuri na wazee kwa mapenzi na kujitolea kwa kuwapa wao chakula kizuri, nguo, uchukuzi mzuri na mambo mengineyo kwa njia iliyo bora na nzuri ili kuwatoshelezea haja zao zote kwa ukamilifu au kwa kuwafanya vitendo vya uwema ili waridhishe akili zao na kuzisaidia siha za miili yao.

**Wajibu kwa Maumbile**

4. Wajibu wa nne ni Vaishwa Deva Yajna. Chakula kinapokuwa tayari, sehemu ya maakuli yaliyotengenezwa kwa siagi safi, na sukari lazima ichukuliwe nje kuachia nje kama ni chungu, chumvi na dawa, na kuugawanya moto na kutiwa humo, imetunukiwa na **(Manu, 3,84.)**

Mtu lazima atoe muhanga wa moto mekoni kwa cho chote kilichotengenezwa jikoni kwajili ya chakula, ili kuendeleza ustawi wa mazingira pamoja beti hizi zi fuatazo za Vedic pamoja na mafungu haya:-

Vyakula hivi vingi vinaweza kutumika kwa kumlisha mgeni ikiwa yupo, au kinaweza kupewa moto. Tena hapo sehemu ya chakula chenye chumvi na bizari ambacho ni kama, supu ya nafaka, mchele uliochemshwa, mboga zilizokwisha kupikwa, mkate na vyakula vyengine lazima vigawanywe katika sehemu 6 na kuwekwa juu ya ardhi: Inasema **(Manu, 3,92.)**

Baada ya kuweka sehemu zile za viumbe wenye yeye awape watu wenye njaa na mashaka au mbwa, kunguru na wanyama wengine. Hapa neno namah lina maana ya chakula, yaani chakula wapewe mbwa, wenye dhambi, watu wa tabaka za chini, mateketezo, wagonjwa wa matende, kunguru, funza, chungu, na wanyama wengine kama hawa wa chui. Hizi ni Sheria za Amri ya Manu kuhusu kuwalisha viumbe hawa wa chini. Hukumu ya muhanga wa moto ni kusafisha

hewa ya jikoni na kutoa kafara za dhambi zinazofanyika bila ya kujua kwa kuunganisha uangamizi wa wanyama wasioonekana.

**Wajibu wa Wageni**

5. Ushirika watano wa dini ni wajibu wa ukarimu. Mgeni au atithi, kama anavyoitwa katika Sanskrit ni mmoja ambaye siku au tarehe yake ya kufika haijulikani. Sasa ni wajibu wa mtu kumkirimu mgeni anayekuja kwake ghafla, ni mwadilifu, ni mhubiri wa ukweli, anakwenda kila pahala kuwafanyia watu mema, ni mtaalamu wakweli na mjuzi wa yasioonekana anaye usika na utakatifu au amri ya nne na ameiacha dunia, kwanza kwa kumpa yeye namna tatu za maji, padya kuosha miguu yake, argha kukoga, na achamaniya kufyonza, tena kwa kumpa yeye pahali pa kukaa kwa heshima yote kwa sababu ya cheo chake, na mwisho kwa kumtumikia yeye kwa chakula, kinywaji na maakulati mengine kwa mapenzi na ukarimu. Tena hapo yeye ayasikilize hayo mafunzo ya dini na elimu ya kidunia, yanayopendelea kupata uadilifu, mali, matakwa na uokovu. Yeye aigeuze tabia yake na desturi zake kuzielekeza na mafunzo yake ya ukweli. Wakati huo watu, wafalme, na wengineo wanatakiwa wawe na heshima ile anayoonyeshwa mgeni.

**Wanafiq.**

Lakini yeye asimhishimu hata kwa maneno huyo anyehujumu Maandishi Matakatifu (Veda) na kufanya kinyume cha mafundisho ya Veda; kama kufanya vitendo vilivyokatazwa na kuvunda kwa uwongo pia ujanja kama wa paka, na kujikunja , kujificha na kukaa kimya ili kuiangalia njia ya panya na wanyama kama huyu, huwarukia wao kuwa na kuwa meza wao; hawa ni wale walio wakaidi na ushupavu wa dini, kiburi, ujinga, hata hivyo hayuko tayari kupokea mafunzo kutoka kwa wengine; hawa ni wadanganyifu, wasemao yasiokuwa ya maana kama wale wa siku hizi wenye kufuata falsafa ya Veda au wenye kusema kama Mungu ni mmoja, "Sisi ni wenye kuweza na dunia ni ya madanganyo tu; Vedas na maandishi mengine ya dini na Mungu pia ni ya khiyalia," na kama wale wanaopayuka; haya yote ni ya udanganyifu ambayo yanasimama juu ya mguu mmoja nakumezwa kabisa, kama ilivyokuwa, katika kuabudu, lakini mara huurukia samaki kumua ili kujitosheleza mwenyewe, Mwenye tabia ya kuipenda nafsi yake tu pia inayosaidiwa na watu wenye dini za kisasa (Vairagis) anayejinyima raha za dunia (Khakis) na washupavu wengine, wapotovu, wapinzani wa Vedas. Kwa, kuhishimiwa, wao huzidi na kuwafanya watu wasiwe waadilifu. Wao wenyewe hufanya kazi zisizokuwa za heshima, huzizamisha adabu za wenzao katika bahari ya ujinga. **(Manu. 4.30.)**

**Akhlaki**

Uzuri wa wajibu tano zilizosemwa ni kuwa kufanya Brahma Yajna au wajibu kwa Mungu hukuletea elimu, akhlaki, uadilifu, ustaarabu, na baraka nyingine, kufanya Agni hotra, mafusho ya moto huadhiri usafi wa hewa, mvua, na maji, na husaidia mvua kunyesha baraka juu ya dunia. Kwa maneno mengine, kuvuta

puumzi katika hewa safi, kuishi kwa usafi, chakula safi na viinywaji safi hukuletea siha uzuri, akili, nguvu, ushujaa ambao huleta nguvu, mali matakwa na uwokovu. Inaitwa Deva Yajna au wajibu kwa kuumba vitu visivyokuwa na uhai kama inavyo safisha hewa na vitu vyenginevyo.

Wajibu kwa wakuu, au Pitri Yajna, ni dhahiri kuwa mtu anapo msaidia mama, baba, wenye hekima, mawalii, mabingwa, basi utaizidisha elimu yake, ambayo itamwezesha yeye kuweza kubagua ukweli na kuukataa uwongo. Sababu nyingine ya kufanya hivyo ni shukrani, kuwa ni sawa kuilipa utumishi wa baba na mama unawafanyia watoto wao na watoto kufanya hivyo kwa uhaba na mwalimu kumfanyia mwanafunzi wake katika kumulimisha.

Matumizi ya Balivaishwadeva Yajna au wajibu kwa viumbe visivyoonekana imeshasemwa kabla.

Hakuta kuwa na maendeleo katika nchi ikiwa hakuna wamisheni wakuzunguka (atithis). Safari zao kote nchi kuhubiri ukweli na kuusimamisha ukuaji wa ulaghai na kuwafanya watu wakae kila pahali ili wapate elimu ya kweli nyumbani. Pia, ujumbe wao huwezesha kuwepo kwa dini moja baina ya watu wote wa dunia. Bila ya msaada ya watu hawa wa dini shaka za watu katika mambo mbali mbali haziwezi kuondoshwa, na bila ya shaka kuondoshwa hapawezi kuwa na uaminifu kamili wa dini. Iko wapi furaha bila ya uaminifu?

**Kuamka Mapema**

Mtu lazima amke kwenye usiku wa manane au ni gharis ya nne ya usiku kabla ya jua kuchomoza, nenda usalani, tawadha, fikiria maisha ya kidini na ya nadilifu pia jaribu kuyatambua maradhi ya mwili, Mwombe Mungu Mweza, na katu usifanye kitendo kusicho cha halali - **(Manu, 4,92.)**

**Insafu ya Kulipiza Kisasi.**

Kwa sababu insafu iliyofanywa haiwezi kuwa haina maana; lakini haileti athari yo yote inapofanyika. Kwa hivyo mjinga haogopi kufanya dhambi. Lakini uwe na hakika kuwa kutokuwa mwadilifu huendelea kukata mizizi yako ya furaha pole pole **(Manu, 4,172.)** Mpango wake wa kazi unaendelea kama ifuatavyo, **(Manu, 4,174.)**

Mtu dhalimu anayepita mipaka ya uadilifu, kwanza huwa tajiri kama tanki la maji, ambalo maji yake yanamwenea kote tanki linapopasuka kwa kuwaibia watu wengine mali zao kwa uwongo, madanganyo, ulaghai, yaani, kuipinga Veda; kuuhifadhi, uadilifu, hadaa na udhalimu mwingine; tena hapo yeye hupata utajiri, mali, chakula, kinywaji, mavazi, magari, cheo, heshima, maongozi; siyo yeye huwatisha adui zake kwa udhalimu; lakini mwishoni huangamia kwa natija za udhalimu wake kama mti uliokatwa mizizi.

**Mazoezi ya Ukweli**

**(Manu, 4,175.)** Wacha mtu mtaalamu, anayeifuata dini ya kweli

ilisomeshwa na Vedas, ambapo mtu lazima ajiepushe na mchanganyiko wa mabaya na mazuri na aukubali ukweli na kuukataa uwongo, na kipi ni cha haki, na kuishi kwa njia ya ukweli na ya sheria, Somesha wanafunzi wake kwa adabu na haki.

**Amani na Watu kumi na Tatu.**

**(Manu, 4, 180.)** Wacha mtu ye yote asipinge, gombana au bishana na mwenye kujinyima au kasisi, pamoja na mwalimu au mfunzi mwenye tabia nzuri, pamoja na mkufunzi, pamoja na mjomba, pamoja na mgeni ambaye siku yake ya kufika au kuondoka hazi julikani pamoja na wanaokutegemea, pamoja na mtoto, pamoja na mzee, pamoja na mgonjwa, pamoja na daktari au mtaalamu wa Ayurveda, pamoja na majamaa au watu wa kabila moja, pamoja na mkwe (baba wa mume) na majamaa wengine, pamoja na rafiki, pamoja na mama, pamoja na baba, pamoja na dada, pamoja kaka, pamoja na mke, pamoja na mtoto wa kike na pamoja na watumishi.

**Watu Waovu Watatu**

**(Manu, 4, 190.)** Namna tatu za watu huzama katika bahari ya huzuni kutokana na vitendo vyao viovu kama mashua ya mawe inapotiwa baharini, viz, (1) Wale ambawo hawana utakatifu, ukweli na vitendo vyengine vyenye bidii, (2) wale ambawo hawana elimu (3) wale ambawo ni wapokeaji wakubwa wa zawadi kutoka kwa wenzao kwa jina la dini. Si kama wao wanazama katika bahari ya huzuni lakini wanawazamisha na wale wanaotoa hizo zawadi pia pamoja nawo.

Utoaji wa mali iliyopatikana kwa haki kwa hawo watatu waliotajwa humwangamiza mtoaji katika maisha yake na mpokeaji katika dunia nyingine. **(Manu, 4, 193.)** ikiwa kuna watu wa namna hiyo, wamekaaje hawo watu?

**(Manu, 4,194.)** Kama yeye, anayetaka kuvuka kwenye maji marefu katika mashua ya mawe, huzama mpaka chini, basi wale watu wawili wajinga, mtoaji na mpokeaji, wote huenda chini kwenye majimbo ya adhabu.

**Alama za Unafiki**

**(Manu, 4, 195.)** Mtu huyo ahisabiwe kuwa jambazi na mtu duni kabisa kama paka ambaye hafanyi kitendo cha uadilifu, lakini anawadanganya watu kwa jina la dini, ambaye mwenye tamaa ya uchu au uchoyo, ambaye ni mlaghai, anayejidai kwa ukubwa wake mbele ya watu wa kawaida, ambaye ni muaji wa wanyama na mchukiaji wa binadamu, ambaye ana kuwa na usuhuba mzuri na mbaya.

**(Manu 4, 196.)** Mtu huyo afikirie kuwa mtu wa chini kama korongo, ambaye ni mnyamuvu kupata umashhuri; ambaye yuko tayari kulipa kisasa cha kifo kwa mtu yo yote ambaye anaye msingizia kupotea kwa senti mbili; yeye ambaye ni jambazi wa kutosha kujisaidia mwenyewe ikiwa ni kwa hila, dhuluma, au kwa uhadaa; yeye ambaye hashindwi kwa ushupavu wa dini hata ikiwa ni wa upande usio wa kweli; na yeye ambaye anaudhuru uungwana, kutosheka, na ucha Mungu wa kudhihirisha tu. Watu kama hawa wenye sifa hizi zilizotajwa, ni wanafiki wa dhahiri. Wao wasiaminiwe kabisa au kufanyiwa wema.

**Tharura za Kupata Uadilifu**

Wanaume na wanawake lazima wa kuuze uadilifu wao pole pole kwa ajili ya furaha ya dunia nyingine au baada ya maisha kwa kutompa maumivu kiumbe cho chote kama mchwa anavyoijenga nyumba yake pole pole **(Manu, 4, 238.)**

Kwa sababu, katika safari ya kwenda dunia ya pili hawezi mama, baba, mtoto wa kiume, au hata jamaa wa kabila moja atakayeweza kumsaidia; lakini uadilifu tu peke yake utakuwa mwenzake, rafiki na msaidizi huko ndani. **(Manu, 4, 239.)**

Tazama, roho inazaliwa peke yake na hupata adhabu ya mauti. Peke yake hula matunda ya uadilifu ambayo ni furaha na ufisadi ni mateso **(Manu 4, 240.)**

Lazima ifahamike akilini kwamba mmoja katika jamii huleta kitu kwa kufanya dhambi, na jamii nzima hukila hicho kitu. Mfanyaji wa dhambi peke yake tu hupata adhabu ya kitendo chake, lakini si waliokula naye - Mahabharat, Prajagar, **(Ch. 33, 42.)**

Mtu anapokufa, jamaa zake huacha mzoga wake juu ya ardhi kama donge la udongo na humgeuzia mgogo na kwenda zao nyumbani. Mtu hata mmoja haendi naye lakini uadilifu peke yake tu unamfuata kwenda dunia ya pili. **(Manu, 4, 241.)**

**(Manu, 4, 242.)** Kwa hivyo mtu lazima aanze kutia nguzo za mali ya uadilifu kila siku ili kumsaidia katika maisha ya sasa na kujipatia heri katika maisha ya mbele katika dunia ya pili; kwa sababu, kwa msaada wa uadilifu mtu ataweza kuipita njia ya shida, au ni shida sana kuweza kuipita.

**(Manu, 4, 243)** Pia kwa mtu ambaye dini ni muhimu, na anaye hifadhika na kufanya dhambi katika siku za mbele kwa kuwa mwadilifu, mara moja kwa uwezo wa uadilifu humpata Mungu ambaye umbo lake ni kama mwangaza na mwili wake kama mbingu, ni kama kusema.

Kwa hivyo mtu anayefanya bidii daima, moyo - wenye huruma, mwenye akili zilizotulia, mwenye kujiepusha na watu wahalifu, ukatili, na mtu mwovu na yule aliye mwadilifu, hupata raha kwa kuweza kujimiliki mwenyewe na kwa kufanya zawadi ya elimu na baraka kwa wengine. **(Manu, 4, 246.)**

Lakini lazima ifahamike akilini kuwa yeye anayeiba na dhambi nyingine zote, yeye anayesema, uwongo au anayeuzuia ukweli, ambayo inahakikisha na hufikiria mambo yote, ambayo ni mzizi wao mkuu, na ambawo unachukua na kufanya kazi zote. **(Manu, 4, 256.)**

**(Manu, 4, 156.)** Kwa hivyo mtu lazima auache uwongo na ufisadi mwingine, ajaribu kupata maisha ya ukamilifu kwa kuweka kiapo cha utakatifu na kwa kuzituliza akili, na kujizoeza kuwa na nguvu, ambazo zitampa watoto wazuri kabisa na mali zisizooza. Mtu lazima ajiweke kama mwenye kutunza nguvu zake na kujiepusha na mazoezi maovu katika maisha yake.

Mtu mwovu huzama kwenye dharau baina ya watu wazuri katika dunia, hupata sehemu kubwa ya mashaka, daima huzongwa na maradhi, na hawezi kuishi sana. **(Manu, 4, 257)** Hata hivyo, mtu lazima ajaribu kuishi kwa mujibu wa sheria.

**Raha na Maumivu.**

**(Manu, 4, 159.)** Kitendo cho chote hutegemea juu ya mtu mwingine, kitendo hicho humfanya yeye aepuke kwa uangalifu, lakini cho chote kinamtegemea yeye, na kwa hayo yeye lazima ayazingatie kwa bidii.

**(Manu, 4, 160.)** Kwa yote yale yanayo mtegemea mwingine huleta maumivu; na yote yanategemea juu yake, wache yeye ajue kwa maneno machache iwe ufupisho wa raha na Maumivu.

**Mume na Mke**

Laki cho chote kile kinategemea juu ya mwingine, lazima kifanywe kwa kutegemeana; kwa mfano, kazi ya mwanamume na mke katika nyumba hutegemea juu ya hawa wawili. Wao lazima watende kwa mujibu wa masikilizano katika amani ya daima, mwanamume anayemfurahisha mkewe, na mwanamke anaye mfurahisha mumewe. Wao katu wasigombane, au kuvunja kiapo cha ndoa. Mwanamke lazima afanye kazi za nyumbani kwa kumtii mumewe. Kazi za nje ziwe ni za mwanamume. Wao wajaribu kuhifadhiana ili wasijekuangukia tabia mbaya. Hii iwe sheria ya mtu na mkewe. Ndoa inapofungwa, mtu na mkewe huwa, kama walivyokuwa, wameuzwa kila mmoja kwa mwenzake, haya ni kusema cho chote kile kilichopo katika miili yao kutoka kichwa mpaka miguu, ikiwa ni ishara, ubembelezi au nguvu na yote kama viungo vya umbo, ni vyao kwa umoja. Wao katu wasifanye kitendo cho chote bila ya kukubaliana. Vitendo vya kuvunja moyo zaidi ni uasherati, umalaya, ukahaba na dhambi nyinginezo kama hizi. Hata fikira za mbali kabisa za vitendo hivi visifikiriwe akilini. Mtu lazima atosheke na mke wake, na mwaname kwa mumewe.

**Wajibu wa Ma-Brahmin Katika Maisha.**

Ikiwa wao ni Brahmins, mwanamume lazima awasomeshe watoto wakiume, na mkewe mwenye elimu, awasomeshe watoto wa kike. Wao wawafanye wanafunzi wao kuwa wataalamu na wenye ujuzi mwingi kwa nasaha na hutoba zao. Mwanamke lazima aheshimiwe kama malaika na mumewe, na mume pia aheshimiwe na mkewe vile vile. Kwa muda wote ule wao wako katika mazaoezi katika Gurukul au skuli, wao wamheshimu mwalimu wao kama baba na mama. Waalimu pia lazima wawatendee wanafunzi wao kama watoto wao wenyewe.

**Shahada za Mwalimu wa kiume na Kike.**

1. Pandit au mtu mwenye hekima ni yule mwenye elimu ya nafsi yake; ambaye amejishughulisha na kazi muwafaka, kama kuwa, yeye ni mtu wa maana daima na si mlegevu, yeye haathiriki kwa raha na maumivu, faida na hasara, sifa

na kutokupata sifa; ambaye ni thabiti daima katika mazoezi ya uadilifu, na ambaye akili yake haivutiki kwa kuona vitu vizuri ambavyo hupendeza akilini

2. Ni wajibu wa lazima wa mtu mwenye busara kuzifanya kazi za uadilifu, si kufanya maovu, asijisogeze mbali kutoka kwa Mungu, Veda, mazoezi ya kweli, na kuwa na uaminifu thabiti katika Mungu na dini.

3. Ishara ya, kwanza ya mtu mwenye busara ni ile ambayo inamwezesha kufahamu jambo gumu kwa urahisi na upesi; kuwa yeye amesoma, amesikia maelezo yake, na ameyafikiria maandishi ya kidini kwa muda mrefu; kuwa yeye anajitolea kufundisha wenzake kile anacho kijua yeye ili wenzake wafaulu, kuwa yeye hafanyi jambo lo lote lenye kumletea faida yeye peke yake; na yeye hatoi maoni yake katika mambo ya wengine bila ya kuulizwa na bila ya ujuzi wa saa iliyo sawa.

4. Mtu mwenye busara na mtaalamu ni yule ambaye hataki kupata faida ya bure, ambaye hasikitiki akipata hasara ya kitu, na ambaye hakereki wala hahuzuniki katika wakati wa dhiki.

5. Mtu mwenye busara ni yule ambaye ni bingwa katika mipango yote ya elimu na udadisi, yeye ambaye anaweza kufasiri maudhui ya maandishi matakatifu kwa hekima, na yeye ambaye anaweza kueleza maana ya kweli ya elimu na sheria na kitabu chenye muhtasari wake bila ya shida.

6. Mtu lazima aitwe pandit au mwenye busara, ambaye ufahamu wake uko katika hali kuafikiana na fikira za kweli ya maandishi ya dini, ambaye ujuzi wake unafanana na amri za hoja, na ambaye haharibu tabia na adabu za watu waadilifu, wanaoitwa Aryas (bora) katika Sanskrit.

Po pote pale penye watu kama hawa, wote wanaume kwa wanawake, kusomesha maendelezo ya elimu, dini na uadilifu hawajua mwisho wake; na inaleta raha ya kuendelea ya maisha kote mjini.

Beti hizi zote 6 zilizotolewa kutokana na Vidur Prajagar ya Udyoga Parva ya Mahabharat sura ya 33.

**Alama za watu wasiofaa na wajinga.**

**(Vidur Prajagar ya St. Vidur, Udyoga Parva, Mahabharat, chap. 33.)** Wao wanakusudia: 1. Watu wenye busara huwaita mpumbavu, yeye ambaye hajasoma wala hajasikia kufanuliwa kwa kitabu au maandishi yo yote, yeye ambaye anajiona, yeye japokuwa ni maskini, hufanya maazimio makubwa, na yeye ambaye bila ya kutia mkono wake kwenye kazi yo yote, kufikiria kujipatia hazina za mali. 2. Yeye ni mjinga na anahesabika kuwa ni mbaya miongoni mwa watu, yeye huingia kwenye watu au majumbani mwao bila ya ruhusa au kualikwa, kutaka kujiweka juu kila pahali, husema sana kwenye watu bila ya kuombwa kufanya hivyo, na huamini katika, jambo lisilo sadikika au mtu asiye sadikika.

Nchi yenye watu kama hawa wanaofanya kazi ya ualimu na wahubiri,

wafundishaji na watukufu, mara hufunikwa na kiza cha ujinga, na huhujamiwa na hofu ya dhulma, ushenzi, ugomvi, chuki, hupasuka na chembe, kuzidi huku huleta adhabu ya umasikini.

**(Vidurprajagar. ch. 40.)** Zina maana: Makosa saba ya wanafunzi ni uvivu, ulezi, ya dunia au kujiambatanisha na vitu vya dunia, kujifanya kigugu au kusema mengi, kutoa au kusikiliza hadithi za uwongo, kutotulia au ulegevu katika masomo, majivuno na kujipendelea nafsi yake tu. Wanafunzi kama hawa hawezi kufuzu katika kujipatia elimu.

Vipi mtu mwenye tamaa ya raha, ataweza kupata baraka za elimu? Iko wapi raha ya mtu ambaye amejitolea kuipata elimu? Kwa hivyo mpenda raha awache tamaa ya kupata elimu, na mwanafunzi lazima aiondoshe fikira hiyo akilini mwake raha za akili. Hakuna njia nyingine ya kupata elimu.

**Nguvu ya kupata Elimu.**

Wao peke yao ni vijana wa kweli na huwa wenye elimu, ambawo wanajiwekea heshima za kweli, na wanaweza kuzizuia akili zao, na hawajapata kupoteza udume wao au manii. Kwa hivyo mabwana na mabibi lazima wawe na sifa kubwa. Mabwana lazima wachukue hadhari zile ambazo zitawafanya wanafunzi wao wazoe ukweli, adabu, wajiheshimu, mazoezi ya ukweli, uungwana, kuweza kuzizuia akili zao, utu na sifa nyingine nzuri; na kuwasaidia kuijenga miili yao na nguvu zao za dini kuwa madhubuti na kuwa wataalamu mashuhuri katika Veda zote na maelezo yao mengine. Wao lazima wawe hadhir kuwaziwia wanafunzi wao kuegemea tabia mbaya na kuwafundisha wao kwa bidii na uangalifu.

Wanafunzi lazima wawe wenye adabu, watulivu, wenye heshima kwa waalimu wao na wanafunzi wenzao, wenye fikra nzuri, wenye jitihada. na kufanya kazi kwa bidii ili wajipatie elimu, kubaleghe na kujipatia sehemu yao hima na moyo wa kuwa waadilifu. Hizi ndizo sifa na wajibu wa Brahmins.

**Wajibu wa Kshatriyas**

Wajibu wa wale wenye tabaka la kijeshi utaelezwa katika sura inayoeleza wajibu wa ufalme.

**Wajibu wa Vaishyas.**

Wajibu wa tabaka la wafanyi biashara ni kujifundisha lugha za nchi mbali mbali, namna mbali mbali za biashara, usafirishaji, bei, hadhari; wingi wa vitu na mahitaji ya vitu; kwenda nchi za kigeni, kuanza kazi zenye faida; kuchunga ngombe; kuendeleza ufugaji, viwanda na sanaa; kuzidisha utajiri wa nchi kutumia pesa kuendeleza elimu na dini; kuwa ukweli, mwaminifu, kuwa mwadilifu katika biashara; na kuvitunza vitu vyote ili visije kupotea bure.

**Wajibu wa Shudras.**

Wajibu wa mfanya kazi au watu wa tabaka la chini wawepo nyumbani

kufanya kazi za namna zote, wawe mafundi wa sanaa ya mapishi, kuwatumikia na kuwasaidia watu wa tabaka lile walilozaliwa tena, na kujipatia maisha yao kutoka na mikono yao. Watu wa tabaka hili wawapatie wasaidizi hawa chakula, kinywaji, nguo, pakukaa, na kila kile kinacho hitajika katika harusi zao au kuwapatia chakula kutokana na malipo yao ya mwezi.

Tabaka nne hizi ziishi kwa usalama, kwa kufahamiana, wawe marafiki, na wawepo pamoja kwenye raha na kwenye shida zao, faida na hasara pia. Wao pia wajishughulishe kwe mali na akili kisaidia serekali na watu pia.

**Makosa ya Mume na Mke.**

Mtu na mkewe katu wasitengane.

Kunywa pombe, kujishirikisha na wahalifu, kujikimbiza na mume, kusafiri kwenda ngambo kwa kutoa sababu ya kwenda kutoa heshima kwa mashekhe wa uwongo, kulala na kuishi katika nyumba ya mtu mwingine ni makosa sita ambayo humletea aibu mwanamke aliye olewa. Pia pana makosa ya wanaume **(Manu, 9, 13.)**

Kutengana kwa mume na mke ni wa namna mbili; Kwenda kufanya biashara nchi nyingine. 2. Kufa. Dawa ya mtengemano wa kwanza ni mtu lazima aende na mkewe aendapo nchi nyingine kufanya biashara. Hasa ni kusema mtengamano wao usiwe wa muda mrefu.

**Koa Tena.**

Q. Wanaume na wanawake lazima wafunge ndoa mara nyingi?

A. Si mara moja na wakati mmoja i.e. katika urefu wa maisha yote.

Q. Lazima ziwepo ndoa nyingi wakati mbali mbali?

A. Ndiyo; kwa mfano, **(Manu, 9, 178.)**

Wanaume na Wanawake ambawo ndoa yao ilifanywa tu, lakini hawajaonana kimwili, i.e. wanawake kuwa bikira na wanaume hawajua mambo ya uchu, lazima waoe tena. Wanaume na wanawake wa tabaka ya kisisi, jeshi na wafanyi biashara, ambawe wameonana kimwili basi lazima wasioe tena baada ya kifo cha mwenzi wake.

Q. Kuna ubaya gani kufunga ndoa tena?

A. 1. Kutakuwa na mapenzi haba baina ya mume na mke: kwa sababu watawacha wenzi wao wanapopenda na kuanza kushirikiana na wengine 2. Wanapooa baada ya kifo cha wenzi wao, wao watachukua mali za wakwe zao, na jamii zao wataanza na ukhasama pamoja 3. Jamii nyingi zenye ukoo mzuri zitaangamia na kuharibika kabisa, na mali zao zinatapotea na upepo. 4. Uadilifu wa utakatifu wa wanawake na wanaume utaangamizwa. Haya na mengine kama haya ni mabaya yanayofuatana kufunga ndoa tena au uwingi wa ndoa. Hata hivyo haya yasifuatwe na tabaka ya kuzaliwa tena au tabaka ya juu.

omo wa tabaka pia utaangamiza jamii. Wanaume na wanawake ;ukia zinaa na ufisadi mwingine, na watatoa mimba na dhambi nyingine Hata hivyo ni bora wao waoe tena.

hata. Ikiwa wanaume na wanawake watapendelea kuishi maisha ya u hapata kuwa na uhalifu. Kuendelea na utakatifu wao mambo ;ita kuwa ya manufaa, wao wanaweza kuchukua mtoto wa kiume wa ao kulea, ikiwa watapenda kufanya hivyo. Itazuia watu kuzini. Ikiwa wao zi kuweka utukufu wao, wao wanaweza kupata watoto kwa ndoa ya (muungano wa muda maalum wa ndoa).

ıi tafauti baina ya - kuoa tena na niyoga?

ma katika ndoa, bi harusi huacha paa la wazazi wake na kuishi katika ya bwana harusi, na kuwa hana hasa uhusiano na baba yake, basi katika njane huishi katika nyumba ya bwana wake aliyekwisha kufa. 2. Watoto ı kiume hurithi mali ya bwana wake aliyekwisha kufa. Wao hawahesabiki watoto wa kiume mume wa mama yao, wala wao hawawezi kushika jina kuwa la jamii yake. Wala yeye hatakuwa na uwezo wo wote juu yao. vao watajulikana kama ni watoto wa mume wa mama yao aliyekufa, na ıtika jamii hiyo, na mali zao wao watarithi, na hiishi katika nyumba hiyo. ıume na wanawake waliooana wao lazima watasaidiana, lakini wanaume awake waliоungana kwa niyoga kwao si lazima kufanya hivyo. 4. ıno wa wanaume na wanawake waliooana ni wa daima mpaka kufa kwao; ale walioungana kwa niyoga, huvunjika huo mwungano baada ya wao upata watoto. 5. Wanaume na wanawake waliofunga ndoa hufanya kazi ıyumba pamoja kwa sababu ya kuwa na nyumba hiyo moja tu; lakini ıe na wanawake walioungana kwa niyoga hufanya kazi zao nyumba zao ıbali.

əria za ndoa na niyoga ni sawa, au mbali mbali?

na tafauti kidogo: Tafauti kidogo zimeshaelezwa hapa juu. Na nyingine ıaume na wanawake wanaoungana kwa ndoa wanaweza kupata watoto ıi katika mwungano wa niyoga wanaweza kupata watoto 4 tu, na si zaidi. ıkdi hufungwa ya vijana na wanawari, basi hata katika niyoga akdi va ya mjane wa kike na kiume. Kijana na mwanamwari hawawezi na kwa niyoga. Si kama watu wawili wanaoishi kwa pamoja daima, nume na mwanamke walioungana kwa niyoga hawaishi pamoja. Wao ane isipokuwa wakati wa mwanamke anapo weza kushika mimba. Ikiwa nke anafunga akdi ya niyoga kwa faida yake, yeye atengane na nume wake wakati wa mimba yake ya pili. Ikiwa mwanamume anafunga niyoga kwa faida yake mwenyewe basi mwungano wake pia uvunjike ıimba ya pili pia. Lakini mwanamke huyo huyo awalee watoto kwa muda ka miwili au mitatu na kisha atamrudishia mwanamume hawo watoto.

Kwa hivyo, mjane mwanamke anaweza kuwalea watoto wawili wa mwanamume na watoto wawili kwa kila mwanamume aliyeungana naye kwa niyoga. Pia mjane wa kiume anaweza kuwalea watoto wawili wake na wawili wa kila wajane 4. Kwa hivyo, watoto kumi wanaweza kupatikana kwa mwungano wa watu wawili, kama Veda inavyopendelea. **(Vide. Rig. X. 85. 45.)**

Ina maana: Ewe mtu, uliobarikiwa kwa mali na nguvu za kuweza kupata watoto, mfanye mwanamke huyu aliyeolewa awe na furaha au mjane huyu wa kike awe na furaha na awe na watoto wazuri. Pata watoto 10 kutoka kwa mwanamke huyu aliyeolewa na mhesabu kuwa kama mtu wa kumi na moja wa jamii hii. Ewe mwanamke, wewe pia, lazima uzae watoto kumi kwa mwanamume aliyeoa au wa niyoga na mhisabu yeye kuwa ni mtu wa kumi na moja wa jamii. Kwa mujibu wa ubeti wa Veda, mwanamume na wanawake wa takatifu wa jeshi na pia wa tabaka za wafanya biashara katu wasipate zaidi ya watoto 10; kwa sababu, uwingi wa watoto, huonyesha udhaifu wa miili yao; kutofahamu haraka, maisha mafupi; na pia baba na mama wa watoto hawa pia huwa wadhaifu, hawaishi sana, na huweza kupata maradhi, na kupata taabu nyingi katika maisha ya uzee.

Q. Huu mwungano wa niyoga ni kama kuzini.

A. Mwungano wa mwanamume na wanawake waliyekuwa hawajaona unaitwa zinaa, pia ikiwa mwanamume na wanawake wanaoungana bila ya niyoga pia ni zinaa. Kwa hivyo, inaonyesha dhahiri kuwa si zinaa ikiwa ndoa imefungwa basi pia ikiwa akdi ya niyoga imefungwa kama inavyotakika basi pia si zinaa. Kama ilivyokuwa si zinaa, dhambi au aibu katika mwungano wa wanaume na wanawake wanapooana kwa mujibu wa sheria za kidini, kwa hivyo pia isifikiriwe kuwa si zinaa, dhambi au aibu katika mwungano wa niyoga ikiwa umefanywa kwa mujibu wa sheria za Veda na maandishi matakatifu.

Q. Ni kweli. Lakini inaonyesha kama ni vituko vya malaya.

A. La; kwa sababu kumwingilia malaya huwa haina idhani sheria za dini za kumteua mwanamume. Lakini sherehe za niyoga inaungwa mkono na sheria kama ya ndoa. Pasiwe na aibu katika kuingiliana kimwili kwa mwanamume na mwanamke walio unganishwa kwa niyoga kama inafungwa ndoa ya harusi. Wanao zini wanaume na wanawake watengane navyo vitendo vya kihalifu.

Q. Sisi tunaona dhambi katika mafundisho ya niyoga.

A. Kwa nini hamwoni dhambi katika ndoa, ikiwa mnaiona katika desturi za niyoga? Kwa hakika ni dhambi kuzizuia sherehe za niyoga. Kwa sababu, kwa mujibu wa sheria za tabia katika maumbile ya Mungu, mvutano baina ya wanaume na wanawake hauwezi kuzuilika ila kwa watu wale walio kubali kujitolea kuyawacha ya dunia, ambawo ni wataalamu, na ni wafuasi wa yogis. Kwani wewe huoni kama ni dhambi kutoa mimba, kuangamiza mtoto aliyekuwa tumboni mwa mama yake na masha ya wajane wa kike na kiume? Kwa sababu,

ikiwa wao wangali vijana, wao lazima watapendelea kupata watoto na kufurahia mambo ya uchu; lakini ikiwa haya yatazuiliwa na serekali au na tabaka zao, basi wao watafanya vitendo viovu na vya dhambi kwa siri. Njia iliyopo ya kuzuia umalaya na zinaa na uovu ni ile tu ya kujizuia na tamaa za uchu, la kukataa mwungano - kufunga ndoa tena au niyoga. Ikiwa itawezekana, basi ni vyema na uzuri. Lakini ikiwa hapatakuwa na watu wenye hima za utakatifu, basi wao waoane tena na kuruhusiwa kufunga akdi ya niyoga wakati ule unaotakikana. Tena hapa itawezekana kuuangamiza umalaya na kuweza kupatikana utu kwa njia iliyo sawa ya mapenzi na kuzaliwa kwa watoto walio wazuri. Itakomesha kabisa na kuleta mwisho wa dhambi za kutoa mimba. Zinaa ipo baina ya wanaume wa tabaka la chini na wanawake wa tabaka la juu, na umalaya wa makahaba na wanawake waliokuwa hawana maana kwa kuwaharibu wanaume wazuri, uharibifu wa jamii za watu wa juu, kuusimamisha uadilifu, mashaka ya wanaume na wanawake, utoaji wa mimba na dhambi nyingine kama hizi huondoshwa kwa kuwepo kwa ndoa na niyoga. Kwa hivyo kuwepo kwa niyoga kupendelewe.

Q. Sherehe gani ziwepo katika akdi ya niyoga?

A. Sherehe za niyoga ziwe kama za ndoa. Kama harusi, mwungano wa niyoga lazima ubarikiwe na kukubaliwa na watu wazuri na jamii zote mbili pia. Kwa mfano, mwanamume na mwanamke wanapotaka kuungana kwa niyoga, wao lazima waweke ahadi hiyo mbele ya jamii zao kuwa wao wanafunga akdi ya niyoga, kwa sababu ya kuzaa watoto, na wao watatengane baada ya kumaliza kazi hiyo.

Ikiwa wao bado wataendelea mwungano baada ya hapo basi wahesabiwe wenye dhambi na wanaweza kutiwa adabu na watu wao au na serekali. Wao waonane mwezi mara moja ili wapate watoto. Baada ya kushika mimba wao wataishi miaka yao mbali mbali.

Q. Niyoga lazima ifanywe katika kabila yake mwenyewe au baina ya watu wa tabaka mbali mbali?

A. Mwanamke lazima aingiane katika niyoga hasa na mtu wa tabaka lake, au aliyekuwa mtukufu zaidi kuliko yeye; kwa mfano, mwanamke wa tabaka ya wafanyi biashara afanye akdi ya niyoga mwanamume wa tabaka la mfanyi biashara, jeshi au tabaka la wakasisi; mwanamke wa tabaka la kijeshi, na mwanamume wa tabaka hiyo hiyo kama yeye mwenyewe au wa tabaka la wakasisi; mwanamke wa tabaka la Ki-Brahmana, mwanamume wa tabaka la Ki-Brahmana. Sababu hasa ni kuwa uzazi lazima uwe wa wanawake wa tabaka lile lile au wa tabaka la juu zaidi, lakini si kwa tabaka lililo chini zaidi ya tabaka lake. Sababu hasa ya kuwaumba wanaume na wanawake ni kueneza kabila au aina za watu walioungana katika ndoa au niyoga kwa mpango unaotueleza dini au mafundisho ya Vedas.

Q. Nini dharura ya niyoga kwa ajili ya mwanamume, kwa sababu yeye anaweza kuoa tena?

A. Sisi tumeshaeleza kuwa wanaume na wanawake wa tabaka la walilozaliwa tena wanaruhusiwa na Vedas na maandishi mengine matakatifu kuoa lakini mara moja, na si mara mbili. Ndoa ya vijana na wanawari inafungwa kwa haki, lakini si haki au uadilifu ndoa iliyofungwa baina ya mjane wa kike na kijana aliyekuwa hajaoa, au ndoa baina ya mwanamwari na mjane wa kiume. Mwanamwari hataki kuolewa na mjane wa kiume basi hata kijana naye hataki kumwoa mjane wa kike. Mwanamwari hamtaki mtu aliyekwisha kuoa kuwa mume wake, wala kijana hamtaki mwanamke aliyekwisha kuolewa, wanaume na wanawake itawabidi waungane kwa niyoga. Ni sawa kuwa wale waliiofanana ndiyo wanaooana kama kwa mifano iliyokwisha kuelezwa hapa juu.

Q. Jee kuna maamrisho ya Vedas kwa akdi ya Niyoga kama yaliyopo ya ndoa?

**Vedas na Niyoga.**

A. Kuna maamrisho mengi kuhusu Niyoga. Tazama hapa na yasikilize. Inasema Rig. Veda, Mandala X, Sukta 40 na Mantra.

Ashwina: Ewe mwanamume na mwanamke, vidhaveda: Kama ni mjane wa kike: Akrinute: huzaa watoto kwa vizuri, devaran: kwa mume wake wa pili na, yosha: mwanamke aliyeolewa, maryam: Kwa mume wake, sadhasthe: kwa kulala na yeye katika kitanda kimoja napahali pa moja, basi wewe pia ufanye hivyo. Ulipata wapi vitu vyako - bhipitwam karatah: na katika wakati gani, kuhoshatuh? Wewe unaishi wapi? Pako wapi pahali papo pa kulala, - ko vam shayutra? Wewe ni nani na ipi ni nchi yako?

Q. Ikiwa mtu hana ndugu mdogo wa kiume basi mjane wake atafunga akdi ya niyoga na nani?

A. Na mume wake wa pili, anaitwa devara. Lakini neno devara halina maana hiyo wewe unayo amini kuwa. Tazama, Nirukta inasema nini kuhusu haya.

**Devara.**

Devara ni yule ambaye ni mume wa pili wa mjane; ikiwa yeye ni ndugu yake mdogo mumewe, au yeye ni wataka ile ile aliyo huyu mjane, au wa tabaka la juu. Kwa ufupi, devara ni yule ambaye yeye anajiunganisha kwa akdi ya niyoga.

**(Rig. 10, 18, 8.)** Ewe mwanamke mjane, kata tamaa zote za mume wako aliyekufa tafuta na mchukue mume mwingine baina ya wanaume wanaoishi na yatie akilini na ifuate sheria, ikiwa mwungano wa niyoga umefanywa kwa faida ya kumwoa tena mwanamume, mtoto anyezaliwa katika mwungano wa niyoga atakuwa yeye, na ikiwa uhusiano wa niyoga umefanyika kwa faida yako wewe, mtoto atakuwa wako. Hata hivyo amini katika sheria hii, na mwache mwanamume anayeikubali niyoga afungamane nayo.

**(Atharva 14.2.18.)** Ewe mwanamke, ambaye hampi taabu mumewe na mume wa pili, anayejinadhifisha kuwa na huruma kwa nyumbani: wanyama, mfuasi na mtii kwa sheria za dini, kujaliwa na uzuri na elimu, kubarikiwa na watoto wanaume wazuri, wajukuu wakiume na majamaa wengine, mama wa watoto wa kiume walio shujaa na werevu, wanaelekezana na mume wa pili, na mtumishi wa raha kwa mume au mume wa pili.

**Manu juu ya Niyoga.**

Yeye anasema, **(9,69.)** Ikiwa mwanamke bila ya kumjua mume wake huwa mjane, ndugu mdogo wa mumewe aliyekufa anaweza kumuoa.

Q. Mara ngapi mwanamume au mwanamke anaweza kufanya akdi ya niyoga?

Pia, majina gani hupewa waume wa mwanamke aliowapata kwa niyoga?

**(Rig X, 85,40.)** Ewe mwanamke, jina la kwanza: mume, aliyekuoa wewe, ni 'soma' kwa ulainifu wake na sifa nyinginezo, zile za mume wa pili uliyempata kwa niyoga ni 'gandharva' kwa kuwa yeye amemjua mke mmoja tu, na yule mume watatu uthara: baada ya haya mawili ni 'agni' kwa uadilifu wa joto la mapenzi, na waume waliobakia yako kutokana na turiya kutoka wa nne mpaka wa kumi na moja uliowapata kwa niyoga kuendelea kwa majina ya wanaume 'manushyaja'. Kwa mfano, kwa mijibu wa ubeti, Rig. X, 85, 45, mwanamke anaweza kuwa na waume moja baada ya moja mpaka wawe kumi na moja kwa njia ya niyoga.

Q. Kwa nini sisi tusichukue neno 'ekadasha' kuleta maana ya watoto wanaume kumi na wakumi na moja kuwa mume wa mwanamke?

A. Ikiwa wewe utafasiri ubeti wa eda hivyo, basi kutatokea mapinzano.

Pia mwanamke hawezi kupata mume wa pili kwa mujibu wa tafsiri yako.

Anasema **(Manu, IX, 59, 58, 159.)** Mjane mwanamke anaweza kuchukua mwungano wa ndoa ya niyoga na ndugu mdogo au mkubwa wa mumewe aliyekwisha kufa kutokana ukoo wa kufikia daraja ya sita, mwanamume wa kabila yake, au aliye wa tabaka la juu. Lakini mwungano wa niyoga uharusiwa pale mjane wa kiume na wa kike wanataka kuzaa watoto katika niyoga kwa sababu wao hawakuweza kuzaa kabisa. Kwa maneno mengine, kutoweza kuzaa watoto, mwungano wa niyoga unaweza kufanywa baina ya mwanamke na ndugu wa mumewe mdogo au mkubwa kwa sababu ya kupata watoto. Lakini hawa walioungana wanaingiliana ki miwili kwa kujipatia furaha za uchu tu baada ya kuzaliwa kwa watoto, basi wao lazima wasihishimiwe. Wakati wa mkataba wa mwungano wa niyoga unakwisha kwa ishara ya mimba ya pili. Wao wasionane tena baada ya hapo. Ikiwa mwungano wa niyoga unafanywa kwa faida za wote wa wili, basi lazima umalizike baada ya mimba ya nne. Kwa vizuri, watoto 10

wanaweza kupatikana kwa mwungano uliotajwa hapa juu. Baadaye kuingiliana kimwili kati ya wanaume na wanawake inahesabiwa kuwa ni uchu, na wao hudharauliwa. Pia ikiwa wanaume na wanawake waliofunga ndoa na wakaendelea kuingiliana kimwili baada ya mimba kumi wao pia hudharauliwa na kufikiri vibaya na wenye uchu. Ukweli ni kuwa, ndoa na niyoga hizi zote ni za kuleta watoto tu lakini si za raha ya uchu tu kama wanavyofanya wanyama.

Q. Jee niyoga ya mwanamke hufanyika baada ya kifo cha bwana wake au hata anapokuwa hai?

A. Pia hata anapokuwa hai; Mwanamume anapojiona kuwa yeye hawezi kupata watoto, yeye lazima ajikere kwa kumwachia mkewe kwenda kwa mwanamume mwingine, kwa kusema: Ewe mwanamke mwenye bahati, mwenye haja ya sifa, sasa fanya mtafute mwingine: kuliko mimi, kwa sababu wewe hunatamaa ya mtoto kutoka kwangu. Lakini yeye amtumikie mume wake wa ndoa kama kawaida. Na kwa namna hiyo hiyo, mwanamke aliyekuwa na maradhi, na shida zingine, na anapojiona kuwa yeye hatoweza kuzaa watoto, lazima amruhusu mumewe kuungana na mwingine, kwa kusema: Ewe bwana wangu, sasa kata tamaa zote za kupata watoto, kutoka kwangu, na kuingia katika mwungano wa niyoga na mwanamke mjane mwingine na upate kuzaa watoto wako mwenyewe. Niyoga ilifanywa na wake wa mfalme Pandu, Kunti na Madri, na wanawake wengine wazee. Pia, Vyasa alifanya mwungano wa niyoga na wake wa kaka zake, Vichitravirva na Chitrangada, kwenye mauti zao na kupata Dhritrashtra juu ya Ambika, Pandu juu ya Ambalika, na Vidur juu ya mfanyi kazi wa kike. Hizi na kama hizi ni dalili dhahiri za itikadi za niyoga.

**Manu anasema IX, 76.** Mwanamke aliyeolewa anangoja mume wake kwa muda wa miaka minane ikiwa yeye amekwenda kwa ajili ya kutafuta elimu miaka sita anamgonja ikiwa yeye amekwenda kutafuta umaarufu, na anamgoja miaka 3 ikiwa yeye amekwenda kutafuta mali na vyenginevyo. Baada ya kumalizika miaka hiyo yeye lazima apate watoto kwa akda ya niyoga. Anaporudi mume wake wa ndoa, basi mwungano wa niyoga ukatike.

**(Manu, 9.80.)** Sheria hizo hizo zinaambatana na wanaume wazuri. Kuwa mwanamume anaweza kuishi na mkewe kwa muda wa miaka 8 ikiwa yeye ni tasa, i.e. yeye hajachukua mimba tokea kuolewa mpaka kufikisha miaka 8. ikiwa watoto wamekufa basi angoje miaka 10, angoje kwa miaka kumi na moja ikiwa kila mkewe anapozaa anazaliwa mtoto mwanamke; na asimgoje kabisa ikiwa mkewe ni mfidhuli; na baada ya miaka hii yote yeye lazima apate watoto kwa mwanamke mwingine kwa njia ya akdi ya niyoga. Ikiwa mwanamke anamwona mume wake ni dhalimu sana, basi yeye amwache na afanye niyoga na bwana mwingine na kuzaa watoto wa kumrithi mume wake wa ndoa mali zake. Hizi ni amri na sababu za Swayamvara na ndoa za niyoga, ambazo watu lazima wazifuate ili jamii zao ziweze kuwa bora.

**Urithi**

Kama watoto wa wanaume na wanawake waliofunga ndoa, wanaitwa aurasa, basi pia wale watoto wa niyoga wanarithi mali za baba zao.

Sasa, wanaume na wanawake, lazima wafahamu kuwa shahawa ya mwana mume na mwanamke ni vitu vyenye thamani sana. Yo yote anaye vipoteza vitu hivi vya kuleta maisha kwa kuwaendea malaya au kwa mwanamke usiyemjua au kwa kwenda kwa wanaume wahalifu, ni mjinga mkubwa. Hata wakulima wajinga na wafanya kazi wa mashambani hawapandi mbegu zao ila mashambani mwao au bustanini mwao tu. Ikiwa mbegu za mboga zina thamani kama hii, na hata wakulima wajinga wanaifuata sheria hiyo kwa bidii, basi hakuna mjinga mkubwa zaidi kuliko huyo anyezitupa mbegu za mti wa binadamu katika shamba baya; kwa sababu yeye hawezi kupata matunda yake baadaye. Pia, 'Atma vai jayate putrah' anasema kuhusu maandishi ya Brahmana. Ni maana kuwa, Roho inazaliwa katika mtoto wa kiume.

Haya ni mafumbo kutoka kwa Sam Veda katika Nirukta, III. 4 - Nyinyi mnazaliwa kutokana kwenye mbegu ya kila kiungo na moyo. Kwa hivyo nyinyi ni roho yangu. Nyinyi hamtakufa kabla mimi! Bora nyinyi muishi miaka *100*. Ni dhambi kubwa kupanda katika danguro na mashamba mengineyo ya dhambi ambamo mnatoka vi wili wili vya watu wenye uadilifu na masharifu, au kuzifanya shamba nzuri kuwa na mbegu za uhalifu.

**Hoja ya Ndoa**

Q. Kwa nini sisi tufunge ndoa? kwa sababu ndoa huwaletea taabu wanaume na wanawake na kujilazimisha kujiziwia na kupata maumivu. Kwa hivyo, wao waishi pamoja ikiwa yapo mapenzi baina yao; na ikiwa mapenzi yamekwisha wao watengane.

A. Ni tabia ya wanyama na ndege, na si ya binadamu. Ikiwa ndoa usiwepo katika jamii za watu, 1. Kazi nzuri za jamii zitaangamia. Hapa atakaye mtumikia mwenzake, 2. Zinaa itazidi sana, na watu wote watapata maradhi, na kudhroufu na kufa haraka.sana. 3. Hapana atakaye mwogopa mwenzake au kuona aibu atakapofanya mabaya, 4. Hapana atakaye watazama wazee, 5. Uchu na ukahaba utazidi, maradhi, udhaifu, na maisha yatakuwa mafupi na jamii nyingi kumalizika kabisa, 6. Hapata kuwa na wenyeji na warithi wa mali za yo yote, 7. Hapana atakaye kuwa na hukumu ya kitu kwa muda mrefu. Kwa hakikisha kutokuwapo haya yote na mengi mengineyo ya uhalifu kuwa ya daima, chuo cha ndoa ni cha pekee cha kufuatwa.

Q. Ikiwa pana ndoa moja tu, mwanaume mmoja atamtia mimba mke mmoja tu, na mwanamke mmoja na mume mmoja. Mwanamke akiwa ana maradhi yasiyo dawa, au mwanamume anaugua daima, na wao wote ni vijana, na wao hawawezi kijizuia kimwili; basi wao wafanye nini?

A. Swali hili limejibiwa wakati tulipoeleza sheria za niyoga. Ikiwa mwanamume

hawezi kujiziwia kimwili kwa muda wa mwaka mmoja, ambapo mkewe anamimba, yeye afanye niyoga na mwanamke na kumpatia huyo mwanamke watoto. Lakini hairuhusiwi kabisa mwanamume kuzini au kufanya umalaya.

**Tabia na Uaminifu.**

Kuishi ni kuwa, wao lazima kadiri iwezekanavyo wajifanye wawe nia ya kujipatia wasiokuwa nayo; hifadhi walichonacho, zidisha kilicho kuwapo, tumia kilichozidi kwa ubora wa nchi. Wao lazima wafanye kazi zinazowapasa kufanya kwa vyo vyote kwa uwezo wao na kwa mapenzi na uzuri wa tabia kama ilivyokwisha tajwa, kuzifanya akili zao tabia na miili daima kutumikia wenzao na jamii kwa pamoja. Wao wasijifanye wavivu na wajitolee kuwatumikia mama, baba, mkwe wa kike na kiume; wawapende rafiki zao, jirani mfalme, mtaalamu madaktari na watu wenye uadilifu; na wahalifu kuwafanyia vyengine i.e., kuucha uadui kuwa upande wao na wao daima wawafanyie mema. Kadiri wao wawezavyo, wao watumie pesa zao na nguvu zao kuwasomesha watoto wao na kuwafunza ili watoto wao waweze kuwa wataalamu wa kweli na rai wazuri. Kwa kuwa waaminifu katika mambo yao wao wajifanye watakatifu, na huu utakatifu utawapatia nafuu.

**Muhanga wa Farasi na Ng'ombe.**

Wao wasiamini haya na mengine kama haya:-

1. Brahmin aliyeanguka ni bora kuliko Shudra asiyejifikiria; kwa sababu ng'ombe mkavu ni mtakatifu, lakini si punda mwenye kutoa maziwa.

2. Muhanda wa farasi, muhanga wa ng'ombe, kutoa sadaka ya nyama, kupata watoto na ndugu wa kiume wa mume, ni tabia tano zilizokatazwa katika kaliyuga (wakati wa sasa)

3. Mume wa pili wanaruhusiwa wanawake wanapopatwa na shida za namna tano, viz. kupotea kwa maume zao, kifo, ukanithi, kukataliwa na kuharimishwa.

Hizi beti za uwongo za code ya Parashar. Ni nini kilicho gawanyika zaidi kuliko haya, na si ya uadilifu, ambapo mwovu aliyezaliwa mara mbili anahesabika kuwa ni bora na mwadilifu na Shudra au mtu wa tabaka ya chini kuwa ni mtu duni. Jee punda mke hastahiki kutazamwa na wachukuzi na wenginewo kama ng'ombe mtoaji wa maziwa au asiye maziwa katika zizi la ng'ombe? Pia mfano huu si sawa; kwa sababu Brahmin na Shudra ni binadamu, na ng'ombe na punda ni wanyama. Ikiwa sehemu, ijapo kuwa, ya mfano inasema pamoja na uthabiti, beti haziwezi kupata imani kutokana na jambo lisilofaa na sababu zao.

2. Ashwalambha anapotoa sadaka ya farasi na Gavalambha anatoa ng'ombe i.e. kuwachinja na kutoa muhanga kwa moto, haijatukuzwa katika Vedas, kwa nini kuzuiwa kwake hakuko katika kaliyuga (wakati wa mashindano) kinyume cha Veda? Ikiwa kuzuiwa kwa kitendo hiki kiovu ni sawa kufuatwa,

idhini yake itasadikiwa kwa kufuatwa katika wakati wa Treta na mizunguko mengine. Sasa yote haya hayawezikani kauminika kuwa kitendo hiki cha dhambi kilifanyika wakati wa uadilifu. Pia kuna idhini ya kukataa katika Vedas na katika maandishi mengineyo ya kweli. Kwa hivyo, kuzuiliwa kwake hakuna maana. Ikiwa kula nyama inakatazwa, ukatazo huo ni wa daima. Veda inapo ruhusu kupata watoto kwa devara au mume wa pili wa mwanamke kwa nini mwandishi wa ubeti huu anabweka bila ya sababu? Ikiwa mwanamke anafanya niyoga kwa urafiki nyumbani mume wake anapokuwa amekwenda nchi nyingine, yeye atakuwa mke wa nani mume wake wa kwanza anaporudi wakati huo? Ikiwa itasemekana ni mke wa mume wake wa kwanza, sisi tunaamini hivyo; lakini mengi yamepitwa inavyoonekana katika Code ya Paashar.

3. Jee kwani kuna dhiki za namna tano tu kwaajili ya mwanamke? Wakati wake wa dhiki ni zaidi ya dhiki hizi tano; kwa mfano, mumewe anapokuwa mgonjwa wa kitandani kwa muda mrefu, kutosikilizana kwa mume na mke, na mengineyo. Hata hivyo beti hizo zisifutwe.

**Vitabu vya Kudanganya.**

Q. Haya, wewe husadiki yale aliyoyasema Mwenye Hekima Parashar anasema?

A. Maneno yanaweza kuwa ya mtu yo yote, hata wawe wakubwa vipi. Kwakuwa kinyume cha Vedas, basi hawezi kukubaliwa. Pia si maneno ya Parashar.

Madhumuni ya kuandika vitabu na kutumia majina ya watu wanaoheshimiwa duniani kote ni kwa vitabu hivyo viweze kukubaliwa na wote kwa majina yao makuu na kuwaletea wandishi wake riziki nyingi. Kwa hivyo, vitabu hivi vina maandishi mengi ya upuuzi. Isipokuwa baadhi ya mafunzo ya Vedas, lakini si maandishi mengine. Sheria hii inaweza kuhesabiwa kuwa kweli kwa vitabu vya uwongo.

**Umuhimu wa utunzaji wa Jamii na Nyumba.**

Q. Ati maisha ya jamii ndiyo ya mwisho kwa umuhimu kuliko yote katika maisha, au ni muhimu zaidi kuliko yote?

A. Tabaka zote za maisha ni kubwa zaidi ukuhisabu kazi zao.

Lakini Manu anasema **6, 90.** Amri zote zinapata uthabiti wake kutokana na tegemeo la dunia hii, kama mito yote midogo na mikúbwa huzurura huku na huku mpaka inafika kwenye bahari. Hapana hata amri moja inaweza kuchukulika na kufuzu bila ya kuwepo amri hii muhimu.

Kama viumbe vyote vinaishi kwa kupata usaidizi wa hewa, pia amri zote za watu zinaweza kuwapo kwa kupokea amri ya mwenye nyumba. **(Manu, 3, 77.)**

Kama amri za maisha ya wenye kuendesha nyumba kila siku wanajiwekea amri tatu ya elimu, ya mtawa na ya dini, kwa kuzifanya kuwa ni zawadi na sadaka za chakula na mahitaji mengineyo, ina hesabika kuwa ni msingi wa amri na ni njia kuu kuliko zote. **(Manu, 3, 78.)**

Kwa hivyo, yeye ambaye anautaka uokovu na raha, lazima, azifuate amri kwa uangalifu. Watu wasiokuwa thabiti na waoga hawawezi kutekeleza kazi za

amri hizi **(Manu, 3, 79.)**

Basi mtu lazima afuate wajibu wake na kukubali na kushika jukumu lake. Maisha ya jamii ya wajibu nusu za wajibu za dunia. Ingekuwa hakuna sheria za dunia, basi ingekuwa ziko wapi sheria za elimu, za mtawa na dini ingekuwa hakuna kuzaliwa kwa watoto? Yeye ni mwenye uchu yule ambaye anazilaumu amri za dunia. Yeye anayezifuata, anastahiki sifa zote. Lakini maisha ya kijamii huwa yenye nufaa hapo tu, bwana na bibi wa nyumba wametosheka na wanaporidhiana, wamesoma na wana elimu, wenye nguvu na wenye ujuzi wa kazi zote za nyumbani katika kila njia. Kwa hivyo, asili kubwa ya maisha ya ndoa ni kufuzu na kumaliza masomo ya kujiendeshea maisha na yale yaliyotajwa hapo juu ya kujichagulia ndoa mwenyewe (Swayamvara). Kwa ufupi huu ndio muhtasari wa kurudi kwa mwanafunzi nyumbani baada ya kumaliza elimu, ndoa na maisha ya dunia. Sasa kujipumzisha na kazi na kujinyima yataelezwa katika sura inayofuata.

**Muhtasari**

Anopamaliza masomo mwanafunzi lazima arudi nyumbani, ambapo baba yake au mwalimu wake atamtunukia ng'ombe, na yeye atapata ng'ombe wa pili kutoka kwa mkwewe wakati wa harusi yake.

Hapo tena yeye ataoa msichana wa kabila lake, ambaye hahusiki na mama yake kwa daraja ya sita ya ujamaa na pia hahusiki na jamii ya baba yake. Huyo msichana asichaguliwe kutoka jamii isiyoadilifu, wenye maradhi ya kuweza kuambukiza kama kifafa, ukoma, matende & C. Msichana awe na sura za kupendeza na jina zuri pia na awe amesoma sawa na mumewe **(Manu 3, 4, 8, 9.)** Ndoa za nchi za mbali huleta mambo mazuri, huchanganya damu, huifanya hali ya binadamu kuwa nzuri, huifanya siha kuwa bora kwa kupata mgeuzo wa hali ya hewa, huepusha ugomvi wa jamii, na huleta mambo mapya na watu wageni kujuana.

Kwa majibu wa Dhanwantary, baba wa dawa za India, mwanamume awe miaka 25 na mwanamke awe miaka 16 wakati wa ndoa. Manu inaamrisha msichana aolewe na mtu aliye na shahada miaka mitatu baada ya kupata hedhi. (IX, 90). Ndoa ya mwanamke ya umri wa miaka minane haitakiwi kama ilivyotajwa katika Parashar's Code, kwa sababu maandishi hayo si ya kweli. Veda ambayo ni takatifu zaidi kwa sheria na amri katika dini na sherehe, inaamrisha ndoa ifungwe wakati watoto wanapokuwa wamekua sawa sawa ambapo msichana amesoma na pia anauwezo wa kuzaa watoto. **(Rig. III, VIII, 4, IV, 16.)** Jamii zinazofunga ndoa wawe na hiari zao wenyewe katika kufunga ndoa. Wao wanapomaliza kuchaguana, wanaweza kuozwa skuli au katika nyumba ya bi harusi.

Shahada zao lazima zionyeshe tabaka zao katika jamii. Tabaka zao za kuzaliwa hazisaidiwi kitu na maandishi matakatifu. Manu, inasema, X, 65. Watu

wa tabaka la chini huenda kwenye tabaka la juu kwa uwezo wa uadilifu wao, na pia wale wa tabaka la juu hushuka chini kwa uhalifu wao. Tabaka zimefanyika kwa mujibu wa kazi unayoifanya. Kazi ya askofu ni kusoma, kusomesha, kusaidia kwenye sherehe, kutoa na kupokea sadaka; pia kujizoweza kutosheka, kujinyima nafsi yake, kutubia, usafi, kuvumilia, uaminifu, Sayansi, na uaminifu kwa Mungu. Kazi za shujaa ni kusoma utakatifu, kufanya vilivyo vitakatifu vya siri, mazoezi ya sanaa za kijeshi, na kuwa na khofu ya Mungu. Kazi za wafanya biashara ni kusoma, kujua, biashara, kuzalisha na kuweka pesa kwa kupata faida isiyo zidi ya mali anayoiweka. Kazi za mtumishi ni kupika na kuwasaidia hawa waliotajwa hapa juu katika njia mbali mbali. Hizi ni tabaka nne za jamii za watu. Wale wasiofuata sheria za kazi zao huleta uharibifu. Kupinga haya i.e. ukabila kwa uwezo; ubeti wa kumi na moja wa sura ya 31 ya Yajurveda imetengenezwa, ambayo inasema kuwa Brahmanas wanazaliwa kutoka mdomoni kwa Mungu, na mengineyo. Lakini haya si ya kweli, hasa ilivyokuwa Veda inaeleza kuwa Mungu hana mdomo au kiungo cho chote chengine cha mwili. Maana hasa ya kweli ni kuwa mdomo ni kiungu kizuri zaidi kuliko vyote mwilini, kwa hivyo Brahmanas ni bora zaidi katika viumbe kwa ujuzi wao elimu, na mengineyo. Hapo jamii haileti maana kuwa ni Mungu.

Baada ya ndoa, mtu na mkewe waingiliane kimwili kila baada hedhi tu. **(Manu, III, 50.)** Ikiwa ipo ishara ya mimba katika mwezi wa pili, wao wawache mambo ya kuingiliana kwa kimwili mpaka mtoto anazaliwa. Wakati wa mimba mama ale chakula cha kujenga mwili na si cha kuleta madhara. Kiwe cha uji na mashendea, siagi na matunda. Mwanamke atunzwe na kuangaliwa vizuri, na mume na mke wapendane sana. Wanawake lazima waheshimiwe na wanaume wote wale wenye kutaka maendeleo. M. III, 55, 56.

Katika maisha wao waseme yale yaliyo ya kweli, na katu wasiseme ya uwongo, Manu, IV. 38. Wao wasiache kuifuata elimu na matumizi ya Vedas. Wao wafanye yale waliyotumikiwa na wao. Wao daima wazifanye kazi tano muhimu viz. Kumwabudu Mungu, muhanga wa moto, utumishi kwa wakubwa, huruma ya wanyama na ukarimu kwa wageni. Manu, IV, 21. Sala isaliwe asubuhi na jioni na si mara tatu kutwa. Manu, II, 103. Wao wasiwaheshimu wanafiki, wapinzani wa Vedas, washupavu wa dini, au wadanganyifu (ambawo wanajiita Mwenyezi Mungu). Wao lazima waamke mapema, wasifanye maovu ya kuangamiza jamii zao. Manu, IV, 174. Pasiwepo na vita na waziri, mwanafunzi, mwalimu, mjomba, mgeni, mlezi, mtoto, mzee, mtoto wa kike na mtumishi. Manu, IV. 179, 180. Wao wajiepushe na wahalifu, waongo wenye dhambi, wafanyi biashara ya dini, wahuni, wajanja, wanaojidai, wachinjaji, wanaafiki na wahalifu. ib. 195.

Kuwa na uadilifu na kuweza kuutumia ni muhimu sana hasa baada ya kuona kuwa vyote utaviwacha hapa duniani isipokuwa uadilifu tu ndio unaofuatana na roho kwenda dunia ya pili Manu, 240. Yeye ameokolewa na atamwona Mungu ambaye ni mwadilifu - ib. 243. Tabia nzuri huleta maisha ya ukamilifu, watoto wazuri na mali isiyoweza kuoza, na kuondosha vilema - ib. 156. Amri nne hizi

lazima ziishi na urafiki na nia njema, maaskofu ni wakusomesha, mashujao kulinda, wafanya biashara kufanya biashara na watumishi kusaidia watu. Mume na mke waishi kwa masikilizano, na waaminiane. Wao waishi pamoja kote nyumbani na katika nchi za kigeni kwa kadiri iwezekanavyo. Wanapotenga na kwa mauti, tabaka tatu za juu haitakiwi wafunge ndoa tena, lakini ikiwa hawapo warithi basi wapate watoto kwa kufanya niyoga katika tabaka zao wenyewe au katika tabaka la juu. Baina ya wajane wa kiume au wakike ndoa haitakikani kwa kupungua kuwepo kwa mapenzi, ugomvi kuhusu mali za marehemu baina na jamii za wanaotaka kufunga ndoa tena hufutilia mbali jamii nzuri, na kupotea kwa utakatifu wa mwanamke. Tafauti ya niyoga ni kuwa kila upande unaishi katika nyumba zao wenyewe, watoto wanaopatikana huwa wa yule anayewalea, kila upande ünajitegemea mwenyewe, uhusiano wao huvunjika watoto wanapozaliwa na watoto wawili au wanne tu wanaiweweza kuzaliwa tu. Niyoga inaruhusiwa na Veda. Rig, X, LV, 45. Inaonekana kama zina kwa kutotumika. Lakini kama ndoa, inafanywa kwa idhini za jamaa na kusherehekewa kwa kufuata kanuni za dini. Si kwa ajili ya vijana na wanawali. Ikiwa mwanamwari anampoteza mumewe kabla ya kumjua, yeye lazima aozwe tena. Manu, IX, 178. Ni yule aliyekuwa amempoteza mwenzake anaweza kufanya niyoga ili apate warithi wa mali zao. Baada ya kuzaliwa kwa watoto, ikiwa wao bado wanaendelea na uhusiano basi wao huwa wenye makosa. Ikiwa mume ni khanithi au mwanamke ni tasa basi uzazi uendelezwe kwa kufanya niyoga ya wakati maalum. Tazama Rig, X, X, 10 na mfano wa wake zake Pandu. Mwanamke na mwanamume lazima wapate watoto kumi tu ikiwa kwa ndoa au nyoga; kwa sababu, kuzaa sana hudhoofisha umma. Kama vijana hawataki kuwaoa wajane wa kike, na wanawari pia hawataki kuolewa na wajane wa kiume, niyoga itawalazimikia watu, ikiwa watawachiliwa kufanya wapendavyo.

Tabaka zote nne ziishi kwa wema na udugu; kuitumikia na hali nzuri ya jumuia ya madola, na kuwatumikia wazazi wao majirani, mfalme, wataalamu, madakitari na watukufu wenginewo. Kwa vyo vyote mwangaza wa elimu usizimwe. Wao wawe waaminifu katika vitendo vyao vyote na wajaribu kupata uokovu. Kufikiria tabaka za juu na chini ukomeshwe. Yeye unayoyafanya ndiyo yanayokuletea heshima kwa wote. Muhanga wa farasi na ngombe na kula nyama, iliyofanywa na St. Parashar, ni uwongo dhahivi wa maaskofu wa baadaye. Fikra kama hizi za udhaifu haziruhusiwi na umuhimu na mari ya pili za nyumbani, ambayo inatilia nguvu amri zote nyingine za jamii. Manu, VI, 90.

Ewe Mola! Kwa ikhlasi na kwa kustahili dini, nina weka ahadi na Wewe kuwa mimi sitafanya dhambi kwa makusudi na viungu vyangu vitano vya jamii moja, na namna tano za hisia; viz, ulimi-onja, pua-nusa, jicho-ona, shikio-sikia, kiganja na mgongo wake - kugusa, utupu - uchu, moyo - kutaka, shingo - usemi, kichwa - fikira, mkono - vitendo.

**Sandhya (Kuabudu)**

Lakini ewe Bwana! Mimi ni mnyonge na kwa hivyo ninakutegemea wewe. Takasa na zifanye ziwe hisia zangu zenye nguvu. Wewe Mwenyewe. Mungu wakuishi milele takasa kichwa! Mungu Mtukufu takasa macho! Mungu Mwenye

Furaha itakase shingo! Mungu Mkubwa utakase moyo. Baba wa wote utakase tupu au shauko za kinyama! Mungu mwenye Busara itakasa miguu! Mungu Mwandani tena litakase bongo! Mungu aliyeenea kote patakase kote!

Ee Mungu wa maisha! Ee Mungu wa utakatifu! Ee Mungu Mkubwa! Ee Mungu Baba! Ee Mungu wa Hekima! Ee Mungu wa ukweli!

Sababu na chembe ndogo ndogo zilizawa na tabia iliyojaa, hapo tena likaja fujo, tena nguvu au harakati, tena bahari,

Baada ya nguvu na bahari ikaja harakati za dunia. Mtawala wa dunia hufanya siku na usiku bila taabu.

Mfanya aliumba, kama kwanza, jua na mwezi, vinavyongaa na vitu vinavyopenya nuru, mbigu na sehemu za furaha.

Ewe Mwenye Busara na Mtakatifu! Wewe uko mbele yetu, Halisi, Mfalme wetu na mlinzi. Wewe umetengeneza jua ambayo mishale yake inaleta maisha kwenye ulimwengu. Sisi tunakusujudia wewe kwa shukrani kwa utawala wako wa haki, ulinzi mwema, na zawadi ya maisha. Kwa ukarimu huu wote, Ee Mungu! sisi tunakushukuru wewe kwa unyenyekevu, na mweke yeye, anayetuchukia sisi au yule tunayemchukia sisi, kwako wewe tu.

Ee Mungu Muweza, Wewe uko upande wetu wa kulia Mtawala wetu na Mlinzi wetu kutokana na wadhaifu. Wewe unawapeleka watu wenye hekima kutusomesha sisi. Sisi tunakuinamia & C. (As 1.)

Ewe mwenye kustahili kuabudiwa! Wewe uko nyuma yetu sisi daima, mfalme wetu na mlinzi wetu kutokana na wadhaifu. Wewe umetengeneza chakula ambacho kinatupa maisha duniani (As 1.)

Ewe baba! wewe uko upande wetu wa kushoto, mfalme wetu, unayejitegemea mwenyewe, na mlinzi wetu. Nguvu zako zinafanya damu zetu kuzunguka ili kuliendesha maisha yetu na kutuwezesha kufanya vitendo vingi duniani. (As. 1.)

Ewe Mungu uliyeenea kote! Wewe uko chini ya mfalme wetu, na mwenye kuilisha maisha yetu na miti yenye vivuli na mizizi yenye kutambaa unayo zaa matunda mbali mbali (As. 1.).

Ewe Mungu mkubwa! Wewe uko juu, mfalme wetu, Mwendelezi, na Mlinzi. Wewe hutuletea mvua ili konde zetu zipate maji, ambazo zinatunza maisha yetu. (As. 1.)

Na sisi, kwa kumjua Mungu na baraka zake zote, mbele ya kiza cha ujinga, yote ya furaha, mkubwa wa wote, kujipatia kwake jua la maisha yetu na mwangaza wa roho zetu!

Kila kitu cha dunia ni kama bendera za kumwonyesha Yeye, Mtakatifu,

Mwumba wa dunia zote na Jua la maisha, kwa viumbe vyote.

Ijapokuwa vitu vyote vinamwonyesha yeye, hata hivyo, Ee Mola! Lakini wa Ajabu na umacho saa zote, na ni Tegemezo wa pepo zote, hata jua, mwezi, na moto. Wewe ni mwenye pepo na dunia, na mbingu pia. Wewe ni mfanyaji na ni Roho za vinavyoweza kwenda na vitu visivyokwenda. Na sisi tufikiri, kusema na kutenda yaliyo sawa!

Lile jicho lililo macho daima ni safi na la milele kwa ajili ya uwema wa wataalamu. Tuweze kuona masika mia! Na sisi tuseme masika mia! Na sisi tuwe huru masika mia! Na tena pia kwa masika (Masika kwa maneno ya mashairi, ni mwaka mmoja.)

Ewe Maisha yote! mtukufu wa yote! Furaha yote! Bwana wa juu, chini na sehemu za furaha, mwimba wetu, mwenyezi Mungu, sisi tunatafakari kwako Menye kustahiki kuabudiwa kwa umbo la mwangaza mtakatifu, ambawo unaondosha kiza cha dhambi kutoka akilini. Na wewe waangaze watalamu wetu!

Sisi tunakusujudia wewe, ambaye ni wa furaha tupu, raha zote, mwenye kutoa nafuu na Mwingi wa matakwa ya uadilifu, Mwenye ukimyaa na Amani yote.

## SURA V.
## KUSTAAFU NA KUTENGUA.

**Kwa kustaafu**

Daraja ya utaratibu wa maisha ya binadamu kwa mujibu wa Shatpatha. Sura ya XIV. nikuwa baada ya kumaliza kuwa wanafunzi mtu lazima ajichukulie kazi za nyumbani, na baada ya kumaliza kazi za nyumbani, ni kustaafu na mambo ya ulimwengu, na baada ya matengenezo ya kustaafu kwa kazi za kiroho, kuchukua amri ya utakatifu na kukataa na kujinyima. Pia Manu anasema VI. 5.

**Wakati wa kustaafu.**

1. Mtu aliyezaliwa tena na mwendeshaji wa nyumba ama ni Brahmana, Kshatriya au Vaishya ambaye amemaliza kabla ya siku zake za kuwa mwanafunzi naye ameitunukia nyumba kama inavyotakiwa ambaye ni msalihina na wa kushika dini na ni bwana wa mawazo yake lazima astaafu na kuishi katika mwitu au mbali na makao ya watu. 2. Pia mwenye nyumba anapoona nywele zake zinakuwa nyeupe na ngozi yake inaregea na kukunjika, na mtoto wake wa kiume amepata mtoto wa kiume; yeye lazima aanze kustaafu. 3. Kuacha kutumia *chakula kitamu, nguo za kupendeza, na maisha ya mjini ya raha, na kuwa* wachilia watoto wa kiume kumtazama mama yao au kumchukuwa pamoja na yeye, yeye aisha pahali pa upweke shambani au mwituni. 4. Achukue pamoja na yeye nguo kamili za kujitolea, yeye awache mji na kuishi shambani au mwituni na kujiziwia matamanio. 5. Yeye lazima afanye madhubahu tano au wajibu wa dini na kuishi kwa kula nafaka mbali mbali, mboga nzuri, mizizi, matunda, na vinavyoota chini ya ardhi vinavyolika, kama viazi vitamu, awakirimu wageni wake huko. Zaidi, Manu anasema katika Code yake VI, 8, 26.

1. Yeye lazima aishi maisha ya kusoma, na ukarimu, ni kuwa aweanasoma na kusomesha Veda, awe amejiweka mwenyewe, mkarimu, awe ni bwana wa kumiliki akili yake, mwalimu, mwema kwa wote, mtoaji lakini si mpokeaji wa cho chote. 2. Asiwe mwangalifu sana wa mwili wake, mtakatifu wa milele, ni kuwa, asiende kwa mkewe ikiwa yuko na watu, alale kwenye sakafu, bila ya kupenda kwa wanaomfuata au wenye kutegemea vitu vyake mwenyewe yeye aishi kwenye mizizi ya miti. Pia Mundakopanishat anasema I, II.

Wataalamu waliokimya, wanaofuata ukweli kwa uadilifu, utukufu na wanaojinyima ya dunia katika upweke wa mwitu, na kujisaidia wenyewe kwa kuomba sadaka na kujipatia janat na kujinadhifisha na dhambi, kufurahia kwepo kwa Mungu, ambaye ataishi milele, asiye kuwa na ila, alieyeenea kote, hakui na haozi, na mwenyezi mwenyewe. Pia Yajurveda inasema, XX, 24.

Mtawa au mwenye kuishi mwituni lazima atake sana kuwa mtakatifu kwa kufanya sadaka ya moto na kuwa na tabia njema na kumwamini Mwenyezi Mungu. Yeye ajipatie sifa hizi kwa njia nyingi ambazo si rahisi kama vile awe na marafiki wazuri, afanye mazoezi ya yoga, fikira njema, ambazo zitampa elimu

ya utukufu na takatifu. Baadaye atakapo taka kuziwacha anasa za dunia yeye lazima ampeleke mkewe kwa watoto wake wanaume na ajinyime yote ya dunia, ni kama, kuishi kwa Padri na kuhubiri uadilifu. Haya ni ya kujistaafu au ni maishi ya mtawa kwa ufupi.

**Kwa Kujistaafu.**

Manu anasema, VI. 33, Baada ya kwisha kuishi katika maisha ya kustaafu wakati wa sehemu ya tatu ya maisha yake, ni kuwa, katika mwaka wake wa 50 mpaka 75, yeye lazima awache muungano wote wake wa vitu vya dunia katika sehemu yake ya nne ya maisha yake, na kwa askofu, mtu wa dini au Sannyasi.

Q. Jee yeye anakuwa na dhambi, ambaye anapitia mambo ya kutunza nyumba na kuwa na maisha ya mtawa na kujinyima ya dunia?

A. Anaweza kuwa na dhambi au asiwe nazo pia.

Q. Kwa nini unajibu jawabu za namna mbili?

A. Si za namna mbili kwa sababu yeye mwenyewe kujinyima katika miaka ya kwanza na baadaye kuwa mwenye uchu, huwa mwenye dhambi mkubwa; lakini si hivyo ikiwa ni mwadilifu na mtu mkweli. Anasema maandishi matakatifu ya Brahmana:

Kujinyima lazima ujizoweshe kutokana na mambo ya nyumbani au astaafu siku ile ile ambayo matamanio yake yanaujia akilini mwake.

Mwaandishi ya kwanza yanaeleza namna ya kawaida ya kujinyima; hii ni kujinyima na mambo ya nyumbani, na njia ya tatu ni ile, mtu aliye mtaalamu kamili, mwenye akili za kutulia, na hana matamanio ya uchu, na mwenye hamu ya kuwatendea mema wenzake, yeye anaweza kujinyima tokea anapokuwa mwanafunzi, Veda pia inaamuru kujinyima katika vipande vifuatavyo yatayah, Brahmanansha, vijanatah. -, Wattalamu huwa wenye kujinyima. Lakini inasema Kath Upanishat, II. 23.

Yeye hamkumbuki Mungu hata anapojinyima kwa uwezo wa elimu nyingi, yeye ambaye hayuko mbali na vitendo viovu, yeye ambaye hajatulia, ambaye akili yake haifikiri, na yeye ambaye akili yake haitosheki. Tena, ib. III. 13.

Mtu mwenye hekima aliyejinyima lazima aziziwie fikira zake na maneno kutokana na kutokuwa mwadilifu, na kuwaongoza wao kwenye elimu na kuwa wao wenyewe, na kutakuwako na elimu na ujuzi wa Mwenyezi Mungu, na tena kuifanya akili iliyotulia kuwa na ujuzi wa Mungu ambao unapatikana. Anasema, Mundak, II, 12.

Baada ya kuona raha za dunia zinavyopatikana pamoja na nyusi zenye jasho, mtu mtakatifu lazima ajizoweze kujinyima; kwa sababu, Mungu ambaye ni mtakatifu, kuwa yeye hachoki, na hawezi kufikiwa kwa vitendo vya kidini. Hata

hivyo yeye achukue zawadi mikononi mwake na kwenda kwa mwalimu, mjuzi wa Vedas na anayemjua Mungu, kwa madhumuni ya kupata elimu takatifu. Yeye atayatatua matatizo yake yote. Lakini yeye asiende kwa watu, ambawo, wamezama katika ujinga, lakini wanajifanya kuwa ni wenye busara na wajuzi. Wajinga na wenye fikra za chini, wao ni viongozi vipofu wa vipofu na huangukia katika mashimo ya huzuni. Kunywea katika ujinga mzito, lakini hufikiria kuwa wao ni wenye furaha na wametosheka, kwa kuwa waigaji wadanganyifu, ni watoto tu kwenye wataalamu, na wameleweshwa kwa kiburi cha kazi, wao hawajui Mungu ni nini wala wao hawawezi kuwaongoza wenzao kwa kwenye elimu yake. Kuwa kigeugeu, wao hupata maumivu ya uzazi na mauti **(Mundak, II, 8, 9.)**

Mundak Upanishat, III, tazama 2. ubeti 6. Hata hivyo, wale walio sannyasi au waliostaafu katika nia ya Mungu, wao ambawo wanawo uhakikisho wa ukweli kwa akili ya kusoma Vedant au masomo ya ubeti wa Vedic na kwa kujizoeza kuwa mwadilifu, na wale ambawo akili zao zimetakaswa na kujistaafu na kujirudisha nyuma na kustaafu, kupata furaha ya uwokofu kwa Mungu, na wakati wa uwokovu unapokoma, rudi duniani. Bila ya uwokovu maumivu ya uchungu ambaye mwili ni mrithi, haiwezekani kuangamia, kama tunavyosoma.

Katika Chhandogya Upanishat, sehemu ya 8, sehemu 1, 2, Wote wenye miili hawawezi kuwa mbali na uchungu wa maumivu. Ambapo roho isiyokuwa mwilini huishi na Mungu inapotakaswa, yeye hapati maumivu au raha za dunia.

Shatapatha K. 14, Pr. 5. Br. 2. K. 1. Kujinyanyua juu ya matamanio ya dunia, viz. umashuhuri, mali, raha, heshima na mapenzi ya watoto, mtu aliyestaafu wanaishi kwa kuomba sadaka na kupitisha usiku na mchana kwa kutekeleza namna zote za wokovu.

Baada ya kupanga kwa kujitolea kwa Mungu, na kujitupa kwenye uzi wa utakatifu, na fundo kwenye taji, na ishara nyinginezo, na badala ya pepo zao mto-prana: pumzi unazozitoa nje apana: unazo zivuta, vyana: nguvu za ubongoni, udana: nguvu za kuyeyusha chakula, na samana: nguvu za kujiendesha, kwa ajili wa mioto mitano ya muhanga, Brahamana mjuzi wa Vedas, lazima awache nyumba na kuishi maisha ya kujitolea ya Sannyasi: yeye ambaye amejinyima na ya dunia. **(Manu, VI, 38.)**

Baada ya kutoa msamaha kutokana na woga wa wanyama, mtu mtakatifu ambaye amejinyima na kustaafu mambo ya nyumbani kutoa amri tukufu, na yeye huusomesha uadilifu na elimu takatifu ya Vedas ambayo imeteremsha na Mungu, hupata sehemu ya uokovu iliyojaa mwangaza. (elimu) (ib. 39.)

Q. Ni nini hiyo dini ya Sannyasi au mtawa?

A. Dini ya watu wote ni moja tu, viz, mazoezi ya haki, kujizowesha ukweli, kuukataa uwongo, ukarimu, ukweli, na ya uadilifu kama haya. Lakini kazi maalum za Sannyasi au mtu wa dini ni:

**Kazi za Askofu.**

**(Manu, VI, 46.)** Askofu anapokwenda njiani yeye asitazame hapa na pale lakini ayaweke macho yake juu ya njia tu na kwenda. Yeye lazima anywe maji yaliyo chujwa kwa kitambaa, na daima aseme kweli. Yeye lazima atafakari vyema, na kuufuata ukweli na kuukataa uwongo.

ib. 48. Wakati wo wote mtu anapokuwa amehamaki naye anapohutubu au kusema au maneno ya chuki yake yeye, au kumsengenya, yeye asikasirike naye; lakini bali iwe kinyume, yeye lazima aseme yale yaliyokuwa mazuri kwa ajili yake. Bila ya sababu ye yote yeye asiseme uwongo, aitolee kafara hotuba yake, toa kutokana na tundu hizo saba, kama ilivyo, mdomo, tundu mbili za pua, macho mawili, na mashikio mawili.

Kwa kuwa imara katika imani yake mwenyewe na Mwenyezi Mungu, kuisha katika uhuru wake mwenyewe, na kujiepusha na kula nyama na vinywaji vizito, askofu lazima aendelee kuhutubu hutuba za kuendeleza dini na elimu duniani, kujipumzisha na nguvu za roho kwa furaha yake mwenyewe:- **(Manu, VI, 49.)**

Azifunge nywele zake, masharubu na ndevu, na azikate kucha zake, yeye achukue pamoja na yeye chombo kizuri na vitu vyake, na avae nguo zilizotiwa rangi kwa mkangazi au kusumbha. Bila ya kuwa na shaka ya nafsi yake na akili yake kuwa timam kwa Mungu, yeye lazima ende apendapo, bila ya kumdhuru kiumbe cho chote - ib. 52.

Yeye lazima ajiziwie na kuwangukia uovu, auache unyama au kupendelea au kuchukia, na asiwe na ukhasama na binadamu ye yote, yeye lazima ajiendeleza na nguvu ili apate uokovu. - ibid, 60.

Yeye lazima awe mwadilifu daima na kuwafanya wengine kufanya hivyo pia. Yeye asimshutumu au kumsifu mtu ye yote katika dunia, yeye asipendelee upande wo wote kwa wote na katika hali yo yote. Yeye inataka afahamu kuwa vitu, bakuli, kitamba cha rangi na ishara nyinginezo si vitu muhimu vya dini. Kazi muhimu zaidi ya mtu wa dini au Sannyasi ni kuwafanyia mema watu na wote wenye akili kwa kuwa fundisha wao ukweli na kuiendeleza elimu - ib. 66.

Kwa sababu, kuchanganyisha unga wa matunda ya Strychnos potatorum au mti wa nirmali katika maji yenye matope huyasafisha: hata bila ya kufuata njia hii, kuiponda na kuitia katika chupa, na kufanya tena kila unaposikia jina lake, maji ya mtu hayawezi kusafishika.

Brahman au Mcha Mungu wa dini takatifu, lazima afanye mazoezi ya kuvuta puumzi za udani kama awezavyo, na kusema neno moja Om na majina saba ya Mungu, yanayoitwa vyahritis kama sheria inavyoeleza. Lakini katu asivute puumzi hizo kasoro kuliko mara tatu. Kuvuta puumzi za nguvu ni mmoja katika msingi wa kazi. - ib. 70.

Kwa sababu, kuendeleza kuvuta puumzi huondoa dosari za akili kama kupasha moto na kuyeyusha huondoa taka za madini.

Kwa hivyo mtu mtakatifu au Sannyasi lazima aondoshe dosari za akili, mawazo ya ndani na mazoezi ya kila siku ya kuvuta puumzi za ndani, dhambi za dharna: kuabudu kwa jina la Mungu; uovu wa kujiambatanisha na vitu vya dunia kwa uvumilivu na mawazo ya moyoni; na tabia ya kusadiki kuwa Mungu hayuko au dosari ya roho kuhusu furaha na huzuni, ujinga na kutokamilika kwa kutafakari bila ya kukoma kuhusu sifa takatifu (ib. 72.)

Kwa kutafakari na kujitazama yeye lazima achungulie katika njia za Mungu, kukaa moyoni katika kuifanya roho ifanye kazi, na kuanza kujua kuwepo kwake Mungu Muweza katika vitu vyote, vidogo na vikubwa, ambayo elimu yake ni ngumu kupatikana kwa asiejua na ujinga. - ib. 73.

Hapa usipokuwa Sannyasins au watu watakatifu waliojitolea wanaweza kupata hali ya kheri au uokovu na kuwasaidia wengine pia kuyapata haya duniani, kwa kutomchukia mtu, kwa kuyawacha yenye raha za uchu, kwa kufanya kazi zilizowekwa na Vedas, na kwa mazoezi ya kujinyima raha za dunia kwa nguvu. - ib. 75.

Askofu anapokuwa huru kutokana na kutaka vitu vya dunia vya namna yo yote ya uchu wa nyama, na kutakaswa na kutokuwa na matamanio ya kupenda na vitendo vya matamanio ya mwili, yeye hupata raha ya pekee katika maisha ya sasa na baada ya kufa. - ib. 80.

ib. 91. Hata hivyo, mwanafunzi, mwendesha nyumba, mtawa na mtakatifu lazima afanye mazoezi yafuatayo ya tabaka kumi za uadilifu.

**Mambo Kumi Muhimu ya dini.**

ib. 92. - 1. Dhriti au ustahmilivu-daima kuwa na ustahmilivu. 2. Kshma au usamehevu-kustahmili kusengenywa na sifa, heshima na kutokuwapo na heshima, faida na hasara na mageuzi kama haya, na kujiweka katika hali ya kujiweza katika yote haya. 3. Dama au ucha Mungu - daima mtu ajifanye awe katika mazoezi ya uadilifu, na kujiziwia kufanya yaliyo si ya haki, hata mtu asifikirie kufanya maovu. 4. Asteya au uaminifu-kuwacha kuiba, haya ni kuwa mtu asichukue kitu cha mwenzake bila ya ruhusa, kwa hila, madanganyo, au udanganyifu, kinyume cha amri ya Vedas au sheria za biashara, ambazo zinasimamisha uaminifu. 5. Shouch au utakatifu-kuweka usafi wa ndani kwa kuwacha kupendea, kuchukia, na mengine kama haya ya kupendelea sehemu moja, na usafi wa nje kwa kutumia maji, kupaka-udongo na mengineyo kama haya. 6. Indriya - nigrah au kuweza kuziziwia hisia - daima zipime hisia kabla ya kufanya kitendo kisichokuwa cha uadilifu na kuzifanya hisia ziwe za kufanya wema. 7. Dhi au sababu - kuweza kuwa na sababu za kujiweka mbali na matumizi ya vinavyolevya, kuziangamiza sababu; kwa kukimbia mbali na urafiki wa walio waovu; kwa kuwacha kuwa mvivu, kujiona na uovu mwingine; kwa kutumia vitu vizuri, kuwa na marafiki wazuri; na kwa kufanya mazoezi ya yoga au kuwa na mawazo ya taamuli. 8. Vidya au elimu - elimu sahihi ya vitu vyote kutoka duniani mpaka kwa Mungu, kuitumia hiyo elimu kwa ajili ya faida ya maisha na kuushika

ukweli. Ukweli uwemo katika vitendo yale yanayoelezwa katika maneno, kueleza katika hotuba yale yaliyomo katika nia, na kuyaeleza yale ya nia kwa kuonyesha yale yaliyomo akilini. Haya yote yanasimisha na kuonyesha elimu hapa; kinyume cha ujinga wake. 9. Satya au ukweli - kukijua kitu kama kilivyo, kusema kweli na kuutumia huo ukweli kama inavyotakikana. 10. Akrodh au mutulivu - kuuwacha ukali na kupendelea na kujizowesha utulivu na kupendea uwema wa kweli.

Mazoezi kumi ya haya muhimu ya dini ni lazima kwa watu wote katika tabaka za maisha. Ni wajibu muhimu wa maaskofu au watawa kujizoweza wao wenyewe na kuwafanya wengine wayafuate haya pia katika maisha.

ib. 81. Hivyo askofu anapata raha katika Mwenyezi Mungu kwa kuweza kuyawacha maovu yanayotokana na mwungano wa vitu vya dunia, na kujinyanyua juu ya raha na huzuni na mambo mengine ya kinyume yanayo patikana duniani. Ni wajibu mkubwa wa Maaskofu kuwaonyesha watu ukweli wa vitu vyote na wa vitendo pia, kuwafanya wao wa uwache uovu, kuwaondolea wao shaka zao zote, na kuwafanya wao wafanye ya uwema.

Q. Ni wajibu wa Brahmana peke yake kujinyima na kuyawacha ya dunia au hata tabaka kama za jeshi na wengineo pia wanaweza kufanya haya?

A. Ni wajibu wa Brahmana peke yake tu kufanya haya, kwa sababu, mtu anaitwa Brahmana ni yule ambaye ana elimu ya kutosha kutokana na matabaka yote, mwema na mwadilifu kwa wote. Hakutaleta faida yo yote kutokana mtu asiye na elimu ya kutosha, uwema na uadilifu, ucha Mungu, na kutojishughulisha na raha za dunia. Hata hivyo usemi, kuwa Brahmana peke yake tu na si wengine, anawezo wa kujinyima au Sannyas. Hii hapa ni amri ya Manu.

Mwenye kutoa sheria mkubwa anasema, VI, 97. Ewe mtabiri, ni wajibu wa Brahmana kwenda mujibu wa kazi za tabaka nne za maisha - kuwa mwanafunzi, maisha ya jamii, maisha ya utawa na maisha ya kujinyima. Uwema wa kujinyima ni kuwa hukupa furaha ya mungu hapa chini na furaha ya milele ya uokovu baada ya kufa. Baada ya haya, sikiliza sheria za wafalme kutoka kwangu.

Kwa hivyo, ni dhahiri kuwa Brahmana peke yake anawajibu kujiweka katika maisha ya kujinyima raha za dunia. Walinzi na tabaka nyinginezo wanaweza kubarikiwa kuwa wanafunzi au Brahmacharya.

Q. Kitu gani ni cha muhimu kuweza kuwa Sannyas au maisha ya mtawa?

A. Kustaafu na ya dunia au kuwa mwalimu wa dini ni muhimu kama kwa sheria za jamii kama kichwa kwa mwili wa mtu; kwa sababu elimu na dini haiwezekani kuwepo bila ya haya. Pia, amri nyinginezo zina muda mfupi wa kuwaongoza watu kwenye njia ya haki kwa sababu ujuzi wao wa elimu kuhusu mambo ya nyumbani na mazoezi ya kutubu dhambi. Ni vigumu kwao kutenda matendo ya haki na ya kutopendelea upande wo wote wao hawawezi kuufanyia wema dunia kwa jumla kuwa kama ya utakatifu, kwa kuwa huru kutokana na mambo ya dunia. Kwa sababu, yeye anazo saa za kutosha ambazo wengine hawana za

kuendeleza elimu ya vitu kwa uwezo wake wa kuwa na elimu sahihi. Lakini mtu aliyejichukulia amri takatifu kutoka maisha yake alipokuwa mwanafunzi, anaweza kutendea wema zaidi watu kwa ujumla kwa kuwafunza wao ukweli kuliko yule ambaye amefanya ya kawaida tu ya kuendeleza nyumba na ya maisha ya mtawa.

Q. Kuweza kujinyima ya dunia ni kinyume cha nia ya Mungu; kwa sababu ni nia yake Mungu mwenyewe kuuendeleza uzazi wa binadamu, Mtu ambapo haoi. yeye hawezi kupata watoto. Ikiwa kustaafu na mambo ya dunia ni kitu kikubwa katika maisha, na watu wote watafanya hivyo, basi binadamu watakuwa hawapo tena.

A. Watu wengi hawapati watoto hata wakioana, au ikiwa watoto wanazaliwa basi hawaishi. Kwa hivyo watu hawa wanakwenda kinyume cha sharia ya Mungu. Ikiwa wewe unasema hivyo kama wanavyosema washairi wengine. Pana makosa gani pale, ikiwa kitu hakitendeki hata kwa kuchukua maumivu na njia zote kukifanya? Kuna moja, sisi tunauliza maumivu ni makubwa vipi ikiwa watoto wengi wanapatikana wakati wa kuishi kwa ujamii, ambawo hugombana na kupigana kwa kutenda vitendo vya kushindana au vya uadui. Kuna pingamizi nyingi kutokana na upinzani wa fikira. Mtu ambaye amejistaafu na dunia analeta mapenzi ya kusikilizana miongoni mwa watu kwa kuhubiri dini iliyosomeshwa na Vedas, yeye atawavusha mamia na maelfu ya watu. Pia yeye atakuwa ni sababu ya kuwa na jamii njema kama wanavyofanya maelfu ya wenye kuendesha nyumba. Watu hawawezi kustaafu kwa sababu wao hawawezi kujinyima na raha za dunia. Wale ambawo watakuwa watu waadilifu kutokana na nasiha za watu watakatifu, watakuwa, kama ilivyo, watu wa wale wenye utakatifu.

**Maaskofu wa Kisasa.**

Q. Waliostaafu wanasema; sisi hatuna kitu kile tunafanya duniani. Kuna faida gani kukikera kichwa kwa madanganyo ya dunia? Kwa nini tusiishi kwa furaha baada ya kupata chakula na nguo? Sisi tuishi kwa kutosheka kwa kujiamini kuwa ni Brahmana (Mungu) na kuhuburia hayo hayo kwa kila mwenye kuuliza, ni kusema kuwa - (Wewe ni Mwenyezi Mungu; Brahma), isiyodhurika kwa uvundo wa maasi au sifa za uwema; kwa sababu, ujoto na ubaridi ni sifa za mwili, njaa na kiu za puumzi, raha na maumivu ya nia, dunia ni madanganyo, mambo ya dunia ni ya kufikiria tu au si ya kweli. Kwa hivyo, ni mwafaka kwa mtu mwenye hekima asijifungashe nayo. Vitendo vizuri vyote na viovu anavyovitenda mtu, ni sababu za harakati za mwili na akili, lakini si za roho; haya ni mafunzo yetu. Lakini wewe unasemaje kuhusu Sannyas au kustaafu, ni ya ajabu kidogo na ni tofauti kuliko mawazo yaliyopokelewa. Sasa, ni kweli na nini uwongo?

A. Kwa nini wao hawapendi vitendo vizuri? Tazama, Manu anavyoagiza, Vaidikaishchaiva karmabhih, ni muhimu kwa Sannyasis au maskofu kufanya kazi kama ilivyo fanyiwa wasia na Vedas, ambayo inahimiza ukweli uliofuatana na uadilifu. Wao wanaweza kuwachia kazi ya kula na kuvaa? Ikiwa wao hawawezi kuziwacha kazi hizi basi wao hawa angamii na kuwa si wenye dhambi

kwa kuziwacha kazi nzuri? Wao hawatakuwa wenye dhambi nyingi, ikiwa wao wanapokea chakula, nguo na mahitaji mengine kutokana na mwenye kuiendesha nyumba na wao wasilipe kwa njia yo yote? Kama macho ni ya kuonea, mashikio ni ya kusikilizia na yatakuwa hayana maana ikiwa hayafanyi hivyo. Katika njia hii hii, ikiwa makasisi hawahubiri ukweli wala wao hawasomi na kuyaeneza matumishi ya Vedas na maandishi mengine matakatifu, wao ni mzigo usiokuwa wa maana juu ya ardhi. Kuhusu kukiri kwao, hayo hayana maana kurihangaisha vichwa vyao na hotuba zao za dunia ya madanganyo na mambo kama hayo, ni wahubiri wa madhehebu haya ambawo ni hugeuka waongo na wenye kufanya madhambi, kujumlisha kufanya dhambi. Kitendo cho chote kunachofanywa na hudhaniwa ni sifa ya roho inayozaa matunda.

**Tofauti Baina ya Mungu na Roho.**

Wale wanafikiria kuwa roho ya mtu ni Mwenyezi Mungu, wanalala kwenye kitanda cha waridi cha ujinga; kwa sababu rohoni haina mwisho, yenye ujuzi kidogo na Mungu ni hawezi kumalizika, aliyeenea kote na mjuzi wa yote. Mungu ni wa daima na milele, mtakatifu, aliye macho daima, kabisa kwa tabia lakini roho wakati mwingine tu huwa huru na mara nyingine huweza kuathirika na vitendo vyake. Mungu maisha yuko juu ya ujinga. Mungu haumii maumivu ya kuzaliwa na kufa, 'ambayo roho huvumilia. Hata hivyo uwongo wao wakusomesha.

Q. Ati ni kweli maaskofu wako mbali na wajibu wa kazi; hawatumii moto kwaajili ya chakula chao au kugusa shaba kama pesa?

A. La, Mtu yule anaitwa Sannyasi au askofu, ambaye anamjua Mungu na ambaye amewacha kufanya vitendo vya uovu na ni mwenye tabia nzuri. Hivyo askofu ni mfanyaji wa uwema na asiyefanya vitendo vya uasi.

**Q. Kusomesha na kuhubiri kuna fanywa na watu tu wakawaida. Askofu au mtu wa dini hana cho chote kumhusu kazi hizi.**

A. Mtu wa kawaida anaweza kuhubiri ukweli na kusikiliza kwa kuongeza juu ya hayo; lakini wao hawana kuwa wasipendelee upande mmoja au hawana wakati wakutosha kufanya hayo kama askofu alivyo na wakati. Kwa mfano, ni wajibu wa watu, wanaoitwa Brahmanas (maaskofu makasisi). Kwa hivyo watu lazima wasomeshe na kuhutubu ukweli miongoni mwa wanaume na wanawake. Lakini Brahmanas hawapati wakati mwingi kama wanavyopata maaskofu wanaosafiri kwenda kuhutubu Brahmans wanapo tenda kinyume cha mafundisho ya Vedas, askofu tu anaweza kuyatazama na kuwaziwia wasifanye hivyo. Hata hivyo, ikiwa ni lazima kustaafu na kufuata amri.

Q. Ati ni kweli kuwa askofu lazima atumie usiku tu kwenye kijiji na si zaidi ya hapo, kama ilivyosemwa: 'Eka ratrim vased grame', & C.

A. Ni kweli kwa mujibu wetu, kwa sababu mtu hawezi kufanya uwema mwingi kwa watu kwa kukaa pahali pamoja kwa muda mrefu. Mwungano na pahali hapo

huzidi. Mapenzi na machukizo huzidi kwa ajili ya vitu vya hapo. Ikiwa kufanya uwema mwingi kuwa ni mwisho wa kuona kwa kuishi kwa muda mrefu pahali pamoja, basi ni kama ni kwa Mfalme Janak, ambako wakasisi wa amri ya Panch Shikha na maaskofu wengine walikaa kwa muda wa miaka mingi. Lakini kuwa usiishi pahali pamoja, ni uzushi wa watu wa madhehebu ya kisasa tu; kwa sababu ikiwa askofu anakaa kwa muda mrefu, basi vitimbi vyao vitaanza kujulikana na wao watamalizika.

Q. Ati ni kweli kuwa mwenye kuumpa askofu sadaka ya dhahabu atatiwa motoni kama ilivyosemwa ndani ya maandishi.

A. Pia ni kwa ajili ya wapinzani wa amri za jamii, wenye madhehebu na wenye ngano za dini za ki zimwi; kwa sababu ikiwa askofu anapata pesa, wao watakataa uwongo wao mwingi, ambao utawaletea hasara. Pia mawaidha ya askofu yatawafanya wawe huru kutoka na wenye kufuata madhehebu. Lakini kuomba kwao na vitu vyenginevyo vimo mikononi mwao wao watawaogopa wenye kutoa mbinu za kale. Hapo hufikiriwa kuwa ni vizuri na yenye sifa njema kutoa sadaka kwa wajinga na wenye kujipendelea wenyewe, basi hapana dhara yo yote au dhambi kuumpa mwenye elimu na maaskofu wenye ukarimu.

Mtu lazima aampe askofu namna mbali mbali ya vitu vya thamani, dhahabu na vyenginevyo vya thamani. Basi, yale yanayokatazwa ambayo yamekuwa ni mabishano hayana maana, ikiwa mtoaji atakwenda motoni kwa kutoa dhahabu kuumpa askofu, basi atakwenda peponi kwa kuumpa fedha, lulu, almasi, na madini mengineyo na mawe ya thamani. (Manu. 6.)

Q. Pandit au Brahmin wa kawaida amefanya makosa kukisoma kitabu, ambacho lazime kiwe: 'Yati haste dhanam dadyat': yeye atakwenda motoni yeye ambaye anaupita mkono wa askofu kwa pesa.

A. Kitabu hiki pia kimeandikwa na mjinga kwa kufikiria tu, ikiwa mtu anampa askofu pesa kwa kuziweka juu ya mkono wake, anakwenda motoni, yeye atakwenda peponi akiziweka kwenye miguu yake na kwa kuzifunga fundo katika kipande cha nguo. Basi mambo kama haya yakuagua tu hayana maana kukubaliwa. Kwa kweli ikiwa askofu akiweka pesa zaidi kuliko anazohitaji kufanyia mambo yake mwenyewe, yeye ataingiwa na uwoga wa wezi na kuwa na mwungano wa mambo ya dunia. Lakini yeye aliye mtaalamu, hawezi kufanya kitendo cho chote cha kujipendelea mwenyewe ambacho ni kinyume cha utakatifu, wala yeye hatajifunga na dunia, kwa sababu yeye ameshaziona na kuzifurahia raha zote alipokuwa akiendesha nyumba na kuwa mwanafunzi pia. Na yeye ambaye amekula kiapo cha amri takatifu cha kuwa mwanafunzi, hawezi kuangukia ya dunia hata kwa vyo vyote.

Q. Watu wanasema kuwa ikiwa askofu anakuja kwenye karamu ya kumkumbuka 'Shradaha', kama inavyoitwa katika Sanskrit, au amealikwa kula hapo basi manes hukimbia na kuanguka katika jahanam.

A. Kwanza, haiwezekani na ni uwongo kuwa mtu aliyekwisha kufa huja kwenye karamu, au kuwa chakula cha shradaha huenda kwa mababu waliokwisha kufa; kwa sababu ni kinyume cha mafundisho ya Vedas na hoja zake. Ikiwa wao hawaji kabisa, basi ni nani anaye kimbia? Vipi roho zinaweza kuja, ambapo zina zaliwa tena baada ya kufa kwa mujibu wa karama zao za uzuri na ubaya katika utawala wa sheria ya haki ya Mungu? Hivyo, ilikadi hii imetokana na watoaji ngano za zimwi na waombaji katika nguo za rangi, na yote kwa pamoja ni uwongo.

Kwa hivyo, ni kweli kuwa askofu anapokwenda kwenye karamu ya wafiwa iliyo fanywa kwa kinyume cha amri za Vedas na maandishi matakatifu, yata angamizwa na mwisho wake kuletwa, na madanganyo kujulikana.

Itakuwa taabu kwake kuishi maisha ya utakatifu na hataweza kuzizuia fikira zake, lazima asijiunganishe na amri takatifu tokea anapokuwa katika maisha ya uanafunzi. Lakini kwa nini yeye asifanye hivyo, nani afanye? Yeye hawi mtumwa wa mawazo, yeye ambaye anajua uovu wa tamaa za mwili na faida ya utakatifu. Nguvu zake zitangamia kama mafuta, kwa kusema, katika moto wa wangavu. Afya haina haja ya daktari na dawa, kama mgonjwa. Katika namna hii hii, mwanamume au mwanamke hawezi kuoa, kitu chake cha maisha ni kuwa kuendeleza sababu za elimu na dini tu, na mema ya watu wa dunia nzima, kwa mfano, amri ya wanaume ya Panch Shikha na Gargi na wanawake wengine wa kizamani. Kwa hivyo, watu waliofuzu vilivyo lazima wajiunganishe na amri ya ukarani. Ikiwa mtu asiye na hekima anakuwa askofu, yeye mwenyewe atajiangusha na kuwaangamiza wengine pia. Askofu aliyejitolea kabisa au 'parivrat' Sannyasi ni kama bwana mkubwa katika dunia, si kama mfalme anaheshimiwa na wale anawo watawala tu, lakini askofu anaheshimiwa kila pahala.

Moja katika uadilifu wa Chanakya unasema kuwa mfalme na mtu aliye na elimu hawawezi kuwa sawa sawa; kwa sababu mfalme anaheshimiwa katika nchi yake, lakini mtu mtaalamu ana heshimiwa na kustahiwa kila pahali.

Kwa hivyo, maisha ya mwanafunzi ni ya kujipatia elimu, mazoezi ya uadilifu, na kukua kwa mwili na mengineyo kama hayo yanayotakikana, maisha ya ndoa ni ya kutumika kufanyia kazi hasa iliyo ya bora zaidi; maisha ya kustaafu kwaajili ya akili timamu, habari za kuangalia sana, kuzidisha elimu, na kufanya ya kutubia; na kueneza mwangaza wa Vedas na maandishe mengine ya kweli, kufanya mazoezi ya kumcha Mungu na uadilifu safi, kuviwacha vitendo vyote vya nasi, kuhubiri ukweli na kuyakataa yenye shaka za watu katika ukweli. Lakini wale wasiofanya sawa sawa wajibu wa amri takatifu wa kuhubiri ukweli na kuonyesha njia ya kweli, huanguka kwenye uwema na kustahiki kwenda jahanamu. Kwa hivyo, askofu lazima afanye mema ya dunia kwa kuhubiri ukweli, na kuyatatua matatizo ya waongo, asomeshe Vedas na maandishi mengine matakatifu, na kuziendeleza sababu za dini ya Vedic.

Q. Jee wale wale pia huhesabiwa kuwa ni maaskofu ambawo wanaitwa Sadhus, Vairagis, Gosains, Khakis & C.? (Kuna tabaka mbali mbali za waliojitenga na ya dunia au masikini wa Kihindi.)

A. La. Kwa sababu hakuna shahada hata moja ya amri ya roho unaweza kuiona katika hawa. Wao huenda kinyume cha mafundisho ya Vedas, na kuheshimo mafunzo ya watawa wao wenyewe au wavumbuzi wa madhehebu yao zaidi kuliko yale ya Vedas. Wao huipandisha dini yao mpaka mbinguni.

Kwa kuolewa katika mipango ya uwongo wa madhahebu yao, wao huwavuta watu kwa werevu kufuata madhehebu yao kwa sababu za kujipendelea nafsi zao tu. Baada ya kutenda mema duniani, wao huwapoteza watu kupitia njia iliyo chini iliyohabirika na kujitosheleza wao wenyewe. Hapana shaka hata kidogo katika haya. Wao hawawezi kutambulikana katika midhamu ya dini. Wao peke yao ni wenye uadilifu, wanao jihini wenyewe na roho kubwa, ambawo wanajifanya wenyewe kuzifuata njia za uwema na kuwafanya wengine pia wafuate hayo; wao ambawo wanafurahia baraka za maisha ya sasa na kuifanya dunia pia ujifurahie, kwenda kwenye njia ya Mungu na kuwaonyesha wengine pia njia hiyo. Kwa ufupi kwaajili ya maelezo za amri ya jamii ya utakatifu. Sura inayofuata itaeleza kuhusu amri za ufalme.

**Muhtasari**

Sehemu hii ya maisha inatolewa kwaajili ya elimu, na ya pili kwaajili ya ulimwengu, ya tatu, kutoka mwaka wa 50, lazima utumika katika kustaafu, ambayo inahitaji kufanywa matukufu matano, ya dhana, kula mboga tu, kusoma na kusomesha elimu, kuwa mwenye huruma kwa wote, usiwe mpokeaji wa sadaka, na kuendelea kuchugua katika mambo ya roho. Mtawa anaweza kumweka mkewe pamoja naye au kumwacha kwa watoto wake wa kiume. Sehemu ya nne ya maisha katika kusomesha dini na kustaafu na kumfikiri Mungu kwa kutafakari, kuwa mbali na matamanio matatu, viz. kwaajili ya watoto, mali na ufahari. Mtu aliyestaafu lazima ende kutoka mahali pamoja na kwenda pahali pengine kusomesha ukweli, insafu, ukarimu, na amri nyinginezo za Mungu. Yeye mwanamke au mwanamume lazima aishi kwa chakula safi na vinywaji safi, na asimwumize kiumbe cho chote, asikasirike na mtu, bariki mtu hata akikulaani, funga nywele, vaa nguo ya zambarau, na kuweka vitu. Dini au uadilifu uzoezwe na kusomeshwa na unatiwa sahihi na tabia kumi viz. ustahmilivu, usamehevu, kujinyima, ukweli, usafi, kuwa bwana wa fikira, uwe mwenye busara, elimu, ukweli na bashasha.

Maaskofu wa kidunia tu wanazuwia kutoa zawadi waliojistaafu, nayo si kweli, kwa sababu hawa waliostaafu wanajua njia bora ya kutumia pesa. Brahmins au watu walio wataalamu peke yao lazima wajiunge na amri takatifu lakini si wengine, ilivyokuwa wao wanawekufanya mema zaidi ya dunia.

# SURA VI
## WAJIBU WA KIFALME

Manu, mtoaji mkuu wa sheria za zamani, anasema kuwaambia maaskofu waliomwendea yeye kuuliza umuhimu wa sheria, kuwa, baada ya kueleza wajibu wa tabaka nne za watu na vyuo vinne vya jamii 1. Yeye ataendelea kufahamisha yale ya kifalme, ni kusema, shahada zipi ni za kifalme, ana uwezo gani, na anazo sababu zipi za kuweza kufanikiwa, VIII, 1. Yafuatayo ni njia ya 2. Vipi mpigana vita anasomeshwa na kufundishwa kama Brahmin aliyesoma vilivyo, lazima aiendeshe nchi kwa mujibu wa katiba kwa haki: ib. 2. Bwana anasema, Rig. III, 38. 6.

Mfalme na watu waungane na kuunga Baraza tatu kuhusu mambo ya Elimu, Dini, na Utendaji wa Kazi. Kwa ajili ya maslahi yao, kwa kuiendeleza elimu na kwa kulinda shirika la serekali na nchi, ambayo inaupamba ustaarabu wa watu kwa taalimu, uhuru, dini, uadilifu na mali.

**Ath. K. 15, Anu. 2. Varg. 9M. 2.**
**Ath. K. 19, An 7, Varg. 55, M. 6.**

Halmashauri au Baraza tatu, katiba, pamoja na siasa ya serekali kuhusu vita na amani, na jeshi lazima walinde ustawi wa serekali. Kuhusu mfalme na wafuasi, mfalme lazima atake kuwa na kiongozi mkuu anayefuata sheria, za katiba za mahakama, na wafuasi wengine wafuata amri za serekali. Kwa maneno mengine, mtu mmoja peke yake tu asiwe na nguvu zote za serekali; Mfalme kuwa ni mkuu wa Baraza, lazima iwe chini yake; Mfalme na Baraza lazima zote mbili ziwe masuulia kwa watu, na watu lazima wawe chini ya Baraza. Ikiwa haya hayafuatwi, kama Shalpath inasema.

Kand 13, Prapathak 3, Barh 3, Kandika 7, 8, shirika linalotawala na kuwa huru kutokana na watu na lenye nguvu zote, na kuimiliki nchi, itawaangamiza watu. Kuwa mfalme wa peke yake na mwenye uhuru kamili huwa mwenye kudharau kazi zake na huwaangamiza watu. Yeye huwakandamiza watu na, kama ilivyo, huwala. Kwa hivyo, mtu ye yote asiwachiwe serekali peke yake. Mfalme wa pekee huwaangamiza watu kama simba na kama wanyama wengine wanavyo waangamiza viumbe wenye siha na nguvu. Yeye hawezi kumwachilia mtu anyanyuke na kuwa juu yake. Yeye atawaibia wenye mali, atawanyanganya na atawatia adabu bila ya kuwa na hatia yo yote ili atimize muradi wake.

Atharvaveda, K. 6, Anu. 10, V. 98, M. 1. Mfalme amteuwe msimamizi mkuu, ambaye ni mwendelezaji mkubwa wa mambo ya jamii za watu, ambaye ataweza kuwashinda maadui, ambawo hawawezi kushindwa na adui, yeye ambaye anamshinda mfalme kwa uzuri, yeye ambaye anapendeka sana, yeye mwenye nguvu zaidi za kusimamia, yeye ambaye ni mkarimu na mwenye sifa njema, yeye ambaye anatenda vitendo vizuri, na mwenye tabia nzuri, mwenye kujihishimu, na mwenye uhakikisho ambaye anaweza kupata pakukubaliwa, na ambaye ni mashuhuri sana.

anaweza kupata pakukubaliwa, na ambaye ni mashuhuri sana.

**(Yaj, 9, 40.)** Enyi watu na mfalme aliyesoma, ufanyeni ulimwengu huu uwe hauna maadui, fanyeni haki kwa kumchagua kwa pamoja msimamizi wa mfalme juu ya bwana, ambaye ni rafiki wa wote, aliye na elimu ya kutosha nahaki, aliye daima mbali na mapendeleo, kulinda mali za watu na serekali yenye ustawi ya utawala wa dunia nzima, yenye watu wengi wenye elimu, ili kuendeleza sababu za mafanikio.

**(Rig, I, 39, 2.)** Bwana anasema; Ewe mwenye kutawala, fanya silaha zako, bunduki, mabomu, bunduki za mrao, mikuki, panga, jambia, na silaha nyinginezo ziwe zinye nguvu na zenye maana katika kuwaangamiza maadui na kujihami na mashambulio; na kuponya majeshi yako yawe yenye kusifiwa na yenye uwezo ili uwe mshindi wa daima. Lakini fanya hizo silaha na mavazi ya askari yasiwe ya maana sana kwa yule ambaye ni wakulaumika na asiye na vitendo vya haki. Kwa ufupi, utawala hustawi na kuendelea ikiwa wale watu wake ni waadilifu. Kuchaguliwa kwa watu wenye elimu kuwa ni maafisa wa elimu na watu wenye imani na walio wataalamu kuwa ni wakuu wa baraza na watu majabari kweli na wenye sifa vitendo, na silika, kuwa ni wasimamizi wa baraza lenye amri ambalo linaleta mafanikio ya namna zote na maendeleo. Watu wote lazima watii na wafuate sheria na mipango ya maongozi ya serikali kwa wote pamoja na baraza zake tatu. Wao wakubaliane katika kazi zote ambazo zinaleta faida kwa watu. Wao inawabidi kufanya yale yenye faida kwa jamii yote na yote yale yanayohusika na dini. Wao wanao uhuru wao wenyewe kutenda katika mambo yao ya ndani.

**Raisi au Msimamizi.**

Shahada au sifa za Raisi ni:- Yeye lazima awe mwenye kuendeleza utajiri, mwepesi kama umeme, mwenye mapenzi kwa wote kama hewa na maisha. Yeye afahamu nini watu, wanataka, asipendelee upande wo wote kama hakimu asiyependelea; awe mwenye kuendeleza haki dini, na elimu kama jua; adui wa kiza cha ujinga, yasio ya haki, mwangamizi wa maovu kama moto; mzuizi wa maovu kwa njia nyingi kama Varuna au mzuizi; mwenye kutoa faraji kwa watu walio wazuri kama mwezi; na mjazi wa mali kama bwana wa mali. Mtu mwenye kuwa na sifa hizi, lazima achaguliwe kuwa Raisi.

Mtu yule ni imara kuwa Raisi wa jamii au baraza, ambaye ni thakili kama jua, ambaye analeta khofu katika mioyo wote kwa nguvu zake na anawahukumu wao, na ambaye hawezi kutazamwa na mtu duniani kwa jicho la hasira.

Mtu yule anafaa kufanya Raisi ambaye anaweza kuwashinda waovu, na anawo uwezo mwingi kama moto, hewa, jua, mwezi, dini, na ambaye anauendeleza utajiri.

**Mfalme**

Nani ni mfalme wa kweli? Anasema Manu, VII, 17 - 19, 24 - 28, 30, 31,.

Yule ambaye ni malipo, ndiyo mtu hasa, kama ilivyo, ndiye mfalme. Pia (malipo ya sheria) ni mtoaji wa haki na mtawala wa wote; ni mwakilishi na mdhamini wa kazi za tabaka nne za watu na vyuo vyao vinne. Manu, VII, 17.

Inawahukumu watu wote, na ni mlinzi wa raia wote. (sheria ya haki ya malipo) huamka watu wanapolala. Hivyo, watu wenye busara huiona sheria au malipo yake kuwa ni uwema au ni dini, ib. 18.

Sheria inapofuatwa kwa mujibu wake hasa inawafurahisha watu wote; lakini inapatolewa bila ya kufikiria, inamwongamiza mfalme kutoka pande zote. ib. 19.

Kutokuwapo kwa haki inawaharibu watu wa tabaka zote na huzivunja baraza na vyuo vyote. Kutokuwapo kwa haki huwafanya watu kuwa na uchungu.

Wao huanza kuzidharau kazi zao na kufurahia amani na furaha ambapo ustadi wa haki kama mtu wakutisha mwenye rangi nyeusi na macho mekundu anawinda miongoni mwa watu kuangamiza uhalifu, na ambapo mtoaji wa haki au anayetia adabu ni mwadilifu na mtaalamu.

Wataalamu humhisabu yeye kuwa ni hakimu, ni mtu aliye sawa wakutia adabu, ambaye ni wa kusema kweli, anayetenda baada ya kufikiria, yeye ambaye ana busara, na yeye ambaye ni mfalme raisi mtaalamu katika kupata mafanikio ya uadilifu, mali na raha. ib. 26.

Mfalme anayetawala kwa haki, anaendeleza dini, mali, na raha za maisha. Lakini mfalme anayekalia kiti cha uhakimu, ambaye ni mwenye anasa nyingi, mjanja, thakili, na mwenye akili fupi, anaangamia kwa haki ya kumlipizia kisasia. ib. 27.

Kama haki ni mbaya sana na pia ni njema haiwezi kushikwa na mjinga, na asiye mwadilifu. Ina mwangamiza mfalme khaini. ib. 28.

Kwa sababu yeye aliyekuwa hasaidiwe na watu wenye busara, ambaye si mtaalamu, asiekuwa na mazoezi, mwenye uchu, asiye na akili, hawezi kutoa amri ya adabu au kuweka sheria kwa haki. ib. 30.

Lakini yeye peke yake ni msafi wa akili, tabia njema, anayekuwa na marafiki wazuri, anayetenda vitendo kwa mujibu wa sheria za uadilifu, na kusaidiwa na nasihia za watu hodari, na ambaye ni mwenye busara anauwezo wa kuweka sheria na haki kwa vilivyo. ib. 31.

**Wajumbe Wakuu.**

Kwa haya Manu, anasema, XII, 100, 110 - 115. Watu wanavyojua Vedas kwa vilivyo na maandishi mengine matakatifu, wenye ujuzi wa kutosha katika mambo yao, waadilifu, wenye uwezo wa kuweza kuziziwia fikira zao na wenye tabia njema, lazima wachaguliwe katika afisi nne (1) amiri jeshi na mwenye amri ya mazao yote (2) Mkuu wa polisi na uendeshaji wa sheria (3) mwenye nguvu juu ya wote (4) mwenye amri za kifalme, haya ni kusema, amiri jeshi, Mkuu wa

kuendesha kazi, mkuu wa sheria, na mfalme lazima wawe wataalamu katika elimu za kuhusu kazi zao.

**Baraza.**

Amri au hukumu ya baraza za watu kumi walio wataalamu, au ikiwa hawapo, basi watu wataalamu, lazima isiwe kuwa ni makosa au isibishaniwe na mtu ye yote. ib. 110.

Wanachama wa baraza hili lazima wawe wataalamu wa Vedas nne, elimu halisi, Nirukta au mfuasi wa Vedic, sheria na maandishi mengine matakatifu. Lakini ikiwa wao ni wanafunzi, wanaume wenye jamii, na mtu aliyejitenga na ulimwengu, hapo itakuwa baraza yenye sifa njema ambapo itakuwa haina watu waliopungua kumi. ib. 111.

Maamuzi ya bunge iliyo na watu watatu waliisoma na kuijua vilivyo Rig, Yajur, na Sama, Vedas, hawawezi kukosewa na mtu ye yote.

Pia, hata hukumu ya maslaha katika sheria na mtu mmoja wa dini au Sannyasi ambaye anaijua Vedas yote na wa kwanza kuliko wote wale waliozaliwa tena, na ihesabiwe kuwa ni sheria bora zaidi; kwa sababu iliyofanywa na majlisi ya milioni na milioni tatu za wajinga basi isikubaliwe.

Baraza lisifanyike kwa watu wale wanaoona kwa maelfu, ambawo ni wenye vilema vya elimu ya Vedas, mazoezi ya wanafunzi, uadilifu na uwema mwingine wa adabu, na fikira zilizo sahihi, na wale walio Brahmin kwa kuzaliwa lakini wanaishi kama Shudras. ib. 114.

Sheria inayosomeshwa na wajinga wasio wataalamu, wajinga wa kutojua usimamizi wa Vedas, wasikubaliwe kabisa. Kwa sababu namna mia za dhambi zinawazonga wao, wale ambawo wanafuata mafunzo ya wajinga Manu, XII, 115.

Kwa hivyo, watu wajinga wasichukuliwe katika baraza hizi tatu za juu, ya elimu, ya dini, na ya sheria au ya uendeshaji wa kazi; lakini kinyume na haya zichukue watu walio wataalamu na waadilifu.

**Wanachama wa Mabaraza.**

Kwa sababu, watu tena hapo na hapo tu huwa wafalme, Ma-Raisi na wanachama wa baraza ya watawala, wanapokuwa wamesoma matawi matatu ya elimu ya Vedas nne, kwa majina ni, wajibu, ucha Mungu na falsafa, na kuzijua vilivyo; sheria za kiroho za haki na sheria, mantiki, uchunguzi wa tabia za Mungu viz, elimu iliyo sawa ya kujulia, vitendo, na asili ya Mungu, kwa maneno mengine, sayansi ya utakatifu, mila na tabia za watu, na kufanya uthabiti na maswali.

Wana haraza wote na raisi lazima wazitiishe fikira zao na waweze kuzimiliki, daima waufuate uadilifu na kuuepuka uovu, na kuwa fanya wengine pia kuwa mbali nayo. Kuukazanisha miili yao, wao wajizoeze yoga ua taamuli; kwa sababu, yeye ambaye hawezi kuziamrisha fikra zake, kama, matakwa,

tamaa, na mwili wa kihayawani, ni kuwa, kama ilivyo, raia zake mwenyewe, hataweza kuwa shinda raia zake yeye mwenyewe ataweza kuwadhibitika.

Kwa azma thabiti, yeye lazima auepuke kwa vyema uovu namna kumi unaotakana na mapenzi ya raha na uovu namna nane za uovu zinazotokana na hasira, ambapo ni dhiki kwa mtu kuepukana nayo. Yeye pia awasaidie wengine watokane nayo. ib. 45.

**Uovu wa Hasira**

Kwa sababu, mfalme ambaye anajiangamiza katika maovu kumi yanayo zaliwa na raha za mapenzi hupoteza uadilifu na mali, ni kama, utawala, utajiri na mambo mengineyo. Yeye ambaye anajiangamiza katika uovu wa namna nane unaotokana na hasira, huupoteza hata mwili wake. ib. 46.

Uovu wa namna kumi unaotokana na mapenzi ya raha ni (1) kuwinda au riyadha; (2) kucheza kamari, chowpar (karata) na michezo kama hii; (3) kulala mchana; (4) kuzisikiliza hadithi za mapenzi; jambo la aibu au kuwasengenya wengine; (5) kuwaingilia wanawake; (6) kutumia vinavyolevya, - divai, afyuni, bhangi au kinywaji kinacho tengenezwa kwa majani ya bangi, au kuvuta majani ya bangi, kuvuta kasumba, na vyenginevyo vinavyolevya; (7) kuimba; (8) kupiga vyombo vya muziki; (9) kudansi au kutazama dansi, kwenda kwenye ngoma; na (10) kuzurura ovyo ovyo tu. ib. 47.

Uovu wa namna nane kutokana na ukali ni (1) Kusengenya (2) kuzini i.e. kumwingilia mke wa mtu kwa nguvu, (3) kuchukia (4) wivu, ni kama, kutoweza kumwona mwenzako anapata. (5) kutafuta makosa kuonyesa sifa uzuri kuwa ni makosa na makosa kuwa sifa nzuri (6) kufuja, ni kama kusema kupoteza pesa na mali nyinginezo katika njia zisizo za uadilifu. (7) kusema kwa ukali, na (8) kuwatia adabu watu bila ya kuwa na makosa makubwa au kuwaita majina. ib. 48.

Yeye lazima awache tamaa ya mali, naye ni fikra ya mtaalamu mzizi wa uovu unaomwangukia mtu na inatokana na raha ya furaha na hasira za ghafla, ib. 49.

Uovu mkubwa unaotokana na raha ya mapenzi ni - 1. tabia ya kulewa au kutumia vitu vya kulevya, 2. kucheza kamari au kucheza dadu, 3. usuhuba mwingi wa wanawake, 4. kuwinda. Tabia hizi nne ni mbovu na chafu sana. ib. 50

Uovu unaotokana na mapenzi ya furaha na hasira kali, uovu wa namna tatu unaoleta maumivu makubwa, kwa majina ni, 1. kuwatia adabu watu bila ya makosa, 2. kutumia maneno makali, na 3. kutumia pesa katika njia zisizo halali. ib. 51

Uovu namna saba unaotokana na kujiingiza sana na raha za uchu na hasira nyingi zisizozuilika, huzidi kuchukiza kadi zinapoendelea mbele, viz. kutumia pesa bila ya madhumuni thabiti si mbaya sana kuliko maneno makali, maneno makali kuliko kutokuwapo kwa haki, kutokuwapo kwa haki kuliko kuwinda, kuwinda kuliko usuhuba na wanawake, ufisadi kuliko kucheza kamari, kucheza kamari na kulewa, ni uovu mkubwa kuliko uovu wote. ib. 52.

Kanuni katika kadhia hii ni bora kufa kuliko kushirika vituko viovu. Kwa sababu, ikiwa mtu mwenye vituko viovu ataishi maisha marefu, yeye atafanya dhambi zaidi na atazama chini zaidi katika shida, kuugua maumivu zaidi. Lakini ikiwa mtu hajazoea kufanya vitendo vya uovu anakufu, yeye atakuwa amefurahia raha. ib. 53.

Kwa hivyo, mfalme hasa na raia zake kwa jumla lazima wajiepushe na kuwinda kulewa, na tabia nyingine mbaya; lakini, kinyume cha mambo ni haya, kuwacha yenye uovu na furaha ya uchu na kujipatia sifa zenye uadilifu, tabia, na taratibu za kazi, wao lazima wafanye kazi nzuri.

**Mawaziri**

Watu wa namna gani lazima wawe wanachama wa mahakama ya kifalme na mawaziri wake, inaitaniwa na Manu, VII, 54 - 57. 60 - 64.

Mfalme awachague mawaziri saba au nane walio zaliwa katika mipaka yake na nchi yake, wajuzi wa Vedas na maandishi matakatifu, shujaa na hodari, na mwenye azimio yasiokubali kushindwa, waliotoka katika ukoo mzuri, mwenye elimu, mkubwa au muhimu, mwadilifu, na mwenye hekima. (M. 7.54.)

Kwa sababu, bila ya msaada maalum hata kitendo kidogo ni taabu kutendeka na mtu peke yake. Mambo kama yalivyo, vipi kazi kubwa ya serekali itaweza kufanyika na mtu peke yake? Kwa hivyo, ni mpango mbaya kumfanya mfalme peke yake kukadidhiwa na mambo yote ya serekali katika mikono ya mtu mmoja peke yake. ib. 55.

**Maudhui ya Kushauriana.**

ib. 56. Raisi lazima kila siku awashauri mawaziri wake walio hodari na wataalamu kuhusu mambo ya serekali, kama 1. kuleta amani na watu wengine, 2. vita, 3. kuweka nidhamu, 4. ustawi kumhujumu adui mwovu katika wakati mwafaka wa mtu, 5. kuhifadhi matumishi ya serekali, kuwaweka kwa nidhamu jeshi, 6. kuweka amri katika majimbo yanayotakiwa na kuyafanye yawe na amani na mbali na hatari, kazi kama hizi lazima zifikiriwe na fikira zake ziwe wazi.

**Uamuzi Kwa Watu Wengi.**

Yeye lazima aulize shauri za wana wa baraza kuhusu mambo ya serekali kwanza mmoja mmoja tena kwa pamoja na kukata shauri kwa kupiga kura za watu wengi kwa faida yake mwenyewe na wengine. ib. 57

**Mawaziri, Wenye Maarifa.**

Manu, 7, 60. Yeye awachague mawaziri wengine, walio imara, wenye hakima wenye tabia timamu, wenye asili kubwa, wenye uwezo kupata vitu vinavyo hitajiwa, na aliyejaribiwa vyema na maarifa.

(M. 7.61). Yeye lazima awaajiri maafisa na wanaume wengi wenye nashati,

wenye nguvu, walio wenye akili na waliochaguliwa, kama inavyotakikana kwaajili ya kutekeleza kazi za nchi kwa ukamilifu.

**Mawaziri wa nchi za nje na Nyumbani.**

Yeye lazima awachague watu walio hodari, shujaa, wenye nguvu, watu waadilifu wa ukoo mzuri, kwenye wadhifa wa kazi muhimu; na wenye haya, na watu waoga kwaajili ya kazi za ndani za idara za nyumba.

**Balozi**

Yeye amchague mtu yule kuwa balozi wake anaye toka katika jamii ya kujulikana mwenye nia za ukweli na maana zake na mwenye tabia njema, mwadilifu wa moyo, mwenye uwezo wa kuyatekeleza matukio yatayokuja, mwenye uwezo wa maandishi na bingwa katika kazi zake za ubalozi.- ib. 63.

Balozi lazima awe mwenye kushikilia sana kazi za serekali, apende kazi zake, awe hukhlisi, msawi wa moyo, awe hodari katika kazi za kukumbuka sawa sawa, bila ya kusahau mambo yaliyopita zamani, kutenda kwa mujibu anavyotakiwa na mji na wakati, mzuri wa sura, hodari na mlumbaji - ib. 46. Mtu mwenye sifa hizi anastahiki kuwa balozi wa mfalme.

**Maofisa na Majukumu Yao.**

Manu, VII, 65, 66, 68, 70, 74 - 78. imeeleza namna za watu na kazi ambazo wapewe wao:-

Waziri mkuu lazima ahakikishe kuwa haki inafanyika katika kutoa adabu, na kuwa isitolewe adabu isiyo ya haki. Idara ya fedha na kazi za juu za serekali lazima ziwemo katika mikononi mwa mfalme. Baraza ya serekali lazima lirakibishe kazi zote. Nguvu za kuleta amani au urafiki na mji wo wote au kutangaza vita akabidhiwe balozi au waziri wa mambo ya nje. 65.

Ni balozi ambaye huleta mwungano na kukata mwungano na kugawanya na kutengana waovu katika ululivu. Yeye lazima afanye mambo ambayo yataleta mtengamano miongoni mwa maadui. 66.

Raisi, mawaziri wote au wana wa baraza, balozi na mawaziri wengine lazima wahakikishe hila za mfalme mwenye hasama na watu wake, na kujihifadhi vyema ili wasije wakaleta dhara au shida kwenye nchi yao. 68.

Yeye lazima awake watu wake katika nchi mandhari mazuri ya mwitu, mali na nafaka; kati kati ya haya yeye afanye ulinzi wa namna nyingi, ilivyozungukwa na wanajeshi, iliyojengwa kwa udongo, iliyozungukwa nalindi la maji na mwitu pande zote, iliyozungukwa na jeshi kote, na kuhifadhiwa na milima kote. Kati kati yao, yeye afanye mji wake, ambawo umezungukwa na boma. ib. 70.

Kwa sababu, mtu mmoja tu aliye na mkuki hapo anaweza kuwapinga wanaoshambulia mia, na maaskari mia waliowekwa hapo wanaweza kupigana na maadui elfu. Kwa hivyo ni muhimu kujenga ngome. ib. 74.

Boma hilo lipewe silaha nyingi na makombora, pesa na vyakula, magari na vitu vya kusafiria na Bramins wataalamu wanaostahiki na kuhubiri mashine na namna mbali mbali za zana, majani, malisho, maji na mahitaji mengineyo. 75.

Katikati ya ngome hilo, yeye ajenge nyumba ya kuishi inayopata maji, na kupambwa na miti, na maua na vitu vinavyo lindwa kwa njia zote, muafaka kuishi humu wakati wote, iliyo pakwa rangi, na iweze kuwa na ofisi zote za serekali. 76.

Baada ya kumaliza masomo yake katika maisha ya uanafunzi, yeye lazima aoe *mwanamke mmoja tu, mzuri, mkamilifu,* wa *kuvutia, aliye zaliwa katika* jamii la kisharifu wa tabaka la kijeshi, mchangamfu wa tabia, anaye elekezana naye katika elimu, tabia na harakati. 77.

Yeye lazima aweke kasisi na askofu, kwa sababu wao watafanya muhanga wa moto, kuabudu kila baada ya wiki mbili, na ibada nyinginezo za dini za hiyo nyumba; na yeye mwenye lazima awe ameshughulika na kazi za serekali, kuziendeleza kwake kwa vizuri, ni kama ibada yake, kutafakari na vitendo vyengine vya ibada, ambapo yeye atumie usiku na mchana wa maisha yake ili kazi yo yote isije ika haribika. 78.

**Ushuru au Mapato ya Serekali.**

Yeye apate ushuru wake wa mwaka kutokana na mkusanyaji mwadilifu, na Raisi - mfalme na machifu wa kubwa, na baraza lote kwa jumla wao wote lazima watende yale yaliyo sawa na nadhari ya Vedas na wao wawe wazuri kwa raia loco parentis. Manu, VII, 80.

Baraza la serekali lazima liwachague maofisa wanao kagua kazi mbali mbali za serekali. Itakuwa wajibu wao kuona kuwa wafanya kazi wote wa serekali katika afisi mbali mbali wanafanya kazi zao na kutimiza wajibu wao kwa mujibu wa sheria na kanuni za nchi (serekali). Wao wa heshimu ikiwa wanafanya kazi vizuri na kwa bidii na wawatie adabu kwa haki ikiwa wao wanatenda kinyume cha amri. ib. 81.

Kueneza mwangaza wa Vedas wakati wote, ni mali isiyoweza kwisha ya wafalme, mfalme na baraza lazima wamhishimu vyema yule anayetoka kutoka chuo kikuu (Gurukul) baada ya kumaliza masomo yake ya Vedas na maandishi matakatifu wakati anapokuwa mwanafunzi. Wao pia wawahishimu kua wataalamu wafunzi. ib. 82.

Njia hii itaendeleza elimu katika utawala na kuleta mafanikio makubwa kwa watu. Wakati wo wote mfalme aliyekuwa chini ya himaya ya watu wake anapoitwa kupigana na mtu mwingine, sawa na yeye, aliye wa chini au wa juu kuliko yeye; yeye akuita wajibu wa kijeshi akilini mwake, asikatae kuingia vitani na yeye na lazima apigane kwa ushujaa ili ajipatie ushindi. ib. 87.

Wafalme wanopigana katika vita kwa nguvu zao zote, bila ya kuogopa na kugeuza migogo yao, ili kuwa ua adui, hupata furaha. Wao wasirudi nyuma kutoka kwenye vita. Hata hivyo, kumshinda adui, ni sawa kujificha na alipo yeye;

kwa sababu, mtu lazima awe na hila kama hizo ili aweze kumshinda yeye. Wao wasishindwe upesi au kujiangamiza kwa upuuzi kama simba anapounguzwa na uchungu wa risasi ya silaha. ib. 86.

**Sheria za Ushujaa.**

1. Wanajeshi, kakiziweka akilini mwao sheria za ushujaa au kanuni watu waadilifu, lazima wasipigane vitani, na mtu ambaye amesimama hapa au pale, kama mwoga, kama kuunganisha viganja wakati wa kusalim amri kama nywele zinavyoregea, kama kukaa, na kusema "Mimi ni mkimbizi; (2) kama kulala, kama kuzimia, kama kuwa utupu, kama kuwa bila ya mikono, kama ni mtazamaji wa vita, kama ni sahibu wa adui; 3. kama kuumwa na maumivu ya majaraha; kama mwenye huzuni, kama yule aliyeumizwa vibaya, kama mwoga anavyotishika, na kukimbia. ib. 91, 92, 93.

Lakini watu kama hawo wachukuliwe na kufanywa mahbusu, na wale ambawo hawajambo kidogo miongoni mwao, basi lazima watiwe jela. Wao wapewe chakula na nguo za kutosha. Walioumia wasichokozwe ili wasisikie maumivu. Wao wapewe kazi ambazo wataziweza. Lazima ifahamike kwamba kuwa katu wasiumizwe wanawake, watoto, wazee, wagonjwa, au waliopatwa na msiba. Watoto wao lazima watazamwa na kusaidiwa kama wako mwenyewe. Wanawake zao pia waangaliwe na kuwekwa kama dada na ndugu wa kike wanavyowekwa bila ya kuwatazama kwa jicho la uzinifu. Amani inapokuwa imesharudi vyema, wale watu ambawo hawatakiwi kunyanyua silaha tena, lazima waachiliwe huru kwa hishima na kupelekwa makwao na kwenye nchi zao. Lakini wale wanaofikiriwa wataleta matatizo ya amani, wao lazima wawekwe kuzuizini.

Askari anapokimbia cheo chake kwa ajili ya hofu vitani, lazima atiwe adabu anapopatikana na hatia ya uhalifu kwenda kinyume cha serekali; yeye atajichukulia matokeo yote ya vitendo viovu vya mtu mwenye amri zote za jeshi. ib. 94.

Bwana wake anajichukulia sifa ambazo zilikuwa zimpe yeye furaha kote hapa na baadaye pia. Ikiwa mkimbizi anauliwa, yeye hapati heri, yeye hupoteza matunda yote ya vitendo vyake vizuri. Yeye hapati sifa ambazo zinapatikana na yeye mwenye kupigana kwa hadhi kwa mujibu wa amri ya vita. ib. 95.

Sheria lazima isivunjwe na amiri jeshi au askari ambaye ameyateka magari, farasi, tembo, miavuli, pesa, nafaka, ngombe na ngombe wa maziwa, wanawake, na vitu vyote vya namna nyingine, na chupa ya siagi safi, mafuta na maji mengine azipokee kuwa kama ni zawadi zake za sheria za vita. ib. 96.

Lakini wanajeshi wampe mfalme sehemu moja katika kumi na sita ya zawadi zao. Mfalme pia awape maamiri jeshi na maaskari sehemu moja ya sehemu kumi na sita ya ngawira iliyotekwa kwa pamoja na majeshi. ib. 97.

Wale waliouliwa vitani sehemu zao zipewe wale walio jamaa zake kama wake na watoto wao. Wake zao walio wajane na watoto wao maskini lazima watazamwe na kulipiwa na serekali. Watoto wanapo baleghe, wao wapewe kazi

kwa mujibu wa uwezo na nguvu zao. Yeye ambaye anapenda kuona nchi yake inaendelea, heshima, mafanikio, neema, na maendeleo ya ufalme, katu asizivunje sheria za vita.

**Wajibu wa Watawala.**

Mfalme na baraza la nchi litake 1. kupata yale waliokuwa hawana, 2. kukilinda vyema kile kilichopatikana 3. kuzidisha mapato. 4. kuzidisha utajiri kwa kuendeleza elimu na dini, kuwapo wanafunzi na wahubiri wa njia ya Vedic, na kuwasaidia mayatima wasiojiweza na maskini. **(Manu, VII, 99.)**

Yeye lazima ajaribu daima bila ya uvivu kutimiza tabaka nne za kiapo au wahii watabaka la kijeshi.

Yeye ajaribu kupata kitu hata kwa adhabu kile ambacho hawezi kukipata, kukitunza alichokwisha kipata, kukizidisha kile kinachotunzwa kwa hamu na mzidisho wa namna nyingine wa kisheria, na kutumia kulicho zidi katika mali hiyo daima kama ilivyoelezwa hapa juu. ib. 101.

Yeye asimfanyie mtu ye yote ujanja, bali atende mambo ya iklasi katika mambo yake na daima awe macho na ni hadhir, kuikamata uhalifu wa wengine kuipusha hatari zake hapo. ib. 104.

Adui hata moja asijue udhaifu wake au mahali panapoweza kupigwa, lakini yeye ajue sehemu zisizo za nguvu za maadui wake. Yeye azifiche sehemu zake ambazo zinaweza kutekwa na adui kama kasa anavyovificha viungo vyake kutokana na hatari. ib. 105.

Kama korongo anapoangalia kwa makini apate fursa ya kukamata samaki, basi mwache yeye atafakari juu ya mali aliyoikushanya; baada ya kuizidisha hizo mali zake, mwache azijaribu nguvu zake kama simba anapotaka kumhijumu adui; wache awaangukie adui kama chui mafichoni, mwache awe mara mbili kuliko sungura anapokabiliwa na adui mkali, na tena amhujumu kwa ghafla. ib. 106.

**Maongozi**

Kwa hivyo, raisi mwenye hamu ya kuendelea na kufuzu awahukumu wote wale waliofanya makosa makubwa, wahalifu, wezi katika nchi kwa 1. msamaha. 2. zawadi, 3. mgawanyiko; na hata haya hayafaulu kuwafanya wakubali, basi waletwe kwenye hukumu ya 4. nguvu kwa silaha. ib. 107.

Kama mkulima anapoondoa kapi na hawezi kuyaharibu mazao yake, basi mfalme pia awaangamive wahalifu na wezi na kuihami nchi. ib. 110.

Mfalme ambaye bila ya kujalia anawaangamiza raia zake kwaajili ya kupenda raha, basi ataangamia upesi kabla ya kifo chake pamoja na jamaa zake na kutokuwa na nchi yake tena. ib. III.

**Uangamiza wa Utawala.**

Kama udhaifu wa mwili huyakata maisha ya wenye roho, basi hata maisha ya wafalme pia, ni kusema kuwa nguvu zao na vitu vyao, pamoja na jamaa na mali zao, huangamizwa kwa kudhoofishwa na watu. ib. 112.

Kwa hivyo, mfalme na watawala wa utawala wake lazima wajaribu kuifanya serekali yao ifaulu, na mambo ya utawala yafanywe kwa uangalifu. Furaha ya mfalme huyo huendelea kuzidi yeye ambaye amejishughulisha kwa njia zote kuihifadhi nchi yake na raia zake. ib. 113.

**Usimamizi**

Kwaajili hii, yeye awe na afisi ya serekali baina ya wawili, watatu, watano na vijiji mia, kuwa weka humo maafisa wake ambawo wana uwezo wakutosha wa kuiendesha kaziza serekali. ib. 114.

ib. 115. Chifu mmoja achaguliwe kwa kila kijiji, na mwingine kwaajili ya vijiji vyengine kumi, watatu juu ya vijiji 20, wa nne kwaajili ya vijiji 100 vya mji, wa tano kwaajili ya vijiji 1,000 vya mji.

Kama ilivyo sasa kuwa pana Patwari mmoja katika kijiji kimoja, au thana; kituo cha polisi katika vijiji kumi kama hivyo, na thana kubwa kwenye vituo viwili vya polisi, na zaidi ya thana tano kama hizo thanas moja ni tehsil au afisi ya kupokea kodi za serekali na zaidi ya tehsil 10 kuna afisi moja ya wilaya. Mpango huu wote wa namna ya kuiendesha serekali umetolewa katika Manu yetu na watoaji wa sheria wengine.

Yeye afanye mpango wa kutawala kwa mujibu wa ilivyo elezwa hapa juu na kuamrisha kuwa mkuu wa kijiji kimoja kila siku lazima apeleke habari kwa siri kwa bwana wa vijiji kumi yote yale wa uhalifu na kuvunja sheria yaliyotokea katika kijiji chake.

Kwa njia hii hii, maafisa wa vijiji kumi wapeleke habari zao kwa maafisa wa vijiji 20 yale yaliyotokea katika vijiji kumi vilivyo chini yake yeye. ib. 116.

Afisa aliyekuwa wa vijiji 20 lazima apeleke habari kila siku yaliyotokea katika vijiji 20 kwa mkuu wa vijiji 100. Mkuu wa miji 100 apeleke habari zake kila siku yanayotokea katika wilaya yake kwa mkuu wa miji 1000. ib. 117

Maafisa watano wanaoangalia miji 10 lazima wapeleke habari kwa mkuu wa vijiji 100, na wakuu kumi wa vijiji 1000 kila mmoja alete habari ya yote yanayotokea kila siku kwa mtawala wa vijiji 10,000 na kwa Baraza la serekali ya vijiji 100,000. Baraza za utawala hizi zote lazima wapeleke habari za dunia nzima kwa mtawala wa baraza la dunia nzima.

Shughuli za miji hiyo, ikiwa zimefanyika ni kwa umoja au mbali mbali, basi wazi wa mfalme mwingine aziangalie, yeye ambaye ataathirika kwa vilivyo, na hawezi kuwa hatayaona. ib. 120.

Ma raisi wa wili wa kila kijiji cha 10,000 achaguliwe hivyo kuwa mmoja wao

awe msimamizi wa upande wa nyumba, awe na mahakama na matawi mengine yenye amri, na wengine wawe wanasafiri kwenda kuangalia wafanya kazi wa serekali.

Mji mikubwa lazima iwe mizuri, iwe na majengo marefu na yenye nafasi, yenye haiba kama mwezi wenye kuleta uhuru, ambapo watu wenye elimu, ambawo wanawo ujuzi wa kila namna katika elimu, lazima wakae ili kuyaangalia mambo ambayo yatamwendesha mbele mtawa na wanaotawaliwa, na kuchunguza amri na sheria za elimu. ib. 121.

Wajumbe na wapelelezi wa wekwe chini ya msimamizi mkuu. Mfalme lazima ajifunze sifa na aibu za raia wake wote wa utawala wake kwa kuwatumia police wa siri, ambawo ni watabaka mbali mbali. Wahalifu lazima watiwe adabu na wenye kustahiki sifa waheshimiwe. ib. 122.

**Maafisa wa Amani.**

Watu wanaochaguliwa na mfalme kwaajili ya ulinzi wa watu lazima wawe wema, wenye ujuzi, wataalamu, na kutokana kwenye jamii nzuri; wahalifu, wezi, majambazi na wavunja amri wengineo wageuzwe upande mwingine wa kazi kwa kuwaajiri wao katika kazi za serekali na kuwaweka chini ya maafisa waliotajwa hapo juu, na kuwageuza watu wahalifu hawo kuwa walinzi wa amani ili wawalinde watu. ib. 123.

Ikiwa mtumishi wa serekali anapokea rushwa kutoka kwa mshitakiwa na mshitaki ili isifanye haki na apendelee na kuishinda sheria, mfalme azichukue mali zake zote, ampe adabu ya kutosha, na kumfukuza na kumpeleka katika nchi ambaye asiweze kurudi tena. Ikiwa yeye hatiwi adabu, uovu wake utawafanya wengine kufanya hivyo kama alivyo fanya huyu. Lakini khofu ya adabu hiyo itawavusha kutokana na mazoezi ya uovu. ib. 124.

Mtumishi wa serekali lazima apewe sehemu kadha ya ardhi au pesa na serekali kila mwezi, kila mwaka, kila mara, au mara moja kwa pamoja, ili waweze kujiweka wenyewe kwa heshima, ili wasije wakababaishwa kwa hongo. Wale waliwo wazee, pia wapate pesa kutoka kwenye malipo yao ya zamani. Lazima ifahamike kuwa malipo yao huendelea maisha yao yote, lakini si baada ya kufa kwao. Watoto wao watazamwe na wapewe kwa mujibu wao. Wadogo zao na wajane wao pia wapewe na serekali malipo maalum ili waweze kujitazama wenyewe kwa mujibu wa sifa na urefu wa kazi zao. Lakini serekali wasimamishe malipo hayo ikiwa wao watajifanya kuwa waovu. Mpango huu ufuatwe vyema.

**Kodi.**

Katika kuwatoza watu kodi katika nchi, mfalme au serekali lazima ifahamu kuwa maafisa na watumishe wengine wa serekali, pamoja na raia wote wafurahie baraka na raha zake. Manu, VII, 128.

Mfalme apokee kodi kidogo kila mwaka kutokana kwa raia wake kama

mdudu, ng'ombe mchanga au nyuki anavyo fyonza chakula kidogo kidogo. ib. 129.

Yeye asikate mizizi ya urahisi wake au ya wengine kutokana na tamaa; kwa sababu, yeye ambaye anaikata mzizi wa kazi na raha, hujiletea shida mwenyewe na huwaletea wenzake pia. ib. 139.

Mtawala aliye mkali na mwenye huruma katika kufanya kazi zake, huheshimiwa sana kutokana na ukali kwa waovu na kuwa na huruma kwa wale walio wema. ib. 140.

Hivyo ndivyo yeye awatawale watu wake. Yeye awalinde watu wake daima kwa kuwa mwadilifu katika kazi zake na asiwe mwenye kuidharau. ib. 142.

Mfalme pamoja na mawaziri wake na watumishi wamekufa na hawaishi, katika kuwepo kwake, maisha na mali za watu katika utawala wake wanalilia kutaka msaada wanachukuliwa na wezi. Mfalme kama huyu atapatwa na maafa ya maumivu makubwa. ib. 143.

Wajibu mkubwa wa wafalme ni kuwa hifadhi raia zake. Mfalme anayepokea ushuru kama ulivyoelezwa katika sura ya 7 ya Manu au kama ilivyowekwa na baraza linalotawala, anapata sifa na anafurahiya raha lakini hupata maumivu, ikiwa anafanya kinyume cha sheria zilizotajwa hapa juu. ib. 144.

**Kazi Za Kila Za Mfalme.**

Kuamka baada ya nusu ya usiku, kwenda msalani na kukoga, yeye lazima asali na kumwomba Mungu, toa sadaka ya moto, waheshimu wataalamu na watu waadilifu, kula chakula na kuingia kwenye sebule wa waliohudhuria. Manu, VII, 145.

Kwa kusimama hapo, yeye lazima aonyeshe mapenzi kwa raia zake waliokuja hapo na kuwaaga kwa mapenzi, aonane na waziri wake mkuu kuhusu mambo ya serekali. ib. 146.

Tena hapo mfalme aende kutembea naye kwenye kiduta cha mlima, kwenye chumba cha siri, kwenye ukimyaa wa mwitu ambako hakuna hata majani ya kukera, au kwenye pahali ambapo hakuna watu, yeye aonane na waziri wake mkuu kwa utulivu, bila ya kuwa na hamaki. ib. 147.

Mfalme yule anaweza kuitawala dunia nzima ijapokuwa hana mali, siri yake kubwa na mipango ya vitendo vyake kwaajili ya uzuri wa watu ambawo wamezama na kujificha kutoka kwenye elimu za wengine. Hivyo, yeye asifanye kazi hata moja mpaka ikubaliwe na wenye mabaraza yote.

**Maarifa ya Namna Sita.**

Mfalme, mawaziri na watumishi wengine wa serekali lazima wafahamu kuwa kazi zao ni za namna sita ambazo lazima zifanywe vyema baada ya kufikiriwa vizuri, viz. mpango kuhusu handaki au kuzungusha boma; isiyo weza

kuharibiwa kwa mashambulio, amani, kuanzisha vita na maadui waovu, kuligawa jeshi katika sehemu mbili ili kupata ushindi, kufanya urafiki na mfalme mwenye nguvu. Manu, VII. 161.

**Tabia Zao Mbili.**

Mfalme lazima afahamu wazi tabia mbili za amani, na vita, mashambulio, ulinzi, namna mbili ya mgawanyiko wa mazao, na marafiki. ib. 162.

Namna mbili za amani ni mkataba na adui au na rafiki pamoja na nafasi yake, lakini yeye aendelee na mpango wa kazi wa sasa na wa siku zijazo. ib. 163.

Vita viko vya namna mbili, moja ni kutangaza kuwepo au kutokuwepo kwaajili yake mtu mwenyewe; na vyengine ni vya kupigana na kwa kumwudhi adui au kwa kuanzisha urafiki. ib. 163.

Namna mbili za mashambulio ni safari kinyume cha adui kwa sababu kutoweza kujiziwia pamoja na usuhuba au bila ya udugu. ib. 165.

Namna mbili ya vitendo ni kurudi nyuma kwa mujibu wa saa au kutokana na sababu au kubaki kimya bila ya kutenda kitu cho chote kwako kwaajili ya kugombezwa na rafiki. ib. 166.

Kugawanyika kwa jeshi na wakuu zake katika sehemu mbili kwaajili ya kufaulu unaitwa mgawanyiko wa namna mbili. ib. 167.

Namna mbili za mwungano wa kidugu ambapo mfalme anapoomba msaada wa mfalme mwenye nguvu zaidi au mtu mkubwa kwa kumwogopa adui au kutimiza mpango maalum wa kitendo. ib. 168.

**Vita.**

Yeye anapojua kuwa wakati kadha vita vitamlelea shida kidogo, lakini wakati mwingine hugeuka kuwa vya faida kwake na ushindi. Yeye lazima afanye mapatano na awe mwenye saburi mpaka wakati uwe muwafaka naye. ib. 169.

Wakati ambapo watu wote wanafuraha sana na wamo katika hali nzuri, na yeye pia anafikiri hivyo kuwa yumo katika hali njema, basi ni wakati kuanza chuki au aanzisha vita dhidi ya adui. ib. 170.

Yeye anapoona kuwa majeshi yake yana bashasha, nguvu na wako tayari, na jeshi la adui halina nguvu na haliko tayari, yeye lazima aanzishe kujiingiza naye. ib. 171.

Jeshi linapokuwa limepungua nguvu na usafirishaji, yeye lazima kwa uangalifu na pole pole afanye urafiki na adui na abaki nyumbani. ib. 172,

Mfalme anapoona kuwa adui ananguvu nyingi, yeye lazima ayazidishe majeshi yake au aligawanye katika sehemu mbili ili apate mradi wake. ib. 173.

Yeye anapajua kuwa maadui watamshambulia karibu, yeye lazima afanye

urafika kwa haraka na mfalme mwingine aliye mwadilifu na mwenye nguvu. ib. 174.

Yeye lazima afanye bidii kuwatumikia kama ni mkubwa watu wale na jeshi lake ambalo linapigana na kuwashinda adui. ib. 175.

Ikiwa yeye atayaona makosa katika vitendo vya suhuba zake, yeye lazima bila ya kusita na kwa uwerevu ajiingize na kupigana vita naye.

Yeye asiwe mbaya kwa mfalme mwadilifu, lakini, kwa kinyume chake, yeye awe rafiki wa daima na yeye. Mipango iliyoelezwa hapo kwanza ni ya kumshinda mfalme mwovu na mwenye nguvu. ib. 176.

Mwache mfalme mwenye siasa apange mipango yake yote na achukue hatua ambazo hapana usuhuba, nguvu zisizo upande wo wote, au maadui wanaweza kujipatia faida kwake. ib. 177.

Mwache yeye azifikirie faida na hasara za mipango yake yote ya sasa ambayo zinafanyika au itafanyika hapo mbele. Tena hapo yeye ajaribu kuyamaliza yale ambayo hayataleta faida na kuyashika ya faida. ib. 178.

Mfalme yule hawezi kushindwa na maadui zake ambaye anazifikiria faida na hasara ya mipango yake ya mbele, yeye ambaye anakata shauri anapoulizwa kitu, na yeye ambaye anajua kipi cha kufanywa vitendo vinapomalizika. ib. 179.

Mtawala, hasa raisi wa utawala, lazima ajaribu awe na ushirikiano, nguvu zisizopendelea na adui wenye nguvu, na asiwaachilie kwaajili ya dharau tu, wafanye kinyume cha anavyotaka yeye. Hii inaitwa kwa ufupi hekima ya siasa au maongozi ya serekali. ib. 180.

**Uvamizi.**

Mfalme anapokwenda kinyume cha adui yake, yeye lazima afanye mipango ya kuwahami raia zake; achukue magari ya jeshi lake, awasafirishe wanyama, silaha, makombora na silaha nyinginezo kwa mpango; na awaweke wapelelezi wa siri wakumletea habari za nchi iliyo na uadui nawo na wao wanataka kuishambulia. Manu, VII, 184.

Kuzifanya njia zake ziwe madhubuti zile za nchini-za maji-bahari na mito, za hewani, yeye lazima ayachukue magari yake ya vita, askari wapanda farasi, silaha, makombora, chakula, vinywaji na vitu vyenginevyo vya kutosha. Tembo wa kwenda kwenye ardhi, avuke maji kwa mashua: aruki hewani kwa mabofu na vyenginevyo. Yeye pia achukue askari zake. Baada ya kujiweka tayari na mambo yote na baadaye ya kutangaza mabishano, yeye aanze kwenda pole pole kufikia alipo adui. ib. 185.

Yeye ajitahadhari katika maneno yake yote anapoongea na watu wa siri wa adui, na kujionyesha kuwa rafiki na yeye. Kuwaonya adui, kuhusu mipango yao; mtu aliye adui moyoni, lakini anajifanya kuwa ni rafiki, lazima ahisabiwe kuwa ni adui mkubwa. ib. 186.

Yeye lazima awazoeze wafanya kazi wote wa serekali katika sanaa ya jeshi, yeye mwenyewe pia ajifunze, na kuwafundisha raia wengine pia. Wale peke yao ambawo wameshapata ujuzi wa kutosha wa kiaskari, wanajua kupigana vyema na kuwaamrisha wengine kupigana.

**Maarifa ya Vita**

Wanapokuwa wameshapata mazoezi aliongoze jeshi kwa mpango wa kama wafanya kazi, wakubwa na wadogo na kujitayarisha kama kukokota gari, na wakimbie kama nguruwe dume, wanapoanza kukimbia mmoja baada ya mmoja, na wakati mwingine wakimbie wote kwa pamoja, au kama mamba wanavyokwenda majini. Au, yeye aliweke jeshi lake kwa kulipanga kama shindano, ambayo ni kali huku mwanzoni na ni nene huku nyuma, na uzi uwe mnene kuliko shindano yenyewe. Au, aliweke jeshi lake wanapokwenda kupigana vitani kama kunguru ambaye anaelekea kwenda chini kutoka hewani. ib. 188.

Yeye alizidishe jeshi lake upande ule ambawo hatari inafikiriwa kutokea. Yeye mwenyewe ajiweke kati kati ya jeshi lote ambayo wamzunguke kama yungi yungi. ib. 181.

Yeye lazima awaweke wakuu wa jeshi na maafisa wengine, ambawo watapigana pamoja na majeshi na kuamrisha kwenda kwao, pande zote nane. Yeye aliweke mbele jeshi lote kuelekea mapigano yalipo; lakini pia mipango madhubuti ifanywe pande nyingine zote; kwa sababu wanaweza kuhujumiwa na askari wa adui upande mwingine. ib. 189.

Kingojo cha askari ambawo ni madhubuti katika kazi zao za sanaa za vita, yakilifanya jeshi shupavu, amunifu, hodari wa kufanya usimamizi na kuendelea kupigana, na ambawo akili zao ziko huru na mbali kutokana na fikira za kutokuwa waminifu lazima wawekwe pande zote nne za jeshi. ib. 190.

**Zatiti za Vita.**

Maaskari lazima wasongamane wanapopigana na adui wanaohesabika kuwa wenye nguvu. Wakati wa hatari, wao wapanuliwe. Yeye anapohitajiwa kupigana anapoingia mjini, ngome au kulikata jeshi la adui, yeye avipange vikosi vyake kama shindano au kama ncha za panga mbili, kisha apigane kote kiwili na kuendelea kuingia. Baada ya kuviweka vikosi vyake namna mbali mbali, tena hapo yeye awapeleke kupigana. Ikiwa bunduki na risasi zinapiga mbele, vikosi vitambae chini kama nyoka juu ya ardhi katika kushambulia. Wao wanozikabi bunduki, wao lazima wawachinje wapiganaji wa bunduki au wawateke na kwelekeza midomo ya bunduki kuwaelekea adui, askari walioko juu wawachambulie adui na bunduki hizo, kuwana na kusonga mbele. Kati kati pawepo na maaskari wa kupanda farasi. Wao wawashambulie adui mara moja na kuvivunja vyeo vyao na kuwafanya mahabusi au wawafanye wapigane upande wao.

Katika vita vya nchi kavu vikovi kwa magari ndiyo na farasi ndiyo wanapigana, kwenye maji mashua zinajazwa kwa askari, kwenye maji kidogo askari hupigana kwa kujiweka kwenye migongo ya tembo. Wao wapigane na mikuki na mishale katika misitu na nyika na kwenye mchanga wao wapigane kwa panga na jambia. ib. 192.

Wakati wa kupigana askari washangiriwe na kusifiwa. Wakati vita vinapomalizika, wao wote waburudishwe kwa maneno matamu, ya kuonyesha ushujaa na werevu, na watoshelezwe na mahitaji zaidi kama chakula, vinywaji, silaha, makombora, dawa, na misaada mengineyo. Yeye katu asipigane au aamrishe vita bila ya kufuata sanaa ya kupigania vita. Yeye lazima aviangalie vita hivyo ili aweze kuona majeshi yake kama yanapigana kwa hia au yanamtia aibu tu. ib. 194.

Wakati, ikiwa anaona anataka kuwaonya majeshi, yeye awazunguke adui na kuwa songa songa, na kupatisha taabu nchi, kuharibu, au kuviangamiza vyakula, maji, na moto. ib. 195.

Mizinga yake, kuta zilizozunguka mji na shimo refu lenye maji nje ya boma lazima lichafuliwe na kubomolewa. Usiku adui watishiwe kwa mashambulio. Kila kitu kifanye ili kuweza kumtisha. ib. 196.

**Mapatano**

Yeye anaposhindwa basi mapatano yafanywe na kutiwa sahihi. Na ikiwa inafikiri kuwa bora, jamaa kidogo wa mfalme na waadilifu wafanywe kuwa mfalme, na yeye aambiwe kutia sahihi kwenye sharti, ya kuwa yeye atatii amri, kama kuwa, yeye atatenda yaliyo ya kweli, na atawatawala watu kwa haki. Haya yatiwe kwenye ubongo wake na watu wa namna maalum apewe yeye kumsaidia yeye katika mambo ambayo kwenda yakaleta ghasia tena katika siku za mbele. Adui aliyeshindwa aheshimiwe kwenye baraza la machifu wakuu kwa kupewa vito na vitu vyenginevyo vya thamani. Lakini kisifanywe chochote ambacho kina msaidia kujiendesha mwenyewe. Ikiwa atawekwa kizuizini, yeye awekwe kwa heshima ili huzuni za kushindwa ziweze kumwondoka na aweze kuishi tena kwa raha. ib. 203.

**Namna ya Kuwaweka Wafungwa.**

Hivyo, sababu ya uadui ni unyanganyi wa mali ya mtu na sababu ya urafiki ni kumrudishia mali yake mtu, na hasa kuwekwa vizuri wakati wa dhiki. Ni bora zaidi kumpa kila anachotaka. Katu asichokozwe au kuzomewa, au kutumiwa maneno kama haya "Wewe umeshindwa," atumiwe kwenye mazungumzo yote pamoja naye. Lakini, kinyume cha haya, maneno kama haya yatumike "Wewe ni ndugu yetu" & C. yatumike kwaajili yake yeye, na daima aheshimiwe. ib. 204.

**Mwangano wa Kirafiki.**

Faida ya msaada wa rafiki ulioungana ni kuwa mfalme hapati nguvu

kutokana na mali na mipaka kama anavyopata kutokana na rafiki aliyeungana naye ambaye mapenzi yake ni ya daima na ambaye anauwezo wakupima mambo ya siku za mbele na kuzishinda sababu zilizopo sasa mbele yake, au hata kutokana na rafiki aliyeungana naye asiye na nguvu. Manu, VII. 208.

Mfalme husifiwa ikiwa na rafiki aliye na ujuzi wa dini na mwenye hesani akifanyiwa uwema; mwenye bashasha na furaha na mpendwa, hata akiwa ni mdogo na si mwenye kujulikana sana. ib. 209.

Yeye inataka afahamu vizuri kuwa asifanye uadi na mwenye busara, mtukufu, shujaa zaidi, mwerevu, mwenye hisani, na mtu mstamilivu kwa sababu ye yote anaye fanya uadui na mtu kama huyu, atapatiwa na majonzi. ib. 210.

**Nguvu za Kati Kati**

Mwenye nguvu za kati kati, ni yeye anayestahiki sifa, tabia nzuri, elimu ya watu wazuri na wabaya, akili shujaa na mwenye moyo mpole, na anayeongea juu juu tu.

**Kazi za Kila Siku za Mfalme.**

Kama ilivyokwisha elezwa, mfalme lazima aamke mapema asubuhi, aende msalani, na kukoga, asali na kutafakari kwa Mungu; atoe muhanga wa moto na pia awaambie wengine pia wamfanyie hivyo, aonane na mawaziri wake wote, aende mahakamani, awaone watumishi wote na wakuu wa jeshi, awamkie, afanye mazoezi ya kijeshi yeye mwenyewe na wengine pia, awakague farasi wote, tembo, ng'ombe na wanyama wengine, pia akague ghala za zana za vita, hospitali, na hazina kwa macho yake mwenyewe, aondoe hitilafu zo zote atakazo kuziona katika humu, aende kwenye viwanja vya mazoezi, afanye mazoezi hapo, akoge, na aende kwenye vyumba vya siri, nyumba ya jamii yake, na watumishi wake wapeleke chakula mchana. Yeye ale chakula ambacho kimekaguliwa vyema, kitacho mzidishi akili, nguvu na haiba, kitachaangamiza maradhi, chenye maakulati mbali mbali na vinywaji na vyenginevyo vya kuliwa, vyenye harufu nzuri, haluwa na vyakula vyengine vingi vizuri vyenye kujenga mwili na kuleta nguvu, ili yeye afurahie raha na furaha. Hapo ataweza kufanya kazi zake za serekali na kuweza kuyaendeza mambo yake.

**Daftari ya Ushuru**

Kwa ajili ya ushuru yeye achukue sehemu moja ya 50 ya faida juu ya dhahabu na fedha kutoka kwa wafanyi biashara na wafanya kazi, 6th, 8th, au 12th sehemu kutoka kwenye mchele na nafaka nyinginezo. Manu, VII, 130.

Ikiwa yeye anachukua pesa za ushuru, yeye achukue kwa kawaida ile ambayo wakulima na watu wengine wasipate taabu ili wasiweze kupata chakula, kinywaji na pesa. Kwa sababu kufaulu kwake mfalme unazidi kwa utajiri, siha na chakula na vinywaji vingi. Mfalme lazima awape raia zake sababu za kupata raha kama watoto wake mwenyewe na raia wamwone mfalme na watumishi wa serikali kama baba zao. Hii ni kweli kuwa wafalme wa wafalme ni wakulima na watu

wengine wanaotafuta mkate na mfalme ni mlinzi wao. Atakuwa mfalme wa nani, ikiwa hawako raia? Na watu watakuwa raia wa nani ikiwa hayuko mfalme? Wote wawili wanao uhuru wao katika mambo yao lakini si hivyo katika jumuia yote, ambaye inahitaji mapenzi na kujitolea. Hivyo mfalme au mtumishi ye yote wa serikali anaweza kuchaguliwa bila ya idhini ya watu. Watumishi wa serikali na raia wasiende kinyume cha amri ya mfalme. Hiyo imeelezwa kwa ufupi sayansi ya siyasa ambayo ni somo lake mwenyewe mfalme mwenye serikali. Yeye ambaye anataka kujua kwa urefu lazima ajitosheleze mwenyewe Vedas nne Amri za Manu maongozi ya Shukra, Mahabharat na maandishi mengine matakatifu.

**Mipango Ya Hakimu**

Haki ifanywe kama ilivyoelezwa katika sura ya 8 na 9 ya Amri za Manu. Hata hivyo sisi tukupa kwa ufupi hapa chini.

**Haki 18 Za Sheria**

Baraza, mfalme, na hakimu lazima kila siku wafikiria sababu za kuridhisha ambazo zinaangukia haki hizi 18 za sheria kwa mujibu wa mabishano yanayotokana na matumizi ya kawaida na sheria za amri; wao wanapoziona sheria ambazo hazijatajwa katika amri na wanaona umuhimu wao, wao lazima wafanye sheria nzuri inayowezekana ambayo itaweza kuwasaidia wote mfalme na raia. Haki 18 ambazo matatizo yote yanatatuliwa nayo ni, Manu, VIII, 4 - 7:-

1. Mapatano ya deni matatizo kuhusu kukopesha na kukopeshwa, 2. Rahani - mtu anapokataa anapotakiwa kukitoa kitu au pesa zilizowekwa, 3. kuuza mali bila ya mwenyewe. 4. masumbuko yasiyo ya haki miongoni mwa washiriki. 5. kuitwaa tena zawadi. 6. upungufu au kulipa mshahara kasoro. 7. Kutofanya (ya kutenda kinyume) cha mkataba. 8. matatizo ya kubadilishana, 9. Matatizo baina ya mwenye ngombe na mchungaji. 10. ushindani wa mipaka. 11. kumwumiza mtu kwa kumpiga sana. 12. Maneno mkali au uwongo, 13. Uwizi, unyanganyi, 14. halifu sheria au kitendo cha kuhujumu, 15. kuzini, 16. mabadilisho kuhusu kutoweza kufanya kazi kuwa kama mume na mke, 17. ubishano wa urithi, kucheza kamari au kusema uwongo au watu kwenye hatari ya mchezo. Hizi ni hekima 8 za kufahamiana.

Katika kuzifikiria kesi hizi mfalme afanye haki baada ya kufikiria ushahidi wa watu wengi na pia kuipitia sheria ya zamani, ni kuwa, yeye asimpendelee mtu.

**Umuhimu wa Haki.**

Wanachama wote wa mahakama wanahesabiwa kuwa wameumia, ambapo haki ina tafutwa na kutokuwa na usawa, na mahakimu hawatoe mshale wa kutokuwa sawa kwenye haki au kuondoa aibu yake na kuwangamiza kutokuwapo na usawa, kwa maneno mengine ni kuwa wasio na hatia hawaheshimiwi na wahalifu hawatiwi adabu. ib. 12.

Mtu mwadilifu na mwenye haki katu haingii mahakamani na inaingia, yeye lazima aseme kweli; yeye anyeuziwia ulimi wake anapoona haki haifanyiki, au anasema kinyume cha ukweli na haki, ni mwenye dhambi mkubwa. ib. 13.

Watu wote katika mahakama hiyo wamekufa, kama ilivyo, na hata mmoja hana uhai, ambapo haki inauliwa kwa kutokuwapo na usawa na ukweli kwa uwongo mbele ya wanasheria wake. ib. 14.

Haki iliyo aangamizwa, humwangamiza aliye iangamiza, na haki ikitunzwa humtunza mtunzaji wake. Hata hivyo, katu usiiangamize haki, bila ya kuangamizwa, ita kuangamiza wewe. ib. 15.

Wataalamu humwona yeye kuwa ni watabaka la chini kabisa ambaye anaipinga haki ambayo inaleta mali na kunyunyiza baraka zote. Kwa hivyo, mtu ye yote katu asiiangamize haki. ib. 16.

Katika dunia hii haki na uadilifu peke yao tu ndiyo rafiki wa mtu na ndiyo anayokwenda nayo baada ya kufa. Vitu vyote vyengine au marafiki huondoka mwili unapokuwa umekwisha na yeye anatengana na wenzake wote. Lakini usuhuba wa haki hauwezi kukatika. ib. 17.

**Dhambi Katika Haki.**

Pale ambapo haki haifanyiki katika mahakama ya serekali kwaajili ya kupendelea upande mmoja, inagawanyika katika sehemu nne ambapo moja inagawanywa baina ya wahalifu au wasiofanya haki, ya pili na mashahidi, ya tatu na mahakimu, na ya nne na raisi mfalme wa mahakama isiyokuwa na haki. ib. 18.

Mfalme na mahakimu wote wa mahakama wako mbali na dhambi na kuwa watakatifu ambapo wale wanaostahiki kutiwa adabu wana tiwa, anayestahiki kusifiwa anasifiwa, anayestahiki heshima anaheshimiwa; na mfanya wa dhambi peke yake tu anapata dhambi. ib. 19. Sasa sisi tutaeleza sifa za mashahidi.

Haki, wataalamu, watu walio wa kweli wa tabaka zote, wanaoijua sheria katika kila upande, wakò mbali na mapendeleo, na wenye ukweli, wachukuliwe kuwa mashahidi kwenye kesi, lakini si watu wenye tabia kinyume na hizi Manu, VIII, 63.

Wanawake waje kuwa mashahidi kwaajili ya wanawake, wale walio zaliwa tena kwaajili ya walio zaliwa tena, watu wa tabaka la wa fanya kazi kwaajili ya watu wa tabaka lao, watu wa tabaka la chini kwaajili watu wa tabaka lao. 64.

Katika kesi zote za kutumia nguvu, wizi, zinaa, kumharibia mtu jina, kumvunjia mtu heshima, hakimu inaweza asikague uwezo wa mashahidi. Mpango huu ni wa muhimu sana ilivyokuwa vitendo hivi hufanywa kwa siri. 65.

Wacha yeye afikirie kesi hizo kwa mujibu wa wingi wa mashahidi pande zote mbili, kwa ushahidi wa mashahidi wa tabia njema kwenye usawa wa namba zao, na kwaajili ya uhakikisho wa Brahmin aliye bora kabisa yaani, mwaguzi waaguzi wakuu na anchorts au yatis. ib. 66.

Mashahidi wako wa namna mbili, wale ambawo wameona kitendo kikifanyika na wale ambawo wamekisikia kutoka kwa wengine. Wanapoulizwa kutoa ushahidi wao mahakamani, mashahidi wanaosema kweli, wasije

wakahesabiwa kuwa hawana imani na kutiwa adabu; lakini wale mashahidi wanaosema uwongo watiwe adabu kama inavyotakiwa. ib. 67.

Shahidi anayesema kinyume cha yale aliyo yaona au kuyasikia katika mahakama ya mfalme au kwenye baraza la watu wazuri, yeye lazima atapata maumivu kama ya jahanamu kwa kukatwa ulimi wake katika maisha yake, na atanyimwa raha baada ya kufa. 68.

Maneno ya shahidi lazima yakubaliwe na hakimu, ambayo yeye atayafanya ya fanane na kesi ya kushakwa; lakini, kinyume cha haya, yeye ayakatae yale yeye anayo yasema kwa kusita sita. 72.

Mashahidi wanapoletwa mahakamani hakimu, mawakili na wanaosihi, lazima wawasemeshe kwa utulivu mbele ya mshitakuwa na mshitaki. 73

Enye mashahidi! tamkeni na ukweli yale nyinyi mnayoyajua yaliyotokea kuhusu jambo hilo mnaloulizwa baina ya vyama viwili; kwa sababu ushahidi wenu unatakiwa katika jambo hili. 74

Mashahidi wanaosema ukweli, wanapata furaha katika maisha mengine, anazaliwa katika jumbo jengine kufurahia utukufu, na anapata sifa katika maisha ya hapa na ya baada ya hapa; kwa sababu inatangaza kuwa maneno haya haya kuwa ni heshima na aibu. Yeye ambaye anasema kweli, anaheshimiwa; lakini shahidi mwongo analaamiwa. 75.

Kwa ukweli ni ushahidi uliosafishwa kutokana kwenye dhambi, kwa ukweli ni haki iliyo endelezwa; ukweli lazima, kwa hivyo usemwe na mashahidi wa tabaka zote. 78.

Roho ni shahidi wake mwenyewe, na roho ni yenye kujitegemea mwenyewe; kwa ujusi huu, enye mabwana, msiziaibishe roho zenu, mashahidi bora kuliko watu wote Kwa maneno mengine, ukweli umo katika akili zenu, nia na maneno; na kinachopinga haya yote ni uwongo. 79.

Mtaalamu hamwoni mtu yo yote kuwa bora kuliko yeye mwenyewe, ila yule ambaye hana shaka katika akili yake naye anazijua fikira zake zote za ndani, anapotoa ushahidi wake.

Enyi watu wakutaka uzuri! sikweli kuwanyinyi mseme uwongo mnao ufikiri akilini mwenu, "Mimi niko peke yangu," mtu hanioni mimi; lakini mwogope anaye jua yote Mungu, ambaye anakaa katika moyo wako katika umbo la nguvu za ndani, na ambaye anaona vitendo zuri na viovu, wewe lazima daima useme kweli. 81.

**Ushahidi**

Ushahidi unaotolewa kwaajili ya tamaa, kuvutiwa kwa akili, khofu, urafiki, mapenzi, majuto, ujinga, na utoto, lazima yote haya yasiwe ya maana.

Mfalme atowe adabu za njia nyingi yatakayoelezwa, shahidi anayesema uwongo kwa sababu ya hayo yaliyosemwa hapa juu. ib. 119.

**Adabu.**

Ikiwa yeye anatoa ushahidi wa uwongo kwaajili ya tamaa ya mali, yeye lazima atoe faini ya 1000 panas au Rs. 15-0-; ikiwa ni kutokana na mvutio wa akili, 250p. au Rs. 3-2-0; kwaajili ya khofu, Rs. 6-0-0, ikiwa ni kutokana na urafiki, Rs. 12-0-0; ikiwa ni kutokana mapenzi, Rs. 25; ikiwa ni kutokana na ghadhabu, Rs. 46-14-0; ikiwa ni kutokana ujinga Rs. 6; ikiwa ni kutokana na utoto, Rs. 1-9-0. ib. 120, 121.

Kuna pahala 10 pa kutilia adabu, kwa majina ni kama viungu vya·uzazi, tumbo, mikono, miguu, macho, pua, mashikio, mali na mwili, ambapo adabu hutiliwa. 125.

Adabu ziliyoelezwa juu na zitakazo tajwa tena baada ya hapa tu ndiyo zitolewe; kama kwa mfano, ushahidi wa uwongo kutokana na tamaa lazima, iwe na faini ya Rs. 15-10-0.

Lakini kila mhalifu maskini apigwe faini ndogo, tajiri alipe mara mbili, mara tatu, na mara nne yake, hii ni kusema, hakimu atoe adabu kwa mujibu wa hali ya pahali hapo, wakati, mhalifu na namna ya uhalifu wenyewe. 126.

Kwa sababu, adabu isiyo ya haki inaangamiza sifa njema za zamani, na ya siku zinazokuja wakati wa maisha duniani na huwa sababu ya dhiki baada ya maisha haya. Huwa ni sababu ya maumivu hata katika maisha mengine ya baadaye. Hivyo, adabu isiyo ya haki katu isitolewe kwa mtu ye yote. 127.

Mfalme ambaye hatoi adabu yo yote kwa wenye kustahiki, na kutoa kwa wale wasio stahiki, i.e. huwa wachia wahalifu, na kuwatia adabu wale ambawo haitaki watiwe adabu; humletea jina baya sana anapoishi bado na hupatwa na adabu kubwa baada ya kufa. Kwa hivyo, yeye amtie adabu yule tu aliye tenda kosa, na katu si kwa asiyekosa. ib. 128.

**Namna Za Adhabu**

Adhabu ya kosa la kwanza ni kuambiwa, i.e. ni kuwa mkosa lazima akaripiwe; kwaajili ya kosa la pili, akaripiwe zaidi, i.e. yeye akaripiwe tena - Kwa nini ukafanya jambo ovu kama hili? Kwa mara ya tatu anyanganywe mali yake; mara ya nne, adabu ya kupigwa, i.e., kuchapwa na fimbo au akatwe kichwa. ib. 129.

Kwa kiungo cho chote cha mwili ambacho mwizi alikitumia kutenda kosa kwa kinyume cha watu, hata kiongo hicho kitolewe na mfalme, i.e., akatwe ili kuzuia uhalifu miongoni mwa watu. Manu, VIII, 334.

Ikiwa mhalifu ni baba, mhisani, rafiki, mama, mke, mtoto wa kiume, au askofu wa nyumbani, hawezi kuachiliwa bila ya kutiwa adabu na mfalme ikiwa wao hawafanyi kazi zao vyema, i.e. mfalme anapochelewa kutoa hukumu, yeye asimpendelee mtu, lakini atoe adabu vyema. ib. 335.

Katika uvunjaji wa sheria kama huo, ambapo mtu wa hivi hivi anatozwa faini pice mmoja, mfalme anatiwa adabu ya pice elfu, i.e. mfalme lazima atiwe

adabu mara elfu zaidi kuliko mtu wa kawaida; waziri, nikuwa msaidizi wake mfalme wa matumizi yake, mara 800; mtu aliye chini yake mara 700; mmoja chini ya mtu huyu mara 600; na kama hivyo kwendea chini ya cheo, mtu wa mwisho na hafifu i.e. mtu wa chini apate adabu kasoro kwa mara nane, ikiwa watu walio katika kazi za serekali hawatiwi adabu zaidi ya raia tu, wao watawaangamiza raia. Kama simba anazuiliwa kwa kupigwa sana na mbuzi kwa kupigwa kidogo kwa hivyo hata wafanya kazi wa serekali kutoka mfalme kushukia chini kwa mfanya kazi wa kawaida watiwe adabu zaidi kuliko raia wa kawaida wanapofanya makosa.

Katika njia hii hii, ikiwa Shudra akitumia akili kidogo na akifanya kosa yeye atiwe adabu mara nane zaidi kuliko mtu wa kawaida; ikiwa ni Vaishya mara 16, ikiwa ni Kshatriya mara 20; ikiwa ni Brahman, mara 64, au mara 100 au mara 128.

Kwa maneno mengine, watu lazima wapate adabu zaidi na zaidi tena kwaajili ya makosa yao kwa kadiri ya elimu yao kuwa kubwa na kwa kadiri ya vyeo vyao kuwa vikubwa na vya juu katika jamii. ib. 337 - 338.

Maafisa wa serekali na mfalme anayependa kufanya ya haki na kupata sifa asicheleweshe kutoa adabu kwa haraka kwa wezi, kuzuia uhalifu kwa kutumia nguvu. ib. 344.

**Sifa Ovu Mno Za Mtu.**

Yeye ni mbaya zaidi mwenye kutenda uovu wa kutumia nguvu kuliko, mwenye kuvunja heshima, mwizi, au mwenye kuleta uchokozi. ib. 345.

Mfalme ambaye hamtii adabu mtu anayefanya uovu wa kupigana na anamstahimilia tu, basi huangamia haraka, na chuki huanza katika nchi 346.

Si kwaajili ya urafiki, au kwaajili ya utajiri mwingi, mfalme amwachie mfanyaji wa uhalifu, na kuwaletea mashaka watu wote, bila ya kumfunga au kumkata viungo huyo mhalifu.

Mwache aue bila ya kufikiria, i.e. fikiria baada ya kuua watu ambawo ni wahalifu, au watoto wa kiume na watu wengine, au baba na wazee wengine, au Brahmans au wale walio na ujuzi katika maandishi mengi kuhusu kazi zao, wanafanya upendeleo na kuua wengine bila ya kosa lolote. 350.

Mtu huwa hajafanya kosa lo lote ikiwa atamchinja mtu mwovu na wauwaji, ama kwenye hadhara au kwa siri; kwa sababu kuua uchungu kwa uchungu ni, kama ilivyokuwa, ghadhabu inayojijenga juu ya ghadhabu. ib. 351.

Mfalme yule ni bora zaidi ambaye katika utawala wake haishi mwizi, wala mzinifu, wala mvunja heshima, wala jabari, mwizi, wala mvunja sheria au asiyefuata amri za maamrisho ya mfalme. ib. 386.

**Adhabu Ya Kuzini.**

Endapo mwanamke, anapo mdharau mumewe kutokana na majivuno ya uzuri wa jamii, anazini; basi mwache mfalme aamrishe auliwe kwa kutafunwa na

mbwa mbele ya wanaume na wanawake wengi. Manu, VIII, 371.

Katika njia hii hii, mwanamume ambaye ni thakili anampuuza mkewe, na zini na mke wa mtu mwingine, au anakwenda na malaya, lazima alazwe chini ya kitanda cha chuma kilichopashwa moto sawa sawa mpaka kikawa chekundu na achomwe yungali mzima mpaka awe majivu mbele ya wanaume wengi. ib. 372.

Q. Nani awatie adabu mfalme au malikia, hakimu au mkewe, ikiwa wao watazini na mambo mengine ya kuvunja sheria?

A. Baraza la utawala. Wao lazima watiwe adabu kubwa zaidi kuliko watu wa kawaida.

Q. Kwa nini mfalme na wengine waliotajwa hapo juu, wakubali makosa yao?

A. Mfalme pia, ni mtu mwenye bahati na moyo safi. Ikiwa yeye hatiwi adabu kwa kosa na kama yeye hayakubali makosa yao, basi kwa nini watu wengine wafuate sheria na kupata adabu. Pale ambapo watu wote, maafisa wakuu wa serekali, na baraza la utawala linataka kutoa adabu kwa haki, mfalme peke yake tu atafanya nini? Ikiwa hapana sheria kama hiyo, mfalme, waziri mkuu, na watu wote wengine wenye nguvu, wanazama katika yasiyo ya haki, wanaizamisha haki na ukweli, kuwaangamiza watu wote, basi wao wenyewe wataangamia. Kwa nini, kumbuka maana ya ubeti ambawo unasema kuwa adabu inayotolewa kwa mujibu wa sheria inaitwa mfalme na haki. Nani ni dhaifu zaidi kuliko yule ambaye anaiangamiza?

Q. Hii adabu kali si bara bara kwa sababu, mtu hawezi kukifanya au kukirudisha tena kiungo cho chote. Adabu kama hivyo isitolewe.

A. Wale wanaoiona kuwa ni kali sana hawafahamu madhmuni ya siasa; kuwa, adabu kali ya mtu mmoja itawafanya wengine wote wakimbie mbali na utendaji wa vitendo viovu. Wao watawacha kufanya vitendo viovu na watajiweka kwenye njia ya kazi. Ukweli ni kuwa si shida ya adabu kali litawaangukia watu wengi. Ikiwa watatiwa adabu ndogo, uhalifu utazidi. Ile unayoiita wewe adabu ndogo huwa nzito mara millioni kumi zaidi kutokana na kutolewa kila mara uhalifu unapozidi. Kwa sababu, watu wengi wanapoufanya uhalifu, adabu japo ndogo itatolewa. Kwa mfano, ikiwa adabu ya mtu inafikilia kuwa ni ratili 80 naya mwingine ni chhataanks nne, au nusu ratili, hizi zote pamoja huwa 1 md. 4 ch. Hapo kwa ujumla na inapogawanywa kila mtu anapata 20 srs. na 2ch. ya adabu. Kitu gani wakosa wanafahamu kwa adabu isiyo kuwa ngumu? Pia, ikiwa adabu ya mtu mmoja inakuwa maund moja, na watu elfu wanapata 4 ch ya hiyo Adabu yao ya jumla huwa 6 md. na robo. Kwa kuwa si ya watu wote, huwa ni nzito na ngumu zaidi; na kuwa maund moja ya adabu ni ndogo na rahisi.

**Ushuru Na Bima**

Mfalme lazima aweke namna ya ushuru juu ya safari kwa mujibu wa urefu wa safari, bandari za bahari, na uendelezi wa nchi ulio na maji ya mito na vijito.

Haiwezi kuhakikishwa na kuwa maalum kwa ajili ya bahari. Lakini yeye anaweza kufanya orodha za ushuru wa forodhani ili apate faida yeye na wenye meli kubwa kwenye bahari. ib. 406.

Lazima ifahamike akilini kuwa wao ni waongo wanaosema kuwa ati hakukuwapo na meli kubwa hapo zamani. Mabaharia wanaosafiri katika nchi na bahari za kigeni lazima wauhami uhuru wa raia wenzao katika nchi zote na kuona wao hawapati shida yo yote kutokana na kutojiweza.

Mfalme lazima kila siku akague ufanyaji wa kazi maofisini; tembo, farasi, na namna nyingine za usafirishaji, kodi za daima na mapato na matumizi muhimu, mashimo yake ya madini na vito vya thamani; na hazina zake. ib. 419.

Kwa kuzisimamia na kujijulia mambo yote kwa vilivyo, yeye huwa anaiweka nchi yake huru kutokana na uhalifu na fujikia kwenye la utulivu. ib. 420.

**Siasa katika Sanskrit**

Q. Sanskrit inayo siasa kamili au si kamili?

A. Kamili. Kwa sababu, siasa yo yote iliyopo katika dunia, imechukuliwa kutokana na Sanskrit. Kuhusu haya hapana ushahidi ulioandikwa ua uhakikisho, Manu, VII.3.

Baraza la utawala lenye watu walio wajuzi vilivyo lazima wafanye amri ambazo zitamwendelea mbele mfalme na rai zinazo fuatana na uadilifu. Wao lazima na daima waangalie kuwa wao wasiruhusu ndoa za watoto wadogo kufungika. Hata miongoni mwa vijana wao wasikubali kupanga au kuruhusu ndio bila ya masikilizano na idhini. Utakatifu uangaliwe vyema. Uzinifu na kuweza kuoa mke zaidi ya mmoja pia isiruhusiwe. Kwa hivyo, akili na mwili uweza kuwa wa nguvu kamili. Kwa hivyo, ikiwa nguvu za akili zitaendelezwa na nguvu za mwili kudharauliwa, mtu mmoja mwenyewe nguvu atawashinda watu mia wenye elimu. Lakini ikiwa nguvu za mwili zitaendelezwa, na si nguvu za roho, kazi nzuri za serekali haziwezi kuwekwa bila ya elimu. Bila ya utawa ulio sawa sawa, yote huanza kutawanyika wenyewe; Chuki, ugomvi na ushindano huwaingia, na hufanya uangamivu wao. Kwa hivyo, daima jaribu kuzizidisha nguvu za akili na mwili. Hakuna nguvu ambaye inaangamiza upesi nguvu na akili, kuliko zinaa, na uchu. Hasa tabaka la wapiganaji vita lazima wawe wenye miili yenye nguvu na viungo vyenye nyama, ikiwa wao ni watumwa wa fikira zao, basi serekali ya nchi itaangamia. Pia inatåka ifahamike kuwa raia wafuatane naye mfalme-yatha raja tatha praja. Kwahivyo, mfalme na maafisa wa serekali katu wasifanye vitendo viovu, lakini kinyume cha haya wao waonyeshe mifano mema kwa kufuata sheria na kuwa wema.

Haya ni wajibu wa ufalme kwa ufupi. Kwa ujuzi zaidi, Vedas, Amri za Manu, sura, VII, VIII, IX. Uadilifu wa Shukra, Vidur Prajagar, Shanti Parva ya Mahabharat kuhusu kazi za mfalme na kazi wakati wa shida na vitabu vyengine viangaliwe. Baada ya kuijua Sanysi ya siasa, watu wataweza na kufuzu kuiendeleza serekali ya majimbo na dunia nzima. Wao wajifanye kuwa ni raia wa Mungu.

Ni mafunzo ya Yajur Veda. Mungu ni mfalme wetu. Sisi ni watumishi wake na tunamtii. Naye kwa baraka zake atume serekali ya dunia, na atufanye sisi kuwa zana zake za kueneza ukweli na haki? Katika sura inayofuata sisi tutaandika kuhusu Mungu na Vedas.

**Muhtasari**

Rig. III, XXXVII, 6 na Shat. XIII, II, 7 inasema kuwa mfalme na watu wake waunde Baraza tatu, Elimu, Dini na Uendeshaji wa kazi. Mtu mmoja peke yake asiwe na nguvu zote za serekali, mfalme awe ni mkuu wa baraza zote. Sifa za raisi na maraisi wa baraza mbali mbali ni kuwa wao wa shughulikie kutaka kuendeleza ustawi wa nchi, uzuri wao wa elimu na ujuzi na tabia pia na mkabala wao na watu, Nchi huendelea na kufanikiwa endapo watu wake ni waadilifu. Pia ustawi wao unahitaji uchaguzi wa watu waliosoma na wenye elimu, kuchaguliwa kwa watu wataalamu kuwa ni wakuu wa baraza la dini, na watu waliosoma na wema kuwa waendesheji wa kazi. Utiifu wa sheria unatakikana kuwepo kote.

Kwa mujibu wa Manu, VII, 17-31. Sheria ya kutoa adabu ya haki basi ndiyo mtawala wa kweli wa serekali, kwa sababu kutokuwapo kwa haki huwaharibu watu wote. Mfalme anayekwenda kwa sheria ya haki huleta ustawi wa watu. Kwa hivyo watu, wanaoijua Vedas na Maamrisho kwa vilivyo mwema, hajipendelei nafsi yake, na mpole lazima achaguliwe kuliendesha jeshi, na kuendeleza mambo ya uadilifu na ya juu kabisa, na kuendeleza amri za kifalme. Wanachama wa mabaraza pia wawe wataalamu wa maandishi yote matakatifu. Si watu kasoro kuliko kumi walifanye baraza, na hesabu ya kanuni yake kuwa tatu. Watu wajinga wasitiwe kwenye baraza, kwa sababu hukumu ya watu wa jinga hata ikiwa ni elfu huwa haina maana, na ambapo hukumu ya mtu mmoja tu ambaye ni mtaalamu mwema ina hesabika kuwa ni sheria bora kabisa.

Mfalme asiwe na (1) uovu kumi unaotokana na mapenzi na raha, na (2) hamaki za namna nane zinazotokana na ghadhabu. Nazo ni (1) kuwinda, kucheza kamari, mdako, kulala mchacha, kupenda hadithi, uhalifu, anasa, kulewa, bangi, kuvuta hashish, kuimba kupiga muziki, zurura zurura; (2) kusengenya, kuzini, uovu, wivu, ubishano, asrafu, lugha kali, na adabu isiyo ya haki.

Bunge lazima liwe na mawaziri saba au nane walio tokana katika ukoo mtukufu, elimu nyingi na tabia nzuri. Cho chote kisifanywe bila, idhini yao (Manu, VII. 54, 64). Mfalme awe amri ya hazina na kazi muhimu, amani. Mambo

yote yafikiriwe na kura za wingi.

Miji ufanywe kati kati ya pahala, uhifadhiwe na tabia na sanaa. Nyumba ya Serekali uwe na ofisi zote kubwa, ngome madhubuti iwepo yenye silaha na vyakula.

Kuendesha kazi za serekali vyema, ofisi za serekali ziwe mbili, tatu, tano au vijiji mia. Afisa aliye mwongozi wa kijiji kimoja apeleke habari kwa mkuu wa afisa wa vijiji kumi, na huyu kwa mkuu wa vijiji ishirini, na kadhalika. Afisa wa vijiji elfu kumi apeleke habari za jimbo lake kwenye Baraza la utawala, ambalo lina wajibu wa kupeleka habari kwa Mfalme wa Dunia.

Kutoza kodi au ushuru iliyowekwa katika Manu, VII, 130, imewekwa kuwa sehemu moja ya 50 ya faida ya vilivyotengenezwa, sehemu ya 6 ya mazaao ya kilimo. Ikiwa sarafu zinachukuliwa kutozea ushuru, lazima ifikiriwe ili watu wasipate shida ya kutaka chakula. Kwa ufupi, ushuru uwe mdogo kama iwezakanavyo, kama maziwa yanayo nyonywa na ndama au damu ya mdudu mdogo. Ushuru pia unatozwa kwenye njia na safari za bahari.

Watumishi wa serekali askari na jeshi wapate mishahara kila mwezi au vipande vya wao wapate penshan wanapostaafu, na jamii zao, na watoto wao wasaidiwe na serekali wao wakifa. Hongo, litiwe adabu kali kwa kunyanganywa mali yote au kuhamishwa kwenye nchi.

Kazi za jeshi zimegawanyika katika amani, vita, mashambulio, kujihami, hila na urafiki. Kila mmoja imejigawa tena mara mbili. Kwa mfano, amani na adui au na mwingine na mwenzake, mgawanyiko wa jeshi katika sehemu mbili & C. (Manu, VII, 161 - 176.) Katika vita vya sheria za ushujaa lazima wekwe, kama wasimpige aliye karibu yake katika vita, askari waliojeruhiwa, waliolala, wakimbizi, & C. Adui aliyetekwa aheshimwe katika mahakama na inaonekana kuwa sawa arudishwe tena kwenye nchi yake, ambapo akifa apewe jamaa zake, kusaidiwa na washauri walio waaminifu. Mateka wa vita wa tazamwe vyema, kuhusu chakula, dawa na wawekwe kwa amani.

Mambo yanayo husu mahakama, (Manu, VIII, 3 - 19) inayo namna kumi na nane za matatizo viz. deni, amana, uuzaji, ushirika, mishahara, zawadi, mapatano, mabadilishano, uenyeji, mipaka, kuvunja heshima, kuharibu jina, uwizi, zinaa, mabisano, urithi, kamari. Mahakama huja pale haki haitolewe kama inavyotakika. Kesi zisikilizwe na wanao zipigania, mawakili mbele ya hakimu na pamoja na ushahidi (Manu, VIII. 68 - 91), ambaye mwenye tabia timamu. Ushahidi unaolelewa kwa ajili ya tamaa ya pesa, wazimu, khofu, urafiki, mapenzi, ujinga, kulipia kisasi na utoto, haihisabiwi.

Faini hutozwa kwa mujibu wa uhalifu, ni kuwa mfalme hutozwa mara elfu zaidi ya mtu wa kawaida. Adabu itiwe kwa kupigwa kwenye utupu, tumbo, ulimi, mikono, miguu, macho, pua, masikio, mwili, na mali. Wala isije ikazuiliwa kwa mtu mwenye heshima, kama Brahmans, jamaa, baba mwalimu & C.

wanapopatikana na hatia. Zinaa inatiwa adabu ya kifo mwanamke akatwe katwe na kupasuliwa vipande vipande na mbwa na mwanamume aunguzwe lihali yuko hai mpaka awe majivu jivu kwa kuwekwa kwenye kitanda cha chuma kilicho kimoto. Kutolewa adabu kali zaidi huwazuia maasi kufanyika.

Mfalme azikague afisi kila siku pia akague, jeshi na hazina, ili kila kitu kiweze kuenda vizuri na kuzidisha furaha za watu.

Mfano huu wa mazoezi ya kizamani ya mpango wa serekali ni sifa ya kwanza iliyotokana na Manu, mtoaji mkuu wa sheria za zamani za kale za Bara hindi.

## SURA YA VII

## MUNGU NA VEDAS.

**Ya Mungu.**

Rig. 1. 1/64. 39.) Tumetoa tafsiri ya beti hizi tulipoeleza elimu ya wanafunzi. Hata hivyo ina maana hii:- Watu wale wasiokubali kuwa Mungu yuko, wapumbavu, na daima wamezama katika bahari ya huzuni, yeye ambaye hajui, wala hajaribu kutafuta kupata kuyajua, wala hamfikirii Mungu, yeye ambaye tabia zake maumbile na elimu yake ni takatifu na ya ajabu ambamo dunia, jua na dunia nyinginezo zimo humo, aliyeenea kama mbingu ilivyoenea kote; na ni Mwenye Enzi, Mungu wa miungu. Elimu Yake yeye tu huwapa binadamu furaha ya milele.

**Miungu 33.**

Q. Wewe unakubali na kuamini kuwa Vedas inasema kuhusu miungu mingi?

A. La; hakuna hata mnongono wake katika veda zote nne ili kuhakikisha kuwepo kwa miungu mingi. Lakini, kinyume na haya imeandikwa wazi kuwa hapana ila Mungu mmoja tu.

Q. Ni kitu gani cha miungu kimeelezwa katika Vedas?

A. Vitu ambavyo ni vya ajabu na si vya kuwaida, vinaitwa devatas; mfano dunia. Lakini haipo po pote wala haielezwe kuwa ni kitu cha ajabu kama Mungu. Tazama hapa, ubeti huu huu wa Vedic unasema kuwa. Miungu peke yao tu ndiyo waabudiwe ambamo miungu yote wamo humo. Ni makosa ya watu kulichukulia neno devata kuwa na maana ya Mungu, yeye ambaye ni mkubwa kuliko miungu yote, anaitwa Mahadeva au Mungu Mkuu; kwa sababu, Yeye peke yake ni Muumba, Mlinzi, Mwangamizi wa dunia; Yeye ni Hakimu na Mtawala mkubwa. Miungu 33 ubeti uliomo katika Vedas umeelezwa katika Shatapatha. Kuna Vasus 8 au makao ya viumbe (uliyotokana na vas: kuishi,) i.e udongo, maji, moto au mwangaza, hewa, mbingu, jua, mwezi na sayari; Rudras II au njia muhimu zilizotokana na ru: kulia, kama ni kupotea nguvu hizi muhimu kwenye mwili, ikiwacha kuishi, majamaa waliofiwa wanapo lia), i.e asili ya aliyo zaliwa (apana), kutoa puumzi (prana), nguvu (vyana) au nguvu za kujiendesha, nguvu za kumeza (udana) nguvu za kupumzika au kuponya, mzunguko (samana) piga mbweu, (naga) kupepesa (kurma) njaa (kirkala), piga miayo (devadatta) nguvu za kuoza (dhananjaya) na nafsi (jivatma); Adityas 12 au alama za nyota, (zinazotokana na ada: kuchukua) i.e ya jua (aditya's) kwa njia hii ya jamii za nyota huchukua au hufupisha maisha ya viumbe; Indra ua nguvu za umeme, linatokana na sababu kubwa ya nguvu na maendeleo; Prajapati au bwana wa viumbe au Yajna (kazi) kujitolea; kwa sababu ni sababu ya kuitakasa hewa, maji, mvua, na sayari. Pia inatoa heshima kwa wenye elimu, na ni mama wa uvumbuzi na namna mbali wa vitu. Hawa ni miungu 33, wenye kuwa na sifa za ajabu waliotajwa juu. Sura ya 14 ya Shatapatha inasema wazi kuwa Mwenyezi Mungu ni Bwana wa vitu vyote na

ni mkubwa wa wote. Yeye ni, kama ilivyokuwa, hali 34 za utakatifu, na ni peke yake wa kusifiwa. Maandishi mengine matakakifu yana hakikisha kuwa na sifa hizi hizi pia. Ingekuwa watu wameshaona maandishi haya, wao wasingepotea kwenye njia ya kweli na kuangukia kwenye shimo la upotovu, kuwa kuna uwingi wa miungu katika Vedas.

**Umoja wa Mungu Mkuu.**

Yaj. XL. 1. Ewe mtu, mwogope Mungu, ambaye yumo katika kila kitu katika dunia na anavizuia yeye; Yeye ni Bwana wa Kweli. Usitake utajiri wa wengine. Kuwa na haki na wacha yasiyo ya haki. Furahia maisha kwa kufuata dini ya kutenda yaliyo ya kweli.

Rig X. 48. 1 na 5. Mungu Mkubwa anawaambia wote: Enyi watu, Mimi ni Bwana, Mimi nilikuwapo kabla ya nyinyi wote, Mimi ni Bwana wa dunia yote. Mimi ni sababu ya vyote vilivyomo ndani ya dunia, Mimi ni mshindi wa wote ni mpaji na mshikaji wa mali yote. Watu wote lazima waniite Mimi Baba kama watoto wanavyowaita wazazi wao. Kuwasaidia wote. Mimi huwapa namna mbali mbali za chakula kwa wote duniani nzima na ni namna ya furaha zao. Kwa kuwa Mwenyezi, Mimi ni mwangaza wa dunia yote kama jua, Mimi katu sisumbuki. Mimi sifi. Mimi ni mfanyaji wa mali katika umbo la sayari. Nijue Mimi kuwa ni mfanyaji wa dunia zote. Enyi roho, niombeni Mimi kwaajili ya mali ya elimu na heshima nyinginezo kwa kutenda yaliyo mema kwa kupata nguvu na maaendeleo. Katu musiukate urafiki wenu na Mimi.

Rig. X 49. 1. Enyi watu wangu, mimi humpa mali za milele za elimu na heshima nyinginezo kwa mtu anayenitukuza Mimi kwa mazoezi ya ukweli. Mimi ni Brahman, ni kuwa mwonyeshaji wa Vedas, ambayo inanienzi Mimi kwa ukweli, na kwa hiyo mimi huendeleza elimu ya wote. Mimi ni Mwongozi wa ukweli, Mbariki wa mfanyi kazi nzuri (yajna) na ni Mwuumba na Msimamizi wa dunia yote na mambo yake yanayoonekana. Kwa hivyo usijiondoshe kwangu Mimi, wala kuabudu au tambua nguvu za kitu chengine cho chote badala yangu Mimi.

Yaj. 13. 4. Ubeti huu wa Yajur Veda. Unamaana kuwa: Enyi watu, na mapenzi yote na kujitolea mpende Mungu na Roho yenye furaha; ambaye alikuwapo kabla ya kuumbwa, ambaye ni Mwuumba, Mlinzi na Msimamizi wa yote jua na vyenginevyo vinavyo ngara, na ambaye ni roho ya ndani ya Bwana wa wote ambawo walikuwapo na waliokuwa wapo sasa, na pia ambawo watakuwapo baadaye. Yeye amefanya na Yeye ndiye anayewahifadhi viumbe vyote vya dunia kutoka duniani mpaka kwenye jua.

**Uhakikisho Wa Kuwapo Kwa Mungu.**

Q. Wewe unasema maneno mengi ya Mungu. Lakini vipi utahakikisha kuwepo kwake?

A. Kwa namna nyingi, nazo ni uhakikisho wa akili, ufahamu, na kwa milihani mengineyo ya akili.

Q. Uhakikisho kama huu hauwezi kutumika kwenye kesi ya Mungu.

A. Ny. 1, 1, 4. Ni mithali ya Maharshi Gotama na Ufahamu au falsafa ya Nyaya. Ina maana ya kuwa: Ufahamu au ushahidi wa kuendelea ni elimu inayotokana na akili inayo ungana na nia, shikio, ngozi, jicho, ulimi, na pua pamoja na sauti, mguso, umbo, utamu, harufu, furaha, maumivu, ukweli, uwongo, na vitu vyenginevyo. Lakini ufahamu uwe uko mbali na shaka au makosa. Fahamu akilini kuwa akili na nia zikiungana na vitu, lakini si na vitu ambavyo sifa zao zimo. Ni kuwa, viungo vinne, viz, ngozi, na vyenginevyo vinavyowekuguswa, umbo, mwonjo, na harufu; na nia iliyoungana na akili hufamisha kitu ambacho ni ulimwengu. Katika namna hii hii, ufahamu wa Mungu hutokana na ufahamisho wa ajabu katika dunia ya dhahiri na elimu pamoja na uadilifu. Akili au roho inapoichochea nia, na nia inaisaidia akili kwenye kitu cho chote, ikiwa ni wizi au uhalifu mwengineo wo wote au uadilifu mwingine, na inapoanza kukifanya kitendo hicho, matakwa yake na hukumu yake huwa kwenye hicho kitu chenyewe. Katika wakati kama huu wa hofu, wasi wasi nawibu huzidi katika moyo wa mtu kwa ajili ya kazi za uhalifu' na uhodari, uthibitisho, furaha, na faraja kwa ajili ya kazi nzuri. Sauti hii ya ndani au ufahamisho hautokani na haraka, lakini unatokana na Roho Isiyo na Mwisho. Akili inapojishughulisha kumjua Mungu katika utakatifu wake wote kwa nia, hufahamu yote mawili (Mungu na roho). Mungu anapodhihirika katika ushahidi kamili, shaka gani itakayo kuwapo hapo na ushahidi na mitihani mengine ya uhakikisho wa elimu ya Mungu? Kwa ajili elimu ya uhakikisho hudhahirisha sababu.

**Kuwepo Kote Kwa Mungu.**

Q. Jee Mungu yuko kote, au Yeye hukaa katika mwahala maalum?

A. Yeye yuko kote. Kwa sababu, ingekuwa Yeye yuko mahali kadhaa tu, Yeye asingeweza kuwa roho ya ndani ya wote, mjua yote, mwenye kuzuia yote, mwuumba yote, muweza yote, na mwangamizi wa yote. Kwa sababu, kitendo cha mtendaji hakiwezi kutendeka kwenye pahali mbali na uwezo wake.

**Mungu, Huruma na Haki.**

Q. Jee Mungu ni mwenye huruma na haki?

A. Ndiyo.

Q. Sifa hizi, viz, huruma, na haki ni kinyume cha mwenziwe. Kufanya haki hakuleti huruma, na vivyo hivyo kwa sababu, haki ni kutoa zawadi na adhabu kwa mujibu wa vitendo, si zaidi wala kasoro; na huruma ni kumwachia mhalifu bila ya adhabu.

A. Tafauti baina ya haki na huruma ni ndogo kabisa; kwa sababu zote mbili zina kazi za namna mmoja. Sababu ya adabu ni kumzuia kufanya uhalifu na kupata maumivu. Huruma ni msamehe mtu kutokana na maumivu. Maana yako wewe ya haki na huruma haina ukweli. Kwa kuwa, haki, ni kumtia mtu adabu, mtu yule ambaye amefanya kitu kiovu basi kwa mijibu wa kosa lake na tabia ya

kosa hilo. Ikiwa mhalifu hatiwe adabu basi huruma itaangamia, kwa sababu kumsamehe mtu aliye na hatia ni kuleta maumivu kwa maelfu ya watu waadilifu? Kusema sawa sawa, huruma huonyeshwa kwa kumtia jela mhalifu na kwa kumzuia kufanya mabaya. Ni huruma kwake pia. Na adhabu yake itakuwa ni kitendo cha huruma kwa maelfu ya watu.

Q. Basi kwa nini huruma na haki maneno mawili mbali mbali? Ikiwa yana maana moja, basi huwa haina maana kuwa mbali mbali. Ingekuwa bora, kama lingekuwapo neno moja tu. Kwa hivyo inaonyesha kuwa kitu cha haki na huruma si namna moja.

A. Kwani hakuna maneno yenye maana moja, na hakuna neno lenye maana nyingi?

Q. Ndiyo yapo maneno kama hayo.

A. Basi kwa nini wewe una shaka?

Q. Kwa sababu sisi tuna sikia watu wanavyosema.

A. Sisi tunayo sikia yote mawili ya uwongo na ya kweli duniani; lakini ni wajibu wetu kuya hakikisha baada ya kuyafikiria sana. Tazama hapa, ni huruma kubwa ya Mungu kuwa Yeye amewapa hawa viumbe vitu vya namna nyingi baada ya kuwaumba katika dunia kwa ajili ya matumizi yao. Huruma ipi tena inaweza kuwa kubwa kuliko hii? Sasa, faida ya haki ni dhahiri kama ilivyo dhahiri raha na maumivu, zaidi au haba, miongoni mwa watu wanaoonyesha vitendo vyao wenyewe. Tafauti baina yao ni kuwa huruma ni kutaka na kitendo cha kuleta nafuu na kuondoa maumivu ya wengine, na haki ni kitendo cha dhahiri au ni vitendo kama vya kutilia adabu kupiga, kuchana chana na adhabu nyinginezo. Sababu hasa za huruma na haki ni kuwa zuia watu wasifanye uovu na kuponyesha maumivu yao.

**Mungu Ni Roho.**

Q. Mungu ana mwili au hana mwili?

A. Hana mwili; kwa sababu, ingekuwa Yeye anawo mwili, Yeye asingeweza kuenea na kuwepo kote, na ingekuwa sifa. Ya kujua yote na sifa nyinginezo kuwa zisitimie. Kwa sababu vitu maalum vina sifa maalum, tabia na vitendo. Pia vitu hivyo maalum haviwezi kuepukana na joto na baridi, njaa na kiu, maradhi, uovu, mtengamano, na namna nyinginezo za maumivu. Fikra hizi zinatufanya sisi kujua kuwa Mungu hana umbo wala hafanani na kitu cho chote. Ingekuwa Yeye ni kitu na ana umbo maalum basi pia angekuwapo aliye mkubwa kuliko Yeye ambaye alitengeneza Yeye na kumtia pua, mashikio, macho, na viungo vingine vyote ili kumpa Yeye umbo. Hailinganishi na cho chote kuwa vitu sisivyo fanana na vinapo ungana lazima vikubali pasipo na uthibitisho vitu vyake na akili za mwunganishaji, au, ikiwa itashindaniwa kuwa Mungu Amejuiumba Mwenyewe kutokana na kutaka Mwenyewe, basi inajibiwa kuwa inaonyesha dhahiri kuwa yeye hajakuwa na umbo kabla ya kuumba mwili wake. Hata hivyo, Mungu hana

mwili, lakini kwa kuwa hafanani na kitu Yeye hufanya na kuritia umbo vitu vyote vya dunia kwa sababu zisizo julikana.

**Mungu Ana Nguvu Zote.**

Q. Mungu ana nguvu zote?

A. Ndiyo. Lakini sisi ni kama neno hili linavyosema na kuleta maana yake hasa kuwa ana nguvu zote. Maana yake ni kuwa Mungu hataki msaada hata mdogo wa mtu ye yote kwa kufanyia kazi yake ya kuumba, kulinda, na kuangamiza, na kuzifanyia roho haki kwa mujibu wa sifa zao. Kwa maneno mengine, Yeye anafanya kazi zake zote kwa uwezo wake Mwenyewe.

Q. Sisi tunaamini ya kuwa Mungu hufanya yale anayotaka Mwenyewe, kwa sababu hapana aliye juu ya Yake Yeye.

A. Yeye anapenda nini? Ikiwa wewe utasema kuwa Yeye anapenda yote na anaweza kufanya yote sisi tunakuwuliza wewe ikiwa Yeye anaweza kujiua Mwenyewe, umba Miungu Mingi, ajifanye mwenyewe mjinga, na aibe, azini, na afanye maovu mengine na aumwe na maumivu? Ilivyokuwa vitu hivi ni kinyume na tabia yake havifanani na sifa zake na vitendo vyake, uhakikisho wako kuwa Yeye anaweza kufanya yote, unaanguka chini, na haufananishwe na yale yanayo mhusu Mungu. Basi maana ya mwenye nguvu zote iliyotolewa hapa, ni ya kweli tupu.

**Mungu ni Wa Milele.**

Q. Jee Mungu ana mwanzo?

A. Ndiyo. Hana mwanzo ni moja kuwa hana sababu au wakati wa alioanza kuwapo. Vitu vyote hivi vimetolewa kwa urefu katika sura ya kwanza, ambayo inaweza kutazamwa.

**Matilaba Ya Mungu**

Q. Mungu anataka nini?

A. Yeye anawatakia mema wote na anataka kuwa wote wapate raha na faraja, lakini kwa urahisi. Yeye hamfanyi mtu awe muhitaji wa mwenzake bila ya kufanya dhambi.

**Sifa, Sala na Kuabudu.**

Q. Ni sawa kuimba utakatifu wake, kusali na kumwabudu Mungu?

A. Ndiyo ni sawa.

Q. Mungu atamwondolea au kumsamehe mtu yule anaye imba utakatifu wake, anasali na kumfikiria yeye, kwa kuziweka kando sheria zake?

A. La.

Q. Basi ina maana gani kuimba utakatifu wa Mola.

Ni mapenzi ya Mungu na kuendeleza mbele tabia ya yule anyeabudu, sifa na vitendo kwa nguvu za wale wenye utakatifu, Matunda ya sala ni unyenyekevu, bidii, na kujipalia msaada. Faida ya kuabudu ni mwungano na Mwenyezi Mungu na kuanza kumjua Yeye. (*Kila mmoja wao, sifa, sala na ibada, ni za namna mbili*, viz, dhahiri, saguna na kinyume ni nirguna.)

**Stuti au Kuimba Sifa za Mungu.**

Q. Zieleze hizo wazi wazi.

A. Yaj. 40. 8. Kwa mfano, Mungu ameenea ~~kote~~ Roho Takatifu, mwepesi kuliko mwepesi zaidi, mwenye nguvu zote, mtakatifu, mwenye kujua yote, roho ya ndani mwenye kutawala ni wa milele, anayejitosheleza mwenyewe Mungu Muweza. Yeye ni mgawaji anayetufungulia wazi elimu ya kweli ya vitu kutokana Vedas, injia ya haki ya elimu, kwa watoto wake wa milele kutokana na kwa yote ya daima na milele. Haya ni maelezo halisi Mungu au Saguna Stuti, haya ni kusema, kutambua sifa halisi za Mungu. 2. Yeye hana mwili, ni kusema hivyo. Yeye hana umbo au kuwa alizaliwa na wanawake. Yeye hagawiki, wala hana *mishipa na mambo mengine*, na katu hafanyi maovu. Maumivu, adhabu na ujinga hana kabisa Yeye maelezo ya namna hii ya Mungu, ambayo yanapinga sifa za mwunganisho, chuki, na sifa nyinginezo za Mungu, inaitwa kuwa ni maelezo yaliyo kinyume na maelezo ya Mungu au Nirguna Stuti.

Sifa nzuri lazima ziigwe katika tabia zake mtu mwenyewe na katika vitendo; katika maneno mengine, mtu lazima mwenye kufuata haki kama Mungu. Msemo wake wa Mungu huwa hauna maana, yeye ambaye anarudia sifa zake kama mjinga au kasuku bila ya kuyafuata na kuendeleza mbele tabia zake mwenyewe.

**Sala.**

Yaj. 32. 14. Ewe Mungu! mwenye utakatifu Mwenyezi Mungu, tufanye sisi tuwe na hekima katika maisha haya, tubariki sisi na hekima kwa madaha Yako ambayo wataalamu na wacha Mungu wakusalia Wewe.

Yaj. 19. 9. Wewe ni Mwangaza, utue huo mwangazi katika mimi pia na kwa madaha yako. Wewe unao ushujaa usiokwisha, mimi pia nivike huo ushujaa kwa mwema wake! Wewe una nguvu za milele, mimi pia nipe nguvu. Wewe unawo uwezo usiokwisha, mimi pia ni uwezo kamili pia! Wewe huonyesha ushungu wa vitendo viovu na kwenye vitendo visivyo vya insafu, itengeneze tabia yangu ikufuate Wewe. Wewe kuvumilia masengenyo yote, kusifiwa na watu na pia kuwavumilia wenye dhambi kwako, nifanye niwe mvumilivu kama Wewe!

**Usafi wa Akili**

Yaj. 34. Ewe bahari ya huruma, iwe nia yangu ijitolee kwa wema kutokana na madaha Yako; i.e. madhumuni iwe kuendeleza faida za viumbe wenzangu na mwenyewe pia, na katu nisiingiliwe na kuwafanyia wenzangu madhara.

ib.2.Ee mdani wa wote! weke nia yangu kwenye wafanyao wema na katu nisifanye ubaya na nishike pale ambapo penye kuwahifadhi wataalamu na kuwafanyia kazi zao na kuchukua nafasi zao vitani na katika vitindo vyenginevyo, niwe wa namna mbali, mwenye nguvu nyingi, na mbaya na kukaa katika viumbe vyote.

Ifanye nia yangu (manas) ambayo ni elimu bora zaidi, inayo waamsha wengine, na kuwa katika hali ya kutojua, ambayo ni taa ya milele ya viumbe na bila ya kuwa na kifo, na bila hiyo hapa awezae kufanya hata kazi ndogo ya namna yo yote, iwe mbali na sifa za uhalifu na ijae utakatifu na uadilifu mwingine.

ib. 4. Ewe Bwana wa dunia, ifanye nia yangu iwe sawa kama inavyowailimsha wanaojua yale yaliyokwisha pita na ujuzi wakujua yatakayokuja na yaliyopo sasa; kama vile akili ya milele ya mjuzi wa yote kwa kumweka yeye karibu na Mwenyezi Mungu; kama elimu inavyo rithiwa na kitendo kama kinavyofuatana na hisia tano za asili, akili na roho ya binadamu; na kama inavyokua inaweka akili yote; na itunukiwe na mwungano na elimu ya dini, kwa kuwa huru na vizuizi vyote na shida.

ib.5. Ewe Bwana wa wote mwenye elimu kubwa! ifanye nia yangu ipate elimu ya Rig. Yajur, Sama, na Atharva Vedas kama spoke za gurudumu zinavyoungana kwenye kitovu chake; na iwe kama inadhihirisha nafsi, mjuzi, aliyeenea kote, shahidi wa viumbe na mwondoshaji wa ujinga, daima ijitolee kwenye elimu.

ib. 6. Ewe mtawala wa yote Bwana! ifanye nia yangu ambayo ni kama nia za wote, ambazo zinawachukua watu sana huku na huku kama lijamu ya farasi kwa wingu au mpiganaji vita anavyo wapeleka farasi wake, na inajiweka katika roho kwa hamu, na kwa wepesi sana, zizuie nia zangu zote kutokana na adabu mbaya na daima ziongoze kwenye njia iliyo ya ukweli. Nipe mimi baraka hizi. Ee Bwana!

Yaj. 40. 16. Ee Mwenyezi Mungu! mtoaji wa furaha, unaye jiangaza mwenyewe, mjuaji wa yote! tubariki sisi na mpango kamili wa elimu kutoka kwenye njia nzuri, tuweke sisi mbali na vitendo viovu na tabia mbaya katika sisi. Kwa unyenyekevu wote, sisi tunaimba utakatifu wako mwingi sana, Ee Mungu tufanye sisi tuwe watakatifu.

Ee Mshindi! (Rudra) Mungu Muweza ambaye anawatembelea waovu kwa dhuki kama ni natifa ya uovu wao, usiwake dhiki vijana wetu, vizeee, watoto, mababu, wamama, wapenzi wetu, na majamaa, kuangamia. Tuongoze sisi kwenye njia ambapo sisi hatutafanya, dhambi na tusitiwe adabu na wewe!

Ee Mwalimu Mkubwa, Mwenyezi Mungu tuongoze sisi kutoka kwenye njia ya uwongo na kuelekea kwenye ukweli, na tuhifadhi sisi kutokana na kiza cha ujinga na kutuweka kwenye mwangaza wa elimu, na tuhifadhi sisi kutokana na maradhi ya mauti na tupe sisi furaha ya uwokovu na ya milele. Kwa maneno mengine (saguna) iliyo ndio (nirguna) maombi yaliyo ya kinyume ni kuwa Mungu anatajwa kwa kufikiriwa Yeye na mwenyewe kuwa karimu au kuwa mbali na sifa nzuri au mbaya kama ni uthibitisho wa kujua matokeo ya ufungamano au udhihirisho. Shat XIV, 3, 1, 30.

**Matumizi ya Ibada**

Mtu lazima afanye yale anayoyaabudia. Kwa mfano, mtu anaye omba *ufahamu mwema, lazima ajaribu sana kufuata huo ufahamu. Kwa maneno yaliyo* rahisi, mtu lazima ajirejeshe kwenye ibada baada ya juhudi yake mwenyewe. Mtu

yo yote asiombe dua ambayo Mungu hawezi kuikubali, kama - Ee Mungu, waangamize adui zangu, nifanye niwe mkubwa kuliko wote, mimi peke yangu nihishimiwe, wengine wote wanitegemee mimi na wewe chini yangu na mengineyo. Kwa sababu, ikiwa maadui wawili wanaomba uangamizo wa kila mmoja wao, basi jee Mungu atawaangamiza wote wawili? Ingekuwa ni bora dua zake zikubaliwe au kufaulu yule mwenye mapenzi zaidi, inaweza kujibiwa kuwa adui wake atapata adhabu kidogo ambaye mapenzi yake ni haba. Dua kama hizo huwashajiisha watu kuomba wanapokuwa na makosa: Ee Mungu tupe mkate uliokwisha pikwa, ifagie nyumba yangu iwe safi, zifue nguo zangu, na nilimie mimi viwanja. Watu wanaotegemea msaada wa Mungu kufanyiwa yaliyoelezwa hapa na wanapoteza wakati wao bure na kuwa wavivu, wao ni majuha wakubwa. Kwa sababu, yule ambaye anavunja amri ya Mungu ya kujichokesha hawezi kuwa na furaha. Hii ni.

Ygi XL. 2. Mungu anaamrisha kuwa mtu lazima atake kuishi miaka 100, i.e. maisha yake yote, na afanye kazi saa zote. Yeye asiwe mvivu. Aone wanyama wote na vitu visivyo na uhai vilivyoumbwa wanafanya kazi zao za kawaida na daima wanazifanya vilivyo. Mtu inambidi ajifunze na kutokana na ardhi na sayari ambazo daima vinakwenda na kuzunguka na kutokana na miti ambayo daima inaota. Mungu humsaidia mtu ambaye anafanya kazi za ibada kama mtu mmoja anavyomsaidia mwingine anaye fanya kazi. Mungu hukukalidua za mwenye huruma, lakini katu hawa saidii watu katika vitendo viovu, kama watu humwandika kazi yule anayefanya kazi na si yule aliye mvivu anaye jikalia tu, la, wao hawataki hata kuona uso wake; watu humwonyesha mtu njia kwa macho lakini humwonyeshi kipofu na akaweza kuona. Ikiwa mtu anasema kuwa sukari ni tamu, lakini hajikeri nafsi yake kuitafuta, basi yeye hawezi kuipata sukari, wala hawezi kuipata ladha yake. Lakini mtu anayejihangaisha, huifikia sukari bila ya muda mrefu kupita.

**Upasana: Ibada,: Inayomfanya Mtu Kuwa Karibu sana na Mungu.**

Ni ubeti wa Upanishat. Maana yake ni mwenye ujuzi wa kuwa na mwungano na Mungu na mtu, ambaye fikra zake zimezama katika kumfikiri Mungu, ambaye yeye ni mwenye Mungu, na yeye ambaye ujinga wake na uovu mwingine unaondoshwa kutokana na mwunganisho, hauwezi kuelezwa kwa maneno kwa sababu unahisiwa katika roho na fikra za ndani kabisa. Neno Upasana (ibada) maana yake ni kumjua Mungu. Maelezo yote ya namna nane za yoga au namna za kumfikiria Mungu, lazima ziendeshwe zote ili kutanabahi au kumwomba Mungu kwa roho yote, anayeenea kote.

**Yamas na Niyamas.**

Yoga. I. 30. Mithali hii inatoka katika falsafa ya Yoga. Maana yake hasa ni kuwa yeye ambaye anataka kujua ibada, basi achukue hatua muhimu kama yeye asimchukie mtu yo yote, daima awapende wote, kusema kweli, katu asiseme uwongo , kutoiba kamwe, uwe mwaminifu katika mambo yake, awe mtakatifu au aweze kuzizuia hisia zake, kutokuwa mdanganyifu, kuwa mnyonge na si

mutakabir. Hizi sifa tano (yamas) pamoja huifanya kuwa ni sehemu ya kwanza ya Yoga au ibada.

Yoga. I. 32. Mtu lazima ajiweke msafi wa nafsi kwa kuyawacha yale yote ya chuki na ubaya na usafi wa nje kwa kutumia maji ya kukogea na usafi mwingine kama huu. Mtu lazima ajichokeshe kwa haki na ukweli. Yeye lazima asiwe na furaha nyingi au kujidai anapopata faida au bahati, wala asihuzunike akipata hasara. Yeye awe na bashasha, auwache uvivu, daima awe na nashati, avumilie raha na maumivu. Yeye afuate dini na sheria zake lakini katu asifuate kutokuwa na dini. Yeye lazima asome na asomeshe maandishi ya kweli na vitabu vyenginevyo na awe na marafiki wazuri. Yeye lazima afikirie sana maana ya Om, jina takatifu ya Mungu, ambalo yeye alitamke kila siku. Yeye lazima ayatolee maisha yake kufanya na kuzitekeleza amri za Mungu. Hizi sifa tano (niyams) pamoja ndiyo inaitwa sehemu yapili ya Upasana au ibada. Sehemu yingine sita au daraja za ibada zimetolewa katika "Utangulizi kwa Sharti juu ya Rig. na Vedas nyingine".

Mtu anapotaka kufanya ibada, yeye afuate intidhamu, na ajiweke pahali mbali, pahali safi, ajikalishe kwa raha, ajizoeze kuvuta pumzi za nguvu, azitazame fikra zake kuhusu vitu vinavyoweza kuonekana na asiweke fikra zake katika tumbo la dini, moyo, shingo, taji, kufuli, au po pote penye utii wa mgongo.

Yeye ajifikirie mwenyewe na Roho Takatifu na wajishughulishe katika kumfikiri Mwenyezi Mungu, apate nguvu za Sanyama au ustadi.

**Matumizi Ya Ibada.**

Mtu anapofanya mambo haya, akili yake na hisia zake za ndani hutakasika na hujaa ukweli. Yeye kila siku huendelea katika elimu ya dini mpaka anafikia uokovu. Yeye ambaye anafanya mazoezi ya ibada kama ilivyoelezwa, hufaulu daima. Sasa ibada ya kweli ni kumfikiri Mungu kuwa ni mwenye uwezo wa kujua yote na mengine kama haya; na kinyume cha ibada ni, kujishughulisha na kumfikiria Mwenyezi Mungu aliyeenea ndani na nje ya roho, na kama kuwa yuko mbali na sifa za vitu, kama umbo, ladha, harufu, mguso na kadhalika. Matumizi ya ibada ni kitu ambacho kiko sawa na mtu anayetetemeka kwa baridi lakini anaanza kuona raha anapo ukaribia moto ambawo unamwondolea baridi. Kwa njia hii hii, kumkabili Mungu uovu na dhiki zote huondoka na tabia hutakasika, vitendo vya roho pia na huijaza hiyo roho kwa uadilifu sawa na ule wa Mungu. Kwa hivyo, ni lazima kufanya tena ibada ya Mungu, kumsalia yeye, na kumwabudu yeye. Lakini pia kuna faida nyingine inayopatikana unapofanya hivyo, nayo ni, roho itakuwa na nguvu na kuweza kuiweka akili iwe timamu hata katika milima ya dhiki na shida. Yeye ataweza kuyakabili yote haya. Jee ni faida ndogo hiyo? Yeye ambaye hafanyi tena ibada za Mungu, sala Zake na kumwabudu Yeye, huwa hawana hisani na ni mjinga mkubwa pia kwa hivyo, ni kutokuwa na hisani na dharau ya kijinga kuzisahau baraka zake, la, kuto kumwamini Mungu, ambaye ametupa vitu vyote hivi duniani ili roho zistarehe.

Q. Vipi Mungu anaweza kufanya kazi za akili, ilhali yeye mwenyewe hana macho, mashikio, na mengineyo?

Ubeti huu ni wa 19 wa sura ya 3 ya Shwetashwatar Upanishat. Una maana kuwa, Mungu hana mikono, lakini Yeye anatengeneza na kuishika dunia uzima kwa mkono wake wa nguvu. Yeye hana miguu, lakini ilivyokuwa yuko kote, Yeye ni mwepesi wa wote katika mwendo wake Yeye hana kiungo cha kuonea lakini Yeye anawaona viumbe vyote katika mwangaza wao wa kweli. Yeye hana mashikio, lakini Yeye anasikia sauti za wote. Yeye hana ujuzi wa ndani, lakini Yeye anajua yote. Hapana hata mmoja duniani anaye mfahamu Yeye. Kwa kuwa Yeye ni wa milele, bora kuliko wote na ameenea pote, Yeye anaitwa Purusha au Mwenyezi Alieenea kote. Yeye anafanya kazi ya akili na ya moyo kwa Uwezo Wake.

Q. Watu wengi wanamfikiria kuwa hatendi wala hajui.

A. Ni ubeti wa 8 wa sura ya 6 ya Shwetashwatar Upanishat. Maana yake ni - Hapana tawi au uzazi wa Mungu, aliyefanana na tabia yake Yeye. Yeye hana haja ya mwingine amwendeshe au kitu cha kufanyia kazi yake. Hapana aliye sawa na Yeye au mkubwa kuliko Yeye. Nguvu zake hazina kifani, ni kusema kama, Yeye ana elimu isiyo na mwisho, nguvu zisizo na mwisho, na uwezo usio na mwisho. Vyote hivi ni kitu kimoja cha tabia Yake. Ingekuwa Mungu hana uwezo na nguvu, Yeye asingeweza kuifanya na kuiweka na kuiangamiza dunia. Hivyo yeye Yuko kote, na alivyo ana akili yeye ana nguvu na uwezo wa kutenda?

Q. Yeye anapofanya kitu, ni cha maisha au si cha daima?

A. Ilivyokuwa Yeye ni mwenye busara na mjuzi wa yote, Yeye vitendo vyake vina mpaka na wakati ulio sawa. Yeye hafanyi vitu zaidi au kasoro.

**Pasipo Mwisho wa Mungu.**

Q. Jee Mungu anajua mpaka wake mwenyewe?

A. Mungu ni mjuzi wa kila kitu, na anawo ujuzi kamili ambawo unamfanya yeye ajue vitu katika mwangaza wao wa kweli au kama wao walivyo katika tabia zao. Mungu hana mpaka, hivyo ujuzi wake mwenyewe kama hauna mpaka ni wa tabia na wenye elimu ya kutosha. Kinyume chake itakuwa ni ujinga. Ni elimu ya matatizo kufikiria kitu kisicho na mpaka kama chenye mpaka na hivyo. Yathartha darshanam jnanam - Elimu ya kweli inayo mkisio wa kitu kwa mujibu wa sifa, tabia na nguvu, na watumizi yake. Kinyume cha elimu hii ni ujinga.

**Kuwepo Kwa Mungu.**

Mungu ni wa pekee, naye yuko mbali na ujinga na upungufu mwingine wo wote; kutokana na matakwa maovu kuchukia na tamaa ya kufurahia matunda ya vitendo vya mchanganyiko. Yoga 1, 24.

Hapana uhakikisho wa kuwapo kwa Mungu ambawo unaweza kutazamiwa kuwa ni ushuhuda wa akili (pratyaksha) Hapo pasipo na uhakikisho wa hisia, mitihani mengineyo, kama kurejea kwa na kama sheria za mantiki zitumike. Pia, inaweza kuwapo kuhusu mantiki ili kutaka uhakikisho kama sifa unazozaliwa

nazo katika kitu. Kitakatifu. Tena hapo kutokuwapo kwa ushahidi wa akili na mantiki huondoka yote haya kwa satwa za maandishi matakatifu au watu wenye elimu. Hatahivyo kuwepo kwake Mungu hauwezi kuhakikishwa. Sankhya 1. 12. 5. 10.

A. Hapana ushahidi wa akili wa kuwepo kwa Mungu, iliyofikiriwa katika mithali ya hapo juu, wala Mungu si sehemu ya kitu cha dunia. Mungu Muweza anaitwa Purusha kwa kunena aliyeenea kote duniani kwa kuwa Yeye ni tafauti na mtu haya ni kusema, kutokana na kuenea katika vitu vyote. Mtu (mimi) pia anaitwa Purusha kutokana na kuenea katika mwili wote. Kwa sababu, inasemekana kuhusiana na mambo haya.

Sankhya. V. 8. 9. 12. Ikiwa hakuna mwungano wa Purasha (Mungu) na Pradhana (tabia) mwungano wa sehemu katika Mungu zitakuwa hazi epukani au mchanganyiko huo utatokana na Mungu. Mchanganyiko huo unapatikana duniani, ambawo ni mazao ya mwungano wa tabia (kitu) na nguvu (zisizoonekana). Katika njia hii Mungu angekuwa mchanganyiko. Kwa hivyo, Mungu si sababu ya kitu cha dunia, lakini Yeye ni kitu au sababu muhimu yake. Ingekuwa dunia imezaliwa kutokana na akili, ingekuwa yenye nguvu zote kama Muweza, hiyo ni chemu chemu ya nguvu na mali zote. Lakini kama ilivyo si sababu ya vitu inayoifanya dunia, lakini kama inavyosemekana hapo juu. Yeye ni muhimu au sababu ya busara. Pia, Shwetashwatar Upanishat huifanya tabia (kitu) kuwa ni kitu cha kusababisha dunia. Hivyo:-

Ni ubeti wa 5 kutoka kwenye sura ya tatu. Tabia (Prakriti) ambayo inaumbua na inafanywa sathwa (akili) raja (nguvu), tama (nguvu au kitu), zinatiwa katika kiumbe katika umbo lake na maumbile kwa maneno mengine, Tabia huchukua hali mbali mbali ambazo zinaweza kugeuka na Mungu ilivyokuwa hawezi kugeuzwa, katu hageuzi. Hali yake na kuonekana katika umbo jengine. Yeye daima habadiliki na yuko kimya. Hata hivyo, yeye ambaye anaichukulia. Kapilacharya kuwa hana dini, yeye mwenyewe yuko hivyo Walii hakuwa mtu asiye mkubali Mungu; pia Mimansa si kama haimkubali Mungu kama vile inavyo ifanya dharma (sifa) na dharmi (kitu) Vaisheshika inasema wazi wazi kuhusu Ishwara (Mungu) Nyaya inamwita Mwenyezi Mungu Atma kwa hivyo yeye Muweza anaitwa. Ishwaro (Mungu) ambaye ana uwezo wa kuwepo kote na sifa nyinginezo.

Nani ameenea kote, na mwenye elimu isiyo na mpaka na sifa nyinginezo, na yeye ambaye ni mdani wa roho zote. Huyu ni Mungu kwa mujibu wa Mimansa Vaisheshika na Nyaya.

**Itikadi Ya Kuzaliwa Tena.**

Q. Jee Mungu ana nyama, au jee Mungu anazaliwa tena?

A. La, Munga hazaliwi tena. Inasema Yajur Veda:

Umoja au Upweke wa Mungu hauza hiwi. Yeye ni mtakatifu na si kama kitu

cho chote na mengineyo. Amri hizi zinahakikisha kuwa Mungu katu hazaliwi.

Q. Bwana Krishna anasema (Gita, IV. 7) kuwa yeye anazaliwa pale dini au uadilifu unapodharauliwa.

A: Kuwa Kinyume cha Vedas, maneno haya hayawezi kukubaliwa kuwa kweli. Lakini inawezekana kuwa Bwana Krishna alitaka kuihifadhi dini na mawalii na ndiyo akasema yeye atazaliwa tena katika umri wote ili kuwahifadhi waadilifu na kuwaangamiza waovu, haya ambayo hayawezi kupingwa; kwa sababu:- Mwili, roho na mali za watu wazuri yote haya ni kwa manufaa ya watu. Hata hivyo haiwezi kuleta uhakikisho wa utakatifu wa Bwana Krishna.

Q. Ikiwa ni hivyo, kwa nini watu huzungumza na kuamini kuzaliwa tena mara 24 kwa Mungu katika dunia?

A. Wao hufanya hivyo, kwa sababu hawajui maana yake Vedas. Wao wanapotezwa na dini zao, wao wenyewe ni wajinga, na wanaangukia pale penye shaka na patupu. Kwa hivyo, wao husema na kuamini katika mambo mabaya kama haya.

Q. Ikiwa Mungu hazaliwi tena duniani vipi Kansa, Ravana, na majambazi wengine wataweza kuuliwa?

A. Kwanza; yeye ambaye amezaliwa na mwanamke, lazima akionje kikombe kichungu cha mauti. Kansa, Ravana na majini wengine wao si kitu mbele ya Mungu, ambaye anaumba, kuhifadhi na kuiangamiza dunia bila ya kuzaliwa tena au bila ya kuwa na umbo la binadamu. Kuwapo kwake kote, Yeye huijaza miili ya Kansa, Ravana, na majini wengine. Yeye anaweza kuwaua wakati wo wote Yeye anaopenda kwa kuangamiza umuhimu wao. Yeye anaweza kwenda kwa jina jengine, lakini mjinga anayesema kuwa Mungu mwenye sifa zisizo na kikomo, vitendo, na tabia, anazaliwa na anakufa ili amuue kiumbe kisicho kuwa na maana? Ya pili; ni uwongo kusema kuwa Yeye amezaliwa ili awahifadhi wenye dini na watiifu; kwa sababu kuwahifadhi mawalii wanaotenda kwa mujibu wa amri Zake, Mungu ana nguvu zote. Kwani vitendo vya kumua Kansa, Ravana na majini wengine, na kunyanyua Govardhana na milima mengine, ni vikubwa zaidi kuliko vile vya Mungu kuumba dunia jua, mwezi na sayari nyinginezo kuvihifadhi na kuiangamiza? Ikiwa mtu atafikiria kazi za Mungu katika kuumba, yeye atamalizia, bhuto na bhavishyati, kuwa hapana mwingine, wala hapata kuwapo mwingine kama Mungu. Ya tatu; sababu hazihakikishi kuzaliwa tena kwa Mungu. Ni kama kusema kuwa nafasi isiyoonekana inaletwa katika tumbo la uzazi au inashikwa katika ngumi ya mkono, ambayo ni uso usioelekea, na haiwezi kuwa kweli. Kwa sababu nafasi haiwezi kupimika na ipo kila pahala na kwa hivyo haiwezi kutiwa katika kitu au eneza nje ya kitu. Kwa namna hii Mungu kuwa yupo kote na ameenea kote, haiwezi kusemwa kuwa aje au aende pahali po pote. Mtu kuja kwake na kwenda kwake. Kuja kwa mtu na kwenda pahali kadha hufanyika tu pale yeye anapokuwa hayuko. Kwani Mungu hakuwapo katika tumbo la uzazi hata Yeye akatoka kutoka humo? Yeye

hakuwapo nje ili yeye ametoka kutoka ndani? Nani bali wajinga tu wanaweza kusema ya Mungu na kuyasadiki. Kwa hivyo, kuingia na kutoka kwa Mungu, kuzaliwa na kufa hakuwezi kuhakikishwa.

Pia, lazima ufahamu kuwa Yesu na watu wengine kama yeye hawakuzaliwa tena kutokana na Mungu. Kuweza kutaka, kuchukua, kusikia njaa, kiu, khofu, huzuni, furaha, maumivu, kuzaliwa, kufa, na sifa nyinginezo za binadamu, wao walikuwa wanaume.

**Msamaha wa Dhambi**

Q. Jee Mungu huwasamehe dhambi za mawalii na watifu wake?

A. La, kwa sababu, ikiwa Yeye atawasamehe dhambi zao, haki Yake itaondoka na watu wote watafanya dhambi. Wakijua kuwa dhambi zinasamehewa, wao watafanya zaidi na kupata nguvu za kuwa waasi. Kama mfalme anapousamehe uhalifu raia zake watakuwa hawana khofu kufanya zaidi, na vibaya zaidi na zaidi kuliko za kwanza. Kwa sababu, wao huamini kuwa mfalme atawasamehe na wao wanao uhakikisho wakupata msamaha kwa kumsujudia mbele yake. Tena hawa ambawo hawafanyi uhalifu, wataanza kufanya maasi ilivyokuwa hawana wasi wasi wa matokeo yake. Hivyo, ni wajibu wa Mungu awahukumie kwa vitendo vyao kwa mujibu wa sifa na aibu zao, na si kuwasamehe.

**Uhuru wa Roho**

Q. Jee roho inatawaliwa au iko huru kufanya, au yeye anavitegemea vitendo vyake kwa Mungu?

A. Yeye yuko huru kufanya kazi zake, lakini azifuate sheria za Mungu, Swatantrah karta - Mithali hii ya Panini maana yake ni mfanya kitendo ni yule ambaye yuko huru, au hatawaliwi.

Q. Unakusudia nini kusema kama huru hatawaliwi?

A. Mtu yule yuko huru ambaye mwili nguvu za utu, akili, hisia za ndani na viungo vinginevyo ni muhimu. Ikiwa yeye hayuko huru kufanya atakavyo, yeye hawezi kuwa mtiifu wa kuwa mwadilifu na adu wa vitendo vyake. Kwa mfano, maaskari wa jeshi lo lote wanawauwa watu wengi katika vita au kwa uchochezi wa bwana wao na kamanda, na wao hawashitakiwi kuwa wameua. Kwa njia hii hii, ikiwa watu watafanya cho chote kwa mujibu wa amri au kwa nguvu walizopewa na Mungu, sifa njema au mbaya haiwezi kuwatokea wao. Mungu atafurahia matunda ya vitendo vyao. Pepo au jahanam, i.e raha au maumivu, yatakufa kwa ujumla kwa Mungu. Mtu anaye mwua mwenzake kwa silaha, anatiwa adabu peke yake, lakini si silaha yake. Kwa namna hii hii, roho inayojitegemea haiwezi kuwa na dhamana kwa uwema au uovu wa vitendo vyake yeye. Hivyo, roho ziko huru kufanya zinavyotaka kwa nguvu zao wenyewe. Lakini zinapofanya dhambi, wao wanapata shida za vitendo vyao kwa mujibu wa sheria za haki za Mwenyezi Mungu. Kwa hivyo, roho inayo uhuru wake wa kutenda, lakini inamtegemea Mungu kuvuna matunda ya vitendo vyema au viovu.

Q. Ingekuwa Mungu hakuzifanya roho na kuziipa nguvu, isingeweza kufanya kitu. Kwa hivyo, roho hufanya kwa lazima au nguvu kutokana kwa Mungu.

A. Roho haifanywi au haiumbwi. Hiyo haina mwanzo kama Mungu, na sababu za kitu duniani ni kama kuzitumikia kadhia tu. Makao ya roho, mwili na tundu za hisia zinatengenezwa na Mungu. Lakini vyote hivi vinavitegemea roho. Yeye ambaye anafanya dhambi kwa fikra, maneno, au vitendo, huadhibika peke yake kwa matokeo ya vitendo vyake, lakini si Mungu. Kwa mfano, mtu fulani kachimba chumba kutuka kwenye mlima, na akamwuzia mfanyi biashara, na kwake yeye mhunzi akainunua hiyo chuma na akatengenezea upanga. Askari akaununua huo upanga na akamwua mtu kwa upanga huo. Kwa njia hii hii, Mungu mwumba wa mwili na viungo, hapati adhabu za matokeo ya vitendo vyake mwili, lakini huifanya roho iadhibishike. Ingekuwa Mungu alikuwa ni sababu au mchochozi wa vitendo, hapana mtu ambaye angekuwa ana dhambi; kwa sababu, Mungu alivyokuwa ni mtakatifu na ukweli, hawezi kumshawishi mtu kufanya uovu. Kwa hivyo, roho iko huru kutenda. Kwa njia hii hii, Mungu pia Yuko huru kutenda.

**Sifa za Mungu na Roho.**

Q. Aina gani za umbo, sifa, tabia na asili walizonazo roho na Mungu?

A. Zote mbili zina akili, na asili za zote mbili ni takatifu, haziwezi kufa, na zenye uadilifu. Lakini vitendo vya Mungu ni kuitengeneza dunia, kuitunza na, na kuiangamiza, kuviweka vitu vyote pahali pao na kuvifanya vifuate sheria, kuvitunza kwa zawadi na kuvitia adabu kwa wema na uovu, na wajibu mtakatifu kama huu. Kazi za roho ni kueneza uzao, na kuvitunza vizazi vyao, kutengeneza na kazi nyinginezo, kufanya wema au ubaya. Sifa za Mungu ni elimu ya milele. furaha, mjuzi wa yote, na nguvu nyinginezo zisizo onekana. Sifa za roho ni:- Ny. 11. 10.

Vai, III, II, 4. Ichha: matamanio ya kupata vitu; dwesha: kuchukia maumivu na maovu; prayatna: ushujaa na nguvu; sukha: furaha; dukha: masikitiko na majonzi; jnana: busara, elimu, makumbusho, ni sifa za roho mashuhuri kwa Nyaya na Vaishashika; lakini ya pili pia ina prana: kutoa puumzi; apana: vuta puumzi; nimesha: kufunga macho; umesha: kuyafungau; mano: imani, makumbusho, ufahamu; gati: mwendo; indriya: intidhamu ya akili; antarvikara njaa, kiu, furaha, huzuni na mapenzi mengineyo; ambazo sifa za roho ni mbali na za Mungu. Hizi ni tabia ya kujua kuwepo kwa roho: kwa hivyo, hiyo roho si yenye mwili. Sifa hizi huwepo hapo, roho inapokuwa ipo katika mwili tu. Lakini inapotoka katika mwili yote huondoka kutoka kwenye mwili. Kwa sababu, sifa ambazo zinakuwapo kwenye kitu na inapokoma kuwapo, ni sifa zake muhimu. Hivyo, mwangaza unakuwa haupo ikiwa hapana jua au taa, lakini daima huwepo ikiwa jua na taa zipo. Kwa njia hii hii, elimu ya Mungu na roho inawezekana kutokana na sifa zao tu.

**Busara ya Mungu na Uhuru wa Mtu.**

Q. Mungu anaona yaliyopita, yaliyopo sasa na yatakayo kuja baadaye. Yeye, kwa hivyo anajua kitatokea nini katika siku zijazo. Cho chote anachokusudia Yeye roho itafuata. Hivyo roho haipo huru, na Mungu hawezi kuitia adabu kwa haki; kwa sababu roho inafanya kadiri Mungu ameamua kwa wema wake na kwa elimu yake ya kuona mbele.

A. Kusema kama Mungu anaona sehemu tatu za wakati, ni kitendo cha ujinga. Kwasababu yaliyopita yalikuwapo na hayapo sasa, na ya baadaye ni yatakayo tokea hapo, hayapo bado. Kwani Mungu husahau yale aliyo yajua hapo zamani? Jee Yeye atajua yale ambayo hayajui hivi sasa? Hivyo elimu ya Mungu iko sawa daima, bila ya mkato, ya daima na ya sasa. Yaliyo kwisha pita na ya sasa yanasemwa na mtu. Lakini ukuipitia elimu ya vitendo vya binadamu, inaweza ikasemwa kuwa Mungu ni mwonaji wa sehemu tatu za wakati. Kumhusu Mungu mwenyewe, hayo haya mwathiri yeye. Mtu anayo ya fanya katika uhuru wake mwenyewe, Mungu anayajua kwa nguvu za hisia zake. Roho zinatenda kama Mungu anavyojua, kuwa, Mungu anaijua elimu yake ya zamani ya sasa na ya baadaye na katika kuzifanyia haki roho kwa mujibu wa sifa zao. Roho pia ziko huru kwa mujibu wake hivi sasa na ziko huru kabisa kutenda. Kwa uwema wa elimu ya Mungu kuwa haina mwanzo, elimu Yake kote kuwili kwa vitendo vya roho na kuzitia adabu zinapovunja sheria Zake pia haina mwanzo. Namna zote mbili za elimu zake ni kweli. Inawezekana kuwa ujuzi wake wa vitendo vya binadamu ni kweli na ule ufuzi wa kuwatia adabu ni uwongo? Hivyo hakuna ubadilifu katika hali zetu sisi.

**Pahali Pa Roho Katika Mwili.**

Q. Jee roho imeenea katika mwili mzima au iko pahali pamoja tu?

A. Ipo pahali pamoja. Ingekuwa ipo mwilini kote, basi mambo kama haya ya kwenda, kulala, usingizi bila ya kuota, kifo, kuzaliwa, mwungano, mgawanyiko, mwingilio, matokeo katu yasengetokea. Hivyo, umbo la roho ni ndogo na haionekani, au bora zaidi, hafifu au yenye hila nyingi, na Mungu bado ana hila nyingi zaidi kuliko mwenye hila yo yote, asiye na mwisho, mjuzi wa yote, na ameenea kote. Ni kisa hichi ambacho uhusiano baina ya Mungu na mtu uhusiano wa aliyeenea kote na aliyeenewa.

**Uhusiano Baina ya Mungu na Mtu.**

Q. Kitu hakiwezi kuwapo pali penye kitu chengine ambacho kilikuwapo tokea hapo mwanzo. Kwa hivyo, uhusiano baina ya Mungu na mtu hauwezi kuwa mmoja wa kuenea na wa kuenewa, lakini mmoja wa mwungano au wa chama.

A. Sheria hii ni kweli kwa kuhusu vitu na vinginevyo kama hivyo, lakini ni ya namna tafauti. Hivyo, kwa mfano, chuma ni kizito au ni kikubwa kwa umbo na moto ni mwepesi zaidi na hafifu. Kwa hivyo, moto huingia kwenye chuma na nguvu za umeme huenea kwenye mbingu. Kwa njia hii hii roho ni nzito zaidi

:o Mungu, na Mungu ni hafifu zaidi kuliko roho. Hatimae Mungu huenea :a roho. Juu ya hayo uhusiano baina ya aliyeenea na aliyenewa uhusiano ıgine baina ya Mungu na mtu kwa upande mwingine ni aliyeokolewa na kozi, anayeabudiwa na anayeabadu bwana na mtumishi wake, mfalme na baba na mtoto, na mengineyo.

**ınzo Ya Vedant.**

Ikiwa Mungu ni tafauti na binadamu nini maana ya "mafunzo makuu" haya ıa vakyas) ya Vedas?.

Haya si mafunzo ya Vedas. Lakini ni vipande kutoka kwenye vitabu, 'yoitwa Brahmanas. Navyo haviitwa Mafunzo Makuu po pote katika ıdishi thabiti. Yana maana - aham: mimi brahma: katika Brahman au nyezi Mungu, asmi amini. Hapa umbola kuzirai limetumika. Kuwa. chah Kroshanti-Viazi vinaita. Lakini kila mmoja anajua kuwa viazi havina na kwa hivyo havina nguvu za kusema. Kwa hivyo sentensi hii maana yake ı watu wanaovikalia hivo viazi vinaita. Kwa njia hii hii, mafunzo yaliyotajwa juu lazima ya fasiriwe. Inawe kusemwa kuwa vitu vyote vinaishi na Mungu - :nstha (kuisha katika Brahman)? Inajibiwa kwa kukataliwa, kuwa kuwa vitu vyote vinaishi katika Mungu na hapana kitu kingine ıofanana kwa sifa na kumkaribia Mungu kama roho, ambayo inayo elimu ya nyezi Mungu na huwepo na Mungu wakati wa uwokovu. Kwa hivyo, ;iano wa Mungu, sifa za roho ni kuwepo, ni kusema kama, roho hukaa na gu. Lakini haihakikishi kuwa imefanana na Mungu na roho ya binadamu. o, ikiwa mtu anasema kuwa yeye na mtu mwingine wako wamoja, yeye usudia wao hawakatawi. Kwa njia hii hii, roho ilivyokuwa imenyweya a katika Mungu kutokana na mapenzi katika hali yake ya nguvu, inaweza, na au kufikiria kuwa Mungu na hiyo roho ni mmoja i.e. hazipingani, lakini ıngana na ziko karibu sana na wanaoishi nawo. Kuwa roho peke yake ıyo inatengeneza tabia zake, ghadhabu, na kitendo kwa pamoja na zile za gu inaweza kudai kuwa ni mwenzake au urafiki, au upungufu na Mungu.

Haya, utifasiri vipi hii: Brahmana au Mungu tram, wewe, roho,: (asi) ni i.e., ›ho, (twam) wewe (asi) ni (tat) Mungu?

Unakusudia nini kwa neno tat? Ikiwa unasema Brahma, hapo tena unatumia gufu huu? Imesemwa wapi hata iletwe hapa?

Kutokana na maamrisho yaliyotajwa kabla, viz.

Wewe hata hujaona hiyo Chhandogya Upanishat. Ikiwa wewe umeiona weza kuiona kuwa halipo kamwe neno kama brahma hapo. Wewe ;esema hivyo, ambayo ni uwongo. Kwa kinyume chake, Chhandogya ıishat inayo, hapa neno kama hili brahma ndani yake.

Basi wewe unakusudia nini kwa kutumia neno tat?

Kuwa Mungu inafaa kumjua, roho ya ndani kabisa, yeye ambaye ni mwema

kabisa na roho wa dunia nzima na roho ya binadamu, nafsi, na anajiweka mwenyewe - ch. Pr. 6 Kh, 8, M, 6, 7.

**O Shwetaketo. Mtoto wangu mpenzi!**

Wewe umeungana na Mungu, roho ya ndani kabisa. Tafsiri hii ni moja na ile ya Upanishats. Kwa sababu jumbo hili limetokana na Brihadaranyaka Upanishat. Shat. 14, 6, 7.

Rekodi ambazo wakati mmoja zilikuwa ni za hekima nyingi Yajnavalkya alimwambia mkewe Maitreyi: "Ee mpenzi, roho iliyo pumbavu haijui kuwa mwenyezi Mungu Manani, ambaye yuko hadhir daima kwenye roho, na pia yuko mbali naye pia, ameienea hiyo roho. Mungu, msikili wake au mwili wake ni nafsi ameienea roho kama roho ilivyoenea katika mwili. Kwa kuwa tafauti au mbali na nafsi, Yeye anayashuhudia mema na mauvu yanayotendwa, hutoa zawadi au nafua na adhabu kwa mujibu wa amali na huwafanya wafuate sheria Zake. Mungu huyo huyo wa milele ni roho ya ndani kabisa inayoamrisha, kwa maneno mengine amekuenea wewe, mjue yeye". Nani ataweza kuyafasiri haya? Ayamatma Brahma.

Mimi ni mwenyezi Mungu, hatamkwana na watu walio wachawi au samadhi, ni kuwama yeye anasema kuwa Muweza aliye kuwapo ndani yake yeye, yupo kila pahali. Kwa hivyo, wafuasi wa kisasa wa Vedanta wanao kuwa na uhakikisho wa Mungu na roho, hawajui falsafa ya Vedanta.

Q. Mungu anasema: Baada ya kuiumba dunia na mwili wa binadamu, Mimi nimeenea katika dunia na mwili kwa umbo la nafsi, ili mimi niweze kueleza majina na umbo la vitu - 'nama rupa,' dunia ya kupigiwa mfano. Mungu mwenyewe ameenea katika dunia baada ya kuiumba na mwili pia Haya ni maamrisho kutokana na wahii. Vipi wewe utaweza kuyafasiri haya vyengine? Ch. Pr. 6. Kh. 3. M. 2. Tait. An 6.

A. Ikiwa wewe unayajua maneno, maana yao, na maana ya sentensi, wewe hutayafasiri vibaya hivyo. Kwa sababu lazima ifahamike akilini kuwa hapa pravesh 1st (inaingia) na unaprawesh 2nd (inaingia baadaye) zinatajwa. Mungu anaonyesha taalim ya dunia na namna nyinginezo za elimu kwa mujibu wa Veda kama ikiwa yeye alingia mwilini baada ya roho kuingia. Yeye amezitia roho kwenye mwili na Yeye mwenyewe akaingia ndani. Ikiwa wewe unajua maana ya neno anu: baada, wewe katu hutaifasiri kinyume hivyo.

Q. Mimi ninamwona Deva Datta hasa huko Mathura wakati wa mvua, ambaye nilimwona Kashi wakati wa siku za joto. Hapa mfano wa mji wa Kashi na wa wakati wa joto unawekwa upande mmoja, na fikra ya Deva Datta inapewa umuhimu wote. Ni mfano wa umbo la kinyume - 'bhaga tyaga lakshana,' au madanganyo. Kwa njia hii hii, hali ya hewa kuingia katika majimbo yaliyofishika, wakati, maya (nguvu) na sifa nyinginezo za Mungu; na pia mahali, wakati ujinga elimu haba na sifa nyinginezo, kutokana na roho kwa sheria za

madanganyo; na kwa kufikiria sifa zao za akili peke yake, sisi tunaona lakini Brahman mmoja au Mungu tunatilia mkazo yote mawili. Hii ni lugha ya istiara, inayoitwa 'bhaga tyaga lakshana', ambapo mengine yaengezwa na mambo mengine yanatolewa. Hivyo kutukuwapo kwa sifa za Mungu za ujuzi wa yote na vile vile sifa zilizokuwa dhahiri na sifa za roho zenye mipaka ya ujuzi na nguvu, na kufikiria akili tu inahakikisha madhehebu ya kutokuwepo kwa miungu wawili: 'Adwaita'. Utaipa jawabu gani?

A. Wewe unaamini kuwa Mungu na roho kuwa ni ya daima?

Q. Sisi tuaamini kuwa zote mbili hufa, kwa kuwa zenye shuruti zenye kuwaza au kuwapo kutokana na upadhi - Matakwa, hisia, maisha.

A. Wewe unaamini upadhi (sifa zisizo muhimu) kuwa ni za milele, na daima?

Q. Kwa mujibu imani yetu.

Hii ni kitu cha Shariraka na mistari yake ni hii maelezo yake. Sisi wafuasi wa Vedanta, huamini sehemu sita za zisizona mwanzo, kwa majina ni 1. roho. 2. Mungu, 3. Brahman au Mwenyezi Mungu, 4. tafauti dhahiriri kati ya Mungu na nafsi, 5. ujinga, 6. mwungano wa ujinga na roho. Za hizi Brahman peke yake tu ndiye hana mwanzo na mwisho, na hizo tano zilizo bakia hasa tu ndiyo hazina mwanzo na mwisho; kama 'pragabhava'. Hizi tano huendelea zaidi endapo pana ujinga. Mwanzo wake haujulikani, kwa hivyo havina mwanzo. Hivyo huangamia elimu ya kweli inapopatikana, kwa hivyo yana mwisho na ni vya kupita njia tu.

A. Beti hizi mbili za Ki-Sanskrit zako si za kweli. Kwa sababu, kuwepo kwake Mungu hakuwezi kuhakikishwa kwa kuamini kwako bila ya mwungano wa madanganyo (maya) na (Mwenyezi Mungu) Brahman; Kuwepo kwa roho, bila ya mwungano wa ujinga na Brahman. Hivyo, 'tachichoteryogah', ambayo wewe unaihesabu kuwa ni kitu chenyewe hasa cha sita, hakipo; na kwa hivyo, imetiwa pamoja na vitu vitano hasa, viz taalima: avidya, madanganyo: maya, nafsi: jiva na Mungu: ishwara. Basi Mungu hajafanywa bila ya Brahman, madanganyo na elimu. Kwa hivyo, kumweka Mungu mbali na taalima na Brahman, ni ujinga. Hivyo, mambo mawili hasa tu yanaweza kuhakikishwa hasa katika mpango wako wakuamini, viz. Brahman na si sita kama yalivyotiwiwa mkazo mbeleni.

Pia, wewe unaweza kumhakikisha Mungu na roho kuwa wamestahikisha sababu na athari, pale wewe unapo hakikisha ujinga upo katika kisicho kuwa na kikomo, cha milele, takatifu chenye busara, huru, aliye kuwa yupo kote Mwenyezi Mungu (Brahman). Mungu kamili hawezi kuwa mtakatifu, ikiwa wewe unaamini ujinga upo katika sehemu ya Brahman au Mwenyezi Mungu, itakuwa inatembea sehemu zote zake (Mungu), kwa kutengana na si ya asili. Itaifanya sehemu ile ya Brahman kuwa ujinga, pale panapokwenda, na sehemu ile itangara kwa elimu pale palipoondoka. Katika hali hii wewe huwezi kuiita sehemu yo yote ya Brahman kuwa haina mwanzo, takatifu, na mjuzi wa kila kitu. Sehemu ya Brahman ambayo imo katika mpaka ya ujinga, itaweza kuuhisi

ujinga. Nje na ndani Brahman atagawanyika. Ikiwa wewe utasema hapana madhara ikiwa Brahman amegawika, hapo itakuwa haijagawanyika. Ikiwa yeye hajagawanyika, Yeye hawezi kuwa mjinga. Ujinga au maarifa yanayo kwenda kombo kuwa ni sifa, Yeye atakuwa na mwungano wa daima na baadhi ya vitu. Ikiwa hivyo, uhusiano wake au ujamaa kuwa muhimu inangeweza kuwa ni ya kupita au ya kupigiwa mfano wa ajabu. Kama mwili mzima huhisi maumivu ukiwa na jipu upande wo wote wake, basi pia Mungu mzima hupambana na ujinga, furaha, maumivu, na madhara mengineyo ikiwepo katika sehemu moja yake yo yote. Ikiwa wewe unadhania Brahman kuwa ni nafsi kutokana na sifa zinazo athiri na kutokana na mwungano wake na hisia zake za ndani, mimi ninakuuliza wewe ikiwa Brahman ameenea kote, au yeye yupo kwenye sehemu maalum tu? Ikiwa wewe utasema ameenea kote na sifa ni (upadhi) ni halisi au za sadfa, haya ni kusema, ipo kwenye sehemu moja tu na mbali, kwani hisia za ndani huondoka au ipo hapa daima bila ya kusogea?

**Hakuna Ujinga Katika Mungu.**

A. Inasogea.

Q. Brahman anasogea kwa hisia za ndani, au iko upande mmoja na haisogei?

A. Haisogei.

Q. Hisia ya ndani inapoiwacha sehemu moja ya Brahman, inajitoa kwenye ujinga, na sehemu ile ya Brahman ambayo imebayo imeshikana nayo, itageuka kuwa na ujinga. Pia, mambo yatakapo kuwa hivyo, uokovu na ya dunia au adhabu ya kutengwa na Mungu pia itakuwa ni ya muda. Hapata kuwapo na ukumbusho wa vitu vilivyoonekana au sikika jana, kama vile mtu hawezi kukumbuka yale aliyoyaona mwenzake; kwa sababu, ilipoonekana au sikika, ilikuwa wakati tafauti na pahali mbali; na ilipojaribiwa kukumbukwa, ilikuwa ni wakati mwingine na pahali pengine. Ikiwa itasemwa kuwa Mwenyezi Mungu ni mmoja na hajagawanyika na kwa nini yeye si mjuzi wa yote? Ikiwa wewe unaseama kuwa hisia za ndani ziko mbali mbali na kwa hivyo Brahman kuwa mbali mbali na alitafautishwa, kwa hivyo hana roho, na kwa hivyo itakuwa hana elimu au ujuzi. Ikiwa wewe utasema kuwa si Brahman wala hisia ya ndani inafikiria au inauwezo wa kuwa na elimu nyingi; lakini mwangaza wa ufahamu (chidabhasa) inayoishi katika hisia ya ndani (antah karana) huwa ufahamu au mpokeaji; kwa hivyo, kwa mwenye ufahamu huwa ni mpokeaji kutokana na hisia za ndani. Kwa nini basi haina nguvu na haba katika elimu ya jicho? Hivyo wewe huwezi kumfanya Mungu au kuanzisha ufafanuzi wa kuwepo kwake Muweza, Brahman na nafsi kwa mwungano wa sifa za vitendo na sababu zake. Lakini Ishwara: Mungu ni jina la Brahman, na nafsi; jiva ni dhahiri kutokana na Brahman asiye na mwanzo, asiyeumbwa, na asiyekufa. Ikiwa wewe utasema nafsi ni jina la mwangaza wa ufahamu - Chidabhasa, basi itaweza kuangamia kwa kuwa ya kupita tu. Nani basi atafurahia uokovu? Kwa hivyo, Brahman hajawa nafsi na wala nafsi haijawo Brahman, na pia katu hazitakuwa hivyo.

**Maelezo Ya Vedantic.**

Q. Chhandogya Upanishat, Basi vipi kutokuwapo wawili uhakikishwe? Namna zetu za kuamini huhakikisha kuwa ni Mungu mmoja tu (Brahman) kutokana na kutokuwapo na mwingine, isipokuwa Brahman, mbali, kama, asiyefanana na haonekani. Ikiwa nafsi ni nyingine kama hiyo, vipi kutokuwapo nafsi nyingine ibakikishwe?.

A. Kwa nini wewe unaogopa, kwa kuangukia kwenye madanganyo? Fikiri sheria za uwingi wa majina na sifa. Yanaleta faida gani? Ikiwa wewe utasema kuwa sifa zinasifu, lazima inataka ufahamu kuwa sifa huyasifu na kuyaeleza majina. Katika neno lakuzingatiwa ni adwaita (si-mbili) inaisifu jina Brahman. Sifa yake ni kuwa inamgawanya Brahman, yeye ambaye hana wa pili wake, kutokana na roho nyingi na vitu vingi, na sifa yake ya kueleza ni kuwa ina hakikisha umoja wa Mwenyezi Mungu mkubwa. - Brahman.

Hivyo, mtu alimwambia mwenzake kuwa Deva Datta alikuwa wa pili katika matajiri baina yao, na Vikram Singh alikuwa wa pili kwa yo yote baina ya watu mashujaa katika jeshi lile. Jee hii inahakikisha kuwa hakuna aliye tajiri isipokuwa Deva Datta mjini, na hapana aliye shujaa isipokuwa Vikram Singh katika jeshi lile? Hakika wako watu walio hafifu kuliko wao. Pana miviringo, sayari na vitu vyenginevyo kama hivi. Kuwepo kwao hakuwezi kukataliwa kwa kuwa ni wapili kwa visivyo kuwapo. Kwa njia hii hii, roho na tabia si kama Brahman, lakini hivyo ni hafifu kuliko Brahman.

Kwa hivyo imesha hakikishwa kuwa Brahman ni mmoja daima, na roho na vitu vipo katika mzingira navyo ni vingi.

Kuitenga mbali na mchanganyiko huo wote na kuhakikisha umoja wake, sifa adwaita au geni inatumika ya Brahman. Kwa vyo vyote ina hakikisha kutokuwapo kwa nafsi, tabia, na dunia ya ajabu, wala haikatai kuwepo kwao. Lakini, kinyume na haya, vyote hivi vipo, ijapokuwa si sawa na Brahman. Haileti madhara yo yote uthibitisho wa kutokuwa wawili au kuwapo wawili. Usibabaike. Fikiri na jaribu kuyafahamu haya.

Q. Sifa za kuwepo, akili nafuraha ya Brahman, na sifa za maisha, dhahirisho, na ukunjufu wa nafsi hudhahirisha mfanano wao. Kwa nini wewe unayapinga haya?

A. Mfanano wao hauwezi kuhakikishwa kwa kufanana na sifa zao kidogo. Hivyo, kwa mfano, vilivyomo na visivyomo vya dunia, maji, moto na vyenginevyo haviwezi kufanyika kuwa namna moja. Hivyo si vimoja na pia hivyo hivyo kama ilivyo hakikishwa na heshima zao na sifa zao zisizofanana, kama, harufu, maparuzo, ugumu, na sifa nyinginezo za dunia; na umaji maji, uwepesi, ulainifu, na sifa nyinginezo za maji; mwangaza, joto, na sifa nyinginezo za moto haviwezi kuhakikisha mfanano wa vitu hivi. Chukua mfano mwingine. Mtu na nyuki wanaona kwa macho yao, wanakula kwa midomo, wanakwenda kwa miguu, na hata hivyo wao si namna moja. Mtu anayo miguu miwili na nyuki anayo miguu mingi. Hizi sifa za kutofanana zinaonyesha kutofanana kwao. Kwa

njia hii hii, elimu isiyo na mwisho, furaha, nguvu, harakati, kiwa huru na madanganyo, na kuenea pote kwa Mungu ina heshimu. Yeye kutoka na nafsi, ambayo sifa zake si nyingi za elimu, nguvu, mwili, makosa, na mengineyo ambazo zina mweka mbali na Muweza. Hizi zinahakikisha kuwa hivi si vimoja. Pia sifa zao ziko mbali mbali. Mungu ni mwepesi zaidi na ni mwenye busara kuliko roho. Hata hivyo wao wako tafauti.

Q. Ni ubeti wa Brihadaranyaka Upanishat. Yeye huingiwa na hofu ambaye huonyesha tofauti baina ya Brahman na roho; kwa sababu, hofu huja kutoka kwenye roho.

A. Hiyo haisemi vile unavyofikiria wewe. Maana yake sahihi ni kuwa mtu anaweza kuwa na hofu ambaye anakataa kuwepo kwa Mungu, anayeamini kuwa Mungu anakikomo mahali kadha tu na ni mbali na undani wa mtu, na kutenda yaliyo ya kinyume na Maamrisho yake, sifa, khulka na tabia, au anakisasi na mtu mwingine. Hivyo, mtu huingiwa na khofu ambaye anajiweka mbali na Mungu, au anagombana na watu na kusema: "Mimi ninakuona wewe si kitu na huwezi kuniumiza mimi," au huwaumiza wenzake na kuwagandamiza wengine. Pia watu wanapoishi kwa umoja kwa hali zote, wao huhesabika kuwa wamoja. Hivyo watu wanasema kuwa Deva Datta, Yajna Datta, na Vishnu Mitra wote hawa ni wamoja, i.e. wao ni marafiki.Kutokuwapo na chuki huleta furaha, na kuwepo kwake huleta maumivu.

**Tofauti Ya Mungu Na Roho.**

Q. Jee mwungano au mtengamano wa Mungu na roho ni wa daima. Wao hungana au hawaungani na kuwa wamoja na kitu kimoja?

A. Nusu ya swali hili limejibiwa hapa juu. Hata hivyo, umoja wao au mchanganyiko wao unafanyika kwa sifa zao za namna moja - Sadharmya na uhusiano wa lazima - anvaya bhava; kama vitu vya mwili ni vimoja pamoja na mbingu kutokana na kitu kimoja na kutokana na kutokuwa wao mbali mbali. Lakini wao ni tofauti kutokana na jambo la kweli, kuwa mbingu iko kote, hafifu, haina umbo, haina mwisho na ina sifa myinginezo zilizo za ajabu; maumbo ya vitu ni mbali, yanaonekana na yanayo sifa nyinginezo zilizotafauti. Dunia, na vitu vyenginevyo haviwezi kuwa mbali na mbigu kwa sababu ya uhusiano wao maalum; i.e., kuwepo kwao unategemeana, lakini pia hivyo ni mbali mbali kwa mujibu wa tofauti katika tabia zao. Kwa njia hii hii, roho, dunia, na vitu vyenginevyo vyenye umbo haviwezi kuwapo zaidi ya Mwenyezi Mungu kutokana na kuwepo kwake kote; lakini wao hawako sawa kwa umbo na tabia. Kwa kuutazama mfano wa kila siku. Udongo, mbao, chuma na vitu vyengine vya jengo vilikuwapo mbinguni kwenye pahali tafauti kabla ya kujengwa nyumba. Inapo jengwa, hivyo bado vinakuwapo mbinguni; na vinapovunjwa na kuangushwa chini ie., pale ambapo vitu vyake vyote vimeshakwenda kwenye asili zao, bado huwa vipo katika mbingu. Kwa maneno mengine, haviwezi kuwa mbali na mbingu saa zote. Kwa kuwa na umbo tafauti na tabia kutokana na mbingu, katu haikuwa namna moja nayo wala haiko hivyo sasa, wala haitakuwa hivyo kamwe.

Kwa njia hii hii roho na dunia nzima na vitu vyake visivyo na hesabu ijapokuwa vimeenewa na Muwezà, viko dhahiri katika nyakati zote kutokana kwa Mwenyezi Mungu; na kwa kuwa tafauti na Yeye kwa umbo na tabia, wao katu hawako namna moja na Yeye. Siku hizi uwerevu wa wafuasi wa Vedanta unapoongozwa vibaya kama ule wa mtu mwenye miwani ya jicho moja kama wao hawajali sifa zinazotafautisha - vyatirekabhava na kutilia mkazo yale ya namna moja - anvaya au tabia za namna moja. Hapa kitu ambacho hakina sifa za kweli (saguna) na za uwongo (nirguna), muhimu au sifa za asili (anvaya), vinavyo tafautisha tabia (vyatireka), kama hiyo (sadharmya) na si sawa na (vaidharmya) uadilifu, na sifa za kutafautisha (visheshana bhava.)

**Jambo Lisiloelekea**

Q. Vipi ala moja itakuwa na panga mbili? Vipi sifa nzuri na mbaya, sifa na si sifa, kuwa ni moja na kuwa kitu kimoja?

A. Tazama hapa, sifa za kitu ni umbo, kuonekana na mengineyo; sifa za binadamu ni elimu na mengineyo kama haya, ambayo hayamo katika vitu. Kwa njia hii hii, akili ina sifa za kutaka, nia na kama haya. na haina mambo yale, kwa majina ni, umbo na kama haya. Nazo zinaelezwa zaidi! Saguna ni nani mwenye sifa na nirguna nani asiye na sifa. Wanazo sifa zao za asili na kuwa hawana sifa zilizo kinyume na wao, vitu vyote inasemekana vina tabia zao na havina tabia pia. Kitu kinaweza kutolewa na sifa tu, lakini daima kinajulikana kwa wingi wa tabia zake kutokana na kinyume na sifa zake. Kwa njia hii hii, Mungu inasemekana kuwa ni saguna au anazo sifa kwa kuwa Yeye anayo elimu isiyo na kikomo, nguvu, na sifa nyinginezo kama hizo. Yeye pia ni nirguna au bila sifa kwa kuwa Yeye kuwa mbali na vitu kama kwamba Yeye hana umbo na mengineyo, na kutokana na sifa za binadamu, kama, chuki na mengineyo kama haya.

Q. Watu huwaita wale wasiona umbo kuwa hawana tabia na kuwa na umbo huwa na tabia i.e. Mungu anapokuwa hana nyama Yeye huwa hana tabia; lakini Yeye anaumbo jengine, Yeye inasemekana kuwa ana tabia,

A. Ni dhana ya mjinga, mtu asiye na elimu tu. Wale ambawo hawana namna ya elimu yo yote, hupayuka payuka kama wanyama, kama wagonjwa wazimu wanaposema, kwa hivyo yale yanayosemwa na wajinga huwa hayana maana.

**Mungu ana Ngoa Au hana.**

Q. Mungu ana ngoa au Yeye hana?

A. Yeye hana, Kwa sababu, mtu huwa ana ngoa kwa kutaka kupata kitu bora zaidi nje yake. Lakini Mungu hana kitu nje Yake yeye wala hapana kitu ambacho ni bora kuliko Yeye. Kwa hivyo, yeye hawezi kuwa na ngoa. Virakta au mtu anayejitolea ni yule ambaye huyawacha yale aliyokuwa nayo. Mungu kuwa yupo kote, hawezi kukiwacha kitu. Kwa hivyo Yeye si mtawa.

Q. Mungu anayo matamanio?

A. La, si kama mtu. Kwa sababu mtu huwa na matamanio ya kitu ambacho hana au kitu bora zaidi, na kukipata kitu hicho humletea furaha maalum. Sasa, Mungu hana matamanio yo yote, kwa sababu hapana kitu ambacho Yeye hawezi kukimiliki au kukipata, na ambacho ni bora kuliko Yeye. Pia, kwa kuwa ana furaha ya kutosha, Yeye hana matamanio ya kitu cho chote. Hivyo, hakuna uweza wa matamanio katika Mungu. Lakini yeye ana ikshana: ujuzi wa ndani wa namna zote za elimu - darshana ambayo ni uwezo na nguvu za kila kilichoumbwa. Mengi kuhusu elimu ya Mungu ijapokuwa ni kwa ufupi, hata hivyo watu wazuri wanaweza kuyashika kwa urefu wao wenyewe.

**Ya Veda.**

Q. Mungu ni nini kuwa ni nani ameiteremsha Rig Veda, Yajur Veda, Sama Veda, na Atharua Veda? Ath. K. 10 Pr. 23, An 4. M 20.

A. Yeye ambaye amefanya yote, anasaidia vyote, huyo ni Mungu, Mwenyezi Mungu.

Yaj. XL. 80. Bwana Mungu anajitosheleza mwenyewe, mtakatifu, wa milele, na si mwenye mwili, anawafundisha watoto wake wa milele, roho za binadamu, mipango yote ya elimu kutokana na Vedas kwa intidhamu katika mwangaza wa kweli wa hali zao njema.

Q. Wewe unaamini kuwa Mungu ana mwili au hana mwili?

A. Hana mwili au bila ya kitu.

Q. Ikiwa Yeye hana mwili, vipi yeye angeweza kusomesha elimu ya Vedas, na vipi matamshi ya herufi iliwezekana bila ya kuwa na mdomo? Kwa sababu, matamshi ya herufi lazima huhitaji ulimi na viungo vya mdomo, na juhudi ya ulimi.

**Taratibu ya udhihirisho.**

A. Ilivyokuwa Mungu Mkubwa ni mwenye nguvu zote na ameenea kote, Yeye hana haja ya kuwa na mdomo na viungu vya kusemea ili kuisomesha elimu ya Vedic; kwa sababu herufi zinatamkwa kwa mdomo na ulimi ili kuwapasha habari watu wengine kutoka kwa msemaji, lakini si kujiambia mwenyewe. Kuna mambo mengi hufanyika akilini bila ya matamshi ya maneno. Yafunge mashikio kwa vidole na tena sikiliza namna ngapi ya sauti zinafanyika hapo bila ya kutumia ulimi na mdomo. Kwa njia hii hii, Mungu amedhihirisha elimu kwa roho kwa uadilivu wake yeye kuwa wa roho yenye utawala wote. Umuhimu wa matamshi ni kuzieleza fikra zako kwa wengine. Ilivyokuwa Mungu hana mwili, ameenea kote, Yeye anadhihirisha Elimu Yake ya Vedic kwa roho kwa uadilifu Wake kwa kuwa dhahiri katika undani wao.

Mtu aliyeangazwa na udhihirisho, huitoa elimu yake kuwa wenzake kwa matamshi ya mdomo. Kwa hivyo kutokuwa na mdomo wa kuhutubia hauwezi

kusimama katika jambo hili la Mungu.

**Wakati Na Mwenye Kupokea Mdhihirisho wa Vedic**

Q. Kwenye akili ya nani na wakati gani Mungu alidhihirisha Vedas?

A. Mwanzoni alipoanza kuumba Mungu aliidhihirisha Veda kwa roho ya kila mmoja wa wataalamu wanne, wanaoitwa Agni, Vayu, Aditya, na Angira. (Shat 11, 4, 2, 3,.)

Q. Ni ubeti kutoka kwenye Shwetashwatar Upanishat VI. 18. Kwa mujibu wake, Mungu alidhahirisha Vedas kwenye akili ya Brahma. Tena kwa nini inasemwa kuwa ilidhihirishwa kwenye roho za wataalamu, Agni & C.?

A. Mungu aliifanya iwafikie kutoka kwa Agni na wengineo kufikia kwenye akili ya Brahma. Tazama Manu anasema nini, 1. 23.

Mwanzoni Mwa Mungu Mkuu, baada ya kuwatengeneza watu, alimbariki Brahma na Vedas nne kutokana na wataalamu wanne, wanaoitwa Agni na wenginewo. Brahma alipokea Rig, Yajur, Sama, na Atharva Vedas kutoka kwa Agni, Vayu, Aditya na Angira.

Q. Kama Mungu aliidhihirisha Vedas kwa wataalamu hawa wanne tu,na si kwa wengine, Yeye inahakikisha kuwa yeye anapendelea upande mmoja.

A. Wataalamu hawo wanne walikuwa takatifu kuliko roho zote. Wengine hawakuwa kama hawa. Hivyo, elimu takatifu iliangazwa humo mwao.

**Kwa nini Vedas ziko katika Sanskrit.**

Q. Kwa nini Mungu aliidhihirisha Vedas katika lugha ya Sanskrit na si katika lugha nyinginezo za nchi?

A. Ange thihirisha Yeye katika lugha nyingi, Yeye angekuwa mpedeleaji wa upande mmoja au zaidi. Kwa sababu, watu wa nchi ambazo Vedas ilidhihirishwa, wao watapata fursa za kusoma na kuzisomesha, lakini watu wengine wataona ni vigumu sana. Hivyo, udhahirisho ulifanywa kwa lugha ya Sanskrit, ambayo si ulimi wa nchi yo yote,. Lugha ya elimu ya Mungu lazima iwe namna moja na sare kwa wote, kama vitu ya kawaida, kama ardhi na mengineye ni ya namna moja katika nchi zote na wakaazi wa hapo pia ni sababu ya sanaa na ujenzi, ili watu wa nchi zote wawe na kazi sawa sawa za kuisoma na kuisomesha Vedas, ambayo inahakikisha kuwa Mungu hapendelei ko kote. Pia ni asili ya ndimi nyinginezo.

Q. Kuna uhakikisho gani kusema kama Vedas zimefanywa na Mungu, na si na wengine?

**Uhakikisho Wa Uthihirisho Wa Vedic.**

A. (1) Kuwa kitabu kimetengenezwa na Mungu na si na wengine, ambapo maadishi yake yako kamili pamoja na sifa, tabia na asili ya Bwana, ambaye ni mtakatifu, mjuzi wa yote, mwenye haki, mwenye huruma, na mwenye sifa

takatifu, tabia na asili.

(2) Kuwa kitabu kimeongozwa na Mungu na hakina mambo yaliyo kinyume na tabia, ushahidi wa hisia, na kanuni halisi za sheria, na vilivyoelezwa na mawalii na wataalamu.

(3) Kuwa kitabu kimeongozwa na Mungu ambacho kinaeleza mpango wa elimu bila ya makosa na madanganyo kama ilivyo sheria ya elimu ya Mungu.

(4) Kitabu kimeandikwa chini ya uongozi wa Mungu Mkuu, ambacho kinamweleza Mungu, dunia, sababu; athari, na nafsi kama Mungu Mkuu alivyo hasa, na mipango mengine ya sili kama yalivyo.

(5) Vedas ndivyo zilivyo kama itakiwavyo kuwa, kuwa ziko sawa na ukweli wa ushahidi wa hisia na kanuni nginginezo za sheria na tabia za watu waliye watakatifu wa kweli. Vitabu vyenginevyo vya dini kama vile Biblia, Korani, na vyengine kama hivi, si vya Mungu. Mambo haya yamezungumzwa kwa urefu katika sura za 13 - 14 za kitabu hiki.

**Umuhimu Wa Mdhihirisho.**

Q. Hakuna umuhimu wa Vedas kuwa vimetokana na Mungu, kwa sababu watu wanaweza kutengeneza vitabu kwa kuendeleza elimu zao pole pole.

A. La, wao hawawezi; kwa sababu ni muhali kupata athari bila ya sababu. Watu wasiostaarabika hawa kuwa wanavyuoni mpaka walipopata waalimu si kwa kufuata tabia tu. Hata sasa hapana mtu anayekuwa mtaalamu bila ya kuongozwa na mwenzake mwingine. Kwa njia hii hii, ikiwa Mungu hakuwaamrishi watu wenye hekima mwanzoni mwa kuumbwa na ingekuwa wao hawajaitoa hiyo elimu yao kwa wenzao; watu wote wangebakia wajinga. Kwa mfano, ikiwa mtoto atalelewa kwenye pahali pa ukiwa au kwenye watu walio wajinga au wanyama, yeye pia atakuwa kama wao atapokuwa mkubwa. Jambo hili limetolewa mfano katika Bhils wasiostaarabika na washenzi wa Bara Hindi. Watu wa Egypt, Greece, Europe, na nchi nyingine zilikuwa wajinga na hazikuwa na elimu, mpaka mwangaza wa elimu ulipokwenda kwao kutoka kwa Aryavarta. Wakaazi wa Amerika walikuwa wajinga na bila elimu kwa muda wa miaka mamia, maelfu na milioni, mpaka Columbus na watu wengine walipokwenda huko, ambapo wao walikuwa wataalamu na wastaarabu·kwa kupata elimu kutoka kwa hawa. Hivyo hivyo, binadamu walipewa elimu na ustaarabu na Mwenyezi Mungu mwanzoni mwa kuumbwa, na wao waliiendeleza elimu kwa kuwapa wanao kuja baada yao bizazi mpaka kizazi chengine.

Yoga 11, 26. Bwana Mungu alikuwa mwalimu wa Agni na mawalii wengine alipoanza kuumba kama sisi watu tu tunakuwa wataalamu na kuelimishwa sasa tunaposomeshwa na waalimu wetu. Mungu hazirai kamwe na awe hana akili kama binadamu anavyozirai katika hali ya kuota ndoto na katika mafuriko ya dunia. Elimu yake ni ya milele, na kwa hivyo lazima iendelezwe kama ni ukweli usio na shaka kuwa elimu au maarifa aliyowapa yasingepatikana kama ingekuwa hapa kuwa na mpaaji.

Q. Vedas zilidhihirishwa katika lugha ya Sanskrit ambayo Agni na mawalii wengine walikuwa hawaijui. Vipi basi tena waliweza kujua maana za Vedas?

**Asili Ya Brahmanas (vitabu)**

A. Mungu aliwafanya wafahamu maana ya Vedas. Hapo mawalii, wajuzi wakuu waliabudu utakatifu wa Mungu katika hali nzito ili wajue maana ya ubeti wa Vedic, Bwana Mungu, aliiangaza maana yake katika akili zao. Pale maana ya Vedas ilipoangazwa katika akili za mawalii wengi na wataalamu wa falsafa, wao waliandika vitabu kuhusu haya na maisha ya wanajimu. Vitabu hivyo vinaitwa Brahmanas, kama ni, maelezo ya (Vedas) pia yaitwa Brahma. Zaidi ya haya, jina la mnajibu daima linatolewa kwa ajili ya ukumbusho wake pamoja na ubeti wa Vedic wenye maana dhahiri, ambawo haukufanywa hapo mbele na haukufundishwa mpako hapo. Hawo wanaowaita wanajiimu kuwa waandishi wa beti za Vedic hawasemi kweli. Wao wanafahamisha wazi maana ya beti za Vedic.

**Tafauti baina ya Vedas na Brahmanas.**

Q. Vitabu vipi vinaitwa Vedas?

A. Mkusanyiko wa Rig, Yajur, Sama, na beti za Atharva na mashairi, lakini si vyenginevyo.

Q. Vipi wewe utayafasiri mashairi na misemo na maandishi mengineyo ya hekima kama haya:- Majina ya Mantras (beti) na Brahmanas Veda.

A. Tazama (1) Neno Veda daima linaandikwa mwanzoni na mwishoni mwa kila sura ya Samhita, ambayo ni mwungano wa maneno kajtika beti za Veda. Lakini haijatolewa mwanzoni wala mwishoni mwa sura ya maandishi ya Brahmana. (2) Katika Nirukta, sura. 5. sec. 3, 4, sisi tunaona.

Ni misemo ya Panini, IV, II, 66. Inaonyesha wazi kuwa Veda ni sehemu ya mashairi na Brahmana ni sehemu ya maelezo. Kwa habari zaidi kuhusu haya, utangulizi wangu wa Maelezo ya Rig na Vedas nyingine ziangaliwe. Humo imehakikishwa kuwa (3) haiwezi kuwa ni mawazo ya Katyayana, kuwa yenye uhasama kwa serekali au watu wenye satwa. Ikiwa itakubaliwa, Veda katu haiwi ni ya kale; kwa sababu Brahmanas wanaweka habari za wanajimu wengi, wenye hekima na wafalme. Na ni dhahiri kuwa habari za mtu daima huandikwa baada ya kuzaliwa kwake, na kitabu chenyewe pia huandikwa baada ya kuzaliwa kwake. (4) Vedas havina historia ya mtu, lakini hasa maneno haya yanaelezwa ambayo yanafahamisha mpango maalum wa elimu. Havina majina ya mtu ye yote au maelezo ya hadithi yo yote ile maalum.

**Maelezo ya Vedas.**

Q. Matawi mangapi au sehemu ngapi zimo katika Vedas?

A. Kuna 1, 127.

Q. Unakusudia nini ukisema "matawi" au sehemu?

A. Maelezo au maelezo wazi wazi yanaitwa "matawi" (shakhas) au sehemu?

Q. Watu walio wataalamu wa dunia huyahesabu sehemu zinazohusu Veda kuwa ni matawi.

A. Ikiwa utafikiri kidogo wewe utauona ukweli. Kwa sababu (1) "matawi" yote au sehemu zinajulikana kwa majina ya Ashwalayana na wenye hekima wengine. Lakini ubeti au sehemu ya mantra inajulikana kwa jina la Mwenyezi Mungu. (2) Vedas nne zinaaminiwa kwa zimefanywa na Mungu na Ashwalayani na "matawi" mengine yanaitwa kwa jina ya wenye hekima wengine ambawo waliyaandika haya. Matawi yote au sehemu ya maelezo kwa mujibu wa mashairi na mantras ya Veda; kwa mfano, tawi la Taitteriya linaeleza maelezo ya "Ishe tworj twaiti" na mengineyo. Lakini, Vedas hasa (sehemu muhimu) haieleze kwa kitabu wala kwa mstari wa kichwa. Kwa hivyo Veda nne ni mizizi ya "mtu wa elimu" uliopandwa na Mungu, na Ashwalayani na maelezo mengine yako mengi, iliyolelewa au kutengenezwa na wenye hekima na wenye falsafa, lakini si na Mungu. Kwa maelezo zaidi kuhusu haya "Utangulizi wa Maelezo ya Vedas, yanaweza kuangaliwa. Kama watu wanayo moyoni hali njema ya watoto wao kutokana na mapenzi ya wazazi na mahaba kwa watoto wao, basi pia Mwenyezi Mungu, kutokana na mapenzi Yake yasiyo na kikomo kwa binadamu, aliwadhihirisha Vedas wao, ili wao wapate kutoka kwenye kiza cha ujinga na waji hadhari wasije waka nasa kwenye utando wa madanganyo, wao wanaweza kulifikia jua la sayansi na elimu ya kiroho na kuishi katika raha kamili na furaha, waendeleze mbele elimu na raha daima.

**Udaima wa Vedas.**

Q. Vedas ni za daima au ni za kupita tu?

A. Vedas ni za daima. Kwa sababu Mungu ilivyokua ni wa milele, sifa Zake ni kuwa ana ujuzi wa yote na mengineyo pia ni ya daima. Sifa, athari na tabia za vitu vya daima pia ni vya milele, na vile vya kupita, hupita.

Q. Kitabu hiki (vitabu vya Vedas) pia ni cha milele?

A. La, kwa sababu kimetengenezwa kwa karatasi na kuandikwa kwa wino. Vipi kita kuwa cha milele au kisoweza kuangamia? Lakini maneno yake, umuhimu wao na uhusiano wao ni wa milele na wa daima.

Q. Inaweza kuwa Mungu aliwapa wenye hekima fikra zenye maarifa mengi na tena wao wakayatengeneza kuwa Vedas.

A. Hapana elimu bila ya kitu cha kujulishwa. I. Ila ujuzi wa Mungu, mtu hana nguvu kufanya gayatri na beti nyinginezo kwa mujibu wa sheria za Gayatri na beti nyinginezo, shadja na mambo, mengineyo kuhusu muziki na kinanda, udatta (kali), anudatta (ya chini) na swarita (sisimua) tamko la sauti; kasoro kwa maandishi ya kuandika kitabu chenye kuenea pote. Hapana shaka kuwa mawalii na wenye kujua falsafa baada ya kuisoma Vedas, waliandika Vyakarana (nahau) Nirukta (elimu ya lugha), Chhanda (kanuni za kutunga mashairi) na makala

mengine ya kueleza namna mbali mbali za elimu. Ikiwa Mungu asingeithihirisha Vedas, hapana mtu ye yote angeweza kufanya kitu. Kwa hivyo, Vedas ni hotuba za Mungu. Watu wote lazima wafuate mafundisho yake Ye yote anapoulizwa yeye anafuata dini ipi, yeye ajibu kuwa dini yake ni Vedic, hii ni kusema, yeye anakubali mafunzo ya Vedas. Kwa ufupi kwaajili ya Mungu na Vedas. Sasa tuna kwenda kwenye maelezo ya muumba.

**Muhtasari.**

Vedas zinatangaza umoja wa Mungu mkubwa. Mungu alikuwapo kabla ya yote. Yeye ni sababu ya ndani kabisa ya dunia, na huwapatia viumbe wote chakula. Yeye amedhahirisha Vedas, anawaongoza waadilifu, anaibariki kazi nzuri, na ni muumba, mlinzi, na mwangamizi wa dunia iliyo dhahiri. Yaj. XL. 1. XIII, 4. Rig. XX, VIII. 1, 5. Yeye yupo kote mwenye huruma na mwenye haki Yeye ni Roho ya ndani, asiye na kiwili wili, Mwenye enzi zote, wa milele na mjuzi wa yote. Yeye anawatakia kheri wote.

Ushahidi wa kuwepo kwa Mungu umeonyeshwa katika mafundisho ya umbo la dunia, na katika elimu na uadilifu. Hofu, akili inavyo hisi inapofanya uovu na inapoona raha inapowafanya wema wengine, ni kutokana na Mungu na kwa hivyo ni uhakikisho dhahiri wa kuwepo kwake Mungu.

Yeye peke yake tu aabudiwe kwa kuimba sifa Zake, kwa kumsalia Yeye, na kwa kumwabudu Yeye. Kumwabudu Yeye wakati mwingine huitwa saguna na nirguna, - kukubali na kupinga. Ni kukubali kuwa saguna, pale wanaoabudu wanakubali au wazisema tena sifa za Mungu; kama, Mungu ni mtakatifu, mwenye haki, na mwenye huruma. Ni kinyume au nirguna, pale yeye anapozipinga sifa nyinginezo za Mungu; kama Mungu hajazaliwa, si wakuonekana na wakuleta kifo. Sababu za kumsifu Mungu ni kuziingiza sana akilini sifa za kuigiza tabia; kwa sababu Mungu ni mwenye huruma, sisi tusimuue mtu mwenye akili na wenginewo.

Sala lazima ziwe kama zilivyotolewa kama katika Yaj. XIX, 9 - Wewe ni Mwangaza, nipe mwangaza kutokana na Rehema Zako! Wewe ni mwenye huruma nifanye mimi niweze kuwashinda adui zangu! Ifanye nia yangu iwe mbali na uovu na ijaze usafi na uadilifu Yaj. XXXIV, 3. Mtu afuate yale anayoyasalia, na ayaombe yale yaliyo ya uadilifi na wema.

Sala huzirahisisha akili na kuzijaza furaha isiyoelezeka. Lazima mazoezi yafanywa kwa mujibu wa sheria za Yoga au tafakara, ambayo inayo daraja nane ambazo zinakupeleka kuiangaza akili, viz, mazoezi ya sheria za adabu, kufuata sheria za dini, sheria za kuvuta puumzi, kuweza kuziiwia hisia, mwili ambawo unaelekezana na akili, kuweza kufuata sheria, kumfikiria Mungu, na usingizi wa furaha.

Wao hawasemi kweli wanaposema kama kuna miungu 33 katika Vedas. Kuna namna 33 za kuwapo, viz 8 Vasus - jua, mwezi, dunia, maji, mwangaza, hewa, na mbingu; 11 rudras - kuvuta pumzi, kutoa puumzi, kuweza kusaga

chakula tumboni, kutafuna, mzunguko wa damu, kupona baada ya ugonjwa, kuoza, njaa, kwenda mbweu, na kupiga miyao: 12 adityas, jamii ya nyota za Zodiac 1. moto wa umeme; 1. kazi za kuleta afya.

Si kweli kuamini kuzaliwa tena kwa Mungu ili kumwua jini na kuwahifadhi mawalii; kwa sababu Mungu anaweza kuzifanya kazi hizi bila ya kuwa na nyama. Ni kinyume cha Vedas kuamini kuwa Krishna alikuwa Mungu. Yeye alikuwa roho adilifu na mwenye nia njema.

Ni imani ya uwongo kuwa Mungu anasamehe dhambi. Ikiwa yeye anafanya hivyo, Haki Yake itapotea. Roho iko huru, hujivunia matunda ya vitendo vyake. Tafauti baina ya Mungu na roho ni ile kuwa Mungu hana mwisho, anaifanya dunia, anaisimamisha haki, roho ina mwisho na imo katika kuendeleza insia, na inafanya vitendo vyema na viovu. Inadhihirisha, hisia, matakwa, busara, kuvuta puumzi, makumbusho, njaa, kiu, & C. vyote hivi havipo katika Mungu. Uhusiano wa Mungu na roho ni kuwa Mungu ameenea katika Roho, Mungu baba na roho ni mtoto wa kiume & C. Baadhi wanasema kuwa Vedas inaamini katika mfananisho wa Mungu na roho. Tattwamsi - wewe Mungu. Elimu hiipo katika maandishi halisi ya dini. Maana yake ni kuwa wewe katika Mungu Muweza. Inasemwa na Shwetketu. Shatapatha inasema. Ya amani 'tishthati'. Mungu anakaa katika akili Wale wanawo dhihirisha utambulisho, zinaondoa sifa za kutafautisha na hushikilia sifa za kawaida. Hii si njia sawa ya kuhakikisha vitu. Hivyo, miti inaota na wanyama wanakua hivyo miti ni wanyama, huu ni upuuzi.

Mungu aliyeitengeneza dunia, ameidhihirisha Vedas, Rig, Yajur, Sama na Atharva, iliiwailimishi binadamu kwa elimu kwaajili yao. Mawalii wale walioonyeshwa mwangaza wa Vedas wanaitwa Agni, Vayu, Ravi na Angira. Manu, 1.23.

Uhakikisho wa Veda unatengenezwa na Mungu dhahiri pamoja na sifa zake, tabia na asili. Wala hau tengani na sheria za mazingira. Elimu yake iko mbali na kitisho. Inamweleza Mungu, dunia, kama zilivyo hasa. Imehakikishwa na mawalii na wataalamu. Ikiwa itasemwa kuwa hakuna lazima ya mdhihirisho kwa sababu mtu anaweza kuendeleza elimu yake ya kawaida; inajibiwa kuwa ingekuwa hivyo, wahuni wa nchi nyingi wangekuwa wastaarabu; lakini haikuwa hivyo, wao walionyeshwa mwangaza wa elimu kutoka India. Hivyo Mungu alileta mdhihirisho wa Vedic mwanzoni mwa mwuumbo.

Inasema falsafa ya Yoga, Mungu ni mwalimu wa zamani wa mwuumba wa tokea zamani. 1. 26.

Si sawa kuwaita Brahmans kuwa ni Vedas, ambayo ni sehemu ya kitu tu; kwa sababu, Brahmanas ni maelezo, vipande vyao vinaanzia na Vedas - Panini, IV. II. 66. Vedas ina fikira na dhana, na si karatasi na wino tu, ni za milele, na kuishi katika akili ya Mungu. Hapana binadamu anaweza kufanya ulinganifu, hati, na matamshi kama zilivyotolewa katika Vedas, iliyo ya hekima kuu.

## SURA VIII

## MUUMBO, UTUNZAJI NA UANGAMIZI.

Rig. 10. 129. 7. Ee mtu, Yeye ni Mwenyezi Mtakatifu, kutoka kwenye mikono yake Yeye dunia hii ya vitu vingi ilitokana, Yeye huiweka na pia kuangamiza, Yeye ambaye ni Bwana wa dunia, na katika Yeye dunia hii huishi, huenda na hufa. Mjue yeye na usiamini kuwa kuna mwumba mwingine wa dunia.

Rig. 10. 129.4. Dunia hii yote ilifunikwa na kiza kabla ya kuumbwa, ilikuwa katika tofani, isiyojulikana, na kama ya mbingu. Ilikuwa haina maana yo yote kabla ya ukubwa wa Mungu, i.e. ililala bila ya kuwa na maana yo yote mbele ya Mungu muweza. Baadaye Munga alitoa gizani na kwenye hali isiyo ya faida ye yote na kuifanya kuwa ionekane na iwe yenye maana kwa uwezo wake Mkuu.

Rig. 10. 129. 1. Ee mtu, mtumikie Mungu, Roho ya Milele, kwa upendo wako, ambaye ni mzuizi wa jua na vitu vingaravyo vyote, yeye ambaye amekamilika na asiye na wa pili wake bwana wa dunia hii. Bwana huyu anayejisaidia mwenyewe alikuwa kabla ya dunia kuumbwa na ameitengeneza dunia yote na sayari nyinginezo kama jua pia zimeumbwa na Yeye.

Yaj. 31. 2. Ee mtu, Yeye ni mfanyaji haya yote yaliyokwisha pita, ya sasa na yatakayo kuja ya mbele ya dunia, ameenea kote, yeye ambaye ni sababu ya kuto kufa, ambaye ni bwana wa roho zote, na yeye yuko dhahiri kwenye dunia na kwenye vitu vyote, na katika akili.

Tait Briguvall An. 1. Yeye ni Brahma au Mwenyezi Mtawala na kazi zake Yeye ndizo zilizoleta sayari hizi zote na vitu vyenginevyo, ambamo viumbe huishi na kufa. Tamani kumjua Yeye.

(Vedant,) I. 1. 3. Mwenyezi Mungu ni wakujulikana, ambaye ni sababu ya mwuumbo, Utunzji, na uangamizi wa dunia.

Q. Dunia hii ilizaliwa na Mungu Mkuu au na mwingine?

A. Imetokana na Mtakatifu, au na sababu yenye akili, lakini vitu vilivyomo humu ni vya asilia (pra kriti).

Q. Kwani Mungu akuyaumba mazingira au Prakriti?

A. La, hayo hayana mwanzo.

**Vitu Vitatu Vya Milele.**

Q. Wewe unakusudia nini ukisema havina mwanzo? Na vitu vingapi havina mwanzo?

A. Mungu, roho, na sababu ya dunia (sababu). Hivi vitatu havina mwanzo.

Q. Nini uhakikisho wake?

A. Brahm Mwenyezi Mungu) na nafsi zote mbili ni (dwa) sawa kwa uadilifu wa

nafsi zao na zinajilinda na sifa nyinginezo (suparna) Zime husiana kama iliyoenea na iliyoenewa. (sayuja). Wana urafiki baina yao (sakhaya) wao ni wa milele na hawana mwanzo. Hivyo (samanam) pia ni mti (Vriksha) ambayo ni sababu hasa matawi yake ni vitendo ya dunia yenye vitu, na imeendelezwa mpaka kufikia uinamizi na mwangamio. Ni kitu cha tatu kisicho na mwanzo. Sifa, tabia na mazingira ya vitu vitatu hivi pia havina mwanzo. Ya viwili hivi, roho na nafsi, ya pili huyaonja matunda ya uwema na uadui, yanayozaliwa na mtu wa dunia (swadwatti) kwa matokeo ya kazi, zinazongara kila pahali ndani na nje. Mungu yuko dhahiri na orho, na tabia (desturi au prakriti) iko dhahiri baina ya Mungu na roho. Lakini vyote vitatu ni vya milele na havina mwanzo. Kwa maneno mengine, Mungu ameamrisha kutokuwa na mwanzo na mtakatifu wa milele kwa watoto, roho, na elimu kutokana na mdhihirisho wa Vedas. Rig. 1. 64. 20, Yaj. 40. 8.

Kutoka Shwetashwatara, IV, 5. ambayo inasema kuwa mazingira (prakriti), roho, (jiva) na Roho Takatifu (paramatma) hazijaumbwa, kuwa, wao hawajazaliwa, wala havina umbo na nyama. Hizi sababu tatu za dunia nzima, ambazo ziko wao wenyewe bila ya sababu nyinginezo. Nafsi isiyo na mwanzo inaathirika kwa sababu zake za kujifurahisha mazingira yasiyo na mwanzo au utawala wa sababu. Lakini Roho Takatifu haiathirki kwa hayo, wala haina faida.

**Ya Asili au Prakriti.**

Sifa za Mungu na roho zimetolewa. Sasa tunakuja kwenye asili au kawaida (prakriti.).

Sankhya I, 61. Prakriti au kawaida ni sehemu ya tatu au mchanganyiko wa sifa tatu, kwa majina. (sattwa) safi (raja) kati kati na (tama) janja ya kuendelea milele, na kuwa katika hali ya ulevi. Ikatengeneza kitu cha akili (budhi) ambaye huleta fikira na mawazo (ahankara). Hii huumba asili tano (panch tanmatras) zinaelekeza namna tano ya vitu, hisia kumi, na nia au nguvu za fikra. Asili tano huzaa vitu vitano. Hizi zote huifanya nambari ya arki kuwa 24. Ya 25 ni mtu au akili (purusha), utu au takatifu. Ya arki hizi prakriti au kitu katika hali yake halisi haiozi, na akili au kitu kilicho juu kabisa hisia au maisha na asili tano au vitu vitano ni mazao ya prakriti au ugeuzi wa kitu na sababu ya hisia, nia (mana) na vitu kwa jumla. Mtu au akili si tabia, vitu, wa si mazao ya kitu cho chote.

Q. Mafumbo ya pia ni ya Upanishats. Kwa hakika ulimwengu huu wote ni Brahma. Vitu mbali mbali na yeye si cho chote. Wote wao ni maumbile ya Brahman.

A. Kwa nini wewe unafasiri vibaya vipande hivi? Kwa sababu Upanishats hiyo hiyo ina:

O Shwetaketu, maji yaliyotukuzwa kuwa ni sababu halisi ya kutoka kwa dunia ya furaha, matokeo yake kutokana na joto; na joto kuwa matokeo kutoka

sat; halisi, kuwa ni sababu, ambayo ni ya milele, na au, ya jina prakriti au kitu cha kwanza, mzizi na nguzo ya dunia yote.

Dunia hii yote inayoonekana ilikuwa kama kitu kisicho cha kweli kabla ya mwumbo, na ilikuwapo katika umbo lisiloonekana pamoja na nafsi katika Brahman na Prakriti si kama haikuwapo. Kwa mujibu wa maneno "sarvam" khalu hata yote, inaonyesha dalili ya asili ya jumbo. Mfanya kiini macho anajenga nyumba kwa kuchukua tufali kutoka hapa na changarawe kutoka pale. Kwa sababu imetolewa katika.

*Maneno fulani ya Katha Upanishat. Neno au fungu la maneno ni muhimu* yanapowekwa mahali pao katika sentensi au masimulizi; lakini huwa ya upuzi yanapowe kwa mbali mbali na kuwekwa kwa ulinganifu na mengine; kama vile viungo vya mwili huwa vyenye maana vinapokuwa pamoja, lakini huwa havina maana vinapogawanyika kutoka kwenye mwili. Nisikilize mimi. Maana yake ni; Ee roho, mfikiri Mungu, ambaye ni sababu ya mwumbo, mtunzaji na mwangamizi wa dunia; ambayo ipo katika uwema wa maumbile yake na mtunzo na nguvu za kutunza, na zipo na Yeye. Usimsifu mtu ila Yeye. Hakuna mchanganyiko wa vitu mbali mbali katika Yeye, ambaye yuko na habadiliki na haonekani na mwerevu kabisa. Lakini namna mbali mbali ya asili ya kuonekana kwa nguvu za Roho Takatifu.

**Asili za dunia**

Q. Kuna asili ngapi za dunia?

A. Tatu, kwa majina 1, Nimitta: yeye asili ya ustadi 2. Upadana: yeye asili ya kitu, 3. Sadharana: ya asili ya kutendea kazi.

1. Asili yenye ustadi ni ile ambayo inafanya kitu na bila ya ustadi hakifanyiki cho chote; wenyewe haijafanywa, lakini inafanya nyingine yenye umbo tafauti na yenyewe. 2. Yenye asili ya kitu ni kuwa bila ya hicho kitu hapana cho chote kinachoweza kufanywa, ambacho kinageuzwa kuwa na umbo tafauti na ambacho kinaoza. 3. Asili ya kutendea kazi ni ile ambayo ni msaada kwa kufanya kitu na ni njia ya wote. Sababu muhimu na kubwa ni Mwenyezi Mungu ambaye anaifanya dunia yote kutokana na kitu, kuilinda, na kuiangamiza, paa, na kuwaweka wote katika sheria zao. 2. Roho ni ya asili ya kawaida, ambayo inaleta matokeo tafauti kutokana na vitu vya kawaida katika dunia. Asili ya kitu ni prakriti: kitu cha kwanza au chembe ndogo kabisa, inayoitwa kitu cha kujengea dunia zote. Kuwa kama kifu au si kifu, hakiwezi kujitengeneza kuwa cho chote, wala kujiozesha wenyewe. Lakini kinasimamia kwa haja ya kingine kwaajili ya kujitengeneza au kujiozesha wenyewe. Wakati mwingine kitu kimoja kifu na tepetevu, hugeuka na kuangamiza chengine. Kwa mfano, mbegu ambazo zimetengenezwa na Mungu, zinatoa mizizi zinapofikiwa katika ardhi na kunyunyuziwa maji, na kua miti mikubwa. Lakini inapokaribiwa na moto na vitu vyengine vinavyoangamiza, miti hiyo huangama. Hata hivyo intidhamu ya kukua kwao, kugeuka na kuangamia imo mikononi mwa Mungu na binadamu: Kitu kinapotengenzwa, asili zake ni elimu, sanaa, nguvu, mikono na asili nyinginezo za namna mbali mbali; majira na saa ni asili zake za kawaida.

Kwa mfano, mfinyanzi anapofinyanga chungu, yeye ni sababu wa ufinyanzi huo, udongo ni kitu cha asili yake; gurudumu, mkono, na zana nyinginezo ni asili ya kawaida zake; majira, wakati, anga mwangaza, macho, mkono, ujuzi, kitendo, na mengineyo ni asili ya kitu na ya kuendea cho chote hakiwezi kufanyika au kuangamizika bila ya asili hizi tatu:- asili ya ustadi, kitu na kazi ya kutendea.

**Kusadiki kuwa Ulimwengu Wote ni Mungu.**

Q. Vedantins wa kisasa au wafuasi wa falsafa ya Vedant wanamhesabu Mtawala Mkuu kuwa ni asili ya pekee, ambamo asili ya, kutendea na asili ya ustadi kuwa zime ungana-abhinna nimitta upadana karana-asili isiyogawanyika kutokana na kazi ya kutendea na asili ya kitu. Kwa mfano, Mundaka Upanishat inasema; I. I. 7.

**Buibui hutengeneza utando wake mwenyewe kwa nyuzi zilizotoka mwilini mwake mwenyewe na hachukui kitu cho chote kutoka nje.** Hapo tena yeye huishi na kucheza cheza humo. Kama njia hii hii, Brahman (Mwenyezi Mungu) ameitengeneza dunia kutokana naye mwenyewe na kujigeuza Yeye Mwenyewe kuwa katika umbo la dunia hucheza na Mwenyewe. Ni nia ya Mungu Na tumainio ya kuwa wengi japokuwa ni mmoja ya haya ni kuwa, umbo la dunia. Yeye amekuwa ulimwengu, kwa nguvu za fikira zake tu. Kwa sababu, maelezo juu ya Mandookyopanishat yanasema.

Gourhpad, 31. Kile ambacho hakina mwanzo wala mwisho, pia hakina katikati wala wakati huu wa sasa. Dunia haikuwapo katika mwanzo wa mwuumbo; lakini Mungu peke yake alikuwapo. Hapatakuwa na dunia hapo mwishoni au uangamizi wa mwisho utapofika wa dunia. Kwa nini basi, Mwenyezi Mungu si dunia nzima?

**Tafauti baina Ya Mungu na Kitu.**

A. Ikiwa Brahman ni asili ya kitu cha dunia kama wewe unavyo kubali, yeye ataweza kugeuzika na kuweza kuoza; kwa sababu sifa, tabia, na asili ya kitu huendelea na sababu zake, ambazo huoza.

Vaisheshik, I. I. 24. Ni mithali ya falsafa ya Vaisheshik. Maana yake ni: matokeo yana sifa kama zile za asili ya kitu. Sasa, 1. Mungu Muweza ni wa kweli, mwenye akili, mwenye furaha, dunia kuwa ni sababu ya asili ya kitu, si ya kweli, haina uhai au ni mfu na haina furaha. Yeye hajazaliwa, lakini imeubwa. Yeye haonekani, lakini inaonekana. Yeye hajagawanyika, lakini imegawanyika. 2. Ikiwa dunia imezaliwa na Mwenyezi Mungu, basi sifa za vitu vilivyo humo pia vitapatikana katika Yeye. Kwa maneno mengine, Yeye atakuwa kitu kama dunia. 3. Pia dunia, i.e. ulimwengu na maumbo ya peponi lazima yawe yenye akili kama Yeye. Mfano wa buibui hausaidii mithali yako, bali inaikanusha. Asili ya kitu kama cha nyuzi za mtando ni kitu cha mwili wa buibui, na roho inayoishi ya buibui ni kitu chenye athari ya utando. Ni dhahiri katika za ajabu za Mungu; kwa sababu, roho haiwezi kuzalisha nyuzi kutoka kwenye mwili wo wote lakini ila ule wa buibui. Kwa hali hii hii, Mungu aliyeenea kote (Brahm) ameitengeneza umbo

la dunia au prakriti (kitu cha kwanza) na tofani zilizomo katika yeye katika umbo lisiloonekana na kutoa mwili na kuweza kuonekana juu yake. Yeye ameenea humo, na anafuraha kuwepo kama shahidi wa dunia. Kuhusu kuamini kuwa Bwana ameona, amefikiri na kutaka kuwa Yeye lazima aitengeneze dunia na atukuzwe, maana yake ni kuwa dunia inapotengenezwa, Mungu atukuzwe kama roho inavyofikiri; jua, amuni, kuhutubu na kusikiliza, yale yanayodhihishwa Mwenyezi Mungu, ambaye amejiweka katika maumbo makubwa, lakini dunia takapo angamia, hapana atakaye mjua Yeye ila Mungu mwenyewe na wale waliojipatia uokovu. Kwa maelezo ya Upanishat, ni ya uwongo na ya kubabaisha. Kwa sababu dunia haikuwa ikionekana na kujulikana na itaendelea kutoonekana na kutojulikana kutoka mwanzo wa uangamizi mpaka wakati wa kuumbwa tena. Kwa sababu inasemwa katika Rig. Veda, 10, 129, 3. Pia, Manu inasema, 1, 5.

Maana yake ni: dunia hi yote ilifunikwa na kufichwa kwa kiza wakati wa uangamizi na kabla ya muumbo. Ilikuwa hivyo wakati wa mwanzo wa uangamizi. Wakati ule ilikuwa haijulikani, kwa sababu hapana aliyefikiri cho chote juu yake na haikuwa akiijua kwa akili kutokana na tabia zake. Haitaweza kujulikana wakati wa hali hiyo. Daima inajulikana kama ilivyo sasa, ambapo tabia zake zinajulikana kwa akili, na zinafaa kutumika. Tena, mwandishi anaandika, kuwa dunia haipo hivi sasa, haya hayana maana; kwa sababu, yale yanayojulikana na kufahamika kwa sababu ya ujuzi na uhakikisho thabiti haiwezi kuwa ila yale yaliyo ya kweli.

**Nia ya Muumbo.**

Q. Nini nia ya Mungu ya kuiumba dunia?

A. Nini itakuwa nia yake kama hakuiumba?

Q. Ingekuwa Yeye hakuitengeneza yeye angekuwa na furaha na roho zisingeweza kuona raha na maumivu.

A. Ni maneno ya wavivu na masikini au watu wenye shida, lakini si ya mashujaa na majasiri. Raha gani au maumivu yanasikika na roho wakati wa uangamizi? Ikiwa raha na maumivu ya wakati wa muumbo yanaendelea, kufikiriwa na kulinganishwa, basi raha inaishinda maumivu zaidi kwa mara nyingi. Roho nyingi zilizo safi na zienye uadilifu zinapata raha za uokovu kwa kuitengeneza mipango ya kuwa mbali na raha za dunia.

Wao hukaa bure wakati wa mchafuko kama wanavyo lala wanapokuwa katika usingizi usiokuwa na ndoto. 2. Vipi Mungu angeweza kabla ya uangamizi kuziipa roho zawadi au adhabu kuwa ni matunda ya uwema na vitendo viovu vilivyofanyika wakati wa muumbo? 3. Vipi roho zingeweza kufurahia matunda hayo? 4. Ikiwa wewe utaulizwa sababu gani zipo kwa kuwepo kwa macho shaka bila shaka wewe utajibu kuwa nuru inapatikana kwa kuwepo kwa macho. Kuna faida gani kwa Mungu kuwa na elimu, nguvu na vitendo vya kuitengeneza dunia? Kwa swali hili huwezi kutoa jawabu nyengine ila ile sifa hizi Zake zipo ili

kutengeneza dunia. Pia, 5. Mungu ana haki, huruma na sifa nyinginezo, hapo tu itazaa matunda hapo Yeye anapoitengeneza dunia. 6. Nguvu Zake zisizo na mwisho inaanza kutumika kwa kadiri Yeye anapotengeneza, kusaidia, kuangamiza na kuirekibisha dunia. Kuchukulia mfano. Sifa muhimu ya jicho ni kuona. Hivi hivi sifa muhimu ya Mungu ni ukarimu, kwa sababu Yeye daima anatupa au anatoa, rehema na baraka zisizoweza kuhesabika kwa roho kwa kuiumba dunia.

Q. Kipi ni cha mwanzo au kilikuwapo kwanza, mbegu au mti?

A. Mbegu; kwa sababu mbegu, asili, asili ya kwanza, asili ya nguvu, asili ya kawaida, na maneno kama haya yenye maana moja, Aassi inaitwa mbegu yafuatayo kuwa ni mwisho.

**Uwezo Mkuu Wa Mungu.**

Q. Ilivyokuwa Mungu ana uwezo mkuu, Yeye anaweza kutengeneza asili na nafsi. Ikiwa Yeye hawezi basi, Yeye hawezi kuwa mwenye uwezo Mkuu.

A. Maana ya Uwezo Mkuu imetolewa hapa juu. Lakini ni mwenye Uwezo Mkuu na anaweza kufanya yali yasiyoweza kufanyika? Ikiwa Yeye anaweza kufanya yasiyoweza kufanyika, kwa mfano, kutengeneza matokeo ya asili, basi Yeye bila ya sababu anaweza kumtengeneza Mungu mwingine, Yeye afe, awe si kitu, aadhibike kwa maumivu Yeye mwenyewe, asifanye haki, asiwe mtakatifu, ageuke kuwa mwovu na mengineyo! Mungu hawezi kugeuza sheria za asili kama moto una moto, maji ni baridi, ardhi ni mfu, na kama haya. Sheria za Mungu ni za kweli, hazipunguki na zimekamilika. Hivyo Yeye hazidalishi. Kwa hivyo, neno uwezo mkuu linamweleza Mungu tu ambaye anaweza kufanya kazi Zake zote bila ya msaada wa mwingine ye yote.

**Mwili Wa Mungu.**

Q. Mungu ana mwili? Ikiwa Yeye hana mwili, Yeye hawezi kuitengeneza dunia bila ya mikono, miguu na vyenginevyo. Lakini ikiwa Yeye anawo mwili basi hapatakuwapo na pingamizi.

A. Mungu hana mwili wa kitu cho chote. Yeye mwenye mwili si Mungu kamwe. Kwa sababu, kuwa na mwili, Yeye lazima hataweza kuwa na nguvu zote, mbali mbali na akiwa na mpaka wa vitu, bila ya wakati na mahali pa kutosha. Yeye atashikwa na njaa, kiu, ataoza, mbadiliko, joto, baridi, homa na maradhi mengineyo. Hizi ni sifa za mtu na ziko mbali na sifa za Mungu. Wewe unajua vilivyo kuwa wewe na sisi tuna miili na hatuwezi kuizuia kuoza chembe ndogo ndogo kabisa zilizojiweka pamoja na vitu vyenginevyo. Kwa njia hii hii, Mungu kuwa na mwili wa kitu asingeweza kuutengeneza umbo la dunia kwa vitu visivyoonekana na vitu vinavyoonekana. Ijapokuwa Mungu hana viungo vya mwili vya kuhisia kama mikono, miguu na vyenginevyo; hata hivyo nguvu Zake, uwezo, na utakatifu wake ni wa milele. Yeye anaitumia haya katika kazi zake, ambazo haziwezi kufanywa na roho na asili. Ilivyokuwa Yeye ni mpole zaidi

kuliko tabia au kitu na roho, Yeye amevienea vyote hivi, na hivyo anaweza kiviunda kuwa na umbo la dunia yenye vitu.

Q. Kwani wewe hujui kuwa watu wanayo miili, kwa sababu wazazi wao walikuwa na miili? Ingekuwa wao walikuwa hawana miili basi watoto wao pia wangekuwa hivyo pia. Kwa hivyo hivyo, ikiwa Mungu hana mwili, basi dunia iliyo umbwa na Yeye pia haitakuwa na mwili.

A. Suali hili lako ni la kitoto. Kwa hivyo, mimi nimesema sasa hivi kuwa Mungu si mwenye asili ya kitu cha dunia; lakini Yeye ni wa asili ya matokeo, ambayo haina umbo lo lote; lakini wao ni wengi zaidi na ni mstadi zaidi kuliko vitu vyenginevyo.

**Hakuna kitu bila Ya Sababu.**

Q. Mungu hawezi kufanya kitu bila ya sababu?

A. La; kwa sababu haiwezekani kukileta kitu ambacho hakina maana. Ni kama mazungumzo ya mtu ambaye anasema kuwa yeye ameona harusi ya mtoto wa kiume na wa kike wa mwanamke tasa. Wao walikuwa na mkuki wa pembe za mtu, na wote walivaa mashada ya maua ambayo yalichanua mbinguni. Wao walikoga kwenye mto wa madanganyo ya macho, waliishi katika mji wa madanganyo. Huko wao wana mvua bila ya kuwa na mawingu, mavuno ya nafaka bila ya kuliima ardhi, na vitu vyengine visivyoweza kufanyika. Hivyo hapana matokeo bila ya kuwa na asili. Kwa mfano mtu anasema, Mimi nilikuwa sina wazee, sikuzaliwa na ye yote. Mimi sina ulimi mdomoni lakini, ninasema. Ilikuwa hapana nyoka katika shimolakini alitoka kutoka humo. Mimi sikuwapo po pote, wala wao hawakuwapo po pote; lakini sisi tumekuja hapa. Maneno kama haya yanawaelekea walevi au wenda wazimu tu.

**Sababu au Monad haina Sababu**

Q. Ikiwa haiwezi kuwapo kwa kitu bila ya sababu, nini sababu ya sababu?

A. Nini ni sababu au mifano tu; isiyokuwa matokeo ya mengine. Ikiwa kitu ni sababu ya nyingine na matokeo ya kitu kilichofuata, haiitwa sababu safi au mrahisisho au monad. Hivyo, kwa mfano, ardhi ni sababu ya nyumba na vitu vyenginevyo. Pia ni matokeo au mazao ya maji na vitu vyenginevyo. Lakini asili sababu ya mwanzo, haina mwanzo. Inasema falsafa ya Sankhya I. 67.

Hapana mzizi wa mizizi, hapana sababu ya sababu. Hivyo sababu ya vitu vyote yenyewe haina sababu. Hivyo, kuna sababu tatu za lazima mwanzoni mwa matokeo yo yote au kitu. Kwa mfano, kutengeneza kitambaa inahitaji nyuzi za pamba, mashine ya kufumia nguo na vitu vyenginevyo vya kufumia. Kwa njia hii hii, muumbo wa dunia ina sababu zake za kuwapo kwake Mwenyezi Mungu, kitu cha kwanza kabisa, wakati, anga na roho, haya ni kuwa, hivi havina mwanzo na vilikuwapo kabla ya muumbo, Ikiwa kimoja katika hivi kitaitaka dunia katu havitakuwapo.

**Pingamizi za Kutokuwapo Kwa Mungu Zinajibiwa.**

Q.1. Wasioamini kuwa Mungu yuko wanasema kuwa hapa kitu cho chote kile ambacho ni kitu kilikuwapo kabla ya muumbo. Kitakuwapo wakati wa mwisho wa dunia. Kwa sababu kuwepo ambayo ipo sasa, ita punguzwa na kuwa kutokuwepo, i.e. itakuja kuwa si kitu.

A. Anga, mbingu, isiyoonekana, na sifuri au sifuri, pia zinaitwa kuwa si kitu. Ni kitu kisichokuwa na uhai. Vitu vyote havionekani, kama kuwa ni mstari wa ncha moja. Mistari ya chembe ndogo kabisa kupindwa kufanywa umbo la duara kwa nakshi ya Bwana, kwenda kutengeneza ardhi, milima, na maumbo mengineyo. Asiyefahamu kitu si kitu chenyewe hasa.

**Wakiristo na Waisilamu.**

Q.2. Kutokuwapo huzaa kuwapo; kama kuangamizwa kwa mbegu huzaa mche. Ikiwa mbegu itakatwa, huoni ishara ya mchee humo ndani. Ilivyokuwa mche haukuwapo katika mbegu, ni dhahiri kuwa inazaliwa kutoka cho chote.

A. Nguvu ambayo inaangamiza mbegu, ilikuwapo humo ndani. Ingekuwa haipo, vipi ingeweza kuoza? Isingeweza kuwa mche.

Q.3. Mtu haathirki na matokeo ya vitendo vyake, kwa sababu vitendo vingi vinaonekana kama havizai matunda. Hivyo inaonekana kuwa hiyo imo katika nguvu za Mungu kuwa mtu apate msuko suko wa vitendo vyake mwenyewe. Mungu huvifanya vitendo vi zae matunda ambawo Yeye anayapenda, na kuwa Yeye. hayapendi, basi havizae matunda. Hivyo, ni dhahiri kuwa matundo ya vitendo yamo katika mikono ya Mungu.

A. Ikiwa natija za vitendo vyote viko katika mkono wa Mungu, kwa nini Yeye haziwafikii watu bila ya kufanya kitendo? Kwa hivyo, Mungu anawapeleka natija za vitendo kwa mujibu umwafaka wao Yeye hawezi kumjazi au kumwadhibisha mtu ambaye hajakifanya kitendo. Lakini kwa mujibu wa sheria ya Mungu, mtu huvuna kile alicho panda.

**Asadikiye**

Q.4. Vitu vinazaliwa bila ya sababu muhimu; kuwa, miiba ya mchogoma ni mikali na yenye ncha, lakini mili mingine haina miiba. Hata hivyo, inaelewekana kuwa muumbo unapofanyika, miili, na vitu vyengine vinazaliwa bila ya sababu muhimu.

A. Sababu muhimu ni kuwa ile inamozaliwa. Kwa nini mchongoma hauzaliwi bila ya mti usiona miiba?

**Wafuasi wa Vedanta**

Q.5. Vitu vyote lazima vizaliwe na viangamie, hivyo vyote ni vya muda na si vya daima. Huu ni ubeti kutoka katika kitabu kadha. Maana yake ni kuwa kwa mujibu wa wafuasi wapya wa Veda ambawo wamewekwa kuwa ni wa namna yatano ya wasiokumbali Mungu, Hesabu na maandishi ya vitabu bilioni ni ile

Brahm au Mwenyezi Mungu ni ukweli wa pekee au kuwepo kwa hakika; na dunia iliyobaki ni ya madanganyo tu. Nafsi haiko tafauti na Brahm.

A. Ikiwa uimarisho wa yote uko thabiti, yote hayawezi kuwa ya muda mfupi.

Q. Ikiwa uimarisho wa yote pia ni wa muda mfupi, kama moto unapozimwa baada ya kuziangamiza kuni.

A. Hiwezi kusemwa kuwa kile kinachoweza kuonekana sawa sawa, ni cha uwongo, na kuwa sababu muhimu isiyoonekana ni kuwa si ya daima. Skuli ya kisasa ya Veda inaamini muumbo wa dunia kutokana na Mwenyezi Mungu (Brahman.). Haya, Mwenyezi Mungu au Brahman kuwa ni wa milele, matokeo yake au zao inaweza kuwa si ya daima au ya uwongo . Haiwezi kupatikana kuhakikisha kuwa dunia si ya kweli na ni ya kuwazwa tu kama ndoto, au mawazo ya nyoka katika kamba inapokuwa kizani; kwa sababu mawazo au uwongo ni sifa. Sasa, sifa haiwezi kuwa nyoka kutokana na mchezaji wake wa mawazo ni wa daima, nafasi yake lazima iwe ya daima. Ikiwa si hivyo, mchezaji lazima ahesabiwe kuwa si madhubuti na si imara. Pia, ndoto haiwezi kuotwa bila ya kuviona au kivisikia vitu hivyo unavyoviota pale unapokuwa umacho. Vitu vya kweli vinavyoviona unapokuwa macho vinawacha alama katika akili kwa kuwa na mungano na akili, na kuiweka elimu katika nafsi. Alama hizi zinafahamika na kuonekana na akili unapokuwa unaota. Sababu ya kitu inakuwapo wakati wa kuota, kuwa vitu vya ndani vinaendelea kuwapo wakati wa kutokuwapo kwa elimu katika usingizi mkali. Ikiwa ndoto inaweza kuotwa bila ya alama zo zote za hapo mwanzo, mtu aliyefanywa kipofu wakati wa kuzaliwa kwake lazima auote mwangaza. Kwa hivyo, pana alama tu katika ndoto, na vitu vyake vya kweli vipo katika asili yake ya nje.

Kwa sababu, ni ujinga wa vitu vya kweli wa vitu vya dunia katika usingizi mzito, lakini si katika mzimiko wake wa kabisa. Ni kama vile vitu vilivyo nyuma ya mgongo wa mtu. Hivyo haviwezi kuoondoshwa kabisa. Basi haya haya yanafuatwa na ndoto na usingizi mzito. Hivyo, yaliyosemwa hapa juu, kuwa, Mwenyezi Mungu, roho, na kitu au sababu za dunia, hazina mwanzo na ni daima, ni kweli.

**Wafuasi wa Budha na Jain.**

Q.6. Ilivyokuwa sababu tano ni za daima, dunia nzima ni thabiti na ya daima.

A. Haya si kweli, ikiwa vitu vyote ni vya daima, sababu ambazo mazao yake na uangamizi unajulikana vilivyo; umbo lote la dunia na vilivyomo, vitu na vyenginevyo vyote, ambavyc vinazaliwa na kuangamia, lazima viwe vya daima; lakini haviko hivyo. Hivyo, mazao au matokeo hayawezi kuwa ya daima na thabiti.

Q.7. Yote yako dhahiri. Hapana kitu kimoja. Cho chote kile sisi tunachokiangalia, sisi hatuwezi kuona kuwa kuna kitu chengine kiko ndani yake.

A. Kitu cha vitu, wakati, pahali, roho ya ndani kabisa, jinsi na maumbile ni ya thabiti na hayabadiliki. Hawezi kwa na cho chote mbali kutoka na wao. Hivyo vitu haviko dhahiri na mbali mbali. Huonekana kuwa hivyo. Kuna kitu kimoja kinachopiga mstari yote.

Q.8. Kitu hakiwezi kuwapo katika chengine, kama vile ng'ombe hayumo katika farasi au farasi hayumo katika ng'ombe, lakini ng'ombe yumo kwenye ng'ombe na farasi kwenye farasi? Hivyo wao hawawezi kuwa hawapo. Ikiwa hakuna vitu, vipi kuwepo kwao katika wao kwa wao uhakikishwe?

**Wanaoamini.**

Q.9. Asili inazaa.dunia; i.e. inatoka kwa ghafla; kama mchanganyiko wa maji na chakula huoza na huzaa funza, kuwapo kwa mbegu, dunia, maji huleta nyasi, mimea, mawe na vitu vyenginevyo. Mawimbi yanaletwa upepo mapochanganyika na bahari. Povu la bahari linatokana na mawimbi. Udongo mwekundu, ndimu na maji ya limau inapochanganyishwa na kupondwa, hutoa unga mwekundu (rori). Kwa njia hii hii, dunia inatokana na asili ya sifa za vitu. Hapana anayevitengeneza.

A. Ikiwa dunia inatokana na asili au kwa ghafla, basi katu isiangamizwe. Ikiwa uangamizi unafikiri kuwa ni sifa zake, hapatakuwa na mtengenezeko wake. Ikiwa vyote viwili mtengenezeko na uangamizi inafikiriwa kuwa ni uko tokea kwanza katika vitu, hapatakuwa na mdhihirisho na alama za kuzaliwa na kuangamia. Ikiwa sababu dhahiri inafikiriwa kuwapo kama ni wazi na kuangamiza dunia, lazima ifikiriwe kuwepo kama ni dhahiri kutokana na vitu vilivyo zaliwa na kuangamia. Ikiwa mazao na maangamizi ni ya kawaida, hawezekani kuwapo mmoja na wakati mmoja. Ikiwa muumbo ni wa kawaida au wa ghafla basi vipi kuwa hapana dunia nyingine, mwezi, jua na sayari nyinginezo na nyote zinatokeza na kuwapo karibu na zile zilizokuwapo hivi sasa? Nyasi zo zote, mimea funza, na namna nyinginezo za mboga au maisha ya mnyama yanazaliwa kutokana na mwungano wa mbegu. nafaka maji na mambo mengine ya vitu vya asili, hivyo vinatengenezwa kutokana na vitu vilivyo tengenezwa na Mungu; lakini si bila ya wao. Hivyo, kwa mfano, kuutengeneza unga mwekundu (rori), vitu unavyo vihitaji, kwa majina ni, udongo mwekundu, ndimu, maji ya limau yanayo patikana katika sehemu mbali mbali za mji, haviji pamoja bila ya kuwekwa pamoja na mtu. Pia, unatengenezwa kwa kuvichanganyisha kwa vipipo maalum, na si kwa kutia hichi za idina kile kuwa kasoro. Kwa njia hii hii, vitu mbali mbali na namna mbali mbali za wanyama hawawezi kutokana au kuzaliwa kwa mujibu ya wanavyotaka wao wenyewe bila ya Mungu kuwaunganisha kwa hekima Yake na makusudio.

Q. Hapakuwapo, yupo, na hapatakuwapo mtengenezaji wa dunia hii. Lakini ipo kwa sababu ilikuwapo tokea wakati usio kuwa na mwanzo. Hikuzaliwa, wala haitaangamia kamwe.

A. Hapana kitendo kinachofanyika, wala kitu kinachoumbika kutokana na kitendo bila ya mtendaji. Dunia na vitu vyenginevyo ambavyo vina dhihirisha

makusudio katika mwungano maalum wa vijiji, haviwezi kutokuwa na mwanzo. Kile kinachozaliwa na mwungano wa viungo, havikuwapo kabla ya mwungano huo, wala havitabaki baada ya mkatizo. Ikiwa wewe huamini haya, basi wewe lazima nyachungue kuyahakikisha juu ya kipande cha jiwe gumu sana, almasi, chuma cha pua na vitu vyenginevyo vilivyo vigumu, kwa kuvunja vipande vidogo vidogo kwa kuvinyonga nyonga au kuvigeuza kuwa jivu, na kuona kama havijatengenezwa na sehemu ndogo ndogo au chembe ndogo kabisa. Ikiwa vimetengenezwa kwa chembe ndogo kabisa basi lazima viwachane na kuwa katika sehemu zao za asili kwa wakati kupita.

**Si Mungu Lakini Ni Roho**

Q. Hapana mwanzo wa Mungu. Roho ambayo inakuwa yenye busara kwa kujipatia hekima zote na uwema mwingineo, na kuwa yenye nguvu kabisa kwa kujipatia nguvu za ajabu zisizoonekana na mengineyo kwa kusaidiwa au kwa yoga anaitwa Mtawala Mkuu.

A. Ingekuwa hakuna Mungu asiye na Mwanzo, mwuumba wa dunia, vipi dunia ambayo imejaa uhai, ambayo inaisaidia roho, na ambayo imetengenezwa kwa mtengenezo wa sababu za kulimaliza miili ya wanyama, sehemu za akili, inaweza kutengenezeka? Bila ya haya nafsi hawezi kupata nguvu. Bila ya nguvu vipi itaweza kuwa yenye busara zote na nguvu zote. Hata iwe na busara vipi na nguvu nafsi inaweza kuwa kwa kupata nguvu za siri, haiwezi kujipatia nguvu sawa na nguvu za Mungu, ambayo ni ya kawaida Yake, ya milele, na isiyoweza kushikika, na isiyokuwa na mwisho. Hivyo, ikiwa ujuzi wa nafsi inaendelea na kufikia kiwango cha juu kabisa pia utakuwa na kikomo na nguvu zake pia zitakuwa na kikomo. Katu hainaweza kujipatia ujuzi na nguvu zisizona mwisho. Tazama hapa, hapaja kuwa na hata mmoja mpaka sasa, ambaye angeweza kuugeuza mpango wa asili ya Mungu. Wala hapata kuwa na mtu kama huyo. Mungu ambaye alikuwapo tokea wakati usiokuwa na mwanzo, anaziweka sheria, kuwa macho lazima yaone, na mashikio yasikie. Sasa hapana hata yogi ye yote au nguvu za siri zo zote zinaweza kugeuza haya. Roho katu haiwezi kuwa Mungu.

**Umoja Wa Muumbo.**

Q. Mungu hutengeneza dunia za namna nyingi zenye kipindi cha wakati mrefu na vipindi au ya namna hiyo hiyo?

A. Dunia ilikuwa kama hii hapo zamani na itabaki kuwa hivi hivi mbeleni. Yeye haifanyi kuwa tafauti.

Rig. 190. 3. Mungu amelitengeneza jua, mwezi, umeme, ulimwengu, anga na mbingu vitu vyenginevyo vya peponi wakati huu wa sasa kama Yeye alivitengeneza wakati uliokwisha pita. Yeye ataitengeneza kwa mpango huu huu katika wakati ujao. Kwa hivyo, kazi za Mungu daima ziko na umoja wala hazina makosa au ila. Kuwa kazi za mtu zina ila na zinatafautiana, na ujuzi wake unaweza kuzidi au kupungua. Lakini si hivyo kwa kazi za Mungu.

**Uthabiti Wa Falsafa Sita.**

Q. Ati Vedas na maadishi mengine ya kweli yana uthibitisho kuhusu muumbo, au haya uthibitisho?.

A. Yote yanayo uthibitisho.

Q. Ikiwa haya pingani, vipi yote yataweza kupatanishwa? Falsafa gani ya hizi sita ni ya kweli? Hivyo, kwa mfano, sisi tunaona katika hizi.

Tait, Br. V. An. I. Kutoka kwa Mungu na asili inazaliwa mbigu au anga, ambayo inaonekana kutokana na vitu vinavyochanganyika pamoja kila pahali kuwa katika hali ya asili. Kwa kweli asili haizaliwi: vitu vitapatikana wapi na chembe ndogo kabisa inayokuwapo katika anga? Baada ya anga kujitoa katika hewa, tena moto, tena maji, na tena ardhi ambamo zinatoka sayari ambazo huzaa vakuliwa ambazo huzaa shahawa, ambamo mtu au mwili unazaliwa. Huu ni mpango wa muumbo katika maandishi haya ambamo anga inaonekana kwanza. Chhandoya inatengeneza moto na nyingine hutangulia. Maji ya Aitereya na nyinginezo katika kueleza muumbo. Vedas hutokana na muumbo wakati mwingine kutoka kwa watu pengine Hiranya Garbha na mengineyo. Mimansa inaandikia muumbo kwa kitendo au nguvu ya ulimwengu. Vaisheshik inaiweka kwenye wakati, Nyaya kwa sehemu ndogo kabisa, Yoga kwa jambo la ujasiri au ushujaa, Sankhya kwa Prakriti au Tabia, na mfuasi wa Vedanta kwa Brahman. Sasa, ipi ni ya kweli na ipi ni ya uwongo?

A. Sababu zote hizi ni za kweli na hapana iliyo ya uwongo; lakini uwongo ni yule ambaye hayafahamu haya. Kwa sababu Mwenyezi Mungu Mkubwa ni mstadi wa asili; na Tabia au Prakriti ni asili ya kitu cha dunia, Mghariko mapotokea, muumbo huanza kwa mujibu huu hapa juu, viz, mbingu au anga ya juu na kadhalika. Mbingu na hewa hazijaangamia, lakini moto na mengineyo yameangamia, muumbo huanza kutokana moto na kadhalika; moto wa umeme hauangamii, muumbe huanza kutokana na maji na mengineyo yanayofuata haya. Kwa maneno mengine muumbo huanza kutokana na kila mghariko mpaka pale uangamizi ulitokea. Purush, Hiranyagarbh na maneno mengine yameelezwa katika sura ya kwanza ya kitabu hiki kama ni majina ya Mungu Mkubwa. Lakini matatizo au ubishano ni ule ambawo unasema hadithi tafauti ya mmoja na kisa kile kile kwa wakati tafauti katika kazi. Wewe utaona intidhamu iliyokamilika iliyoenea katika skuli sita za falsafa katika tabia hii. Kwa mujibu wa Mimansa, hapana kazi katika dunia, ambapo katika kufanyika kwake hapana kitendo au nguvu zinatumika. Kwa mujibu wa Vaisheshik, hapana kitu kinaweza kufanyika bila ya wakati au saa. Nyaya inaendelea kuweka kuwa hapana kitu kinachoweza kufanyika bila ya kuwapo kwa chembe ndogo ndogo kabisa, au asili ya kitu. Yoga inauhakikisho kuwa kitu hakiwezi kufanyika bila ya ujuzi, busara, akili. Kwa mujibu wa Sankhya, kitu hakiwezi kufanyika bila ya mwungano wa vitu. Wafuasi wa Vedanta wanaitilia makazo kuwa hapa kitu kinachoweza kuzaliwa bila ya sababu ya kitu. Hivyo muumbo hufanyika kutokana na kazi za asili sita, kila mmoja ya asili hizi imeelezwa kwa urefu na kila skuli ya falsafa. Hivyo

hazibishana wao kwa wao. Ni kama watu sita waliojiunga kuiezeka juu ya kuta na kufanya nyumba. Sawa sawa na haya ni skuli sita za falsafa zimetoa sababu za muumbo kwa kutokuchoka. Ni kama hadithi ya tembo wa kipofu.

**Tembo wa Kipofu.**

Hapo zamani za kale mtu mmoja aliwapa watu watano walio vipovu na mmoja aliyeona kidogo sehemu ya tembo. Hapo yeye aliwauliza hawo watu huyo alikuwa ni mnyama gani kwa fikira zao. Mmoja katika wao alisema kuwa ilikuwa kama nguzo, mwingine kama ni pembua, watatu kama mchi, wanne kama ufagio, watano kama ni jukwa, wasita alisema kuwa kilikuwa kitu cheusi na kidogo kama nyati katika umbo la kupumzika juu ya nguzo.

Kwa njia hii, watu wote na kidogo waliojifunza vitabu vya kisasa tu, lakini hawaja vikagua vitabu vilivyoandikwa na mawalii na wafuzi wa falsafa, la, wale ambawo wamebobea katika Sanskrit na Vitabu vya lugha tu kama vilivyoandikwa na watu waliona elimu haba, wameshughulika vibaya kupotezana na kugombana wenyewe kwa wenyewe bila ya kuwa na sababu. Mafunzo yao haya stahiki sifa za wenye busara na wenye akili: kwa sababu, vipi kipofu atajikinga na asianguke kwenye shimo la dhiki akimfuata kipofu mwingine? Sawa sawa na haya ni ulaghai huangamiza yote yaliyo mazuri na ya kwendelea, kwa watu wenye dini ya kisasa, kuwa na elimu ya juu juu, uwejawa na mapendeleo, na kupewa moyo na roho ya anasa nyingi.

Q. Wakati matokeo hayazaliwi bila ya asili, kwanini hakuna asili ya asili?

A. Ee nyingi watu wapenzi, kwa nini hamjuulizi kidogo? Tazameni hapa, pana vitu viwili duniani, viz, asili na matokeo. Nini ni asili, si ni matokeo, na hapo inapokuwa ni matokeo, huwa si asili. Mtu anapokuwa haifahamu dunia, yeye hawezi kupata ukweli na elimu iliyo ya kweli ya vitu. Isikilize falsafa:-

**Muumbo Nini?**

Muumbo ni mwungano wa jambo la ajabu, ambayo ni kitu na maumbo yanayoonekana yaliyotolewa na kuendelezwa kwake na kuwa yasiyoonekana asili zao; yamebadilika katika hali zao kutoka kwenye mwungano wao maalum; mwanzo wa kazi ya vitu ambavyo ni vijanja na vya kujulikana baina yao wenyewe, vinazaliwa kutokana na Tabia, ambayo ni usawa wa vitu vitatu vya kuendelea, viz., sathwa, (mngaro), raja (vitendo), na tama (ugumu).

Kwa maneno mengine, tabia au Prakriti ni usawa wa kutokuwa na mwanzo na sababu za milele za sathwa, raja na tama. Inazaa vitu, vyakujulikana na hafifu. Vitu hivi vilivyotokana hapa huanza kuungana, na mwungano wao huu maalum na huleta mabadiliko wa hali zao. Japokuwa ni hafifu na hayaonekani

kwanza, huanza kuwa mzito na vitu vilivyo vikubwa na kuwa katika mambo ya ajabu ya dunia iliyopo sasa. Kuwepo kwa mambo haya kunaitwa muumbo. Haya, asili ni kitu cha kwanza, au hupanga kwa vitu vyengine viungane na ni matokeo baada ya mtawanyiko au mchanganuo, na kile kinachoweza kugawanyika. Matokeo ni kile kinachozaliwa baada ya mwungano wa vitu au vitu vya asili, na haiko katika hali ile ile baada ya mchanganuo. Kusema kuhusu asili ya asili, matokeo ya matokeo, mfanyaji wa mfanyaji, sababu ya sababu, mwisho wa mwisho, ni kama kumwita kipofu kuwa mwonaji, msikilizaji kiziwi, mjuzi mjinga. Kuna jicho la jicho, taa ya taa, jua la jua? Kile kinachozaa, ni asili, na kile kinachozaliwa ni matokeo. Yeye ambaye anaigeuza asili kuwa matokeo, ni mfanyaji.

**Pia, yaangalie Gita inasema nini:-**

Ni ubeti wa 16th kutoka kwenye sura ya II ya Gita. Maana yake ni kisichokuwapo katu lakiwezi kuwapo hasa, wala kilichokuwapo kinaweza kupunguzwa na kufanywa kuwa si kitu hasa. Sababu hizi mbili zimehakikishwa hasa na wana wa falsafa. Vipi mshupavu, asiye na haki, mwenye nia avu, mjinga washenzi watafahamu haya kwa urahisi? Kwa sababu mtu, ijapokuwa ni mwenye elimu na anawo marafiki wazuri, hata hivyo hachukui taabu ya kufikiri yeye mwenyewe na kuyaendea mambo na kuyachungua vyema, daima yuko chini katika shimo la madanganyo. Wamebarikiwa watu wale ambawo wanajua sheria za elimu ya sehemu zote na kujaribu kuzijua, na baada ya wao wenyewe kuyajua, wazisomeshe bila ya hitilafu. Hivyo, yeye hajui cho chote yeye ambaye anaamini dunia inaumbwa kutokana na cho chote. Wakati unapowadia wa kuitengeneza dunia, Roho. Mtakatifu huziunganisha chembe ndogo ndogo ya kitu. Katika sehemu ya kwanza ya maendeleo huwa kidogo nzito kuliko tabia erevu ya Prakriti au kitu inaitwa Mahat tattwa (kitu kikubwa). Bado kile kilicho kizito zaidi kuliko hicho kinaitwa Ahankara. Hapo tena huja Ahankara vitu vitano vijanja (sukshma bhuta). Tena vinazaliwa viungo vitano vya kutilia mkazo vya hisia, viz, shingo (sauti), mikono, miguu, viungo vya uzazi, mavi; ya kumi na moja ni nia au manas huzaa vitu vitano kwa intidhamu, kupunguka sana au kuzidi kutokana na asili zao hasa, na yakuonekana sana na sisi sote. Wao huzaa namna nyingi za mimea, miti, na vitu vyenginevyo, na kutokana na hivi huja vitu vya vyakula, ambavyo huzaa mbegu, shahawa, mayai ya wanawake, ambayo huza mwili. Lakini muumbo wakati wa kwanza haukuwa ni mwungano wa mume na mke: Kwa sababu Mwenyezi Mungu anaitengeneza miili ya mwanamume na mwanamke na kuitia roho, tena kukua kwa sehemu za uzazi huendelea. Utizame mwili, vipi umetengenezwa kwa busara! Uchunguzi wake unamfanya mwenye elimu kustaajabu. Katika mwili utaona mpango wa mifupa, nidhamu ya mishipa, mpango wa nyama, mfuniko wa ngozi, wengu, maini, mapafu, mishipa ya moyo, mwungano wa ajabu wa roho na mwili. Umbo la kichwa linayo akili, mizizi ya uhai na nywele. Zitazame kucha na mwoto mwingine, sehemu hafifu ya macho, mtetemeko wa mishipa kama waya ya simu, zile sehemu za mwili kama kifuko mnamofanyizwa maji, msisimko katika sehemu za hisia, sehemu zinazokufanya

uamke, uote na uwe katika hali ya usingizi ya roho, mnyunyizo na mzao wa mwili mwendo wake, kutosheka na namna nyinginezo za hali yake, yote haya ni muumbo wa ajabu, na hauwezi kutenganezwa na ye yote ila Mungu. Hapana mtu ila Mungu Muweza anayeweza kuitengeneza dunia, iliyo jaa vito vya thamani na vitu; maisha ya mimea mingi yasiyoweza kuonekana kwa macho tu; mambo yaliyohusika na rangi mbali mbali, kijani, nyeupe, majano, nyeusi na rangi za kati na kati, zilipakwa kwenye majani, maua, matunda, mizizi na mengine kama haya. Isipokuwa Mungu tu, hapana anayeweza kuyatengeneza majani, mau, matunda, nafaka, mizizi mikubwa, na mizizi iliyotiwa ladha mbali mbali, - tamu, chumvi, isiyona ladha kali, kali, inayowasha; na namna ya kustaajabisha; dunia zisizoweza kuhesabika, jua milioni, miezi na nyota; mtengenezo, mgeuzo, ulinzi, kufuata kwao kwa sheria, na mipango mengine ya asili yake. Mtu anapokiona kitu, yeye huanza kufahamu vitu viwili, cha kwanza kuwepo kwa kitu kama kilivyo; cha pili ni mpango wa mfanyaji wa kitu hicho kwa kukiangalia vyema. Kwa mfano, mtu hukiona kitu kizuri cha kupambia katika mwitu. Kwa kukiangalia vyema anaona kuwa kimetengenezwa kwa dhahabu na fundi stadi. Kwa njia hii hii, ufundi wa muumbo wa ajabu, wa dunia wenye wanyama wengi unahakikisha kuwepo kwake mwandishi, Mtawala Mkuu wa muumbo wote.

**Muumbo Wa Kwanza.**

Q. Kipi kiliumbwa kwanza, mtu au dunia na vitu?

A. Dunia na vitu vyake viliumbwa kwanza, kwa sababu bila ya hivyo makaazi na msaidisho wa mtu hautaweza kutokea.

Q. Alikuwapo mtu mmoja au walikuwapo wanaume wengi mwanzoni mwa dunia? Walikuwapo wengine pia?

A. Watu wengi waliumbwa hapo mwanzoni mwa dunia; kwa sababu, Mungu huzizaa hizi roho mwanzoni mwa dunia, sifa za kazi zao huwawezesha wao kuzaliwa katika nyumba ya Mtakatifu. Inasema Yajur Veda. Hapo tena watu waliumbwa, inakwenda kuhakikisha kuwa wengi, i.e. mamia na maelfu ya watu waliumbwa hapo mwanzoni. Uchunguzi unahakikisha kuwa watu ni watoto wa zazazi wengi.

Q. Watu na wanyama wengine waliumbwa katika hali utoto, ujane, au utu uzima, au sehemu zote tatu za maisha katika mwanzo wa dunia?

A. Katika ujane. Kwa sababu, ingekuwa Mungu aliwatengeneza watoto kwanza, kusaidiwa kwao ungeta kuwepo kwa watu wengine. Ingekuwa Yeye aliwatengeneza kuwa wazee, pasingekuwapo mwungano wa ki mwili. Hivyo aliwaumba katika hali ya ujane.

**Mwanzo Wa Dunia**

Q. Kuna au hakuna mwanzo wa dunia?

A. La, hakuna hata mmoja. Kama mchana huendelea na kufuatwa na usiku na usiku kufuatwa na mchana, haya ni kusema, kufaulu kwa mwangaza na kiza ni

daima tangu wakati ulipoanza: hivyo ndiyo muumbo hufuatwa na uangamizi, uangamizi kufuatwa na muumbo, ni kusema mzunguko wa intidhamu ya dunia unaendelea daima na hauna mwisho. Hakuna mwanzo wala mwisho wake. Mwanzo na mwisho wa muumbo na uangamizi ni kama ule wa mchana na usiku. Kama Mwenyezi Mungu, nafsi, na matokeo ya dunia (kitu) ni vitu vitatu vya milele kwa asili ya tabia; pia ni muumbo na ulinzi, na kuwepo kwake dunia isiyokuwa na mwanzo kwa sifa za kurithiwa. Kama mkondo wa ziwa daima ni wa namna moja, sasa unafurika, na sasa ni mkavu, sasa ni mafu na sasa unafurika katika nyakati za mvua, na kupotea kabisa katika siku za joto; hivyo hivyo ni maendeleo ya ulimwengu kuhusu kuendelea kwake. Sifa zake Mungu, tabia na asili haina mwanzo. Muumbo wake, ulinzi wake na uangamizi wa dunia pia hauna mwanzo: Vitendo vyake mwenyewe Mungu havina mwanzo wala mwisho, kama vile hakuna mwanzo wa mwisho wa sifa zake, tabia na asili yake.

**Hitilafu Ya Maisha.**

Q. Ni mpendelea wa Mungu kuwa Yeye ameziza baadhi ya roho ya wanadamu, wengine katika hali za hikatili za simba na kama wanyama wakulindwa, wengine kuwa katika hali ya paa, kama ng'ombe na wanyama wengine wasio wakali, wengine kwenye enzi ya mboga, na kwa wengine tena kuwa katika hali ya mnyama wa kutambaa na kama wa nyama wanaotambaa.

A. La hakuna mapendeleo ya Mungu kuhusu haya. Kwa sababu, mtafautisho katika maisha ni kwa mujibu wa kazi zao walizozifanya katika muumbo uliyopita. Ingekuwa Mungu hakujali sifa zao katika mgawanyiko wa uzazi wao, Yeye angekuwa amependelea.

**Pahali Pa Muumbo Wa Mtu.**

Q. Mtu wa kwanza aliumbwa wapi?

A. Kwanza aliumbwa katika Trivishtapa sasa inaitwa Tibet.

Q. Palikuwa na namna na kabila moja tu la watu, au palikuwapo na matabaka mbali mbali ya watu hapo mwanzoni mwa dunia.

A. Palikuwapo na kabila au tabaka moja tu, la binadamu. Baadaye, kwa mujibu wa Rig. Veda.

Watukufu na waadilifu wanaitwa Aryas, wataalamu, devas au mungu, na wa chini na wahshi Dasyus au wezi na wajinga. Hivyo watu waligawanyika katika sehemu mbili, Arya na Dasyu. Zaidi kuhusu Rig. Veda inasema, - Uta shudre uta arye, - (Ria imetolewa katika Atharva.) - Kwa mujibu wa haya, Ma-Arya waliwekwa katika sehemu nne, viz, Brahmanas (maaskofu), Kshtriyas (mashujaa) Vaishyas (wafanyi biashara), na Shudras (watumishi). Watu wenye elimu waliitwa Aryas, watu wajinga waliitwa Shudras na Anaryas.

**Mjio Wa Ma Arya.**

Q. Vipi wao walikuja hapa?

A. Wakati ngomvi baiha ya Ma-Arya na Dasyus i.e. wataalamu, miungu na mashetani wajinga, kuwa wa kila mara na vibaya zaidi: Ma-Arya, ukichukulia ardhi hii ya (India)kuwa ni nchi bora zaidi katika dunia, walikuja hapa kufanya makaazi yao hapa, na hivyo ikapewa jina la Aryavarta au makaazi ya watukutu.

Q Nini mipaka ya Aryavarta?

Manu, 11, 22, 17,. Himalayas iko Kaskazini, Kusini iko Vindhyachalas na Mashariki na Magharibi iko bahari na hii ndiyo mipaka yake. Kwa maneno mengine, Mipaka hiyo inaitwa Aryavarta, ambayo inajipanua mpaka Attock au Indus ya magharibi, na mpaka Irravady, inayonyanyuka kutoka kaskazini mwa Nepal na mpaka Brahmaputra, ambayo inaipaka Assam Mashariki na kuangukia Bay ya Bengal ya mashariki; na kutoka kwenye mstari wa kati wa Himalaya unaendelea mpaka Rameshwara ya kusini, iliyogawanyika na milima ya Vindya na kuzungukwa na Ghats. Inaitwa Aryavarta, kwa sababu walikuwa watu wa Miungu au watu wenye elimu kwa kuwa ilikuwa ni makao ya Ma-Arya.

Q. Nini hasa jina lake la halisi, na walushi hapo kabla ya Ma-Arya?

A. Halikuwa na jina hasa kabla ya hapo. Pia hapajakuwa na watu kabla ya makaazi ya Ma-Arya. Kwa sababu, Ma-Arya walikuja kwenye ardhi hii kutoka Tibet muda mfupi tu baada ya mwanzo wa dunia.

Q. Wengine wanasema, wao walikuja kutoka Iran. (Persia), hata hivyo wao waliitwa Ma-Arya. Ardhi hii kabla ya wao ilikaliwa na washenzi, waliokuwa wakitwa Asuras na Rakshasas, na Ma-Arya walijiita wenyewe miungu wa Devatas. Wao walipopigana pamoja, vita vyao viliitwa vita vya miungu na pepo mbaya katika hadithi za pepo.

A. Yote haya ni ya uwongo mtupu; kwa sababu huu ni ubeti wa Rig Veda 1.51.8. Yameshasemwa kitambo hapa juu kuwa jina, Arya, walipewa wale walio wema, wajuzi, watakatifu; na wapinzani wao au watu wenye sifa za kinyume na hawa, walitawaliwa na kuitwa Dasyus au wezi, waovu, watendaji maasi, wasio na dini, wajinga. Pia, Brahmanas, Kshatriyas, na Vaishyas waliitwa Dvija au walio zaliwa mara ya pili na Ma-Arya na Shudras, Anaryas au wajinga. Wakati haya huwa ni satwa ya Veda. Wataalamu wapambanuzi hawawezi kuamini mitindo na upunzani wa wageni. Katika vita vya miungu na pepo wabaya, vilivyotokea katika milima ya Himalaya kati ya Ma-Aryas na Dasyus, washenzi au wachawi (Assyrians), Arjuna na Mfalme Dasharatha walijiunga kutoka Aryavarta kuwasaidia miungu kuwazunguka ushindi wa Asuras (wachawi). Kutoka haya ni dhahiri kuwa watu walioishi katika nchi kuwazungukia nje ya Aryavarta kwendea Mash. Kusini, kusini, Ku. Magh., magharibi, M.K., Kaskazini, K.M. ya Himalaya, waliitwa Asuras (washenzi wa kihindi). Kwa sababu, wakati wo wote

wakiwahujumu Ma Arya waliokuwa wanaishi katika majimbo ya Himalaya, watoto wa kiume wa kifalme na wafalme wa nchi hii waliwasaidia katika hujuma zao. Vita vilivyopiganiwa kusini na Ramchandra, inaitwa vita vya miungu na wachawi, lakini vinaitwa vita vya Rama na Ravana, au vita baina ya Ma Arya na Rakshasas (wa shenzi wa kihindi). Hapana hata kitabu kimoja cha Sanskrit kilichosema kama Ma-Arya walikuja kutoka Iran, na waliwashinda majambazi katika vita vya nchi, waliwakimbiza na wakajiweka kuwa watawala wa nchi. Vipi basi maandishi ya wageni yasadikiwe katika ushahidi?

**Dasyus au Washenzi.**

Manu X., 45, 11. 23. Pia, nchi nyinginezo zinaitwa nchi za Dasyus na Washenzi. Kutoka ushahidi huu ni dhahiri kuwa wakaazi wa nchi zilizo katika Mashariki, M.K. Kaskazini K.M. magharibi wanaitwa Dasyus, Mlechchhas (washenzi wa kihindi) na Asuras (wachawi); na watu wanaoishi katika nchi za K.M., kusini, K. magh, mpaka Aryavarta, wanaitwa Rakshasas. Walio upande wa pili wa Aryavarta ni Nagas, na nchi yao inaitwa Patal, ambayo inaonyesha kuwa ipo chini ya miguu (pa: Migu na tal chini.) Walikuwapo wafalme wa hawa Nagas, i.e nasaba za Nagas. Mmoja wa watoto wao wa kike, aliyeitwa Ulopi, aliolewa na Arjuna. Kwa maneno mengine, utawala wa Ma Arya ulikwishia kutoka Ikshwaku mpaka Kowrawas na Pandawas juu ya dunia nzima na kwa hali moja uliendeleza dini ya Vedas katika nchi nyinginezo. Uhakikisho wake ni ule kuwa mwana wa kiume wa Virat, mtoto wa kiume wa Virat alikuwa Manu, watoto kumi wa kiume wa Manu waliitwa Marichi na kama hivi na wafuasi wake saba waliitwa Swayambhara na wengineo, wote walikuwa wafalme. Wafusi wao, waliitwa Ikshwaku na wenginewo, walikuwa wa wafalme wa mwanzo walio watawala Aryavarta. Lakini sasa wala si kwa ajili wa bahati yao mbaya, uvivu, dharau na ugomvi wa wao kwa wao Ma Arya walipoteza utawala wao wenyewe uliokuwa usiogawanyika, uhuru, na wenye amani; na haba sana kuongea utawala wao wa nchi za kigeni. Utawala wo wote waliouwachilia wao umekanyagwa na wageni. Wafalme haba sana walio kuwa wako huru. Siku mbaya zinapokuja, watu lazima wapate taabu nyingi. Uzuri wo wote unawofanyiwa wao Utawa wa Nyumbani ni bora zaidi kuliko wote mwingine. Utawala wa kigeni japokuwa ni wenye uhuru wa dini na wenye upendeleo wa kabila, ijapokuwa ni wa busara kwa wazazi, na uliojaa kwa huruma na haki, si wenye mustakbali wa amani kamili na furaha. Lakini ni shida sana kuondoa uovu wa namna mbali mbali, mfundisho ya kidini, na mpambano ya upataji wa mahitaji. Bila ya kuyaondosha yote haya, ni vigumu kuendeleza hali nzuri za watu. Hivyo, utawala wo wote na sheria zake za uongozi yote yametolewa katika Vedas na katika maandishi mengine matakatifu iliyafuatwe na watu wazuri kuwa ni kama wajibu wao.

**Wakati wa Muumbo.**

Q. Muda gani umepita tokea dunia umeumbwa?

A. Ni miaka elfu moja, mia tisa na milioni sitini kwa nambari zilizokamilika dunia iliumbwa na Veda kudhihirishwa. Urefu wa haya imetolewa katika

Mwanzo wa Maelezo kuhusu Vedas, ambayo inaweza kutazamwa kuhusu haya. Huu ulikuwa ni wakati wa muumbo na kukua kwa dunia. Inajulikana vyema kuwa kipande cha kitu ambacho hakiwezi kugawanyika tena kinaitwa "atom" (paramanu). Mwungano wa hivi 60 huifanya kuwa bitu kinachoitwa anu. Mwungano wa anu mbili hufanya kile kinachoitwa dwianuk au anu mbili, ambayo ni kitu cha hewa. Mwungano wa hii mara tatu huifanya kuwa ni kitu kinachoitwa moto, na nne ya haya huyafanya maji na tano ya hizi huufanya udongo. Pia mara tatu ya anu hufanya trasarenu au chembe, na chembe mbili kama haizi huifanya dunia na vitu vyengine vinayoonekana. Katika njia hii ya intidhamu Mungu ameitengeneza dunia na nyota nyinginezo.

**Mshikilio wa Dunia**

Q. Nani anaishikilia dunia? Baadhi ya Hydra (Shesha) ambaye anavyo vifiniko elfu vya kichwa, anainyanyua dunia juu ya kichwa chake. Mtu mwingine anasema kuwa ipo juu ya pembe ya ng'ombe. Watatu anasema kuwa haijanyanyuliwa na mtu. Wanne anasema kuwa hewa ndiyo inainyanyua. Watano anahakikisha kuwa nguvu za sayari inaiweka kwenye pahali pake huko peponi. Wa sita anasema kuwa ilivyokuwa ni nzito basi inadindimia chini katika mvuke wa anga. Haya ni baadhi ya maoni kuhusu kwa kushikiliwa kwa dunia. Sasa, ipi katika hizi ni ya kweli na yakuweza kusadikiwa?

A. Yeye ambaye anasema kuwa dunia inashikiliwa juu ya kichwa cha nyoka, pembe ya ng'ombe dume, lazima aulizwe kuwa ilishikiliwa juu ya kitu gani wakati wa wazazi wa hawo wanyama walizaliwa. Pia, kitu gani wao wanakishikilia huyo nyoka na ng'ombe? Waislamu wanaokubali haya mambo ya ng'ombe watazishika ndimi zao wakati wa suali hili. Lakini mtu anayeshikilia kuwa ni nyoka atasema kuwa nyoka anapumzika juu ya kobe ambaye anaelea juu ya maji. Maji haya yameshikwa na moto, ambayo inasaidiwa na hewa, hewa huishi katika mbingu. Mtu huyu lazima aulizwe juu ya nani wanaegemea wote. Ni mmoja katika kumi kuwa atasema Mungu ndiye anayewashika wote. Ikiwa ataulizwa kuwa watoto wa nani hawa nyoka na ng'ombe, yeye atasema kuwa Kashyapa alikuwa mvulana wa Kadru na ng'ombe dume ni wang'ombe jike. Marichi, baba wa Kashyapa alikuwa mtoto wa kiume wa Manu ambaye alikuwa mtoto wa kiume wa Virat. Brahma, baba wa Virat, aliishi katika asubuhi wa muumbo. Palikuwapo na tabaka tano kabla ya uzazi wa nyoka. Nani aliinyanyua dunia hapo? Kwa muhtasari wa maneno, juu ya nini dunia ili puumzika wakati wa tuseme, uzazi wa Kashyapa? Yeye tena hapo atasema: Wewe umenyamazishwa na mimi nimenyamazishwa.! Waulizaji wote wawili na msikilizaji wataanza kupigana. Kwa kweli ni kuwa aliyebakia ni Shesha au makombo. Hivyo, waandishi wengine walisema kuwa Shesha ndiye anayeinyanyua dunia. Wengine bila ya kuya fahamu haya vyema, walifikiria kuwa ni nyoka. Lakini ilivyokuwa Mungu anabaki baada ya muumbo na uangamizi wa dunia, Yeye anaitwa Shesha, Omega, na dunia inanyanyuliwa na Yeye. Atharwa Veda inasema, Kanda 14, varga, 1. ubeti wa 1, - Satyenottabhita bhumih, kuwa Satya au ukweli ambawo ni mbichi daima na hauwezi kuangamizika katika sehemu tatu za wakati na ambawo ni Mungu, anainyanyua dunia, kama hivi, na dunia nyengine zote -

uksha dadhar prithiwim uta dyam. Huu ni ubeti kutoka Rig Veda. Inaonekana kuwa mtu anapoiona dunia uksha akaifasiri kuwa ni ng'ombe dume; kwa sababu pia lina maana ya ng'ombe dume. Lakini alifanya mjinga mwenyewe kuwa yeye hakufikiri kuwa ng'ombe dume ataweza kuwa na nguvu za kutosha za kiinyanyua dunia kubwa kama hii. Neno uksha maana yake ni jua ambalo linaletea dunia mvua ambayo inairutubisha. Jua linaizuia dunia kwa nguvu za nuru yake. Lakini hapa hapana ila Mungu anayeliziwia jua na dunia nyinginezo.

Q. Vipi Mungu anainyanyua sayari kubwa kama hizi dunia?

A. Mbele ya Mungu Muweza dunia zisizo na hesabu si cho chote ni kama chembe ndogo tu, kama katika mbingu kubwa dunia si kitu ndani yake, ni kama tone la maji katika bahari kubwa. Mungu ameenea kote ndani na nje kila pahala. Yajur Veda inasema: Vibhuh prajasi - Roho ya ndani, imewaenea viumbe vyote, na anawanyanyua wote. Ingekuwa Yeye, hakuenea kote kama Wakristo, Waislamu na Purinians (Hekaya Za Kihindi) zinavyodai, Yeye asinge inyanyua dunia nzima; kwa sababu, hapana anayeweza kukinyanyua kitu bila ya kuwepo mikononi mwake.

Q. Kwani dunia na sayari nyingine huzunguka au ziko papo hapo?

A. Hizo zinazunguka.

**Dunia inaizunguka Jua.**

Q. Wengine wanasema kuwa jua ndilo linazunguka na dunia imesimama tu. Yapi katika haya ni ya kweli?

A. Yote haya nusu ni ya uwongo. Kwa sababu Veda inasema:

Yaj. III. 6. Dunia hii pamoja na maji yake yote yanaizunguka jua. Kwa hivyo dunia inasogea.

Yaj. 33. 43. Jua linaleta mvua, iliyotengenezwa kwa mwangaza na joto, ni ya ajabu katika pepo iliyo juu yetu. Yeye anawatia maisha katika viumbe kwa kuwaletea mvua na mishale yake. Yeye ni sababu ya kuona ya vitu vyote vyenye miwili. Yeye anawavutia vitu vyote, na aizunguka miale yake mwenyewe, lakini yeye haizizungukii sayari zenye mipango kama yake. Kwa njia hii, kila mpango. Umewekewa mwangaza na sayari nyingine zinaangazwa na kuvutiwa naye. Hivyo Ath. K. 14, An. 1, M. 13 anasema. Dunia na sayari nyingine zinapata mwangaza kutokana na jua kama mwezi pia. Lakini kubadilika kwa mchana na usiku kuko daima. Hivyo, sehemu ya dunia ambayo imegeuka jua, inaangazwa na inasemwa kuwa inafurahia mchana; na sehemu ambayo iko upande mwingine wake, ni kiza na usiku unatawala huku. Kwa maneno mengine, kuchomoza jua, kuuchwa kwa jua, alfajiri, mchana, usiku wa manane, na mgawanyiko mwingine wa saa, daima upo katika sehemu nyinginezo za dunia, haya ni kusema, inapokuwa ni asubuhi katika Aryavarta, ni jioni katika upande mwingine wa dunia kama Amerika. Inapokuwa ni mchana au usiku wa manane katika Aryavarta, ni Asubuhi au mchana huko Amerika Watu wanaposema kuwa jua

linasogea na dunia haisogei, wote ni wajinga kwa sababu, ingekuwa ni hivyo, basi pangekuwapo na mchana na usiku wa miaka elfu nyingi. Pia jina la jua ni bradhnah. Yeye ni mkubwa mara mia na maelfu nyingi kuliko dunia na Yuko mbali na dunia kwa maili milioni kumi. Ikiwa mlima unaizungukia mbegu ya bizari, itachukua muda mrefu, lakini itachukua muda mfupi kwa mbegu ya bizari kuuzunguka mlima. Kwa njia hii, mapinduzi ya dunia yanazaa jambo la mchana na usiku pamoja na faragha kubwa, lakini pia ni hivyo katika mpango wa jua kusogea. Wale wanaoliamini jua kuwa halisogei, pia hawajui elimu ya nyota; hivyo, ingekuwa halisogei, lisingemulika kutoka upande mmoja kwendea wa pili; pia kitu kizito bila ya kuzunguka mbinguni. Ma Jain wanaosema kuwa dunia haizunguki lakini inashuka kwa utaratibu, na kuwa pana majua mawili na miezi miwili katika Jamboodwipa (Asia), wao wamelala usingizi mzito katika ulevi wa majani. Ikiwa linakwenda chini, itavunjika kuwa vipande vipande ingekuwa hakuna mizunguko ya hewa iliyo vizungusha hapo na wakaazi wa sehemu ya dhiki hawatapata hewa na wale waliokuwa chini watapata zaidi kuliko wanavyohitajia, na mzunguko wa hewa utakuwa wa namna moja. Ingekuwa kuna majua mawili na miezi miwili, wangiangamiza kuwepo wa mwangaza na kiza kila wiki mbili. Kwa hivyo, dunia moja inayo mwezi mmoja tu, na dunia nyingi lakini zina jua moja tu.

**Dunia Nyingine Zinazokaliwa**

Q. Nini hivi jua, mwezi, nyota na sayari? Jee zinazo viumbu au hazikaliwi?

A. Zote hizi ni dunia zinazokaliwa na jinsi za watu. Nasema Shatapatha, K. 14, Pr. 6, Br. 7, Kandika 4,

Dunia, maji, hewa, mbingu, mwezi, nyota na jua vinaitwa Vasus (makao), kwa sababu vitu vyote na viumbe vyote wanaishi humo. Wao ni wakaazi wao. Ilivyokuwa hivyo ni makao, vinaitwa Vasus. Pale jua, mwezi na nyota nyinginezo ni wakaazi kama dunia, hapawezi kuwapo na hata kivuli kidogo cha shaka kuwa wao wanakaliwa na viumbe. Kama dunia hii ndogo ya Mungu imejaa watu na viumbe vyengine, dunia zingarazo hizi zote hazikaliwi? Hapana kazi ya Mungu ambayo haina sababu. Ikiwa dunia hizi zote ambazo haziwezi kuhesabika hazina watu na viumbe wengine, zinaweza kuwa na faida yo yote? Hivyo, watu na viumbe vyengine vimo humo.

Q. Watu na jamii nyingine wanazo sura namna moja, viungo kama vile vya watu wa dunia, au wao wako tafauti?

A. Inawezekana kuwa wao wawe tafauti kidogo, kama Machina, Ma Negro, Wahindi, Wazungu wanazo hitilafu katika viungo vyao, rangi, na umbo. Kwa njia hii, ipo tafauti katika miili yao inapokua. Lakini jinsi hujipatia aliyefanana naye katika dunia hizi zote kama zinavyofanya juu ya dunia hii: na viungo na nyafasi zao katika mwili vinafanana huko kama hapa. Inasema Rig. Veda, X, 190. 3. 3.

Mungu, mwuumba, amelitengeneza jua, mwezi, majimbo yanayo ngara, dunia, mbingu ya dunia zote, na furaha ya maisha inapatikana katika mzunguko uliokwisha pita katika njia hiyo hiyo Yeye ameufanya mzunguko huu. Yeye ametengeneza vivyo hivyo katika dunia nyinginezo, wala hapana tafauti.

Q. Kuna Veda kama hizi zilizodhihirishwa katika dunia zile?

A. Veda hizi hizi zimedhihirishwa huko kama vile utawala wa mfalme ni wa namna moja kote kwenye utawala wake, basi ni hivyo pia na Mtawala Mkuu; Bwana wa mabwana, sheria zilizowekwa katika Vedas imetiliwa nguvu katika muumbo wote.

**Mfalme Wa Mungu.**

Q. Ilivyokuwa roho na vitu kama Prakriti havina mwanzo na havijatengenezwa *na Mungu, Yeye lazima asiwe na nguvu juu yao; kwa sababu vyote hivi* vinajitawala.

A. Kama mfalme na raia zake wanajiweza, na raia wako chini ya mfalme basi roho pia na viumbe vyote ni viumbe vya Mungu. Ilivyokuwa Mungu ni mwandishi wa wote katika dunia, mtoaji wa matunda ya vitendo vyao, mlinzi wa wote, Mwenyezi Mungu; vipi roho na viumbe wasio na miili wasiwe chini Yake Yeye? Hivyo, roho ziko huru kutenda zinavyotaka, lakini wanamtegemea Mungu katika kuvuna matunda ya vitendo. Hivyo, Mungu Muweza anaumba, analinda na anaiangamiza dunia yote.

**Muhtasari.**

Mwenyezi Mungu alikuwapo kabla ya muumbo wa dunia, ambayo ilifunikika na kujichika katika shida, - Rig. X. CXXIX 3. CXXI. 1. Nakshi ya Mungu ikaileta dunia hii kuwapo na kuonekana - Taita II I. Kuna vitu vitatu ambavyo ni vya milele, viz. Mungu, roho na kitu. Rig. 1. CLXIV. 20. Mungu anaitengeneza dunia kutokana na kitu kwa ajili ya kuzifurahisha roho. Shwet. IV. 5. Sifa muhimu za kitu ni sattwa (kuwepo) rajas (nguvu) na tamas (ulegevu); ambayo ina zaa vitu vitano-dunia, maji, moto, hewa, anga ya juu ; na hisia 10, - nguvu za kuonea, kusikia, kunusa, kuonja, kugusa. Wengine wanasema kuwa Mungu alikuwapo hapo mwanzoni tu na Yeye aliiumba dunia kutokana na Yeye *mwenyewe kama buibui anavyouzaa utando wake (Mundak; Si kweli. Mungu ni* sababu nguvu zote, na wakati na mwahali, nakshi na nguvu ni sababu za vitu vya dunia. Ikiwa Mungu ameifanya dunia kutokana na Yeye mwenyewe ingekuwa yenye akili; kwa sababu ya kitu huendeleza sifa zake kwenye matokeo yake. - Vaish. 1. 24. Lakini Mungu ni busara tupu na mjuzi wa yote.

Kitu cha muumbo ni nguvu za Mungu na zinaweza kutumika kwaajili ya uzuri wa roho, ambazo hazina njia nyingine za kufurahia matunda ya vitendo vyao vilivyotendwa katika maisha mbali mbali kabla ya kuzaliwa wakati wa mwendo wao wa milele.

*Inasemekana kuwa Mungu ana nguvu zote. Anaweza kuumba bila ya kuwa* na cho chote cha kuumbia. La, Mungu haendi kinyume na sheria zake

mwenye. Kwa mfano, yeye hawezi kutenda dhambi, kufa, au kuzaliwa. Mungu hana mwili. Yeye kitu si kitu. Inaulizwa kuwa ikiwa hapana kitu kinachokuja bila ya sababu, nini sababu ya Mungu? Mungu ni sababu, na sababu ambazo ni rahisi, hazina sababu zao. - San. 1. 67. Hakuna mzizi wa mzizi. Hivyo hakuna sababu ya sababu.

Wakiristo na Waislamu wanasema kuwa Mungu anaiumba dunia kutokana na si cho chote. Lakini si kweli; kwa sababu, ni sheria ya Mungu kuwa cho chote huzaa cho chote. Wengine wanasema mtu hapati natija ya vitendo vyake. Mungu huumpa ampendayo Yeye. Inaulizwa kwa nini Mungu hawapi mapendeko yake watu bila ya wao kufanya kazi yo yote. Wafuasi wa Buddha na Jain wanaweka uwezo wa vitu. Lakini dunia haiko imara kama inavyojulikana kwa majaribio.

Wengine wanasema kuwa skuli sita za falsafa zilizowekwa kwaajili ya muumbo wa dunia kwa sababu mbali mbali hivyo zina mabishano. La; zote zina elekezana. Kuwapo kwa sababu sita, kila mmoja inajichukua kwa kitu chake; kama, Vedant inamweleza Mungu kuwa ni sababu ya nguvu zote; Nyaya, chembe isiyo gawanyika zaidi ya hapo kuwa ni sababu ya kitu; Yoga, ingekuwa ni sababu yake ya kawaida: Vaisheshik, Mimansa, na Sankhya, wakati, kitendo, na asili kuwa ni sababu ya vitu.

## SURA YA IX

### 1. ELIMU NA UJINGA

### 2. UTUMWA NA UHURU

Yaj. 40, 14. Yeye ambaye anaitambua elimu na ujinga pamoja, anakishinda kifo kwa kuzifanya kazi na kujipatia uokovu kwa kuipata elimu ya kweli. Ujinga umeelezwa kama hi.

Yoga. 11. 5. Kuiamini dunia isiyokuwa imara na mwili unaooza kuwa ni wa daima, i.e kuiona dunia ya vitendo kuwa ya daima na ya milele, na kukifanya kiwili wili kuwa ni cha malaika kwa fikra ya kukiweka daima kwa sababu za nguvu za roho au nguvu za Yoga, na itikadi nyinginezo zisizo za maana kama hizi ni daraja ya kwanza ya ujinga. Imani ya utakatifu na uchafu wa kitu kama mwili wa mwanamke asherati umefanywa kwa mwili uliooza wa mnyama (na shauki nyinginezo za uasherati) na pia mazoezi kama yale ya kusema uwongo, kuiba na uovu mwingine, huleta namna ya pili ya ujinga. Fikra ya raha katika namna hasa ya maumivu ambayo hutokana na shirikiana na vitendo vya raha za anasa na uasherati kupitia mpaka bila ya shaka ni namna ya tatu ya ujinga. Namna ya nne ya ujinga ni ule wa kujikiri mwili wa mtu au akili, na kitu kuwa ni roho. Namna hizi nne za elimu isiyo ya kweli au fikra za uwongo huitwa kuwa ni ujinga. Kinyume cha elimu hii, ni kusema, kukiona kitu kisicho dumu kuwa ni cha kudumu, kitu cha daima kuwa ni cha daima, kitu kichafu kuwa ni kichafu, kisafi kuwa ni safi, raha kuwa ni raha, si ya nafsi kuwa si ya nafsi, mwenyewe kuwa mwenyewe, kwa ufupi ni kukijua kama kilivyo katika tabia.

Elimu ni ile ambayo inatupa sisi fikra ya kweli na iliyo sawa ya kitu. Ujinga ni ule ambawo hautupi sisi fikra halisi ya kitu kutokana na hasa asili yake ilivyo. Kazi na utiifu pia huitwa ujinga, kwa sababu ni majina ya vitendo vya ndani na nje; lakini havitoe elimu hasa. Hivyo, ubeti wa Veda unasema kuwa hapana anaye weza kuyashinda maumivu ya kifo bila kutenda vitendo vya uwema na kumcha Mungu. Kwa maneno ya urahisi, kazi takatifu, utiifu wa kweli, na elimu hutuongoza kwenye uokovu; na kazi zisizo za haki, kama vile kusema uwongo, kuabudu wanyama na mawe, na elimu ya uwongo huuleta utumwa wa dhambi. Hapana mtu anayeweza kuwa bila ya kitendo, fikra, na namna ya elimu hata kwa mara mmoja. Kwa hivyo, kufanya kazi za uadilifu, kama vile kusema kweli na uadilifu mwingine; na kuwacha uwongo na kazi nyingine za uovu, lete sababu za uokovu.

**Iliyotumbukia au ya dhambi.**

Q. Nani ametumbukia au amejifunga katika dhambi?

A. Roho ambayo imejitoa kwenye uadilifu na kujitia katika ujinga.

**Laana Ya Milele na Uokovu**

Q. Utumwa na uhuru au kuangamia na kuokoka huwa ni wa kawaida au hotokea tu kama ajali, i.e hutokea kutokana na hafla kadha au sababu?

**Mungu na Roho Inabainishwa.**

Q. Ubeti huu unatokana na ulinganifu wa Mandaka Upanishat. Maana yake ni - Roho kuwa Mungu, yeye hana kizuizi, haya ni kusema, yeye hapitii kizuizi kuzaliwa tena au kuwa mtumwa wa dhambi. Hapana anayeweza kujichagulia sababu au matakwa ya matokeo ya uokovu. Roho haina uokovu wo wote. Hivyo vipi mtu atapata uhuru, yeye ambaye hajapata kufungwa katika roho?.

A. Uthibitisho huu wa Vedantins mpya si wa kweli; kwa sababu roho ilivyokuwa ina nguvu maalum tu imefunikwa na kiza; yeye hugeuka na kuwa na asili ya kiwiwili kwa kuja na mwili; yeye huingia tabuni kwa kufurahia matunda ya vitendo vya dhambi, hujaribu kuyaepuka haya, hupenda kuwa mbali na maumivu, na kuwa imefanya huru kutokana na maumivu ya mwili na kujipatia furaha ya kumpata Mungu, hufurahikia baraka za uokovu.

Q. Sifa zote hizi ni za kiwili wili na za hisia ya ndani, lakini si za roho, kwa sababu hiyo roho iko juu ya uwezo mzuri au uovu na ipo kama akili safi au kama ni mtazamaji tu. Joto na baridi na vyenginevyo vinaweza kufikia kiwili wili tu. Roho iko kamili na haiathiriki na hivyo.

A. Mwili na hisia ya ndani ni kitu tu. Havioni joto au baridi, wala havifurahi kitu cho chote. Viumbe vyenye hisia kama watu na wanyama, wanarihisi hivi. Kwa njia hii hii, puumzi pia si zenye uzima au kitu. Hazi sikii njaa au hazioni kiu; lakini viumbe vyenye puumzi wanaona njaa na kusikia kiu. Pia, nia au manas pia haina uhai au uzima au fikra, haiwezi kuona raha au maumivu. Kwa kinyume cha haya, roho huona raha au maumivu kutokana na nia. Kama vile roho huhisi raha au maumivu kwa kuwa mjulikano wa vitu, kama sauti ya kukubali au kukataa na mengineyo kama haya, kutokana na kiungo cha nje cha kuhisia, kama, mashikio na vyenginevyo; hivyo inaathirika na matakwa, chuki, ubaguzi, ukumbusho na hisia za kuwa peke yake, na yakustahimili heshima na aibu kwa kupitia sehemu nyingi, kama, nia, ufahamu, ukumbusho, kujijua mwenyewe, ambazo ndiyo hisia za ndani. Kama vile mtumiaji wa upanga anatiwa adabu ya kuua lakini si upanga, pia roho inahukumiwa kupata raha na maumivu kwa sababu hiyo ndiyo inayotenda vitendo vizuri na viovu kwa kuutumia mwili, hisia, hisia za ndani na nguvu zilizo muhimu. Roho si shahidi tu wa vitendo vizuri na viovu lakini ni mfanyaji wa hayo yote na inaadhibika kwa matendo yake. Mungu mmoja ni shahidi wa pekee wa vitendo vyetu. Lakini roho inayofanya vitendo hivyo, hupata adhabu yake. Yeye si Mungu, ambaye yeye ni shahidi wa mambo.

**Roho: Marudishio Ya Mungu.**

Q. Roho ni marudishio ya Mwenyezi Mungu. Marudishio katika kioo haiwezi kuumia kioo kinapovunjika. Kwa njia hii hii, roho kuwa ni mrudishio wa Mwenyezi Mungu inayoonyeshwa katika hisia ya ndani hustahmili kuwa hali ya kati, hisia ya ndani inakuwapo. Hapo inapoangamia, roho inapata kuwa huru au hupata uokovu.

A. Ni maneno ya kitoto. Kwa sababu, kitu kinaonekana katika ukatikati wa kitu; kama, uso wa mtu na kioo vyote ni vitu, ambavyo vipo mbali mbali. Ingekuwa havipo mbali mbali, basi kimoja kisingeweza kuonekana katika chengine. Lakini Mwenyezi Mungu si kama kitu cho chote na hana umbo kuwa ameenea kote. Yeye hawezi kuonekana katika kitu kimoja.

Q. Wewe huoni kuwa mbingu iliyoenea kote na isiyo na umbo inaonekana katika maji mengi yaliyo shuari? Kwa njia hii hii, Roho Takatifu anaonekana katika hisia ya ndani iliyo safi. Mwonekano huu unaitwa 'chidabhasa' - picha au mwonekano wa akili.

A. Ni mapayuko ya upuuzi ya mtu aliyekuwa na akili ya kitoto. Kwa sababu mbingu si kama haionekani, vipi itaonekana kwa macho na mtu ye yote?

Q. Kwani mbingu haionekani kama kuba la kiza na buluu juu ya vichwa vyetu?

A. La, Haionekani hivyo.

Q. Basi, ni nini?

A. Ni hewa, kuwa ni vipande vya ardhi, maji na moto vinaonekana vikielea mbali mbali. Rangi ya kibuluu inatokana kuzidi kwa maji ya mvua katika hewa, ambayo yanaifanya vumbi, kuelea kutoka kwenye dunia, kuonekana kuwa buluu na yenye kiza. Hii ndiyo inaonekana katika maji au kioo. Lakini mbingu hasa haionekani, au kuonyesha katika kitu.

Q. Haya, mazoezi ya maisha ya kila siku sisi tunapo pahali tulipopafunga katika gudulia, nyumba ya watawa au ni katika mawingu au kuenea kote. Kwa njia hii hii, Mwenyezi Mungu aneitwa Mungu na roho kutokana na sifa ya kinachozunguka (upadhi), kwa jina ni ulimwengu na hisia ya ndani. Gudulia, nyumba ya watawa na mawingu yanapoangamia, pia vile vilivyo vizunguka hivi vinaitwa mbingu kuu.

A. Maneno haya pia ni kama yale watu wajinga. Kwa sababu, mbingu katu haivunjiki kuwa vipande vipande. Katika mazoezi, sisi tunasema niletee gudulia na mengineyo. Hivyo haya si ya kweli.

**Sehemu Ya Mwangaza Wa Mungu.**

Q. Hisia zote za ndani zinaelea katika chidakasha ya Mwenyezi Mungu au mwangaza uliofungiwa katika akili ya binadamu, kama vile samaki na vinyama vyengine vya maji vinaishi katika maji, na ndege na wanyama wengine kama hawa huruka katika mbingu. Wao wenyewe hawana uzima, lakini wanafanywa kuwa na uhai kwa nguvu zilizoenea kote za Mwenyezi Mungu kama kipande cha chuma kinavyo pata moto kwa moto. Hivi vinakwenda, lakini mbingu na Mungu hawendi. Hivyo hakuna makosa au ubaya katika kuamini roho kuwa ni Mwenyezi Mungu.

A. Habari hizi zako, pia, si za kweli, kwa sababu, ikiwa Mwenyezi Mungu aliyeenea kote awe roho ili aweze kujimurika katika hisia za ndani, kwani Yeye

ndiye au siye mwenye nguvu zote na sifa nyinginezo zisizo na mwisho? Ikiwa wewe utasema kuwa Yeye hana kutokana na Yeye kuweza (kuonekana) au kuwekwa kuwa na mwisho, basi sema ikiwa Mungu anao mwasho na amegawanyika, au ikiwa yeye anaweza kuonekana. Ikiwa wewe utasema kuwa Yeye haonekani basi hapana kioo kinachoweza kumwonyesha Yeye Ikiwa hapana kioo au mwisho wake Yeye, vipi Yeye ataweza kuwa mjuzi wa yote? Ikiwa wewe utasema kuwa Yeye anajisahau Mwenyewe inaonyesha anakwenda pamoja na hisia za ndani, kama ilivyo, lakini si hivyo si hivyo kwa uwezo Wake Mwenyewe, tena hapo Yeye Mwenyewe haendi, sehemu hiyo Yake ambayo imeachiliwa huru kutokana na hisia ya ndani, itakuwa ya nguvu zote, takatifu, na dhahiri; na sehemu ile iliyokaliwa na hisia ya ndani, iliangukia kwenye uwongo. yenye mwisho na ujinga. Hivyo Mwenyezi Mungu mzima atafanywa awe patupu na hisia ya ndani. Kuwa ni matokeo ya kawaida, mwunganisho wa roho na mwili na uhuru wake kutoka hapo utakuwa wa mara moja. Ikiwa hayo unayo yasema wewe ni ya kweli, hapana roho itakayo kumbuka yana yoonekana au kusikika: hivyo, Brahman huyo hayupo ambaye aliona au alisikia. Hata hivyo Brahman na roho haziko namna moja. Wao ni vitu mbali mbali.

**Dunia ni Adhyaropa au Dhana.**

Yote haya ni mfano wa adhyaropa, i.e. kuchukulia kitu kimoja kwa chengine. Kuamrisha na mtungo wa elimu yetu, dunia nzima na mambo yake inatakiwa kuwepo katika Brahman (Mwenyezi Mungu). Kusema sawa sawa.

Q. Nani ni mwandishi wa adhyaropa au mdhaniyaji?

A. Roho

Q. Nini roho?

A. Roho ni akili iliyowekwa na hisia ya ndani

Q. Kwani akili iliyonamwisho iliyowekwa na hisia ya ndani ni tafauti na kitu chenyewe hasa na Mwenyezi Mungu, au ni huyu huyu Mwenyezi Mungu?

A. Ni huyu huyu Mwenyezi Mungu.

Q. Ni Mwenyezi Mungu ambaye ameamrisha kuwepo kwa dunia katika Yeye mwenyewe kwa kupotewa akili?

A. Wacha iwe hivyo. Kwani kuna dhara ipi kwa Mwenyezi Mungu kutokana na haya?

Q. Kwani mtu yule ni mwongo ambaye anafanya dhana ya uwongo?

A. La; kwa sababu, kile kinacho dhaniwa au kuelezwa kwa nia au maneno, ni yote ya uwongo.

Q. Hivyo, kwani Mwenyezi Mungu si wa kudhaniwa na mwandishi wa uwongo kwa kufanya dhana Zake au kutoa habari kwa nia au kwa kusema?

A. Wacha iwe inayokuwa. Inasaidia kuthibitisha mambo yetu.

Heko, Vedantins wa uwongo! Nyinyi mnahakikisha kuwa Mungu, ambaye ni ukweli wa hakika, mapenzi ya kweli, fikra takatifu au nia, kuwa ni mnafiki na mwandishi wa uwongo! Kwani si ni sababu za hali zenu za dhiki? Nini Upanishat, mithali, au Veda inasomesha kuwa nia ya Mungu ni ya uwongo na Maamrisho Yake ni ya Uwongo? Uthibitisho wako unahakikisha mithali: i.e. mwizi anamtia adabu afisa wa polisi. Sababu ya kawaida ni kuwa afisa wa polisi anamtia adabu mwizi. Lakini ni kinyume cha mazoezi yote kuwa mwizi anamtia adabu afisa wa polisi. Kwa njia hii, kuamini kwako ni uwongo na mithali zako si za kweli, wewe unakata ila zako za kufahamu kwa Mwenyezi Mungu si kwaajili ya kitu cho chote. Ikiwa elimu yake Mwenyezi Mungu ni ya uwongo, Maneno Yake ni ya uwongo. Vitendo vyake pia ni vya uwongo; Yeye atakuwapo sana kila pahala. Kwa sababu, Yeye yuko kila pahali sawa sawa. Yeye daima ni mkweli dhahiri; wa fikra za kweli, wa maneno ya kweli, na wa kitendo cha kweli. Ila za hapa juu ni zako, lakini si za Mwenyezi Mungu. Kile wewe unachokiita kuwa ni elimu, lakini ni ujinga. Adhyaropa yako au utabiri wako wenye makosa au kuchukua kitu kimoja kwa ajili ya chengine pia ni uwongo. Nini zaidi, ikiwa si kipande cha wongo safi na rahisi kujifikiria mtu kuwa Mwenyezi Mungu bila ya kuwa hivyo kwa makusudio na nia zote, na kumfikiria Mwenyezi Mungu kuwa ni roho? Mungu ambaye ameenea kote, katu hawi na ukomo au kutengenezwa, mjinga, na kukomeshwa kwenye mwili, kwa sababu, ni tabia nafsi kuwa mjinga, kuwa na mwisho, kuwekwa pahali pake kuwa si muhimu, na yenye ujuzi mdogo. Lakini si hivyo ni Mwenyezi Mungu.

**Uokovu na Kutwaa Utu.**

Q. Nini uokovu?

A. Ni moja ambamo uhuru unapatikana.

Q. Uhuru unatakiwa kutokana na nini?

A. Roho hutaka kuwa huru na nini.

Q. Kutoka nini wao wanataka kuwa huru?

A. Kutoka yale wao wanajaribu kuyaepuka zaidi.

Q. Kitu gani wao wanajaribu kukiepuka?

A. Maumivu au huzuni.

Q. Wao hupata kitu gani baada ya kupata uhuru kutokana na maumivu, na wao huishi wapi?

A. Wao hupata furaha na kuishi katika Mungu.

Q. Nini njia za uokovu na nini huleta utu?

**Njia za Uokovu.**

A. Nazo ni: kuyatii maamrisho ya Mungu; uhuru wa kutokuwa na dini (upungufu), ujinga, marafiki wabaya, fikra ovu au uhusiano, na uchu usio sawa au wa bila ya kiasi katika raha mbaya, ukweli, ukarimu, elimu, haki bila ya mapendeleo, kujitolea kwa sababu ya uadilifu au dini, kumkumbuka Mungu, kumsalia Yeye, kumwabudu Yeye au kutafakari, katika njia hizi zote zilizotajwa hapa juu, kujipatia elimu, kuifundisha, kazi ya kuaminika, kuiendeleza elimu, kuwa na njia za uadilifu katika mambo, kufanya kila kitu bila ya kupendelea upande wo wote, usawa na uadilifu; kama haya na mengineyo ambayo yanakuongoza kwenye uokovu; na kazi za kinyume na haya kama kuvunja sheria za maamrisho ya Mungu, na vipindi vyengine kama hivi humfanya binadamu kupata taabu ya kutoweza kuupata utu.

Q. Kwani roho inamezeka katika Mungu katika hali ya uokovu, au inabaki kuwa kamili au inajiweka peke yake?

A. Inajiweka peke yake.

Q. Inaishi wapi?

A. Inaishi katika Mungu.

Q. Mungu (Brahman) yuko wapi? Kwani roho iliyookoka inaishi katika pahali maalum, au inakwenda kila pahali ipendapo kwa uhuru wake?

A. Roho iliyookoka inazunguka kwa uhuru bila ya kizuizi katika Mungu ambaye ameenea kote, na elimu yake na furaha iliyokamilika.

**Asili Ya Roho.**

Q. Roho iliyookoka ina mwili?

A. La.

Q. Vipi basi itahisi furaha na kufurahia raha?

A. Inakuwa na sifa zake halisi zote na nguvu, kama vile kufikiri vyema na kama haya, lakini iko huru na mwungano na kiwili wili. Hivyo, kwa mfano Shatapatha inasema, Kand 14.

Kiwili wili au viungo vya hisia havifuatani na roho katika hali ya uokovu; lakini inakuwa na sifa zake muhimu na safi. Kwa maneno yaliyo ya rahisi, roho katika uokovu inageuka, kwa sifa za nguvu zake, kuwa shikio ili kusikia, ngozi kugusa,, jicho kuona, ulimi kuonja, pua kunusa, nia kutaka au kuwaza, akili kujulia, ukumbusho kukumbukia, na akili kujijua mwenyewe. Mwili wake ni mzuri kabisa unategemea nguvu za kutaka mwenyewe. Kama roho inafanya kazi zake muenyewe katika dunia kwaajili ya viungo vyake vyenye hisia, roho pia inafurahia furaha za kila namna za nguvu zake katika hali nzuri.

**Sifa za Roho.**

Q. Namna ngapi na nguvu zipi inazo?

A. Nguvu yake ni zaidi ya namna moja.

Lakini kuichambua hiyo, imejaliwa na nguvu za namna 24, kwa majina 1. nguvu 2. ushujaa 3. mvutio 4. hisia 5. harakati 6. hofu 7. ubaguzi 8. kitendo 9. ujasiri 10. mkumbuko 11. imani 12. matakwa 13. mapenzi 14. chuki 15. uhusiano 16. mtengano 17. umbo 18. uangamizi 19. kusikia 20. kugusa, 21. kuona 22. kuonja 23. kunusa 24. kujua. Juu ya haya ndiyo inapata furaha na raha katika uokovu wake. Ingekuwa imemezwa au kuangamizwa katika uokovu, nani angeifurahia raha yake? Wao ni wajinga sana wanaoutazamia uangamizi wake kuwa kama ni uokovu. Kwa sababu, uokovu wa roho ni kuishi kwa raha katika aliyeenea kote asiye na mwisho, na Mungu mtakatifu kuliko wote baada ya kupata uhuru kutokana na dhiki. Vide Shariraka mithali ya Vedant, IV. IV.

**Roho Haimezwi.**

10. Badari, baba wa Vyasa, anaamini kuwepo kwa roho na nia yake katika hali ya uokovu; haya ni kusema, Parasrha ambaye anaitwa Badari anafikiria kuwa roho na nia yake haitazamishwa katika Mwenyezi Mungu au kuangamizwa.

11. Pia Jaimini acharya (profesa) anaamini kuwepo kwa mwili mwerevu wa mtu aliyeokoka ni kama ule wa nia, wa hisia, wa nguvu za kuvuta puumzi na sifa nyinginezo.Yeye anauletea kuto kuwapo kwao.

12. Mwana falsafa Vyasa ni wa kote kuwepo na kutokuwepo katika uokovu, haya ni kusema, roho inayo nguvu yake iliyo safi na isiyotengenezwa; sifa zake ambazo si safi, tabia ya kuwa na dhambi, kuweza kupata maumivu na shauke ovu zinaiangamiza kabisa.

**Upanishats kuhusu Uokovu.**

Ni Ubeti kutoka Katha Upanishat, 11. vi 10. hali ambayo nia inatakasika na kusaidiwa na hisia tano za kutilia mkazo za kushikana na nafsi, na ambapo akili inaimarika na imani, inaitwa hali ya juu kabisa ya uokovu. Inasema Chhandogya.

1. Mtafute Mungu na taka kumjua Yeye ambaye yuko huru kutokana na aibu za dhambi, uzee, kifo, huzuni, njaa, kiu; ambaye nia yake ni ya kweli, fikra zake ni za kweli; kumtegemea yeye ambaye anawasaidia kuwa ni matakwa yaliyookolewa, ambaye anajua vipi kuchagua na kuyatimiza yote ya uokovu na usafi wa mtu. 2. Roho ifiyookolewa inajifurahisha kwa kuviona vitu kwa macho ya mbinguni na kuyapata haya kwa intidhamu ya akili safi Roho iliyookolewa iliyozamishwa katika Mwenyezi Mungu, huonja furaha ya uokovu. Wataalamu baada ya kupata uokovu, hutafakari kwa Mwenyezi Mungu, ndani na mwangaza wa yote. Kwa sababu hii wao wanazifikia dunia zote na matakwa

wanayotaka, wao hupata mpaka watosheke. Roho zilozookolewa, kusitikisa uzi usiona uhai, huishi katika uhuru kamili katika pepo katika Mwenyezi Mungu katika mwili mtakatifu uliotengenezwa kwa nia. Kwa sababu roho zilizofungwa katika viwili wili haziwezi kuwa huru kutokana na maumivu ya dunia. 3. Kama mila ilivyo kuwa hapo zamani za kale Prajapati alisema kumwambia Indra: Ee mtu tajiri na unayestahiwa, mwili huu mzito ni kwa kawaida utapatwa na kifo Ipo, kama ilivyokuwapo, katika mdomo wa kifo kama mbuzi katika mdomo wa simba. Mwili huu ni nyumba ya roho isiyo na mwili wala kifo, nani, hivyo, daima amezongwa katika raha na maumivu; kwa sababu, raha za dunia za roho iliyomo katika kiwili wili inatosheka katika hali hiyo; lakini furaha na maumivu ya dunia haziitahiri roho isiyo na mwili iliyo ukoka, ambayo inaishi katika Mwenyezi Mungu, na ye yote anaye furahia raha.

**Kurudi kutoka Kwenye Uokovu.**

Q. Jee roho mara moja zikishapata uokovu, zitaonja tena kikombe kichungu cha uhai usio dumu juu ya dunia? Kwa sababu, satwa kama hizi; Chh. Pr. 8, Kh. 15., Vedant, IV, iv, 33, na Gita:-

Gita. inaonyesha kuwa uokovu ni kitu ambacho hakiwezi kurudi tena kwenye dunia ya vitu.

A. Uhakikisho huu si kweli, kwa sababu inapingwa kajtika Vedas. Rig. 1.24. Sank - I - 159.

Inaulizwa: Jina la nani si tuliheshimu kuwa tukufu? Mungu yupi anaye ngaa miongoni mwa wasiokufa anayetu maisha tena katika dunia hii baada ya raha yetu ya furaha ya uokovu, na kutupatia nafasi ya kuwaona baba na mama? Kwa haya inajibiwa: Sisi tumheshimu yule ambaye ni wa milele, mtakatifu wa daima na mwenye furaha jina lake ndiyo liwe takatifu, yeye ambaye anatupatia sisi furaha ya peponi, pia anatupa maisha duniani kutokana na wazazi, na anatufanya tuone nyuso za baba na mama. Mwenyezi Mungu ndiye anayeuongoza uokovu na ni Bwana wa viumbe vyote.

Roho za duniani na za mbinguni daima zilikuwapo kama zilivyo hivi sasa. Maisha ya duniani na ya peponi katu hayaangamiziki, kwa maneno yaliyo rahisi, maisha ya mwili na uokovu si ya milele.

Q. Aangamizi wa maumivu unaitwa uokovu ambawo una kuwa wa milele; kwa sababu, unatokea unapojigomboa kutokana na maisha ya kuwapo na uovu na unapojitoa katika dhambi za kuzaliwa na maumivu, elimu ya uwongo na ujinga, tamaa ya mali na vyenginevyo, mazoezi ya uasherati na raha mbaya, maisha ya dunia na dhiki usizoweza kuziepuka. Nyaya. 1. 2.

A. Si lazima kuwa neno "atyanta" (kupita kiasi) lile maana ya kuwa ni uangamizi kamili. Hivyo, kwa mfano, Mtu huyu anaumwa na maumivu "makali" ua unafurahia "raha bila ya kiasi". Inaonyesha kuwa mtu anapata raha nyingi na maumivu. Kwa njia hii hii, neno atyanta (kupitia kiasi) lina maana moja katika kipande kilichopo hapa kutoka katika falsafa ya Nyaya.

**Urefu wa Uokovu.**

Q. Ikiwa roho itarudi kwenye maisha ya mwili kutoka kwenye uokovu, muda gani itaweza kuishi katika hali ile ya furaha?

Mundak III, II, 6. Roho zilizookolewa, baada ya kupata uokovu na kupata raha katika Mwenyezi Mungu kwa muda wa Mahakalpa, huiawacha pepo kwaajili ya dunia. Wakati wa muda huu mrefu wa Mahakalpa unahesabiwa: 43, 20,000 miaka huufanya kuwa ni mzunguko sehemu nne za umri, unaoitwa chatur yuga katika Sanskrit; Viz Sat Yuga, 1728, 000, Treta Yuga 1296,000; Dwapara Yuga 864,000, Kali yuga 432,000. Tena umri huu mara nne au mzunguko kama huu huufanya kuwa ni usiku na mchana mmoja: ahoratra, siku 30 kama hizo hufanya mwezi mmoja, miezi 12. kama hiyo huufanya mwaka mmoja, miaka 100 kama hiyo hufanya Mahakalpa moja au Pranta kalpa au ni kipindi kirefu cha wakati. Sasa, ihisabu nambari ya miaka kwa kujumlisha. Huo ni muda wa furaha katika uokovu.

Q. Watu wote wa kawaida na waandishi wa maandishi matakatifu kwa pamoja wanaamini kuwa huwezi kurudi kupata maisha kutoka kifo kutokana na uokovu.

A. Haya hayawezi kuwa; kwa sababu, nguvu za roho kama hizo, kama mwili na vitu vyenginevyo, vina mwisho. Vipi matokeo ya kazi zao ziwe hazina mwisho? Roho hazina nguvu zinazoweza kwisha, zinaweza kufanya vitendo visivyo na mwisho, zinaweza kuchagua sababu zisizo na mwisho kuhakikisha raha ya furaha isiyo ya mwisho. Hivyo wao hawawezi kufurahia furaha isiyo na mipaka. Isiyo ya daima maana yake ni kuwa haina mwisho au mwisho wa milele. Ikiwa roho hazirudi tena kwenye dunia kutokana na hali ya uokovu, mambo ya maisha ya uchu yataangamia kabisa hapa duniani.

**Roho Kuumbwa Tena.**

Q. Mungu huzirudisha tena roho zilizo okoka pamoja na roho zilizoumbwa upya kwenye ardhi. Hivyo hazi wezi kwisha.

A. Ikiwa hivyo ni kweli itaifanya roho kuwa si ya daima au si ya kudumu: kwa sababu, kile kina choumbwa, kina hakika kuwa kitaangamia. Kwa hivyo, roho itaangamia baada ya kupata uokovu kwa mujibu wa itikadi Yako. Itaifanya uokovu kuwa si wa daima; na pahali pa uokovu utajaa bila ya kiasi, kwa sababu watakuwa wapo wanaofika lakini hapana atakaye kuondoka, hivyo hapata kuwa na mwisho wingi au uzidisho wa kila mmoja. Hapata kuwa na raha lakini uovu usio na shaka. Itakuwa kama sukari isiyo na uchungu. Ikiwa hakuna kichungu, vipi sisi tutajua kitamu? Kwa sababu mfarakano wa ladha tafauti hutufanya tubague zote mbili. Mtu ambaye hali na hanywi kitu ila vitamu na vyenye ladha, hawezi kusikia utamu zaidi na raha kama yule ambaye huonja vitu vyote vyenye ladha na vizuri. Ikiwa Mungu anatunukia vitendo vyenye mwisho pamoja na matokeo yenye mwisho, haki Yake na usawa utapeperushwa na upepo. Ni alama ya busara kumtwika mnyama mzigo ambawo ataweza kuunyanyua. Mtu hulaumiwa anaye mtwika mwenzake ratili 800 ikiwa mwenzake anaweza kunyanyua ratili 80 tu. Kwa hivyo, si sawa kuwa Mungu amutie mtu furaha isiyo na mwisho yeye ambaye ana ujuzi na nguvu kidogo. Ikiwa Mungu anaumba roho

mwisho yeye ambaye ana ujuzi na nguvu kidogo. Ikiwa Mungu anaumba roho mpya, kitu kutokana na anachoumbia, kita kwisha: kwa sababu hata mali iwe nyingi vipi, basi ita kwisha tu ikiwa sasa au baadaye; hivyo, ikiwa hapana kitu kitacho kuwapo, lakini zitakuwa ni picha tu bila ya kitu kilochotiwa humo. Hivyo, inaonyesha kuwa ni kweli utawala wa kweli ambawo roho unapana kwa uokovu na pia kurudia hapo tena. Kuna mtu anyependelea zaidi maisha yote ya gerezani au adabu ya mwilini kuliko kufanywa kwa muda tu? Ikiwa hakuna kurudi kutoka kwenye uokovu, basi ni kama kufungwa maisha. lakini ni kuwa mtu hatakuwa na dharura ya kufanya kazi kupata mkate huko. Kunyonywa kwa roho katika Mwenyezi Mungu, ni kama kifo cha kuzama baharini.

Q. Roho itahifadhiwa milele na itaishi kwa raha na furaha Mungu anahifadhiwa milele na mwenye furaha ya kukamilika. Katika maneno haya hamna ila.

A. Mungu hana mwisho katika kuwepo na nguvu, na wa sifa zisizo na mwisho za tabia na asili. Hivyo Yeye hawezi kuangukia ujinga na mzunguko wa maumivu. Lakini roho hata inapokuwa imeokolewa, si yenye utakatifu na busara ya kukamilika, na isiyo na nguvu za milele, tabia na asili. Roho si kama Mungu na si sawa na Yeye.

Q. Ikiwa ni hivyo, uokovu ni kama maisha na kifo. Hivyo, haina maana kuijaribu.

A. Uokovu si kama uhai na kifo, kwa sababu, kwani ni kitu kidogo kuwa uwe huna dhiki na kuishi katika furaha ya uokovu mpaka dunia iumbwe na kuangamizwa mara 36,000? Kwa nini wewe unajihangaisha kupata mkate, unapajiona kuwa unakuwa na njaa siku moja baada ya kula chakula? Kwa nini mtu asijikere kuupata uokovu, ambapo inahesabikana kuwa ni lazima kujaribu kuponyesha njaa na kiu; kwa kupata utajiri mdogo, utawala na heshima; kwa hivyo kuileta ndoa na kupata watoto, na mambo mengine kama haya ya sababu za dunia? Ijapokuwa kifo ni cha hakika, hata hivyo uhangaisho hufanywa ili kuwepo. Kwa njia hii, ijapokuwa roho hurudi duniani kutokana na uokovu, hata hivyo hapana njia ila lazima kujaribu kuipata.

**Njia za Uokovu.**

Q. Njia gani ni za kupata uokovu?

A. Njia au sababu baadhi yao zimeelezwa hapa juu. Lakini njia hasa ziliyo ni kama hizi:-

1. (a) Yeye ambaye anautamani uokovu, lazima ajaribu kuokolewa katika wakati wake wa uhai, haya ni kusema, uwache uwongo na chuki nyinginezo, ambayo matokeo yake ni huzuni na majonzi, na ujifunze kumcha Mungu, uadilifu, na sifa nyinginezo, ambazo matokeo yake ni raha na starehe. Hivyo, ni kanuni kuwa yeye ambaye anataka kuwa mbali na maumivu na kufurahia raha, lazima aruke kutoka kwenye uovu na kufanya yale ya uadilifu na ucha Mungu.

Mzizi wa huzuni ni maisha ya uovu, sababu ya raha na furaha ni kufuata maisha ya uadilifu.

(b) Mtaka uokovu lazima azifuate sheria za kazi ambazo zinataka kufanywa na vitendo vitolewe, na kujifunza kutafautisha sifa nzuri na mbaya, ukweli na uwongo, sawa sawa na kuwa na marafiki wazuri.

(c) Elimu ya mafundisho matano ya maisha, zinazoitwa, panch kosh, ambazo zina kuwepo kwa binadamu, lazima zipatikane. Mipango 5 au mifuniko ni (1) Anna maya kosh: viungu vya chakula (mwili wa binadamu) wenye ngozi na nyama, mifupa, mishipa, mishipa ya damu, damu, shahawa, vyote vilivyo tengenezwa na udongo na vitu vya maji maji; (6) Pranamaya kosh: utaratibu muhimu (umbo la puumzi), lenye prana: kutoa puumzi; apana; kuvuta puumzi, samama: mpango wa kusaga chakula ambawo huanza kutoka kwenye kitovu na kugawanyika, arki mbali mbali za chakula kwendea kwenye sehemu mbali mbali za mwili, udana: kitendo muhimu ambacho kinapitisha chakula na kinywaji chini ya shingo na kuleta nguvu na bashasha, vyana: nguvu ambazo zinaisaidia nafsi kutulia pia kazi za mwili kutumika na kutenda mengine: (3) Manolmaya kosh: utaratibu wa kinyama uliona nia, hisia na hisia tano zilizo changamka; i.e., kusema au sauti, miguu, mikono, viungo vinavyo usafisha mwili, viungo vya kuzalia, nguvu zao, kwa majina, tamko, mwendo, nguvu za kushika, kunya na kukojoa, kuzaa; (4) Vijnanamaya kosh: utaratibu wa kitaalamu, wenye akili, mkumbuko, na aina tano za hisia, i.e shikio, ngozi, macho, ulimi na pua, nguvu za kuskikia, kuhisi au kugusa, kuona, kuonja, na kunusa; ambazo ni sababu za roho kupata elimu; (5) Ananda maya kosh: Utaratibu wa dini unadhihirisha mapenzi, bashasha, daraja ya uwingi au uhaba wa raha, furaha, na vitu kama gari. Kutokana na utaratibu huu wa namna tano, roho hufanya vitendo vyake, ibada na kujipatia elimu.

Kuna hali tatu: (1) jagrita: hali ya kuamka, (2) swapna: hali ya kuota, (3) sushupti: hali ya kukoroma ya akili. (Hizi lazima zisomwe ili jijua mwenye kutoka si mwenyewe)

(b) Kuna namna tatu ya miili: (1) Sthoola: Unaoonekana, kiwili wili. (2) Sooshma: isiyoonekana, mwili wa kitu uliyotengenezwa kwa mwunganisho wa vitu 17, viz, prana tano- namna ya uhai uliotajwa hapo juu, prana indriya tano: hisia za kutia nguvu, sooshma bhoota tano: vitu au asili ya vitu, mana: nia, na buddhi: akili: Mwili huu wa kitu unafuatana na roho katika muda kutoka kuzaliwa mpaka kufa. Ni wa namna mbili, viz., (i) bhoutik mwili au kiwili wili, ambawo ni sehemu za vitu; (ii) sabhavik: mwili wa tabia, uliokuwa na sifa za kuzaliwa nazo za roho. Namna hii ya pili ya mwili hufuatana na roho katika uokovu ambapo hufurahi kwaajili yake. (3) 'karana' au mwili wa kiwili wili, ambawo unapatikana katika hali ya usingizi - usingizi bila ya ndoto. Kuwa ni kitu katika tabia, iko kila pahali na ni ya namna moja kwa roho zote. (4) Turiya: miwili au hali juu ya kiroho ni ile ambamo roho inanyweka katika raha kwa kuweza kumtambua Mungu katika hali ya usingizi. Nguvu za hali hii safi ya kiroho inayopatikana katika usingizi ni msaada dhahiri kwa roho katika uokovu.

Wacha ifahamike akilini kuwa roho inatambulikana kutokana na taratibu hizi zote, hali na miili; kwa sababu inajulikana na watu wote dhahiri kuwa wakati wa kufa wa mtu ni ule ambapo roho imewacha mwili. Roho hii ni mwanzishi wa hali zote na miili, nguvu za wao wote, shahidi wao, mfanyaji wao, na mfurahiaji wao au mtumizi. Ni wajinga na wasiojua kitu ndio wanaosema kuwa roho si mfanyaji na mrahiaji wao; hivyo, wao ni hawana mwili na ni mfu bila ya kuwepo kwake roho. Wao hawawezi kuona raha na maumivu, wala wao si shahidi wa vitendo vya uadilifu na chuki. Lakini roho inatenda na kuhisi raha na maumivu kutokana na viungo vyake. Hisia zainapokuwa zimekaliwa na vitu vyao, zitaungana na hisia akili huangukia pamoja na nia ilikuleta machofu ya mwili kwa kitendo cho chote cha uwema au uovu: fikra za akili hapo tena zinainama juu ya vitu vya nje. Katika hali ya jambo inazaliwa akili raha, ushujaa, kutokuwa na hofu, woga wa vitendo viovu, shaka na aibu. Ni sauti ya Mungu inayokaa katika sisi. Yeye ambaye anaitii sauti hii na vitendo kwa mujibu wa uongozi, hupata furaha ya uokovu. Lakini yeye ambaye anakwenda kinyume chake, hupata adhabu ya huzuni matokeo juu ya maisha ya kiwili wili kilichopo.

II. Njia ya pili ya uokovu ni Viveka: hukumu au ubainisho. Ni kujua ukweli na uwongo baada ya ubaguzi ulio wa kweli na tena kuchagua vitendo vya uadilifu na kukataa vya uovu. Inaitwa hukumu ya kweli. Iko na elimu ya kweli ya viumbe vyote kutoka duniani mpaka kwa Mungu kama ni tabia zao, tabia na kitendo au nguvu; na tena ni utiifu wa maamrisho ya Mungu, kuifanya akili imwabudu Mungu, zisiwepo tabia zilizo kinyume na maamrisho Yake, na matumizi sahihi ya dunia.

III. Njia ya tatu ya uokovu ni shat sampatti au sifa sita. Ni kufanya namna sita za vitendo: (1) Shama: Kuuziwia akili na hisia za ndani kutokana na ghasia za kupigana na daima kuitumia kwenye uadilifu. (2) Dama: kuziondoa hisia na mwili kutokana na uchu baada ya vitendo viovu kama kuzini na maasi mengine, na kuifanya nafsi na hisia zitawale katika kazi za uadilifu. (3). Uparati: kutojali, kwake daima hutuweka mbali na maasi, na watu kufanya vitendo viovu. (4) Titiksha: ustahmilivu, uvumilivu, na daima kujitahidi kuupata uokovu baada ya kuiwacha raha na shida kutokana na sifa nyingi na masengenyo, faida na hasara kwa kiwango cho chote. (5) Shraddha: Imani madhbuti katika mafunzo ya watu mashuhuri wanaojulikana sana kwa ukweli wao, mafunzo, na utakatifu. (6) Samadhana: Utulivu wa akili. Zote daraja hizi sita hutengeneza njia za uokovu.

IV. Mumukshutwa: hamu kuu ya uokovu i.e. si mapenzi ya kitu cho chote ila ya uokovu na njia zake za kuupata, kama vile wenye njaa na kiu hawafikiri kitu ila chakula na kinywaji.

Hizi ni njia nne za uokovu, na kuna njia nne ndogo ambazo zinaitwa, anubandha. Mtu aliye na sifa hizi ni mtetezi wa uokovu au adhikari.

**Njia Ndogo.**

Annubandhas au sifa ndogo kwaajili ya uokovu ni nne kwa hesabu, viz., (I) Adhikari: mtu aliye na sifa ya uhodari katika njia nne za uokovu zilizosemwa. (2) Sambandha: ujuzi uliokuwa sahihi unaopatikana, i.e, uokovu, ambawo unamtambua Mungu; na njia za kupata, i.e elimu ya Vedas na maandishi matakatifu, na kuifuata elimu hii. (3) Vishayi: mtu ambaye madhumuni ya masomo yake ni kumjua Mungu, ambayo ni nanga ya maandishi halisi (4) Prayojana kitu au sababu, au matakwa makubwa kwa ajili ya kupata furaha ya uokovu, ambayo ni summumbonum, baada ya ukombozi kamili kutokana na maumivu ya namna yote. Hizi dharura nyinginezo za ukamilifu wa akili au uokovu.

**Vitu Vyengine.**

Kuna vitu vyengine, vinavyoitwa shravana chatushtaya: daraja nne za njia za uokovu, ambazo lazima zifuatwe baada ya nyendo. Nazo ni· (1) Shravana: kusikiliza kwa makini na kwa uvumilivu mafunzo ya mtu aliye mtaalamu hasa. Uelekevu mwingi unahitajika kutumika kwenye elimu ya kiroho, ni maarifa makubwa sana ya elimu kuliko nyingine zote. (2) Manana: tafkira, kufikiri kwa hali ya kupumzika yale mtu aliyoyasikia, kuyauliza yale uliyo na shaka nayo, kumwuliza msemaji na msikilizaji kufikiri sawa, na kujipatia utulivu. (3) Nididhyasana: Majaribio na mtihani. Utilivu na tafkira zinapo ondoa shaka na kuthibitisha imani, kitu kinachoulizwa lazima kichunguliwe katika usingizi ili kuhakikisha ikiwa ni kweli yale yanayo semwa au fikiriwa juu yake, i.e. kuyaona haya kwa mambo yaliyopita (4) Sakshatkara: kutambua i.e. elimu ya kweli ya kitu kwa mujibu wa umbo lake, sifa, na tabia.

**Madokezo Ya Dhahiri.**

Wacha na daima epukana na hisia nyeusi (tamo gunas) i.e. uchungu, uchafu uzembe, dharau na sifa nyinginezo za chini; sifa za ukali (rajo gunas) i.e husda chuki, matakwa, kiburi, si sawa na ila nyingine.

Jichukulie sifa kama za ukweli, utulivu, utakatifu elimu, na kufikiria vizuri Pia, pendelea urafiki (maitri) na watu wenye furaha, waonee huruma (karuna watu wenye huzuni, waonyeshe huruma (muditia) kwa ukarimu; endelea kutojal (upeksha) i.e. si urafiki na waouvu, wala si uadui na wao.

Wanaoutafuta uokovu lazima watafakari kwa muda wa saa mbili kila siku ili nia na vitu vya ndani vyengine vingeweza kujulikana kabisa. Tazama hapa. Sis ni watu wenye akili na wenye uwezo wa kujua, na ni waonaji wa nia, kwa sababı sisi tunaiona nia sawa sawa hapo inapotulia, kuwa dhaifu, iliyofurahi au kutulia Kwa hivyo, sisi tunazijua hisia, puumzi na njia nyinginezo muhimu. Sisi tunayaikumbuka yaliyo kwisha pita na tunavitambua vitu vingi mara mmoja na wakati mmoja. Sisi ni wasimamizi na wazuwizi wa viungo na hata hivyo tuko dhahiri kutokana na wao wote. Ingekuwa sisi hatuko dhahiri kutokana na wao wote sisi tusingeweza kuwa mawakili wenye jukumu, watumizi, warakibishaj

mambo, na niwaendeshaji wa viungo vyote.

Yoga, II, 3. Za sababu tano za maumivu, zilizotajwa katika mithali hii, avidya: ujinga umeelezwa hapa juu. Asmita ni mbabaiko wa roho na mjuzi, ambawo ni nguvu dhahiri.

Raga ni mapenzi ya utulivu. Dwesha ni chuki na maumivu. Abhinivesha ni khofu ya maumivu ya kifo. Viumbe vyenye akili vinataka kuishi milele na hawataki kufa au kuuacha mwili.

Watu lazima waziepuke sababu hizi tano za maumivu kwa mazoezi ya falsafa ya vitu na kufurahia raha ya peponi kwa kumtambua Mwenyezi Mungu.

Q. Hapana anayeamini katika namna hiyo ya uokovu ambawo wewe unaeleza. Tazama Ma-Jain wanaamini katika uokovu wa jiwe ambapo aliyeokolewa hukalia kimyaa. Wakiristo wanaouokovu wao katika pepo ya nne ambako watu hufurahi kwa kuoa, kushinda, kuimba, kucheza ngoma na kuvaa nguo nzuri. Wafuasi wa Mohammed wanauweka katika pepo ya saba, Vamamargis katika Shripur, Shivites katika Kailasha, Vaishanavas katika Vaikuntha, Gosains wa Gokula katika Goloka ambapo watu huishi kwa raha katika baraka ya wanawake wazuri, chakula kitamu, vinywaji vya kuburudisha, mavazi mazuri, makaazi mazuri na raha za kuingiliana ki mwili. Wafuasi wa Puranas wanaamini katika uokovu wa namna nne, viz. (1) Salokya: makaazi karibu na Mungu, (2) Sanujya: kuishi na Mungu kama ndugu yake mdogo, (3) Sarupya: kuwa sawa na Mungu kwa umbo la kuabudu, (4) Samipya: kuishi na Mungu kama watumishi. Wanaoiamini Veda wanahesabu uokovu wa Sayujya: Mwungano na Mungu kuwa ni kujishughulisha katika ibada ya Mwenyezi Mungu.

A. Uokovu wa Kikiristo na wa Ki-Muhammad utaelezwa hasa katika sura ya 12, 13, na 14 ya kitabu hiki. Kuhusu, Vamamargis ambawo wanaamini kuwa wao wata wafurahia wanawake kama ni miungu ya kike ya mali, wataangamia kwa kula nyama na kunywa mvinyo, na kupitisha maisha katika kuimba na kustarehe; raha zao za peponi si bora zaidi kuliko zile za dunia? Kwa njia hii, raha za Shivites na Vaishnavas ambawo wanawaza kuwa wao watapewa maumbo kama ya Mahadeva na Vishnu na wataunganishwa na wanawake kama Parvati na Lakshmi kustarehekea maisha ya juu, tafautiana na wafalme wale walio tajiri katika nia zao hapatakuwa na magonjwa katika pepo na ujane utakuwa ni wa milele, tabaani ni upuuzi na ni muhali; kwa sababu magonjwa unafuatana na raha, na mwozo na uzee unatokana na ugonjwa. Wafuasi wa Puranas wanaweza kuambiwa, vidudu, funza, mbu, wanyama mwitu na wanyama wengine wanajipatia uokovu kwa njia za kitabiya kama ni yao za namna nne zilizotajwa hapa juu; kwa sababu, dunia zote hizi ni za Mungu na viumbe vyote wanaishi humo. Hivyo, uokovu kwa kuishi katika jimbo la Mungu unapatikana bila ya shida yo yote.

Uokovu kuwa utakriban kwa Mungu pia inapatikana kwa tabia, kwa sababu Mungu ilivyokuwa ameenea kote yuko karibu na viumbe vyote. Sanujya uokovu, ambapo mtu huwa ndugu mdogo wa kiume wa Mungu, upo mkononi mwa mtu

tokea hapo bila ya taabu, kama roho ambayo ni mtu, ni hafifu kuliko Mungu katika kila kitu, na kuwa mwenye akili ni jamaa wa Mungu. Sayujya uokovu kwa uungamisho ni pia ni wa tabia; au roho kuwa zimeenewa na Mungu zimeunganishwa na Yeye. Kuhusu uaminifu wa wasiomwamini Mungu, kuwa ni mrudisho wa kitu kwa kitu baada ya kifo, ni uokovu mkubwa kabisa, unaushinda kwa kusema kuwa unapatikana na mbwa, punda, na wanyama wengine wa daraja ya chini. Mipango hii si uokovu bali ni namna ya utumwa; kwa sababu, madhehebu haya mbali mbali huchukulia Shivapur, uokovu wa jiwe, pepo ya nne, pepo ya saba, Shripur, Kailasha, Vaikuntha, Goloke kuwa ni mwahala pa uokovu uliowekwa katika mahali maalum. Ikiwa wao wataondoka mahali hapo, wao wataupoteza uokovu wao. Watu waliookoka na kuwekwa mahali hapo ni kama wale waliofungwa mnamo utumwa wa manicipaa. Uokovu wa kweli unakuwa na uhuru kwenda po pote waliooka watapenda, wala hapatakuwa na pungamizi kwao, wala khofu ya namna yo yote, shaka, au maumivu. Kuzaliwa ni kuengezeka na mauti ni uangamizi. Waliookoka huzaliwa tena wakati mwingine kwa utu.

**Kuutwaa Utu.**

Q. Kwani kuna maisha ya mara moja (kuzaliwa) au kuna maisha ya mara nyingi ya roho?

A. Kuna maisha ya mara nyingi au kuzaliwa kwa roho.

Q. Ikiwa kuna maisha ya mara nyingi, kwa nini hakuna makumbusho ya kuwapo na ya kufa?

A. Elimu ya roho ni ya upungufu. Roho si mwonaji wa tabaka tatu za wakati, na hivyo haikumbuki matokeo yake ya maisha yaliyopita. Akili ambayo inajipatia elimu au ujuzi, haiwezi kujua masomo mawili wakati mmoja na umoja. Kuacha suali la makumbusho ya maisha yaliyopita, sisi hatuwezi kukumbuka mambo ya maisha haya ya sasa yaliyotokea miaka mitano iliyopita, au nini kilitokea tulipokuwa katika tumbo, mwili ulipokuwa unakua, au sisi tulipozaliwa. Kwa nini hakuna makumbusho wa vitendo vilivyotokea wakati wa kuwa katika hali ya kazi baina ya usingizi mkali, unaoitwa sushupti katika Sanskrit, ijapokuwa sisi kwa kweli tunafanya kazi zaidi ya moja katika kuamka na kuota? Wewe utasema nini ukiulizwa kama wewe ulifanya nini wakati wa dakika ya kwanza baada ya saa nne ya subuhi ile ile ya mwezi wa 5 wa mwaka wako wa kumi na 13, au katika miaka 12 iliyopita? Uso, mikono, mashikio na macho yako yalielekea upande gani? Kitu gani kilikuwa ndani ya akili yako? Kwa maswali yote haya wewe unajibu kwa kuyakataa. Wakati hali hii ya makumbusho ya sasa, huleta shaka ya uhakikisho wa matokeo ya yaliyokuwapo, ni kujifanya kama mtoto anavyotoa maneno mengi yasiyo ya maana. Usahau ni baraka, au mtu atakufa kwa maumivu ya kupita kiasi kwa kukumbuka dhiki zote zilizo kuwapo hapo zamani. Ikiwa mtu anajaribu kujua ya zamani na yatakayo kuja ya maisha, yeye hawezi kufanya hivyo; kwa sababu, elimu na nguvu za roho

hawizina uwezo wa kufanya hivyo. Haya yote yanaweza kujulikana na Mungu tu. Na si kazi za roho hata kidogo.

Q. Ilivyokuwa roho haijui tangu kuwepo kwake Mungu na Mungu anaipa adabu kwa dhambi zake za maisha yaliyopita, haiwezi kutengenezwa tena wala haiwezi kupata uwema kutokana na adhabu kwa ajili ya kutisha. Kwa sababu, ikiwa roho ina ujuzi wa kujua dhambi zake za zamani na pia ya matokeo yake, itaweza kuwa isifanye uovu tena.

A. Namna ngapi za elimu wewe unaimini kuwa zipi?

Q. Namna nane, zinazo itiwa pratyaksha na sheria kama hizi.

**Pasipo Usawa wa Hali.**

A. Basi kwanini wewe hufahamu kuwepo kwa roho za hapo kabla kwa kufuata sheria, mali, ufahamu, elimu, umaskini, uzembe, ujinga, na kama vile raha na maumivu wakati mbali mbali katika dunia kutokana na kuzaliwa mpaka kufa kwa watu? Kwa mfano daktari na mtu wa kawaida wawe wagonjwa. Daktari atajua sababu ya maradhi yake; lakini mtu wa kawaida hatajuwa sababu ya ugonjwa wake, kwa sababu yeye hajausomea udaktari. Hata hivyo, mtu wa kawaida atajua wakati wa kupata homa au maradhi mengine kuwa yeye lazima amekula chakula kibaya ambacho kimemletea shida hii. Kwa njia hii, kwa nini wewe hufahamu kuwepo kwa roho kutokana na uchunguzi wako wa kustaajabisha si wa usawa wa raha na maumivu katika dunia? Ikiwa wewe huamini katika kuwepo kwa zamani kwa roho, wewe lazima ukubali kuwa Mungu hajakamilika; hivyo, vipi yeye bila ya kufikiria haki yake na uadilifu huwapa watu umasikini na namna nyingine za dhiki bila ya wao kufanya dhambi katika maisha yaliyopita; au tawala, utajiri, na uzembe bila ya kufanya kazi nzuri katika maisha yaliyopita? Lakini haki ya Mungu inawekwa kwa watu wa baadaye kwa kuwapa raha au maumivu kwa mujibu wa sifa zao au sifa mbaya zao za kabla ya kuwapo kwao.

Q. Mungu anaweza kuwa mwenye haki ikiwa patakuwa na maisha moja tu ya roho kwa sababu, cho chote anachokifanya mfalme mwenye nguvu nyingi, ni haki. Tazama, mfanyaji kazi wa bustani anapanda miti mikubwa na midogo katika bustani yake. Yeye huikata mengine, huyangoa mwengine, huyalinda mengine na kuikuuza mengine. Mtu anaweza kufanya atakacho na vitu vyake mwenyewe. Hapana aliye juu Yake Yeye kukaa na kuhuku yale anayoyafanya Yeye, au kumtia adabu Yeye ambaye hamwogopi mtu ye yote.

A. Mungu hufanya yale yaliyo ya haki na katu hafanyi yasiyo ya haki. Kwaajili ya haya ndiyo Yeye anaabudiwa na yuko juu ya yote. Yeye si Mungu ambaye atenda kinyume cha sheria za haki. Kwa mfano, mfanya kazi wa bustani analaumiwa kwa kupanda miti njiani au katika pahali ambapo si sawa bila ya kufuata intidhamu, kwa kuikata miti hiyo, ambayo ilikuwa haitaki ikatwe, kwa kuipanda miti isiyo takiwa, na kwa kuikuuza iliyo sawa. Kwa njia hii hii, Mungu atalaumiwa kwa kufanya cho chote bila ya sababu. Ni lazima kwa Mungu

kufanya haki; kwa sababu, Yeye ni mtakatifu na mwenye haki kwa tabia. Ikiwa Yeye atatenda bila ya kufikiria Yeye atafedheheshwa na kuza chini kuliko mahakimu wa viumbe. Kwani mtu hapatwi na lawama na kupoteza heshima katika dunia hii, yeye ambaye anawaheshimu watu bila ya wao kufanya kazi nzuri, na kuwatia adabu wale ambawo hawaja fanya uovu? Ilivyokuwa Mungu avunji sheria za haki, Yeye hamuogopi mtu.

**Kabla Ya Mwisho**

Q. Mungu humpa mtu kile ambacho Yeye alikusudia kuumpa, na hufanya yale aliyokwisha kusudia kufanya.

A. Makusudio Yake na nia ni moja pamoja na vitendo vya roho, lakini si vyengine. Ikiwa vitafanywa bila ya kufikiria vitendo vyao, Yeye atafanya makosa na atakuwa si mwenye haki.

**Usawa Kwa Wote.**

Q. Watu wa tabaka la chini na juu wao wote hupata raha na maumivu yaliyo sawa. Watu wakubwa wana mashughuli makubwa, na watu wa kawaida wana fikra kidogo. Fikiria, kwa mfano, mfanyi kazi wa benki anayo kesi ya Rs. 100,1000 mahakamani. Yeye anakwenda huku siku moja yenye joto katika gari la ki fakhari lililo nyanyuliwa na watu kwenye mabega, pamoja na mwavuli mzuri wakumfunika. Anapopita katika hali hii ya ufakhari huko sokoni, watu wajinga wana sema: Haya ni matokeo ya vitendo vizuri na viovu. Mtu amekaa kwa raha katika gari, na wengine wanalinyanyua kwenye mabega bila ya kuvaa viatu, jua kali kwenye vichwa vyao na njia iliyomoto chini ya miguu yao. Lakini wenye akili wanajua kuwa kila mahakama inapokaribia, mtu huyo wa benki huzuni zake zinazidi na wachukuzi wanafurahi kufikiria kuwa mzigo unakaribia kuondoka. Mahakama inapofikiwa, mfanyaji wa benki anafikiria kuwawona mkuu huyu na yule au msomaji wake au kuzungumza na mawakili. Yeye ana wasi wasi kuwa atashinda au atashindwa katika kesi. Yeye amepotea katika matokeo. Lakini wachukuzi wanapumzika kwa raha chini ya kivuli cha mti na kuvuta sigara na baada ya mazungumzo wao wanashikwa na usingizi mkali na kulala. Ikiwa mtu huyu atashinda kesi hii, yeye atapata furaha kidogo. Lakini yeye akishindwa, yeye atazama katika bahari ya huzuni. Lakini wachukuzi wako vile vile kama walivyo kuwa hapo mwanzo. Chukua mfano mwingine Mfalme anapolala kupuumzika juu ya kitanda kizuri na laimi, yeye hapati usingizi kwa mara moja. Lakini mfanya kazi anaye lala kwenye changarawe na mawe au kwenye udongo, anapata usingizi mara moja. Mfano huu ni mzuri kila pahala.

A. Ni mashindo ya watu wa jinga. (1) Ikiwa mtu mkubwa anaulizwa kuwa mchukuzi, katu yeye hawezi kukubali kufanya hivyo. Lakini mfanya kazi akiulizwa kuchukua nafasi ya mtu mkubwa, yeye atafanya hivyo kwa moyo mkunjufu. Ingekuwa dhiki zao ni sawa au ni usawa wa hali zao za maisha, wao katu wasingekubali kuwacha nafasi zao kuwa za juu au chini. Tazama, mtu mmoja amezaliwa na malaika wa ujuzi, uadilifu, na mfalme aliyetukuka; na

mwingine ametoka katika mkee wa maskini mkataji wa majani. Wa kwanza anapata raha zote tokea anazaliwa mpaka anakufa, na wa pili anapata taabu zote katika maisha yake yote. Wa kwanza anapozaliwa, yeye anakogeshwa katika maji yanayo nukia, kitovu chake kinakatwa kwa ufundi na daktari hodari, na mipango mizuri inatengenezwa kuhusu kunyonyeshwa na kulishwa kwake. Yeye anapotaka kunywa, hupewa maziwa yenye sukari mpaka ashibe mwenyewe. Kumfanya awe na furaha, watumishi watiifu, michezo, na vyenginevyo anapatiwa kumchukua yeye mahali pazuri na kumlea kwa raha na mapenzi. Kwa upande mwingine, mtoto wa mwanamke masikini anazaliwa mwituni wala hapana hata maji ya kumkosha. Yeye anapotaka kunywa maziwa yeye anapigwa kwa boksi au kofi la uso. Yeye analia kwa uchungu mkali lakini hapana anaye mshughulikia yeye. Ikiwa visa vyote hivi visivyosemekana au baraka zisizohitajwa zinatolewa kwa watu bila ya wao kufanya uwema au uovu wo wote, Mungu hawezi kuji nusuru kuwa ni mwenye kupendelea na si mwenye haki. (2) Pia, ikiwa raha na taabu zinabarikiwa kwetu bila ya kazi ye yote, basi pasi wepo na pepo wala jahanamu baada ya maisha ya sasa. Kwa sababu, ilivyokuwa Yeye amewapa watu raha na dhiki bila ya wao kutaka wenyewe, Yeye anaweza kuwapeleka wengine peponi na wengine jahanamu, kama Yeye anavyopenda baada ya maisha yao ya duniani. Kwa mujibu wa haya watu wote wata kuwa hawana dini na wenye tamaa. Kwa nini wao wafanye kazi nzuri? Kwa sababu, pana shaka kuwa ikiwa mtu atapata zawadi ya kitendo cha uadilifu. Imo katika mikononi mwa Mungu, ambaye atafanya anavyopenda Yeye. Ikiwa mambo ni kama haya, hapana mtu atakaye kuogopa kufanya uovu, na ubaya utazidi katika dunia, na uadilifu utaangamia na kupotea kabisa. Hivyo, ni sawa kuamini kuwa maisha ya sasa na mambo yaliyopo yako sawa na matokeo ya vitendo vilivyotendwa katika maisha yaliyopita; na maisha yanayokuja ya watatengenezwa kwa mujibu wa vitendo vinavyotendwa katika maisha ya sasa.

**Roho za binadamu na wanyama.**

Q. Kwani roho zilizopo katika mwili wa binadamu na mnyama ni za namna moja au ni tafauti?

A. Roho zote ziko namna moja kwa tabia, lakini huwa takatifu au si safi kwa mujibu wa vitendo vyao vizuri au viovu.

Q. Ni kweli au si kweli kuwa roho ya binadamu huingia katika mwili wa mnyama au kinyume? Ni kweli au si kweli roho ya mwanamke huingia katika mwili wa mwanamume au kinyume?

A. Ndiyo roho huingia kutoka mwili mmoja kwendea wapili. Kwa sababu, mwovu anapozidishi vitendo vya uovu, roho ya mtu huingia katika mwili wa mnyama. Vitendo vyema ni vingi zaidi kuliko viovu, roho huenda juu zaidi kwendea miili ya miungu na wataalamu. Pale vitendo viovu na vizuri viko sawa sawa, roho inazaliwa kama mtu wa kawaida. Tena miongoni mwa watu, kuna namna tatu za watu wanaopatikana na kuhusu miili yao na mengineyo, kwa mujibu wa vitendo vyao au wao ni wazuri zaidi, wa kati na kati, au wa chini

kabisa, kwa mujibu wa uadilifu na uovu wao. Pale matokeo yanapo zidi ya uovu juu ya uadilifu basi unatiwa katika miili ya wanyama wa daraja ya chini, roho hupanda kwenye mwili wa binadamu, kama vitendo vyake vya uadilifu na uovu vya maisha ya kwanza viko sawa sawa katika matokeo yao. Hivyo hivyo, pale matokeo ya kuzidi ya uadilifu au uovu yanafurahiwa roho hupitia kwenye mwili wa mtu wa kawaida. Kuondoka kwake kutoka kwenye mwili kunaitwa kifo-mrityu. Muwungano wake na mwili unaitwa kuzaliwa-janma. Pale inapouwacha 'mwili', na kwendea sehemu ya juu kabisa ya mbinguni - yamalaya. Hivyo, Vedas inasema kuwa yama ni jina hewa ya au ya mbingu - 'yamena vayuna'. Si ya kufikiriwa Yama (Malaika wa Mauti) wa Garura Purana. Mkatawo wake maalum utatolewa katika sura ya II ya kitabu hiki. Baada ya mwungano wa muda katika sehemu ya mbingu ya juu kabisa, Mungu anaiweka tena katika uhai kwa mujibu wa sifa za uadilifu na uovu wa vitendo vyake. Huingia katika miili ya wanyama kwa nguvu za mbinguni, hewa, chakula, kinywaji au tundu za mwili kwa amri ya Mungu. Baada ya kuingia kwake katika miili hii, hupitia katika shahawa na kuwekwa katika tumbo la uzazi, inapotia mwili, yeye huja na huona mwangaza. Roho inawekwa katika mwili wa mwanamke, ikiwa matokeo ya vitendo vyake vitaweza kujulikana, na mwili wa mwanamume ikiwa utaweza kustahmilika humo. Inazaliwa kuwa mhasi pale ambapo shahawa ya kiume na yai la kike la uzazi yako sawa sawa wakati wa mwingiliano. Hivyo roho inapitia katika uzazi na katika kifo kwenda katika miili mbali mbali, mpaka inapopata uokovu kwa kufanya kazi nzuri na tafakari na kupata ujuzi wa roho; hivyo, kazi nzuri huleta matokeo mazuri katika kiwili wili cha binadamu, na kufurahia raha na uhuru, kutokana na maumivu ya maisha na kifo kwa muda wa miaka mingi sana - maha kalpa.

Q. Uokovu unapatikana katika maisha moja au katika maisha mengi?

A. Unapatikana katika maisha mengi kwa sababu, Mundak II, II, 8.

Roho hukaa katika Mungu ambaye ameenea nje na ndani yake, pale ujinga wake wa ndani unatoka au fundo la linakatika, na shaka zake, kuondoshwa, na vitendo vyake viovu kuangamizwa.

Q. Ati Roho inachanganyika na Mungu au inabaki mbali na Yeye katika uokovu?

A. Inabaki mbali; kwa sababu, ikiwa inachanganyika na Mungu nani atafurahia furaha ya uokovu? Tena njia zote za uokovu zitapeperuka na upepo. Si uokovu bali ni uangamizi kabisa wa roho. Kuwa roho peke yake inapata uokovu, ambayo inatii maamrisho ya Mungu, inafanya kazi nzuri, na kujiweka na watu wazuri, na kufanya mazoezi ya Yoga na njia nyingine za uokovu. Inasema Taittiriya Upanishat, III, I.

Roho inajua kuwa Mungu wa ukweli wa milele, ujuzi, furaha anakaa katika akili yake na yeye mwenyewe, inapata matakwa yake yote kutimizwa inapoishi katika uwewo wa Mwenye kuwepo kote; kwa maneno mengine, roho inapata

uwema kama huo unataka kupata. Tena hapo ni uokovu wa kweli.

Q. Vipi roho itafurahia raha na uokovu bila kuwa na mwili, ilivyokuwa raha za dunia bila ya kiwili wili cha kitu?

A. Swali hili limejibiwa juu, sisi tu lazima tuengeze kuwa roho inafurahia raha ya uokovu kwa msaada wa Mungu, kama inavyofurahia raha za dunia hii kwa kitu chenye mwili. Roho iliyookoka hutembea kwa uhuru katika Mwenyezi Mungu. Ina ona muumbo wote kwa heshima yake ya kuwa mjuzi safi. Inaonana na roho nyinginezo zilizookoka. Yeye huanza kuyazoea masomo ya intidhamu ya muumbo, na huzitembelea zote dunia zote zinazoonekana na zisizoonekana. Yeye inaviona vitu vyote ambavyo ni vya kujulikana. Kina inavyojua zaidi inafurahi zaidi, Kwa kuwa safi na bila ya ila katika uokovu, roho huwa yenye ujuzi kamili na kuzijua tabia za vitu vilivyo hapo. Furaha hii maalum ya uzidisho wa ujuzi inaitwa Swarga au pepo, na kupata maumivu mengi kutokana na ra za uovu, naraka au jahanamu. Swah maana yake ni raha. Pepo ni ile ambamo watu hupata raha. Kinyume chake ni adhabu au jahamamu, Raha za dunia zina pepo ya kawaida - Samanya Swarga. Furaha inayopatikana kutokana na kumpata Mungu ni ya namna peke yake au pepo kuu: Vishesha Swarga. Watu waovu wote bila ya shaka wanajaribu kupata raha na kuziwacha dhiki zote. Lakini haziwezi kupata raha, na kuwa mbali na shida ikiwa hazitafanya mwema wo wote na hawa wachi kufanya uovu; kwa sababu hayo hayawezi kuangamiza sababu zilizopo, au mizizi ambayo imezama chini zaidi.

Kuuwacha kwetu kwa uovu huleta mwisho wa maumivu yetu kama mtu unavyoangamizwa kwa kukatiwa kwa mizizi yake. Vide Code ya Manus Sura.

XII, 8, 9, 25 - 33, 35 - 38 kwaajili ya namna tafauti za matunda yanayo zaliwa na uadilifu na uovu.

Haya yanasaidia kusema kuwa na mwahakikisho wa uzuri, wa kati na sifa mbaya, mtu lazima ajiendeleze na kuzisimamisha sifa mbaya.

**Alama za Tabia Ya Mtu.**

Yeye lazima pia ajue kuwa nguvu za kiungu za kusema na mwili mzima kwa jumla, kila mmoja hujichumia matunda ya uzuri na uovu unaofanywa nao, - 8.

Mtu katika maisha yake mengine huwa mtu wa dhambi zilizofanywa naye na mwili, kama uwizi, zinaa, mauaji ya waadilifu, na vitendo vyengine viovu. Yeye huzaliwa tena kama ndege, mdhalimu na au mnyama mwingine wa daraja ya chini kwaajili ya dhambi zilizofanywa na kiungo cha kusemea. Yeye huzaliwa kama mtu wa daraja ya chini kwaajili ya kufanya dhambi na nguvu za kufanyia - 9.

Sifa inayoenea katika mwili wa wanyama hawa, inawalazimisha kuionyesha katika maisha yao. - 25.

**Guna Tatu**

Sattwa ya roho: sifa nzuri inaonyeshwa na hamu yake ya elimu, tama: sifa zenye kiza kwa ujinga wake, na raja: nguvu kwa mapenzi na chuki. Sifa hizi tatu za tabia zimeenea katika vitu vyote vya dunia. - 26.

Wao lazima wahakikishiwe. Akili inapokuwa na furaha, nia ya utulivu, imetosheka na imeelekea kwenye usafi, lazima ijulikane kuwa sifa nzuri - Satwa guna - inaishinda, na sifa nyeusi na zenye harakati - Rajo guna na Tano guna - zinasukumwa nyuma. - 27.

Roho na nia zinaposhikwa na huzuni, maskini wa raha, mwenye kupenda raha za uchu, na afiye na kazi ya kuzunguka huku na huku, ni hakika kuwa sifa ya harakati - rajo guna - ni ya kwanza na sifa nzuri na zenye kiza sattwa guna na tano guna - ziko nyuma - 28.

Wakati akili na nia zimeshikana na kupata vitu vya dunia, kutoona kwa akili, iliyozama katika raha za uchu, na isiyoweza kubagua baina ya sababu zilizo za hakika na zilizokuwa si hakika; ni hakika kuwa sifa zenye kiza - tamoguna - ni ya kwanza kabisa, tena ni sifa za uzuri na harakati - sattwaguna na rajoguna - zina kwenda chini. - 29.

Sasa sisi tunaeleza kwa urefu, uzuri, wa kati na kati na ubaya wa matokeo ya sifa hizi - 30.

Maonyesho ya sifa nzuri - sattwa guna, ni mazoezi ya Vedas, kutenda yale yanayo fuatana na dini, uendelezi katika elimu, matakwa ya utakatifu, uzuizi wa hisia, vitendo vya uadilifu, na tafakari za kiroho. - 31.

Wakati sifa ya harakati - rajoguna - inapodhihirika sana, na sifa nzuri na zenye kiza hurudi nyuma katika uzembe; mapenzi ya kazi, kuwa cha kuwa mstahmilivu, kukubali vitendo vya uwongo na kupendelea raha za uchu, huwa dhahiri katika mtu. - 32.

Sifa nyeusi ya hisia inapoamka na nyingi mbili kupotea, tamaa nyingi, ambayo ni mzizi wa uovu, inapoinuka kifuani; uzembe mwingi, usingizi, kutokuwapo kwa ustahmilivu, ukatili, kutokubali kuwepo kwa Mungu haya ni kusema, kutokuwa na imani katika Veda na Mungu, mgeuzo wa hisia za ndani, kutokuwa na utulivu au ufahamu, na kuzamia katika raha za uchu na kuzidhihirisha kuwa ni matunda ya mapenzi. - 33.

Pia, aibu, shaka, na wasi wasi hujitokeza, katika akili katika kufanya vitendo na katika kutaka kufanya hivyo, watunga mashairi na wapigaji wa zumari hata katika umasikini; ni ishara ya sifa za harakati - rajo guna - kuja kuwa katika mchezo. - 36.

Akili inapotaka kujua yote, inapata uadilifu, wala haioni haya kufanya kazi nzuri, na inapenda kufanya kazi kwa mujibu wa uongozi wa hisia na kanuni za dini, ni dhahiri kuwa sifa nzuri - sattwa guna - ni yenye kuzidi katika Mungu. - 37.

Tabia kubwa ya mapenzi au tamo guna ni kutaka na uchu, kuwa ya kitendo au rajo guna ni kutaka mali nyingi, na ile ya sifa nzuri au sattwa guna ni ibada au mapenzi ya uadilifu. - 38.

Lakini sifa za harakati ni bora kuliko kiza, na uzuri ni bora kuliko yote.

**Matokeo Ya Uadilifu.**

Sasa tunaendelea kuweleza hali zile ambazo zinapatikana kwa roho katika uadilifu wa sifa tatu za tabia:- Manu XII. 40, 42, - 50, 52.

Mtu mwenye sifa nzuri huwa Mungu au mtaalamu; yeye ambaye aliyetunukiwa na sifa za harakati, huwa mtu wa kawaida; na yeye ambaye anayo sifa nyeusi, huenda kuifunjia heshima nje. - 40.

Wao waliobobea katika tabia mbaya, wanapitia katika maisha ya mimea, funza, vidudu, samaki, nyoka, kobe, ng'ombe na hayawani. - 42.

Wale wenye tabia kidogo ya ubaya, wanazaliwa kuwa tembo, farasi, watu wa daraja ya chini, washenzi, wafanyaji wa vitendo viovu, kama simba, chui, nguruwe dume, au nguruwe. - 43.

Wale wenye kuwa na sehemu nzuri zaidi ya tabia mbaya, wanakuja duniani kama waandishi wanaotunga beti za sifa za watu, ndege wazuri, watu wanaojivuna ambawo wanahimidi wenyewe kupata raha, wachawi wauaji, mashetani wa tabia mbaya; i.e., walevi na wanaofanya makosa makubwa - 44.

Wao wenye kuwa na sehemu iliyo mbaya zaidi ya tabia, kuzaliwa tena kama wapiganaji panga, wachimbaji kwa shoka, mabaharia wachezaji, wastadi wa kuonyesha miujiza, watumishi wenye silaha na walevi. - 45.

Wao wenye kuwa na sifa za kati za harakati za tabia, wanazaliwa kuwa ni wafalme, maaskofu wa wapiganaji vita wa wafalme, mawaziri, mahakemu, mabalozi na majemedari wa jeshi. - 46.

Walio wenye sehemu nzuri kabisa za asili ya harakati wanazaliwa kuwa kama waimbaji, wapigaji ala, watu wenye pesa nyingi, malaika na vichinchiri.-47.

Wenye kuwa na sehemu ya kwanza ya asili nzuri wanazaliwa kama watawa watiifu, mawali, wanavyuoni wa Veda, waendeshaji wa mifuko ya mpira iliyojaa hewa, wanajimu, watunzaji wa miili. - 48.

Wale wenye sehemu ya pili ya asili nzuri wanazaliwa kuwa wanaojitolea, wafasiri wa Vedas, waalimu wa Vedas, nguvu za umeme, na elimu ya miaka, walinzi, wataalamu, wana falsafa wenye uwezo wa kazi nyingi. - 49.

Wenye sehemu ya tatu ya asili ya tabia nzuri wanazaliwa kama wanajimu wa Ki-Veda - Brahma, waalimu wa maamrisho na sheria za tabia, wajenzi, wa namna nyingi za uchukuzi na mifuko yenye puumzi, Vishwasrija, au mafundi, watakatifu, hodari sana, wenye kuzisitiri nyota, na mabwana wa asili. 50.

Mjinga ambaye anajizamisha katika raha za uchu kutoka kwenye utumwa wao mpaka kwenye hisia, na ambaye anaiwacha dini na kufanya dhambi, wanazaliwa kama wapotovu na wanapatwa na maradhi mabaya ya huzuni. - 52.

Watu kama hawa wanajichumia namna mbali mbali ya matunda kwa mujibu wa sifa nzuri na mbaya za vitendo wanavyo tenda chini cha nguvu za kazi za asili tatu za tabia za usafi, nguvu na mapenzi - sattwa, raja, na tama gunas. Wale ambawo wanapata uokovu, wako juu ya nguvu hizi za sifa au za kuwa Mungu mmoja za tabia. Kwa kuwa haiwezi kuathirika kwa nguvu za vitu hivi, wao lazima wawe wenye kujitolea sana ili kupata uokovu. Kwa sababu, inasemekana kuwa mithali za Yoga za Patanjali, - 1, 2, 3.

Mtu lazima aizuie akili yake kutoka kwenye kazi za nguvu na mapenzi raja na tama, pia kutokana na nguvu zile za asili zilizo safi na nzuri - sattwa, na kujifanya yeye mwenyewe kuwa wa asili nzuri na safi. Tena Yeye lazima pia azishinde hizo na aituli akili, haya ni kusema, iweke na Mungu na ifanye iwe inatumika kufanyia kazi za uadilifu. Utulivu wa namna hii wa sehemu ya mbele ya kichwa inaitwa utazama akili, ambao ni mzunguko wake wa sehemu zote unasimamishwa na mwisho wake kuletwa. Akili inakuwa nzito na uhalifu wake kupimwa, inateremshwa na kuwekwa mbele na baraka za Mungu, mwonaji wa yote. Hizi ni njia au sababu za uokovu zichaguliwe na mwanafunzi wa uokovu. Pia mithali ya falsafa ya Sankhya inasema. I. 1.

Uokovu ni kazi kuu ya ushujaa wa kuepukana na namna tatu za maumivu, viz. (1) adhyatmik: maradhi ya mwili, (2) adhibhowtik: uovu wa maisha: (3) adhidaivik: dhiki za bahati mbaya za tabia, i.e., mvua nyingi, joto jingi, baridi nyingi, uhalifu wa akili na wa hisia.

Sasa sisi kwenda kueleza sheria za tabia na chakula kilicho sawa na si sawa cha mtu.

**Muhtasari**

Ujinga unasemekana kuwa ni sababu ya dhiki kutokana na kifo na elimu inapatisha tabia nzuri na kuleta uokovu. Yaj - IV - 14. Ujinga ni kuamini yale yasiyo ya kweli, kama kuamini kuwa dunia imesimama haisogei. Yoga II. 5. Elimu ni fikra ya kweli ya kitu, kama roho ni ya milele. Ujinga huleta uongo, uzembe, na dhambi nyinginezo, na hivyo huzaa dhiki. Elimu inawaongoza watu kwenye kazi za uadilifu, kama kusema kweli na kama haya, na pia ni njia ya uokovu.

**Kutenda dhambi na uokovu si tabia lakini vinapatikana. Si kweli kuamini kuwa roho ni yenye dhambi kwa tabia au iliyo nyimwa, kwa hivyo, uokovu hautawezeka kupatikana. Na uokovu kama ni matokeo ya elimu ni dhahiri inapatikana.**

**Pia si kweli kuamini kuwa roho ni Mungu au ni picha ya Mungu. Kwa sababu, Mungu hana mwisho na roho ina mwisho kwa njia zote. Kuhusu roho**

kuwa ni mwangaza wa Mungu iliyo fungwa katika hisia za ndani, inatosha kusema kuwa inamfanya Mungu kuwa anayeweza kugawika, hasa ilivyokuwa ni ameenea kote. Pia, ujinga ambawo unatolewa wazi na roho, itasifiwa na Mungu, ambayo si sawa. Hivyo, roho ni iko mbali na Mungu, na kuishi mbele yake ni uokovu. Maana yake ni kujipatia elimu, urafiki wa watu wazuri, kuwa mbali na uchu, na mazoezi ya vitendo vya uadilifu. Kuidhihirisha tabia ya roho, ni lazima kujua yale yanayoitwa Panch Kosh, mifuniko mitano inayomfanya mtu. viz. I. viungo vya uhai - ngozi - nyama, mifupa, mishipa, moyo, damu, shahawa; (2) uhai hasa - kuvuta puumzi, kutoa puumzi, kusaga chakula, mchanganyo, mzunguko au kupona; 3. mpango wa kinyama - nia, hisia, msemo (kusema) kwenda ufahamu, upungufu, kuzaa au kuengezeka; 4. nidhamu ya akili - ufahamu, makumbusho, kuona, kusikia, kunusa, kuonja, kugusa au kuhisi. 5. ya kiroho - mapenzi, uchangamfu, raha, furaha. Hali tatu ni kuamka, kuota, na usingizi mzito. Miili mitatu ni wenye kuonekana vitu na tabia. Hali nne zinaitwa turiya ambamo roho huishi katika uokovu. Ni uhuru kamili. Kutaka kusikia, inachukua nguvu za kusikia, na mengine Yeye ni mbali na kutokana na hali hizi na Mungu.

Namna nyingine za uokovu ni haki ya kweli, tabaka sita sifa - kutosheka, kujizuia, tofauti, ustahmilivu, imani, tafakari. Matakwa ya dhati ya uokovu, elimu ya kweli ya Mwokozi, kuyasikiliza masomo ya kiroho, kufikiri, kuchungua na kudhihirisha yale yanayosomeshwa, pia hi lazima.

Namna nne za uokovu wa ngano za zamani, kwa majina ni, salokya: Kuishi katika mipaka yake Mungu, samipya: kuishi na Mungu kama ni ndugu mdogo wa kiume, sarupya: kuwa kama Mungu, sayujya: kunyonywa katika Mungu, si sawa. Hayo yote yameshapatikana katika dunia, kama Mungu ameenea kote. Kuzamia si uokovu lakini ni maangamizi.

Uokovu hauwezi kutokea katika maisha moja. Hivyo roho inazaliwa mara nyingi ili ipata ukamilifu. Si sawa kuamini katika maisha moja ya roho. Kwa sababu mgawanyiko sawa sawa wa furaha katika dunia lazima uwe matokeo ya vitendo vizuri na viovu vilivyotendwa na roho ilipo-kuwapo hapo mwanzo. Ikiwa si hivyo, Mungu atakuwa si wa haki kuwafanya wengine wenye furaha na wengine wawe wenye dhiki. Lakini Mungu ni mwenye haki. Hivyo ya sasa ni matokeo ya zamani. Haki ya kutia adabu anayo Mungu tu katika mfalme wake.

Hivyo, mtu lazima aziendeleze sifa zake nzuri, na sifa za namna nyingine mbili ambazo ni za kutenda na kutendwa. Sifa hizi - sattwa raja, tama - zinapatikana katika wanyama wote na vitendo vyao vinawapeleka kwenye adhabu mbali mbali.

Urefu wa uokovu ni muda mrefu wa miaka mingi au parantakala (Mundak Upanishat III.II.6) wenye 311, 040, 000, 000, 000 ya miaka ya binadamu, baada ya haya roho huanza mwendo wake wa milele.

Roho zile ambazo hazijaribu kupata furaha hii, huendelea kupata dhiki za kuzaliwa na kufa katika nyama.

## SURA YA X.

## ADABU NZURI NA MBAYA NA CHAKULA MWAFAKA NA SI MWAFAKA.

Tabia nzuri ni kufanya kazi za uadilifu, heshima, utu, urafiki wa watu wazuri na mapenzi ya kutaka kupata ufuzi; na kinyume cha kinaitwa tabia mbaya. Inasema Manu, Sura II.

Lazima ifahamike akilini kuwa cho chote kinachoaminiwa daima na kufanya na watu wenye busara walio mbali na mapendeleo ya upande mmoja na chuki, na zinakubaliwa na hisia zao, ni dini ambayo lazima iaminiwe na kufuatwa. - 1.

Kujipendelea sana kutokujipendelea kabisa si vitu vizuri zaidi duniani. Kwaajili ya elimu ya Vedas na ufanyaji wa kazi zilizoelezwa na Vedas zinaweza kutimizwa pale penye nia tu. - 2.

Ikiwa mtu anasema kama yeye hana haja na hisia au yeye anaweza kuwa hivyo, yeye katu hawezi kuwa hivyo, kwa kazi zote, viz, kujihini, ukweli, yama, niyama na uwema mwingine ni matokeo ya kutaka. - 3.

Kwa mwendo wa mikono, miguu, macho, nia inaadhirika kwa hamu au kutaka. Ikiwa hapatakuwapo na matakwa, ingekuwa hakuna mfunguo na mfungo wa macho. - 4.

Kwa hivyo, faida za Vedas zote, na maonyesho ya Manu, mafunzo ya maandishi yaliyoandikwa na Rishi au wacha Mungu, mifano ya watu wema na, kazi zile ambazo zinazitosheleza hisia, haya ni, kuendelea na aibu, hofu, au shaka, lazima yote yafuatwe kwa ulinganifu. - 6.

Tazama hapa, mtu anapotaka kusema uwongo, kuiba, na ubaya mwingine, hakika katika moyo wake huwepo hofu, shaka na aibu. Hivyo kazi kama hizi lazima zisifanywe.

Mtu aishike dini ile ambayo ni sawa katika mafunzo pamoja na maandishi na falsafa, Vedas, mifano ya uadilifu, hisia, baada ya kufikiri sana pamoja na mwangaza wa ujuzi, na kuchungua maamrisho ya Mdhihirisho na mkubalio wa husia. - 8.

Kwa sababu, mtu anayefuata dini iliyosomeshwa na Vedas na kwa sheria zisizopinga Vedas, hupata umashuhuri duniani na daraja ya juu kabisa katika nyingine baada ya kifo chake. - 9.

Kazi zote zifanywe na zisizofanywa lazima zihakikishwe kwa usaidizi wa Shruti (Mdhihirisho) ambawo ni Vedas, na Smriti au Dharma shastras (sheria takatifu).

**Kazi Za Dini.**

Mtu asiyeiheshimu Vedas na maandishi mengine matakatifu yaliyoletwa kwao, lazima wadharauliwe na watu wakubwa wenye hadhi, kwa sababu yeye anayeidharau Vedas, ni mtu asiye mwamini Mungu. ; 11.

Tabia nne zinazoonyesha dini, ni utiifu wa mafunzo ya Vedas, kufuata sheria, mifano ya watu wazuri, na kazi za ukarimu zinazosimamiwa na hisia. - 12.

Yeye ambaye hajapotezwa na uovu wa vitu vya dunia na uchu au kujishughulisha sana na raha za uchu, peke ya anafaulu kujipatia ujuzi wa dini. Vedas ni kubwa na ni ya juu kabisa yenye mafundisho kwa wale wanaotaka kuisoma dini. 13.

Ni sawa kwa watu kuzifanya sherehe za dini, kama Nisheka na nyinginezo za watoto wa Brahmanas, Kshatriyas na Vaishyas kwa mujibu wa mila takatifu zilizoelezwa na Vedas, ambazo zinasifiwa hapa na baada ya hapa. - 26.

Shereha za kunyoa nywele au kuzifunga, lazima zifanywe wakati wa umri wa miaka 16 kwa Brahmana, miaka 22 ni kwa Kshatriya, miaka 24 kwa Vaishya. - 65.

**Nywele na Ndevu.**

Kwa maneno mengine, wao lazima wanyoe ndevu, masharubu na kichwa ila kishungi tu kibakishwe baada ya sherehe. Wala zisiwekwe baadaye. Lakini watu katika pahali pa joto watizame raha zao za kuweka nywele. Katika nchi za joto, nywele zote pamoja na kishungi zinyolewe au kukatwa, kwa sababu nywele kwenye kichwa huleta joto jingi mwilini. Pia hupunguza ufahamu. Kula hakufanyiki vyema kwa kuweka masharubu na ndevu, na takataka za chakula pia hubakia katika nywele kwenye midomo na shingo.

Kazi muhimu ya mtu ni kuzibania hisia zake ambazo zinaifanya akili kupendelea raha za uchu, kama mwendeshaji gari zuri huwaweka farasi wake ili awaendeshe kwenye njia iliyo sawa sawa. Kwa njia hii hii, yeye ajaribu kupata uwezo wa kuzizuia kwenda kwenye njia ovu na kuziongoza kwenye njia nzuri. Manu. II. 88.

Kwa sababu, mtu lazima hupata lawama kwa kuziruhusu hisia zake kuzamia katika raha na kutokuwa na dini. Yeye anapozishinda kwenye uadilifu, yeye hupata mafanikio aliyo ya taka. ib. 93.

Ni hakika kuwa moto huunguza zaidi, mafuta, samli safi, tunaitia katika moto huo. Kwa njia hii hii, matakwa hayawezi kutosheka kwa kuvakamia, bali huzidi. Hivyo, mtu katu asiwe wa kupenda sana. - ib. 94.

Mtu ambaye hajazibana hisia zake, anaitwa mwovu, vipradushta. Mtu kama huyo wa hisia zisizobanika hawezi kufaula katika elimu ya Vedas, katika kuumcha Mungu, kujitolea, katika yamas au uzuri wa kawaida wa namna tano, na mazoezi ya dini, Mtu mwenye kuziweza hisia zake na mwenye akili ya dini peke yake hufaulu katika kazi zote. ib. 97.

Hivyo mtu lazima apate hisia tano, za ufahamu na hisia tano za vitendo na nia, hisia II, katika nguvu zake; kuweka mwili katika siha nzuri kwa kula kidogo na kunywa na mazoezi ya Yoga au kuvuta puumzi refu; na kuwa bwana wa vitu vyote kwa uadilifu. - ib. 100.

Mtu ambaye amezibania hisia zake ni yule ambaye hapendi kusikia akisifiwa, pia haoni vibaya kusikia masingizio yake, ambayo haoni raha kugusa vitu laini, ambaye haoni maumivu akianguka katika shida, ambaye haoni raha akiona vitu vizuri; wala hasikitiki akiona vitu vibaya, wala hafurahii kuonja vyakula vitamu na hasikitiki akila vyakula visivyo na ladha nzuri, wala hafurahii harufu nzuri na hakereki na harufu mbovu. - ib. 98.

Halijibu suali bila ya kuulizwa au anapoulizwa na mtu asiye na haki au mshawishi. Mbele ya watu kama hawa, mtu mwenye busara ajiwekee heshima yake. Lakini yeye ajadiliane mbele ya watu wema na wenye kutaka kujua, japo kama hajaulizwa. - ib. 110.

**Asili Za Heshima.**

Kwanza ni mali; ya pili ni jamaa, ukoo au kabila; ya tatu ni, umri; ya nne ni kazi nzuri; na ya tano ni elimu iliyo bora kuliko zote, vitu hivi vitano ni asili ya heshima; lakini jamii ni bora kuliko mali, umri kuliko jamii, kazi nzuri kuliko umri, ujuzi kuliko kazi nzuri; i.e. kila mmoja ya vitu hivi vilivyotajwa ni bora kuliko kimoja kilicho mbele yake. - ib. 136.

Mtu anaweza kuwa na umri wa miaka mia, lakini bila ya elimu na ujuzi wa kiroho lakini ni mtoto tu. Lakini yeye ambaye anaeneza elimu ya kiroho na habari zenye faida, ijapokuwa ni kijana, lazima awe kama mtu mzima au mzee; kwa sababu, maandishi yote humweleza mjinga, asiyesoma na mtu wa kupenda ya dunia kuwa kama mtoto, na mtaalamu na mtu mwenye busara kuwa ni baba. - ib. 153.

Mtu ambaye ameiona miaka mingi, na ambaye nywele zake zimekuwa na mvi, ambaye anazo pesa nyingi, au ambaye ana jamii kubwa, hawi mwenye heshima au mtu mkubwa; lakini ni sheria iliyowekwa na wanavyuoni wa falsafa kuwa yeye ni mkuu ambaye ni mkubwa katika mzunguko wa elimu ya kiroho miongoni mwao. - ib. 154.

Brahman huwa mheshimiwa kwa kusoma na kuwa na busara, Kashatriya kwa nguvu na ushujaa, Vaishya kwa mali au pesa, na Shudra kwa umri. - ib. 155.

Nywele zenye mvi hazimfanyi mtu apate heshima ya wote, lakini wataalamu humwangalia yeye kama ni mtu ambaye anastahiki heshima ijapokuwa ni kijana. ib. 156.

Yeye ambaye hajasoma, ni kama tembo wa ubao au paa wa ngozi. Kwa njia hii hii, mtu mjinga ni binadamu kwa jina tu (katika dunia.) - ib. 157.

Mtu lazima awe mwenye elimu kwa kujipatia elimu, awe mwadilifu, na

daima ausomeshe ukweli kwaajili ya uzuri wa binadamu kutokana na mapenzi na bila ya uadui. Amebarikiwa yule ambaye yeye anayetumia maneno matamu na ya kubembeleza katika mafunzo yake ya ukweli unaendeleza uwema na huuondoa uovu miungoni mwa watu. - ib. 159.

**Tabia.**

Mtu akoge kila siku, aziweke nguo zake kuwa safi, atumie chakula na kinywaji safi, aishi katika makaazi penye hewa safi; kwa sababu, usafi wa haya ni lazima kuziendeleza fikra na siha ya mwili, na haya huyageuza kuwa ushujaa. Usafi uendelezwe mpaka uondoe taka, uchafu na harufu mbaya.

Manu I. 108. Mazoezi ya ukweli na uadilifu mwingine ni tabia inayosomeshwa na Vedas na maamrisho ya sheria za haki.

Kazi ya baba, mama, mwalimu na mgeni inaitwa ni ibada. Kazi kubwa ya mtu kufanya yale yaliyokuwa yenye faida kwa dunia na kuwacha kutenda yaliyo ya dhara kwa dunia. Urafiki wa wasiomwamini Mungu, waongo, watu wasio na kheri, majambazi, wanaojipendelea nafsi zao tu, watu walio wa ongo, wadanganyi, na watu waovu, lazima waepukwe kabisa. Urafiki wa wasema kweli, wanao mcha Mungu, na wapendaji wa uzuri wa watu uendelezwe. Haya yanaleta tabia nzuri. Yaj. XVI. 15., Atho. IX. XV. 17. Tait Pr. 7, An. II.

**Nchi za Nje na Safari.**

Q. Kwani tabia za watu wa Aryavarta, zinaharibika kwa kwenda kwenye nchi za kigeni?

A. Maoni haya ni ya uwongo, kwa sababu tabia ina usafi wa nje na ndani, ukwali, na mazoezi ya uadilifu kama huu. Hivyo mtu anapoviendeleza hivi po pote anapo kuwapo, yeye atakuwa na tabia nzuri, na wala hawezi kupotea. Lakini ikiwa mtu atatokwa na adabu hata katika India, yeye atakuwa ni mtu anaye kufuru dini yake. Inasema Mahabharat, Shanti Parva, Ch. 327:-

**Usafiri Wa Nchi Za Nje.**

Ni mzungomzo baina ya Vyasa na Shuka kuhusu asili ya uadilifu. (a) Hapo zamani za kale Vyasa pamoja na mtoto wake wa kiume na mwanafunzi Shuka aliyekaa katika Patala ambayo sasa inaitwa Amerika. Shuka alimwuliza baba yake, ikiwa haya yalikuwa ni elimu ya kiroho, au ni zaidi ya hayo. Vyasa hakujiweza kujibu, kwa sababu ilivyokuwa yeye amaeshayakalia haya. Kumpa yeye amri nyingine, yeye alimwambia mtoto wake wa kiume kwenda Mithilapuri na kuliweka swali kama hilo mbele ya Mfalme Janak huko, yeye angeweza kujibu kwa vizuri. Hapo Shuka alianza kwenda Mithilapuri. Yeye alipitia Uengereza, Meru na India na kuja China. Kupitia Himalayas, yeye alifika Mithilapuri (b) Pia, Shri Krishna na Arjuna walikwenda Patala (Amerika) na Ashwatari, ambalo ni jina la meli, na hapo ilimleta hakimu Uddalaka kwa muhanga unaosherehekewa na Mfalme Yudhishthira. (c) Dhritarashtra alimwoa binti mfalme wa Gandhara, sasa inaitwa Kandhar katika Afghanistan (d) Madri, mke

wa Pandu, alikuwa binti wa mfalme Patala wa Iran, (Persia). Arjuna aliolewa na Ulopi, binti wa mfalme wa Patala, ambayo sasa inaitwa Amerika (e) Ingekuwa watu hawajenda nchi na visiwa vya kigeni, vipi mambo kama haya yangepita?

**Safari za Bahari.**

Ushuru juu ya meli inayokwenda baharini iliyoelezwa katika kanuni ya Manu inaonyesha kuwa safari zilikuwapo za ardhi za kigeni kutoka Aryavarta.

Mfalme Yudhishthira alifanya karamu yake ya kifalme - rajasuya yajna, Bhima, Arjuna, Nakula na Sahadev walikwenda kwenye robo nne kuwaalika wafalme wa dunia kwenye karamu hiyo. Ingekuwa walifikiria kuwa safari za nchi za kigeni ni dhambi, wao wasinge kwenda huko.

Hivyo watu wa Aryavarta wa zamani walifanya safari kwenda kwenye safari zote za kigeni kwa ajili ya biashara, kazi za serekali, na safari za raha tu. Wasi wasi wa kisasa wa uangamizı wa utakatifu na dini kutoka usafiri wa kigeni ni kutokana na watu wajinga, upotevu na kueneza ujinga tu. Watu wasio na wasi wasi kufanya safari kwendea nchi, na visiwa vya kigeni, huanza kuendeleza kwa kuchanganyika na watu mbali mbali wa nchi nyingine na kwa kuzichungua tabia na mila zao, na kuwa mashujaa kuendeleza biashara n'serekali yao. Wao hupata mali nyingi kwa kuwa tayari kuucha uovu na kujichagulia tabia nzuri. Ajabu, watu hawa wanahesabu wao kuwa wenye ila na dini yao kuangamia kwa kuangukia wanawake na makahaba waliozaliwa na watu waovu; lakini wao wanahesabu hawa. kuwa walioharibika na mchacho kuingiliana nao kwa watu wakubwa wa dunia! Ikiwa si matokeo ya ujinga basi ni nini? Hakika, ni kweli kuwa mwili, shahawa, na vitu vyengine vya walaji nyama na walevi kuwa ni vikavu na vyenye kuleta madhara, inaogopewa kweli kuwa Aryas hawawezi kuwa kuteremshwa hadhi kwa kukutana na hawa. Lakini hakuna uharibifu wala dhambi kujua kazi na uwema kutoka kwao. Pia, hakuna dhara kuiga sifa zao nzuri na kuyawacha yale yaliyo maovu, kama vile ulevi na uchu. Ilivyokuwa wajinga wanaamini kuwa ni dhambi kuwagusa au kuwaona wao, wao hawawezi kupigana na wao; kwa sababu, kupigana huwalazimisha kuwaona na kuwagusa. Kwa watu wazuri, kuwacha mapenzi ya siyo sawa, chuki, dhulma, kusema uwongo na uovu mwingine; na kuendeleza kutokuwa na adui, mapenzi, huruma, tabia nzuri na upole, huleta tabia nzuri na mwendo mzuri. Pia, wao wafahamu akilini kuwa dini imehusika na roho zao na kazi zao. Pale sisi tunapofanya kazi nzuri, kusafiri katika nchi za mbali na za kigeni na visiwani hawawezi kutuletea sisi uovu. Uovu una zaliwa kutokana na dhambi. Hakika, ni lazima kabisa kuwa na imani katika dini inayosomeshwa na Vedas na kujua pingamizi za dini za uwongo, ili sisi tusidanganywe na kuamini mazingaumbo. Inaweza kuwapo uendelezi wo wote katika nchi bila ya utawala na biashara na nchi za kigeni na visiwani? Hapa wezi kuwa na kitu ila umasikini na huzunı pale watu hawaendi kwaajili ya biashara kuvuka mipaka ya nchi zao kwendea mwahali wageni wanatawala na kufanya biashara. Maaskofu wa ki Rumi wanafikiri kuwa ikiwa wao wakiwafunza watu na kuwa ruhusu wa kusafiri katika nchi za kigeni, wao

watakuwa wenye busara na hivyo hawata tegwa katika mitego yao ya uwongo, ambawo utauondosha heshima na maisha. Hivyo wao wameengeza dhiki katika kula, kunywa na kuishi, kuwa wao kwenda wasijaribu kwenda katika nchi za kigeni. Lakini watu lazima waifanye kuwa ni sheria kwao kuwa katu wasile nyama na wasinywe mvinyo kwa vyo vyote. Ingekuwa haijahakikishwa na watu wenye busara wote kuwa desturi miongoni mwa wafalme na mashujaa wa kula chakula katika chowka, au pahaliposuguliwa mavi ya ng'ombe au tope, hata wakati wa vita na kupika kwa mikono yao wenyewe, ni sababu hakika ya kushindwa kwao?. Lakini tabia nzuri ya shujaa katika vita ni kula mkate na kunywa maji na mkono mmoja na kuua adui kwa mkono mwingine na huku awe juu ya farasi, tembo, au kwenye gari au kwenye miguu yake mwenyewe. Tabia nzuri ya mpiganaji vita ni kushinda na tabia mbaya ni kushindwa kwake. Ni ujinga wa watu hawa wajinga kuwa wao wameupoteza uhuru, raha, mali, serekali, elimu, na ushujaa kwa kuwa wamejishughulisha sana na kula na kunywa, na sasa wamekaa bure na kufunga mikono. Wao wanahamu ya kupata pesa kidogo kununua chakula chao na kupika na kula. Lakini hamu yao huwa haizai matunda. Kwa kufagia pahali pa kulia, panapoitwa chowka, wao wanayo, kama ilivyokuwa, iliifagia Aryavarta, kwa kila kitu kizuri na kukiangamiza. Ni lazima kuwa pahali wanapokulia chakula, lazima pa oshwe, patengenezwe na mavi ya ng'ombe au udongo, pa fagiwe, na pasafishwe taka zote na uchafu.

**Namna mbili za kutengeneza Chakula.**

Q. Nini maana ya sakhari na nikhari?

A. Sakhari ni chakula kile kilichotengenezwa ambacho kinapikwa katika maji peke yake, na nikhari ni kile ambacho kinapikwa kwa samli safi na maziwa. Majina mengine ya kutengeneza chakula katika maji ni chokhi, pakki, - cha kuchomwa tu. Desturi hii ni pia ni ya udanganyifu iliyowekwa na maaskofu waki-Rumi wa kiuongo. Ilivyokuwa ni raha kula chakula kama hicho na kunywa vinywaji ambavyo vina maziwa mengi na siagi ilitumiwa, na ilivyokuwa vyakula vingi vinateremshwa tumboni kwa urahisi, watu hawa wameyaweka haya. Kuweka haya upande, pakka ni chakula kile ambacho kinapikwa juu ya moto au kina iva juu ya wakati, na kachcha ni kimoja si kama hichi. Pia si kweli kusema haya daima kuwa lazima chakula kilichopikwa au kuiva ndiyo kiliwe, lakini si kile hakijapikwa au hakijaiva, kwa sababu dengu na nafaka nyingine na matunda yanaliwa mabichi.

Q. Waliozaliwa mara mbili au kupata uzima mara ya pili Brahmans Kshatriyas na Vaishyas wanakula chakula kilichopikwa na wao wenyewe au lazima wao wale kile kilichopikwa na Shudras?.

A. Wao lazima wale chakula kilichopikwa na Shudras, kwa sababu, wanawake na wanaume wa wale waliozaliwa tena lazima wajishughulishe kusomesha mambo ya kwendesha serekali, kuchunga ng'ombe, kulima shamba, na kazi za biashara. Wao wasile, ila wakati wa bahati mbaya, kutoka kwenye vyombo vya Shudra, au chukua chakula kilichotengenezwa nyumbani kwake: Hii ni amri ya haya:-

Hii ni mithali ya Apastamba. Shudras, i.e. wanawake na wanaume wajinga hufanya kazi katika nyumba za Aryas kupika chakula na kazi nyinginezo za mikono. Lakini wao lazima wajiweke wenyewe na nguo zao safi. Wanapopika chakula katika nyumba za Aryas, wao lazima waifunge midomo yao kwa kitambaa ili mate na puumzi zao zisije kuchanganyika na chakula. Wao lazima wajinyoe na kukata kucha kila siku nane wapike chakula baada ya kukoga, na kula baada ya Aryas kula chakula chao.

Q. Pale unapokula chakula kilichopikwa kwa mafuta kinapoguswa na Shudra kinakatazwa, vipi kitaweza kuliwa kinapo pikwa na yeye?

A. Itikadi hii ni ya kufikiriwa tu nani ya mwongo; wao wanayo, kama ilivyokuwa, hula chakula kilichotengenezwa na dunia nzima na nacho ni taka tu, wale wanaokula sukari ilikuwa haijasafishwa,sukari, siagi iliyosafishwa, maziwa yaliyotengenezwa unga, mboga, matunda na mizizi. Hivyo, kwa mfano, Shudras, washona viatu, matopasi, Waislamu, Wakiristo, na watu wengine kama hawa, wanalima miwa mashambani, huisafisha huikamua na kuitoa maji. Wao hufanya kazi katika njia hii na mikono isiyokoshwa baada ya kwenda msalani. Wao kuichukua miwa hii na kuitia katika mashine. Wao huinyonya nusu na kuikamua nusu. Wanapoyapasha moto maji ya miwa, wao hupika mikate yao pia. Katika mpango wa kuitengeneza sukari, wao huifuta na viatu vichafu, vilivyojaa uchafu, mkojo, na mavi. Watu hawa huyatia maji maziwa kwa kutumia vyombo vyao vichafu pia vinavyotumika kwa kusafishia siagi majumbani mwao. Baada ya kusaga mahindi, wao huukusanya unga kwa mikono michafu. Matone ya jasho lao huanguka kwenye unga. Vitu vingi kama hivi hutokea katika kutengeneza mtengenezo kama huu. Pia huwa hivyo hivyo wanapotengeneza matunda, mizizi na mizizi minene. Vitu kama hivi vinapoliwa, wao huwa kama vile wamekula chakula kwa mikono ya watu wengine.

Q. Hakuna mkatazo wo wote kula matunda , mizizi, maji ya matunda na mengineyo yaliyotengenezwa bila ya wenyewe kuona.

A. Haya, wewe utakula chakula kilichotengenezwa na matopasi au wafuasi wa Mohammed mbali na kwako. Ikiwa wewe utasema, pa, tena hapo chakula kilichotengenezwa bila ya kuona pia huwa ni chakukatazwa kuliwa. Hapana shaka kuwa nyinyi Aryas inawezekana kuwa mtaweza kufanywa mkubali kunywa na tabia nyingi mbaya kwa kula vyakula vilivyotengenezwa na wengine wanao kula nyama na wanaokunywa. Lakini hapana dhara ya kugawanyiana chakula miongoni mwa Aryas. Ni shida sana kuleta maendeleo bila ya umoja katika dini, kuwa na mwenzako katika dhiki na raha au mwenzako katika faida na hasara, na huruma katika majonzi na furaha. Lakini kula chakula kwenye meza moja na watu wote haitatatua mambo yote. Ila desturi mbaya ziepukwe na nzuri ziendelezwe, hivyo hapatakuwa na maendeleo lakini uovu utakuwa ndiyo matokeo. Serekali ya kigeni katika Aryavarta ndiyo sababu ya kutokuwapo kwa umoja, mfarakano wa dini, kuutumia vibaya utakatifu au Brahmacharya, kutokuwapo kwa hima ya kutaka kupata elimu, ndoa ya utotoni bila ya

makubaliano ya pande zote mbili, raha, kusema uwongo na uovu mwingine, ujinga wa kutoijua Vedas, na mengineyo. Ndugu wawili wa kiume wanapopigana, wageni wa nje hujiingiza. Wewe umesahau vituko vya Mahabharat (vita vikuu) ambavyo vilitokea miaka 5,000 iliyopita? Tazama, watu wote waliojiunga na vita hivyo walichukuwa vyakula vyao wakati ule. Kutokuwa na umoja na mtengano uliwaangamiza Kauravas, Pandavas na Yadavas.

Kilichofanyika kishafanyika, lakini inasikitisha maradhi haya haya bado yanatuathiri sisi kwa bahati mbaya. Haijulikani hii jini huyu mbaya atatuacha sisi kwaajili ya uwema na uzuri wetu wote. Jee itawashinda Aryas na kuwanyima raha na kuwazamisha katika dhiki na kufa kama mbwa? Aryas bado wanayaengeza mashaka yao kwa kufata njia ya ubaya wa Duryodhana na uovu, mwuuaji wa jamaa zake mwenyewe na mwangamizi wa nchi yake mwenyewe. Mungu tuonee huruma, ili ugonjwa huu uangamie miongoni mwa sisi Aryas!

Vyakula vinavyoamriwa kula na vile vilivyoziwiliwa ni vya namna mbili, kwa majina (1) Sehemu moja kwa sheria au Dharma Shastra (2) yale yanayoruhusiwa na vitabu vya utabibu. Hivyo, kwa mfano, sheria inasema.

Manu, V. 5. Waliozaliwa mara mbili (Brahmans Kshatriyas na Vaishyas) lazima wasile mboga, matunda, mizizi na vyakula vyengine ambavyo vinatokana kutoka na uchafu, mkojo, na vitu vyengine vichafu.

Manu, 11, 177. Vitu vile visitumiwe katu ambavyo vitamfanya mwana chuoni, vitu vile kama vinavyolewesha, majani ya bangi - ganja, kasumba na dawa nyinginezo.

Wao wasile vyakula vilivyo chacha, vilivyoharibika, vinavyonuka au kwa njia yo yote ambayo haijatengenezwa kabla. Wao wasile vyakula vinavyotokana na mikono ya washenzi, wanaokula nyama na kunywa mvinyo, na miile ile ambayo imejaa chembe za nyama na mvinyo.

**Umuhimu Wa Ng'ombe**

Wao wasiwaue na wasiwaache wengine kuwaua wanyama muhimu. Kwa mfano, ng'ombe mmoja hutoa maziwa, siagi safi na ndama, mke na mume, mpaka kufikia muda wa namna moja ya watu kama 475600 kuwapatia maziwa na chakula. Kufahamisha. Ng'ombe wengine hutoa ratili 40 za maziwa na wengine ratili 4 kila siku. Kwa maziwa ya ng'ombe mmoja kwa siku moja ilikuwa ratili 22. Pia, ng'ombe wengine hutoa maziwa kwa muda wa miezi 18 na wengine kwa miezi 6. Tena wakati wa kutoa maziwa kwa ng'ombe utakuwa miezi 12. Sasa, ng'ombe mmoja hutoa maziwa mengi wakati wa maisha yake na kuwatosheleza watu 24, 960 wakati mmoja. Huzaa ndama 6 wa kiume na 6 wa kike, ikiwa wawili katika hawa watakufa, watabaki 10. Hivyo maisha yote ya ndama watano wa kike watawapatia maziwa ambayo watawatosheleza watu 124,800 wakati mmoja. Wala ndama dume waliobakia watazalisha nafaka katika maunds 5000 ambayo ilawalisha watu 25000 wakati mmoja, ikiwa mtu anakula ¾ ya ratili 1¼ ratili kila

siku. Sasa, vyote viwili maziwa pamoja na nafaka, zinazotokana na ng'ombe jike na dume wakati wa maisha yao, yatawalisha watu 374,800 wakati mmoja. Kwa hivyo, ng'ombe mmoja katika maisha yake atawasaidia watu 475,600 wakati *mmoja.*

Ikiwa nyakati hizi zitazidishwa, watu wasioweza kuhesabika watalishwa na mnyama huyu wenye faida. Pamoja na kulima, ng'ombe dume huwafanyia binadamu kazi nyingi kwa kuwaendeshea vigari vyao na kwa kuwabebea mizigo yao Ng'ombe jike ni wenye faida sana kuwa ni mzazi. Pia, nyati ni mwenye faida kama ng'ombe dume. Kwa sababu hii, maziwa ya ng'ombe na samli yake safi huleta siha nzuri zaidi ya akili kuliko maziwa ya nyati. Kwa nja hii Aryas wanawahesabu ngombe kuwa ni mnyama muhimu kwa watu wataalamu wengine pia wanafikiria haya.

*Maziwa ya mbuzi wakati wa maisha yanaweza kuwalisha watu 25,920 wakati* mmoja. Kwa njia hii, tembo, farasi, ngamia, kondoo, na wanyama wengine kama hawa ni wenye faida sana kwa watu. Wale wanaowaua wanyama hawa, wanahesabika miongoni mwa wauaji. Tazama Aryas wanapotawa kwenye nchi, wanyama waadilifu kama hawa hawakuchinjwa. Tena hapo watu wa Aryavarta na wa nchi nyingine waliishi kwa raha sana; kwa wingi wa maziwa, samli safi, ng'ombe dume na jike walizaa nafaka nyingi, maziwa, vyakula vyenginevyo kwaajili ya raha ya wote. Lakini tokea wageni walaji wa nyama ambawo wanawachinja ng'ombe na wanyama wengine walipoianzisha utawala wao katika nchi, dhiki za watu zinazidi kwa sababu;

Chanakya X. 13. Hapawezi kuwa na maua na matunda ya mti, mizizi yake inapakuwa imekatwa.

Q. Ikiwa hapana atakaye waua wanyama, chui na wanyama wengine walio wawindaji watakuwa wengi mpaka watawaangamiza ng'ombe wote na wanyama wengine wa kinyumbani na kuufanya ukarimu wako na huruma ya ng'ombe kuwa isiyo ya maana.

A. Ni wajibu wa walawala kuwatia adamu wanyama wakali na si watu, kuwaua, ikiwa ni lazima.

Q. *Basi nyama yao itupwe baada ya kuuliwa?*

A. Inaweza kutupwa au kupewa wanyama wanao kula nyama ili waile. Au bora iunguzwe. Ikiwa walaji nyama wataila, haitaleta hasara, yo yote kwa dunia; lakini tabia ya mtu huyo itakuwa ya kidhalimu, na inawezekana kuwa yeye awe mwuaji kwa wakati kupita.

**Chakula Kilicho Sawa**

Si sawa kula au kutumia kile ambacho kimepatikana kwa dhara, isiyo sawa ua halali, ujambazi, madanganyo na uovu mwingine. Lakini ni sawa kula na kufurahia kile kilichopatikana bila ya dhara, kwa ye yote na kwa uadilifu. Pia, mchele, ngano na nafaka nyingine, matunda, mizizi, njugu, maziwa, siagi, sukari

na vyakula vyenginevyo ambavyo vinaleta siha, huondoa maradhi, na huzidisha nguvu za akili, ushujaa na umri, lazima viliwe kwa intidhamu na wakati ulio sawa baada ya kutengenezwa kwa ufundi na kupikwa. Vyakula vyote ambavyo havipatani na mwili wa mtu lazima viipukwe. Lakini vyakula ambavyo vinaelekezana na tabia za mtu, lazima vitumiwe; hivyo ni vitu vyao ambavyo vimechaguliwa.

**Kula Pamoja.**

Q. Kuna dhara yo yote ya kula pamoja kutoka kwenye chombo kimoja?

A. Ndiyo, kuna dhara kufanya hivyo; kwa sababu, tabia na hamaki za mtu mmoja hazisikilizani na za mwingine. Hivyo, mtu mwenye afya anaye kula na mwenye ukoma au ugonjwa wa kuambukiza, hupata ugonjwa kwa kuambukizwa, na damu yake kuharibika. Ni vibaya kula pamoja watu wengi, na wala hakuna uzuri kufanya haya. Hivyo, inasema Manu, II, 56.

Makombo ya chakula wasipewe wengine, wala mtu asile na mwenzake kutoka kwenye chombo ki moja. Watu wasile sana, na wala wasizunguke baada ya kula bila ya kukosha mikono yao na mdomo.

Q. Nini maana ya mafundisho 'Gororuchchishtabhojanam'?

A. Maana yake ni baada ya mwalimu kula chakula chake, mtu ndiyo ale chakula kilichowekwa upande na kiwe hakikuguswa, haya ni kusema, mwalimu alishwe kwanza na tena hapo mwafunzi ndiyo ale chakula chake.

Q. Ikiwa makombo ya chakula yasiliwe,hapana atakaye kula asali ambayo ni makombo ya nyuki, kunywa maziwa ambayo ni makombo ya ndama na kula chakula chake mwenyewe baada ya tonge ya kwanza kwa sababu chakula kilichobaki huwa ni makombo ya chakula chake mwenyewe.

A. Asali ni makombo kwa jina tu, lazima iliwe kwa sababu ni arki ya majani mengi. Ndama hunywa maziwa ambayo yanatoka nje na si yaliyo ndani. Hivyo si makombo. Lakini chuchu za ng'ombe lazima zisafishwe kwa maji safi kabla ya kukamwa katika ndoo iliyosafi. Makombo ya chakula chake mtu mwenyewe hakileti madhari kwa afya. Tazama hapa, inachafua moyo kula makombo ya mtu mwingine. Hapana mtu anayeona dhiki kuusafisha ndomo wake mwenyewe pua, shikio, macho, viungu vyenginevyo na uchafu wao, vyenginevyo. Lakini yeye anachukua kugusa mavi ya wengine. Hivyo, ni kawaida kuwa desturi hii ya watu haipingani na amri ya tabia, na hapana mtu lazima ale makombo ya chakula cha wengine.

Q. Haya si lazima mume na mke wale makombo wao kwa wao.

A. La, kwa sababu khulka za miili yao iko tafauti.

**Kula Pamoja**

Q. Niambie kuna dhara gani kula chakula kilichotengenezwa na mtu ye yote.?

Kwa sababu, miili ya Brahman mpaka ile ya watu wa daraja la chini imetengenezwa kwa mifupa, nyama na ngozi. Damu ya mwili wa Brahman ni sawa na ile ya mwili wa mtu wa daraja ya chini. Kwa matokeo haya kuna dhara gani kula chakula cha mikono ya binadamu ye yote?

A. Hapa dhara katika haya kwa sababu shahawa na yai la uzazi la kike linalozaliwa katika mwili wa mwanamume na mwanamke wa daraja la chini si safi hivyo na kuwa mbali na uchafu, harufu mbaya au ila nyingine ya namna nyingine kama yale ya Brahman na miili ya mke wake, ambawo unaolishwa chakula kilicho safi na kikamilifu. Kwa sababu mwili wa tabaka la chini umejaa chembe au vumbi na harufu mbovu na vitu vyengine. Lakini si hivyo na Brahmans na tabaka jengine la juu. Kwa hivyo, ni sawa kula chakula cha mikono ya Brahmans na matabaka mengine ya juu, na si sawa kula chakula cha mikono ya watu wa tabaka la chini, kama matopasi, washona viatu, na wanaharamu (chandals - vizazi vya mwanamke Brahman na Shudra au mtumwa). Haya, ikiwa wewe utaulizwa, wewe utakuwa na adabu nzuri mbele ya mkweo wa kike, mtoto mwanamke, au mke wa mtoto wa kiume, kama vile yeye ni mke wako mwenyewe, kwa kuona kuwa mwili wake umetengenezwa na ngozi na vitu vyenginevyo kama vile vya mke wako? Jee wewe utaona aibu na kuzuia ulimi wako. Ilivyokuwa vitu vilivyooza, na kunuka vinaweza kulika kama vile vitu vyenye ladha vinalika kwa mikono na mdomo, wewe pia utakula kama haya?

Q. Kama wewe unavyosafisha na kutia palaster pahali unapokula na mavi ya ng'ombe, kwa nini wewe hupasafishi kwa mavi yako mwenyewe? Kwa nini si pahali unapokula (chumba cha kulia chakula) huwa si safi kwa kutia mavi ya ng'ombe?

A. Mavi ya ng'ombe haya nuki sana kama uchafu wa binadamu. Harufu ya ng'ombe haiondoki upesi sana kwenye eneo? Hayati doa kwenye kitambaa wala kuchujua. Mavi makavu ya ng'ombe haichafui kama udongo. Pahali palipotiwa mavi ya ng'ombe huonekana maridadi sana. Pia, nzi, siafu na funza wengine wengi na vidudu huzuru jikoni mara kwa mara kutokana na uchafu wake, ilivyokuwa siagi, sukari na takataka za chakula zinatupwa chini wakati wa kula chakula, na pale chakula kinapotengenezwa. Ikiwa pahali hapafagiwi na kusafishwa kila siku, basi karibu pataonekana kama choo. Kwa hivyo, jiko na pahali pa kulia chakula lazima pasuguliwe kila siku kwa mavi ya ng'ombe na mchanga na kufagiwa kuwa safi kabisa. Ikiwa pahali pametiwa mawe au kujengwa kwa chakaa, panaweza kusafishwa kwa maji. Hadhara hii itaondosha vipingamizi vyote. Ikiwa wewe unapinga kupasafisha pahali pa kulia kwa mavi ya ng'ombe, sisi tunakuuliza ikiwa ni bora au si sawa kuuwasha moto kwa mavi makavu ya ng'ombe, kuwasha pyapu kwa majivu ya mavi ya ng'ombe, na kupaka saruje kwenye kuta za nyumba ya mavi ya ng'ombe na matumizi mengineyo, ni ya kuleta upingamizi. Hapana shaka ye yote kuwa yote haya haya pingwi kabisa

Q. Ipi ni bora, kula chakula kwenye pahali pa kulia, au nje yake?

A. Chakula kiliwe katika pahali palipo safi na pazuri. Lakini wakati wa vita,

kinaweza kuliwa hata juu ya mgongo wa farasi, kaktika magari, ukiwa umekaa au kuchutama kwenye ardhi kama hali itavyokuwa.

Q. Lazima sisi tule chakula kilichotengenezwa kwa mikono yetu wenyewe, na si kwa mikono ya wengine?

A. Hapana dhara hata kidogo kula pamoja na Aryas wote, ikiwa chakula kinatengenezwa kwa usafi kamili. Kwa sababu, wanawake na wanaume wa Brahman, Kshatriya na makabila ya Vaishya wanajishughulisha katika kupika, kusafisha pahali pa kula, na kuvisugua vyombo; wa hawataweza kuendeleza elimu yao na sifa nyinginezo za juu. Wakumbuke wafalme, mashujaa na wana falsafa wa dunia ambawo walihudhuria karamu ya kifalme (muhanga) ya Mfalme Yudhishthir alikula chakula kutoka kwenye jiko hilo hilo. Lakini dini mbali mbali kama zile za Wakiristo na Waisilamu zilipoenea katika nchi, watu waligawanyika kwa kutokuwa na umoja. Wageni hawa waliaanza kunywa mvinyo na kula nyama na namna nyinginezo za nyama, ambazo zilileta shida kama milima katika desturi za kula na kunywa. Tazama, wafalme wa Aryavarta walifanya urafiki wa ndoa na wafalme wa Kabul, Kandhar, Persia, Amerika, Uropa na nchi nyinginezo na kumwoa Gandhari, Madri, Ulopi, na mabinti wa falme wa nchi hizo. Shakuni na wageni wengine walikula chakula na Kouravas na Pandavas. Hapa kuwa na uadui baina yao. Kwa sababu katika siku hizo palikuwa na dini moja ya Vedas katika dunia nzima. Watu wote waliamini na waliwaona wenzao kuwa kama ni sehemu zao wenyewe. Wao walikuwa wakioneana huruma nyingi katika raha na majonzi, ustawi na msiba. Kwaajili ya haya imani ilitawala kwenye uso wa dunia; na watu wafurahia raha na starehe. Lakini sasa kuna msiba mwingi na uadui kuhusu kuzidi kwa wafuasi wa madhehebu mbali mbali. Ni wajibu wa kwanza wa mtu mwenye busara kuuondoa msiba huu. Mwenyezi Mungu Mkubwa aioteshe mbegu ya dini ya kweli katika moyo wa watu wote ili madhehebu ya uongo yangamie haraka kwaajili ya uzuri ya wote. Ni jambo muhimu linalohitaji kufikiriwa. Kuwacha hisia mbaya, wao wajishughulishe kuiendeleza imani na furaha ya wote.

Mengi ya desturi na makosa, kwaajili ya chakula kilichoruhusiwa na kukatazwa.

Sura ya 10 inamaliza nusu ya kwanza ya kitabu hiki. Sababu kwa nini sura za nusu ya kitabu hihi hazina mapingamizi maalum ya dini a uwongo, ni kuwa mpaka watu wa sasa watengenee katika kuhukumu na kuagua baina ya kweli na uwongo, wao hawawezi kufahamu sababu ya upinzani wa kijumla wa madhehebu ya uwongo. Kwa hivyo, nusu ya kwanza ya kitabu zinaeleza maamrisho ya dini ya kweli. Nusu nyingine, ambayo ina sura nne itaelezea hasa kuunga mkono wa kweli na kupinga dini za uongo. Sura ya kwanza ya sura hizi nne inatoa hesabu na pingamizi za dini za Wahindi, ya pili ni ya Jain, ya tatu ni ya Wakiristo, na ya nne ni ya Waislamu. Mwishoni, sura ya kumi na nne itaeleza kwa ufupi dini yetu wenyewe. Wale wanaopenda kujua pingamizi kwa urefu, lazima wazisome sura hizi kwa utulivu. Lakini upingamizi kwa jumla wa dini mbali mbali pia

umetolewa kwa ufupi katika sura kumi zilizofuata. Yule ambaye atazisoma sura kumi na nne bila ya kupendelea na kwa macho ya haki na usawa, atabarikiwa kwa ukweli na furaha. Lakini yule ambaye anakisoma na kukisikiliza kitabu hiki kwa ushupavu wa dini, mapendeleo na wivu, ataona dhiki kukifahamu. Hivyo, yeye ambaye haiweki fahamu yake vizuri kwenye kitabu hiki, yeye hataiona alama iliyowekwa na mwandishi na kuangukia kwenye shimo la makosa. Ni wajibu muhimu wa watu wenye busara kupambanua ukweli kutoka kwenye uwongo na tena kuukubali ukweli na kuukataa uwongo na hapo kupata mazuri ya daraja la juu kabisa. Wao peke yao wataweza kuufurahia uwema na kuwa wataalamu, na kujipatia ukweli wa dini, sababu ya mali, mtosheko na matakwa na furaha uokovu, pitisha maisha yao katika raha na bashasha za dunia.

**Muhtasari**

Desturi nzuri inatiwa alama kwa ukweli, heshima, unyonge, urafiki mzuri na elimu ya haki, na dabu mbovu ni kinyume cha haya. Inafuatana na dini isiyopendelea po pote, mapenzi, hisia na mazoezi ya wenye hekima. Kuweka nywele kwenye kichwa na shingo ni jambo la hiari. Kuweza kuzizuia hisia ni lazima. Kutumbukia katika haya hukupeleka kuwa mwovu. Kula kidogo na kufanya kazi, mazoezi ya kutafakari, na njia ya haki katu zisiwekwe kando. Heshima, adabu nzuri, heshima ya mtu mzima na masomo lazima yaonyeshwe. Mali, jamii, umri, ukarimu, na elimu huzidisha heshima. Katika kushukia kwenye ukoo uliotajwa hapa.

Usafiri kwenye nchi za kigeni na Safari za bahari zilikuwapa tokea zama za kale. Mahabharat, Shanti Parva, Ch. 327 inaeleza kuwa Shuka Deva alisafiri kwenda Uropa, Tartary na China; Bwana Krishna kwenda Amerika (Patal) kwa meli (Ashwatari), Wafalme wa Aryavarta walioa katika nchi za kigeni. Malkia wa Dhritarashtra, Gandhari, alikuwa binti wa Kandhar.

Aryas wote wale kwenye meza moja. Utengenezaji wa chakula ni kazi za Shudras (Apastamba). Ulaji wa nyama na vinywaji vizito daima viipukwe. Chakula kiliwe kwenye mikahawa safi, na sheria za kijinga zinazoitwa chowka lazima zikataliwe. Wapiganaji vita wanaweza kula chakula chao kwenye migongo ya farasi.

Kula nyama kunamfanya mtu awe na tabia ya ukatili na huangmiza faida za wanyama. Kwa mfano, ng'ombe anayetoa maziwa ratili 22 kwa siku moja kwa muda wa mwaka 12, atawalisha watu 24, 960 kwa mara moja. Ndama wake wa kike watano na ndama dume 5, wataleta maziwa na nafaka ya kuwatosha watu 374,800 kwa wakati mmoja. Hivyo ng'ombe mmoja katika uhai wake anawalisha watu 475,000 kwa wakati mmoja. Mbuzi, kondoo, na farasi pia wanawaletea faida nyingi binadamu. Hivyo wanyama hawa wasichinjwe kwaajili ya chakula kabisa.

गुरु विरजानन्द दण्डी
सन्दर्भ पुस्तकालय

MWISHO

परिग्रहण क्रमांक ...7890......
दयानन्द मठ

# THE TEN PRINCIPLES

## *Of The Arya Samaj*

1. **God, His Characteristics:** The Primordial Root - the Eternal Unseen Sustainer - of all true knowledge and of objects made known by true knowledge - any of all these - is the Supreme God.

2. ***His Attributes and Worship:*** *God is Personification of Existence, Intelligence* and Bliss. He is Formless, Almighty, Just, Benevolent, Unborn, Endless, and Infinite, Unchangeable, Beginningless, Incomparable, Support of All, Lord of All, All-pervading, Omniscient, and Controller of all from within, Undecaying; Imperishable, Fearless, Eternal, Holy and Maker of the Universe. To Him alone is worship due.

3. **His Word, The Veda:** The Veda is the Scripture of true knowledge, It is the paramount duty of every Arya to learn and teach The Veda, to hear it read and to recite it to others.

4. **Truth:** We should ever be ready to embrace truth and to forsake untruth.

5. **Righteousness:** All acts should be done in accordance with Dharma after deliberating what is right and wrong.

6. **Benevolence:** The prime object of the Arya Samaj - the Vedic Church - is to do good to the world, that is, to promote physical, spiritual and social good of every sentient being.

7. **Love and Justice:** Our conduct towards all should be guided by love, Righteousness and Justice.

8. **Nescience and Science:** We should dispel "avidya" - nescience, and promote "vidya" - science, spiritual and physical.

9. **Individualism and Altruism:** No one should be content with promoting his good only; on the contrary, he should look for his good in promoting the good of all.

10. **Subordination and Liberty:** All men should subordinate themselves to the laws of society calculated to promote the well-being of all; they should be free in regard to the laws promoting individual well-being.

656